# JINIUCHAWI NA USHIRIKINA KAMA MKAKATI WA UCHIMUZI KATIKA RIWAYA TEULE ZA MAUNDU MWINGIZI

**NEEMA GEORGE MTURO**

**Tasnifu hii Imewasilishwa ili Kutosheleza Mahitaji ya Shahada ya Uzamifu katika Idara ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Nairobi**

**2018**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijatolewa kwa mahitaji ya kutosheleza Shahada katika Chuo Kikuu kingine chochote.

Sahihi……………………………… Tarehe……………………

Neema George Mturo

REG. NO: C80/99107/2015 (Mtahiniwa)

Tasnifu hii imewasilishwa kwa madhumuni ya kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi na washauri tulioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi kupitia Idara ya Kiswahili

Sahihi……………………………… Tarehe…………….........

Dkt.Zaja Omboga (Msimamizi)

Sahihi……………………………… Tarehe………………........

Prof. Kineene wa Mutiso (Msimamizi)

## TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa mume wangu mpenzi Lughano Lutengamaso Kusiluka ambaye siku zote nilipokata tamaa alinitia moyo nisonge mbele na hata kukesha nami. Naitabaruku pia kwa wanangu wapenzi Lulu na Luisa, baraka zao ndio mafanikio haya.

Vilevile naitabaruku kazi hii kwa wazazi wangu wapendwa Bwana na Bibi George Mturo, ambao walinilea na kunisomesha mpaka shahada ya uzamili na kunifanya niwe na kiu ya masomo hata kumalizia shahada hii ya uzamifu. Aidha sitasahau mchango wa mama mkwe wangu Bi Kusiluka ambaye alinitia moyo sana katika kipindi hiki cha miaka mitatu. Mungu akubariki sana na akupe maisha marefu.

Nawapenda nyote, Mungu awabariki.

## SHUKRANI

Awali ya yote, naichukua fursa hii kumshukuru Mungu kwa uhai, nguvu, baraka na uwezo wa kuiwazia na kuishughulikia tasnifu hii nzima. Pili, maadamu ulimwengu umenitia darasani, ukanifundisha maana ya kurudisha wema kulikotokea wema, ama hisani kulikojiri hisani, sina budi kulipa deni hili la wema japo kwa asante kwa wasimamizi wangu wapendwa Prof. Kineene Wa Mutiso, Prof Kyalo Wadi Wamitila na Dkt. Zaja Omboga ambao waliufuatilia utafiti huu kwa makini hatua baada ya hatua na kunielekeza na kunikwamua nilikokuwa nimekwama, nawapenda sana. Uongozi na mawaidha ya busara waliyonipa yamenifungua macho katika maswala ya kiusomi kwa njia ya kipekee. Mungu awabariki na kuwaongoza katika shughuli zenu zote.

Napenda kukishukuru Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira ambao ndio walidhamini masomo yangu kwa muda wa miaka mitatu. Aidha nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipowashukuru baadhi ya wahadhiri wenzangu wa Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira ambao wamekuwa msaada mkubwa katika shule yangu kwa namna moja ama nyingine japo ni wengi nitawataja baadhi yao ambao ni Dickson Mlowezi, Dkt Mutua, Sophia Laiser, Lawi Mauyo, Dkt Rose Munisi, Perida Mgecha na Gestuta Tilia

Pia napenda kuwashukuru wahadhiri wa Chuo Kikuu cha Nairobi katika idara ya Kiswahili lugha na isimu toka mwanzo wa shule yangu kwa kuwa pamoja nami na hatimaye leo hii nafuzu elimu hii ya uzamivu miongoni mwao akiwa Prof Habwe, Prof Iribe Mwangi, Dkt Thom Olali na Dkt Hanna. Mungu awabariki sana.

## YALIYOMO

**UNGAMO** .................................................................................................... i

**TABARUKU** .................................................................................................... ii

**SHUKRANI** .................................................................................................... iii

**YALIYOMO** .................................................................................................... iv

**VIFUPISHO** .................................................................................................... viii

**UFAFANUZI WA ISTILAHI ZILIZOTUMIWA** .................................................... ix

**IKISIRI** .................................................................................................... xii

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI KWA UJUMLA** ........................................ 1

1.1 Usuli wa Mada .................................................................................... 1

1.2 Tatizo la Utafiti .................................................................................... 9

1.3 Maswali ya Utafiti .................................................................................... 10

1.4 Madhumuni ya Utafiti .................................................................................... 10

1.5 Sababu za Kuchagua Mada .................................................................................... 11

1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti .................................................................................... 13

1.7. Msingi wa Nadharia .................................................................................... 14

1.7.1 Nadharia ya Uhalisiajabu .................................................................................... 14

1.7.2 Nadharia ya Semiotiki .................................................................................... 19

1.8 Mapitio ya Maandiko .................................................................................... 27

1.8.1 Dhana ya Jiniuchawi na Ushirikina .................................................................. 27

1.8.2 Dhana ya Uchimuzi Katika Kazi za Fasihi ........................................................ 35

1.8.3 Dhana ya Ishara .................................................................................... 36

1.9. Mbinu za Ukusanyaji Data .................................................................................... 44

1.10 Uchanganuzi wa Data na Uwasilishaji wa Data ................................................ 45

**SURA YA PILI: DHANA YA UCHIMUZI, JINIUCHAWI NA USHIRIKINA KAMA VIPENGELE VYA UHALISIAJABU** ........................................................ 47

2.1 Dhana ya Uchimuzi na Historia Yake ................................................................ 47

2.1.1 Kanuni Kuu za Uchimuzi .................................................................................. 53

2.2 Uchimuzi Katika Kazi za Fasihi ......................................................................... 56

2.3 Uhalisiajabu kama Dhana Iliyobeba Kipengele cha Jiniuchawi na Ushirikina..... 62

2.3.1 Kipindi cha Uhalisia Hakiki ............................................................................ 62

2.3.2 Kipindi cha Uhalisia wa Kijamaa ................................................................... 64

2.3.3 Kipindi cha Uhalisiajabu .................................................................................. 66

2.4 Hitimisho ............................................................................................................ 67

**SURA YA TATU: MANDHARI, MATUKIO YA KIJINIUCHAWI NA USHIRIKINA NA UCHIMUZI WA DHAMIRA NA MAUDHUI KATIKA RIWAYA TEULE ZA MWINGIZI** ........................................................................... 69

3.1 Utangulizi ............................................................................................................ 69

3.2 Ufasiri na Maana ya Mandhari ............................................................................ 69

3.2.1 Aina za Mandhari katika Riwaya Teule za Mwingizi ..................................... 72

3.3 Mandhari na Matukio ya Kijiniuchawi na Ushirikina Yalivyochimuza Dhamira na Maudhui katika Riwaya ya *Vita vya Mapenzi* ........................................................... 73

3.4 Mandhari na Matukio ya Kijiniuchawi na Ushirikina Yalivyochimuza Dhamira na Maudhui katika Riwaya ya *Mzimu wa Waufi* ........................................................... 104

3.5 Mandhari na Matukio ya Kijiniuchawi na Ushirikina Yalivyochimuza Dhamira na Maudhui katika Riwaya ya *Tanzia* ............................................................................ 122

3.6 Maswala Ibuka ya Kiutunzi na Kiufasiri ............................................................ 137

**SURA YA NNE: USAWIRI WA WAHUSIKA WA KIJINIUCHAWI NA KISHIRIKINA KAMA MKAKATI WA UCHIMUZI KATIKA RIWAYA TEULE ZA MWINGIZI** ........ 143

4.1 Utangulizi ........ 143

4.2 Uchimuzi katika Uhusika ........ 144

4.3 Uainishaji wa Wahusika na Uchimuzi katika Riwaya Teule za Mwingizi ........ 147

4.3.1 Uchimuzi wa Dhamira kwa Mkabala wa Wahusika wa Kijiniuchawi na Ushirikina katika Riwaya ya *Vita vya Mapenzi* ........ 148

4.3.2 Uchimuzi wa Dhamira kwa Mkabala wa Wahusika wa Kijiniuchawi na Ushirikina katika Riwaya ya *Mzimu wa Waufi* ........ 205

4.3.3 Uchimuzi wa Dhamira kwa Mkabala wa Wahusika wa Kijiniuchawi na Ushirikina katika Riwaya ya *Tanzia* ........ 237

4.4 Hitimisho ........ 260

**SURA YA TANO: ISHARA NA UASHIRIAJI KAMA MIKAKATI YA UCHIMUZI KATIKA RIWAYA TEULE ZA MAUNDU MWINGIZI** ........ 261

5.1 Utangulizi ........ 261

5.2 Uhalisiamazingaombwe Katika Ishara na Uashiriaji katika Riwaya za Mwingizi ........ 261

5.3 Mwegemeo wa Kisemiotiki katika Riwaya Teule za Maundu Mwingizi ........ 267

5.4 Mbinu za Kiishara na Uashiriaji katika Riwaya za Maundu ........ 273

5.4.1 Kifo kama Ishara na Uashiriraji ........ 276

5.4.2 Njozi kama Ishara na Uashiriaji. ........ 284

5.4.3 Pete Kama Ishara na Uashiriaji ........ 287

5.4.4 Rangi kama Ishara na Uashiriaji ........ 296

5.4.5 Mazingira kama Ishara na Uaishiriaji wa Uasilia ........ 303

5.4.6 Mandhari za Mijini na Vijijini kama Ishara na Uashiriaji ........ 308

5.4.7 Wanyama na Viumbe Majini kama Ishara na Uashiriaji ............................ 311
5.3.8 Majina ya Watu na Mahali kama Ishara na Uashiriaji ................................ 317
5.3.9 Tamaa ya Ukwasi na Ubinafsi kama Ishara na Uashiriaji ........................... 319
5.3.10 Mifumo ya Dini na Itikadi kama Ishara na Uashiriaji ............................... 321
5.3.11 Hitimisho ........................................................................................ 327
**SURA YA SITA: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO** ............... 328
6.0 Utangulizi ........................................................................................... 328
6.1 Muhtasari wa Matokeo ......................................................................... 328
6.2 Upimaji wa Madhumuni ........................................................................ 330
6.3 Mapendekezo ...................................................................................... 333
**MAREJELEO** ........................................................................................... 334

## VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| **khj:** | Kesha Tajwa |
| **MW** | *Mzimu wa Waufi* |
| **T** | *Tanzia* |
| **TUKI**: | Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili |
| **VM** | *Vita vya Mapenzi* |

## UFAFANUZI WA ISTILAHI ZILIZOTUMIWA

**Uchimuzi:** Dhana inayorejelea mbinu na taratibu za kiutunzi katika fasihi zinazotumiwa kuangazia au kuweka wazi tukio, kitu au usemi fulani mbele au kwa namna wazi hivi kwamba lugha inayotumiwa huweka kipaumbele katika tukio, kitu au usemi wenyewe na inaangazia upekee au upya wa uelezaji. Huu ni utaratibu ambao unaonyesha jinsi ambavyo lugha ya kifasihi inavyoweza kutumiwa kuusawiri uhalisi wa maisha au uhalisi unaoakisi maisha. Kwa hivyo, lugha hiyo inaweza kujumuisha ukiukaji wa kaida za lugha ya kawaida kwa makusudi ili kuakisi uhalisi huo mpya, wa kipekee au uhalisi katika mipaka ya uwezekano tu.

**Ishara:** Ni kitu kinasimama kuwakilisha kitu kingine mfano, msalaba ni ishara ya ukristo, ufu au imani ya ufufuo; nguo nyeusi katika tamaduni za Kimagaribi ni ishara ya maombolezo

**Uashiriaji:** uashiriaji ni mtindo na ufundi wa kisanaa wa kutumia vitu, maneno, hali na matukio kwa kusudi la kuwasilisha wazo kidhahania.

**Uhalisiajabu/Uhalisiamazingaombwe:** Ni dhana ya kiutunzi na ufundi wa kiuandishi unaodhihirisha uhalisia wa kufikirika tu, uhalisia wa kiajabu, kindoto na wakati mwingine wa kimazingaombwe, uhalisia unaojibainisha katika mipaka ya uwezekano tu. Ni uhalisia uliongia katika uhakiki wa fasihi bunifu katika miaka ya 1940 kama njia ya kuchanganua na kuhakiki fasihi inayochanganya mambo ya kihalisi na mambo ya kimiujiza, kijini, kishirikina na kimazingaombwe kama ilivyo katika riwaya zinazochanganuliwa katika tasnifu hii ambapo mtunzi ameishia kujenga riwaya zinazowasilisha tajriba changamano. Uhalisia huu unajibainisha sana katika kazi za kifasihi ambazo zimeandikwa katika mtindo wa kimazingaombwe ili kuonyesha uhalisia wa maisha kama unaodhihirika kwa mara kwanza.

**Uajinabishaji/Ostraneniya:** Ni utaratibu katika fasihi unaotumia sifa ya lugha matumizi katika mazingira yasiyokuwa ya mazoea (kuna msambao mkubwa wa mandhari za aina hii katika riwaya zinazochanganuliwa katika tasnifu hii) ili kuizindua hadhira iweze kulielewa jambo

linalozungumziwa kwa kina zaidi. Huu ni utaratibu wa kiuandishi unaohusika hasa na uchimuzi wa hali ya kumfanya msomaji kulitazama upya na kwa kina jambo ambalo limechukuliwa kwa wakati mwingi kuwa la kawaida.

**Jiniuchawi:** Ni ile tabia ya mtu kuwatesa wengine na kuwa na tabia za kutumia vitu vya ajabuajabu katika mazingira fulani ya kutisha na kuogopesha. Jiniuchawi hufanya mambo yake katika ulimwengu usio wa kawaida na wakati mwingine jiniuchawi hutumika kuwatesa wengine kwa njia za kimazingara.

**Ushirikina:** Ni tabia ya kuamini mambo ya uchawi na mizimu, mambo yasiyoelezeka kisayansi

**Uhalisia wa kihakiki:** Ni dhana ya kifasihi itumiwayo kurejelea mikabala ya uchanganuzi wa kifasihi unaojishughulisha na uhalisia unaoibuka kutokana na udhihirishaji wa sanaa, sayansi na taratibu za kuchambua, kuchanganua na kuhakiki maandishi na kazi za kifasihi kwa kubainisha vijenzi vya kazi hizo, sehemu na vipengele vya ujenzi wa kazi hizo, uainishaji na upangaji wa kazi hizo katika makundi na tanzu, uamili na miundo ya kazi hizo, ulinganishaji, upambanuaji, ufasiri na utathmini wa kazi za kifasihi kwa jumla. Aina hii ya uhakiki imeshirikishwa katika uchanganuzi wa riwaya za Maundu Mwingizi.

**Uhalisia wa kijamaa:** Ni mbinu ya utunzi na uhakiki inayomzingatia binadamu kama uti wa mgongo wa kuwepo kwa ulimwengu na maana ya ulimwengu huo. Hali kadhalika ni aina ya uhalisia unaokusudiwa kuonyesha ubora wa ujamaa kama mfumo fanifu wa kiutawala na ki-uzalishaji mali. Istilahi hii iliasisiwa na kuingizwa katika fasihi kama utaratibu rasmi wa kuhakiki na kuchambua fasihi ya kijamaa kwa nia ya kuonyesha mwingiliano ulioko kati ya uchambuzi wa fasihi na ujenzi wa itikadi ya kijamii.

**Kiashirii:** Ni kiwakilishi/sauti/wasilisho la kimaandishi.

**Kielekezi:** Ni uhusiano wa ishara na kiashiriwa.

**Msimbo:** Ni kaida au dhana zinazowaunganisha wasomaji wa kazi za kifasihi na waandishi wake.

**Ishara za kitaashira:** Ni kiurejelezi/kiutamaduni.

**Kihemenitiki:** Ni kiusimulizi/kiutambaji au kiurejelezi.

**Uishara:** Ni hali ya matumizi ya ishara; uashiriaji.

**Ishara Bia:** Ni ishara za kiulimwengu au za kimataifa yaani ni ishara ambazo zinatumia vitu, dhana na hali ambazo watu karibu kila mahali ulimwenguni wanahusiana nazo.

**Ishara violwa/vionwa:** Ni ishara zinazoonekana kwa macho.

**Mandhari ya kinjozi/ kidhanifu**: Ni mandhari ambayo huwezi kuihusisha na uhalisi ni mandhari ya kufikirika tu.

**Mandhari ya kinelbelini**: Ni mandhari ambayo hupatikana katika kazi za kifasihi za kiuhalisiajabu ambapo hali ya uajabu au umazingaombwe huhusishwa. Huchanganya sifa za mandhari ya kiuhalisi (kijiografia) na mandhari ya kiutopia au ya kinjozi.

**IKISIRI**

Utafiti huu unahusu jiniuchawi na ushirikina kama mikakati ya uchimuzi katika riwaya za kimajaribio za Maundu Mwingizi za *Vita vya Mapenzi (2012), Mzimu wa Waufi (2013)* na *Tanzia* (2015). Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa ni kuonyesha jinsi mandhari za kijiniuchawi na kishirikina zinavyotumiwa kimkakati kuchimuza dhamira na maudhui mbalimbali, hali kadhalika zinavyotumiwa katika usawiri na uchimuzi wa wahusika wa kijiniuchawi na kishirikina katika riwaya za Mwingizi. Madhumuni mengine ya utafiti huu yalikuwa ni kubainisha jinsi ishara na uashiriaji zinavyotumiwa kama mikakati ya uchimuzi katika riwaya za Mwingizi. Ili kufanikisha utafiti huu, nadharia mbili zimetumika—nadharia ya uhalisiajabu na nadharia ya Semiotiki. Nadharia ya uhalisiajabu imetumika zaidi katika utafiti huu kwani riwaya zilizochanganuliwa katika utafiti huu zimekitwa zaidi katika maswala ya kihalisiamazingaombwe. Kwa upande wa Semiotiki, nadharia hii imetumika zaidi katika sura ya tano kwani sura hii imejikita zaidi katika kuangalia ishara. Kwa hiyo, nadharia hii imesaidiana na nadharia ya uhalisaiajabu katika kufanikisha utafiti huu mpaka ukakamilika. Utafiti huu kwa kiasi kikubwa umekuwa ni wa maktabani uliohusisha usomaji, uchanganuzi na utathimini wa riwaya za *Vita vya Mapenzi (2012), Mzimu wa Waufi (2013)* na *Tanzia* (2015) za Maundu Mwingizi na ndizo zilizotupa data ya msingi. Uchakataji wa data umeongozwa na makabala wa kitaamuli. Kwa jumla, matokeo ya uchanganuzi wa data kutoka katika riwaya hizi yameweza kujibu maswali ya utafiti, kwani yamebainisha mandhari, wahusika na ishara za kijiniuchawi na ushirikina zimeweza kuchimuza maudhui mbalimbali kama ya uongozi wa kiimla, mauaji na ufadhili wa kisiasa, mahusiano kati ya wahalifu na vigogo serikalini, ung'ang'aniaji madaraka na urithishanaji uongozi, uhuru wa bendera na ukoloni mamboleo, unafiki, uongo, mikataba ya kilaghai, utandawazi, usaliti, maadili, haki na sheria, ukatili, mafao binafsi, uwajibikaji, mifumo ya kiutawala, unyonyaji, malezi, mapenzi, pesa, nafasi ya mwanamke, familia, uaminifu, utii, migongano katika dini, heshima, utamaduni, misukosuko ya kindoa na mahusiano ya kifamilia, unyenyekevu, mitandao ya jinai katika jamii, mali ya umma, dhuluma dhidi ya wanawake na utawala kandamizi. Utafiti huu utakuwa na mchango mkubwa kitaaluma katika uwanja wa fasihi ya Kiswahili katika kuonyesha kwamba riwaya za kihalisiajabu zimeimarika zaidi katika kutumia dhana za jini uchawi na ushirikina kama ufundi au mtindo wa kifani.

# SURA YA KWANZA
# UTANGULIZI KWA UJUMLA

## 1.1 Usuli wa Mada

Kuibuka kwa riwaya mpya au riwaya ya kimajaribio kama inavyojulikana pia katika fasihi ya Kiswahili katika miaka ya hivi karibuni (hususan mwishoni mwa miaka ya 1980), kumeibua pia mambo mengi ambayo katika mitazamo fulani ya kiusomi yanaangaliwa kama visalia vya historia au mambo yaliopitwa na wakati. Mambo kama vile uchawi, ushirikina, ndoto zisizo na mantiki, uchangamano wa mambo ya uhai na ufu, upoteaji wa mipaka ya wakati, utumiaji na uibushaji wa matukio katika mandhari ya kutisha, wahusika wasio wa kawaida kwa mintarafu ya maingiliano ya kibinadamu, matukio ya kutisha na utumiaji mpana wa visasili, ni baadhi ya mambo yajitokezayo katika riwaya hizi za kimajaribio, na kwa upande mwingine, huu ndio wasifu wa riwaya ya kimajaribio katika fasihi ya Kiswahili, kama ambavyo inaendelea kudhihirika katika riwaya nyingi zinazoandikwa katika karne hii ya ishirini na moja.

Upya wa riwaya za kimajaribio unafungamana kwa karibu na uhalisiamazingaombwe ambayo, ni istilahi mpya katika fasihi ya Kiswahili, ila mtindo huu wa kiutunzi ni mkongwe na ulikuwepo katika fasihi simulizi hata kabla maandishi hayajagunduliwa (Senkoro 2007). Japo Said Mohamed anahoji kwamba ni mtindo mpya lakini si mtindo mpya ila tunaweza kusema ni istilahi mpya katika fasihi ya Kiswahili kama asemavyo Senkoro. Mashairi mengi na hadithi nyingi za mwanzoni kabla maandishi kugunduliwa yalitumia mbinu za uhalisiajabu katika kuelezea na kusifia matukio mbalimbali ya viongozi na mashujaa. Miongoni mwa masimulizi hayo ni masimulizi ya Fumo Liyongo kwa kumuonyesha ni mtu mkubwa wa kimo na wa kutisha ambapo katika hali ya kawaida si rahisi kumpata mtu wa aina hiyo.

Lakini kufikia mwishoni mwa karne ya kumi na nane na mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa kulikuwa na riwaya chache zilizokuwa zimetungwa na kushamiri matukio ya uhalisiajabu. Ni katika kipindi ambapo nchi nyingi za Afrika zilikuwa zikitawaliwa na wakoloni kwa hivyo kazi nyingi za kifasihi zilizokuwepo zilikuwa na matukio ya

kiuhalisiajabu kwa ajili ya kuwapumbaza Waafrika ili Wazungu waendelee kuwatawala. Kazi hizo ziliandikwa kwa lugha za kizungu na nyingine za kiulaya na Mashariki ya Kati na ziliweza kutafsiriwa hivyo hivyo hadi katika fasihi ya Kiswahili. Miongoni mwa kazi hizo ni riwaya ya *Sultani Darai* (1884), *Kibaraka* (1896), *Hekaya ya Johnson* (U.M.C.A, 1915) na *Alfu- Lela-Ulela* (1929). Riwaya hizi zilikuwa za vichekesho vyenye matukio ya kiajabuajabu japo hata kabla ya maandishi mambo haya ya kiajabuajabu yalikuwepo katika fasihi simulizi (Mulokozi 1996).

Kwa hivyo, utunzi wa fasihi ulioakisi uhalisiajabu ulikuwapo katika kipindi hiki japo si kwa kiasi kikubwa kama katika kipindi cha sasa. Katikati ya karne ya kumi na tisa (na hasa katika kipindi ambapo nchi nyingi za Afrika zilikuwa zinapambana ili kupata uhuru wao kutoka kwa wakoloni), ndipo tunaona baadhi ya kazi za fasihi zikianza kuandikwa kwa kutumia mbinu ya uhalisiajabu na kujenga taswira za kiajabuajabu katika kuelezea jinsi wakoloni hawa walivyowanyanyasa Waafrika katika nchi zao. Miongoni mwa riwaya zilizokuwepo kuwakilisha kipindi hiki ni pamoja na riwaya ya *Kufikirika* (1946*)*, *Kusadikika,* (1951*), Adili na Nduguze* (1952) za Shaaban Robert.

Shaaban Robert alitumia mifumo hii ya uhalisiajabu katika kazi zake ili kujenga taswira za kuonyesha na kuzungumzia mambo ya kutisha na ambayo katika hali ya kawaida hayawezekani. Kwa mfano, katika riwaya ya *Adili na Nduguze* ametumia mhusika Mrefu ambaye alikuwa na nguvu za kimiujiza, alikuwa na mapaja makubwa na mwili mkubwa na sauti kama ya radi, wasifu ambao japo si wa kawaida kwa binadamu, uhalisi ambao umo tu katika mipaka ya uwezekano. Maajabu mengine ni nduguze Adili kugeuzwa kuwa manyani. Pia katika riwaya ya *Kusadikika*, Shaaban ameonyesha na kuisawiri Kusadikika kama nchi inayoelea angani, wasifu wa kiajabu lakini unaoweza kufikirika. Shaaban Robert alitumia taswira nyingi za kiuhalisiajabu katika kazi zake kuonyesha jinsi mkoloni anavyotawala kwa kunyonya nchi zilizotawaliwa kwa kutumia hila na njia mbalimbali na kuziacha nchi hizo zikielea katika shida na mashaka. Japo pia alitumia taswira za kiajabu katika maswala mengine katika jamii lakini kwa kiasi kikubwa ilikuwa ni kuonyesha jinsi ukoloni unavyozitesa nchi za Afrika. Kwa hivyo,

Shaaban Robert alitumia taswira hii ya uhalisiajabu katika kuyaelezea mambo na matukio ya kipindi hicho.

Baada ya nchi nyingi za Afrika kupata uhuru, zilianza kutokea kazi nyingi zilizoandikwa kwa kukitwa katika mfumo huu wa uhalisiajabu ili kuzungumzia na kudadisi maswala ya ujenzi wa jamii mpya baada ya kung'olewa kwa ukoloni. Fasihi ya Kiswahili haikukwepa maswala ya uchawi na ushirikina kama njia ya kusimulia matukio ya kiuhalisiajabu na wakati huo huo kama mkakati wa kuhakiki maswala ya kijamii, kiuchumi, kisiasa pamoja na maingiliano ya ki binadamu katika jamii. Miongoni mwa kazi zilizotokea (japo haikuwa riwaya), ni *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali* (1968). Mtunzi wa kazi hii anasimulia matukio ya uchawi na ushirikina kiuhalisiajabu lakini kwa namna ya kuingazia jamii ya wakati wake. Katika kipindi hiki kulikuwa na riwaya pia zilizokuwa na matukio ya kiuhalisiajabu zilizosimulia mambo ya jiniuchawi na ushirikina. Miongoni mwa riwaya hizo ni pamoja na riwaya ya *Kurwa na Doto* (1960*)* ya Saleh Farsy, na riwaya ya *Mirathi ya Hatari (*1977) ya Mung'ong'o. Hizi ni miongoni mwa kazi ambazo ziligusa mambo ya kijamii kwa upande wa ushirikina na uchawi.

Mwanzoni mwa miaka ya 1990 miongoni mwa riwaya ambazo zilitumia mtindo wa taswira za kihalisiajabu katika kuendelea kuelezea maswala mbalimbali yaliyojitokeza katika jamii, ni riwaya ya *Nagon*a (1990) na *Mzingile* (1991) za Kezilahabi, *Ziraili* na *Zirani* ya Mkufya (1999), zilizotumia matukio ya kiuhalisiajabu. Lengo la kutumia mbinu hii ya kihalisiajabu ni kuelezea dhana ya maisha kwa kutumia falsafa ng'amuzi. Kwa hivyo, kuna haja kusema kwamba, watunzi hawa walitumia mambo ya miujiza na matukio ya kutisha na yasiyowezekana katika hali ya kawaida katika kuonyesha uwezekano wa kudadisi maswala ya kijamii na maisha kwa jumla kwa kina na kwa upana.

Kuanzia miaka ya 2000 hadi sasa, kumetokea kazi nyingi, hasa riwaya zinazojikita katika mtindo huu wa fasihi ya kimajaribio na mfumo wa uhalisiajabu ambapo

zimeingiza pia kipengele cha uhalisiajabu kama mtindo, mkakati na mbinu ya kiutunzi katika fasihi ya Kiswahili. Kwa hivyo, kipindi cha miaka ya 2000 kimedhihirisha kukua na kukomaa kwa riwaya ya kimajaribio ya Kiswahili kwa kuyazungumzia maswala ya maisha, mitagusano ya kijamii na maingiliano ya kisiasa na kiuchumi kwa kutumia mtindo huu wa kihalisiajabu. Mbinu hii imeendelea kutumika kama kigezo cha kujenga taswira katika kuyaelezea mambo mbalimbali katika jamii. Miongoni mwa kazi hizo ni riwaya za Saidi Mohamed za *Babu Alipofufuka* (2001), *Dunia Yao* (2006) na kwa kiasi *Mhanga Nafsi Yangu* (2012), riwaya za *Mafamba* (2008) na *Watu wa Gehenna (*2012) za Tom Olali, riwaya za *Musaleo! (*2004), *Bina-adamu! (*2002), *Zimwi la Leo* (2002) za Kyallo Wamitila. Hiki ni kipindi cha mabadiliko makubwa katika mkabala na mkondo wa kisanii unaokiuka kaida za uandishi zilizozoeleka kwa kiasi kikubwa. Waandishi hawa, mbali na kutumia uhalisiajabu katika tungo zao, hali kadhalika walikweza ubunifu na ushirikishwaji wa uhalisiajabu kwa kiasi kikubwa kama taswira na mkakati wa kuhoji na kupinga unafiki, usaliti, siasa zembe, ukoloni mamboleo na utandaridhi na matatizo ya ndani kwa ndani katika jamii zetu na pia matatizo kutokana na kani zinazotoka nje ya eneo la Afrika Mashariki.

Waandishi kama Said Mohamed, Tom Olali, Kyallo Wamitila, wanaweza kukisiwa kutumia mtindo wa kiuhalisiajabu kwa kuona kuwa mitindo ya kiutunzi na uhakiki uhalisia na uhalisia wa kijamaa haikuweza tena kuyaakisi maswala ya jamii na hivyo wakataka kuziba pengo lililokuwa limeibuka kwa kutumia mtazamo huu katika kuangazia maswala ibuka yanayokabili mataifa ya ulimwengu wa tatu kwa kutumia mtindo mpya uliosheheni ugothi, uhalisia wa kiajabu na nguvu za giza, ili kumwezesha msomaji kuielewa kwa kina dunia tunamoishi leo. Waandishi hawa wametumia uhalisiajabu kujenga taswira inayodhihirisha uwezekano katika kupiga vita nchi za Kimagharibi jinsi zinavyojinufaisha kwa kutumia utandaridhi wakati Waafrika wanaumia. Zamora na Faris (1995:3) wanahoji kuwa, waandishi wanaotumia mtindo huu wa kiuhalisiajabu wanafanya hivyo ili waweze kuzungumzia maswala ambayo hayangeweza kuzungumziwa au kwa uwazi kwa njia za kawaida au kwa mtindo wa kiuhalisia.

Katika kipindi cha karne ya ishirini na moja, zilijitokeza pia riwaya nyingi zilizohusu mambo ya uchawi na ushirikina japo hata huko miaka ya nyuma zilikuwepo lakini si sana. Riwaya hizo zilielezea hali halisi ya maisha ya watu katika jamii na jinsi jiniuchawi na ushirikina vilivyoshamiri zaidi katika jamii nyingi za kiafrika. Miongoni mwa riwaya zilizoandika kuhusu mambo ya uchawi na ushirikina kama kipengele kimojawapo cha uhalisiajabu ni riwaya ya *Kisura* (2009) ya Akberali Manji, *Usiku wa Balaa* (2015), *Vita vya Mapenzi* (2012), *Mzimu wa Waufi* (2013) na *Tanzia* (2015) za Maundu Mwingizi. Riwaya hizi zote zimejumuisha mambo ya uchawi na ushirikina lakini kwa uwelewa wetu hazikufanyiwa utafiti, hasa wa kuchunguza  na kukadiria ni kwa jinsi gani dhana ya uhalisiajabu inavyoendeleza maudhui anuwai ya kijamii kwa kutumia jiniuchawi na ushirikina kama mikakati ya kuchimuza maudhui hayo.

Ni dhahiri kwamba, baadhi ya riwaya katika vipindi na awamu mbalimbali za historia ya fasihi ya Kiswahili zimekuwa zikisimulia matukio ya kutisha na ambayo katika ulimwengu wa kawaida hayangewezekana, lakini kazi hizo ziliyafanya yawezekane kwani kazi hizi zilitumia mbinu hizi kama taswira katika kuyaelezea mambo mbalimbali yaliyokuwa yanahusika na maswala ya unyonyaji katika jamii, maswala ya falsafa ya maisha, na wengine walitumia kama mbinu ya kupamba lugha na kumvutia msomaji. Kwa hivyo, watafiti wengi waliofanyia utafiti riwaya hizi za kiuhalisiajabu waliona mbinu hii kama taswira ya kufikishia ujumbe wao, na wengine waliitumia mbinu hii ya uhalisiajabu kama nadharia mpya ya kujitosa katika udadisi wa kifasihi na kijamii. Pamoja na kwamba uhalisiajabu umetumiwa kwa mapana katika utunzi wa kazi za kimajaribio, ushirikishwaji wa jiniuchawi na ushirikina katika riwaya hizi za kimajaribio, unajitokeza kama upekee na upya wa kiutunzi unaostahili kuangaziwa kwa undani. Utumiaji wa jiniuchawi na ushirikina kama udhihirishaji wa uhalisiajabu, unajitokeza pia kama mkakati wa uchimuzi katika kuendeleza maudhui anuwai katika kazi teule.

Riwaya mpya za Maundu Mwingizi za *Vita vya Mapenzi* (2012), *Mzimu wa Waufi* (2013) na *Tanzia* (2015) zimo pia katika mfumo huu wa kiuandishi. Swala la jiniuchawi

na ushirikina linajitokeza na kutawala kwa upana wakati matini na wakati hadithi katika kazi hizi kiasi kwamba, tunashurutika kujiuliza, mwandishi huyu anadhamiria nini? Kwa nini amezama hivi katika mambo ya uchawi, ushirikina na majini? Je, mambo haya yanawasilishwa kama maudhui au yanatumiwa kama mbinu, mikakati na nyenzo za kutalii na kuwasilisha maudhui anuwai katika jamii? Maoni yetu ya awali ni kwamba kuna mambo mengi ambayo mwandishi anayazamia kwa sababu haielekei kwamba Maundu Mwingizi anajishughulisha na kujihusisha na jiniuchawi na ushirikina kwa ajili ya mambo hayo tu.

Utafiti huu unadhamiria kuliangalia swala la jiniuchawi na ushirikina kama mkakati wa uchimuzi katika riwaya za *Vita vya Mapenzi* (2012), *Mzimu wa Waufi* (2013) na *Tanzia* (2015) zilizoandikwa na Maundu Mwingizi. Jiniuchawi na ushirikina, kama kipengele kimojawapo katika uhalisiajabu kimetumika kimkakati kuweza kuchimuza maudhui mbalimbali katika riwaya za Maundu Mwingizi. Jiniuchawi inaweza kufafanuliwa kuwa ni ile tabia ya mtu kuwatesa wengine au kuwa na tabia za kutumia vitu vya ajabuajabu katika mazingira fulani ya kutisha na kuogopesha katika hali ya kawaida. Jiniuchawi hufanya mambo yake katika ulimwengu usio wa kawaida na wakati mwingine jiniuchawi hutumika kuwatesa wengine kwa njia za kimazingara. Ushirikina, kwa upande mwingine ni kule kuamini uwezo na mambo ya jiniuchawi na kutafuta mbinu ya kujinusuru kwa kutumia baadhi ya majini (Omari 1993). Hata hivyo, Shorter (1988) anasema dhana ya jiniuchawi na ushirikina hufanana katika tabia zao, kwa sababu zote hutegemea jiniuchawi. Katika kazi za kifasihi, mbinu hii imetumika na wanafasihi wa kimajaribio katika kuonyesha mambo mbalimbali yanayotendeka katika jamii, hali kadhalika kuonyesha athari chanya na hasi za matendo hayo, kwa hivyo mambo haya yametumiwa kama mkakati na dhana inayowezesha uchimuzi uelezaji wa mambo mbalimbali katika jamii, mifumo ya kimahusiano na utangamano wa kijamii.

Jiniuchawi na ushirikina ni vipengele vya uhalisiajabu, au pia ni uhalisiajabu ambao katika maandishi ya kiubunifu hutumika kama uchimuzi wa kuendeleza maudhui mbalimbali. Uhalisiajabu ni dhana iliyobuniwa na msanii wa Ujerumani Franz Roh, na

inahusishwa na waandishi wa Marekani ya Kusini au hata nchi zinazoitwa Ulimwengu wa Tatu, na hutambulishwa na sifa mbalimbali. Sifa hizi ni za kuyaelezea matukio ya kifantasia au ya kiajabu au kichawi na kishirikina kwa namna ya moja kwa moja na kwa namna inayoyafanya yaonekane kama ya kawaida tu (Wamitila 2003). Tunapojadili dhana hii ya jiniuchawi na ushirikina hatuwezi kutoka nje katika swala zima la uhalisiajabu, kwani ndani ya uhalisiajabu ndipo tunapopata kipengele hiki cha jiniuchawi na ushirikina na kipengele hiki kimeweza kubeba vipengele vingine ndani yake kama vile maswala ya kindoto, mandhari za kutisha, wahusika wasio wa kawaida na matukio ya kutisha ambapo vitu vyote hivi tunavikuta katika uhalisiajabu. Vitu hivi vyote vimeweza kuchimuzwa na mwandishi na kutupa maudhui mbalimbali. Kwa hivyo, dhana hii jiniuchawi na ushirikina ni kama mbinu na mkakati wa kujua mambo mbalimbali yanayotendeka katika jamii.

Riwaya ambazo tumezitumia, kwa mujibu wa maelezo tuliyoyatoa hapa, ni riwaya za kimajaribio au "riwaya mpya", kwani zimetungwa kwa mtindo ambao unahusisha majaribio au matumizi ya sifa zinazoelezwa kama za kimajaribio (Wamitila 2008:127). Hii ina maana kuwa ni hali ya kimajaribio katika utanzu wa riwaya ya Kiswahili, kutoka mitindo iliyozoeleka. Hali hii imepelekea utunzi wa kazi za fasihi kupata mabadiliko chanya ili kuepuka kupooza kutokana na mitindo iliyozoeleka na pia kuweza kukabiliana na mabadiliko kadhaa yanayozikumba jamii zetu za sasa. Waandishi nao hawajakuwa nyuma katika kuendana na haya majaribio katika kuandika riwaya ambazo zinatumia mbinu ya jiniuchawi na ushirikina kama mkakati wa kuyaeleza matatizo mbalimbali ya kijamii, kitamaduni, kiuchumi, kisiasa, kielimu na kitekinolojia katika jamii tunamoishi. Kutokana na majaribio hayo, waandishi wa riwaya wamehimizika na hivyo wamesababisha mabadiliko ya kimaudhui na kifani.

Dhana ya uchimuzi katika utafiti wetu vilevile imetumika kama mbinu ya kuweza kuonyesha na kuweka wazi mbinu hii ya jiniuchawi na ushirikina kama ilivyotumiwa na waandishi. Uchimuzi huhusu kufanya sifa fulani zijitokeze wazi zaidi au zibainike zinapoangaziwa kwa usambamba na usuli wa sifa husika. Vilevile mbinu hii hutumika

kuyadokeza mambo fulani au sifa fulani katika kazi za kifasihi kwa namna ya wazi au kuyafanya yajitokeze waziwazi yakilinganishwa na mengine. Mbinu hii hutumiwa na waandishi mbalimbali kusisitiza mambo fulani yanayoonekana kuwa muhimu au yenye uzito katika kazi fulani za kifasihi (Wamitila 2003).

Dhana ya uchimuzi ni dhana ambayo imeibuka kuwa moja ya sifa bainishi za riwaya ya kimajaribio, riwaya ambazo zimesheheni mambo ya kiuhalisiajabu yaani zimebeba mambo yenye ujiniuchawi na ushirikana pia kama nguzo au mkakati wa kuyaelezea mambo mbalimbali yanayotendeka katika jamii kwa kupitia fasihi ya Kiswahili. Hii inatokana na ukweli kwamba, katika riwaya zilizojitokeza tangu miaka ya 1990 ambazo zinahesabiwa kama za kimajaribio zilizosheheni mambo ya kiuhalisiajabu, uchimuzi unajitokeza kwa uwazi. Japo mbinu hii ya uhalisiajabu katika fasihi ya Kiswahili ni istilahi mpya, isipokuwa mtindo ni mkongwe ambao ulikuwepo katika fasihi simulizi hata kabla maandishi hayajagunduliwa lakini mtindo huu haukuwa na mashiko kwa kiasi kikubwa kama sasa na haukuweza kutumia mbinu ya uchimuzi katika kuyaeleza mambo mbalimbali katika jamii.

Waandishi waliotumia mtindo wa kiuhalisiajabu waliona kuwa mitindo ya uhalisia hakiki na uhalisia wa kijamaa haikuweza tena kuyaakisi maswala ya jamii na hivyo wakataka kuziba pengo kwa kutumia mtazamo huu katika kuangazia maswala ibuka yanayokabili mataifa ya ulimwengu wa tatu, kwa mtindo wa kipekee uliosheheni ugothi, uhalisia wa kiajabu na nguvu za giza, ili kuwezesha msomaji kuielewa dunia tunamoishi leo. Waandishi hawa wametumia taswira hii ya uhalisiajabu katika kupiga vita nchi za Magharibi jinsi zinavyojinufaisha kwa kutumia utandaridhi wakati ambapo Waafrika wanaumia. Zamora na Faris (1995:3) wanasema waandishi hawa hutumia mtindo huu wa uhalisiajabu ili waweze kuzungumzia maswala ambayo hayangeweza kuzungumziwa kwa uwazi kwa njia ya kawaida au kwa mtindo wa kiuhalisia. Kwa hiyo, uhalisiajabu unapoegemezwa katika jiniuchawi na ushirikiana unakuwa ni ufundi au mtindo wa uchimuzi katika kuzungumzia maswala tata au nyeti ya kijamii.

Kutokana na ushahidi uliopo ni kwamba, watafiti wengi hawakuweza kuchambua dhana hii ya jiniuchawi na ushirikina kama fani au mkakati wa uchimuzi katika kuangalia kazi ambazo zimejikita katika maswala ya jiniuchawi na ushirikina kuwa ni swala moja la kimsingi katika utanzu huu. Matumizi ya jiniuchawi na ushirikina kama mtindo wa kifani ni tatizo linalohitaji utafiti. Na tatizo hili linaweza likawa linagusa kwa kiasi kikubwa sana jamii katika maswala mbalimbali. Kwa kuwa ni vitu ambavyo vipo sana katika jamii ndiyo maana hata waandishi wanaviandika na vinahitaji kufanyiwa utafiti wa kifasihi ili kujua ni kwa nini waandishi hawa wanasimulia matukio haya ya jiniuchawi na ushirikina kwa njia ya kutisha zaidi katika kazi hizi zenye jumbe za jiniuchawi na ushirikina. Tafiti zilizotangulia yaani za Mugwika (2012), Wanjiru (2013), Vutagwa Magaju (2013), Nyabunga (2005) kama hazikuweza kuchambua jiniuchawi na ushirikina katika riwaya zilizojikita kama mikakati ya uchimuzi katika kuangalia maudhui mbalimbali yanayopatikana katika jamii. Kwani walijikita zaidi katika kipengele cha uhalisiajabu cha ndoto na mizuka. Labda ni kutokana na mambo ya usasa ambayo yamesababisha watu kuona kuwa hakuna haja ya kufanyia utafiti mambo yanayohusiana na uchawi na ushirikina. Kwa hivyo, utafiti huu umeshughulikia swala hili ili kujua watunzi wenye jumbe hizi zenye mambo ya jiniuchawi na ushirikina katika riwaya ya kimajaribio wanawasilisha tu mambo hayo ya jiniuchawi na ushirikana au wametumia mambo haya kama mbinu na mkakati wa uchimuzi kutuwezesha sisi kama wasomaji kuona uanuwai wa maudhui katika ulimwengu uliopo au ulimwengu uwezekanao.

## 1.2 Tatizo la Utafiti

Utafiti huu umeangazia swala la jiniuchawi na ushirikina kama vipengele vya uhalisiajabu, ambapo uhalisiajabu katika maandishi ya kiubunifu hutumika kama uchimuzi wa kuendeleza maudhui mbalimbali. Pia tumeangazia "jiniuchawi na ushirikina kama mbinu, mtindo na mkakati wa uchimuzi katika kuendeleza maudhui ya aina mbalimbali katika jamii". Utafiti huu unachochewa na uelewa wetu kwamba, japo kuna watunzi wa kazi za fasihi waliotumia mifumo ya kiutunzi inayoakisi dhana ya uhalisiajabu na uchimuzi katika riwaya mpya ya Kiswahili, mbali na kuwa watunzi wa

riwaya mpya hujitambulisha kutokana na sifa anuwai, uchimuzi, jiniuchawi na ushirikina zinajitokeza kama sifa zinazopewa kipaumbele zaidi kuliko hizo sifa nyingine, kwani, ndiyo mihimili mikuu ya maudhui katika riwaya za Maundu Mwingizi. Japo watunzi wa riwaya nyingi za Kiswahili wameandika mambo ya jiniuchawi na ushirikina, hakuna watafiti ambao wamefanyia utafiti swala hili la jiniuchawi na ushirikina kifani kama mkakati wa uchimuzi katika kuonyesha na kuhakiki maudhui mbalimbali katika muktadha wa uchanganuzi wa uhakiki wa kazi za fasihi andishi ya Kiswahili.

**1.3 Maswali ya Utafiti**

i. Je, mandhari na matukio ya jiniuchawi na ushirikina yanayojitokeza katika riwaya hizi yanatumiwa kuchimuza maudhui ya aina gani katika riwaya teule za Mwingizi?
ii. Je, wahusika wa jiniuchawi na ushirikina wameweza kuendeleza maudhui ya aina gani katika riwaya teule za Mwingizi?
iii. Je, ni maudhui yapi yaliyochimuzwa katika riwaya teule za Mwingizi kupitia ishara na uashiriaji wa aina mbalimbali?

**1.4 Madhumuni ya Utafiti**

Utafiti huu unaangazia madhumuni yafuatayo;

i. Kuonyesha mandhari na matukio ya kijiniuchawi na kishirikina yalivyochimuza na kuendeleza maudhui mbalimbali katika riwaya teule za Mwingizi,
ii. Kubainisha jinsi wahusika wa kiuhalisiajabu walivyotumiwa kimkakati kwa kuhusianishwa na vipengele vya jiniuchawi na ushirikina kuchimuza na kuendeleza maudhui anuwai katika riwaya teule za Mwingizi,
iii. Kuchanganua ishara na uashiriaji kama mikakati ya uchimuzi katika kuibua maudhui mbalimbali katika riwaya teule za Mwingizi.

### 1.5 Sababu za Kuchagua Mada

Tafiti nyingi zilizofanywa katika fasihi ya Kiswahili kama zile za Nyabunga (2005) Vutagwa (2013), Wanjiru (2013), zilijikita katika uhalisiajabu kwa ujumla na hazikulipa kipaumbele swala hili la jiniuchawi na ushirikina, kama mkakati wa uchimuzi katika fasihi ya Kiswahili. Japo Sanchez (2000),) Schwalm (2009) na Babalola (2016) walilielezea sana swala zima la uhaliasiajabu kwa kadri lilivyozagaa katika fasihi za kilimwengu lakini riwaya za Kiswahili hazikujumuishwa, ila swala hili liliongelewa katika riwaya zilizoandikwa kwa Kiingereza. Aidha, hata kwa wale waliojadili swala la uchawi na ushirikina hawakuweza kulijadili kama ni mada kuu, ila waliweka mahitimisho yao juu ya mambo haya kama kipengele kidogo katika uchambuzi wao wa makala na kuonyesha jiniuchawi na ushirikina kama utamaduni wa kizamani katika makala zao (Mukuthuria 2007). Kumbe mambo haya ya jiniuchawi na ushirikina yanakwenda mbali zaidi na hapo, kwani yanabeba maudhui mbalimbali sio tu ya uchawi na ushirikina, bali pia maudhui yanayoakisi usasa na maswala ibuka katika jamii zetu. Kwa hivyo, kunazo haja za kiusomi zinazoshurutisha kulipa swala hili uzito zaidi kwa kuangalia jinsi mbinu zilizotumika kusimulia matukio haya ya jiniuchawi na ushirikina zinavyoathiri, kwa upande mmoja uendelezaji wa maudhui ya jiniuchawi na ushirikina, na kwa upande mwingine, jinsi ambavyo mbinu hii ya jiniuchawi na ushirikina imetumika kimkakati kama mbinu na nyenzo ya kuendeleza maudhui anuwai katika kazi teule.

Halikadhalika, kwa kuwa utafiti huo wa awali haujaweza kujibu maswali yote kuhusu jiniuchawi na ushirikina, hata hivyo tumeonyesha jinsi ambavyo jiniuchawi na ushirikina ni mkakati wa uchimuzi katika kuendeleza sio tu maudhui ya jiniuchawi na ushirikina, bali pia maudhui anuwai katika mapana na marefu ya jamii. Utafiti huu umeonyesha kwamba swala zima la uhalisiajabu linaweza kutazamwa katika mitazamo mbalimbali na wala sio tu kutazamwa kama maudhui katika upekee wake. Kwa njia hii tumeonyesha kwamba utafiti huu utachochea tafiti nyingi za baadaye zitakazohalalisha uhalisiajabu na vipengele vyake kama mambo yaliyo na umuhimu mkubwa wa kiutunzi na usomaji wa riwaya ya kimajaribio. Ni matumaini yetu kuwa utafiti huu utaamsha ari

mpya kwa wale watakoamua kutumia jiniuchawi na ushirikina na uchimuzi katika kuchambua kazi mbalimbali za fasihi.

Japo kumekuwa na uandishi wa kazi za kutosha katika fasihi ya Kiswahili zinazoegemezwa au zinazozungumzia maswala ya uchawi na ushirikina, wanataaluma wengi wameonekana kutolipa kipaumbele swala hili la jiniuchawi na ushirikina katika kulifanyia utafiti. Labda ni kwa sababu ya maendeleo na mambo ya utandawazi ndio maana swala hili likapuuzwa na kuonekana ni la kishamba. Tumeona ni vyema tulifanyie utafiti kwa kuuliza ni kwa nini limekaidi kupembezwa katika hali hizi za uwazi, kwani mbinu hii imekuwa ikitumika katika kudadisi na kufikisha ujumbe fulani katika jamii unaohusianishwa sio tu na uchawi na ushirikina, bali pia maswala nyeti ambayo yanachimuzwa kupitia dhana hizi za jiniuchawi na ushirikina. Maswala hayo ni kama migongano ya kisiasa, maswala ya imani za kitamaduni na imani za kidini, kiuchumi na kitamaduni na ambayo yameangaliwa kwa kina. Kwa hivyo tumeona ni muhimu kulifanyia utafiti swala hili.

Katika utafiti huu tumelipa uzito swala hili kutokana na sababu kwamba, mambo ya uchawi na ushirikina hayajajadiliwa katika tafiti zilizotangulia kwani watafiti wengi waliegemea katika dhana ya uhalisiajabu kwa ujumla na kuona jiniuchawi na ushirikina kama kipengele tu na kukijadili kwa kiasi kidogo sana. Kwa mfano, katika riwaya ya *Vita vya Mapenzi* Mzee Sufian, Mzee mwenye asili ya kiasia anasababisha ajali ya basi kwa njia ya kiuchawi na anaonekana amekufa lakini baadaye anatokea sehemu nyingine akiwa mzima. Utukiaji huu wote ni katika kuchimuza dhamira za mataifa yaliyoendelea jinsi yanavyoziangamiza nchi ambazo hazijaendelea kwa kutumia vitu na mambo mbalimbali na wao kuendelea kuneemeka. Watafiti waliotangulia pia katika swala la ushirikina hawakuweza kulijadili kwa kina, kwani jiniuchawi na ushirikina unaweza ukawa ni mkakati wa uchimuzi katika kuelezea maudhui mbalimbali yanayopatikana katika jamii kupitia riwaya teule za Mwingizi. Ikizingatiwa kwamba riwaya hizi ni mpya, yaani za kimajaribio katika usomaji wetu wa kazi mbalimbali hatukuona tafiti zozote zilizofanyia riwaya hizi teule.

## 1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu umejifunga katika kushughulikia tu swala la uchimuzi na jiniuchawi na ushirikina kama vipengele katika uhalisiajabu vinavyohusika kama mkakati wa kuibua maudhui katika riwaya teule za Mwingizi. Utafiti huu umeongozwa na nadharia za Uhalisiajabu na Semiotiki ili kutoa ushahidi wa kutosha kuthibitisha kauli na madai yetu. Pia utafiti umeshughulikia vipengele vikuu vinne ambavyo ni vipengele vya jiniuchawi na ushirikina ambavyo vimewezesha uchimuzi wa maudhui anuwai katika riwaya za Maundu Mwingizi, mandhari na matukio ya kijiniuchawi na kiushirikina na jinsi yalivyochimuza na kundeleza maudhui mbalimbali katika riwaya, kubainisha jinsi wahusika wa kijiniuchawi na kishirikina walivyoweza kuchimuza na kuendeleza maudhui katika riwaya za hizi na kujadili jinsi ishara na uashiriaji kama mikakati ya uchimuzi katika riwaya teule za Mwingizi. Sababu ya kufanya utafiti huu kwa kujikita katika malengo haya ni kwamba tumeonelea kuwa maeneo haya tuliyoyachagua ndiyo yameweza kujibu maswali ya utafiti huu vizuri katika kuonyesha jinsi jiniuchawi na ushirikina vilivyotumiwa kama mikakati ya uchimuzi katika kuendeleza maudhui mbalimbali ya kijamii katika riwaya teule.

Aidha, utafiti huu haujajishugulisha na maswala mengine kama vile ploti na muundo wa riwaya isipokuwa tu pale mambo ya muundo yalipoonekana kuwa sehemu ya uchimuzi. Pia katika swala la upatikanaji wa data, utafiti huu umetumia mbinu ya usomaji maktabani tu. Katika mbinu hii ya maktabani tumesoma riwaya husika za Maundu Mwingizi, tumesoma na kuchanganua tasnifu mbalimbali, makala mbalimbali na vitabu vinavyohusiana na mada za uchimuzi, ujiniuchawi na ushirikina. Sababu ya kusoma makala, tasnifu na vitabu vinavyohusiana na mada ni ili kuelewa vizuri na kuzidhibiti nadharia zetu tulizoitumia na hasa teneti zilizo na mahusiko ya moja kwa moja kushadidia kauli zetu, uhusiano na ufasiri wa jinsi swala la uchawi na ushirikina linavyojibainisha na jinsi katika ujitokezaji huo linavyochimuza dhamira na maudhui anuwai. Hali kadhalika kumetuwezesha kubaini mapengo mbalimbali yanayopatikana katika tafiti zilizotangulia na ambayo yamesababisha tufanye utafiti huu.

### 1.7. Msingi wa Nadharia

Utafiti huu umeongozwa na nadharia kuu mbili, nadharia hizo ni za Uhalisiajabu na Semiotiki. Sababu ya kutumia nadharia mbili ni kutokana na sababu kwamba, nadharia moja isingeweza kukidhi upekee wa utafiti, ikizingatiwa kwamba, utafiti unaelekea kukita kuwili—katika maswala ya uhalisiajabu na katika maswala ya uishara na uashiriaji, kwa sababu hii inahalalisha kutumia nadharia mbili.

#### 1.7.1 Nadharia ya Uhalisiajabu

Uhalisiajabu unaelezwa kuwa ni nadharia ya fasihi ambapo mambo ya ajabu, mambo yaliyo nje ya mipaka ya ukawaida na matukio ya kutisha, yanachukuliwa na kutazamwa kama mambo ya uhalisia na ya kawaida tu. Uhalisiajabu ni dhana iliyobuniwa na kuasisiwa na msanii, mchoraji wa Ujerumani, Franz Roh, katika kitabu chake *Nach-expressionismus, magischer Realismus.* Nadharia hii ilibuniwa mwanzoni na Franz Roh (1925), mhakiki wa Kijerumani aliyekuwa anajishughulisha na sanaa ya uchoraji kama njia ya kukabiliana na mfumo wa uchoraji uliojikita katika misingi ya uhalisiafifi. Uchoraji huo ulidhihirisha uhalisia wa kufikirika tu, wa kiajabu, kindoto na wakati mwingine wa kimazingaombwe. Aina hii ya uhalisia iliingia katika uhakiki wa fasihi bunifu katika miaka ya 1940 kama njia ya kuchanganua na kuhakiki fasihi inayochanganya mambo ya kihalisi na mambo ya kimiujiza au kimazingaombwe na kwa njia hii ikaishia kujenga tajriba changamano. Uhalisia huu ulishamiri sana katika fasihi za Latini Amerika ambapo kazi ziliandikwa katika mtindo huo wa kimazingaombwe ili kuonyesha uhalisia wa maisha kama unavyodhihirka kwa mara kwanza. Kazi maarufu katika mtindo huu ni kazi ya mwandishi maarufu Gabriel Garcia Marquez, *One Hundred Years of Solitude* (1971).

Vilevile, nadharia hii iliweza kujitokeza hata katika fasihi zilizotungwa katika nchi zinazoitwa Ulimwengu wa Tatu na hutambulishwa na sifa mbalimbali. Sifa hizi ni za kuyaelezea matukio ya kifantasia au ya kiajabu au kichawi kwa namna ya moja kwa moja na kwa namna inayoyafanya yaonekane kama ya kawaida tu yaani, mpaka uliopo kati ya mambo yanayoweza kupatikana katika ulimwengu halisi na yasiyowezekana huwa mdogo sana (Wamitila 2003).

Roh (1925) alitumia neno uhalisiajabu katika muktadha wa ulimwengu wa sanaa kueleza aina fulani maalum ya kudhihirisha usiri ulioko kwenye maisha ya kila siku bila kuuliza maswali yoyote ya uhalisia huo. Pamoja na hayo uhalisiajabu katika kazi ya sanaa hushughulika na kazi zinazoambatana na zisizoambatana na ujumi wa uhalisia. Jambo hili limejidhihirisha katika riwaya za Maundu Mwingizi kwani zimetumia mambo ya kichawi na kishirikina katika kuangazia mambo mbalimbali katika jamii ambayo katika hali ya kawaida hayangeweza kuzungumziwa.

Chanady (1985) anasema kwamba uhalisiajabu unahusu matukio yasio ya kawaida, ya kimiujiza au chochote kilicho kinyume na uhalisia wa kawaida. La muhimu zaidi ni kwamba matukio yanayotendeka katika uhalisiajabu hayawezi kujitenga na uhalisia kama unavyoeleweka katika miktadha ya ukawaida. Haya ni matukio yasiyo ya kawaida, ya kimiujiza na ni kinyume cha uhalisia wa kawaida. Istilahi ya ‘uhalisiajabu' mwanzoni ilihusishwa na wachoraji katika miaka ya 1920, inatumika kufasili kazi za bunilizi za kinathari za Jorge Luis Borges wa Argentina, na hali kadhalika kazi za waandishi kama vile Gabriel Garcia Marquez wa Colombia, Gunter Grass wa Ujerumani, Italo Calvino wa Italia, Isabel Allende wa Chile na John Fowles wa Uingereza. Waandishi hawa wanasukanisha uhalisia uliochongwa kwa njia maalum katika ruwaza inayobadilikabadilika daima. Waandishi hawa waliwakilisha matukio ya kawaida kwa maelezo ya kina sambamba na vipengele vya kifantasia na kindoto, kwa kutumia mambo yaliyotokana na visasili na hekaya (Abrams 1971).

Uhalisiajabu ni nadharia ambayo inakiuka sifa za uhalisia kama waandishi wa karne ya kumi na tisa na ishirini wanavyoeleza. Katika uhalisiajabu, matukio yasiyoaminika ya (kifantasia) husawiriwa kama mambo ya kawaida. Mambo ya kiajabu yanaelezwa kwa namna ya moja kwa moja na kuonekana kuwa ya kawaida. Hali ya kushangaza na kuogofya huwasilishwa kuwa ya kawaida katika uhalisiajabu; ndoto na uhalisi vinachanganywa (Njogu na Wafula 2007). Tunaona kwamba, vipengele vya nadharia hii hasa vipengele vinavyoashiria maana ya nadharia hii, vimetuwezesha kuweka wazi maswala yanayohitaji msisitizo, vimetuwezesha kuona kwa undani palipo na ukawaida

na palipo na uajabuajabu. Kwa hivyo, nadharia hii imetusaidia katika uchambuzi wetu wa kazi teule, kwani kuna mambo mengi ya ajabuajabu yanayopatikana katika riwaya teule kama yanavyozungumziwa katika nadharia hii, yakiwemo mambo ya kindoto, mambo ya majini na wachawi kujitokeza katika mazingira ya kiajabuajabu na kuwatesa baadhi ya wahusika katika riwaya teule. Mfano ni wahusika Masumbuko na Suhail katika riwaya ya *Mzimu wa Waufi na Vita vya Mapenzi*.

Uhalisiajabu kama ‘kile kinachotendeka wakati ambapo ukweli wa ndani wa mandhari ya juu unapoingiliwa na kitu ambacho ni cha kiajabu kuaminika'. Uhalisiajabu hutumia mbinu za kifasihi simulizi ambazo ni uajabu, umazingaombwe na ufantasia kuonyeshwa kuwa kawaida (Strecher, 1999). Maelezo haya yameweza kudhihirika pia katika kazi zetu teule kwani kunakuwa na mandhari ya kutisha sana, mandhari ya chini baharini, mandhari ya kufikirika, mandhari ya makaburini na kukumbana na vitu vya ajabuajabu. Mandhari ya jiniuchawi na ushirikina imeonekana kwa kiasi kikubwa kuwa imechangia katika uendelezaji wa maudhui mbalimbali katika riwaya teule za Maundu.

Kutokana na kazi za Zamora (1993) na (1995), Danow (1995), Cooper (1998) na Encarta encyclopedia (2002), ufuatao ndio muhtasari wa baadhi ya mihimili ya nadharia ya uhalisiajabu. Mosi, simulizi zote hutegemea uhalisia ambapo kazi za fasihi za uhalisiamazingaombwe husimulia mambo ya kiajabu na ya kutisha kwa namna ya ukawaida na uhalisia. Mathalani, mtu anaweza kuingiwa na inzi tumboni na kuharisha lundo la wadudu hao au marehemu akaweza kuongea. Ni vizuri kuweka wazi kuwa waandishi wa mrengo huu hawavumbui ulimwengu wao mpya bali wanafunua na kufichua mambo ya miujiza na maajabu katika ulimwengu huu huu wa kawaida. Kwa hivyo, yanakuwa matokeo ya kiajabuajabu yanayoonekana ya kawaida, simulizi za kiuhalisiajabu hutawaliwa zaidi na mawazo ya kinjozi, hivyo katika matini ya uhalisiajabu jambo lolote linaweza kujiri, kwa maana kwamba kanuni na kaida za maisha ya kawaida ya kila siku zinaweza kuvunjwa wakati wowote. Mathalani, mtu aliyelala ndani anaweza kujikuta yuko nje asubuhi, wakati mwingine mtu anaweza kuota mbawa na kupaa kama ndege au hata mjusi anaweza kukusemesha kwa lugha

fasaha ya ki binadamu. Wandishi hawa wanalenga kutukumbusha kuwa pamoja na kuwa tunaishi maisha ya kawaida tukilala, kuamka, kufanya kazi na kula lakini yapo maisha ya upande wa pili yaliyosheheni wazimu na maajabu. Mfano mzuri katika utafiti wetu ni pale tunamuona mhusika Nyanzala katika riwaya ya *Tanzia* amekufa lakini akawa anatokea duniani kiuchawi na kuwaambia ndugu zake kwamba, huko aliko anateseka sana halafu anapotea tena ghafla.

Pili, simulizi za uhalisiajabu hushikanishwa na uongo, hekaya na visasili, ambapo waandishi wa uhalisiamazingaombwe aghalabu hupata mvuto, msukumo na nyenzo za taarifa kutoka katika visasili vya zama za kale, visasili vya maisha ya sasa na hata visasili vya imani za kidini, hivyo basi waandishi hawa huegemeza simulizi zao kwenye visaasili hivi kama vyanzo vya masimulizi yao. Katika kazi zetu teule tunaliona jambo hili pia kwani mwandishi anawaonyesha baadhi ya wahusika wakipatwa na mambo ya majini na haya ni mambo yanayowapata kutokana na visasili vya mababu zao katika riwaya za *Vita vya Mapenzi* na *Mzimu wa Waufi*

Tatu, uhalisi na ndoto vinachanganyika. Hakuna mipaka ya uhalisi na ndoto katika uhalisiajabu. Labda wakati mtu anapoota ndipo yupo uhalisini na wakati yupo uhalisini ndipo yumo ndotoni. Ni kawaida kukuta mchanganyiko wa maisha ya ndoto na maisha ya halisi, hali za kufikirika kusiko halisi na zile za uhalisia. Haya yote yanageuzwa na kuchangamana bila kuonyesha mipaka kati yao. Hapa unaweza kukuta matukio yakitukia wakati mtu amelala ama yumo mawazoni na wakati huo huo tukio likitukia katika hali halisi. Hivyo mipaka ya kijamii, kitaifa na kimataifa huvunjwa, maanake ni kuwa wanauhalisiajabu wanajadili mambo yanayohusu ulimwengu kwa jumla bila kujiweka katika mazingira finyu kama vile ya jamii, nchi au bara moja. Hii imetokea katika kazi zetu zote kwa wahusika karibu ya wote.

Nne, wakati na mahali huwa na uhusiano wa kiduara, badala ya kistari. Inamaanisha kwamba, jambo linaweza kujirudia kwa sura nyingine mahali pengine. Ni kweli kwani hali hii inajidhihirisha katika riwaya teule. Tano, matukio hayafuatani kimantiki kama

ilivyo kawaida. Mitindo ya baadhi ya tanzu za fasihi simulizi hutumika. Jambo hili hufanywa kwa kumpeleka msomaji kwenye safari ya hali na matukio ya kikweli na yanayowezekana. Aidha, wasanii hutumia mbinu ya ukumbukaji, mbinu rejeshi, mtiririko wa urazini na ujenzi wa wahusika wenye nafsi mbili. Sita, mazingira ni sehemu muhimu sana katika aina hii ya fasihi. Wanyama, majitu, misitu mikubwa yenye giza totoro, wanyama hatari na mazimwi hurejelewa. Vilevile, mimea, mito, maziwa na bahari huchukua nafasi muhimu katika uandishi wa uhalisiajabu. Haya yote yamedhihirika katika riwaya zote zinazoshirikishwa katika utafiti huu kwani kumekuwa na ujitokezaji wa mazingira ya kutisha sana. Saba, uhalisiajabu unapinga uhusiano wa kadhia zinazotendeka katika maisha ya mtu kiutengano. Hali mbalimbali kama vile za uhalisi na ndoto, kifo na uhai, usasa na uzamani, shamba na mjini, ugeni na utamaduni huonekana zikiingiliana. Pia tukiangalia katika riwaya zetu teule tunaona maswala haya ya ndoto, kifo na uhai yanadhihirika pia, na kwa hivyo mhimili huu umetufaa.

Mihimili hii imesadifu katika utafiti huu kwani mambo yanayojadiliwa katika mihimili hii yameonekana kwa kiasi kikubwa katika kazi teule. Miongoni mwa mambo hayo ni pamoja na tunapozisoma riwaya hizi teule, pamoja na kuichunguza mihimili ya nadharia ya uhalisiajabu, tunaona kuwa, nadharia hii inafaa katika kuchunguza mada yetu ya utafiti. Vipengele vingi vya nadharia hii vinafungamana na vipengele vingi katika riwaya zilizoshughulikiwa. Kwanza, kuna matukio ya kiajabu na ya kifantasia ambayo ni mojawapo ya sifa za jiniuchawi na ushirikina. Matukio haya yanatokea kupitia kwa wahusika na kuzua hali ya kuogofya, kuduwaza na kushangaza. Pili, uhalisi na ndoto vimechanganyika, nayo ni sifa muhimu sana katika uandishi wa kiuhalisiajabu. Mandhari za aina hii zimeonyesha sifa ya utokaji kwenye ulimwengu halisi na kuingia kwenye ulimwengu wa kimawazo, ulimwengu wa kufikirika tu, kisha labda kurudi kwenye ulimwengu halisi.

Tatu, kuna matukio mengi yasiyofuatana kimantiki jinsi ilivyozoeleka kwa sababu ya mvunjiko katika usimulizi. Hadithi za riwaya hizi zina visa vingi ambavyo vinatokea katika kiza kikuu. Mtunzi amefanya hivi kupitia mbinu ya urejeshi, kumbukizi na pia

kujenga wahusika wenye nafsi mbili. Nne, kazi ambazo tunazichambua zina mazingira ya kutisha na kuogofya moja ya mihimili yetu isemavyo na pia kazi hizi zimechanganya baadhi ya tanzu za fasihi simulizi kama vile nyimbo, misemo na kadhalika. Mandhari ya kijiniuchawi na kishirikina ya aina hii imeonekana katika riwaya zetu na imechangia kwa kiasi kikubwa katika kujenga au kuendeleza maudhui mbalimbali kwa kutumia mbinu ya uhalisiajabu. Mihimili hii ya Nadharia ya Uhalisiajabu inaoana na hali halisi za riwaya teule, jambo ambalo limetufanya tuone nadharia hii kuwa ni mwafaka kwa utafiti wetu kwani mihimili hii imetuwezesha kuweka wazi maudhui na mitindo mbalimbali ya kibunifu katika kufikisha jumbe mbalimbali katika jamii.

### 1.7.2 Nadharia ya Semiotiki

Kwa sababu ya hali halisi ya utafiti huu, nadharia ya uhalisiajabu haikuweza kujitosheleza kuwajibikia maswala yote ibuka katika utafiti huu unaokita kwingi, ndio maana ikasaidiwa na nadharia ya semiotiki hasa katika uchambuzi wa sura ya tano japo hata katika sura nyingine imetumika kwa kiasi kidogo. Semiotiki ni nadharia inayotumika katika uchambuzi wa taaluma zinazohusiana na maswala ya lugha kama isimu na fasihi. Nadharia hii imeasisiwa na Ferdinand de Saussure katika kitabu chake kiitwacho *A Course in General Linguistics*, (De Saussure, 1966). Nadharia hii inaeleza kuwa katika taaluma ya lugha kuna vitu viwili ambavyo ndivyo vinavyosaidia mawasiliano kufanyika (Nazarova, 1984). Vitu hivyo ni kitaja na kitajwa; kitaja ni alama au herufi zinazotumika kutaja jina la kitu na kitajwa ni kitu halisi kinachorejelewa na alama au herufi zinazotaja kitu hicho (Scholes, 1974).

Kwa mfano, jina “mbuzi,” ni kitaja ambacho hurejelea vitaja mbalimbali kama vile mbuzi “mnyama” na mbuzi kifaa cha “kukunia nazi.” Mfano huu unathibitisha kauli ya De Saussure (1966) kuwa hakuna uhusiano wa moja kwa moja baina ya kitaja na kitajwa na uhusiano wake ni wa kidhahania tu. Shemweta (2015) anasema Nadharia ya Semiotiki inahusishwa sana na matumizi ya lugha ya ishara na uashiriaji ambapo watunzi wa kazi hutumia kitaja fulani kurejelea kitajwa zaidi ya kimoja au tofauti kabisa na kitaja. Mtunzi wa kazi ya fasihi anaweza kutumia kitaja “mbwa,” kurejelea kiongozi mbinafsi katika jamii. Hivyo ndivyo ilivyo katika utafiti huu katika riwaya ya *Vita vya*

*Mapenzi* kwani ametumia kitaja pete kurejelea mikataba mbalimbali wanayoifanya mataifa ya ulimwengu wa tatu na nchi zilizoendelea huchangia kuzifanya nchi zinazoendelea kuwa maskini na nchi zilizoendelea ziendelee kuwa matajiri. Pia mtunzi katumia kitaja pete katika riwaya ya *Mzimu wa Waufi* kurejelea viongozi wa dini wanafiki wanaotumia dini kama kitega uchumi.

Naye Jameson (1972) anafafanua kuwa katika nadharia ya semiotiki ishara katika lugha hujitokeza katika maneno. Ishara ni maana zaidi ya maana ya kawaida ya neno, misemo, tungo, simulizi, jina la mhusika na mandhari vinapotumika katika kazi ya fasihi. Anaona katika lugha huwezi kutenganisha neno na ishara. Neno moja huweza kuwakilisha ishara mbalimbali katika mazingira hayo hayo au katika mazingira tofauti. Aidha, hapa tunajifunza dhana moja katika fasihi huweza kuwakilisha ishara zaidi ya moja. Hii imesaidia wakati wa kuchambua kipengele hicho katika riwaya teule kwani kuna maneno kama kifo, pete, rangi nyekundu, mwanga, mimba na giza ambayo yamekuwa na maana zaidi ya moja.

Umberto (1976) anadai katika nadharia ya semiotiki ishara ni kitu chochote na kitu chochote kinaweza kufanywa ishara. Anaona katika nadharia ya semiotiki hatujifunzi tu vile tunavyodhani kuwa ni ishara katika maisha yetu ya kila siku, bali pia tunajifunza vile vitu vinavyosimama badala ya vitu vingine kama ishara. Naye Todorov (1982), anaeleza nadharia ya semiotiki ilikuwepo tangu zamani katika historia ya wanafilosofia. Anaendelea kueleza nadharia hii hujihusisha na ishara na ilianza katika karne ya 20. Miongoni mwa waasisi wake katika kipindi hiki ni mtaalamu wa isimu wa Kiswisi Ferdnand de Saussure (1857-1913), mwanafilosofia wa Kimarekani Charles Sander Peirce (1839-1914), Roland Barthes na Roman Jakobson.Wamitila (2002:133) akisisitiza umuhimu wa mihimili ya semiotiki, anaeleza kuwa historia ya semiotiki imefuata mikondo mbalimbali na haiwezekani ikachunguzwa vizuri bila kubaini matapo yaliyoiwekea misingi kuanzia Urasimi wa Kirusi, Shule ya Isimu ya Praque hadi kufikia hatua ya leo inapohusishwa zaidi na wahakiki kama vile Eco, Greimas, Todorov, Kristeva, Derrida na Barthes. Kuzuka kwa nadharia ya semiotiki kunahusishwa na

miaka ya 1970 wakati ambapo kulikuwa na mwelekeo mkubwa wa kuuasi na kuuacha umuundo uliokuwa umeutawala uhakiki wa kifasihi katika miaka ya 1960.

Kulingana na Wamitila (2002: 178–9) Saussure alifafanua lugha kama mfumo wa ishara ambazo huangaza na kuunda 'mkufu wa ishara'. Kwa Saussure, kila ishara huwa na sehemu mbili: kiashirii (sauti au wasilisho la kimaandishi) na kiashiriwa (maana ya kiashirii)**.** Maelezo haya yanadhihirisha kuwa kiashirii ni neno lenyewe na kiashiriwa ni maana yenyewe ya kiashirii. Kwa mujibu wa Saussure, kiashirii ni picha-sauti ilhali kiashiriwa ni dhana. Mtaalamu mwingine ni Sperber (1986) anayeandika kuhusu nadharia ya semiotiki. Akiyafafanua mawazo ya yaliyotolewa na Peirce (1931) kuhusu nadharia hii anasema kitu chochote kinaweza kuwa ishara. Tumeona katika riwaya za Mwingizi hata vikapu vichafu vimeweza kuashiria kitu fulani, Anaendelea kueleza mtazamo wa Ferdinand (khj.) kuhusu nadharia hii anasema ishara hutokea kwa namna tofautitofauti katika mfumo wa maisha ya kijamii na hutokea katika maisha ya kila siku.

Vilivile Chandler (1992) anaposhughulikia nadharia ya semiotiki, anamwona binadamu kama ndiyo chanzo cha ishara na ndiyo mchambuzi wa ishara hizo katika kazi za fasihi. Anaendelea kueleza kuwa wanaosoma na kutazama kazi za kifasihi, hujenga maana fulani kutokana na ubunifu na tafsiri walizonazo juu ya ishara, ndiyo maana alama hutumika na hujitokeza katika maneno, picha, sauti, herufi, ladha, matendo, mtenda au yambwa. Anaendelea kufafanua kuwa kitu chochote kinaweza kuwa ishara, ikiwa tu wanajamii watakifanya kirejelee ili kisimame kwa niaba ya kitu kingine. Aidha, ufafanuzi wa Chandler (khj.) kuhusu nadharia ya semiotiki unatuonyesha umuhimu wa kuitumia nadharia hii katika utafiti wetu, kwani anabainisha wazi binadamu ndiyo chimbuko la ishara na ndiye mchambuzi wa ishara zake mwenyewe. Pia anatuonyesha kutokana na ubunifu na tafsiri binadamu hujenga maana fulani fulani juu ya ishara. Zaidi anatujulisha kuwa ishara hujitokeza katika maneno, picha, sauti, herufi, ladha, matendo, mtenda au yambwa. Hata hivyo, ufafanuzi wa ishara upo pia katika nadharia ya semiotiki, unaonyesha wazi ubora wa nadharia hii katika uchambuzi wa ishara katika

kazi za fasihi. Kwa kuwa utafiti huu, umeshughulikia pia na ishara, nadharia ya semiotiki imetufaa.

Selden (1985:85) na Wamitila (2002) wanapofafanua nadharia ya semiotiki, wanasema neno 'semiotiki' ni la Kiyunani lenye maana ya ishara na lilitumika kuelezea mitazamo ya makundi fulani ya uhakiki wa kazi za fasihi. Makundi hayo yalikuja na mbinu ya uhakiki wa kazi za fasihi kwa kuchunguza ishara za kifasihi zilizotokea katika kazi hizo. Zaidi anaeleza kuwa nadharia ya semiotiki hujikita kushughulikia ishara na uashiriaji katika kazi za fasihi. Katika sura ya tano ya utafiti huu limejadiliwa kwa kina swala la ishara na uashiriaji. Anaona msanii wa kazi za fasihi ndiye huunda ishara na mara nyingi ishara hizo hutokea katika muktadha wa kijamii, kiuchumi, kisiasa na kitamaduni. Pia anaona kuwa mtazamo wake lugha hutawaliwa na mambo makuu mawili ambayo ni kitaje (*a signifier)* akimaanisha umbo ambalo alama inachukua na kirejelee (*a signified*) akimaanisha alama maana iwakilishawayo na alama hiyo.

Wamitila anabainisha kuwa uhusiano uliopo kati ya kitaja na kirejelee ni wa kubuni tu, akiwa na maana hakuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya kitaja na kirejelee katika lugha ila jamii ndiyo hukubaliana kulingana na utamaduni wake. Aidha, kutokana na andiko hili la Wamitila (khj.) nadharia ya semiotiki imetufaa sana katika utafiti huu kwa sababu inaweka wazi jinsi inavyo tumika kuchambua ishara za kifasihi, swala linaloshughulikiwa na utafiti wetu. Hii inatokana na ukweli kwamba, japo semiotiki inahusishwa na ishara za kimsamiati, lakini pia inahusishwa na ishara za kitamaduni, hasa kwa kuzingatia uashiriaji wa kifasihi. Kama ilivyo katika isimu, uelewa wa Ferdinand de Saussure na Charles Peirce unahusika pia katika utambuzi na matumizi ya ishara za kifasihi. Mitazamo hii inachunguza sio tu muundo wa ishara bali pia athari na ushawishi wa ishara hiyo kwa hadhira na maana zake pana katika jamii ya fasihi husika.

Baadhi ya mitazamo inayotumika katika uchanganuzi wa ishara hujaribu kutathmini mahusiano yaliyoko kati ya ishara na maswala ya kijamii na kisiasa na umuhimu wa ishara katika nyanja kama vile utamaduni pendwa. Riwaya za Mwingizi

zilizochunguzwa katika utafiti huu zimesheheni ishara chungu nzima zilizo na maana changamano. Pili ametaja maeneo ambamo mtunzi wa kazi ya fasihi huweza kutumia ishara, anaona ishara huweza kujitokeza katika mazingira ya kijamii, kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni kama ambavyo katika riwaya za Mwingizi ishara hizo zimetokea katika vipengele hivyo.

Aidha, mwandishi Maundu Mwingizi ni miongoni mwa wasanii chipukizi ambao hutumia ishara na mbinu nyingine katika kuwasilisha ujumbe wako kwa jamii. Hata hivyo, nadharia ya Semiotiki tumeitumia kwa sababu inatoa dira nzuri ya namna ya kuchambua na kuchunguza matumizi ya ishara. Uchunguzi wa ishara mbalimbali katika riwaya za Mwingizi umeegemea katika mtazamo wa Wamitila (khj.) anaeleza kuwa nadharia ya Semiotiki huchambua matini za kifasihi kwa kufafanua ishara zinajitokeza katika kazi husika. Kwa maoni ya Nauta (1972:36) kuna matawi makuu matatu ya semiotiki: semiotiki fafanuzi, semiotiki tekelezi na semiotiki halisi. Naye Umberto (1977:9) anarejelea tawi la semiotiki ya wanyama (zuolojia) ambalo ni kiwango cha chini kabisa, nalo huhusu tabia za kimawasiliano za viumbe visivyo binadamu.

Makundi haya manne makuu ya Semiotiki yamegawanywa katika vipera vya semiotiki sintaksia (uhusiano wa ishara katika miundo rasmi ya vipengele vya kifasihi), semiotiki pragmatiki (uhusiano wa ishara na athari zake kwa wanaozitumia), semiotiki semantiki (uhusiano wa ishara na maana ya vitu inavyorejelea) na semiotiki wasilishi.Vipera vingine vya semiotiki ni: semiotiki ya kiakili, semiotiki ya kiutamaduni, semiotiki viumbe hai na visivyo viumbe hai, semiotiki ya kifasihi, semiotiki ya kimuziki, semiotiki ya kijamii, semiotiki ya violwa (ya vitu vinavyoonekana), semiotiki ya kithieta, semiotiki ya kianthropolojia na semiotiki ya filamu (huhusu kanuni na uelewaji wa ishara za filamu). Uchanganuzi wetu wa ishara katika riwaya za Mwingizi umehusisha baadhi ya vipera vya semiotiki kama vile semiotiki ya kitamaduni, kifasihi, viumbe hai na viumbe visivyo hai, semiotiki ya kijamii na semiotiki ya kianthropolojia.

Barthes (1994) anaeleza kwamba kuna aina tano za misimbo zinazotumika katika kazi za fasihi ambazo kwa pamoja huunda nadharia ya Semiotiki. Aina hizo ni msimbo wa kimatukio, kihemenitiki, kiseme, kiishara na kiutamaduni. Msimbo wa kimatukio; msimbo huu unahusu jinsi matukio yanayopatikana katika hadithi au masimulizi fulani yanavyofuatana na jinsi msomaji anavyouunda na kuuelewa msuko wa kazi hiyo kwa kuangalia jinsi matukio hayo yanavyofuatana kiathari au kisababishi. Mtunzi wa kazi ya fasihi huweza kuunda visa na matukio kwa njia ya msimbo wa kimatukio (Solomon, 1988). Kwa mfano, riwaya ya *Vita vya Mapenzi* imetumia matukio ya uchawi ambapo mhusika Sufiani anakufa katika ajali ya basi halafu anamkabidhi Suhail pete na dola kwa masharti ya kumuoa binti yake ambaye ni nusu jini wakati ana mchumba wake Sharifa ambaye wamekuwa naye kwenye mahusiano kwa muda mrefu na walikuwa wanasuburi ndoa tu. Haya ni matukio ya kimsimbo yanayoashiria watu mbalimbali wakiwemo wawekezaji ambao huingia katika mikataba na mataifa ya ulimwengu wa tatu kwa masharti magumu na hatimaye wanaendelea kunufaika wao kwa sababu tayari wameshasaini mikataba na mkataba hauwezi kuvunjwa.Wawekezaji hupata faida kubwa kutokana na kunyonya rasilimali pamoja na nguvu kazi ya mataifa maskini Tanzania ikiwemo.

Msimbo mwingine ni msimbo wa Kihemenitiki, msimbo huu unahusu taharuki na usimulizi. Kwa hivyo, huitwa msimbo wa kusimulia au msimbo wa kutamba hadithi na unaweza kufumbatwa kwenye anwani ya kazi. Aidha msimbo huu unatokana na anwuani ya kifasihi kama jina la kitabu, jina la shairi, kichwa cha igizo/onesho au jina la sura katika riwaya (Mark, 1995). Kwa mfano, katika riwaya ya *Mzimu wa Waufi* msomaji anaweza kujiuliza maswali kama: mzimu wa Waufi nini? Kwa nini mzimu huo? Na mzimu huo ni wa watu gani? n.k. Majina ya riwaya kama vile *Vita vya Mapenzi*, *Mzimu wa Waufi* na *Tanzia* yanatusawiria picha fulani ya kuyafahamu maudhui ambayo yanapatikana katika riwaya hizo. Msimbo wa Kihemenitiki husaidia katika kujenga taharuki kwa wasomaji kwani wanapokutana na jina la kitabu kama *Mzimu wa Waufi* na *Tanzia* hujiuliza harakaharaka kuna nini kinachoelezwa ndani ya hivyo vitabu.

Msimbo wa Kiseme; hutumiwa kuelezea elementi nasibishi ya kisementiki. Semantiki ni taaluma inayoshughulikia maana za maneno katika lugha ya mwanadamu. Katika taaluma ya Semantiki maneno yanakuwa na maana ya msingi na maana ya ziada. Maana ya msingi ya neno ni ile ambayo inaweza kutumika na kurejelewa katika muktadha rasmi wakati maana za ziada za neno zinaweza kurejelewa katika muktadha usiokuwa rasmi. Msimbo wa Kiseme katika taaluma ya fasihi hutumiwa na wanafasihi kujenga dhamira na maudhui kwa kutumia maneno ambayo yanatoa ukaribu wa maana ya msingi ya neno na kile kinachorejelewa na neno hilo kifasihi (Wright, 1975). Katika utafiti huu tumetumia misimbo mbalimbali ambayo imeweza kuonyesha ukaribu wa maana ya msingi katika kuibua maudhui na dhamira mbalimbali.

Msimbo wa Kiishara; unarejelea lugha ya ishara inayotumiwa na waandishi wa kazi za fasihi. (Senkoro, 2006). Hii inatokana na ukweli kuwa, kazi ya fasihi husawiri maisha halisi ya jamii kwa kutumia lugha ya picha na ishara na kisha kuyawasilisha kwa jamii. Msimbo wa Kiishara wa nadharia ya Semiotiki humsaidia mtafiti au mhakiki wa kazi ya fasihi kuweza kubainisha lugha ya ishara iliyotumika katika kazi ya fasihi na kuweza kusema wapi dhamira gani. Mathalani, katika riwaya ya *Mzimu wa Waufi* mtunzi akimsawiri Masumbuko kuwa ni mtu mvumilivu ambaye hakukubali kuyumbishwa na mateso mbalimbali ambayo alikuwa anayapata kutoka kwa wapinzani wake akina Hunudu na hatimaye, akaja kuwa kiongozi wa himaya ya Waswezi na wakawashinda mahasimu wao waliokuwa wanatumia uongozi wao kuwakandamiza wananchi. Haya ni matumizi ya matukio ya kiishara ambayo yanaonyesha umuhimu wa jamii kuwa na viongozi ambao ni wazalendo na wenye nia ya dhati katika kukomboa jamii zao kutokana na majanga mbalimbali likiwemo swala la umaskini.

Msimbo wa mwisho ni msimbo wa Kiutamaduni; Watunzi wa kazi za fasihi hutumia viashiria vya utamaduni katika kazi zao wakiwa na nia ya kuwasilisha dhamira mbalimbali kwa wasomaji. Kwa mfano, mtunzi katika riwaya ya *Vita vya Mapenzi* anamuonyesha mhusika Suhail akiwa ametawaliwa na utamaduni wa Magharibi kiasi kwamba, hata hawaheshimu wenzake na waliomzidi umri kwa kuwa *bize* kusikiliza

nyimbo za kizungu kupitia visikilizio vya masikioni na kuimba kwa sauti ya juu hadi kuwasumbua jirani zake waliopanda gari moja. Kupitia msimbo wa kiutamaduni unaojengwa na matendo ya Suhail tunapata uelewa kuwa, hapa tunaonyeshwa dhamira ya madhara ya utandawazi kwa upande mwingine. Hata ingawa dhana ya msimbo ni muhimu katika nadharia ya semiotiki, lakini  pia utafiti huu umetumia pia mawazo ya Saussure na Peirce kuchanganua matumizi ya ishara katika riwaya za Mwingizi. Kwani Peirce aliukubali uchanganuzi wa Saussure wa ishara kuwa na sehemu mbili: kiashirii na kiashiriwa lakini akaongeza sehemu ya tatu ambacho ni kifasiri ndivyo. Uchambuzi wa tasnifu hii umechambua riwaya teule katika sura ya tano kwa kujiegemeza katika kiashirii, kiashiriwa na kifasiri. Kwa Peirce, kila ishara huwa na yambwa au kitendwa kinachorejelewa.

Wamitila (2002:132) anaeleza kifasiri kama kitu kinachochochea katika akili ya anayetafsiri ishara hiyo, yaani ishara ya pili. Kwa mfano, mtu akikuonyesha simba aliyelala mahali fulani, ile ishara ya simba inaweza kulichochea neno ‘simba’ katika lugha nyingine akilini mwako. Hiki kitakuwa kifasiri. Peirce anasadiki kwamba kila ishara ina misingi inakotegemezwa ili ufasiri wake uwezekane. Anaongeza kuwa misingi hiyo huibua aina tatu za ishara ambazo ni kielekezi, ishara-tanakali na taashira. Kwa hivyo, mawazo ya Peirce ya ishara kutegemezwa kwenye msingi fulani ili kufasiriwa, yaelekea kukubaliana na wazo la Saussure kwamba ishara hazina upekee wa maana isipokuwa zinapofasiriwa katika ‘mkufu wa ishara’. Peirce anasifiwa kwa kuhakikisha kuwa nadharia ya Semiotiki haikuishia kuzisambaza sifa za kitaaluma sana kama ulivyofanya umuundo (Wamitila 2002:133). Wamitila (2002:179) anaendeleza maoni ya Wana-Umuundo kwa kusema kwamba, ishara moja inaweza kuwa na maana nyingi iwapo itawekwa  au kukitwa kwenye muktadha wa kijamii na hivyo jamii kuwa na athari kubwa juu ya maana. Hii ina maana kuwa kiashiriwa hakiwezi kuwa funge. Kilanga (2015) akimnukuu mwanaudenguzi Bakhtin anaeleza ishara kama kitu kinachotegemea kingine kinachozungumziwa kwa kuwa ishara haina maana funge. Hutegemea usemezano wa msemaji na msemeshwa. Mwanariwaya za kiupelelezi

Jacques Derrida aliendeleza wazo la Bakhtin kwa kudai kuwa ishara ambayo ni funge haina kitovu cha maana ya ishara.

Kutokana na mawazo haya tunaweza kusema kuwa viashiriwa vikikitwa kwenye muktadha wa kimazungumzo huweza kubadilika kutegemea muktadha wa kiusemi na iwapo muktadha utabadilika nayo maana inabadilika. Kwa hiyo, inakuwa vigumu kudai kuwa kuna kitovu maalum cha maana mahali popote pale (Wamitila 2002:179-180). Nadharia hii imefaa kiuamili katika utafiti huu kwani mambo yanayojadiliwa katika nadharia hii yamedhihirika sana katika riwaya za Mwingizi zilizochambuliwa. Miongoni mwa hayo mambo ni pamoja na tunapozisoma riwaya hizi teule, pamoja na kuichunguza misimbo ya nadharia ya semiotiki, tunaona na kukubali kuwa, nadharia hii imetufaa katika kuzibaini, kuzitabakisha, kuzichunguza na kuzifasiri ishara mseto zinazohimili mada yetu ya utafiti. Vipengele vingi vya nadharia hii vimefungamana na vipengele vingi katika riwaya tunazozishughulikia.

### 1.8 Mapitio ya Maandiko

Katika sehemu hii inawasilisha mapitio ya maandiko mbalimbali yanayosaidia kushadidia kauli na hoja za utafiti huu , maandiko yaliyopitiwa ni pamoja na maandiko yanayohusu dhana ya jiniuchawi na ushirikina, dhana ya jiniuchawi na ushirikina katika fasihi andishi. Vilevile tumeangalia dhana ya uchimuzi na jinsi inavyotumika katika kazi za kifasihi na dhana ya ishara kwa ujumla.

#### 1.8.1 Dhana ya Jiniuchawi na Ushirikina

Neno "uchawi" limepata maana yake kutokana na kitendo chenyewe, yaani uchawi ni matendo ya watu wenye maarifa kama asemavyo Brain (1981). Uchawi ni nguvu anazozaliwa nazo mtu na akazitumia kudhuru watu wengine kwa siri na pasipo sababu. Wachawi hudhuru kiholela kwa sababu tu wanajisikia kufanya hivyo (Shorter 1998). Shorter anaona kuwa mtu hujisikia kudhuru wengine pasipo sababu lakini Mkundi (2010) anadai uchawi si wa kudhuru tu bali upo mwingine kwa ajili ya kuleta maendeleo. Kwa mfano, Kinjeketile katika tamthilia ya *Kinjeketile* anatumia uchawi kuhamasisha watu kupambana na Wakoloni, hoja hii inadhihirika katika tamthiliya ya *Kinjekitile* iliyoandikwa na Ibrahim Hussein (1969) alivyotumia uchawi wa maji katika

kupambana na Wajerumani. Utafiti huu wa Mkundi umetudhihirishia ukweli kwamba, kazi andishi teule zimebeba pia dhana ya uchawi na ushirikana kama nyenzo ya mapambano mbalimbali katika jamii, kwani tamthiliya ya Ibrahim Hussein inadhihirisha jambo hili pia.

Kuna aina mbalimbali za uchawi na ushirikina. Kuna uchawi wa kutumia wazimu, huu, kwa mujibu wa maelezo ya wataalam wa nyanja hii, ni wa kumfanya mtu ashikwe na wazimu na hatimaye arukwe na akili. Uchawi wa uadui, huu hukosanisha watu, kuna mizizi maalumu ambayo huchomwa kwenye moto, moshi wake ukiwatokea watu, mara moja ugomvi unaanza. Pia kuna uchawi wa kujificha, huu hufungwa kwenye hirizi maalum, mtu akifuata masharti yake, atakuwa na uwezo wa kujilinda na adui yake hata wasiwe na uwezo wa kumwona. Mara nyingi hutumiwa wakati wa safari au wakati wa vita, kwa lengo la kujificha dhidi ya maadui. Mwingine ni uchawi wa kuwatumia wanyama, kama vile paka. Mnyama huyu hutumwa kwa mlengwa, akifika nyumbani kwake huanza kulia kwa sauti, mwenye nyumba akimfukuza kwa kutoa sauti, sauti yake hukwama mpaka hapo atakapofanya maarifa ya kujikwamua. Uchawi mwingine ni ule wa kuwaloga watu. Huu unaweza kumuua mtu/adui/mlengwa bila kumpa sumu wala kumpiga, ila kwa kumchimbia dawa mlangoni, shambani au popote pale anapoona panafaa kwa siri. Aliyelengwa akiiruka dawa hiyo au kuigusa, huugua hadi kufa. Na mwisho kuna uchawi wa kutumia majini. Wachawi wanawatumia majini kama mawakala wao, ili kupata mali kuua au kuangamiza watu au hata jamii.

Kuhusiana na maswala ya majini, magwiji wa taaluma hii husema kuwa baadhi ya majini yanayotumiwa na wachawi ni pamoja na jini la uganga ambalo hutumika katika shughuli za uaguzi. Jini chafu ambalo husababisha mikosi. Jini mauti hili linaua na kumfanya mtu aharibikiwe na akili na afanye mapenzi ya uzinzi kupita kiasi, hata akishauriwa si rahisi kukubali kuacha tabia hiyo mbaya. Jini Sharifu, nalo ni mkuu wa majini yote na linafanya kazi ya uuaji na mambo ya nguvu, linaua watu, mifugo na hata kuharibu mitambo mbalimbali ya viwanda, kwa njia moja au nyingine.Jini kilima nalo linahusika na mambo ya uaguzi.

Aidha jini Maimuna linahusika na mambo ya kutafuta pesa na ni la kufanya mikataba na wanadamu wenye uchu wa pesa na utajiri. Jini Kilimani, linahusika na mambo ya uadui na kufarakanisha watu. Jini Mnyembango, ni la uuaji wa watu na vitu. Jini Shehe ni la kutafutia wanawake wanaume wa kuwaoa kwa wale wanaotafuta msaada kupitia jini hili. Jini Makata na Subuhana, yana sifa za kuua watu au kuharibu vitu papo kwa hapo. Mfano kwa njia ya radi. Jini Kashi kasha na Samba ni majini yenye jini, sifa za kuwinda. Wawindaji ambao ni wachawi wanayatumia kwa malengo ya kujipatia mawindo ya aina yote. Jini Nura lina sifa ya kusababisha ajali mbalimbali (Omari 1993). Mambo haya ya majini yametumiwa katika riwaya za Mwingizi kuchimuza maudhui mbalimbali. Kwa mfano kuna matumizi ya radi katika riwaya ya *Mzimu wa Waufi* ambayo alitumiwa Mzee Kishindo na Hunudu na kufa papo hapo.

Hali kadhalika, kwa mujibu wa maelezo ya (Omari, 1993) kuna aina za ushirikina kama vile:- ushirikina wa mazindiko, ushirikina wa kutumia mizizi, ushirikina wa kupiga ramli kwa waaguzi, huu hufanywa na mshirikina anapomwendea muuguzi ili amwonyeshe anayemloga au anayeharibu mafanikio yake. Ushirikina wa kutumia nyota, huu mhusika husoma viganja vya mikono ili kutambua mafanikio ya mtu au mikosi itakayompata, na kumweleza jinsi ya kuiepuka, ushirikina wa tambiko, huu hufanyika njia panda, mapangoni na misituni. Wahusika hufanya ushirikina huu wakisaidiana na mizimu ili kuleta mvua nyakati za ukame au kuzuia magonjwa mabaya kama surua. Aina hizi za jiniuchawi na ushirikina zimeweza kujidhihirisha vizuri katika riwaya teule kama *Mzimu wa Waufi* ambapo tunaona ushirikina wa matambiko ukifanyika makaburini katikakti ya msitu ambako Masumbuko anafanyiwa matambiko kwa ajili ya kuandaliwa kuwa kiuongozi wa Waswezi. Katika riwaya ya *Tanzia* pia tunaona ushirikina wa tambiko ukifanyika kwenye makaburi kwa ajili ya kumzindika Mzee Mtandi ili aweze kupona ugonjwa wake. Matukio haya yote ya matambiko makaburini na kwenye misitu yameweza kujenga maudhui mbalimbali katika kazi hizi.

Pia dhana hii ya jiniuchawi na ushirikina imeweza kutumiwa kama masimulizi katika riwaya za Grazia Deledela na Tom Morrison. Ebinger (2000) katika tasnifu yake ya

uzamifu anaeleza matumizi ya uchawi na ukichaa kama masimulizi katika riwaya za Grazia Deledela na Tom Morrison. Anasema riwaya hizi zinaeleza tabia mbalimbali zenye mtiririko wa matukio ya usimulizi. Miongoni mwa vitu ambavyo vipo sambamba ni pamoja na matumizi ya uchawi na ukichaa kama mwongozo wa masimulizi katika kazi hii linganishi. Ebinger katika utafiti wake aliona kwamba matumizi ya uchawi na ukichaa yameonekana kwa kiasi kikubwa katika riwaya hizi. Pia aligundua kwamba matumizi ya uchawi na ukichaa yametumika katika riwaya hizi kama njia ya mawasiliano. Matukio hayo ya kichawi na ukichaa ukiyasoma katika riwaya teule utaona yamewasilishwa kwa njia ya uhalisiajabu kwani baadhi ya wahusika wa riwaya hizi wamepitia visa na matukio ya kutisha na ambayo si ya kawaida. Tasnifu hii imetusaidia katika kujua vizuri mtindo wa kijiniuchawi na ushirikina ulivyotumika katika tasnifu yetu ili kuonyesha maudhui mbalimbali katika riwaya teule. Mambo ya jiniuchawi na ushirikina yametumika kwa kiasi kikubwa katika maandishi ya kifasihi za kilimwengu na fasihi ya Kiswahili ikiwemo. Maswala haya ya imani na desturi za uchawi, ushirikina na majini yamo pia katika kazi za fasihi ya Kiswahili.

Aidha, utafiti huu pamoja na kwamba umechanganua jiniuchawi na ushirikina kama mikakati ya uchimuzi katika kuendeleza maudhui mbalimbali katika riwaya teule, ambazo nazo zina mambo ya uchawi, kuna fahiwa ya kuwepo kwa usemezano kati na miongoni mwa kazi za kiutunzi katika fasihi ya Kiswahili. Usomaji na uchanganuzi wetu wa tamthilia hii ya *Kinjekitile* umetuwezesha sio tu kulinganisha mambo ya kiuhalisiajabu yaliyomo bali pia kuitumia kama kigezo cha urejeleaji katika kutafiti maswala ya uhalisiajabu kwa sababu maswala ya jiniuchawi na ushirikina tuliyoyaangazia yanasawiana katika misingi ya matukio ya kiajabu yenye uchawi yanayojibainisha katika riwaya teule zilizoko katika kiini cha utafiti huu. Kwa kutumia njia mbalimbali katika uelewa na udhibiti wetu wa maswala ya uchawi na ushirikina katika tamthilia hii, ni nguzo muhimu katika kuangazia na kuuliza maswali kama maudhui ya riwaya hizi teule yameleta faida yeyote katika jamii katika kujikomboa na maadui zake wa aina mbalimbali.

Ismaili (1969) katika utenzi wake wa *Swifa ya Nguvumali* ametumia uhalisiajabu katika kuyaelezea matukio mbalimbali. Mshairi anamrejelea mtu ambaye alishakufa lakini kwa kuwa aliuliwa na wachawi yuko mahali fulani anaishi kwa huyo mchawi akiwa amekatwa ulimi. Kitendo hiki kinatufanya tuone ni jambo la ajabu kwani katika hali ya kawaida mtu akifa huwa hatumwoni tena. Hali kama hizi zinaibua maswali na maajabu haya yanadhamiria tujifunze nini? Ingawaje mwandishi huyu amesawiri mambo ya jiniuchawi na ushirikina katika utenzi, ambayo kimsingi ni kazi ya kubuni, msambao huu wa mambo ya kiajabu unaturudisha pale pale, tunatakiwa kujifunza nini? Kwa hivyo, kazi yake imekuwa na manufaa kwetu sisi kama watafiti kwa kuwa huo uhalisiajabu unaopatikana katika matukio ya utenzi huu umekuwa unatoa ithibati ya mlandano wa maswala ya kiuhalisiajabu katika tanzu zote za fasihi ya Kiswahili zikiwemo riwaya teule tulizozichanganua katika utafiti huu. Kwa hivyo, kimsingi hoja inayoendelezwa hapa inahusiana na mzagao wa uhalisiajabu kama ulivyoegemezwa katika vipengele vya uchawi na ushirikina katika fasihi ya Kiswahili. Hii ina maana kwamba uelewa wa uhalisiajabu tunaouchota kutoka katika tamthilia na ushairi, unachangia pakubwa uelewa wetu wa maswala haya katika riwaya teule.

.

Vilevile maswala ya jiniuchawi na ushirikina yameonekana katika riwaya ya Mkangi ya *Mafuta* (1984) katika kipengele cha usawiri wa mandhari. Mkangi ametumia mandhari ya kijiniuchawi katika kazi hii ili kuibua maswala mengi ya mifanyiko na mitagusano ya kijamii. Kwa mfano, anaposema "Mtue anasema kuwa, ameshasikia visa vya majini, lakini alichokutana nacho kimeshinda vyote". Hii ni baada ya kujikuta katika mandhari ya kushangaza na wala hakujua alivyofika pale. Ti anaeleza kuwa wakati mwingine huenda mtu akajikuta juu ya mbuyu, huku nguo zake zinaning'inia angani. Mtue anamaka na kumuuliza Ti kama yeye ni ibilisi au jini. Hili linadhihirika hata katika riwaya ya *Tanzia* kwani msiba unatangazwa msikitini na marehemu aliyetangazwa familia haijui kama amekufa kwa sababu wamelala naye ndani na wakati wanaenda kulala alikuwa hajafa, pia wanatafutwa watu waliotangaza huo msiba hawamjui mtu aliyetangaza na ndugu wanaposikia tangazo hilo asubuhi na mapema na wanapokimbia chumbani kwake kumuangalia Nyanzala wanakuta kweli amekufa.

Matukio ya kijiniuchawi yanayojitokeza katika riwaya hii yanathibitisha msambao wa maswala ya uhalisiajabu katika mapana na marefu ya fasihi ya Kiswahili. Wamitila (2003c ) anaziona riwaya hizi za kiuhalisiajabu kama zinazopita ufahamu wetu wa ulimwengu na anapendekeza kwamba, riwaya za aina hii zichunguzwe upya labda kwa mtazamo wa kifalsafa ili kuleta upya wa kimawazo au hata kiuumbuji katika ulingo wa fasihi ya Kiswahili. Wamitila katika riwaya zake za *Bina-Adamu*! (2002) na *Musaleo!* (2004), anatumia uhalisiajabu kimakusudi kwa kutaka kuyaangalia maswala ya kijamii kwa njia ya kiajabu na ya kipekee.

Pia dhana hii ya jiniuchawi imekuwa ikitumika katika hadithi mbalimbali za watoto na wanawake huko Marekani kama anavyoeleza Sanchez (2000). Katika tasnifu yake ambayo inazungumzia swala la jiniuchawi katika jamii ya sasa katika hadithi za wanawake weusi wa kimarekani. Katika tasnifu yake anabainisha umuhimu wa ukweli uliomo ndani ya uhalisiajabu katika hadithi za wanawake weusi wa Marekani za mwishoni mwa karne ya ishirini. Katika utafiti wake alioufanya katika uchambuzi wa riwaya ya *Tom Morrison* aligundua kwamba dhana ya jiniuchawi imetawala kwa kiasi kikubwa katika riwaya hiyo, katika kuonyesha msisitizo wa historia ya Waafrika katika kung'ang'ana na mabadiliko ya utamaduni. Katika utafiti wake alitumia mtindo huu wa jiniuchawi katika kupamba lugha. Tasnifu hii nayo imetusaidia katika uchambuzi wetu kwani, katika matumizi yake ya jiniuchawi katika kazi andishi kufikisha ujumbe wake na pia ameonyesha mbinu hii ya jiniuchawi kama taswira katika kuonyesha utamaduni wa Waafrika jinsi wanawake wanavyojidharau na kuiga tamaduni za wazungu.

Senkoro (2007) anaeleza kwamba kazi nyingi andishi za fasihi zilijaribu kuandika fasihi za majaribio kwa kuingiza vipengele vya kiutamaduni katika kazi kuanzia miaka ya 1960. Miongoni mwa vipengele hivyo ni pamoja na kuingiza swala zima la uhalisiamazingaombwe katika kazi za fasihi andishi na ndio maana waandishi wengi wakajikita kuandika kazi hizo zilizosheheni uhalisiajabu. Senkoro katika mjadala wake, anasema kwamba kazi hizi za kiuhalisiajabu zilikuwepo isipokuwa istilahi hii haikuwepo wakati huo. Miongoni mwa kazi zilizo na vipengele vya uhalisiajabu  ni

*Nyumbani kwa Mchawi* (1961), *Kinjekitile* (1969), *Mashetani* (1970) *Aliyeonja Pepo* (1977), *Hatia* (1972), *Mirathi ya Hatari* (1977), *Lina Ubani* (1984), *Njia Panda* (1981), *Nagona* (1990) *na Mzingile* (1991), *Babu Alipofufuka (2001), Bina Adamu (2002), Kilio cha Jesca (*2004) na *Musaleo* (2004). Kwa hiyo, tunaona kazi hizi za uhalisiajabu zilikuwepo tangu miaka ya 1960 zilitumia uhalisiajabu kama taswira katika kuelezea mambo mbalimbali katika jamii. Lakini istilahi hii ya uhalisiajabu ilikuwa bado kujulikana ila mtindo wake ulikuwa ni wa kiuhalisiajabu.

Riwaya ya *Mzingile* (Kezilahabi) na *Dharau ya Ini* (Wamitila*)* nazo zimeonyesha mambo ya kiajabu sana kwa kuonyesha vitu visivyo vya kawaida, kwa mfano, Kakulu anazaliwa na kuanza kuongea papohapo na kuwafukuza watu katika *Mzingile*. Wamitila (2008) ameshughulikia riwaya hizi katika swala la uhalisiajabu katika kipengele cha jiniuchawi katika riwaya ambapo anaeleza kuwa riwaya ya uhalisiajabu huingiza sifa ambazo zinafahamika na wasomaji. Ametoa mifano katika riwaya mbili ambapo ni vigumu kueleza jinsi Munene anavyofukuzwa na fuvu katika *Dharau ya Ini* au jinsi Kakulu anavyoweza kuongea, kutania watu na kukimbia mara tu anapozaliwa katika *Mzingile*. Matukio ya kiajabu katika *Dharau ya Ini* na *Mzingile* yamekuwa muhimu katika utafiti wetu kwani upitiaji wetu wa kazi hizi umetusaidia kuelewa zaidi juu ya matukio ya kiajabu. Katika kuzichambua riwaya zinazoshughlikiwa katika utafiti huu imekuwa rahisi kuteuwa matukio ambayo si ya kawaida kama ambavyo Wamitila ameweza kufanya. Kwa hivyo, kazi ya Wamitila imetufaa zaidi katika kuchambua matukio ya kiajabu yalivyoweza kuendeleza maudhui mbalimbali katika riwaya teule

Olali (2010), amelidhihirisha jambo hili katika makala yake iliyoshughulikia uhalisiajabu katika riwaya ya *Babu Alipofufuka*. Olali anadai Said Ahmed Mohamed anatumia majaribio na uhalisiajabu kwa mara ya kwanza. Anasema kuwa uhalisiajabu katika riwaya hii unatokea pale kunazuka mzuka mara kwa mara katika kasri la K, katika gari lake na njiani anapoendeshwa na dereva wake. Olali anaendelea kusema kuwa Said Mohamed anatumia sifa za kiuhalisiajabu kuonyesha kuwa shughuli kama hizo hutokea katika hali halisi na katika mazingira ya Uswahilini. Kazi hiyo ya Olali

(khj.) imetupa picha zaidi kwani mwandishi Mohamed ametumia dhana hii ya uhalisiajabu katika riwaya yake katika kuonyesha mambo ya jiniuchawi, tunamuona mzuka anapojitokeza ghafla katika maeneo na mazingira ya kiajabuajabu, japo mtafiti huyu aliangalia muundo wa riwaya za kimajaribio. Utafiti wake umetusaidia katika kuonyesha jinsi riwaya hizi za kimajaribio zilivyosheheni mambo ya jiniuchawi na ushirikina. Riwaya tulizozichambua pia ni riwaya za kimajaribio. Vilevile Olali ameeleza jinsi ambavyo uhalisiajabu unavyotokeza katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* kwa kutaja tu bila kuchambua matukio hayo lakini utafiti huu umeyaangazia matukio kama mkakati wa uchimuzi katika kuelezea mambo mbalimbali yanayosukanishwa na mambo ya kutisha na kuogofya.

Olali (khj) anaendelea kutuonyesha muundo katika *Babu Alipofufuka* ambao ni mtindo mpya katika riwaya za kimajaribio unaoingiliana na mambo ya kifantasia, kiajabu na kiubadausasa na wenye mitindo mipya ya uandishi wa kimajaribio ambao unajaliza katika maswala nyeti ya kimaudhui kama ya utandawazi, dini, filosofia na siasa za kimataifa. Msisitizo wake wa sifa za riwaya hizi ni uandishi unaokiuka kaida za kiitikadi, utathmini wa ujumi kwa ndani na uvunjaji wa kaida za lugha kwa namna inayompa mwandishi uhuru zaidi. Anakiri kuwa msuko wa riwaya hizi ni changamano na hudhihirisha mbinu rejeshi kwa kiwango kikubwa. Kulingana naye, msuko wa riwaya ya *Babu Alipofufuka* upo katika vitengo viwili, yaani wa mhusika mkuu K na wa mzuka wa babu yake. Aidha, pindi mzuka wa babu yake uanzapo kufuata maisha ya K, mambo ya kiajabu yanaanza kutendeka kama vile kupotea kwa chakula cha mbwa wake ‘Doggy', kupata tumbo la kuendesha na aidha kusumbuliwa na mzuka uliomtawala mara kwa mara. Licha ya hayo, mizuka ya watu ambao ilimtendea mabaya hapo awali ilimrudiarudia, hawa walikuwa watu halisi ambao yeye pekee ndiye aliyewaona.

Kutokana na fasihi simulizi za jamii ya Wakikuyu (na zinginezo) mizimu huwatokea walio hai hasa ndotoni ili kujaribu kuelekeza jamii inapokosa mwelekeo. Tunaona mambo kama haya katika utafiti wetu japo Olali yeye ametaja tu pasina kueleza zaidi. Utafiti huu wa Olali umeweka wazi zaidi mbinu hizi za jiniuchawi zilivyotumika na

jinsi zilivyobeba jumbe mbalimbali katika jamii. Pia kuna baadhi ya watafiti ambao walitumia dhana ya uhalisiajabu na kuweka kipengele cha jiniuchawi na ushirikina katika uchambuzi wa kazi zao. Miongoni mwao ni Wanjiru (2013) ambaye aliangalia uhalisia na uhalisiajabu kama dhana kuu katika uendelezaji wa riwaya ya *Babu Alipofufuka* na *Watu wa Gehena*. Katika utafiti huu mwandishi alionyesha jinsi uhalisiajabu ulivyoendeleza riwaya hizo. Pia, kuna watafiti wengine weliotumia dhana hii ya uhalisiajabu kama nadharia katika kutafitia kazi. Miongoni mwao ni Magaju (2004), Nyabunga (2005). Watafiti hawa walichambua kazi zao za fasihi andishi kwa kutumia nadharia ya uhalisiajabu na nadharia hii pia ilijibainisha vizuri katika kazi zao. Tafiti hizi zimetoa mchango mkubwa katika utafiti wetu. Kwa mfano, Vutagwa (2013) anachunguza uhalisiajabu katika kuendeleza maudhui ya dini na akaona uhalisiajabu umeweza kuendeleza maudhui ya kidini kwa kiasi kikubwa. Pia nadharia hizo zilizotumika kwa watafiti hawa zimekuwa mchango katika utafiti wetu kwani nadharia tunayoitumia ni nadharia ya uhalisiajabu.

### 1.8.2 Dhana ya Uchimuzi Katika Kazi za Fasihi

Uchimuzi ni neno lililotokana na ufafanuzi wa Garvin (1964), kama tafsiri ya KiCzech ‘aktualisace'. Dhana hii ilikuwa mashuhuri sana na mwanamuundo wa Prague, Jan Mukarovsky ambaye alilitumia neno hili kurejelea neno la Kiingereza ‘actualization'. Yaani, hali ya kukifanya kitu kiwe halisi kuliko cha kweli. Kwa hivyo, uchimuzi ni mbinu ya kisanaa inayajitokeza waziwazi na ni nguzo kuu iliyotumiwa na mwandishi kusisitiza mambo tofauti yanayobeba uzito na muhimu kupitia kwa matumizi ya lugha na usimulizi kwa njia inayozalisha maudhui mapya yanayoathiri jamii na hata mataifa. Wakati mwingine uchimuzi hutumika kama mbinu ya kuyadokeza mambo fulani au sifa fulani katika kazi za fasihi kwa namna ya waziwazi na kuyafanya yajitokeze waziwazi yakilinganishwa na mengine (Wamitila, 2003). Mbinu hii ya uchimuzi imetumika katika utafiti wetu katika kuonyesha maudhui mbalimbali yaliyowezeshwa kubainika kwa kuegemezwa katika dhana ya jiniuchawi na ushirikina katika riwaya zetu za utafiti.

Mugwika (2012), katika tasnifu ya shahada yake ya uzamili ameshughulikia dhana ya uchimuzi katika uendelezaji wa riwaya ya kimajaribio ya *Mafamba* (2008). Katika

tasnifu yake, anaelezea jinsi ambavyo mwandishi ametumia dhana nzima ya uhalisiajabu kama njia mojawapo inayotumiwa katika kuchimuza mambo yanayoongelewa katika riwaya ya *Mafamba*. Matumizi ya uchimuzi katika tasnifu hii yametupa mwanga katika tasnifu yetu katika kuchambua kazi yetu kwani uchimuzi umetumika kama mbinu ya kuyamulika maudhui mbalimbali. Pia mbinu hii ya uchimuzi ilitumiwa katika utafiti wa Moussa (2012) ambapo katika utafiti wake alichunguza matumizi ya uhalisiajabu na ndani ya uhalisiajabu pia kulikuwa na kipengele cha jiniuchawi kwa kiasi kama chombo cha harakati za kisiasa baada ya ukoloni katika nchi za Kiafrika katika riwaya za Ngugi wa Thiongo *Wizard of the Crow*, Ben Okri *The Famished Road* na Kojo Laing *Woman of the Aeroplanes.* Moussa alitumia mbinu ya uchimuzi katika kuyaweka wazi mambo yaliyoelezewa kwa mtindo wa kiuhalisiajabu ili jamii iweze kujua mambo haya, na aligundua kwamba katika riwaya hizi uhalisiajabu ulitumika kama mfumo wa kifasihi katika kuyaelezea mambo ya ukoloni katika Afrika kwenye riwaya zao. Ilikuwa ni njia ya kufikisha ujumbe kwa nchi zilizotawaliwa na wakoloni kwa kutumia dhana hii ya uhalisiajabu. Dhana hii ya uchimuzi imejadiliwa kwa kirefu zaidi katika sura ya pili.

### 1.8.3 Dhana ya Ishara

Swala la ishara katika fasihi ni miongini mwa maeneo yaliyowashughulisha waandishi mbalimbali na wameshughulikia kipengele hiki kwa namna tofauti tofauti. Wanazuoni hao ni pamoja na Frye (1985) anayesema ishara ni kitu kinachosimama kuwakilisha kitu kingine. Kwa mfano msalaba ni ishara ya Ukristo, nguo nyeusi kwa wazungu ni ishara ya maombolezo. Kwa upande mwingine, ishara huwakilisha kitu kinachoashiriwa. Naye Yanni (1998) anafafanua ishara kwa kusema katika muktadha wa kawaida wa jamii, maji ni ishara ya uhai lakini katika muktadha wa kidini (ukristo) ni ishara ya kifo au majaribu. Hivyo maji au mafuriko ni ishara ya tukio baya katika muktadha wa kidini na wakati mwingine katika muktadha huo huo wa kidini maji ni ishara ya uzima, usafi na matumaini. Aidha, moto ni ishara ya uharibifu katika muktadha wa kidini (Ukristo/Uislam) na upande mwingine katika dini moto ni ishara ya utakaso (kusafishwa). Hata hivyo, ndani ya matini, muktadha na dhamira husadia ishara kutokeza. Kimsingi ishara hailengi maana mahususi bali hupendekeza maana

inayohusiana na kiashirii. Aidha, katika ufafanuzi wa Frye na Yanni (wameshatajwa) wote wanaeleza maana ya ishara na wanakubaliana kuwa ishara ni kitu kinachosimama kuwakilisha kitu kingine na kimsingi hailengi maana ya msingi kama zilivyokuwa ishara kama pete, kifo, mimba, giza ni ishara ambazo hazijalenga maana ya msingi.

Ufafanuzi huu umetusaidia katika sura ya tano kuelewa dhana ya ishara na kutusaidia katika uchambuzi wa kipengele cha ishara na uashiriaji kama mikakati ya uchimuzi katika riwaya za Mwingizi. Hata hivyo, katika maandiko tuliyopitia na hasa andiko la Yaani (khj.) limetufaa zaidi katika utafiti wetu kwani pamoja na kueleza maana ya ishara, pia anatoa mifano kuonyesha namna vipengele vya kiishara vinavyoonekana. Zaidi ameonyesha neno moja linavyoweza kuwakilisha ishara zaidi ya moja katika mazingira hayo hayo kutegemea matumizi yake. Kwa mfano kifo na pete katika riwaya teule za Mwingizi zimeweza kuwa na maana zaidi ya moja.

Kwa upande mwingine, wanazuoni wengine walioandika kuhusu ishara ni pamoja na Meyer (2002), Perrine (2004) na Snowden (2006). Meyer (2002) anasema maana za ishara zimekitwa katika mpangilio wa matini na kwa hiyo zinahimiliwa na miktadha ya matumizi yake. Miktadha inaweza kuwa ya kidini, kisiasa, kijamii na kiuchumi. Naye Perrine anaiona ishara ni kama kitu cha thamani chenye rangi nyingi na kinachoweza kudhihirisha rangi mbalimbali kinapowekwa kwenye mwangaza. Maana za ishara hujitokeza kutegemea miktadha ya kimatumizi. Aidha ishara imekuwa ikiashiria mambo mbalimbali katika riwaya za Mwingizi kulingana na miktadha mbalimbali ya kimatumizi. Mtunzi huyu ametumia uishara katika kumakinikia maswala mbalimbali ya kisiasa, kiuchumi, kijamii na kidini na kuweka wazi maswala ya msingi, ambayo katika hali ya kawaida ingekuwa ni vigumu kuyaeleza pasipo kutumia ishara. Hivyo basi, ishara imetumika kama chombo cha kuweka wazi maswala ya msingi.

Ishara za kifasihi ni kitu kilicho na maana zaidi ya kitu hicho. Ishara ni kitu chenye maana ya kawaida lakini kinamaanisha kitu kingine. Snowden (2006) anasema ishara hujumuisha vitu hai, visivyo hai na vitu dhahania, mfano simba, mtu, na tai katika

ukristo ni ishara ya wahubiri. Hata hivyo, wanazuoni hawa wanaonekana kutumia mbinu mbalimbali katika kutoa fasili ya neno ishara mfano Meyer (khj.) anaona ishara hujitokeza katika matini bila kufafanua zaidi ni aina gani ya matini ambazo anazungumzia, ametusaidia kuelewa ishara hujitokeza katika matini na hutegemea mazingira.

Perrine (khj.) anaonyesha kwamba neno moja linaweza kuwakilisha ishara zaidi ya moja na kuwa katika fasihi ishara ni kitu chenye maana zaidi ya kitu hicho. Fasili yake imetusidia kuchambua ishara katika riwaya teule za Mwingizi na zaidi imetusaidia kutambua neno moja au sentensi yaweza kuwakilisha ishara zaidi ya moja. Pili anafafanua namna ishara hujitokeza katika fasihi, kwa kusema ishara katika fasihi ni zaidi ya maana ya kitu kilichotajwa. Andiko la Snowden (khj.) andiko lake limetusaidia kuelewa maeneo ambamo ishara hujitokeza kwani anaeleza wazi ishara hujitokeza katika vitu hai, visivyo hai na katika vitu dhahania. Aidha, wanazuoni hawa wametusaidia kujua fasili ya neno ishara. kwa kueleza mazingira ambamo ishara hujitokeza na kudhihirika katika fasihi.

#### 1.8.3.1 Dhana ya Uashiriaji

Uashiriaji ni mbinu ya kifasihi ambayo ina historia ndefu. Kulingana na Abrahms (1971:170) uashiriaji kama mbinu ya kuwasilisha maana katika matini za kifasihi ulianzia kule Ufaransa katika karne ya 19. Abrahms anasema kuwa mwasisi wa mbinu hii ni Baudelaire katika diwani yake ya mashairi *Les Fleurs du Mals* (1857) yaani “Maua ya Maovu.” Watunzi wa mashairi ya Kifaransa wa wakati huo kama Rimbaud, Verlaine, Mallarme na Valery walitumia sana uashiriaji uliohusu matumizi ya ishara za ki binafsi. Katika kipindi hiki uashiriaji kama mkondo wa ushairi uliangaliwa kama mbinu ya kukuza maudhui kwa kujenga uwiano, toni na wizani kitaswira kwa matumizi ya lugha teule. Wakati huu uashiriaji uliangaliwa kama mtindo hasa katika ushairi. Baadaye, uashiriaji kama mbinu ya kifasihi ulienea na kuanza kutumika huko Uingereza na Marekani mwishoni mwa karne ya 19 na mwanzoni mwa karne ya 20 katika ushairi.

Nabukonde (2012: 5) akimnukuu Eliot, anasema kuwa "njia pekee ya mtu kuwasilisha hisia zake kwa umbo la sanaa ni kutafuta kitu au chombo chenye mahusiano kama vile mkusanyiko wa vitu, hali, mfuatano wa matukio, ambao utakuwa fomula ya kuwasilisha hisia hizo." Kutokana na maelezo ya Eliot uashiriaji ni mbinu muhimu katika kuwasilisha hisia za mtunzi na wahusika katika matini bila kuonekana kuibeza hadhira kama alivyofanya Mwingizi katika riwaya zake kwa kutumia vitu kama vile pete, vikapu, wanyama, n.k. katika kuwasilisha hisia zake kupitia vitu hivyo. Mwingizi kwa kutumia vitu hivi ameweza kuashiria vitu mbalimbali.

Perrine (2014: 173) anaeleza kuwa uashiriaji ni matumizi ya vitu au matukio katika kazi ya kifasihi kiishara. Mbali na vitu na matukio uashiriaji pia unahusu matumizi ya dhana, jina na mandhari kuibua maana za ziada akilini mwa msomaji. Naye Frye (1985: 452) anadai kuwa uashiriaji ni matumizi ya kipekee ya ishara yanayodhihirisha neno kwa maana yake ya kawaida. Kwa mfano, neno waridi linarejelea ua linaloitwa waridi na dhana inayojitokeza nyuma ya maana, yaani urembo. Kwa sababu hii, ua la waridi hutumika kuashiria urembo au umaridadi.

Uashiriaji hulenga kuibua maana mbili, maana ya kawaida ya kiashirii na maana inayohusishwa na kiashirii. Kama anavyodai Cirlot (1962: 14) uashiriaji kiyakinifu ni mfumo unaorejelea mahusiano changamano ambapo uhusiano mwimo ndio unaotawala. Uhusiano huu huunganisha hali halisi na hali dhahania. Hali halisi hurejelea maana ya kawaida inayojulikana na watumizi wa lugha husika ilhali hali dhahania hurejelea maana ya kifasihi inayowakilishwa na ishara. Kimsingi, uashiriaji ni mtindo wa kisanaa wa kutumia vitu, maneno, hali na tukio kwa kusudi la kuwasilisha wazo kidhahania.

Wanyonyi (2015) anasema watunzi wa kipindi hiki waliotumia ishara ni kama Eliot, Arthur Symons, Cummings na Wallace Stevens. Anaendelea kusema kwamba hii haina maana kuwa uashiriaji ulianza tu katika sehemu hizi za dunia kwa sababu uashiriaji ni mbinu inayojitokeza katika ushairi wa Kiswahili ulioandikwa katika kipindi hiki pia. Kwa mfano, katika *Utenzi wa Al-Inkshafi* (1820) kuna ishara nyingi zilizotumika kama

vile mahame na magofu kuashiria kuanguka kwa ufalme wa Pate. Lililo dhahiri katika maelezo ya Abrams ni kuwa utanzu wa fasihi uliotumia uashiriaji mwanzo ulikuwa ushairi. Mwanzoni mwa karne ya ishirini barani Ulaya kazi nyingi za kifasihi zikiwemo mashairi, riwaya na michezo ya kuigiza zilidhihirisha matumizi ya uashiriaji, hususani zile zilizokuwa na mitazamo ya kidini na kijadi.

Wanyonyi (khj) anaendelea kusema uashiriaji ulibainika katika matukio, mandhari na matumizi ya lugha. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kusadikika* (1951) ya Shaaban Robert, mandhari ya nchi inayoelea angani yanaweza kuangaliwa kama ishara ya taifa lisilo na msimamo wa haki, sheria na maendeleo thabiti. Pia katika riwaya za Mwingizi uashiriaji umebainika pia katika matukio, mandhari na wahusika katika kuashiria mambo mbalimbali. Mfano mzuri katika riwaya ya *Vita vya Mapenzi* ambapo kuna matumizi ya mandhari ya baharini kwa kuonyesha kwamba kuna nchi iko chini ya bahari na inaongozwa na viongozi mbalimbali wanaong'ang'ania mamlaka kwa ajili ya kuendelea kuwanyonya wananchi wao kupitia nyazifa hizo.

**1.8.3.2 Uamilifu wa Ishara na Uashiriaji**

Birkerts (1993) anasema kuwa ishara za kifasihi hupata maana kwa kutumiwa kiuradidi katika kazi za kifasihi au kwa kuwekwa kimakusudi kisanaa katika tukio kama ilivyo katika riwaya za Mwingizi ishara kama vile mwanga, giza na mimba ambazo zimetumika pia kiuradidi katika kumaanisha maana mbalimbali katika kuibua maudhui. Aidha Mutiso (1996) anasema pia ishara na uashiriaji huwa na umuhimu mkubwa katika ujenzi wa kazi ya kifasihi. Ishara huwa kifaa dokezi cha maana za ziada ili kazi ya kifasihi iweze kuibua fikra na hisia changamano bila maelezo marefu. Kwa upande mwingine Njogu na Chimerah (1999: 34) wanasisitiza kuwa ishara hueleweka katika muktadha wa kitamaduni au wa kimatini. Ufasiri wa ishara kwa maana hii hutegemea ufahamu wa utamaduni wa jamii iliyosawiriwa, itikadi zake na uelewa wa mpangilio wa kiubunifu wa ishara katika kazi yenyewe. Kwa hivyo, uashiriaji husaidia kuweka wazi itikadi na tamaduni za jamii.

Naye Nabukonde (2001) katika kazi yake anahoji kwamba, mtunzi wa kazi ya kibunilizi huwa anatumia ishara kuwasilisha hisi zake. Zaidi anataja mahali ambapo vipengele vya kiishara huweza kutokea ambapo ni katika mkusanyiko wa vitu, hali na mfuatano wa matukio. Andiko lake limetusaidia kujua na kwa kiasi kukisia sababu za Maundu Mwingizi kutumia mbinu ya uashiriaji ambayo imemwezesha kuibua ishara mseto na changamani katika riwaya zake. Hoja na kauli za Nabukonde zimetusaidia kubaini, kuorodhesha na kutabakisha ishara kadri zilivyotumika katika riwaya teule za Mwingizi. Vilevile kauli za mwandishi huyu zimekuwa nguzo nzuri ya marejeleo popote pale tulipochambua, tulipofasiri na kusanisi ishara katika tasnifu hii. Hata hivyo, mtazamo wake ni wa jumla mno kwani hataji moja kwa moja ni aina gani ya sanaa inayohusika. Wanazuoni Cirlot, Nabukonde, na Perrine (wameshatajwa) wanakubaliana juu ya uwepo wa ishara katika kazi za fasihi na mtunzi huzitumia kwa madhumuni mbalimbali.

Ni muhimu kutahadharisha kuwa ishara huweza kutumiwa kuashiria maana ya ziada au isiyo ya kawaida katika kazi za kifasihi. Mfano ni ule wa msalaba uliotolewa na Wanyonyi ambao unaweza pia kuwa ni ishara ya kifo kwa sababu ni ishara ya kibia ambayo husisitiza maana fulani.Wamitila (2003:113) alisisitiza mwelekeo huu alipozungumzia matini wingi kwa kusema, Matini ya kifasihi haiwezi kubanwa kwenye maana moja. Huwa ina maana nyingi, yaani uashiriaji wingi. Aghalabu maana hizi huwa hazihusiani. “Dhana ya matiniwingi inahusishwa kwa kiasi kikubwa na mhakiki wa ki-Semiotiki anayejulikana kama Roland Barthes”. Jambo analosisitiza Wamitila ni kuwa, ishara huwa na maana nyingi ambazo hazina uhusiano.

Vilevile ishara huakisi dhima ya ikitisadi katika matumizi ya lugha. Sifa hii inadhihirika katika maelezo ya Kennedy na Gioia (2005: 217) wanaposema kuwa, ishara hazisimamii tu maana moja bali huweza kuwa kivuli kilichotanda kote. Aidha, uibuaji wa fikira na hisia huzifanya ishara ziwe na uamilifu wa kudokeza hali za kisaikolojia katika kazi za kinathari. Kama ilivyokuwa katika riwaya za Mwingizi ishara nyingi zimekuwa na maana zaidi ya moja. Kwa mfano pana wakati rangi nyekundu imekuwa

ikiashiria unyonyaji na unyanyasaji wa wananchi bila hatia na wakati mwingine imetumika katika kuashiria neema.

Otoro (2012) akihoji juu ya **"**Msimbo na Maana katika *Zilizala* " akitumia nadharia ya Semiotiki, alifafanua kwa undani uwepo wa aina tano za misimbo na kufasiri maana za misimbo hiyo kama zinavyoonekana katika *Zilizala.* Alitumia mawazo ya Roland Barthes (1994) kuhusu msimbo wa kisimulizi, kihemenitiki, msimbo wa kitamaduni, msimbo wa kiishara na msimbo wa kihusika. Katika kushughulikia mada yetu, misimbo ya kiishara, kitamaduni, kihusika na kihemenitiki imekuwa yenye manufaa katika utafiti wetu wa kuchanganua matumizi ya ishara katika katika *Vita vya Mapenzi, Mzimu wa Waufi* na *Tanzia.* Sisi hatujafasiri misimbo ya Barthes bali tumechanganua ishara katika riwaya husika. Hata hivyo, tumeegemea mawazo ya mwanaisimu Saussure kuhusu kiashirii na kiashiriwa. Pia tumezingatia mawazo ya mwanafalsafa Mmarekani Peirce kuhusu kielelezo cha ishara chenye pembe tatu, yaani ishara, yambwa na kifasiri.

Naye Perrine (khj) anaonyesha jinsi uashiriaji unavyoopelekea ishara kutokea katika kazi za fasihi na anataja vipengele ambavyo ishara hujitokeza mfano katika matumizi ya dhana, jina, na mandhari ili kuibua maana ya ziada kwa msomaji. Zaidi anaeleza kwamba, katika kazi ya fasihi kuna matukio mengi ya kiishara. Pia amekuwa anazungumzia fasihi andishi kwani anaeleza kwamba ishara huibua maana za ziada kwa msomaji. Hata hivyo, hajaweka wazi ni utanzu gani katika fasihi andishi anaouzungumzia hapa kwa kuwa, anatoa maelezo ya jumla akirejelea kazi za fasihi andishi. Kauli na hoja za Perrine zimetuwezesha kubaini katika utafiti wetu mahusiko na ufasiri wa ishara kama mkakati wa kuwasilisha maudhui ya aina nyingi. Hii ndio maana tumechunguza ishara mbalimbali ambazo zimeonekana katika riwaya za Mwingizi. Katika riwaya za Mwingizi ni dhahiri mna ishara halisi, ishara za kiajabu pamoja na ishara mseto zinazojumuisha uhalisia na uhalisiajabu.

#### 1.8.3.3 Aina za Ishara

Baadhi ya wanazuoni wametaja aina za ishara ambazo huonekana katika kazi za fasihi kwa ujumla. Frye (khj) anataja aina tatu za ishara ambazo ni ishara bia, ishara za kaida, na ishara za kifasihi. Mbatia (2002:23) anafasili ishara ambazo zimepewa maana mahususi na jamii au utamaduni fulani. Anaendelea kueleza ishara za kifasihi ni zile zinazoibuliwa na mtunzi kutokana na ufahamu wake. Vilevile anasema ishara bia ni ishara za kaida na tajriba zake za mazingira alimokulia mtunzi ambazo pia, huitwa ishara za ki binafsi, kwa vile huegemea mtazamo fulani wa matini. Naye Wamitila (khj) anafasili ishara bia kuwa ni ishara ambazo hutambuliwa na waliowengi, yaani jamii ya kimataifa, (matumizi yake hupita mipaka ya jamii ndogo, kabila, kundi la watu au nchi). Anaendelea kusema ishara za aina hii huweza kufasiliwa na kupewa maana angalau moja, kwa mfano, mto katika maisha ni ishara ya misukusuko anayokumbana nayo mtu katika maisha, mvua ni ishara ya neema katika maisha, milima katika maisha ni ishara ya matatizo yanayomkumba mtu na pete ya ndoa katika maisha ni ishara ya mkataba wa kuishi pamoja kama mke na mume.

Utabakishaji huu wa ishara kama wanavyohoji waandishi hawa umetuwezesha kupanua mawazo na mitazamo yetu ya kiuchanganuzi ambapo tumejiepusha kuzungumzia ishara zilizo katika riwaya za Mwingizi kwa mitazamo ya kijumla na badala yake tumezizungumzia ishara zilizoko kimatapo. Kwa mfano, kutambua ni lini ishara husika ni ishara ya kihalisia na lini ni ishara ya kiajabu. Kwa mfano, katika *Vita vya Mapenzi* ilipotokea ajali ya basi, ishara ya wekundu imetawala, wekundu wa damu, wekundu wa begi lililokuwa na pesa, ambapo wekundu huu unawezesha ufasiri mseto wa matukio hayo.

Kwa upande mwingine maandiko ya Frye, Mbatia na Wamitila (wameshatajwa) ni muhimu katika utafiti huu, Frye amebainisha aina za ishara. Uainishaji wake umetusaidia katika utafiti huu kwa kutuwezesha kuzitabakisha ishara pale zimejadiliwa. Mbali na uainishaji wake wa kutaja ishara za kifasihi ambazo utafiti huu umezishughulikia, uainishaji huo umetuwezesha kujaliza ishara nyinginezo na kwa njia

hiyo kutuwezesha sio tu kupanua mjadala, bali pia kupanua mawanda ya uelewa na ufasiri wa ishara. Katika utafiti huu tumeshughulikia pia ishara za kifasihi na maandiko haya yametupa mwanga na uelewa wa namna mtunzi wa kazi za fasihi hutumia mbinu ya kiishara kufikisha ujumbe na kukamilisha maudhui yake. Wote Frye na Mbatia (wameshatajwa), wanataja ishara za kifasihi ambazo utafiti wetu umezishughulikia, hivyo ufafanuzi wao umetusaidia katika uchambuzi wa ishara za kifasihi katika riwaya teule.

**1.9. Mbinu za Ukusanyaji Data**

Ziko mbinu mbalimbali za uteuzi wa sampuli, lakini sampuli ya utafiti huu iliteuliwa kwa kutumia mbinu ya uteuzi wa madhumuni maalumu au sampuli lengwa yaani uteuzi ambao mtafiti kwa makusudi hulenga kuteua kundi la watu/vitu ambavyo anaamini kuwa ni rasilimali anayoitegemea katika utafiti wake. Sababu ya kuteua mbinu hii tuliona kwa kupitia riwaya hizi tatu za Maundu Mwingizi zenye matukio ya kutisha na kuogofya ya kijiuchawi na ushirikina ndiko tungepata data za kutosha kutokana na malengo yetu ya utafiti, na ndivyo imekuwa hivyo.

Utafiti huu umetumia mbinu ya ukusanyaji wa data ya maktabani tumesoma riwaya teule za *Vita vya Mapenzi* (2012), *Mzimu wa Waufi* (2013) na *Tanzia* (2015) za Maundu Mwingizi ambazo zimetupatia data za msingi za utafiti wetu. Yaani maswala na hoja zote kuhusiana na jiniuchawi na ushirikina, na data hizo pia zimejumuisha matukio na mandhari, wahusika, ishara, mahusiano na maudhui mbalimbali ambayo yamechimuzwa na kutuletea dhamira mbalimbali katika riwaya teule. Pili, tumefaidika pakubwa na maandiko, vitabu na majarida mbalimbali katika kuzisoma na kuzielewa vizuri nadharia teule zilizotumika katika utafiti huu, dhana nzima ya uchimuzi kama kiini cha utafiti wetu, dhana nzima ya uchawi na ushirikina, njia za utafiti mpaka kufikia mahitimisho tuliyoyafikia. Tasnifu mbalimbali zimetusaidia kubaini mianya mbalimbali ambayo imepelekea utafiti huu kubaini kwamba kuna mwanya wa kufanyia utafiti kuhusu swala la jiniuchawi na ushirikina kama mkakati wa uchimuzi katika riwaya teule. Katika uchambuzi wetu wa data tumebainisha malengo yetu ya utafiti.

Data zilizokusanywa kutoka katika tasnifu, vitabu na majarida ni zile zilizokuwa zinajadili kwa upana na kwa kina dhana za uhalisiajabu, maudhui yanayojitokeza kutokana na matumizi ya uchawi na ushirikina kama mikakati ya uchimuzi. Kwa upande wa usomaji wa riwaya teule, data ambazo zimekusanywa ni zile zimeweza kuonyesha mandhari na matukio ya kijiniuchawi yalivyopelekea kuibuka kwa maudhui mbalimbali, wahusika wa kijiniuchawi na ishara na uashiriaji kama mikakati ya uchimuzi katika riwaya za Maundu Mwingizi katika kuibua maudhui mbalimbali. Data hizo zimepangwa kulingana na malengo yetu yaani kuanzia lengo la kwanza mpaka la mwisho.

**1.10 Uchanganuzi wa Data na Uwasilishaji wa Data**

Mtafiti amefanya uchambuzi wa kitaamuli[1]. Hivyo, uchakataji wa data umefanywa kwa njia ya maelezo. Uchambuzi wa kitaamuli umetupa fursa kama watafiti kusoma matini husika na kisha kuelewa maana, sababu, maudhui, falsafa, makusudio na mtazamo wake. Kwa kutumia mkabala huu, data zilizokusanywa katika kazi hizi teule zimechambuliwa kwa mkabala wa kimaelezo. Ili kufanikisha hilo, uchakataji wa data umeongozwa na hatua zilizopendekezwa na Willing (2001), ambaye anasema kuwa, kuna hatua sita ambazo mtafiti anaweza kuzifuata wakati wa kuchakata data.

Kutokana na maswali na malengo mahususi ya utafiti katika swala zima la uwasilishaji wa data mtafiti ametumia hatua tatu kati ya hizo sita. Hatua ya kwanza ya uchanganuzi wa data imehusisha kusoma kwa makini matini mbalimbali husika. Hapa mtafiti amesoma riwaya teule za Mwingizi, tasnifu mbalimbali zinazohusiana na zinazoelekeana na kiini cha mada yetu ya utafiti, vitabu mbalimbali na matini nyingine zinazohusiana na utafiti huu. Pili wakati wa kusoma riwaya teule mtafiti amebainisha sura au kurasa za sehemu ambazo zimekuwa zinaonyesha mandhari, wahusika na ishara

---

1 Utaamuli ni aina mojawapo ya mwegamo wa kufanyia utafiti. Katika mwegamo huu, utafiti hutumia zaidi tafakuri katika kuhusisha taarifa mbalimbali za kitafiti na kisha kutoa ufafanuzi kwa kuzingatia misingi ya nadharia husika pamoja na ithibati bayana zipatikanazo ama maskanini (uwandani) au katika matini. Aghalabu, mwegamo huu hutumiwa sana na tafiti zihusuzo fani mbalimbali za sayansi za jamii pamoja za fani za sanaa (kama huu). Tafiti za kitaamuli hutumia mbinu za maelezo, ulinganisho, pamoja na uhusishaji wa data dhidi ya misingi ya nadharia katikakuchanganua data zake na kutolea matokeo. Hii ni tofauti kabisa na tafiti za kitakwimu ambazo huweza kutumia majaribio na mikokotoo ili kupata majawabu kuhusu mabunio ya tafiti hizo (Baradyana na Ame, 2007; Mason, 2010).

mbalimbali za kijiniuchawi na ushirikina zilivyoibua maudhui mbalimbali katika riwaya teule. Katika hatua ya tatu tumewasilisha matokeo ambayo yameweza kuonyesha maudhui mbalimbali kupitia malengo yetu. Upitiaji wa hatua hizi ni muhimu kwani umeweka msingi kwa hatua nyingine zote zilizofuata katika uchakataji wa data za utafiti huu. Kwa kuwa uchambuzi wa data za utafiti huu umefanywa kitaamuli, usomaji kwa makini wa matini husika umetupa fursa ya kuelewa kwa undani vipengele vya mandhari, wahusika, dhamira, ishara, msimamo na mtazamo wa mwandishi wa kazi hizo.

# SURA YA PILI

# DHANA YA UCHIMUZI, JINIUCHAWI NA USHIRIKINA KAMA VIPENGELE VYA UHALISIAJABU

## 2.1 Dhana ya Uchimuzi na Historia Yake

Uchimuzi ni mbinu ya kimtindo na kiutekelezi inayotumika katika uandishi wa kifasihi kuelezea mambo fulani yanayopewa uzito zaidi ya mengine katika kazi za fasihi na kuyafanya mambo hayo yajitokeze waziwazi kama mambo yaliyopewa kipaumbele yakilinganishwa na mengine kidhamira, kidhima na kimaudhui katika kazi husika. Kuhusiana na mbinu hii, Halliday kama alivyonukuliwa na Chatman (1971) anasema kwamba uchimuzi ni ukiukwaji wa kimaudhui na wa kimakusudi wa vipengele vya lugha vinavyochimuzwa na havina budi kuibua dhamira iliyokusudiwa katika ufumaji wa matini.

Uchimuzi, katika mapana na marefu yake, unarejelea mbinu na taratibu za kiutunzi katika kazi za kifasihi zinazotumiwa kuangazia au kuweka wazi tukio, hali, kitu au usemi fulani mbele au kwa namna wazi hivi kwamba lugha inayotumiwa kuweka kipaumbele katika tukio, hali, kitu au usemi wenyewe inaangaza upekee, umuhimu au upya wa uelezaji. Huu ni utaratibu ambao unaonyesha jinsi ambavyo lugha ya kifasihi inavyoweza kutumiwa kuusawiri uhalisi wa maisha au uhalisi unaoakisi maisha. Kwa hivyo, lugha hiyo inaweza kujumuisha ukiukaji wa kaida za lugha ya kawaida kwa makusudi ili kuakisi uhalisi mpya, wa kipekee au uhalisi katika mipaka ya uwezekano.

Katika mitazamo ya awali kuhusu uchimuzi, Leech (1968:57) anasema kwamba ni vizuri katika kazi yeyote ya kifasihi inayoeleza mambo ya msingi katika jamii na ikaonekana kwamba inaweza ikaleta shida katika kufikisha ujumbe kwa njia ya kawaida basi ni bora kutumia uchimuzi ili kuelezea mambo hayo kusalia kukaa kimya. Kwa hivyo, mbinu hii ya uchimuzi imetumiwa na waandishi wengi wa kimajaribio kwa sababu ya ukunjufu wake kimatumizi, ubunifu wake wa kiuwasilishi, ufaafu wake wa kiuwasilishi na utokawaida wake wa kufumbata mambo na kuionyesha jamii mambo

ambayo hayangeweza kuzungumzwa kwa njia ya kawaida, au ambayo hayangeibua athari iliyokusudiwa au yangewasilishwa kwa njia za kawaida. Utokawaida huu unaweza kujumuisha uwasilishaji katika misingi ya ushitukizaji, ufikirikaji upya, uyumbishaji wa mantiki ya kiwakati na uwezekano wa ulimwengu mbadala wa kutazama na kutathmini mambo ya kijamii yachukuliwayo kuwa ya kawaida isipokuwa kwa kutumia mtindo wa uchimuzi.

Leech (1968) anaendelea kusema kuwa fasihi inatambuliwa kwa misingi ya sifa bainifu mbili; uthabiti na utaratibu wa uchimuzi. Uchimuzi katika matumizi ya lugha ya kawaida kama vile ya mazungumzo ama ya uandishi wa habari hutokea bila mpangilio ama utaratibu fulani, lakini uchimuzi katika matini za kifasihi ni muundo unaofuata utaratibu na mfumo fulani mahususi, ambapo sifa kama sitiari hujitokeza na seti moja ya sifa hutawala nyinginezo. Sifa hii inarejelewa na Jakobson (1966) kama "*the dominant*" (sifa tawala). Vinginevyo, dhana ya uchimuzi inaweza kutazamwa ama kama muundo na hivyo, kusisitiza mbinu zinazopewa kipaumbele au kama kiashiria na hivyo kusisitiza maswala yanayoangaziwa. Huu ndio mkabala unaochukuliwa na Van Peer na Hakemuilder (2006) wanapohoji kwamba maana ya uchimuzi inafungamana na dhana ambayo huonyesha ujumbe fulani ambao unakuwa umefumbwa katika matini kwa lengo kumwezesha msomaji aweze kusoma na kuelewa nini kimekusudiwa na mwandishi wa matini kwa ujumla na nini kinachosisitizwa katika ujumla huo wa mambo. Maana hii inatupeleka mbali zaidi katika riwaya za kimajaribio ambazo zimetumia lugha ya kimafumbo kwa kiasi kikubwa na ambayo inamtaka msomaji atulie na asome kwa makini ili ajue kinachomaanishwa kwa ujumla na kinachosisitizwa na mtunzi katika riwaya za kimajaribio. Uhalisi huu wa ujumla wa mawasilisho ya mambo na msisitizo wa mambo mahususi unajidhihirisha katika riwaya teule za Maundu Mwingizi. Hii ni kauli ambayo pia inaafikiwa na Miall na Kuiken (1994: 395) wanaposema kwamba uchimuzi ni mbinu ya kimkakati inayotumiwa kuonyesha mambo yote yaliyo kinyume kwa kuyavunjavunja ili yaweze kuleta maana fulani iliyokusudiwa.

Jan Mukarovsky (1961), anafafanua dhana ya uchimuzi kwa kuhusisha uchimuzi na ukiukaji wa kaida za lugha ya kawaida kwa makusudi ili kuakisi uhalisi mpya. Ukiukaji huo huonyesha uwezo wa kukiuka kaida ambazo katika miktadha ya mazoea hudhihirisha ufasihi katika kazi za kubuni. Anaendelea kusema uchimuzi huibua athari ya *ostraneniya* yaani kufanya ajabu ili kuondoa uzoefu. Mukarovsky (khj) anasisitiza kwamba, uwezo huu wa kukiuka kaida ndio hujenga ufasihi ama usanii katika lugha. Kulingana naye, utaratibu unaoandamana na ukiukaji wa kaida za matumizi ya lugha ndio hujenga kazi ya kifasihi. Hivyo, sababu mojawapo inayotufanya tusichoshwe na kazi za kinathari za kimajaribio ni ule utumikizaji wa miundo ya lugha isiyo ya kawaida inayotuwezesha kutambua ukweli unaowasilishwa kwa njia ya ajabu, mpya au mbadala inayochimuza mambo kadhaa kama ilivyo katika riwaya teule za Mwingizi.

Shklovsky kama anavyonukuliwa na Fokkema na Ibsch (1979:15) anaona fasihi ni taaluma yenye uwezo wa kuifanya hadhira kuutazama ulimwengu inamoishi kwa njia tofauti zinazowezesha kufikirika upya kwa mambo, njia mpya na mbadala tofauti na vile ambavyo imezoeleka katika miktadha ya kawaida. Kwa mfano, katika kusimulia matukio kuna matarajio ya mazoea kwamba, matukio hayo yataelezwa kwa misingi ya mpito wa wakati. Kwa mfano, katika riwaya ya *Vita Vya Mapenzi* ambapo mipaka na mpito wa wakati vimeyumbishwa. Kwa hivyo, usafiri kwa matumizi ya pete unaopuuza uhalisia wa masafa si jambo la ajabu.

Ili lugha iweze kuekezwa na maana ya kifasihi, ni sharti lugha hiyo ibainishwe na kufanywa kuwa ngeni, bunifu na iwezeshayo mitazamo mbadala na vilevile kwa kuitumia katika miktadha isiyo ya kawaida. Upekee wa fasihi hutokana na jinsi fasihi inavyobadilisha kiubunifu kategoria za lugha ya kawaida na kwa namna hii kuwafanya wasomaji kuliona swala fulani tofauti na walivyozoea kuliona kila siku. Mbinu hii hutumika kuelezea kuwa sanaa au fasihi hutuchangamsha na kutukumbusha juu ya maisha na uzoefu wetu kwa njia ngeni. Hii ni sifa ambayo imedhihirika katika riwaya teule za Mwingizi ambapo mwandishi anatudokezea mambo ambayo yanapatikana katika jamii zetu na kwa namna hii kutukumbusha juu ya sifa hasi za viongozi wetu

katika nyanja na harakati mbalimbali za maisha. Kwa upande mwingine riwaya hizi zinatutahadharisha juu ya athari za utandawazi katika nchi zinazoendelea, hali kadhalika kupambanua na kuangazia macho umma kutathmini mambo, japo madogo, yeye athari hasi na madhara makubwa kwa jamii. Haya yote ni mambo yanayowezekana kwa kutumia mbinu kadha wa kadha za lugha kwa njia bunifu na kwa njia mbadala.

Kulingana na Shklovsky (1965), kuna njia kadha za kuonyesha mambo kuwa mageni ama kuondoa uzoefu katika mambo hayo. Athari ya mbinu kama usambamba, tashbihi, urudiaji, na balagha ni kukibadilisha kitu kutoka hali yake ya kawaida na kukifanya kipya, yaani, ilimradi tu upya huo uwe katika upeo wa uwezekano na kufikirika, ndipo maana mpya na ambayo ilikuwepo nayo inajitokeza. Athari za matumizi ya kiubunifu ya mbinu kadhaa zimechimuzwa na kufanya mandhari, maudhui, wahusika na ishara mbalimbali katika riwaya za Mwingizi kujitokeza kwa njia mpya, njia zinazowezekana na zilizo katika upeo wa kufikirika, katika kuieleza hali halisi ya mambo mbalimbali yanayozikumba jamii zetu.

Uchimuzi katika matini za kifasihi hutumiwa kwa makusudi na huwa na maana mahususi. Wakati ambapo msomaji anakumbana na miundo ya uchimuzi katika matini anayoisoma, mbali na kutambua miundo hii, humfanya atafakari motisha kuu ya matumizi ya mbinu hizo kama zilivyotumikizwa na mwandishi katika matini husika. Katika kujaribu kupata motisha, msomaji huweza kupata maana inayosisitizwa na ujumbe ambao unapewa kipaumbele na umewasilishwa na mwandishi katika kazi ya kinathari au ushairi. Kwa hivyo, katika kuhakiki dhana za jiniuchawi na ushirikina kama mkakati wa uchimuzi katika riwaya teuleza Maundu Mwingizi, tasnifu hii imebainisha motisha kuu ya kila mbinu husika kama mkakati wa kubainisha dhamira kuu ya mwandishi.

Kimsingi, mtazamo uliochukuliwa katika utafiti huu unahoji kwamba, uchimuzi ni matumizi ya kiubunifu, mapya na mbadala ya mbinu mbalimbali za lugha katika matini za kifasihi zenye kuibua athari fulani mahususi kwa msomaji na ambazo hujitokeza kwa

uwazi zikilinganishwa na lugha ya kawaida. Kuhusiana na kauli hii, Martindale (2006) anasema kwamba, kuna aina mbili za uchimuzi; aina ya kwanza ni uchimuzi wa usambamba na aina ya pili ni uchimuzi wa ukengeushi au uchepuzi. Anaendelea kusema uchimuzi wa usambamba umekuwa ukijitokeza zaidi katika ushairi kwa kutumia vipengele vya foni, silabi, maneno na sentensi. Na uchimuzi wa ukengeushi umekuwa ukitokea zaidi katika kazi za kinathari na hutumika kuonyesha vitu kinyume cha mazoea katika kazi za kinathari ukiwemo utanzu wa riwaya.

Hakemuilder (2007) anasema kwamba, uchimuzi wa ukengeushi hutumika zaidi katika kazi za fasihi kwa kutumia lugha ya sitiari, mafumbo na lugha ya picha katika kufikisha ujumbe kwa hadhira. Aina hii  ya uchimuzi wa ukengeushi imedhihirika vizuri zaidi katika riwaya za Mwingizi kwani mtunzi ametumia lugha ya ukengeushi inayowezesha ulimwengu wa kawaida, mahusiano ya kimazoea, maingiliano ya kawaida na mitagusano ya kila siku, kufikirika na kuonekana kwa njia mpya au njia mbadala na kwa njia hii kufikisha ujumbe wake kwa hadhira.

Kwa mujibu wa Leech na Short (1981), Peer na Hakemuilder (2007) na Mugwika (2012) uchimuzi ni neno lililotokana na Garvin (1964) kama tafsiri ya neno la lugha ya Czech ‘aktualisace’. Ingawa neno uchimuzi liliundwa kwa njia hii na wanamuundo wa Prague, dhana yenyewe sio uvumbuzi au ubunifu wao, bali mawazo yao yalikuwa tu ukuzaji wa kihistoria wa mawazo yaliyoasisiwa na wana-Urasimu kama Viktor Shklovsky (khj) anayehusishwa na mbinu ya *ostranenia* au uajinabishaji. Kulingana na Shklovsky, umuhimu wa sanaa ni kukifanya kitu kuonekana kama kisicho cha kawaida na kwa namna hiyo kusawiriwa kwa njia mpya.

Ingawa dhana ya uchimuzi ilisisitizwa zaidi na wana-Urasimu katika karne ya ishirini, ni dhana yenye asili yake kutokana na mawazo ya Aristotle katika kazi yake ya *‘Poetics’*. Aristotle alisisitiza kwamba, matini za kifasihi huzingatia kanuni na kwa njia hii mbinu za ukiushi na usambamba huchukua nafasi kubwa. Kwa mujibu wa mawazo yake, uteuzi wa matumizi ya maneno katika kazi ya kifasihi lazima upambanuliwe. Ili

kufanikisha athari hizi matumizi ya maneno yasiyo ya kawaida, sitiari, maneno ya kiajabu na miundo mirefu ya sentensi au maneno hutumiwa. Hali hii imejidhihirisha katika riwaya za Mwingizi kwani mtunzi ametumia sitiari, maneno ya kiajabu na miundo mirefu ya sentensi ni dhahiri kuwa uchimuzi wa ukiushi na usambamba umedhihirika.

Wamitila (2008) anasema kwamba hapo mwanzo neno uchimuzi lilitumika sana katika kazi za kiisimu na ushairi kwa kiasi kikubwa. Lakini sasa neno hili limekuwa likitumika katika bunilizi za kimajaribio katika kukabiliana na wimbi la uhitaji wa jamii na ndio maana hata sanaa nayo imebadilika ili iweze kukidhi mahitaji ya hadhira yake. Uhalisi huu umejitokeza pia katika riwaya za Mwingizi inapozingatiwa kwamba kazi zake zimesheheni sio tu ishara bali pia ulimwengu unaokiuka uhalisia wa mazoea. Kwa mfano, katika *Mzimu wa Waufi* mtunzi anatuchorea ulimwengu ambapo wizi wa mimba ya miezi mitano ni jambo linalowezekana na kwa njia hii anatuacha katika mshangao, kulikoni! Kiusomi, hata hivyo, haya hayaishii katika mshangao ila maswali yanaibuka, mtunzi anachimuza nini hapa?

Jefferies na Mcilntyre (2010) wanasema kwamba, ‘uchimuzi’ ni neno lililoibukia kutoka katika nadharia ya elimumtindo[2]. Wanaendelea kusema kwamba, kutokana na maendeleo ya uchambuzi wa lugha katika karne ya ishirini elimumitindo iliweza kusonga mbele zaidi kwa sababu ya uibukaji wa nadharia ya uchimuzi katika elimumitindo. Lengo la kuanzisha dhana hii ya uchimuzi ni kutaka kuonyesha umuhimu wa kufasili kazi mbalimbali kwa kutumia matini kwa lengo la kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Mtindo huu wa utumiaji wa uchimuzi katika kazi za kifasihi umedhihirika sana katika kazi za Mwingizi. Kwani mtunzi ametumia dhana hii ya uchimuzi katika kuchimuza mambo mbalimbali yanayopatikana katika jamii kama vile

2 Leech (1969:2) anasema elimumitindo ni uhakiki na fasiri ya matini katika mtazamo wa kiisimu. Kama taaluma, inafungamanisha uhakiki wa kifasihi na kiisimu ingawa haijisimamii kivyake. Msamiati mpana wa kimsingi wa uhakiki wa kifasihi hususan kinaya/kejeli, sitiari, usambamba taswira, na jazanda kinyume, hauwezi kufafanuliwa Bila kurejelea dhana za kiisimu. Kwa hivyo, kama msingi wa kutumia taaluma za kifasihi na za kiisimu, elimumitindo ni uwanja ambamo maswala haya hushughulikiwa.

maswala ya uwajibikaji, utendaji haki, wajibu wa viongozi kwa wananchi wao, jinsi utandawazi ulivyoathiri utamaduni na mambo mengineo.

Jakobson (1980), anasema kwamba lengo la uchimuzi ni kujikita zaidi katika uchanganuzi wa matini za kifashi, japo hutumika pia katika kuchanganua matini zisizo za kifasihi kama vile, matangazo ya biashara, mabango, vibwagizo, maandishi ya kitaaluma, hotuba, n.k. Ili matini iwe ya mafanikio haina budi kutumia mbinu za uchimuzi zinazochanganya ala tofauti, ishara, picha au sauti na usasambuaji wake unahitaji matumizi ya mkabala wa uwili. Lengo la pili la uchimuzi uwe wa kiisimu au usio wa kiisimu ni kunogesha lugha iliyotumika kwa kuichachua. Katika misingi ya uelewa huu, tunaona Mwingizi katika kazi zake teule ametumia lugha ya picha, matumizi ya ishara. Kwa mfano katika riwaya ya *Vita Vya Mapenzi* anaonyesha serikali ya Budha iko baharini na wahudumu wake wanafanya kazi zao huko baharini. Mwandishi anachimuza hali halisi kwa kutumia lugha ya picha za jinsi serikali zilizopo huku duniani mambo mbalimbali zinavyoyafanya katika kutokutenda haki kwa wananchi wao. Pia hata kwa wale viongozi wanaopendwa na wananchi kunyimwa mamlaka. Hali hii imejidhihirisha kupitia Sufian katika himaya ya Budha kwani pamoja na kupendwa na wananchi wa Budha lakini utawala uliokuwepo madarakani haukutaka apewe nafasi hiyo bali ulimchagua yule mtu atakayeweza kuficha uovu uliokuwa unafanywa na serikali iliyokuwapo madarakani. Mwingizi ametumia lugha ya picha na ishara kupitia serikali ya Budha kwa kutaka kutuonyesha jinsi serikali mbalimbali katika mataifa ya ulimwengu wa tatu zinavyoendesha siasa zao.

### 2.1.1 Kanuni Kuu za Uchimuzi

Ushirikishwaji wa uchimuzi kiutekelezaji katika utunzi wa kazi za kibunilizi unaegemezwa katika kanuni bainifu zinazosaidia kuweka kipaumbele katika mambo, matukio, hali au mitazamo inayokusudiwa kuangaziwa kwa uwazi na kwa njia hiyo kudhihirisha upekee, upya au unyemi wa makusudi. Kanuni hizo zote ni muhimu ingawaje ni vigumu kuziwekea mipaka kanuni fulani zinazoitawala zaidi katika dhana

hii ya uchimuzi. Baadhi ya mambo ya kimsingi yanayoitawala dhana hii ni pamoja na haya yafuatayo:-

#### 2.1.1.1 Taharuki

Kwa mujibu wa Miall na Kuiken (1994), Van Peer na Hakemuilder (2006) na Van Peer (2007) wanasema kwamba uchimuzi huibua *ustaajabisho*, yaani hali inayowafanya wasomaji kuuliza au kushangaa kulikoni! Ustajaabisho huo huwafanya wasomaji au wasikilizaji kutaharuki kwa vile wanakutana na miundo iliyokengeuka. Miundo iliyokengeuka huvuta hisia za wasomaji au wasikilizaji kwa njia ya kuwaduwaza. Taharuki hii ipo kwa kiasi kikubwa sana katika riwaya za Mwingizi kwani katika sehemu nyingi za riwaya hizi kuna masimulizi ya kutisha, yasiyo ya kawaida na wakati mwingine ya kiajabu yenye taharuki na masimulizi ya mtindo wa ukengeushi. Taharuki, kwa kadri inavyojibainisha katika riwaya za Mwingizi ni dhana inayowezesha ujitokezaji wa utohakika wa matokeo ya tukio, kisa au hadithi nzima katika riwaya. Katika misingi hii taharuki inatumika katika riwaya hizi kuibua shauku, tamaa, kiu na hamu ya msomaji wa riwaya hizi ya kutaka kujua hatima ya tukio, kisa, hadithi au masimulizi fulani. Taharuki inaweza kugawika katika matapo mawili; ya kwanza ni ile inayohusiana na utohakika wa hadhira kujua matokeo ya tukio fulani linalopatikana katika kazi fulani, ya pili inahusiana na kutojua ni lini au ni vipi matokeo fulani yatakavyokuwa. Kwa kiasi kikubwa hivi ndivyo zilivyojengeka riwaya teule za Mwingizi.

#### 2.1.1.2 Uchimuzi Huvuta Hisia

Mbali na ukengeushi wa miundo kuibua mastaajabisho, kikubwa zaidi kinachojitokeza ni kule kuvutwa kwa hisia za wasomaji au wasikilizaji. Miall na Kuiken (1994: 393) wanaelezea kuwa kuna mahusiano baina ya mbinu ya mastaajabisho na uibushaji wa hisia. Kwa hivyo, mastaajabisho si kwa ajili ya mastaajabisho tu bali ni muundo wa kiutekelezi. Mara tu msomaji anapokutana na matini yenye miundo kengeushi, sehemu maalum katika ubongo inayohusika na uibuaji hisia hushughulishwa pia. Kwa mfano, mtunzi ametumia mastaajabisho kama mbinu ya kiutekelezi katika riwaya ya *Mzimu wa Waufi* pale tunapomwona Masumbuko anabadilishwa jinsia yake ya kiume na kuwa ya kike mpaka na sauti kubadilika kuwa ya kike na jini Hunudu.

#### 2.1.1.3 Uchimuzi na Muda wa Tafakuri

Kwa vile uchimuzi katika matini hugusa mioyo ya wasomaji au wasikilizaji mara baada ya kutafakuri kile kilichokengeushwa, kitendo cha kutafakuri huchukua muda na si jambo la papo kwa papo kwa vile kunakuwa na muda wa mchakato wa kuchanganua na weeledi. Mathalani inapotokea msomaji (au msikilizaji) kukutana na ufupishaji, au ukiukwaji wa kanuni au wa miundo ya kisarufi, anahitaji muda wa kuchanganua ni nini kimekiukwa. Au inapotokea msomaji au msikilizaji kukutana na tamathali za usemi kama vile sitiari, tashibiha au istiara n.k., ambapo maana ya neno au sentensi hutegemea uchanganuzi wa kile kilichoashiriwa, muda hupita ili kumuwezesha msomaji au msikilizaji kubaini maana iliyokusudiwa. Hupita kipindi fulani ambapo msomaji huzama katika lindi la fikra na hisia nzito. Katika kipindi hicho msomaji huzama katika fikra na kuushughulisha ubongo wake katika kulinganisha kumbukumbu ya kile akisomacho na maisha yake kwa ujumla na hivyo, kutumia muda kuchekecha ubongoni. Hali kama hizi zimedhihirika katika riwaya teule za Mwingizi. Kwa mfano, kumekuwa na matumizi makubwa ishara, taswira, vitu ambavyo humfanya msomji atafakari na kuchukua muda kidogo katika kung'amua maana aliyoikusudia mtunzi kwa jamii yake.

#### 2.1.1.4 Sifa za Uchimuzi ni za Ki-bia

Je, matumizi ya sifa za uchimuzi huathiri kikundi fulani tu cha wasomaji au wasikilizaji? Tafiti zinathibitisha kuwa wanajamii huguswa sawia na ukengeushi wa miundo na ukiukishaji wa kanuni zilizozoeleka za uandishi au usemaji. Mwanaelimumitindo Van Peer (1986), alifanya utafiti ulioonyesha kuwa athari za uchimuzi kuwagusa watu wa aina zote wakiwemo wasomi na wasio wasomi. Wasomaji au wasikilizaji huathiriwa na ukiushi, na ukiushi huwafanya wasomaji kuvuta fikra kwa muda na hivyo, kuwapa fursa ya kuguswa na matini hizo na kupima thamani ya ujumi uliotumika.

Kwa hivyo, sifa za utaharuki, uibuaji hisia na uchukuaji muda wa kiutafakuri miundo kiukwa huwapata watu wote. Hata hivyo, wasomaji waliopitia vipengele vya kiisimu na uchanganuzi wao watavutiwa zaidi na mbinu ya uchimuzi kuliko wale ambao hawavifahamu vipengele au miundo ya kisarufi. Tunahitimisha kwa kusema kuwa

uchimuzi huibua taharuki, hisia nzito na huchukua muda na una sifa ya kibia. Uchimuzi humstaajibisha msomaji kwa kukiuka miundo iliyozoeleka, ukiukwaji wa miundo hiyo huibua hisia zinazochukua muda kueleweka ipasavyo na pia kumlazimisha msomaji ajifikirishe namna matini ilivyosukwa.

Ndivyo riwaya teule hizi za Mwingizi zilivyobeba taharuki ya hali ya juu kwani kuna wakati msomaji anapatwa na taharuki kubwa. Kwa mfano, pale ambapo katika riwaya ya *Mzimu wa Waufi* tunamwona Masumbuko amebadilishwa jinsia na kuwa mtoto wa kike wakati yeye ni mwanamume kwa sababu ya kupingana na utawala kandamizi wa Hunudu wa kumtaka amtoe kafara mtoto wake wa kiume. Pia tunapata taharuki nyingine katika riwaya ya *Vita vya Mapenzi* pale ambapo Suhail analala ghafla akiwa ndotoni Mzee Sufian anamtokea na kumtaka atii masharti waliyokubaliana lakini Suhail anakataa ndipo anapigwa kibao na Mzee huyu na kumwagia juisi usoni. Suhail anashtuka usingizini na kujikuta amelowa juisi na anahisi maumivu makali usoni ya kupigwa ilihali alikuwa ndotoni.

**2.2 Uchimuzi Katika Kazi za Fasihi**

Dhana ya uchimuzi kwa kadri ilivyotumiwa, inavyotumiwa na inavyofasiriwa katika fasihi, inaibua uelewa changamano. Kwa mfano, Leech (1969:57), akimnukuu mtaalamu wa Czech, Jan Mukarovsky anasema kwamba, fasihi inatambuliwa kwa misingi ya sifa bainifu mbili; uthabiti na utaratibu wa uchimuzi. Uchimuzi katika matumizi ya lugha ya kawaida kama ya mazungumzo ama ya uandishi wa habari hutokea bila mpangilio au utaratibu fulani, ambapo uchimuzi katika matini za kifasihi ni muundo mahususi: ni muundo unaofuata utaratibu na mfumo fulani, ni sifa kama sitiari na hujitokeza na seti moja ya sifa ambazo hutawala na kuwa na kipaumbele juu ya sifa nyinginezo.

Sifa hii inarejelewa na Jakobson (1987) kama "**the dominant**" (sifa tawala). Kauli hii inapotathminiwa kwa makini, inaashiria uwepo wa sifa tawala za kiutunzi katika riwaya teule za Mwingizi. Kwa mfano, sadfa ya ujitokezaji wa matukio ya kiajabu na matukio ya jiniuchawi yametanda na kuzagaa kote katika riwaya hizi. Kuna pia sadfa ya

kukutana kwa watu (wahusika) katika nyakati na hali wasizotarajiwa kukutana. Sadfa imetumika kushtukiza, kusogeza mbele hadithi, kusadikisha mantiki ya makutano na kwa njia hii basi, sadfa inakuwa mbinu/sifa tawala. Leech (khj) anaendelea kusema kuwa, uchimuzi ni wa kaida za kiisimu au kijamii na zinazokubalika. Kwa maoni yake anahoji kwamba, ukiushi wa kisanaa hujitokeza wazi ikilinganishwa na mazingira ya kazi za kinathari, ukiushi wa kiisimu hurejelea umbo lililokiushwa, nayo mazingira yanayozaa umbo hilo huwa ni lugha. Kwa mfano, kama ambavyo jicho hunasa umbo kama elementi muhimu na ya maana katika eneo au uwanja fulani wenye mwanga, hivyo hivyo msomaji wa kazi ya kifasihi hunasa ukiushi wa kiisimu katika kirai kama sehemu muhimu ya ujumbe na baadaye kuifasili kwa kuhihusisha na mazingira ya ruwaza tarajiwa kama tulivyofanya katika kuhakiki riwaya teule za Mwingizi.

Ingawa ufafanuzi huu wa Leech na Mukarovsky unasawazisha dhana ya uchimuzi na ukiushi, tunakubaliana na Kazungu (1982) anapotoa kauli kwamba uchimuzi sio lazima uhusishwe na ukiushi kwa sababu kuzihusisha dhana hizi mbili kama moja na zilizo sawa kumaanisha kuwa mhakiki anafaa achukulie sifa za ukiushi kama sifa pekee ambazo zinastahili kuchimuzwa. Kwa mtazamo wa utafiti huu, uchimuzi ni matumizi ya mbinu mbalimbali za lugha katika matini za kifasihi zenye kuibua athari fulani kwa msomaji na ambazo hujitokeza kwa uwazi zikilinganishwa na matumizi ya mbinu sawia katika lugha ya kawaida. Uchimuzi katika matini za kifasihi, hutumiwa kwa makusudi na huwa na maana. Wakati ambapo msomaji anakumbana na miundo ya uchimuzi katika matini anayoisoma, na kutambua miundo hii, humfanya atafakari motisha kuu ya matumizi ya mbinu hizo za mwandishi katika matini husika. Katika kujaribu kupata motisha, msomaji huweza kupata maana halisi ya ujumbe ambao umewasilishwa na mwandishi katika kazi ya kinathari au ushairi (Mugwika 2012). Katika kuihakiki nafasi ya uchimuzi katika riwaya za Mwingizi tumebainisha motisha kuu ya mbinu husika ili kubainisha dhamira kuu ya mwandishi.

Kwa mintarafu hii, uchimuzi katika kazi za kifasihi na hasa katika riwaya mpya au riwaya ya kihalisiajabu , kama zilivyo riwaya za Mwingizi, huweza kutokea katika

viwango tofauti, tena vingi. Mathalan, kiwango cha kifonetiki, kiwango cha kimaana au kisemantiki ambapo maneno au vifungu tofauti hupewa maana kadhaa na pia kutumiwa kwa njia isiyozoeleka. Kiwango cha kisintaksia ambapo kuna ukiukaji wa miundo ya virai na vishazi na mwisho urudiaji unaochimuza na kufanya mofu, sauti, neno, sentensi au kishazi kujitokeza wazi. Hata hivyo, uchimuzi katika matini za kifasihi hutokana na nia ya mwandishi kutaka kuwasilisha ujumbe fulani kwa uzito, kwa msisitizo au kwa kuupa kipaumbele. Kwa hivyo, mwandishi mwenyewe hubainisha miundo mbalimbali ambayo atatumia ili kuchimuza sifa maalum katika kazi yake. Kwa njia hii, maana ya sifa za miundo ya uchimuzi hutegemea ufasili wa msomaji kupitia jitihada na taswira za usawiri wa sifa na matini anayosoma. Kwa mujibu wa Halliday kama alivyonukuliwa na Chatman (1971), sifa inayojitokeza huchimuzwa tu kwa misingi kuwa, inahusiana na maana ya matini kwa ujumla, uhusiano ambao hufanya kazi maalum au huwakilisha maana fulani.

Kudhihirika kwa uchimuzi katika kazi ya kifasihi kwa mujibu wa Kazungu (1982:33) hutegemea mapenzi ya mwandishi ya kuutumia. Kwa mantiki hii, sio sifa zote hujitokeza kama kiwakilishi cha matini bali sifa ambazo zinaonekana kutoa ujumbe ndizo huchimuzwa. Swala linalobainishwa ni umuhimu wa sifa inayochimuzwa ni juhudi za msomaji zinazomwezesha kutafakari na kutafsiri uhusiano kati ya sifa husika na matini na kwa njia hii, kumpa usawiri mpya wa kazi hiyo. Hii inaelekea kuelezwa ni kwa nini Jakobson (1987) kashikilia kwamba fasihi kamwe haipaswi kuhusishwa na hisia. Kwake sifa bainifu za kihisia katika fasihi ni duni na zinafungamana na uhakika wa maneno ya kiisimu. Anasisitiza ‘ufasihi’, yaani matumizi ya kipekee ya lugha kama msingi wa lugha ya fasihi badala ya kutazama fasihi kwa ujumla au kwa kuzingatia kazi za watu binafsi. Kwa njia hii, Jan Mukarovsky anafafanua dhana ya uchimuzi kuwa ni ukiukaji wa kaida za lugha ya kawaida kwa makusudi na uwezo wa kukiuka kaida ambazo hudhihirisha ufasihi (Freeman, 1970:42).

Uchimuzi huibua athari ya *ostranenia*, istilahi hii kulingana na Wamitila (2003:237) inarejelea hali ya kukifanya kipengele fulani cha lugha ya fasihi kijitokeze wazi

kikilinganishwa na ujitokezaji wake katika lugha ya kawaida. Dhana hii huhusishwa na uchimuzi na humfanya msomaji wa kazi za kifasihi kutambua sifa za kipekee zinazohusishwa na mitindo ya uandishi. Pia dhana hii hutumika kufanya kitu cha ajabu ili kuondoa uzoefu katika kazi za fasihi. Hivyo, sababu mojawapo inayotufanya tusichoshwe na kazi za kinathari ni matumizi ya miundo tofauti tofauti ya lugha isiyo ya kawaida inayotuwezesha kutambua ukweli unaowasilishwa kwa njia ya ajabu inayochimuza mambo kadhaa kama ilivyo katika riwaya za kimajaribio za Mwingizi.Usanii ni njia ya kupata tajriba ya kisanaa ya jambo; jambo husika haliwi muhimu bali njia ambayo inawasilishwa kwayo (Selden, 1988:274). Mukarovsky alionelea na kuufasiri uchimuzi kama njia moja ya kuwasilisha kazi ya kifasihi kwa njia mpya. Mukarovsky anahoji kwamba, uchimuzi ni ukiukaji wa kaida za matumizi ya lugha ya kawaida kwa makusudi na uwezo wa kukiuka kaida ambazo hudhihirisha ufasihi au lugha ya kisanaa (Freeman, 1970:42). Kwa misingi hiyo, Mukarovsky anasisitiza kwamba, uwezo huu wa kukiuka kaida ndio hujenga ufasihi ama usanii katika lugha. Kwake, utaratibu unaoandamana na ukiukaji wa kaida za matumizi ya lugha ndiko hujenga kazi ya kifasihi.

Shklovsky kama alivyonukuliwa na Fokkema na Ibsch (1979:15) anaona fasihi kama iliyokuwa na uwezo wa kuifanya hadhira kutazama ulimwengu inamoishi kwa njia tofauti na vile imezoeleka. Ili lugha iwe na maana ya kifasihi, lazima iajinabishwe na kufanywa kuwa ngeni na vilevile kwa kuitumia katika miktadha isiyo ya kawaida. Upekee wa fasihi hutokana na jinsi inavyobadilisha kategoria za lugha ya kawaida na kuwafanya wasomaji kuliona swala fulani tofauti na walivyozoea kuliona kila siku. Mbinu hii ilitumika kuelezea kuwa sanaa au fasihi kwa hutuchangamsha na kutukumbusha maisha na uzoevu wetu kwa njia ngeni. Hii ni sifa inayodhihirika katika riwaya za Mwingizi ambapo mwandishi anatudokezea mambo ambayo yalitokea na yanaendelea kutokea katika jamii zetu. Kwa namna hii hutukumbusha na kutuasa juu ya sifa hasi za viongozi wetu, hali kadhalika kwa njia hii mtunzi hupambanua na kuangazia macho ya umma kwa mambo halisi, mienendo, tabia, shida na tajriba zinazoifanya jamii kwenda mbele au kudumaa, kwa kutumia mbinu kadhaa za lugha ya ishara.

Kulingana na Shklovsky (khj) kunazo njia kadha za kuonyesha mambo kuwa mageni, ya ajabu ama kuyaondolea uzoefu. Athari ya mbinu kama usambamba, tashbihi, urudiaji, na balagha ni kukibadilisha kitu kutoka hali yake ya kawaida na kukifanya kipya yaani, maana mpya na ambayo ilikuwepo inajitokeza. Athari za kuona mambo upya, mambo katika upeo usio wa mazoea, mambo katika uhalisi na ulimwengu mbadala zinajitokeza kutokana na matumizi ya mbinu kadhaa zilizochimuzwa. Kwa njia hiyo maudhui, mandhari, wahusika, lugha na usimulizi katika riwaya za Mwingizi zimefanywa kujitokeza kwa njia mpya katika kuieleza hali halisi ya mambo yaliyokumba na yanayoendelea kukumba jamii zetu kama inavyodokezwa kiajabu na kijiniuchawi katika *Vita vya Mapenzi*, riwaya *Mzimu wa Waufi* na katika riwaya ya *Tanzia*.

Dhana ya uajinabishaji ilipanuliwa na Mukarovsky, mwanachama wa kikundi cha 'Prague Linguistic Circle' (Kikundi cha Kiisimu cha Prague) kuwa uchimuzi. Kwa mujibu wa Leech na Short (2007:23), Wana-Prague wanabainisha jukumu la lugha ya kishairi au kifasihi kutokana na uchimuzi wa ishara za kiisimu. Hivi kwamba, matumizi ya kiujumi ya lugha huvutia wasomaji kwa njia mpya na yenye kuibua hisia katika lugha, swala linalochukuliwa kutokea Bila mpangilio. Kwa hivyo, tunaona maneno haya ya Leech na Short ni kwa jinsi gani yanaonyesha uchimuzi katika fasihi unaweza kujitokeza kwa kiasi kikubwa hata katika lugha tena katika kipengele cha kiisimu. Swala hili limedhihirika katika sura ya tano katika utafiti huu katika kipengele cha ishara na uashiriaji kama mikakati ya uchimuzi kwani ishara ni miongoni mwa mitindo ya lugha mabayo watunzi wengi wa kimajaribio huitumia.

Tomashevsky (1925), mshirika mmoja wa Shklovsky anatoa mfano wa uajinabishaji kwa kutumia mbinu ya Jonathan Swift ya kuelezea njia za ki binadamu kupitia kwa hadithi yake ya *Gulliver's Travels* (*Safari za Gulliver*). Tomashevsky anasema msimulizi hutumia tasfida katika kuelezea uozo na upumbavu wa mwanadamu kwa njia hii udhalimu wa kitabaka unadhihirishwa. Tunamwoma Gulliver kama mwana baharia anayepotelea baharini baada ya chombo chake kuharibika. Baadaye, anajikuta katika nchi ya majitu ambapo yeye anakuwa mtu wa kimo kidogo sana. Hata hivyo, anapata

uwezo wa kimaajabu wa kuviona vitu ambavyo majitu hayangeweza kuviona. Kwa namna hii, tunapata kuuona ulimwengu mpya. Mwandishi anafanikiwa kuonyesha uozo katika jamii ambao haungetambulika kwa mtazamo wa kawaida. Ndivyo Mwingizi alivyosimulia visa na matukio katika riwaya zake teule kwa kutumia mtindo wa kiajabu lakini kwa kutuonyesha uozo uliopo katika jamii ambao haungetambulika kwa mtazamo wa kawaida.

Pia katika *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (2008), tunamwona mwandishi anatumia vizuu katika kuchimuza uozo uliopo katika jamii kwa kuonyesha jinsi viongozi wanavyowapumbaza wananchi kwa kuwafanya vizuu. Vilevile katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* (2001) mwandishi anatumia Mzuka wa Babu yake K, ili kuchimuza uozo wa kimaadili wa viongozi na kutowajibika kwao kunakojitokeza kupitia kwa K. Hivi ndivyo ilivyo katika mataifa ya Kiafrika. Katika riwaya hizi za Mwingizi, mtunzi anabadilisha majina halisi ya wahusika na mahali ili kudhihirisha uozo wa kimaadili na kutowajibika kwa njia inayochimuza tabia zao na hali kadhalika kuifanya hadithi ya kuvutia kwa kubadilisha usawiri wa jamii zetu kwa njia mpya. Anatumia matukio ya kiajabu kuonyesha fursa za kujiendeleza zilizoko au fursa zilizopotea, anaonyesha adabu na nuksi, uaminifu na usaliti, ustaarabu na utovu wa nidhamu, n.k.

Kwa hivyo, kwa kujikita katika uhalisi wa kifasihi, inahalisi kuhoji kwamba dhana ya uchimuzi ni dhana ambayo imeibuka kuwa moja ya sifa bainishi za riwaya ya kimajaribio katika fasihi ya Kiswahili. Hii inatokana na ukweli kwamba katika riwaya zilizojitokeza tangu miaka ya 1990 ambazo zinahesabiwa kama za kimajaribio, uchimuzi unajitokeza kwa uwazi na vilevile unajitokeza kama kipengele kinachoifasiri riwaya ya kimajaribio. Uchimuzi kwa njia hii unaweza kuangaliwa kama ufundi wa kiutunzi, ufundi ulio na uamili mkubwa katika utunzi wa fasihi. Lakini, hata kama huo ndio ukweli wa kiutunzi kuhusiana na riwaya ya kimajaribio, usomi na utafiti unaohusiana na matumizi ya mbinu hii haujajitokeza kwa kiasi sawia cha utunzi.

## 2.3 Uhalisiajabu kama Dhana Iliyobeba Kipengele cha Jiniuchawi na Ushirikina

Uhalisiajabu ni uhalisi wa kiuandishi, kiutunzi na kiuchanganuzi ambao umepitia katika vipindi na awamu mbalimbali za historia. Uhalisiajabu umepitia vipindi kama vile kipindi cha uhalisia hakiki, kipindi cha uhalisia wa kijamaa na pia kipindi cha uhalisiajabu ambapo katika kipindi hiki tunaona kipengele cha jiniuchawi na ushirikina kikijitokeza kwa uwazi zaidi. Sababu ya kujadili na kuangalia uhalisiajabu kwa mkabala wa mpito wa kihistoria, ni kule kutaka kuwa na uelewa mpana wa dhana hii, kudhibiti sifa zake za kimsingi, kuielewa mijadala iliyoibuliwa na uhalisiajabu kama vuguvugu la kiutunzi, na zaidi ya hayo kutaka kuelewa kama mtunzi Mwingizi yumo katika mkururo ule ule au kama ameukweza uhalisiajabu kwa kuushirikisha na kuhusisha na jiniuchawi na ushirikiana. Vilevile, kuna haja kujiuliza ni kwa nini Mwingizi ameamaua kutumia mtindo huu wa kijiniuchawi na ushirikina kama mbinu ya uhalisiajabu na kuasi mitindo iliyozoeleka.

### 2.3.1 Kipindi cha Uhalisia Hakiki

Wanauhalisia husisitiza uwasilishaji wa maisha ya jamii kwa uaminifu na usahihi mkubwa, kusawiri maisha na michakato ya maisha kama maisha yalivyo. Waandishi wanaotumia uhalisia kama mkabala wa kiutunzi au kiuchanganuzi, wanapendelea kujishughulisha kuwaangalia wahusika, mandhari na matukio ya kawaida au yanayoweza kuonekana katika jamii kama yalivyo. Kwa kujikita katika uelewa huu, Njogu na Wafula (2007) wanahoji kuwa uhalisia wa kifasihi unaashiria uwezo wa kusawiri au kuelezea hali kwa kuzingatia uyakinifu au uhakika wa maisha. Waandishi hawa wanaelezea kuwa, huko Ufaransa kuna waandishi kama vile Flaubert 1850, waliotumia dhana ya uhalisia kuelezea kazi ya sanaa inayoonyesha maisha ya binadamu jinsi yalivyo na uigaji wa mazingira wanapopatikana wanadamu. Wanafafanua kuwa mwanafalsafa Hegel katika kitabu chake kinachoitwa *Aesthetic* (ujumi) alitumia neno ‘uhalisia’ kumaanisha kazi ya sanaa iliyo na wahusika ambao matendo yao yanachochewa na hali ya kisaikolojia iliyowazunguka.

Kwa upande wake, Wamitila (2002) anasema kuwa kazi ambazo zinaangaliwa kama za kihalisia, zinatarajiwa kuwa kama akisiko la hali halisi ya maisha katika jamii inayohusika kwa kiasi kikubwa. Wanauhalisia hujifunga kwenye wahusika wa kawaida au wanaoweza kupatikana katika jamii halisi kuyachunguza na kuyasimulia maisha yao na tajriba zao kwa kusawiri na kuonyesha mandhari na mazingira ya kawaida. Anasisitiza kuwa, uhalisia unapinga au kukataa aina yoyote ya majaribio. Wamitila anaonelea kuwa, waandishi wa kihalisia huchukulia kuwa picha zinazopatikana kwenye kazi zao pamoja na yaliyomo huwiana na ukweli wa jamii zinazohusika. Msimamo huu unaelekea kuamini kuwa ‘ukweli’ na ‘uhalisi’ ni vitu vinavyoweza kuelezeka kwa urahisi jambo ambalo si kweli. Akitoa mfano kutoka katika riwaya ya Kezilahabi ya *Rosa Mistika*, Wamitila (2002:117) anaeleza kuwa riwaya hii imeandikwa kwa kiasi kikubwa kwenye misingi ya uhalisia na ndio riwaya pekee kwa kiasi kikubwa ya Kezilahabi kuandika kiuhalisia lakini kuna tukio ambalo linazua maswali. Rosa anapoletewa maji ya sumu, anayamwaga nje ya nyumba na asubuhi anakuta kichuguu kikubwa kimeota hapo nje. Jambo hili kwa msomaji mmoja laweza kuwa la kihalisia lakini kwa mwingine liwe la kiajabu. Kinachodhihirika katika kipindi hiki ni uwepo wa msisitizo wa uhalisi katika utunzi na uchanganuzi wa fasihi. Lakini hata hivyo, pamoja na kuwepo kwa msisitizo huu, chembechembe za uhalisiajabu zinaanza kujitokeza.

Khaemba (1999:14) anaonelea kuwa, uhalisia hakiki ni muhimu tu kwa kadri unavyoangazia kujimudu katika harakati za mwanajamii kupambana dhidi ya hali dhahiri. Ni wazi kuwa nadharia ya uhalisia hakiki ina upungufu kwani haielezi jinsi binadamu anavyopambana na nguvu za ajabu dhidi ya uwezo wake. Pengine ndipo waandishi wengine wa riwaya kama vile Kezilahabi, Mkangi, Wamitila, Mohamed, Mwingizi na Tom Olali waliamua kuandika kazi za mtazamo wa kiuhalisiajabu, ili waweze kueleza mambo ambayo hayangeweza kuelezeka kwa kutumia uhalisia, au yaliyoweza kuelezeka bayana zaidi kwa matumizi ya uhalisiajabu. Katika kipindi cha uhalisia hakiki waandishi wa uhalisia hakiki hawakuweza kuandika yale mambo ambayo yaliyogusa jamii kwa undani, kwani hata wale walioweza kuandika kazi za kiuhalisia kwa uwazi, kazi zao ziliweza kufungiwa na vyombo vya dola. Kwa

kuonekana kueleza mambo kwa uwazi ndipo tunaona waandishi wengi kama vile Kezilahabi, Wamitila, Said A. Mohamed, Tom Olali, Emmanuel Mbogo na Ibrahim Hussein wakaamua kuasi uandishi wa kiuhalisia wakageukia katika mkondo wa kiuhalisiajabu ili waweze kuelezea mambo ambayo hayangeweza kuelezewa katika hali ya kiuhalisia.

Vilevile, Msokile (1993) anasema uhalisia ulipata upinzani mkubwa sana kwani, watu kama vile Flaubert walijaribu kuonyesha maisha ya *Madame Bovary*, mwandishi mwingine ni Emile Zola aliyeandika riwaya ya *Nana*, riwaya inayoeleza na kuwasilisha mambo na hali za maisha kwa ubayana wa kukereketa. Watunzi hawa wote walipigwa vita kwa kutunga hadithi na kuwasilisha vitabu vilivyoandikwa kwa kuzingatia uhalisia kwa ubayana sana. Inaelekea kwamba wale walioasi matakwa, kaida na madai ya utunzi wa kiuhalisia, waliuona uhalisia kuwa na ubanifu mkubwa, kuwepo na upeo mdogo wa ulimwengu mbadala kuwasilishwa, kubanwa kwa fikira katika ulimwengu wa kufikirika. Hii pengine, ndio maana tunaona hata Mwingizi kuhiari kutumia uhalisiajabu katika kuelezea mambo mbalimbali ambayo yamo katika jamii na ambayo hayangeweza kuzungumziwa katika hali ya uhalisia. Lakini zaidi ni kwamba, kwa kuhiari kutumia mfumo huu wa kiutunzi wa kiuhalisiajabu, Mwingizi anatuwasilia mambo mengi ukiwemo ufasiri mbadala, mitazamo mbadala, ulimwengu mbadala na hata ulimwengu unaowezekana tu kuwepo.

### 2.3.2 Kipindi cha Uhalisia wa Kijamaa

Uhalisia wa kijamaa unahusishwa na mwamko wa siasa na sera za kiuchumi za kijamaa. Kwa misingi hiyo, uhalisia wa kijamaa hukazania kusawiri na kuonyesha maisha kwa kuzingatia mtazamo wa kijamaa ambapo majaliwa ya pamoja na neema ya pamoja inasisitizwa. Uhalisia wa kijamaa ulianza rasmi wakati wa kipindi maalum cha historia na hasa baada ya mapinduzi ya kijamaa ya Urusi ya mwaka 1917 (Msokile 1993). Uhalisia wa kijamaa ulizuka pale wanajamii walipong’amua kwamba mahitaji ya jamii yanatawaliwa na mahitaji ya kiuchumi na wala si fikra za watu au majaaliwa.Uhalisia wa kijamii kama itikadi na mtazamo wa kiutunzi na kihakiki ulikusudiwa kuonyesha

ubora wa ujamaa kama mfumo fanifu wa kiutawala na ki-uzalishaji. Uhalisia wa kijamii na mahusiko yake katika fasihi ni istilahi iliyoasisiwa katika Kongamano la Kwanza la Waandishi wa Kirusi (1934) kama utaratibu rasmi wa kuhakiki na kuchambua fasihi ya Kirusi kwa nia ya kuonyesha mwingiliano ulioko kati ya uchambuzi wa fasihi na ujenzi wa itikadi ya kijamii.Njogu na Wafula (2007:61) wakielezea nadharia ya uhalisia wa kijamaa wanasema:

> Ni mbinu ya utunzi na uhakiki inayomzingatia binadamu kama uti wa mgongo wa kuwepo kwa ulimwengu na maana ya ulimwengu ule. Waundaji wa nadharia hii wameathiriwa na mtazamo wa Kimarx kuhusu ulimwengu na historia. Maxim Gorky, mmojawapo wa waasisi wa uhakiki wa kijamaa, anasema kwamba mambo yote mazuri yanayotamanika ulimwenguni yameumbwa au kuelezwa na binadamu.

Njogu na Wafula (2007:68) wanaendelea kuhoji kwamba, mwandishi wa kiuhalisia huongozwa na mihimili kama wahusika wa kimaendeleo. Hawa ni wahusika wanaonuia kupindua na kuibadilisha hali yao ya maisha. Ni wahusika wenye nia ya kumiliki njia kuu za kuzalisha mali katika jamii yao. Pili, wahusika hawa pamoja na kusawiri matukio ya kihistoria, wanapaswa kutekeleza matendo ya kitabaka. Hufanya hivi kimakusudi au bila kufahamu. Tatu, uhalisia wa kijamaa huzingatia maslahi ya makabwela. Nne, binadamu huonyeshwa kiuyakinifu na wahusika ambao hutumiwa kama vipaza-sauti vya watunzi, hupuliziwa uhai mfano wa wanadamu wa kawaida wanaoishi katika ulimwengu tunaofahamikiwa nao.Tano, wahusika huonyesha matumaini juu ya kizazi cha binadamu. Hii inamaanisha kwamba mtu atakuwa mshindi au ni mshindi dhidi ya unyonyaji na unyanyasaji wa aina yoyote. Sita, lugha inayotumiwa katika uhalisia wa kijamaa inaendeleza malengo na mapendekezo ya walio wengi katika jamii.

Kutokana na maelezo haya, nadharia ya uhalisia wa kijamaa imedhihirishwa kuwa ina upungufu kwa kuwa imekolea itikadi sana hivi kwamba, maswala ya kisanaa yanaweza kupuuzwa. Lugha inayotumiwa inaweza kuwa kavu ikakosa matumizi ya kunga za kifasihi kama vile tamathali za usemi mbalimbali. Uhalisia uwe unaangaliwa kwa mkabala wa kiutunzi au kiuchanganuzi, unaweza kusemwa kuwa ni mkabala wa kifasihi ulio na ubanifu mkubwa wa kiubunifu na kimawazo. Kwa hiyo, bado tunaona kipindi

hiki kinaendelea kuminya uhuru, ukunjufu na uhiari mwandishi wa kazi za fasihi. Mtunzi anakuwa mfungwa katika mikatale ya kaida tasa na chakavu, kaida zisizo na uzalishaji. Pengine inaweza kukisiwa kuwa hii ndio maana Maundu Mwingizi aliamua na kuhiari kugeukia katika mkondo huu wa kiuhalisiajabu ili aweze kuyaeleza vizuri, kwa uhuru, ubunifu na uhiari mambo ambayo yapo katika jamii.

### 2.3.3 Kipindi cha Uhalisiajabu

Kwa kila hali, inaweza kudaiwa kwamba, mifumo na mikabala ya awali ya uhalisia ilihusika pakubwa kwa njia za moja kwa moja na pengine zisizo wazi katika kuzalisha uhalisiajabu. Watunzi waliokuwa wanahisi kubanwa na kufungwa, walihiari kutafuta njia mpya za kujaribisha utunzi wa kifasihi, walihitaji mawanda na upeo mpana wa kufikiri, kuota, kujitosa ndani na kujaribisha mbinu, taratibu na mikakati ya utunzi wa kibunilizi. Kwa hivyo, uhalisiajabu una mianzo yake katika ukiukaji, mgeuko, uasi na mapinduzi dhidi ya mazoea na mikatale yakaida. Pale ambapo haikufikirika kubebesha utunzi wa kihalisia mambo ya kimajaribio, uhalisiajabu ulikuwa tayari kubeba ndoto za kinjozi, ulimwengu wa kufikirika na kufikika kinjozi, ulimwengu wa nchi kavu na ulimwengu wa chini ya maji, uwezekano wa kuwa na pete za kusema na kusemezwa, mimba za kubebwa ubia, wafu wanaokataa maziko na hata kusawiriwa kwa jiniuchawi na ushirikina kama uhalisi wa maisha.

Kama tulivyokwisha kujadili katika sura ya kwanza kwamba uhalisiajabu ni ile hali ya kukiuka sifa za uhalisia kama zilivyozoelewa na waandishi wa karne ya kumi na tisa na ishirini. Uandishi huu wa kiuhalisiajabu ulipamba moto zaidi katika karne ya ishirini na moja kutokana na mtindo wa uandishi wa fasihi ya kimajaribio. Katika uhalisiajabu, matukio yasiyoaminika yaani ya kifantasia[3] husawiriwa kama mambo ya kawaida.

3 Fantasia ni hali ya kuwepo kwa mambo ya ajabuajabu katika kazi ya fasihi yasiyotarajiwa kutokea katika maisha ya kawaida. Ni dhana inayotumiwa kueleza kazi ya fasihi ambayo ina sifa ambazo zinakiuka uhalisia, Wamitila (2003). hivyo basi, fantasia ni hali ya kudhihika kwa matukio ya ajabuajabu yasiyokuwa na uhalisia wa moja kwa moja kwa jamii ndani ya kazi ya fasihi. Kawaida fantasia hupambwa na sifa mbalimbali ambazo ni :- matumizi ya taharuki, kuelezea mambo ya ajabuajabu, kutumia wahusika wa ajabuajabu, matumizi ya taswira kwa wingi na matumizi ya tashihisi.

Mambo ya kiajabu yanaelezwa kwa namna ya moja kwa moja na kuonekana kuwa ya kawaida. Wamitila (2003:274) kuhusu sifa za kiuhalisiajabu anasema:

> Sifa hizi ni za kuyaeleza matukio ya kifantasia au ya kiajabu au kichawi kwa namna ya moja kwa moja, kwa namna inayofanya yaonekane kama ya kawaida tu. Mpaka uliopo kati ya mambo yanayoweza kupatikana katika ulimwengu halisi na yasiyowezekana huwa mdogo mno.

Mwingizi ameamua kutumia mtindo huu wa kiuhalisiajabu kwa kutumia mambo ya jiniuchawi na ushirikina ili aweze kuzungumza mambo ambayo yapo katika jamii ambayo yasingeweza kuzungumzwa katika hali ya kawaida kama aseamavyo Zamora na Faris (1995:3), kuwa waandishi wanaotumia mtindo huu wa uhalisiajabu wanafanya hivi ili waweze kuzungumzia maswala ambayo hayangeweza kuzungumziwa kwa uwazi kwa njia ya kawaida au kwa mtindo wa kiuhalisia.

Mwingizi amezingatia mtindo wa kiuhalisiajabu kwani aliona kuwa mitindo ya uhalisia hakiki na uhalisia wa kijamaa haikuweza tena kuyaakisi maswala ya jamii. Kwa hivyo akataka kuziba pengo hiulo kwa kutumia mtazamo huu katika kuangazia maswala ibuka yanayokabili mataifa ya ulimwengu wa tatu. Maswala haya ni ya mikataba ya kimataifa, uibukaji wa mitandao ya jinai, maingiliano na mitagusano ya kijamii, kunaswa kwa binadamu katika mivutano ya kiutandawazi, na mengineyo sawia na hayo. Kwa kujikita katika mtindo huu wa kipekee unaosheheni ugothi, uhalisia wa kiajabu na nguvu za giza, Mwingizi amebuni kazi zinazomwezesha msomaji kuelewa kwa njia mbadala dunia anamoishi leo. Mashiko ya mtindo huu yanatokana na ukweli kwamba imani za jiniuchawi na ushirikina zipo na zinatawala mifumo ya kufikiri katika maeneo haya, wako manajimu na wasoma nyota na ndoto na ziko taratibu za matambiko na utoaji kafara. Kwa hivyo, kusimulia na kueleza mambo na matukio kwa misingi ya kijiniuchawi na ushirikina si uhalisi ulio nje ya upeo wa kuwazika.

**2.4 Hitimisho**

Sura hii imeeleza dhana ya uchimuzi kuwa ni matumizi ya kiubunifu, mapya na mbadala ya mbinu mbalimbali za lugha katika matini za kifasihi zenye kuibua athari

fulani mahususi kwa msomaji na ambazo hujitokeza kwa uwazi zikilinganishwa na lugha ya kawaida. Pia tumeona watunzi wa kazi za fasihi hutumia mbinu hii ya uchimuzi kwa makusudi kwa lengo la kutaka kutoa ujumbe ambao ni mzito ambao kwa njia ya kawaida ingekuwa ni vigumu kutoa ujumbe huo kama ilivyodhihirika katika riwaya za Mwingizi, kwani ametumia lugha ya picha na mafumbo katika kuonyesha hali halisi ya mambo yanayoendelea katika jamii zetu. Pia katika sura hii tumengalia vipindi mbalimbali vilivyopelekea kutokea kwa uhalisaajabu kama vile kipindi cha uhalisia hakiki ambapo watunzi hawakuweza kuzungumza mambo ambayo yana uzito katika jamii. Pili tumeona kipindi cha uhalisia wa kijamaa ambapo mtunzi wa kazi za fasihi alijikita zaidi katika kueneza itikadi ya ujamaa na kusahau ubunifu. Lakini kipindi hiki cha uhalisajabu mtunzi ameweza kuelezea mambo mazito sana katika jamii kwa kutumia mbinu ya uchimuzi ili kufikisha ujumbe wake kwa jamii jinsi alivyotaka.

## SURA YA TATU

## MANDHARI, MATUKIO YA KIJINIUCHAWI NA USHIRIKINA NA UCHIMUZI WA DHAMIRA NA MAUDHUI KATIKA RIWAYA TEULE ZA MWINGIZI

### 3.1 Utangulizi

Katika sura iliyotangulia, kumejadiliwa na kutolewa maelezo juu ya dhana za uchimuzi, jiniuchawi na ushirikina kama kipengele cha uhalisiajabu. Sura hii inaangalia na kujadili jinsi mandhari na matukio mbalimbali ya kijiniuchawi na ushirikina yalivyopelekea kuibua na kuendeleza maudhui mbalimbali katika riwaya teule za Maundu Mwingizi. Mandhari yanayoangaziwa na kujadiliwa hapa ni pamoja na mandhari ya chini ya bahari, mandhari ya makaburini, maporini, kwenye mapango, mandhari dhahania yaani zisizoonekana na mandhari za kawaida katika jamii, jinsi zilivyochimuzwa na kupelekea kuwepo kwa maudhui mbalimbali katika riwaya zilizochunguzwa katika utafiti huu. Na pia kumeangaziwa matukio mbalimbali yalivyochimuzwa na kuendeleza maudhui mbalimbali.

### 3.2 Ufasiri na Maana ya Mandhari

Mandhari ni sehemu muhimu sana katika kazi ya fasihi hususan katika kazi za kiutunzi zenye mtindo wa uhalisiajabu. Njogu na Chimerah (1999:46) wanabainisha uwanda wa mandhari kuwa ni mahali au makazi maalumu yaliyojengwa na mtunzi na mnamo tukia matukio mbalimbali ya kazi ya fasihi. Ni mazingira ya wahusika pamoja na matukio yanayohusu mahali wanamokaa wahusika hao; mazingira ya kijamii na kiuchumi ya wahusika hao; na nafasi zao za kitabaka. Dhana ya mandhari kwa mujibu wa Wamitila (2008:343) ni pale tunaporejelea wakati, mwanda na umahali katika kazi ya fasihi. Mazingira mbalimbali ya kijiografia hurejelewa ili kubainisha taswira za mandhari. Umuhimu wa kuchunguza umahali na umandhari ni kwa vile hakuna tukio lisilotokea bila ya kuhusisha mahali. Umahali unaohusisha mwanda, mazingira, na wakati wa kutendeka hauna budi pia kuzingatiwa katika uchambuzi. Kuna umahali wa kihalisia ambao wasomaji huutambua na upo bayana katika ramani za maeneo husika.

Mandhari ni kipengele cha fani katika kazi za fasihi. Matendo yoyote ambayo hutokea katika kazi za kifasihi hayana budi kufanyika mahali fulani au sehemu fulani na wakati maalum. Hiki ndicho kitu kinachozingatiwa katika mandhari. Kwa hivyo, mandhari ni dhana ambayo hufichua ni wapi na lini ambapo matukio fulani yanafanyika. Wamitila (2003:108) anashadidia kauli hii kwa kuhoji kuwa mandhari hutumiwa kurejelea wakati wa kihistoria na mahali pa hadithi, yaani mazingira ya kijamii au kijiografia wanamojikuta wahusika wa kifasihi. Kutokana na fasiri hizi, ni dhahiri kwamba mandhari ni nguzo muhimu sana katika uelewa na ufasiri wa kazi yoyote ya kifasihi kwani mandhari hufungamana kwa kiasi kikubwa sana na uibukaji wa matukio, umuktadhishaji wa matukio hayo na ubainikaji wa maudhui yanayobebwa na wahusika mbalimbali katika kazi ya fasihi. Pia mandhari huimarisha matendo ya wahusika kwa kuwa matendo yao yanafungamana na mazingira wanamojikuta. Mandhari huchangia katika kueleza mambo mengi kuhusu sifa na tabia za wahusika, hali zao kwa mapana na marefu na mandhari huweza kuwa mhimili mkuu wa kuyaendeleza maudhui ya kazi ya kifasihi.

Katika kazi za mielekeo ya uhalisia mazingaombwe, si ajabu kukutana na umahali dhahania, wa kimazingaombwe au unaojitokeza kindoto tu. Miji, vijiji, nchi na mitaa ya kweli kama vile Ubungo Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza, Uswahilini Tabora, Bagamoyo, vitongoji vya Mbezi, Banana, Gongo la Mboto, Ilala Boma, Breakpoint na Polisi Kijitonyama, na Buguruni katika riwaya teule za Mwingizi vinatujengea taswira ya nchi ya Tanzania Bara na Jiji lake mashuhuri la Dar es Salaam na nchi ya Yemen na mji wake. Sehemu hizo halisi zinakinzanishwa ingawa kwa uchache na miji ya *Budha* na Bagamoyo ya ujinini katika *Vita vya Mapenzi.* Umahali wa kihalisia pia unadhihirika kwa viashiria vya miji na vitongoji ndani ya *Mzimu wa Waufi* kama Dar es salaam, Buguruni chama, Amana Hospitali, Gongo la Mboto, Ubungo, Tabora, Hospitali ya Kitete, Arusha, Shinyanga, ikikinzanishwa na miji ya kimazingaombwe ya miji ya mizimu ya Waufi na miji ya Viluwa ya Kigoma na Kongo katika *Mzimu wa Waufi*. Taswira inayojijenga ni kuwa matukio yanayosimuliwa yapo ndani ya mipaka ya Tanzania Bara na hasa Jiji la Dar es Salaam.

Katika riwaya ya *Tanzia*, matukio yanatamalaki katika kitongoji cha Kibondo, Kigoma ambacho kinapewa sifa ya vitendo vya ushirikina na uchawi kama kilivyo kitongoji cha Mlingotini cha Bagamoyo katika visasili vya jamii hizo. Vitongoji hivyo vinaashiria imani za uchawi na ushirikina katika jamii ya wa Tanzania. Mwandishi anaeleza mazingira ya Jiji la Dar es salaam, Tabora na kitongoji cha Kibondo ambapo msomaji anayeyafahamu maeneo hayo anawaona wahusika na matukio kiuhalisia. Msomaji pia anashawishika kuwa miji ya kuzimu, miji ya baharini, chini ya ardhi na miji ya misukule ni miji halisi kwani inalandanishwa na mazingira halisia. Mipaka ya miji ya kimazingaombwe na miji halisia inavunjwa katika riwaya teule za Maundu Mwingizi na hivyo kumpa nafasi finyu msomaji kujishughulisha na uhalisia wake na kujishughulisha zaidi na dhamira zinazoibuka.

Mwingizi anautumia uzoefu wake wa maeneo anayoyataja katika riwaya teule ili kuzipa sura halisi kazi zake, ila kwa kutajwa kwa miji ya chini ya bahari na chini ya nyumba huko Bagamoyo- Mlingotini, mzimuni Kibondo, nchi ya Nigeria, na mzimu wa Waufi kunaichimuza mada ya uchawi na ushirikina ili kushadidia madhila ya jamii yake. Mandhari ya vificho ya miji na mashamba mbalimbali na ile ambayo hujitokeza katika majumba yanayotumika kwa uhalifu ni ishara ya mwandishi kuweka bayana madhila ya jamii yake yanayofanywa na baadhi ya wanajamii ambao wameaminishwa na kupewa dhamana na wanajamii walio wengi. Matendo ya wahusika kwa kiasi fulani, yanachochewa na mitagusano inayojibainisha katika mandhari na mazingira yao. Mazingira anamojikuta mhusika yanaathiri kwa kiasi kikubwa wasifu wake kama mhusika. Mara nyingi, wasomaji hupenda kuona mandhari yanayoweza kutambulika, lakini hili haliwezekani katika kazi ambazo haziandikwi katika misingi ya uhalisia. Mandhari huwa na elementi zinazojitambulisha. Elementi hizi ni kama vile eneo halisi la kijiografia kama nyumbani, gerezani, pangoni na msituni; au wakati ambapo tukio fulani linatendeka au kipindi maalumu cha kihistoria au kipindi cha mwaka (mfano msimu wa mvua au kiangazi) (Wamitila 2002: 29).

Kufahamu mandhari katika kazi yeyote ya fasihi kunatusaidia wasomaji kuelewa hisia, imani, tabia na maumbile ya wahusika. Pia mandhari inatupa mwelekeo kuhusu maudhui. Kuna aina nyingi za mandhari zinazopatikana katika kazi za kifasihi kama alivyozieleza (Wamitila 2008:351) kwamba, kuna mandhari ya kijiografia, mandhari ya kihistoria, mandhari ya kidhanifu au kinjozi, mandhari ya kiishara, mandhari ya kidokezi na mandhari ya kiajinabi. Pia Madumulla (2009) anasema kuna aina mbili kuu za mandhari, aina ya kwanza ni mandhari halisi na mandhari ya kidhahania. Hata hivyo, tumeshughulikia aina mbili tu za mandhari ambazo zimeonekana kwa kiasi kikubwa katika riwaya teule za Mwingizi. Mandhari hizo ni mandhari dhahania na mandhari halisi kwani uhalisiajabu unachanganya mambo haya mawili ili kumfanya msomaji aweze kuamini mambo yanayotendeka katika mandhari dhahania na kwamba, yapo katika ulimwengu halisi ila katika kutumia uficho.

### 3.2.1 Aina za Mandhari katika Riwaya Teule za Mwingizi

Katika riwaya teule za Maundu Mwingizi, mandhari zilizojitokeza zinaweza kugawanywa katika kategoria mbili; mandhari za kijiografia au kiuhalisia na mandhari za kidhahania au kinjozi. Kwa kiasi kikubwa mandhari zilizotawala katika riwaya hizi ni mandhari za kidhahania au kinjozi ambazo zimekitwa zaidi katika mambo ya kiuhaliasiamazingaombwe ambapo wakati mwingine inakuwa vigumu kutambua au kubainisha mipaka ya ulimwengu halisi na ulimwengu wa kinjozi au ndoto. Kwa njia hii, katika kubuni na kusawiri mandhari, Mwingizi ameakisi ukweli wa uhalisiajabu wa kuyumbisha na kuvunja mipaka kati ya ulimwengu wa mazoea na ulimwengu wa kufikirika. Mandhari ya uhalisiajabu hutokea ili kuwakilisha uhalisiajabu fulani katika ulimwengu wa kawaida.

Wamitila (2008:351) anadai kwamba mazingira ya kijeografia huwa katika mandhari ya kijiografia nguzo muhimu katika mandhari. Mandhari ya kijiografia ni msingi muhimu wa kanuni ya ushabihikweli[4] katika kazi ya fasihi hususan, kazi zilizoandikwa katika

[4] ushabihikweli: dhna hii hutumiwa kurejelea hali inayofikia katika fasihi amabapo mwandishi huteua na kuwasilisha malighafi yake kwa jinsi inayokaribiana na ukweli kama ulivyo katika maisha ya kawaida.

mkondo wa uhalisia. Anaendelea kusema kuwa kanuni ya ushabihiukweli inasisitiza uhusiano wa karibu kati ya ulimwengu wa kibunifu na ulimwengu halisi kwa kumfanya msomaji aweze kuamini kuwa matukio, mazingira na maingiliano ya wahusika yanayotokea katika ulimwengu huo wa kibunifu yanaweza kukubalika. Kwa mujibu wa Wamitila, mazingira ya uhalisia ndio yanayompelekea mwandishi wa kibunifu kubuni mazingira ya kiuhalisiamazingaombwe ili kuweza kushabihiana na mambo yanayotendeka katika ulimwengu halisi kwa kutumia mtindo wa kijiniuchawi au kimazingaobwe. Kwa upande wa mandhari ya kidhahania au ya kinjozi, Wamitila (2008:352) anasema kwamba hii ni mandhari ambayo haiwezi kuhusishwa na uhalisi.

Mandhari ya aina hii yanaweza kuwa sifa ya kitanzu hasa katika kazi ambazo zina misingi yake katika njozi fulani. Njozi hii inaweza kuwa imeundwa makusudi kama ulinganuzi wa uhalisia fulani. Aina hii ya mandhari ndio imeonekana kwa kiasi kikubwa katika riwaya za Mwingizi. Kumekuwa mandhari za kidhahania katika riwaya ya *Vita vya Mapenzi* ambapo tunakutana na mandhari ya chini baharini wanakoishi na kutamalaki wakuu wa serikali ya Bhudha, Mzee Sufian na watawala wenziwe wa kijini wanakofanya vikao na kuishi huko.

### 3.3 Mandhari na Matukio ya Kijiniuchawi na Ushirikina Yalivyochimuza Dhamira na Maudhui katika Riwaya ya *Vita vya Mapenzi*

Kabla ya kuchambua mandhari na matukio ya kijiniuchawi na ushirikina ambayo yamechimuza dhamira na maudhui mseto katika riwaya ya *Vita vya Mapenzi*, ni vyema tujadili kwa kifupi muhtasari wa riwaya hii. *Vita vya Mapenzi* ni riwaya ambayo inaanza kwa kusimulia safari na maisha ya kijana mmoja aitwaye Suhail aliyekuwa akisafiri kutoka Dar es Salaam kuelekea nyumbani kwao Tabora baada ya kumaliza masomo yake katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Akiwa ndani ya basi anaweka visikilizio masikioni na kusikiliza muziki na upande wake wa pili katika hilo basi alikuwa amekaa Mzee mmoja mwenye asili ya Kiasia aliyekuwa anamtazama mara kwa mara Suhail. Ndipo Suhail akaamua kuweka visikilizio masikioni na kusikiliza mziki.

Suhail akiwa ndani ya gari ghafla basi lao likagongana na lori uso kwa uso. Lori likalisukuma basi lao kwenye korongo na kuuwa watu wengi na wengine wanaumia. Suhail ghafla akajikuta ametapakaa damu lakini hakuumia, akamwangalia pembeni yule Mzee wa Kiasia aliyekuwa karibu naye akaona yuko hoi na taabani akamfuata ili amuokoe lakini yule Mzee akakataa asiokolewe. Mzee yule akasema yeye atakufa tu kwa hivyo akamwambia achukue begi lake jekundu halafu alifungue. Suhail akamsogezea Mzee yule begi akalifungua. Ndani ya lile begi kulikuwa na dola nyingi sana ambazo ni dola mia mia tu.

Baada ya Suhail kuziona zile noti za dola anashangaa sana lakini yule Mzee anamwambia kwamba asishangae kwani lile begi lenye dola atampa tunuku na anamwambia mali zingine atazijua muda ukifika. Kilikuwa ni kitu cha ajabu sana baada ya kumtunuku zile dola yule Mzee wa Kiasia akavua pete yake kubwa yenye kito cha rangi ya njano aliyokuwa ameivaa kwenye kidole chake cha kati na akamshika mkono Suhail na kumvalisha. Suhail akajihisi ameingiwa na ganzi mwili mzima. Suhail akamuuliza yule Mzee ile pete ni nini? Mzee akamwambia ile pete inaitwa "Khatam Budha". Pete hii itakulinda katika maisha yako na akamwambia pesa zote anazompa ni kwa sharti moja tu ambalo si gumu sana. Sharti hilo akamwambia ni ninaomba umuoe Binti yangu na uishi naye kwa wema, amani na upendo. Yule Mzee akajitambulisha kuwa yeye anaitwa Mzee Shemhurish. Pia akamwambia Suhail afanye hima kumtafuta Binti yake anayeishi Bagamoyo anaitwa Shekhia. Wakati hayo yote yakiwa yanaendelea abiria wote pamoja walioathirika na ajali walikuwa wametolewa nje cha kushangaza wao walikuwa bado wapo ndani ya gari lakini wenzao hawawaoni. Lakini Suhail aliposhuka ikaBidi abiria wenziwe wamshangae kwani hawakuona mtu wakati wanabeba majeruhi.

Ajabu Suhail aliposhuka akawaambia abiria wenziwe kwamba anawahi kazini Dodoma kwani hakuomba ruhusa. Ndipo abiria wenziwe wakasema wamkague begi akakubali huku akihofia begi lake lenye dola. Cha ajabu waliliona begi moja tu na lile lenye dola hawakuliona na wakamruhusu aondoke. Suhail aliondoka na kwenda Dodoma akalala

“gesti”, kesho yake akarudi Dar es Salaam hakuendelea tena na safari kutokana na zile pesa alizokuwa nazo akaona ni vema aende Dar es slaam akazitumie zile pesa na kuziweka zingine kwenye akaunti za benki zake. Suhail alipofika Dar es Salaam alifungua makampuni mbalimbali na kununua majumba ya kifahali. Suhail anafikiri amepata kumbe amepatikana kwani yule Mzee Sufian hakuwa ni Mzee wa kawaida. Lilikuwa ni jini ambalo lilikuwa kiongozi mkubwa sana katika utawala wa Budha kule baharini, Mzee huyu yeye alikuwa ni waziri wa fedha na ndiye aliyepewa kinga ya utawala wa Budha ambayo ndio hiyo pete.

Aidha, Mzee huyu alikuwa na ugomvi mkubwa na kiongozi ambaye alikuwa madarakani kutokana na wananchi wa Budha kumtaka Mzee Sufian kugombea nafasi ya jini kiongozi wao baada ya huyo aliyekuwepo madarakani kustaafu. Lakini, kwa kiongozi huyu aliyekuwepo madarakani ilikuwa ni tofauti. Kwani, kiongozi huyu alikwisha kumuandaa kiongozi mwingine wa kushika nafasi yake ili aweze kuficha maovu mbalimbali aliyokuwa anayafanya. Kwa hivyo, kukawa na ugomvi mkubwa baina ya pande mbili, kwa wale waliokuwa wanamtaka Mzee Sufian na wale waliokuwa wanamtaka aliyechaguliwa na kiongozi ambaye muda wake umekwisha.

Kutokana na ugomvi huo mkubwa ndipo Mzee Sufian akaamua kuja duniani na pesa karibu zote za Budha na pete ambayo ilikuwa ndio kinga yao. Ndipo akamtafuta mtu wa kumkabidhi hiyo pete na hizo pesa ili aweze kuziendeleza na kumtunzia siri kwani ilitakiwa binadamu wa kawaida ndio achukue hivyo vitu. Angechukua jini serikali ya Budha ingemuona. Kwa hiyo, Suhail akakubali hizo pesa pamoja na pete kwa ajili ya tamaa zake. Suhail alizitumia zile pesa kwa kufungua makampuni mbalimbali akawa anaendeleza makampuni yake Dar es salaam. Hakurudi tena kwa wazazi wake na kwa mchumba wake aliyekuwa naye kabla ya kwenda chuo kikuu aliyekuwa anaitwa Sharifa. Suhail alimpata Shekhia kwa ajili ya tamaa ya pesa ndiyo maana akaanzisha naye mahusiano kwa lengo la kwamba mahusiano yale yataishia shuleni. Baada ya hapo ataendelea na mchumba wake aliyemuacha kijijini aitwaye Sharifa.

Suhail alipopewa zile pesa zilimnogea akawasahau wazazi wake na hata mchumba wake kwani, walipokuwa wakimpigia simu alikuwa hapokei kabisa. Na akamuoa yule Binti Shekhia ambaye ni mtoto wa Mzee Sufian, wakaendelea kuishi na kuendeleza miradi yao. Wazazi wa Suhail walitaka mtoto wao arudi nyumbani kwa lengo la kuwasalimu na kumwoa mchumba wake Sharifa. Hapo ndipo ikaleta shida kwa Suhail, kwani alikwisha kuingia mkataba na Shekhia na hakutakiwa kuoa mwanamke mwingine. Ilimlazimu Suhail ambembeleze Shekhia ndipo akampa masharti ya kumuoa Sharifa kwamba asishiriki naye tendo la ndoa. Kweli Suhail alikwenda nyumbani kwao na akafanikiwa kumuoa Sharifa lakini alimdanganya kwamba hana nguvu za kiume, japo Sharifa alimng'anga'nia hivyo hivyo ndipo wakaoana. Sharifa hakuweza kufaidi ndoa hiyo kutokana na kwamba Suhail alikuwa muda mwingi na Shekhia pamoja na Mzee Sufian alikuwa anasafiri kimajini kwenda Yemen alikokuwa anajificha Mzee Sufian, ili utawala wa Budha usimuone kwani ulikuwa unamtafuta, kwa lengo la kumuua na kumnyanga'nya ile pete ambayo ilikuwa kinga yao dhidi ya maadui zao. Suhail alikuwa anatumia ile pete kumkinga Mzee Sufian na mahasimu wake wasimuone.

Siku zote kila chenye mwanzo hakikosi kuwa na mwisho japo Suhail baada ya kufanya starehe zote na kuishi maisha ya kimajini na Mzee Sufian alikuja kuumwa na ugonjwa usiojulikana. Ndugu na jamaa zake wakaja nyumbani kumuuguza ndipo Shehe Chaulla akamsihi aseme ukweli juu ya hayo majini yanayomtumikisha ili aweze kupona. Wakati akizungumza ndipo Mzee Sufian akaja ghafla katika kikao kile na Shekhia kwani ile pete ilikuwa haina nguvu tena kwa hiyo wakawa wanahangaika. Na katika kikao hicho ikagundulika kwamba mama Suhail na mama yake Shekhia ni mtu na mdogo wake na Shekhia na Sharifa ni watoto wa mama moja ambaye ni Amanda aliyemsaliti mumewe Fungameza na kwenda kuolewa na jini Sufian na kuzaa na jini huyo mtoto aitwaye Shekhia. Mama Shekhia alimsaliti mume wake ambaye ni baba Sharifa kwa tamaa ya pesa akaenda kuolewa na jini ambalo mwisho wa siku lilimnyonga na kumtoa kafara. Huu ndio ufupisho wa hii riwaya ya *Vita vya Mapenzi*.

Katika riwaya hii ya *Vita vya Mapenzi* maudhui mbalimbali yamechimuzwa kupitia mazingira halisi na mazingira ya kinjozi au dhahania kwa kiasi kikubwa. Kuna upanuaji wa matukio ambapo tunapata mandhari ya kinelibini. Riwaya mpya kama hii ya *Vita vya Mapenzi* haina mipaka wazi ya mawanda ya masimulizi: huweza kuhusisha ulimwengu halisi, ulimwengu dhanifu au wa njozi, kuna mahusiano na mitagusano kati ya binadamu na majini, kuna ndoa hata na uzao kati ya binadamu na majini, na mipaka ya maingiliano kati ya ulimwengu halisi na ulimwengu dhanifu, kati ya uhalisi na ndoto, sio tu imevunjwa bali pia ukweli uliopo umevunjwa. Vilevile hali hii huweza kutokea pale hali ya usimulizi inaachwa na riwaya au mhusika na kujitosa kwenye tathmini ya kisaikolojia (hasa kupitia ndoto). Na jambo hili linatokana na sababu kwamba riwaya hii ni ya kimajaribio iliyojikita zaidi katika uhalisiajabu kama tulivyokwisha kusema katika sura ya kwanza.

Katika riwaya hii mandhari halisi imetumiwa ili kufanya matukio yanayofanyika baadaye kuweza kukubalika kama ya kawaida katika jamii. Mfano wa mandhari halisi katika riwaya hii ya *Vita vya Mapenzi* ni pale mwandishi anatumia mandhari ya Dar es Salaam na mitaa yake mbalimbali, mji wa Bagamoyo-Pwani ambako ndiko matukio mengi zaidi ya kiuchawi na ushirikina yanatukia, mkoa wa Dodoma, mkoa wa Tabora na nchi ya Yemen huko Uarabuni. Mwandishi ametumia mandhari halisi katika kutufanya kuamini kuwa kupitia mandhari hizi, tunaweza kupata picha halisi ya mandhari ya kijiniuchawi na kishirikina katika kuchimuza maudhui mbalimbali. Tunaona hadithi ikisimuliwa katika mandhari ya kinelibini yaani, wahusika wanatoka katika ulimwengu halisi hadi ulimwengu wa kinjozi kupitia mambo ya kichawi na kimajini na kurejea tena katika ulimwengu wa uhalisia. Mwandishi anavunja mipaka ya kimawanda ili kuelezea mazingira tofauti wanamojikuta wahusika.

Mwanzoni mwa riwaya hii Mwingizi anaijenga mandhari ya kihalisia ambayo wasomaji wanatambua ubayana wa stendi ya mabasi Dar-es-Salaam. Mandhari ya ndani ya basi ambapo Suhail akiwa amekaa kwenye kiti akielekea kwa wazazi wake baada ya kumaliza masomo. Ndani ya basi anamuona mtu halisi, Mzee wa Kiasia aliyekaa

kwenye kiti kingine pamoja na abiria wengine na wahudumu. Safari ya kawaida inaanza kwa muda uliopangiwa. Ghafla wanapata ajali ambayo kiuhalisia ni ajali ambayo inaweza kutokea na hutokea mara kwa mara kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo mwendo kasi, ulevi na uzembe au ubovu wa vyombo vya usafiri lakini hii ni tofauti kwani ilikuwa imepangwa na jini Sufian. Mwandishi anamchukua msomaji katika safari ya kawaida na kumuingiza katika muktadha wa kiuhalisiaajabu pale anapoajinabishwa kwa tukio lisilola kawaida katika mandhari ya ajalini na kukubidhiwa pesa nyingi na kupewa masharti ya kuoa mke jini bila ya kujitambua. Mzee Sufian pamoja na kwamba alikuwa naye ameumia sana katika ile ajali lakini alimpa Suhail dola nyingi za kimarekani ili aweze kukubali masharti atakayompa pindi atakapomwambia ayatekeleze. Mwandishi anasema:

> Mzee akainuka kwa tabu sana na kuketi karibu ya begi, kisha akafungua zipu kubwa ya katikati kwenye begi lile, na ndipo Suhail alipopigwa na butwaa, huku akishindwa kuamini iwapo alichokuwa akikiona ndani ya begi lile kilikuwa ni chenyewe, ama anaota. Akili yake ilijaribu kufanya kazi mara kumi kidogo, lakini bado hakupata jibu la kile alichokuwa akikiona. Mzee aliliona hamaniko la Suhail lakini hakujali. Bila shaka alilitegemea, kwani lile begi jekundu lilikuwa limesheni pesa mpaka juu, tena zikiwa ni dola mia-mia tu za kimarekani. (uk 9)

Kitendo cha kuonyeshwa pesa katika mandhari ya ajalini kinakuwa si rahisi kwa mtu yeyote kugundua kuwa ulikuwa ni mtego wa kiajinabishi. Mandhari ya uhalisia yamejengwa kwanza kabla ya kuletwa mandhari ya kiuhalisiajabu. Si Suhail peke yake anayechotwa katika muktadha wa kiuhalisiaajabu, wasomaji pia wanachotwa kwa kule kuaijinabishwa kwa kuonyeshwa kwanza, mazingira ya kawaida kabla ya kuingizwa katika mazingira ya kimazingaombwe. Mandhari hii ya kiuhalisia kabla ya kiuhalisiajabu kwenye ajali hiyo mbaya, inachimuza jumbe nyingi tena mseto kama udhaifu wa nyoyo za binadamu kutekwa na vishawishi vya pesa, uwekaji umuhimu na kipaumbele katika mali badala ya maisha ya binadamu, urahisi wa jinsi viongozi wengi wa mataifa yanayoendelea wanavyofanyiwa hila za kuingizwa katika mikataba hewa inazoitia hasara nchi zao wakiwa na matumaini ya kusaidiwa.

Pia mandhari hii ya ajali hiyo mbaya ya basi inachimuza ujumbe wa jinsi viongozi wengi wa mataifa yanayoendelea wanavyotoa kafara mbalimbali ili waweze kupata nyadhizifa mbalimbali serikalini na wengine waendelee kubaki madarakani. Inaelekea baadhi ya kwani ajali zinazotokea huwa ni kwa ajili ya kafara kama Mzee Sufian alivyotumia majini na uchawi kusabaBisha ajali kwa kuwauwa watu wengi kwa ajili ya maslahi yake binafsi. Kwa sababu, katika ajali ile walikufa watu wengi sana ni wachache sana waliopona na ajali hiyo.

Aidha mandhari hii inachimuza ujumbe wa uwajibikaji na utendaji kazi bora kwa baadhi ya viongozi katika taasisi mbalimbali. Japo Sufian alikimbia kutoka katika himaya ya Budha lakini alikuwa ni kiongozi ambaye alipendwa sana na wanahimaya ya Budha kwa utendaji kazi wake. Ndio maana watu wengi walipendelea agombee uongozi mkubwa katika himaya hiyo ya kijini kule baharini lakini ikashishindikana kutokana na kugawa madaraka kwa kujuana. Ndio maana Sufian anaamua kuondoka kutoka kule baharini na kuja duniani na ile pete na uchumi wa kule Budha kwa lengo la kumtafuta mtu wa kumkaabidhi ili wale majini wa himaya ya Budha wasiweze kumuona. Kwani walikuwa hawana uwezo wa kumuona binadamu aliyekuwa amevaa ile pete ya Budha. Hivyo basi Sufian akatengeneza mazingira ya ajali ili aweze kumkabidhi pete Suhail.

Kwa hivyo, mandhari hii ya uhalisia iliyochanganyika na uhalisiajabu inaonyesha jinsi gani ajali imetokea lakini Sufian anampa pesa nyingi kwa Suhail wakati yeye mwenyewe ana hali mbaya. Tukio hili linaweza kufasiriwa kuwa na maana kwamba, kwa baadhi ya watu, hususan viongozi, kwenye maafa na maangamizi ya wengi, ndiko kunapochipuka neema yao, lakini neema ambayo hatimaye huwa ni ya kisirani na nuksi. Vilevile kupitia mandhari hii tunaona kwamba watu hawa wa mataifa yaliyoendelea wanapokuja katika mataifa ya Afrika wanajidai ni wasamaria sana kwa kutoa misaada kumbe wanatafuta njia ya kuangamiza nchi na wananchi katika nchi za Afrika kwa kuwanyan’ganya ardhi na kuwatesa wananchi. Wakati mwingine huwapa silaha za kivita wananchi ili wagombane halafu wao wajifanye wanakuja kutoa misaada ili waweze kuchuma mali katika nchi za kiafrika.

Mandhari hii ya kwenye basi na matukio ya kwenye basi yamebeba dhamira ambayo inaonyesha jinsi gani nchi maskini zinavyoangamia kwa ajili ya tamaa ya mambo ya kupita na mwisho wa siku zinachukuliwa mali nzuri zaidi. Vilevile mandhari hii inaibua maudhui ya jinsi viongozi wengi serikalini walivyo wa binafsi kwa kung'ang'ania madaraka na kujilimbikizia mali wakati wananchi wao wanateseka mwisho wa siku wanahaibika, kama Mzee Sufian anavyojilimbikizia mali na kung'ang'ania madaraka mpaka inafikia hatua anaamua kukimbia na pete ya serikali ya Budha. Na anaamua kumtafuta mtu wa kumpa pete ili aendelee kuitunza kwa kumpa dola nyingi.

Hali kadhalika, katika mandhari hii mwandishi anachimuza maudhui ya tamaa ya pesa kwani kilichokuwa kinamponza Sufian mpaka kukimbia katika himaya ya Budha ni kunga'anga'nia madaraka ambayo yatampatia pesa nyingi za kujinufaisha yeye na familia yake wala sio kunufaisha taifa lake kwanza, na yeye mwenyewe hatimaye. Ndio maana alipokosa uongozi aliamua kutoroka na mali nyingi ya utawala wa Budha na kuendelea kujinufaisha binafsi na familia yake. Ndivyo walivyo viongozi wengi wa nchi zinazoendelea huingia madarakani kwa lengo la kujinufaisha binafsi na familia zao. Hujenga majumba ya kifahari na humiliki ardhi kubwa kuliko hata wananchi wao.

Hivyo basi, hila za Mzee Sufian kamtamanisha Suhail dola nyingi kwenye begi na kisha kumpatia zote kwa kumpa masharti ya kuwa mfuasi wa majini na kumuoa Binti yake Shekhia. Mtunzi anatuonyesha jinsi Mzee Sufian alivyokuwa anampa masharti Suhail:

> "…pesa zote hizo nakupa wewe, ni za kwako... lakini kwa sharti moja tu, ambalo si gumu sana. Unapaswa umuoe Binti yangu na uishi naye kwa wema, amani na upendo. Ukawe mlinzi na kiongozi wake…sitaki kamwe mwanangu aolewe na majini!"(uk 10).

Baada ya maongezi haya Mzee Sufiani anakufa kimazingaombwe na kumuacha njia panda Suhail. Suhail anajuta anapokuja kugundua lakini akiwa hana la kufanya, kwani "maji yalikwisha mwagika". Mandhari na matukio yote ya kwenye basi yamekuwa ni ya kijiniuchawi kwani, mpaka ajali inapotokea Mzee Sufiani alikuwa pekee ndiye aliyeelewa chanzo chake na madhumuni ya kusababishwa kwa ajali hiyo.

Kwa mintarafu hii, mandhari na matukio haya yote yameweza kuchimuza dhamira ya ubayana hatima ya tamaa kwa watu binafsi, kwa familia, kwa mahusiano ya kifamilia, mahusiano ya wapenzi, na katika daraja nyingine. Mahusiano kati ya walio navyo na wasiokuwa navyo, kati ya nchi tajiri na nchi masikini zinazoitwa nchi zinazoendelea. Hii inatokana na sababu kwamba, katika kukabidhiwa na kupokea kitu cha thamani ndogo sana, watu binafsi, familia na mataifa yanayoendelea yanaingizwa katika nyavu za mikataba isiyoeleweka, mikataba ya unyonyaji, mikataba ya usaliti na uuzaji wa maliasili zetu ambazo tunahiari, japo ni za thamani kubwa, kuchukuliwa kwa faida duni na kisha tunaachwa kuibeba gharama kubwa ya misaada yao na viongozi wa nchi wanashindwa kujitoa kwa sababu walikuwa wameshasaini mikataba.

Katika eneo la ajali, Suhail anaonekana kuwasaliti wenziwe kwani ni kitu cha ajabu, ajali imetokea wenziwe waliponusurika wanaondoa majeruhi lakini yeye alikuwa ndani, ndipo waokoaji wakapatwa na taharuki lakini kumbe alikuwa haonekani kwa sababu ya nguvu za majini alizopewa na Mzee Sufian. Mandhari hii na tukio hili linachimuza dhamira ya viongozi wasaliti pindi wananchi wanaposaidia katika kuimarisha umoja na kuleta maendeleo wenyewe wanaonekana ni kikwazo katika kuleta maendeleo Suhail anafananishwa na viongozi hao. Pia mandhari hii inachimuza ujumbe wa watu wasaliti, wanaowasaliti wenzao kwa ajili ya maslahi yao binafsi hata wakati wa shida na hatari zaidi. Mandhari hii pia inachimuza ujumbe wa kuthamini mali au pesa kuliko maisha ya watu kama tunavyomuona Suhail. Wenziwe wamekufa yeye hana muda wa kuwasidia abiria wenziwe kuondoa maiti ila anathamini pesa alizopewa na Sufian kuliko maisha ya watu.

Pia, mandhari hii inachimuza jinsi watu wengine walivyo na roho ya tamaa kwani wako tayari kuwatoa wenzao kafara kwa ajili ya manufaa yao binafsi. Mzee Sufian aliwauwa abiria wengi sana katika basi hilo kwa lengo la kutaka asiweze kukamatwa na utawala wa Budha ndipo aweze kumkabidhi Suhail pete ya utajiri wa Budha.Unapopewa dhamana huna budi kuiheshimu dhamana hiyo vinginevyo ni kukabiliana na shutuma za usaliti. Suhail anawekwa katika mandhari ya kuamua kukataa au kukubali vishawishi.

Anaonekana kuwasaliti wenziwe badala ya kuwasaidia wenziwe anazidiwa na nguvu ya tamaa na anaamua kuwasaliti abiria wenziwe na kuwadanganya ili mradi aweza kutoroka na pesa alizorubuniwa nazo.

Mandhari ya ajali ya basi inachimuza dhamira ya viongozi wasaliti kwa jamii zao. Suhail anavaa sura ya viongozi wasaliti na wa binafsi. Kwa kuthamini pesa alizorubuniwa na Mzee Sufian kuliko maisha ya watu. Na kwa upande wa Mzee Sufiani mandhari hii inamjengea sifa ya kuwa mtu katili na muuaji ambaye yuko tayari kuwatoa wenziwe kafara kwa maslahi yake. Mwandishi anajenga mandhari ya ajali ya basi kinjozi. Ni mandhari ambayo yapo mbali na uhalisia kwani Suhail aliposhuka kutoka ndani ya basi wakati akikaguliwa na watu waliyokuwa wanaokoa majeruhi, lile begi lenye pesa halikuonekana na wakakagua begi lingine. Mwandishi anasema:

> …Cha ajabu kila abiria pale alikuwa akiliangalia lile begi dogo jeusi tu, na hakuna hata mmoja aliyejishughulisha kuangalia lile begi kubwa jekundu lililokuwa mgongoni ambalo ndilo hasa lenye pesa, Suhail naye aliligundua jambo hilo japo lilimpa faraja lakini lilizidi kumuacha na maswali mengi kichwani (uk 21).

Mandhari ya umazingaombwe yanadhihirika kutokana na tukio hili la ajali. Ni kwa vipi begi dogo jeusi linaokana lakini begi kubwa jekundu lisionekane? Udogo unavaa uhalisia lakini ukubwa unavaa uhalisiamazingaombwe. Mambo madogo yanachukuliwa hatua kama vile wezi wadogo wadogo na lakini wezi wakubwa wanaofilisi mali za umma na kuhujumu uchumi hawaonekani. Aidha mtunzi ametumia tukio hili la kiajabu katika mandhari hii kuchimuza ujumbe unaonyesha ni kwa jinsi gani misaada inayotolewa na nchi zilizoendelea inavyoishia kwenye mifuko ya viongozi tu. Wakati wananchi hawanufaiki kabisa na hiyo misaada na wala hawaioni kabisa. Suhail anafananishwa na viongozi wanyonyaji wa nchi za Afrika. Pia misaada hiyo hiyo baadaye hugeuka na kuwa kama chombo cha kunyonya nchi zinazoendelea kwa kuchuma uchumi mbalimbali katika mataifa yanayoendelea kwani mwisho wa siku hawa watoa misaada huhitaji baadhi ya vitu katika mataifa yanayoendelea na kwa kuwa

wametoa misaada ni lazima viongozi wetu watatoa mali za nchini zenye thamani kwa vimisaada vidogo sana walivyovipata.

Mwandishi anatuonyesha katika mandhari ya nyumbani, Suhail akiwa amejilaza kitandani ghafla kunatukia tukio la ajabu. Suhail anamsikia mtu anamwita na mtu anayemuita hamuoni na anasikia harufu ya marashi makali. Pia anasikia mlango wa chumbani kwake unafunguliwa na anayefungua mlango haonekani. Ghafla anasikia sauti tena nyuma yake ikicheka anageuka na kupata taharuki kwani alimuona Mzee Sufian amemjia nyumbani kwake wakati alishafariki na akawa haelewi ameingilia mlango gani hapo Suhail anaogopa zaidi. Mzee Sufian anasema: "Unataka kufanya nini sasa Suhail? Ebu tulia bwana, ulitegemea nitaingilia mlangoni? Hatwendi hivyo..." (uk. 32).

Mzee Sufian anamtokea kupitia ndoto akimtaka atimize masharti waliyokubaliana kwenye ajali ya basi kwa kuhakikisha anamwoa Binti yake na muda wote awe anavaa ile pete aliyompa. Mzee Sufian anaendelea kusema:

> …pili tafadhali tena sana, nakusisitiza ile pete niliyokupa usiwe unaivua na kuiacha mbali kwani ile ndiyo siri ya mafanikio na ulinzi wako wewe na mkeo mtarajiwa! Najua kuwa tangu ulipoivua wakati unaoga bafuni hukuivaa tena na ukaitelekeza hukohuko!" (uk 33).

Suhail akawa anakataa kutimiza masharti wakati amechukua pete na pesa. Ghafla Mzee Sufian akammwagia Suhail grasi ya juisi usoni na kumpiga kibao mpaka akalia kwa uchungu mkali. Mambo yote yalipokuwa yakiendelea kumbe Suhail yuko usingizini akiota ndoto. Japo alikuwa akiota ndoto lakini tunaona aliposhtuka anaona amelowa juisi na hivyo mtunzi anatumia ndoto na uhalisia katika mandhari hii ya nyumbani kwa Suhail. Mwandishi anasema:

> …Maumivu makali yakamfanya Suhail apige kelele kali na ya uchungu "Yalaaaaa nakufaaa!" kelele hiyo ndiyo iliyomtoa usingizini na kumfanya agundue kumbe alikuwa akiota tu. Akainuka haraka pale kitandani akatazama huku na kule huku akitweta kama labda angemuona Mzee Shamhurish lakini hakuona kitu (uk. 33).

Mtunzi ametumia mandhari hii ya nyumbani kwa Suhail kwenye jumba la kifahari kwa kumuonyesha Suhail akiwa ndotoni wakati matukio hayo yanapotukia. Kupitia mandhari hii ya ndotoni tunaona imechimuzwa dhamira ya viongozi wetu wa Afrika wanavyoishi maisha ya kifahari katika majumba ya kifahari na kuwasahau wananchi waliowachagua na kuwaingiza madarakani. Viongozi hawa wanajinufaisha wenyewe kwa pesa za maendeleo ya wananchi wakati wananchi wao wanaishi maisha magumu kwani hata maji ya kunywa ni shida. Mwisho wa siku wanaposhindwa kutimiza mahitaji ya wananchi wao ndipo sasa ugomvi unaanza na wananchi wanaandamana kutaka na kudai haki zao.

Mbali na maisha ya kifahari kunaibushwa swala la masharti wanayokubali viongozi wa nchi zinazopokea misaada ambayo yanawaweuza viongozi hao kuwa watumwa kiakili na kimatendo na hatimaye wananchi wenyewe huishia kuwachukia na kuwadharau. Maisha wanayojinafasi nayo ni ufahari wa mkopo, ujamala wa mikatale inayoumbua ubinadamu wao.Vilevile, mandhari hii ya ndotoni imetupeleka kujua jinsi viongozi wetu wanavyokuwa watu wema tunapowachagua kwenda kutuwakilisha bungeni lakini pindi wanaposhindwa kutimiza ahadi za wananchi wanakosa kura tena na wengine kushtakiwa kwa ubadhirifu wa pesa za umma.

Pia mtunzi anatuonyesha katika mandhari ya nyumbani kwa Mzee Atrash, Bagamoyo. Anatuonyesha Suhail akiwa ameenda kwa ajili ya kujua Shekhia anaishi wapi maana huyo Binti alikuwa ni jini lakini Suhail alikuwa hajui. Suhail akaanza kujieleza kwa Mzee Atrash ili aweze kupata msaada juu ya pete na pesa alizopewa na Sufian lakini hakujua kwamba Mzee Atrash alifahamu kila kitu kabla hajaanza kujieleza. Lakini yeye akawa anaeleza uongo ndipo Mzee Atrash akamtukana kwa kuongea uongo. Mzee Atrash anasema:“Huwa siongelei habari za mtu hovyo hovyo tu, wala huwa sitoi habari nyeti kwa mtu asiyekuwa makini, wala kwa mtu muongo, au kwa mtu msaliti na mwenye tamaa…”

Akakohoa kidogo Mzee Atrash lakini kabla hajaendelea akawahiwa na Suhail;

> "Sijakuelewa Mzee!" "Utanielewa tu, kwani athari za mtu muongo, msaliti, na mwenye tamaa huzijui?" "Nazijua," alijibu Suhail huku akiwa anamuangalia usoni Mzee yule ambaye yeye hakuwa akimuangalia kabisa zaidi ya kuendelea kukiinamia kitabu chake kidogo kama vile yale ayasemayo anayatoa katika kitabu kile (uk 47).

Hali kadhalika kupitia mandhari hii, mtunzi anachimuza dhamira ya madhara yanayomfika mtu muongo kama ambavyo wafanyavyo viongozi wa serikali hasa wabunge wa nchi nyingi za Afrika. Pindi wanapotaka kugombea ubunge wanatoa ahadi nyingi kwa wananchi na mwisho wa siku hawazitekelezi. Huwa wanafikiri wananchi ni wapumbavu, maana wanarudi tena kuwaomba wawachague na ndipo wananchi wanawatukana na kuwaona waongo na ni watu wenye tamaa japo wenyewe wanahisi wananchi ni wapumbavu. Suhail anafananishwa na viongozi wa aina hiyo; wenye tamaa kwani alikuwa akimdanganya Mzee Atrash nyumbani kwake akijua haelewi kama Mzee Atrash anajua kila kitu kuhusu mahusiano yake na Sufian. Pia mandhari hii inakuza ujumbe wa uongo hata kwa watu binafsi katika maswala mbalimbali kwani uongo huleta migongano baina ya watu kwani kuna watu hutumia uongo ili waweze kupata misaada.

Mzee Atrash anamsimulia Suhail kuhusu Mzee Sufian na kuwa si mwenyeji wa Bagamoyo ni mwenyeji wa Asia alihamia Bagamoyo na kununua eneo kubwa sana na kujenga jumba kubwa la kifahari. Mzee huyu alikuwa ni mfanyabiashara wa madini na mafuta na alikuwa haonekani kwa majirani zake. Mzee Atrash anasema:

> ..bwana yule mwenye asili ya Asia aliyetambulika kwa jina la Sufian au Mzee Sufian kama ambavyo vijana wengi wa hirimu yako walivyomwita kwa heshima, ilisemekana ni mfanyaBiashara mkubwa wa mafuta na madini na kwamba huzungukia mikoa na nchi kadhaa kwa ajili ya kutekeleza Biashara zake hizo. Lakini katika kipindi chote alichokuwa akiishi ndani ya jengo lake hilo hatukuwahi kumjua mke wala mtoto wake zaidi ya vijana wawili wa kiarabu waliotambulika kama watumishi wake!" (uk 48-49)

Kupitia mandhari hii na masimulizi haya mtunzi anatupa picha halisi ya jinsi gani wageni wa mataifa yaliyoendelea wanapokuwa katika nchi zetu wanavyotangamana na wenyeji kwa dharau. Wanakuwa na dharau kiasi kwamba, hawahitaji ujirani na majirani zao japo wapo katika nchi ambayo sio yao. Ndivyo ilivyokuwa kwa Mzee huyo wa Kiasia aliyekuwa mfanyabiashara wa madini na mafuta, tena madini yetu na mafuta ni yetu lakini hakuhitaji kuzoeana na wenyeji baada ya kukaribishwa katika mji wa Bagamoyo huko Pwani.

Kwa kujenga na kuzisawirii mandhari mbili za mijini na mashambani, ambako matukio yanajitokeza katika riwaya ya *Vita Vya Mapenzi*, mwandishi anakinzanisha taswira za ujadi na usasa. Ujadi unaingizwa katika muktadha wa usasa kwa maana kwamba matukio yanayojiri katika maisha ya Suhail yana mizizi yake katika taratibu za kijadi, hususan mahusiano ya kifamilia. Mandhari ya Mlingotini Bagamoyo na Kipalapala, Tabora yanaakisi muendelezo wa fikra za ujadi na imani za kishirikina. Wahusika wanaozaliwa vijijini na kisha kuhamia mijini na kurudishwa tena vijijini hawatengani au hawakengeushwi na uasilia wao, utamaduni wao, na miungano yao ya kifamilia na kiimani. Wanakuwa wawakilishi wa uasilia wao, kwa hivyo, kwa kubaini au kutobaini, wanaendeleza fikra, itikadi na imani za kichawi na kishirikina. Katika hali halisi za kijiografia, vitongoji vya Bagamoyo ambako ni pwani, vinasadikiwa kuwa vitovu vya kujengewa taswira ya ushirikina wa kimajini.

Mwandishi ameendelea kutuonyesha mandhari ya kijiniuchawi chini ya bahari kwamba ni sehemu ambamo kulikuwa na utawala mkubwa na makazi ya kudumu na kulikuwa na himaya iliyokuwa inaitwa Bhudha. Himaya hiyo ilikuwa na utajiri mkubwa sana na kulikuwa na watawala mbalimbali waliokuwa wakiongoza himaya hiyo. Miongoni mwa watawala hao alikuwepo Mzee Sufian aliyeshika nafasi ya juu sana katika utawala huo wa Bhudha. Kilipofika kipindi cha uchaguzi, inabainika kulikuwa na migawanyiko, kila kikundi kikawa kinamwandaa jini aliyeonekana kuwa na uwezo wa kuongoza. Hata kiongozi aliyekuwa anayetoka madarakani, akawa anamuandaa jini anayemtaka yeye ili

aje kumuachia madaraka hayo kwa ajili ya kuficha maovu aliyokuwa ameyafanya. Mwandishi anasema:

> ..sasa ilipoanza kukaribia kipindi cha uchaguzi kila kikundi kikawa kinamuandaa Jini aliyeonekana kuwa na uwezo wa kuukwaa uongozi wa juu wa himaya hiyo ya Budha. Sasa kiongozi anayemaliza muda wake naye akawa anamuandaa jini aliyemtaka yeye ili aje amuachie madaraka hayo kwa ajili ya kuficha maovu yote aliyokuwa akiyafanya kipindi cha utawala wake. Wakati huohuo wanahimaya wengine wa Budha nao walikuwa wamemuandaa Jini mwingine aje ashike madaraka hayo, Jini huyo aliitwa Sufian Bin Shamhurish!" (uk. 52).

Mandhari hii ya kiuhalisiajabu yenye matukio ya kimajini na kichawi chini ya bahari, yamechimuza maudhui mazito ambayo tunayashuhudia kwa kiasi kikubwa katika nchi za Afrika katika swala zima la kipindi cha uchaguzi wa viongozi kama maraisi na wabunge. Uhalisi unaojitokeza ni uwepo wa siasa za migawanyiko, mashindano ya maslahi ya kimakundi yanayojitokeza kama vyama vya kisiasa ambapo kila chama kinamwandaa mtu wake, chama tawala nacho kinamwandaa mtu wake japo ndani ya chama tawala nacho kunakuwa na makundi makundi. Mambo kama haya yanajitokeza sana katika nchi za Afrika. Mfano mzuri nchini Tanzania, makundi makundi katika vyama hasa chama tawala, huwa yapo kwa kiasi kikubwa. Ndani ya chama kunakuwa na kikundi fulani kinachomtaka mtu fulani kuendeleza maslahi ya kikundi hicho. Na raisi aliyeko madarakani ambaye ndiyo muda wake unakwisha naye anamtaka mtu mwingine.

Kwa hivyo, nchi za Afrika zimekuwa zikitumia ubabe hasa kwa upande wa uchaguzi wa maraisi katika kuhakikisha kwamba, raisi aliye madarakani anamteua kiongozi anayemtaka kushika madaraka. Au yeye mwenyewe atang'ang'ania kubaki madarakani hata zaidi ya miaka thelathini ili aweze kuficha uozo aliokuwa anaufanya pindi alipokuwa madarakani. Ndivyo ilivyokuwa katika utawala huu wa kimajini wa Budha chini ya bahari. Hapa mtunzi anaendeleza maudhui mseto kama vile ufukara wa fikira na ruwaza ya vyama vyetu vya kisiasa; laana ya kisiasa inayotokana na maono banifu ya viongozi wa kisiasa, ukosefu wa maoni, mipango na mikakati ya kuendeleza maslahi ya

kitaifa na badala yake kuweka kipaumbele na msisitizo katika uendelezaji wa maslahi ya kimakundi, lakini zaidi uendelezaji wa maslahi ya ki binafsi, sawia na alivyofanya Sufian.

Aidha kupitia mandhari hii tunaona kunakuwa na mahusiano ya kimataifa, na mahusiano hayo kwa upande mmoja yanaonekana kunufaika zaidi kuliko upande mwingine na upande usionufaika ni upande wa nchi za Afrika. Kwa sababu mahusiano haya yamekuwa yakifanyika hasa zaidi katika kuwekeza katika mali ghafi za Afrika. Kwa hivyo, pete ambayo ilikuwa ikitumiwa na utawala wa Budha inaweza kuibua ujumbe wa jinsi mataifa yaliyoendelea yanavyotoroka na malighafi za Afrika zenye thamani sana na kuacha tukiwa tunahangaika na kumtafuta mchawi wakati wachawi ni sisi wenyewe. Kupitia pete iliyochukuliwa na Mzee Sufian katika mandhari ya himaya ya Budha baharini, ni dhahiri kuwa Mzee Sufian anafananishwa na viongozi wa mataifa yaliyoendelea ambao huja katika nchi nyingi za Afrika kwa lengo la kubeba mali ghafi zake zenye thamani kubwa sana kama Mzee Sufian alivyotoroka na pete katika utawala wa Budha. Katika daraja ya mtu binafsi mandhari hii inadhihirisha usaliti unaochochewa na ulafi, ubinafsi, uchoyo na inda.

Hali kadhalika, mtunzi anatuonyesha mandhari ya nyumbani kwa Sufian Bagamoyo ambapo nyumba hiyo kwa nje ilikuwa inaonekana imechoka wala haifai kama vile, watu hawaishi humo kwa mtu ambaye angepita nje angejua hivyo. Lilikuwa ni ghorofa lililochoka sana lakini humo ndimo ulikuwa utawala wa kimajini wa Mzee Sufian kwa sababu Suhail alipoingizwa mle ndani alistaajabu. Pia mwandishi anaendelea kutuonyesha mandhari ya ndani ya jengo hilo kwa kuonyesha ni kwa jinsi gani lina vitu vya dhahabu, nakshi na vitu vya thamani lakini nje limechoka halina thamani kabisa. Mwandishi anasema:

> ……ni kama ghorofa moja lakini lilikuwa ni chakavu kiasi cha kumfanya mpita njia ambaye ni mgeni kuamini kuwa mle ndani hapakaliwi na watu na labda pengine ni gofu tu la kuhifadhia nafaka. Lakini cha ajabu jengo hilo lilikuwa limo ndani ya uzio ambao ulionekana kusafishwa kwa kupaliliwa majani

> yaliyokuwa yakiota pale na kufanya hisia kichwani mwa Suhail kuwa mle ndani kuna watu wanaishi (uk 60).

Vilevile katika mandhari hii ya kiuhalisiajabu Suhail anaingizwa kwenye chumba kilichokuwa kizuri sana, wakati jengo hilo kwa nje lilikuwa chakavu na anakutana na wazee wa Kiasia wapatao tisa. Suhail akiwa anastaajabu ghafla akatokea Mzee Sufian ambaye yeye Suhail alifikiri ameshakufa kwenye ile ajali, kumbe Mzee huyu ni jini na kiongozi wa majini hapo nyumbani kwake. Mtunzi anasema:

> ..ndipo sasa macho ya Suhail kwa mara ya tatu ukiachalia mbali mara ya kwanza kule kwenye ajali na mara ya pili kule usingizini, hapa akamuona Mzee Shamhurish akifika na kupokelewa kwa heshima na furaha na wale watu waliyokuwa wamesimama. Safari hii Mzee Shamhurish akiwa amevaa kanzu nyeupe huku amejifunika kichwani kwa kiremba chekundu kilichomfanya aonekane tofauti na vijana wengine wote mle ndani. Baada ya Salamu Mzee Shamhurish akaketi chini ndipo na wale wengine nao wakaketi.
>
> "Haya bwana Suhail karibu sana Bagamoyo," alivunja ukimya Mzee Shamhurish huku akimtazama Suhail usoni (uk 63).

Suhail alitetemeka akashindwa kuelewa nini kilikuwa kinaendelea katika jengo lile kumbe kwenye lile jingo, Suhail alipelekwa kimajini kwa ajili ya kukutana na utawala wa Sufian ili aweze kusaini mkataba wa kumuoa Shekhia na ilimlazimu afanye hivyo.

Mwandishi kupitia mandhari hii anachimuza maudhui ya sura za ukoloni mamboleoa na jinsi ukoloni mamboleo unavyozitesa nchi za Afrika baada ya kuondoka ukoloni mkongwe. Nchi zilizoendelea zinatumia njia ambazo kwazo mataifa ya Afrika yanajisingizia uhuru lakini ukweli wa mambo ulioko ni kwamba, huu ni uhuru wa kinafiki, ambapo kwa kawaida huwezi ukadhani nchi huru zinatawaliwa lakini zinatawaliwa pasipo wenyeji kujua kwa kupitia ukoloni mamboleo. Mikataba tunayosaini tunajichinja wenywe pasipo kujua. Kupitia mandhari hii mwandishi anamuonyesha Suhail katika jumba la Sufian akisaini mkataba ambao mwisho wa siku unampeleka katika majuto makubwa.

Ndivyo ilivyo kwa mataifa ya ulimwengu wa tatu mikataba wanayosaini na mataifa yaliyoendelea mwisho wa siku huwagharimu kama Suhail ilivyomgharimu mpaka akapoteza maisha. Mwandishi ametumia mandhari ya jumba hili chakavu pia kuchimuza maudhui ya ubovu wa ofisi za serikali katika nchi za ulimwengu wa tatu. Ukizitazama kwa nje ni kama zimechoka kumbe ndani zinasaini mikataba ya vitu vinavyoingiza pesa nyingi sana kama migodi ya dhahabu, madini ya tanzanite, almasi na ardhi. Pesa hizo zinawanufaisha watawala wenyewe na wanajjisahau kutengeneza hata ofisi wanazozitumia kuandikishiana mikataba hiyo, hazifanani na hizo pesa zinazosainishwa katika hiyo mikataba.

Ndivyo ofisi mbalimbali na nyumba mbalimbali za umma zilizvyochoka. Mfano mzuri katika shule nyingi za umma nchini Tanzania ziko katika hali mbaya kwani kuna majengo yameoza mpaka yanataka kuanguka lakini katika majengo hayohayo, ndimo wanamotokea viongozi wa baadaye. Hospitali za serikali nazo zipo ovyo sana wala hazitengenezwi na viongozi wapo ndani ya nchi. Japo wanaona hali ilivyo mbaya lakini wanaendelea kujineemesha na hiyo mikataba kwa kupata pesa nyingi wenyewe. Pia mwandishi anatumia mandhari ya uzuri wa lile jengo kwa ndani wakati nje chakavu, kuonyesha ndani ndimo kuna mikataba ya pesa inasainiwa. Matukio mengi ya kijiniuchawi na kimazingaombwe yanajitokeza katika mandhari ya majumba au majengo ya “zamani”, machakavu na yenye sura za kutisha kwa nje na kukinzanishwa na umaridadi uliomo kwa ndani. Kwa nini mtunzi anatumia taswira ya majumba au majengo ya zamani? Alipokuwa analielezea jumba la Socotra, Yemen katika (uk. 109-110), jawabu linapatikana.

Uchakavu na kutelekezwa ni sifa ya jengo ambalo mtunzi anataka kuwajengea wasomaji wake kama makazi ya kutisha na ya upweke yanayokaliwa na ‘majini’. Mandhari ya kutisha na majumba wanamoishi viumbe wa dunia nyingine isiyo hii halisi inabainishwa na mtunzi. Dunia ya umazingaombwe inawakazi kama vile mizimu, wachawi, misukule, majini na watu walio katika nusu urazini. Dunia hiyo inatisha na ndiyo maana inajengewa taswira ya upweke, ukimya na uchakavu. Kuna usambamba wa hoja ya

kutisha, upweke na uchakavu na mifumo yenye kuwakandamiza wanajamii. Ingawaje inaonekana bado ina nguvu lakini mwandishi anawajengea wasomaji wake taswira ya mfumo unaoangamia na kuchakaa. Kama ulivyo uchawi na ushirikina ambao ni tabia inayoogopesha machoni, lakini kiundani ni mfumo unaoangamia na hauna mashiko. Kupitia taswira za makaburi na majengo chakavu, Mwingizi anatoa rai ya kuangamiza mifumo yote inayowakandamiza wanajamii na kuwarudisha nyuma katika harakati zao za kujiletea maendeleo na ustawi wa jamii.

Mwandishi anavunja mipaka ya matukio ya kishirikina kuwa yana mwanda maalumu na badala yake yanajitokeza mahali popote kama vile katika vituo vya polisi, mahospitalini, kwenye mabasi ya abiria, maporini, na hata kwenye majumba ya kifahari ya Mbezi. Uvunjaji wa mwanda wa matukio ya ukweli na ule wa kimazingaombwe ni jitihada za mwandishi kutaka kubaini kuwa fikra za kishirikina hazina mipaka ya rika, jinsia, usomi, itikadi, na hata vyeo. Msomaji anaonyeshwa tabaka la wakandamizaji wakiwa katika mazingira ya hotelini wakifanya vikao vya kuhujumu uchumi wa nchi (uk 234). Tabaka hilo linaundwa na watu waliopewa dhamana na jamii lakini wanashindwa kuheshimu dhamana hiyo na badala yake wanakuwa ni wasaliti wanaofanya mambo yao kwa vificho. Nyumba wanamofanyia mkutano ni ya kificho;

> Joram ndege aliposhuka aliingia ndani ya jengo lile na kupotelea kwenye *korido moja ndefu* iliyosheheni vyumba vingi kulia na kushoto. Kila chumba kikiwa na watumishi wakiendelea na majukumu yao tofautitofauti. Korido ile ilimchukuwa moja kwa moja mpaka katika chumba kimoja kilicho kwenye kona. . Alipofika hakugonga mlango wala kubonyeza kitufe chochote, mlango ukafunguka wenyewe, Bila shaka alikuwa akionekana kwenye kamera maalumu (uk 234).

Uficho wa tabaka kandamizi unachorwa na mwandishi kupitia chumba maalumu. Mwingizi anatumia neno "kupotelea" na kitendo cha "kutokugonga mlangoni" ambapo kunamjengea picha msomaji juu ya uficho na usiri mkubwa wa mtandao wa wasaliti katika jamii.

Halikadhalika mtunzi anatuonyesha mandhari ya chuoni alikokuwa anasoma Shekhia na Suhail mpaka wakaamua kuwa wapenzi pasipo Suhail kufahamu kuwa Shekhia alikuwa ni jini. Suhail alimpenda Shekhia kwa sababu alikuwa anamtunza na kumpa pesa nyingi ndio maana akaamua kuingia naye katika mahusiano. Mwandishi anatumia mandhari haya kuchimuza ujumbe wa madhara ya mapenzi ya pesa. Kwani, Suhail alimpenda Shekhia kwa sababu alikuwa anampa pesa nyingi wakati alikuwa na mpenzi wake Sharifa. Mapenzi ya aina hii yapo katika vyuo vikuu vingi sana wanafunzi kujiingiza katika swala la mapenzi wakiwa chuoni kwa ajili ya tamaa ya pesa. Wasichana kutembea na baba zao na wanaume kutembea na wanawake wakubwa kama mama zao kwa sababu ya pesa. Mtunzi anamtumia jini Shekhia akiwa na binadamu wa kawaida katika mandhari ya uhalisia, kuyaweka wazi maudhui na kuitahadharisha jamii kuepukana na mapenzi ya pesa.

Vilevile, mwandishi anatuonyesha mandhari halisi ya nyumbani kwa wazazi wake Suhail huko Tabora. Suhail anapofika anashangaa kuona mji haubadiliki mji umejaa bado magofu ya kale hauendelei ndio unazidi kuharibika alishangaa sana. Na hii ni kwa sababu alikuwa hajafika muda mrefu toka ajiingize kwenye mikataba ya utawala wa majini na kupewa pesa nyingi na hata kuwasahau wazazi wake. Suhail anasema:

> "Duh jamani Tabora yetu haibadiliki kabisa, nilitegemea kuwa nitakuta hali imebadilika hata kidogo lakini wapi!" Suhail alivunja ukimya, "Yaani huu mkoa sijui ni nini hasa, nasikia eti wanasema kuna Sharifu sijui aliuachiaga laana zamani sana!" Majibu ya Mzee Kusekwa yalisabaBisha kicheko kikanguruma pale uani kabla ya Suhail kujibu tena (uk. 81).

Suhail anaendelea kumwambia baba yake tatizo ni viongozi yaani, tungepata viongozi wenye dhamira safi, uwajibikaji na uadilifu hakika patabadilika. Naye baba yake akaendelelea kuzungumza kuhusu huo mji sababu ya kutoendelea kutokana na hata sisi wananchi kutokuwa na nia ya mabadiliko. Mzee Kusekwa anasema: "Siyo viongozi tu, yatupasa wananchi sote tuwe na nia ndo mabadiliko yatakuja." (uk. 81)

Mwandishi kupitia masimulizi haya katika mandhari ya nyumbani kwa Mzee Kusekwa anachimuza dhamira ya wasifu wa viongozi wa kisiasa, matarajio waliyonayo wananchi juu ya viongozi wao; wasifu wa kimsingi ukiwa ni kuwajibika, utendaji wa kazi ili wananchi waweze kuboresha maisha yao pia. Pia mtunzi kupitia kwa masimulizi haya anawakumbusha wananchi kuchagua viongozi ambao watajali maisha bora katika miji wanamoishi. Swala lingine linaloibuka kutokana na mazungumzo haya ni kuhusiana na uwepo wa viongozi wasioona,viongozi wasio na ruwaza, malengo na maono; hawa ni viongozi ambao japo wapo nchini mwao lakini wanaishi maisha yanayoakisi uhalisi tofauti na uhalisi wa maisha yawananchi. Wakati pale viongozi tayari wamo peponi katika nyemi na nderemo, wananchi wamo jehanamu, wanasaga meno kwa sababu ya shida juu ya shida.

Kwa upande mwingine tena mwandishi anatuchorea mandhari ya angani ya kijiniuchawi ambapo kupitia mandhari hii tunamuona Suhail anatumia pete kusafiria angani kutoka Tabora mpaka Dar-es-Salaam kwa muda wa dakika tano. Sehemu ambayo ina kilometa zaidi ya 700 kwa ajili ya kwenda kumuomba Shekhia amkubalie kumuoa Sharifa kutokana na Suhail kumsaliti mpenzi wake wa zamani kwa tamaa ya pesa. Mwandishi anatuambia:

> Saa tisa usiku, hali ya ukimya ikiwa imetawala karibu maeneo mengi sana huku walio wengi wakiwa wanavuta shuka tu vitandani mwao, Suhail yeye alikuwa njiani akielekea Mbezi, Dar es Salaam. Hakuwa na usafiri wowote zaidi ya pete yake iliyomtoa pale Tabora kwa kasi ya ajabu baada ya kuiamrisha tu kufanya hivyo. Moja ya faida ya pete ile ilianza kuonekana! Ndani ya dakika tano tu akawa amewasili Mbezi, Dar es Salaam huku wazazi wake wakijua yuko chumbani amelala (uk. 100).

Pamoja na Suhail kwenda kumuomba Sharifa aweze kukubali ili aweze kumuoa mpenzi wake wa zamani aliyemsaliti. Shekhia alikataa kwa sababu alishaingia mkataba na yeye hivyo hawezi kumuacha. Shekhia akamnyooshea pete yake ya kijini maana alikuwa ni jini ikapiga miale mikali ya moto na ikataka kumdhuru.

Kupitia mandhari hii na matukio haya mwandishi anakuza maudhui ya usaliti ambapo katika misingi ya mtu binafsi Suhail anakuwa msaliti mara mbili, alimsaliti Sharifa na sasa yu mbioni kumsaliti Shekiah. Hizi ndizo tata na athari za kuweka tamaa mbele. Lakini inapozingatiwa kwamba kihalisi Sufian na Binti yake Shekiah ni watoro kutoka utawala wa Budha, dhana hii ya usaliti inayoendelezwa hapa inaweza kukuzwa na kuangaliwa katika misingi ya mahusiano ya kitaifa kwamba, mataifa yanayoendelea kupitia viongozi wake yanasaliti matumaini na matarajio ya wananchi kunufaika kutokana na sera chanya za serikali kuinua na kuimarisha hali za maisha ya wananchi. Kwa mfano, viongozi wengi wa mataifa yanayoendelea wamekuwa ni wasaliti kwa nchi zao kwa kuingia mikataba mingi sana, mikataba yenye masharti na mapendeleo kuneemesha na kufaidi wachache, mikataba inayosainiwa pasipo kuwashirikisha wananchi na ilhali hatimaye wananchi ndio wanaobebeshwa mzigo mzito wa kulipa madeni na kuwatumia riba watu fiche wasiokuwa wao wenyewe wananchi.

Kupitia matukio haya tunaona jinsi usaliti huu hatimaye unavyowagharimu viongozi hawa na kudumaza maendeleo ya nchi. Wakati mwingine uzalendo usio tija unawashinda hawa wananchi wanaamua kuandamana kumtoa kiongozi madarakani au kugombana na wawekezaji ambao wamesaini mikataba na viongozi, mpaka wawekezaji wanamua kukimbia. Pia mandhari hii inachimuza ujumbe wa usaliti hata kwa watu katika mahusiano ya kimapenzi kwa wanandoa na hata kwa wachumba kwamba, si mzuri kwani mwisho wa siku huleta madhara. Mtunzi anatumia mandhari hii ya kijiniuchawi kupitia Suhail na Shekhia kuchimuza maudhui ya usaliti.

Mtunzi anatuonyesha mandhari na matukio yanayotendeka huko Yemen ambako ndiko asili ya Mzee Sufian. Wakati Mzee huyu akiwa huko Yemen ghafla pete ya Suhail ya mkononi aliyopewa na Mzee Sufian inaanza kuwaka kwa nguvu hapohapo akasafirishwa kiuchawi mpaka alikokuwa Mzee huyo. Baada ya kufika huko Yemen anawashuhudia wanaume fulani wakimwanguasha chini baba mkwe wake wakitaka kumuua na wakimtaka aonyeshe pete ya Budha iko wapi! Katika jengo fulani huko Yemen. Hao wanaume waliokuwa wanampiga ni miongoni mwa watawala wa Budha

huko chini ya bahari baada ya Mzee Sufian kushindwa uongozi akaamua kukimbia na hiyo pete iliyokuwa inawaongoza. Ndipo utawala huo ukawatuma watu wamtafute popote pale! Wakaenda kumkuta Yemen lakini akiwa hana pete kwa sababu pete ile alishampa Suhail. Mwandishi anatuambia:

> Mzee Sufian Shamhurish naye hatimaye akawa ni miongoni mwa wahanga walioingia kwenye rekodi za kufanyiwa unyama na udhalimu mkubwa ndani ya jumba hilo. Alikuwa akiteswa vikali humo ndani alipoingizwa msobemsobe baada ya kukamatwa ghafla kwa kushtukizwa alipokuwa matembezini, waliomkamata ni makamandoo watatu wa kijini kutoka katika Himaya ya Budha ambapo waliagizwa kufanya msako mkali na kuhakikisha wanamtia nguvuni, kisha wamnyang'anye Pete yao kabla ya Kumfikisha Budha akiwa hai au maiti (uk. 110).

Kupitia mandhari haya ya nchini Yemen na matukio yote hayo ya kijiniuchawi mwandishi anakuza dhamira ya jinsi viongozi wa nchi nyingi za Afrika walivyo wababe hata wakiwa madarakani. Viongozi wa Afrika hata kama wakiingia madarakani kwa njia isiyo halali bado wanaendelea kupambana na wapinzani ambao wamekwisha kuwaachia madaraka. Japokuwa wakati mwingine wapinzani huamua kuwaachia hata kama wameonewa. Viongozi hawa wanafanya hivyo kwa kuhofia kupinduliwa madarakani kwa sababu wanakuwa wameingia kwa njia zisizo halali. Japo kuna viongozi wengine wanaamua hata kuwafunga jela wapinzani wao ili mradi tu kuogopa kupinduliwa kwa kuwa hawakuingia madarakani kiuhalali. Vilevile mandhari haya ya Yemen yanaibua swala la viongozi wa kigeni kuwajibikia ushuru na kodi zinazotolewa na wananchi wa nchi hizo kwani misaada wanayoitoa katika mataifa yanayoendelea ni misaada inayotokana na kodi zizotozwa wananchi katika nchi zao. Ndio maana wanatakiwa kwa hali na mali kuhakikisha kodi za wananchi wao zinazalisha zaidi kwa kuzinyonya nchi zinazoendelea. Kwani Mzee Sufian pesa alizomkabidhi Suhail si zake, amezichukua bila idhini kutoka kwa utawala wa Budha. Kwa njia hii uwajibikaji unakwenda kote kote, kwa viongozi wa nchi tajiri na viongozi wa nchi zinazokopeshwa.

Mtunzi anaendelea kutuonyesha mandhari hii hii ya Yemen ambapo tunaona tukio lingine la ajabu Suhail anapotumia dakika kumi na tano kuwasili Yemen akitumia ungo

kwa ajili ya kwenda kumkomboa Mzee Sufian kutoka mikononi mwa wale makomandoo wa serikali ya Budha. Suhail anafanikiwa kumkomboa Mzee Sufian kutoka mikononi mwa wale makomandoo japo na yeye anapigwa sana lakini baadaye anafaulu kuwashinda hao makomandoo. Mwandishi anasema:

> Majini wale hawakulaza damu wakampokea Suhail kwa kichapo cha haja mpaka Suhail akahisi harufu ya mauti. Wakati majini wale wawili waliyokuwa wamejificha mle chumbani wakiendelea kumshushia kichapo ghafla Suhail akashangazwa na tukio lililotokea ambapo Mzee Sufian aliyeonekana kuishiwa kabisa nguvu, aliruka sarakasi ya ghafla, akatua juu ya meza moja chakavu mpaka ikasambaratika kisha Bila kuchelewa akamrukia mmoja kati ya majini wale akamtandika mateke ya kwenye mbavu mfululizo. Hapohapo Suhail naye akamrukia yule mwingine akampelekea ngumi za nguvu kisha akamshika kichwa na kumvunja shingo yake (uk 112).

Kupitia mandhari na matukio haya ya Yemen katika jumba ambalo walikuwa majini watatu wa Budha na Mzee Sufian kunaonyesha matukio ya kijiniuchawi na ya kutisha yanadhihirika. Mandhari hii na matukio yamechimuza dhamira kuwa na ushujaa kwa wale viongozi wanaoshindwa au wanaodhulumiwa katika nyadhifa mbalimbali kutokukubali kuonewa na kuimarisha umoja kwa wale wafuasi wao. Suhail amechimuzwa katika mandhari haya kwamba ni mtu shujaa ambaye anaunga mkono juhudi za viongozi wao wanaoonewa katika mataifa yote pindi wanapodhulumiwa kura zao.

Pia katika mandhari ya Bagamoyo nyumbani kwa Sufian kumekuwa na matukio yasiyo ya kawaida na ya kutisha kwani Mzee Sufian anapigwa bila kumuona mtu anayempiga, kumbe aliyekuwa anampiga ni komandoo Takadir-Al-harabi wa kundi la Budha. Kundi hili la Budha lilikuwa bado linaendelea kumwandama mpinzani wao kwa sababu aliondoka na pete yao. Pete hiyo ilikuwa ndiyo kinga kwa serikali ya Budha. Kwa hivyo, Mzee Sufian amekuwa akisafiri sehemu mbalimbali akiwakimbia. Japo amekuwa akiwakimbia lakini wamekuwa wakimfuata kwa kumtumia komandoo Takadir ambaye ni mwanamume lakini amekuwa akijibadilisha na kuwa mwanamke akawa anajihusisha kimapenzi na Sufian bila Sufian kufahamu kuwa ni adui yake na ndiye anayempiga Mzee Sufian. Mwandishi anasema:

> Mwili wa Sufian ulizizima kwa hofu na uwoga kila alipokumbuka kuwa kumbe kule ufukweni hakuwa na msichana wa kawaida! Aliduwazwa zaidi na maswali lukuki kichwani mwake kuwa aliwezaje kukaa muda wote ule akikumbatiana na adui Bila ya kumgundua? (uk. 204)

Mandhari hii na matukio yasiyo ya kawaida yatishayo ya kihalisiamazingaombwe ya mwanamume kujibadilisha kuwa mwanamke yanatumiwa na mtunzi kuchimuza migogoro mbalimbali na hasa ya nchi zinazoendelea. Kwanza ni kuonyesha uwepo na mahusiko ya ulipizaji visasi unaochochewa na sababu nyingi mseto kama vile tofauti za kisiasa, mashindano kwenye utaoaji wa zabuni, udhaifu wa miundomsingi na mifumo ya kitaasisi, utegemezi mkubwa unaowekwa juu ya maono ya watu binafsi badala ya ukuzaji wa ruwaza, sera, mifumo, taratibu na taasisi kwa ajili ya maendeleo ya nchi. Ukosefu wa mambo haya unazifanya siasa za nchi za Afrika na zile zinazoendelea kufungika katika mduara wa ulipisaji visasi. Kwa mfano, japokuwa chama tawala huwa kinashinda na kuingia madarakani wakati mwingine kwa njia isiyo halali kabisa lakini bado wanachama wake watatumia rasilimali, fedha, rasilimali za ki binadamu na wakati mwingikuendelea kuwasakama wapinzani wao mpaka inafikia hatua wanaamua kukimbia nchi zao. Pamoja na kwamba wanazikimbia nchi zao lakini serikali haiishi kuwatafuta huko waliko waweze kuwaangamiza.

Mwandishi anachimuza ujumbe mwingine katika mandhari ya kituo cha polisi Kijitonyama tunaona matukio ya ajabu baada ya Suhail kufungwa kwa tuhuma za kusingiziwa kumuuwa Msigwa ambaye ni mwandishi wa habari wa gazeti la *Haki*. Tunaona katika mandhari yale ghafla Suhail anatoweka akiwa chini ya ulinzi bila hata askari kuona mahali alipopitia. Suhail alitumia pete ile ya Budha na ikamuwezesha kutoroka bila polisi kumuona. Baadaye askari mkuu wa kituo cha polisi akawaambia wasiendelee kumtafuta Suhail kwani kuna mchezo mchafu wa kisiasa unaendelea. Mkuu wa kituo cha polisi anasema:

> ..kuna vita ya kisiasa inaendelea nchini mwetu, kambi kadhaa za wasaka uraisi zimekwisha jidhihirisha waziwazi huku kila kambi ikiwa imejipanga vilivyo. Kuuwawa kwa huyo mwandishi wa habari ni kutokana na michuano hiyo, ni

> kwamba huyo marehemu alikuwa mshiriki wa mojawapo wa kambi hizo na inasemekana alitaka kutoa siri….(uk. 218).

Nukuu hii inatuonyesha wazi kwamba, kesi nyingi zilizokuwa zikiendelea hapo polisi japo zilikuwa ni katika matukio ya kimazingaombwe lakini baada ya upelelezi wanagundua kwamba kuna migogoro ya kisiasa inayoendelea pasipo hata wao polisi kujua. Ndivyo ilivyo hata katika nchi nyingi wakati wa kipindi cha uchaguzi kumekuwa na kesi nyingi zinazopelekwa polisi zinazohusiana na uchaguzi ili mradi watu waweze kuchafuana. Hizi ni hali zinazojitokeza kwa sababu ya ukosefu wa ukomavu wa kisiasa, ukosefu wa uwepo wa sera na ruwaza madhubuti, ukosefu au uwepo wa taasisi za kiserikali na kisiasa ambazo ni dhaifu na uegemezwaji mkubwa wa siasa katika mikono ya watu binafsi. Mandhari hii na matukio haya yaliyochanganyikana na uhalisiajabu na uhalisia ya kituo cha polisi yanatumiwa na mtunzi kuonyesha jinsi migogoro ya kisiasa inavyoleta shida katika mataifa yetu na hata kupelekea kufa kwa baadhi ya watu.

Pia tunakutana na mandhari ya hotelini kukiwa na matukio kadhaa yanatendeka. Katika mazingira haya anaonekana Joram Ndege akiingia ndani na kufanya kikao na vigogo wa serikali kuhusu maswala mbalimbali ya kisiasa na kujipongeza kwa mauaji ya Msigwa. Hii ni kutokana na kwamba viongozi hawa wa kisiasa waliamua kumuuwa Msigwa kwa sababu alikuwa akiandika uozo unaofanywa na viongozi mbalimbali serikalini katika gazeti la *Haki*. Mwandishi anawaonyesha jinsi viongozi hao walivyokuwepo katika kikao hicho kwa kusema:

> ….upande wa kulia wa Ibrahim waliketi watu watano; mhe. Hamad Humud (naibu waziri wa nishati na madini), mhe. Abdiroush Warriya (naibu waziri wa fedha) Moris Kungurume (mfanyaBiashara wa madini), na Charles Bikoraimana (mfanyaBiashara wa maswala ya usafirishaji majini)… Kamanda Katinda Kuya (mkuu wa polisi kanda maalumu), Joram Ndege (jambazi wa kutumainiwa) …..(uk. 235)

Mandhari na matukio yaliyokuwa yakiendelea katika hoteli hii yamechimuza dhamira ya hila za kisiasa zinazoendelezwa na watu wachache kwa manufaa yao ya ki binafsi. Kunaibuliwa pia dhamira za udhalimu na unyanyasaji unaowezeshwa au unaofadhiliwa

na viongozi mbalimbali katika mataifa ya Afrika. Kuna mawaziri mbalimbali wakishirikiana na jambazi mkubwa aliyeitwa Joram Ndege wanaopanga mipango mbalimbali ya kuwauwa wale wote wanaokuwa ama wanaoisumbua serikali ya kiimla au wanakuwa kikwazo katika utekelezaji wa miradi inayowanufaisha watu binafsi au makundi mahususi. Mmojawapo waa watu waliouwawa ni mwandishi mashuhuri wa gazeti la *Haki*. Jambo lingine linalochimuzwa ni kwamba, udhalimu, ufisadi na unyanyasaji unaofanywa na wanasiasa ni mtandao mkubwa unaojumuisha watu na maslahi ya ki binafsi ya aina nyingi. Kwa mfano biashara zisizo halali kutegemea ulinzi na ufadhili wa kisiasa, siasa kufadhiliwa na biashara haramu, uhamishaji wa fedha na faida kufadhiliwa na mitandao ya wauaji, ujambazi unanawirishwa kutokana na ufadhili wa kisiasa. Kwa jumla, mitandao ya kufadhiliana kwa njia zisizo halali ndiyo inayotawala nchi za ulimwengu wa tatu.

Msigwa aliuwawa kwa sababu ya kuandika maovu yanayofanywa na viongozi serikalini na mambo yanayohusu maisha yake binafsi. Ndivyo ilivyo kwa mataifa yetu ya Afrika tumeshuhudia wale waandishi wote wanaoandika habari kuhusu uozo unaofanywa na serikali wengine wameuawa, wengine wamemwagiwa tindikali usoni na wengine wamefungwa pasipo hatia. Mandhari hii inatuonyesha jinsi ambavyo polisi wanavyoshirikiana na utawala katika kujenga mtandao mkubwa sio tu wa kuwakandamiza na kuwauwa wananchi, bali pia wa kuendeleza, kufadhili na kuimarisha uporaji wa maliasili ya nchi, fedha za umma na malighafi nyingi zinazokusudiwa kunufaisha umma.

Hivi ndivyo hali ilivyo kwa mataifa ya Afrika, mitandao kama hii ya akina Joram inaakisi uhalisi ulioko barani Afrika ambapo japo siku zote polisi wako kwa ajili ya kutetea maslahi ya dola, lakini wanashirikishwa kwa njia changamano kutetea maslahi ya kitabaka na ki binafsi katika hali nyingi ambapo mwananchi hajumuishwi katika hesabu hii ya ulinzi. Polisi hawana kipaumbele kutetea wananchi ndio maana tunamuona mkuu wa polisi kanda maalum naye yupo katika hicho kikao hotelini pamoja muuwaji na mawaziri na wakuu wa mikoa. Katika mtandao huu wa ushirika, polisi,

wauwaji, wakuu wa mikoa, mawaziri na wafanyibiashara, wadhifa wa kuongoza nchi unadhibitiwa na genge katili linalojitambulisha kama viongozi. Mwandishi anakuza ujumbe kwa kuonyesha jinsi serikali, kwa kuzingizia kulinda usalama wa nchi, isivyo na huruma kwa waandishi wa habari na wapiga mbiu wengine, kwani imekuwa ni kawaida katika mataifa ya ulimwengu wa tatu waandishi wa habari kufa kupitia polisi.

Mwandishi vilevile anatuonyesha mandhari na matukio yaliyokuwa yakiendelea nyumbani kwa Suhail yalivyoweza kuchimuza ujumbe wa madhara ya usaliti katika mahusiano ya mapenzi. Wakati Suhail akiwa mgonjwa ghafla vikatokea vita kati ya jini Shekhia, Suhail, Takadiri na Mzee Sufian. Mzee Sufian akastaajabu baada ya kumuona Mzee Fungameza ambaye ndio baba yake Sharifa aliyekuwa mke wa Sharifa baada ya Suhail kushindwa kutimiza masharti akaamua kuoa Sharifa kwa shinikizo la wazazi wake. Mtunzi anatumia uhalisiamaziangaombwe kupitia mandhari hii kwa kumuonyesha mtu aliyekufa kumbe alikuwa anaendelea kuishi na akaja kufufuka tena ambaye ni Mzee Sufian kwani Mzee huyu anajitokeza ghfla nyumbani kwa Suhail na kuanza kumwita Mzee Fungameza na kuanza kuuelezea umati kwamba enzi alipokuwa hai duniani alimnyan’anya mke Fungameza ambaye alikuwa anaitwa Amanda na akazaa naye mtoto mmoja anayeitwa Shekhia. Naye Fungameza akasimuliwa mkasa wote kwamba alinyan’ganywa mke na Mzee wa Kiasia kwa ajili ya tamaa ya pesa ya mke wake japo alibahatika kuzaa naye mtoto mmoja anayeitwa Sharifa. Mwandishi anatuambia jinsi Mzee Sufian alivyoita kwa mshangao:

> “Bwana Fungameza!” Mzee Sufian aliita kwa mshangao wa hali ya juu na kuacha taharuki ya aina yake. “Sufian? Ni wewe ama naota?” Mzee Fungameza alihoji akiwa haamini. “Ndiye mimi kaka, najuta kwa yote niliyokufanyia….. nisamehe sana.” “Ama kweli malipo ni duniani ahela yaenda hesabu tu….leo umedhalilika mbele yangu. Yule mtu uliyenikasirisha, ukanidhalilisha na kujitapa kwamba hakuna atakayekuweza wewe, hatimaye umewezekana…”Mzee Fungameza alijibu….(uk. 279).

Baada ya mazungumzo hayo ikagundulika kwamba Shekhia na Sharifa ni ndugu japo Shekhia ni nusu jini kwa sababu mama yake alikuwa ni mtu ila baba yake Mzee Sufian alikuwa jini. Suhail baada ya kugundua alilia sana. Suhail anasema:

> “Mungu wangu! Ina maana Shekhia na Sharifa ni ndugu? Tena wa mama mmoja aliropoka Suhail Bila ya kutegemea, mara akaishiwa nguvu na kujikuta anaporoka juu ya kochi kama kiroba. Ni fedheha kubwa kushuhudia ndugu wawili wa mama mmoja kuwa ni wake wa mwanamume mmoja halafu mnakuja kugundua hilo mukiwa nyote ni wajawazito (uk. 280).

Mandhari hii pamoja na matukio haya yanatufundisha siku zote unapomfanyia mtu ubaya kumbuka na wewe utafanyiwa ubaya pia. Hapa, mtunzi anahakiki sifa, tabia na mienendo ya watu binafsi. Tukio hili linawafundisha wanawake au wasichana au vijana ambao wanatafuta pesa kwa njia isiyo ya halali kwa kuamua kuwasaliti wachumba zao hujiingiza katika mapenzi kwa wanaume wenye pesa ili waweze kuzitumia hizo pesa, kama ilivyokuwa kwa huyu mwanamke Amanda. Mandhari hii na matukio yote yaliyokuwa yakitendeka yanatupa ujumbe wa kutufundisha kwamba kila kitu umfanyiacho mwenzio hapa duniani malipo huwa yanaanzia hapa hapa duniani kwanza.

Mbinu ya uajinibishaji inajidhihirisha katika mandhari ya nyumbani kwa Suhail katika *Vita vya Mapenzi* anapokuja kugundua kuwa wameoana ndugu wawili na wote wanaujauzito wake. Suhail alifika hatua ya kusababisha dada kuuwana. Siri inapokuja kugundulika inamstamjabisha kila mtu aliyekuwepo katika mandhari hiyo. Kwani mama yake Suhail alikuwa ni mama mmoja na Amanda aliyekuwa mke wa Fungameza aliyenyang’anywa na Mzee wa kiasia yaani Mzee Sufiani. Kwa hiyo mama yake Suhail alikuwa ni mama mdogo wa Shekhia na Sharifa. Hili lilikuwa ni tukio la kusikitisha. Mwandishi anasema:

> Mshikeshike mwingine, kumbe Amanda ambaye ni mama yao na Shekhia na Sharifa pia ni pacha na mama Suhail, hivyo Suhail ni ndugu yao kabisa na akina Shekhia…. Hakika ilikuwa ni siku ya fadhaa (uk 284).

Mandhari na matukio haya yanabeba dhamira ya kwamba ni vizuri kabla hamjaanza mahusiano ya mapenzi ni vizuri mkafahamiana vizuri pande zote mbili ili msije mkaoana kumbe ninyi ni ndugu wa damu kabisa. Kama ilivyokuwa kwa Suhail, Amanda, mama yake Suhail, Sharifa, Shekhia na Mzee Fungameza. Maswala kama

haya ya kuoana ndugu katika jamii zetu mara nyingi huleta mikosi na hata kupelekea wengine kufa au kuzaa watoto walemavu katika jamii nyingi za kiafrika.

Mwandishi anatuonyesha tena mandhari halisi ya kwenye basi na jinsi Suhail alivyoathirika na utandawazi. Katika mandhari haya, tunaona athari za utandawazi kwani, Suhail akiwa anaelekea Tabora yuko *Bize* na *ipad* na visikilizio kaweka masikioni akifungulia wimbo kwa sauti mpaka anawakera abiria wenzake pasipo yeye mwenyewe kufahamu, huku akiwa anaimba kwa sauti akifuatilia huo wimbo wa mwanamuziki mmoja wa kimarekani. Tukio hili katika mandhari haya linachimuza maudhui ya athari za utandawazi kwa vijana mbalimbali wa nchi za Afrika. Vijana hawa huwa wanajisahau hata wakiwa njiani au kwenye mabasi wakiwa wameweka visikilizio masikioni na wakiimba kwa sauti nyimbo za wanamziki wa kimarekani na kuvaa nguo zinazofanana na wanamziki hao. Vijana hawa hujisahau kwamba ndani ya gari wanawasumbua abiria wenzao na hata barabarani wanawasumbua wapita njia wenzao. Kwa hiyo, Suhail ameathiriwa na utamaduni wa kizungu mpaka anawasumbua wenziwe katika gari kwa kuwawekea mziki wa kizungu kwa sauti kubwa. Japo utandawazi huu pia kwa wale ambao wameweza kuutumia umelata manufaa makubwa sana, kwa sababu hizo tablet zimeleta pia maendeleo kwa kurahisisha kazi nyingi za kitaaluma na kujua mambo mengi yanayoendelea duniani.

Mandhari ya nyumbani kwa Suhail akiwa mgonjwa sana baada ya kuzidiwa na utawala wa Budha na hiyo pete ikawa haina nguvu tena. Suhail alikuwa anaumwa ugonjwa usioleweka madaktari wakampima lakini hawakujua tatizo ni nini. Ndipo Ustadhi Chaullah akatumwa na Mzee Atrash wa Bagamoyo kumwambia aseme ukweli aache kusema uongo kwani alikuwa bado anaendelea kuongea uongo. Ustadhi Chaullah anasema:

> ..Mzee anasema alikukanya kuhusu maswala ya tamaa na uongo …..mbona hujajirekeBisha? Kwa nini umeendelea kumdanganya mkeo Sharifa kwa kila jambo? Na kwa nini mpaka leo licha ya matatizo kukufika shingoni bado hujawaeleza ukweli wazazi wako? (uk 263)

Japo Suhail amekuwa mbishi kuwaeleza wazazi wake lakini ikabidi aeleze ili aweze kupona lakini hakuweza kupona baada ya kugundua kwamba Shekhia na Sharifa na mama yake ni ndugu.

Aidha, jamii inayozungumziwa katika riwaya ya *Vita vya Mapenzi* inashadidiwa kwa uchache na maumbile ya kimazingira (kiangahewa) yenye hali ya hewa ya Kitropiki ambako kuna mvua za mara kwa mara, upepo mkali, vumbi na ngurumo za radi kama sehemu ya hali ya hewa. Mwingizi katika *Vita vya Mapenzi* anawachorea wasomaji wake mandhari ya "nyumba ya mswahili wa pwani" akitupa mfano wa nyumba ya Mzee Atrash, ya aina ya *Msumbiji type*, yenye kupigwa lipu na matofali ya kuchoma. Mazingira yanapambwa na "Miti mirefu ya Minazi, Mitende, Mipapai, Migomba", iliyoonekana kupandwa kiustadi kuizunguuka nyumba hiyo ilipendeza kimuonekano wa eneo lake lenye kijani kibichi cha "miti midogomidogo kama vile Mikomanga, Mipera, Michunga" (uk 44). Hii ni nyumba ya mganga wa pwani mwenye wateja mbalimbali maarufu wanaomtembelea. Ujengaji wa mandhari ya miti na shamba unalandana na shughuli za uganga wa jadi. Mbinu ya kukuza safari ya kutoka katika uhalisia na kumuingiza msomaji katika dunia ya umazingaombwe inawakilishwa na mwendo. Suhail anasafirishwa na kuandaliwa kisaikolojia kuipokea dunia ya ujiniuchawi kwa kuelezwa hadhiti ndefu ya historia ya maisha ya Mzee Sufiani na binti yake Shekhia. Historia hiyo inafumbatwa na usiri na unyeti unaficha hila uongo ulaghai na ukatili. Mandhari ya mganga Atrash huko Mlingotini Bagamoyo inatumika kujenga picha ya mandhari nyingine ya ujijini. Mji wa kijini unaelezwa na mganga kingano:

> Miaka ya nyuma kidogo palikuwa ni Himaya huko chini ya bahari zikiendesha tawala zao. Himaya moja kubwa sana ikiitwa *Budha*, himaya hiyo ilikuwa na utajiri na ulinzi mkali kuliko zote huko baharini, hatamu za utawala wao zilikuwa zikiwaniwa kwa udi na uvumba kama iwavyo huku duniani kwetu ifikapo kipindi cha mchakato wa uchaguzi.(uk 52).

Mandhari ya mji wa kimazingaombwe wa baharini unawekwa wazi kwa wasomaji wakiwa tayari wamekwishapitishwa katika mazingira ya kiuhalisia ya mji wa mganga. Dhamira ya mtunzi ni kulandanisha vita vya uongozi kuwa havina mipaka. Popote pale penye rasilimali kunakuwa na ushawishi wa kugombania uhodhi au kuwa na sauti ya

umiliki wa rasilimali hizo. Mwandishi kwa kusema kuwa hatamu za uongozi zinagombewa huko baharini katika miji ya majini inaendana sambamba na “duniani kwetu” ni mbinu ya wazi ya mwandishi ya kuvunja mipaka ya dunia ya uhalisia na ile ya umazingaombwe. Kwa hiyo mazingira ya shamba na miti yanatajirisha taaluma ya tiba au ulozo wa kimitishamba. Mandhari ya matukio haya yanachimuza ujumbe wa kuwa tamaa ya kupata pesa kwa njia isiyo halali ni mbaya sana kwani kilichomponza Suhail mpaka kuwa katika hali hiyo ni tamaa ya pesa. Mpaka akajiingiza katika utawala wa majini na wachawi lakini mwisho wa yote naye anakufa na pesa ameziacha. Kwa hiyo ujumbe huu unatukumbusha kwamba kila uovu unaotenda hapa duniani hukumu yake huanzia hapa hapa duniani na baadae ahera.

### 3.4 Mandhari na Matukio ya Kijiniuchawi na Ushirikina Yalivyochimuza Dhamira na Maudhui katika Riwaya ya *Mzimu wa Waufi*

*Mzimu wa Waufi* ni riwaya ambayo inasimulia visa na vituko mbalimbali vinavyohusiana na majini, uchawi na ushirikina. Kwa kifupi, katika riwaya hii mwandishi anatumia mtindo au mbinu za kiajabuajabu katika kuchimuza mambo mbalimbali ambayo yapo katika jamii zetu. Riwaya hii inawazungumzia kwa kiasi kikubwa wahusika wakuu wawili japo kuna wengine ambao tutawajadili katika sura ya nne. Mwandishi anatuonyesha vita vikubwa baina ya mahasimu wawili ambao wanatoka katika utawala tofauti wa kijiniuchawi. Mhusika wa kwanza ni Hunudu ambaye anatoka katika utawala wa kiimla na mhusika wa pili ni Masumbuko ambaye kuzaliwa kwake, kulikuwa ni kwa kutatanisha baada ya mama yake kumzaa kwa kuiba mimba ya mke mwenziye iliyokuwa ya miezi sita kiuchawi na kiushirikina kutokana na kwamba, mama huyo yeye ndiye alikuwa Bibi mkubwa lakini hakubahatika kupata mtoto. Ndipo mumewe akaamua kuoa mke wa pili. Bibi mdogo huyu akabahatika kupata mimba na mimba yake ilipofikisha miezi sita, Bibi mkubwa akaiiba kiuchawi na ile mimba ikaamia kwa Bibi mkubwa. Bibi mkubwa huyu akajifungua mtoto ambaye ndio Masumbuko.

Mtunzi anatuambia pamoja na kumzaa Masumbuko, mama huyu alipewa masharti ya kwamba, Masumbuko akishazaliwa ahakikishe anamtoa kafara kwa mizimu hiyo ndipo

aendelee kuzaa watoto wengine, lakini yeye hakufanya hivyo. Kwa hivyo, mizimu ya Waufi ndiyo ikaanza kumtesa na kumsumbua Masumbuko, kila siku alikuwa anatokewa na mfuasi wa utawala wa mizimu ya Waufi aliyekuwa anaitwa Hunudu ambaye ni jini. Mara alikuwa anambadilisha Masumbuko anakuwa mwanamke na anaandaliwa kwa ajili ya kuolewa, siku nyingine anageuzwa kuwa ng’ombe anaandaliwa kwa ajili ya kuchinjwa. Matukio yote haya yalikuwa yanamtokea akiwa ndotoni.

Hunudu alikuwa ndiye kiongozi wa utawala wa Waufi na alikuwa anapambana na utawala wa Waswezi ambao walikuwa ni watu wenye huruma na walikuwa si wakorofi lakini walikuwa wanaonewa sana na utawala wa Waufi. Waufi waliwaua baadhi ya watu wa mizimu ya Waswezi maana walikuwa na uwezo wa kujibadilisha kuwa polisi wakati mwingine, kuwa madaktari, kuwa wachungaji, na kuwa mashehe, kiasi kwamba utawala huu uliwaletea shida sana kwa kila sekta. Waufi walitumia nguvu zao kuwanyanyasa wananchi wasio na hatia na hasa Masumbuko aliteswa sana na Waufi kwani kuna matukio mengi zaidi ya haya tuliyosimuliwa aliyoyapitia. Hatimaye inagunduliwa ni kwa nini Masumbuko anateswa sana na Waufi. Kumbe tatizo lilikuwa ni kwamba mama yake asilia alikuwa ni mtoto wa chifu mkuu wa mizimu na ushirikina katika utawala wa Waswezi, japo yeye alikuwa hajui lakini alipojua aliweza kurejea kwa mizimu yao. Ndipo pakawa na ugomvi mkubwa kati ya Mzimu wa Waufi na mzimu wa Waswezi. Waufi walikuwa wanamtaka Masumbuko kwa sababu mama yake hakumtoa kafara, na Waswezi walikuwa wanamtaka kwa sababu asili yake alikuwa ni Mswezi.

Kupitia mandhari mbalimbali unatokea ugomvi mkubwa kati ya hili jini lililokuwa linaitwa Hunudu na Masumbuko, matukio mbalimbali ya kutisha na ya kuogofya ya kijiniuchawi na ushirikina yameonyeshwa na kuchimuza maudhui mbalimbali yenye jumbe mbalimbali zenye kukosoa na kuelimisha jamii kuhusu maswala ya kisiasa, kiuchumi, utandawazi, mahusiano ya kisaikolojia na maswala ya kiutamaduni. Mtunzi anaeleimisha jamii kwa kutumia mtindo huu wa kijiniuchawi na ushirikina. Mtunzi anaonyesha mwisho wa utawala huu wa Waufi unaangamizwa kabisa na utawala wa Waswezi. Japo Waufi wenyewe walijiona kwamba hakuna mtu anayeweza zaidi yao. Na

baada ya kuteketezwa utawala huu wa Waufi ndipo Masumbuko anachaguliwa kuwa chifu wa Waswezi.

Katika riwaya ya *Mzimu wa Waufi*, kuna upanuaji wa mawanda ya kiusimulizi ambapo tunapata pia mandhari ya kinelbelini na matukio mbalimbali yaliyokuwa yakiendelea. Riwaya hii mpya ya *Mzimu wa Waufi* haina mipaka ya wazi ya kiusimulizi kama ilivyo riwaya ya *Vita vya Mapenzi*. Katika riwaya hii mtunzi ameweza kuhusisha ulimwengu halisi, ulimwengu dhanifu na ulimwengu wa kinjozi na mipaka ya maingiliano kati ya aina hizo tofauti za ulimwengu yamevunjwa. Vilevile, hali hii imeweza kutokea pale hali ya usimulizi inaachwa na kupembezwa na kwa njia hiyo, kuwezesha ukunjufu wa maelezo na masimulizi ya riwaya au kumwezesha mhusika kujitosa kwenye tathmini ya kisaikolojia (hasa kupitia ndotoni).

Riwaya ya *Mzimu wa Waufi* ni riwaya ambayo ina muundo tata usiokuwa katika mtiririko maalum wa kisimulizi hasa kwa mintarafu ya mpito wa wakati na matukio kwani visa na matukio yake vinachanganyikana na kwa hivyo kuibua ukuaji mseto, usimulizi wa kwenda mbele na kurudi nyuma, usimulizi wa kuwa katika ulimwengu razini na kisha kuingia katika ulimwengu wa kinjozi. Utunzi wa aina hii unaweza kukisiwa ni wa kijarabati ni utunzi unaotokana na ukweli kwamba, ni riwaya ya kimajaribio, ambapo inajaribishwa miundo ya kiutunzi, mitindo ya kimasimulizi na pia, miongoni mwa tabia za riwaya ya kimajaribio ni uwepo wa muundo rejeshi.

Mwanzoni mwa riwaya Mwandishi anamwingiza msomaji katika masimulizi na matukio yanayojibainisha katika mandhari ya kinjozi kupitia kwa muhusika Masumbuko akiwa baharini ambako kuna mapango makubwa na moto mkali unaowachoma na kuwatesa watu mbalimbali wakiwemo vijana wengi zaidi. Masumbuko anashuhudia matukio ya kutisha na ya kuogopesha yakifanyika katika sehemu hiyo. Masumbuko anashuhudia watu wakichomwa katika moto mkali kama mikate au ndafu ilhali wenyewe wakiwa bado hai na wengine wakipigiliwa misumari katikati ya vichwa vyao huku ubongo na damu vikiruka juu na kutapakaa angani.

Masumbuko anapelekwa sehemu nyinginyingi na kijana aitwaye Hunudu ambaye ndiye aliyekuwa mkuu wa dini hiyo ya Waufi na kumwonyesha sehemu nyingine, ambako alimkuta kijana mmoja anakatwakatwa kama kuku na damu yake inang'ang'aniwa na wachawi kwa ajili ya kunywewa. Hunudu naye anakunywa hizo damu na kutikisa kichwa kuwa ni tamu halafu anampa na Msumbuko, lakini Masumbuko akawa anakataa, kumbe mambo haya yote yaliyokuwa yanaendelea baharini Masumbuko alikuwa anaota ndoto usingizini halafu anashtuka. Mwandishi anasema:

> Masumbuko akapiga kelele za kukataa huku akitumia nguvu zake zote kupinga kunyweshwa damu ya mtu. *"AAAGGGGHHAHHHGGH."*Kukurukakara hiyo sambamba na kelele za kupinga kunyweshwa damu za mtu ndizo ambazo zilimshtua Masumbuko toka usingizini! Haraka akainuka na kuketi huku akitweta. Akageuka huku na kule, akiwa bado anahema juujuu. Akajiona yupo chumbani mwake juu ya kitanda, ndipo akagundua kwamba alikuwa yupo ndotoni. Akajaribu kujitikisa kichwa na kupikicha macho ili aone kama angali ndotoni au amekwisha amka… Ni ndoto ya ajabu sana ambayo Masumbuko hakuwahi kuiota hata siku moja (uk. 4)

Ndoto hii ilimfanya Masumbuko ashtuke kutoka usingizini na kuanza kumsimulia mkewe. Mkewe akamwambia kesho wataenda kwa mchungaji japo Masumbuko hakutaka kusikia habari za mchungaji. Mtunzi anatumia tukio hili la kiajabu kupitia katika mandhari ya ndoto kuchimuza maudhui ya athari za dini za kigeni zilivyoathiri utamaduni wetu na zilivyoleta migogoro mbalimbali katika jamii. Kupitia Masumbuko na mkewe tunaona kutokuafikiana kwa sababu ya kumwita mchungaji aje amuombee Masumbuko kwa kuwa Masumbuko ni Mwislamu hakupenda kuombewa na mchungaji.

Swala la dini limeleta migogoro mingi sana katika jamii na hata katika maswala ya ndoa watu wamekuwa wakipendana sana lakini kwa kuwa na tofauti za kidini wamekuwa hawaoani. Swala hili la dini linaweza pia kuhusishwa na ung'ang'aniaji imani na tamaduni za kutoka nje kabla ya kuzielewa na kuzitathmini kwa kina. Tabia za aina hii zinaibua mivutano na mikwaruzano iliyo na madhara mabaya. Kwani watu hujitumbukiza katika dini fulani bila hata kuzielewa dini hizo na hatimaye wanakuwa vikwazo kwa watu wengine. Aidha katika maswala haya ya dini kunaibuka pia mijadala

kuhusiana na imani, tamaduni, mionoulimwengu na athari zao katika kushawishi, kuelekeza au kudhibiti mahusiano kati ya watu katika jamii.

Pengine swali analohitaji kujiuliza msomaji ni, kwa nini mtunzi ameweka kipaumbele, msisitizo na uangaziaji mkubwa kwenye mateso, ukatili na ufu katika kusimulia mahusiano ya binadamu katika jamii. Je mambo haya yote yanayomtokea Masumbuko katika ndoto—uwepo wa mapango ya kutisha, kuchomwa kwa watu katika mioto mikali na bado wanasalia hai, watu kupigiliwa misumari katikati ya vichwa huku ubongo na damu zikiruka juu na kutapakaa angani, kunywewa kwa damu ya binadamu—mambo haya yanaashiria nini? Inavyoelekea ni kwamba, mtunzi anasimulia matukio katika riwaya hii kwa misingi ya mizungu (*occult*), yaani kutaka kujenga mwafaka, uelewa na ufahamu wa mambo yaliyofichwa, siri za maisha na ufumbuzi wa mafumbo ya maisha.

Aidha tunaweza kusema hapana shaka kwamba mtunzi anatafakari mafumbo na miujiza ya maisha (*mystical*), mambo yaliyo nje ya uelewa wa kilimwengu yanayohusianishwa na imani za kiroho, kishetani, kimalaika au hata kimajini (*magical powers, practices, or phenomena*). Kuna kauli na hoja zinazotolewa kwamba kujihusisha na maswala ya mafumbo na miujiza ya maisha kunadhamiria kujenga ufahamu na mwafaka wa uelewa ulioko kati ya ithibati za sayansi asilia na imani za kidini na kitamaduni. Hili ni jambo linalodhihirika inapozingatiwa kwamba, pendekezo la kwanza linalotolewa kuifasiri ndoto ya Masumbuko linahusiana na dini ndipo anaitwa mchungaji. Inawezekana kuhoji kwamba ndoto anazozisawiri mtunzi zinazohusiana na mauaji katika riwaya ya *Mzimu wa Waufi* na zinaweza kufasiriwa kuwa ni jaribio la kutaka kung'oa, kuondokana au kuachana na vipengele vya maisha visivyopendeza au visivyotakikana. Kuna mambo mengi ambayo Masumbuko anataka kuondokana nayo lakini kabla ya hilo kuwezekana mambo hayo yanatanza maisha na mahusiano yake na jamii. Huu ni uhalisia unaowatokea binadamu wote.

Kwa upande mwingine, ndoto za Masumbuko zinazohusu mauaji, na kuna mauji ya aina nyingi, ndoto hizo zinaweza kuashiria ghadhabu na hasira kali au hamaki iliyobanwa na

kunyamazishwa dhidi ya mtu au kitu kama vile kutamatisha mauhusiano ya aina fulani. Hivyo hivyo, ni dhahiri kwamba ndoto zinazojitokeza katika riwaya hii zinahusisha visu na mauji kwa jumla na kwa misingi hiyo zinaweza kufasiriwa kuwa na maana kwamba mauaji hayo ya kindotoni yanaashiria mpito, japo ni mpito wa mashaka, kutoka awamu moja hadi nyingine kama inavyoakisiwa katika maisha ya Masumbuko. Pale ambapo ndoto zinahusu watu kukatwakatwa, inawezekana ndoto hizo zinaashiria haja au hamu ya kukata kitu, kipengele cha maisha kinacholeta athari hasi au pia visu katika ndoto za Masumbuko ni ishara ya kutaka kuhitimisha/kukata mahusiano hasi na makundi fulani. Pale ambapo ndoto za Masumbuko zinahusiana na damu zinaweza kuashiria kukatizwa au kutibuliwa kwa nyenzo za kimsingi za maisha. Haya kwa hivyo ni maswala ya kisaikolojia anayoyawasilisha mtunzi katika riwaya hii.

Mtunzi anaendelea kutuonyesha tukio lingine la kiajabu katika mandhari ya kituo cha daladala au matatu maeneo ya Kariakoo Jijini Dar es salaam. Tunamuona Masumbuko akiwa ametoka kumsimulia Mzee Kishindo kuhusu matukio mbalimbali anayokumbana nayo kupitia ndoto anazokuwa anaota kuhusu dini ya Waufi wanaojikita na maswala ya ushirikina na uchawi. Ndipo akiwa katika kituo cha daladala ghafla gari linasimama na kumuita apande ndani ya gari na baada ya kumuangalia dereva anaona ni kama vile hamfahamu. Dereva huyo alikuwa ni mwanamke mrembo akajaribu kujiuliza ni wapi aliwahi kumuona lakini hakupata jibu lakini yule mwanamke mrembo anamfahamu Masumbuko vizuri na kazi anayofanya. Ndipo Masumbuko akapanda gari. Akiwa ndani ya gari akageuka nyuma ya kiti cha gari akashangaa kumuona Hunudu ambaye ni mfuasi wa dini ya Waufi na alizoea kumuona ndotoni mwili wote unakufa ganzi. Mwandishi anasema:

> Masumbuko alizidi kuchanganyikiwa kuona sasa yule kijana ambaye huwa anamsumbua usingizini kwenye ndoto kwa kujisifia kuwa ni kiongozi wa dini ya Waufi, hatimaye leo amekutana naye ana kwa ana akiwa ni yuleyule anayemuona, na kumtokea ndotoni! Kufikia hapo sasa akaamini kuwa zile ndoto hazikuwa za kawaida, bali zilikuwa na jambo zito nyuma yake…na ndipo alipoanza kuyakumbuka maneno ya Mzee Kishindo (uk 26)

Hunudu akamtahadharisha Masumbuko aache tabia ya kuendelea kutoa siri za Waufi na atimize masharti aliyopewa ya kutoa kafara mtoto wake wakiwa ndani ya gari. Kupitia mandhari na matukio haya ya uhalisia na ndoto kuchanganyikana, mwandishi anatuonyesha jinsi utawala huu wa Waufi ulivyokuwa ni wa kinyonyaji na wa kidhalimu. Utawala huu ulikuwa unawatesa watu hata wasipokuwa na hatia kwa kutaka mambo yanayotendeka katika utawala kutoelezwa kwa watu na ibaki kuwa siri ya utawala huu dhalimu hata kama unanyanyasa watu. Ndiyo maana Masumbuko alikuwa anafuatiliwa popote pale atakapokuwa anatoa siri ya Waufi anatishiwa. Katika hali hizi, mtunzi anachimuza ujumbe ambao unaonyesha jinsi serikali au tawala mbalimbali na viongozi wake katika mataifa yanayoendelea wanavyonyanyasa vyama vya upinzani na wananchi pindi wanapotoa siri za serikali kwa yale maovu yanayofanywa huko serikalini. Viongozi wa aina hii wanaoeleza mambo yanayotendeka serikalini yaliyo maovu huwa wanateswa na hata wakati mwingine huuliwa na viongozi wao wakuu.

Halikadhalika, mandhari haya yanaendelea kutuonyesha jinsi Waafrika wengi wanapotaka kuwa matajiri au wanapotaka kutatua baadhi ya matatizo hutumia njia isiyo halali, huangamiza familia zao ili wawe matajiri au waweze kutatua matatizo yao hata kwa kuwauwa watoto wao wanaowapenda au watoto wao wa kwanza. Hili limejitokeza kwa Hunudu kumtaka Masumbuko amtoe kafala mtoto wake wa kwanza. Wengine pia husababisha ajali mbalimbali za magari katika kuhakikisha kupitia maiti zile wanapata utajiri mkubwa kama ilivyokuwa kwa Mzee Sufian katika riwaya *Vita Vya Mapenzi* anawauwa wenziwe kwenye basi hii yote ni kwa ajili kubaki na kuendelea kuwa tajiri

Tukio la ajabu linatokea nyumbani kwa Masumbuko baada ya maji kumfika shingoni wakati mke wake anambembeleza akamwite Mchungaji aje amuombee na hatimaye, Masumbuko anakubali kuombewa na mchungaji. Na baada ya mchungaji kuja akamuomba mke wa Masumbuko atoke nje ndio waweze kuongea. Kilichotokea pale katika mazungumzo kati ya mchungaji na Masumbuko, Masumbuko hakuamini kuona mchungaji akimwambia kwamba, anachotakiwa ni kuwatii Waufi masharti yote

aliyopewa asipofanya hivyo Waufi watamuua kwani hata yeye mchungaji ni mfuasi wa dini ya Waufi. Masumbuko anasema:

> "Mchungaji sikuelewi kabisa unachomaanisha!" Utanielewa tu, iko hivi; mimi pia ni mfuasi wa Waufi…na ukiendelea kujidanganya kutukwepa utaangamia, acha kabisa kutoa siri zetu kwa mkeo na kwenye vijiwe vya kipuuzi, hakuna atakayekusaidia huko!" Masumbuko hakuyaamini maneno yale aliyokuwa akiyasikia kutoka katika kinywa cha Mchungaji, Mtumishi wa Mungu anayeaminika sana katika jamii (uk. 32)

Tukio hili katika mandhari hii linachimuza jumbe mchanganyiko kuhusiana na swala la muonekano na uhalisi, watu wanavyoonekana na wanavyodai kuwa na ukweli wa walivyo. Kwa mfano, ni kweli kwamba katika jamii zetu kuna watu kama vile wachungaji ambao sio watumishi wa Mungu ila ni watu ambao hutumia nguvu za uchawi pia na majini katika shughuli zao mbalimbali kwa kutumia mwamvuli wa uchungaji na kumbe ni watumishi wa wachawi na majini katika utendaji kazi wao. Kwa hivyo jamii inapaswa kuwa makini ili kutambua mambo, kubainisha na kutafakari juu ya taswira za nje na uhalisi wa ndani, kwa mfano si kila mchungaji anaweza akawa ni mtu mwaminifu na anayemtegemea Mungu, wengine wanatumia mwamvuli wa uchungaji kujipatia pesa na wengine kuficha maovu yao.

Mwandishi anaendelea kutuonyesha tukio hili hili linalofanana na la mchungaji katika mandhari ya hospitali pale ambapo Shehe Mwinigoha kaja na Mzee Kikoko kwa ajili ya kumsomea kisomo Masumbuko. Shehe huyu cha ajabu wakati wanazungumza na Masumbuko, shehe Mwinigoha bado anaendelea kumsisitiza kama mchungaji kuwa hatakiwi kutoa siri za Waufi. Shehe anasema:

> Tulia kijana, unataka kufanya nini sasa?""Sheikh, wanamuonea bure tu mke wangu jamani". Yote umeyataka wewe!" "Mimi tena? Kivipi Sheikh?" "Kama ungetunza siri za Waufi unadhani yangefika huku? Yaani nakwambia na hata hivyo una bahati haki ya mungu umemkuta Hunudu kipindi hiki ametulia vinginevyo saa hizi angeshakutia kilema wewe!"*Laahaulah!* Masumbuko alishtuka sana akaanza kutetemeka, hakuamini kabisa maneno yale kama yanatoka katika kinywa cha Sheikh yule, inaonesha Sheikh huyu anajua kila kitu kuhusu dini ya Waufi (uk 46)

Masumbuko anaendelea kumuuliza shehe Mwinigoha kama na yeye ni mfuasi wa dini ya Waufi. Shehe Mwinigoha akasema yeye ni mfuasi wa yule pale karibu na mlangoni. Masumbuko anasimama kumuangalia akakuta ni Hunudu amevaa nguo za kidaktari. Kwa kweli anachanganyikiwa kwa sababu Hunudu ni jini na huwa anamuona katika ndoto akajiuliza amefikaje hospitali. Tukio hili katika mandhari hii linachimuza ujumbe wa kwamba, sio mashehe wote ni wafuasi wa Mtume Muhamad wengine wana majini ya kuwatesa watu na wanatumia nguvu za kichawi na kishirikina kutekeleza hayo. Kwa hivyo, jamii inatakiwa kujihadhari. Vilevile kupitia shehe na mchungaji mwandishi anachimuza pia ujumbe wa jinsi baadhi ya viongozi walivyo wanafiki serikalini. Wanajifanya ni watu ambao wapo kwa ajili ya kusadia wananchi lakini wanajineemesha wenyewe kwa kuishi maisha ya kifahari na watoto wao kusomeshwa shule nzuri na wenyewe pia kutibiwa katika hospitali nzuri wakati wananchi wao wanatibiwa katika hospital zisizo na dawa na zisizo na madakitari wazuri na watoto wao wanasoma shule zisizo na madawati ambazo ni za serikali. Viongozi hawa wanawasahau wananchi ambao waliapa watawatumikia. Katika hali hizi, dini inawasilishwa kama vazi, gubi la kugubika ukweli.

Katika mandhari ya bafuni nyumbani kwa Masumbuko akiwa anaoga, anakumbana na tukio la ajabu baada ya kujikuta anapaka sabuni mwili mzima huku akiwa amefumba macho na anapofungua macho, anajikuta yuko kwenye bafu zuri la watu matajiri sana na anapoangalia sehemu zake za siri anakuta zimebadilika na kuwa za kike. Ndipo Masumbuko anaanza kuogopa sana na ghafla, mtu anampigia hodi na kumwambia mbona anachelewa akaangalia taulo lake hakuliona badala yake anaona chupi ya kike na kanga nyepesi akachukua akavaa. Baada ya kuvaa akatoka bafuni ghafla akakutana na mwanamke aliyekuwa anamuita kwa jina la Shamsa badala ya jina lake la Masumbuko. Baada ya hapo Masumbuko anaingizwa kwenye chumba kizuri chenye vitu vya thamani sana. Mtunzi anasema;

> … alipigwa na butwaa isiyosemeka. Macho yake yaliona bafu tofauti na lile aliloingia kuoga! Aliona yupo katika bafu zuri na la kisasa lenye kila dalili ya kuwa ni la mtu mwenye uwezo mkubwa wa kifedha. Masumbuko

> alichanganyikiwa sana, akawa hajitambui yupo wapi, akaanza kuogopa. Alipojiangalia vizuri mwilini mwake, akajigundua kuwa amebadilika, na hakuwa Masumbuko yule halisi…maana sasa ana maumBile ya kike (uk 59).

Mwandishi anatumia mandhari haya yaliyobeba matukio ya kijiniuchawi kuchimuza dhamira ya jinsi viongozi wanavyojineemesha kwa kuishi katika majumba mazuri ya kifahari wakati wananchi wao wanaishi katika maisha magumu tena wanatumia mabafu ambayo yako nusu hata akioga baadhi ya mwili huonekana. Kwa hiyo, utawala wa Waufi ni utawala ambao unawakandamiza wananchi wake ndio maana watu kama akina Hunudu wanaishi maisha ya raha kwa kuwatesa wenzao. Pia mandhari hii inachimuza ujumbe wa jinsi viongozi walivyo makatili yaani ukiwa msumbufu, ukifanya mambo yaliyo tofauti na utawala, utawala uliopo madarakani watahakikisha wanakufanyia kitu kibaya ambacho kitakufedhehesha mfano kukamata hadharani na kukupeleka magereza au polisi. Kwani kitendo Waufi walichomfanyia Masumbuko hakikuwa kizuri cha kumbadilisha maumbile yake kutoka katika maumbile ya kiume kuwa ya kike na kuandaliwa kwenda kuolewa wakati yeye anajiona kabisa ni mwanamume kwa sababu ametoa siri za waufi, huu ni udhalilishaji.

Hali kadhalika mwandishi ametumia lugha ya picha kwa kumuonyesha Masumbuko anavyobadilika maumbile kutoka katika maumbile ya kiume na kuwa ya kike kwa kuchimuza dhamira ya jinsi viongozi wanavyokuwa wanafiki kwani, kabla hawajapata madaraka wengi wao huwa ni watu wenye hali ngumu sana lakini wakipata madaraka hujibadilisha kabisa na kuwa karibu na viongozi wenzao na kuwasahau kabisa marafiki zao waliokuwa wanaishi nao katika hali ngumu ya maisha kwa kujiona wenyewe ni wa thamani hawafanani nao. Mwandishi anaendelea kutuonyesha mandhari ya nyumbani kwa Masumbuko ambako matukio yanaendelea baada ya Masumbuko kupotea alipokuwa anaoga bafuni kimajini. Ndipo Mzee Kikoko ambaye ndiye baba yake Masumbuko anaamua kumpiga mkwewe kwa kumuita mchawi na ndiye aliyesabaBisha mwanaye kupotea. Mzee Jabu anasema:

> …pili umefanya makosa kumpiga makofi huyo Binti hiyo ni kesi endapo kama ingefikishwa mahakamani ingeweza kukuletea dhahama kubwa sana!" Maneno yale yalimuingia sana Mzee Kikoko, akajuta ndani ya nafsi yake (uk 71).

Kupitia tukio hili tunapata ujumbe kwamba si vizuri wazazi kuingilia ndoa za watoto wao hata kama wameoana dini tofauti hayo ni mapenzi yao. Mzee Kikoko amejenga chuki tangu siku nyingi baada ya mwanae Masumbuko kumuoa Judith ambaye ni mkristo. Kwa hiyo, alikuwa hampendi hata kabla Masumbuko hajawa na majini.Vilevile mwandishi anaendelea kutuonyesha mandhari ya nyumbani kwa Masumbuko kupitia matukio mbalimbali. Masumbuko alikuwa anaishi sehemu moja Buguruni akiwa amepanga nyumba ambazo wanaishi watu wenye hali duni kidogo ya maisha. Nyumba ambayo wapangaji wote walikuwa wanatumia choo na bafu moja. Na hapo nyumbani kwa Masumbuko kulikuwa na ugomvi kati ya Mzee Kikoko na mama mwenye nyumba baada ya Masumbuko kupotea kimazingaombwe akiwa anaoga bafuni. Kupitia matusi ambayo Mzee Kikoko alikuwa anamtukana mama mwenye nyumba anayoishi Masumbuko ni dhahiri, mandhari ya maisha walikuwa wanaishi akina Masumbuko yalikuwa ni ya watu maskini. Mzee Kikoko anatoa kauli hizo mbaya kwa mama mwenye nyumba kwa kusema: "Huna hata haya wakiitwa wenye nyumba na wewe utatoka na hiki kibanda chako cha kuoshea maiti?" (uk. 67).

Kupitia mandhari hii iliyoambatana na matukio ya kijiniuchawi mwandishi anatuonyesha jinsi watu walivyo na umaskini mkubwa nchini Tanzania. Hii inadhihirisha kutokana na vinyumba wanavyoishi wakati viongozi wao wakiishi katika nyumba za kifahari. Na haya maeneo ni maeneo ambayo watu wenye uwezo wa hali ya chini wamekuwa wakiishi kuna vinyumba vya ajabu vya udongo na miti lakini wanaishi hivyohivyo. Utawala wa Waufi ni utawala ambao ulikuwa unatesa na kunyonya wananchi wake ndio maana wamekuwa wanaishi maisha mazuri sana akina Hunudu katika majumba ya kifahari wakati akina Masumbuko wanaishi kwenye vijumba vya ajabuajabu.

Kwa njia hii inahalisi kuhoji kwamba utunzi huu wa kimajaribio umemwezesha mtunzi kuzungumzia maswala mengi ya kijamii, baadhi ya maswala hayo yanajitokeza kwa kuashiriwa tu, mengine kwa kutajwa na mengine kwa kujengewa taswira za aina mablimbali. Kwa mfano, kwa kutaja tu Buguruni na kuzungumzia vibanda kama nyumba walizopangisha watu, mtunzi anafanikiwa kulijadili swala la umasikini, uchochole[5] na utabaka. Ameweza pia kudhihirisha mbio za maisha wanazokuwa nazo masikini katika kujaribu kuondokana na uchochole wao,  kwa mfano, ulinganishaji wa bafu halisi anakoogea Masumbuko na ndoto ya kuhamishiwa hadi bafu la kifahari, ni ndoto ya matamanio, ndoto ya kutaka kufarakana na hali yake ya sasa, ambapo Masumbuko anaweza kuangaliwa kuwa ni kiwakilisha cha nafsi na kiwakilishi cha tabaka.

Mwandishi anatuonyesha mandhari ya mkoani Tabora, Kigoma, Shinyanga kupitia katika masimulizi ya kabla Bwana Kikoko hajaoa mnamo mwaka 1970 na mwaka 1975. Bwana Kikoko alifunga ndoa na Bi Kapemba baada ya ndoa hawakubahatika kupata mtoto kwa takribani miaka minne ndipo wazazi wa Kikoko wakamshauri kijana wao aowe mwanamke mwingine. Mwandishi anasema:

> Tatizo kubwa lililojitokeza kwao, ni kukosekana kwa mtoto. Haikutokea japo mimba iliyoharibika, kama kawaida ya familia zetu, ndugu wakalivalia njuga tatizo hilo si kwa kheri ya kutafuta tiba, bali kwa kumtaka Kikoko amwache mkewe na aoe mke mwingine atakayemzalia watoto. Baba mzazi akahitimisha kwa kutoa amri kumtaka mwanaye huyo aoe mwanamke mwingine ila asimwache huyo wa kwanza (uk 85).

Kwa hivyo, mwaka 1980 Mzee Kikoko akaoa mke mwingine Bi Mwajabu Binti Fundikira. Mke huyu wa pili akababahatika kushika ujauzito ndani ya miezi mitatu lakini mimba ilipokuwa ya miezi mitano ghafla ikayeyuka na ikahamia kwa mke mkubwa Binti Kapemba kiuchawi baada ya kwenda kwao Shinyanga na kurudi akaonekana ana ujauzito mkubwa.  Kwa hiyo, kukawa na ugomvi mkubwa kati ya mke mkubwa huyu na Bi mdogo huyo. Mke mdogo akaamua kwenda kwao Tabora nyumbani kwa mababu

5 Uchochole ni ile hali ya kutokuwa na uwezo kiuchumi kama pesa yaani ufukra uliokithiri

zake huko Kapalapala kwa wazee kulivalia njuga swala hilo wakaushirikisha mzimu wao uitwao Kasomangila. Mzimu huo upo chini ya Waswezi lakini ilishindikana kwani Binti Kapemba naye wazazi wake walikuwa wana mzimu uitwao Waufi. Kwa hiyo, Waufi ulikuwa ni mzimu mkubwa sana ndio maana mimba ikabaki kwa mke mkubwa na akajifungua mtoto mkubwa aitwaye Masumbuko.

Mwandishi anatumia mandhari haya katika kutuonesha matukio mbalimbali ya kijiniuchawi na ushirikina jinsi yalivyochimuza dhamira ya ubaya wa serikali ya kibabe. Kwani, Waufi wanafananishwa na mataifa ya Ulimwengu wa Tatu ambao viongozi wake wengi walioko madarakani ni wababe hawataki kusikiliza chochote kutoka kwa mtu au wananchi. Waufi hujiona wana uwezo hata wa kuwanyang'anya ardhi wananchi na kuwapa wawezekaji wakati wananchi wao wanateseka. Kwa upande wa Waswezi, hawa ni watu ambao wako chini ya dola na hawana sauti hata kama wanaonewa. Kwa upande mwingine mtunzi mwisho wa siku anaonyesha jinsi matatizo ya ugumba yanavyoleta ugomvi na mifarakano katika familia mpaka inafikia hatua Binti Kapemba anaiba mimba ya mwenziwe kutokana na kwamba ndugu wa mwanamume walikuwa wakimsimanga sana ndio maana akaamua kuiba mimba ya mwenziwe ili na yeye asionekana alikuwa ni mgumba kwani jamii nyingi huona kwamba mwanamke asiyezaa mtoto hafai analeta hasara na wengine hudiriki hata kusema anaja choo tu. Lakini pia mtunzi anaweza kuwa anajadili hali za maisha zinazolazimisha watu kutenda mambo yasifikirika, mradi wawe wanajaribu kurekebisha hali za maisha yao.

Halikadhalika, mandhari hii imechimuza maudhui ya mivutano na migongano inayochangiwa na mila na tamaduni mbalimbali katika jamii kwani baadhi ya mila zimesababisha matatizo mbalimbali katika jamii kwa kuweka masharti ya kuuwa watu ili kuweza kufanikisha jambo fulani vizuri zaidi kama ilivyokuwa kwa huyu Binti Kapemba alivyoambiwa na waufi akijifungua huyo mtoto aliyeiba mimba ahakikishe anamtoa kafala kwa kumuuwa. Vilevile mandhari hii inatufundisha jinsi ilivyo vibaya kuuwa watoto au kutoa mimba kwa wale wanawake wanaofanya hivyo. Kwani kuna

wanawake au wasichana wengine wakijifungua mtoto akiwa mchanga humviringisha kwenye mfuko na kwenda kumtupa kwenye takataka au chooni.

Mandhari na matukio haya yanachimuza ujumbe wa kwamba si vizuri kwani mtoto huyo mwisho wa siku anaweza akawa kiongozi mkubwa serikalini kama alivyokuwa Masumbuko kiongozi wa Waswezi na akaja kuwa msaada mkubwa katika familia yake na katika jamii. Fauka na maudhui hayo pia kuna aina ya matabaka ya rangi na utaifa yanayochimuzwa kimandhari katika riwaya hii. Mwandishi anatuonyesha mandhari ya ofisini kwa Masumbuko nje ya ofisi yao iliyokuwa inaitwa Birimuye Holding Ltd. Masumbuko akiongea na mfanyakazi mwenziwe aliyekuwa anaitwa Shamsi akimwambia kwamba amekuja ofisini ili kukopeshwa pesa aende akafanyiwe matambiko huko kwao Tabora baada ya Mzee Kishindo kumwambia kwamba mama aliyemzaa si mama yake bali mama yake ni Bi Mwajabu. Binti Kapemba alichukua mimba ya mwenziwe kiuchawi. Bahati mbaya Shamsi akamwambia alishafukuzwa kazi kwa sababu amekuwa kichaa. Na akamwambia kwamba kama ajuavyo ofisi yao ni ya Mzungu kwa hiyo mambo ya uchawi huwa hawaamini kabisa. Masumbuko anasema:

> ….mbona sikuelewi Shamsi? Masumbuko alishangaa. Ndiyo hivyo kaka, unajua mimi nimekulia uswazi[6] kama wewe, haya mambo ya kishirikina ninayaelewa vema, lakini hapa ofsini kuna watoto wa kizungu hawayaelewi mambo hayo. Wanachoamini ni kuwa wewe umechanganyikiwa. Hivyo wameamua kukusimamisha kazi kwa muda usiojulikana mpaka bosi atakapojiridhisha kuwa umepona, na pia kama utaonekana hapo ofsini kwa kipindi hiki utaitiwa askari (uk 94).

Kupitia mandhari haya ya ofisini kwa Masumbuko mtunzi anachimuza dhamira ya mitazamo tofauti inayotokana na utamaduni wa jamii mbalimbali. Anatuonyesha kwamba wazungu waliopo katika nchi za Afrika hawana budi kujifunza utamaduni wetu na kuuheshimu na sio kupandikiza mila zao kuwa ni bora na za kufuatwa. Masumbuko anafukuzwa kazi bila kupewa hata barua wala yeye mwenyewe kuambiwa hata kwa kupigiwa simu kwa kosa la mtazamo wa kimila.

6 Uswazi ni maeneo ambayo kunakuwa na watu wenye tabia za ujanja na kwa kiasi kikubwa ni maeneo ya watu wasiojiweza sana kiuchumi

Kwa kweli huu ni unyanyasaji wa hali ya juu kwani mambo kama haya yanatokea sana nchini Tanzania katika migodi mbalimbali ya madini ambayo wamepewa wawekezaji wa Kichina, Kijerumani na Kimarekani nk. Wageni hawa wamekuwa wakiwatesa watu weusi kwa kuwachapa viboko pindi wanapokosea na kuwafukuza kama mbwa katika kazi. Kwa hiyo, kupitia mandhari na matukio ya majini yanayomkumba Masumbuko mwandishi anaonyesha jinsi unyanyasaji kati ya watu weusi na wazungu unavyoendelea.

Mtunzi anatumia mandhari ya ndoto katika kuonyesha safari anayopitishwa mhusika Masumbuko na Hunudu kwani safari hii inakuzwa na mwandishi "kuwa ndefu" na kisaikolojia inamjengea msomaji mpito wa kutoka uhalisia hadi umazingaombwe. Ili kushadidia safari ya kuhamishwa kutoka uhalisia hadi dunia ya umazingaombwe, mhusika adui Hunudu anajaribu kuhoji urefu wa kaburi la kumzikia Masumbuko aliyekuwa katika hali ya nusu urazini.

> "Kaburi mlichimba wapi? Hunudu akauliza. "Hapo kwenye shamba la migomba.""*Mna uhakika ni refu*?" "Ndiyo ni zaidi ya futi tisa!" (uk 130).

Ili upatikane ukamilifu wa safari ya kumtoa msomaji katika dunia ya urazini na uhalisia na kumpeleka katika dunia isorazini, njia anayotakiwa kupitishwa inajengewa taswira ya "urefu" kuashiria safari ya mabadiliko. Mbinu ya urefushaji safari ya kimatendo inapelekea kurahisisha safari ya kifikra kuwa rahisi kwa wasomaji. Mtunzi anatumia mandhari hii ya kindoto kupitia motifu ya safari kwa kuchimuza maudhui ya uonevu kwa baaadhi ya watu katika jamii ambao wakipata tu nafasi ya kuwa na pesa huwanyanyasa wasio nazo kwa kuamua kuwafanya chochote wanachotaka.

Kwa upande mwingine Ekolojia ya mapori na vichaka inarejelewa katika muktadha wa "kuchimba dawa" kuonyesha hali halisi ya mazingira ya barabarani nchini Tanzania ambapo badala ya kuwepo kwa vyoo maalumu, wasafiri hujikuta wakihitaji tabawali[7] maporini baada ya safari ndefu kwani sehemu kubwa ya barabara zetu ni mapori. "Abiria wakaanza kuteremka na kwenda kwenye vichaka kwenda kuchimba dawa"

[7] Tabawali maana yake ni ile hali ya kujisaidia kwa haja ndogo au kubwa

(Mwingizi 2013:101). Lakini ghafla mvua ya radi na ngurumo kali inaelezwa kuwa haikuwa ya kweli bali ya kimiujiza na kichawi kupitia Mzee Kishindo anayemshangaa Masumbuko aliyeonekana kulowa. "Halafu mbona umelowana hivyo?" (Mwingizi, 2013:102). Msomaji anaachwa katika mwanda wa uhalisiamazingaombwe.

Msomaji anaogelea katika "angahewa" ya mvua, radi na ngurumo kali inayotokea vichakani na maporini. Anasafiri pamoja na abiria wanaoonekana katika shughuli zao za kawaida, ghafla anataharuki kiuajinabishaji kuambiwa kuwa hali hiyo ni ya kimazingaombwe tu. Fikira za msomaji zinapelekwa katika kubaini kuwa maswala yanayoonekana waziwazi ya kijamii, mipango ya kitaifa na mielekeo inayozungumzwa pengine ni mazingaombwe tu kwani kuna hila zinazoizungukia hali hiyo. Jamii siku zote huonyeshwa na kupewa matumaini ya kupiga hatua za maendeleo lakini mipango hiyo haitafanikiwa katika maisha ya wanajamii hao waliowengi. Wajanja wachache wapo nyuma ya pazia wakipanga hila zao kama alivyo Hunudu katika *Mzimu wa Waufi*.

Mwandishi anatuonyesha mandhari nyingine ya ndotoni kupitia Masumbuko akiwa ameviringishwa kama pipi tayari kwa kwenda kuzikwa akiwa mzima mzima isipokuwa hawezi kuongea. Akiwa amebebwa akawa anasikia maongezi haya kabla hajaenda kuzikwa wakiwa wanabishana wale wanaokwenda kumzika yaani akina Hunudu na majini wenziwe. Maongezi hayo yaliyokuwa ni mabishano ya kumuuwa Masumbuko kwenye kikundi cha wachawi cha akina Hunudu kwani wapo waliokuwa wanataka Masumbuko asiuliwe wakisema hawataki kumuuwa kwa sababu mama yake alikuwa ni mshiriki mzuri wa Waufi na alikuwa ana nidhamu kwa hiyo wasimuuwe. Kutokana na maongezi hayo kukawa na ugomvi katika utawala huu wa Waufi wengine wanataka auliwe na wengine hawataki auliwe kichawi. Mwandishi kupitia mandhari hii ya kindoto anachimuza maudhui ya migogoro mbalimbali katika serikali nyingi. Kwa sababu kuna wakati serikalini nako kunakuwa na migogoro mingi kati ya viongozi kwa viongozi hasa bungeni inapotokea baadhi ya viongozi kutetea hasa maslahi ya wananchi. Ndipo wale ambao wapo kwa ajili ya kutetea maslahi yao binafsi wanachukia na kuanza kuwasimanga wenzao kichinichini. Mandhari hii pia inachimuza

migogoro mbalimbali inayotokea hata katika familia pale inapotokea mtu alikuwa mwema na mchapakazi anapopatwa na matatizo katika jamii. Jamii huwa haisiti kumsaidia kwa sababu alikuwa ni mtu mwema katika jamii.

Pia mwandishi anatuonyesha mandhari ya makaburini na ya nyumbani kwa Mzee Kikoko Tabora. Katika mandhari hii ya makaburini tunaona utawala wa Waswezi umefanikiwa kumchukua Masumbuko na kumpeleka makaburini kwa ajili ya matambiko. Wakiwa makaburini wanakutana na utawala wa Waufi wakiwa na hasira kali wakitaka kumchukua Masumbuko maana alitoka mikononi mwao pindi walipomgeuza kichawi kuwa ng'ombe ili waweze kumchinja kwenye msiba wa Mzee Kishindo. Wakiwa makaburini ghafla gari ya jeshi ikaja kwa ajili ya kumkamata Masumbuko kwa kumuhusisha kwamba anahusika na msiba wa Mzee Kishindo na Kasimba. Vilevile, kukawa na kukamatwa kwa Mzee Jabu na mke wa Kikoko mkubwa kwani nao walihusishwa na mauaji hayo pamoja na Bibi mdogo wa Kikoko. Kitu cha kushangaza pale kituo cha polisi aliyeachiwa ni mke mkubwa wa Kikoko ambaye alionekana kuwa ni muhusika mkuu wa mauaji ambaye muda wote alikuwa na Kikoko anayetafutwa naye kwa mauaji.

Katika mandhari hii na matukio ya kiajabu kama haya, mwandishi anachimuza maudhui ya uwajibikaji katika utendaji kazi katika ofisi mbalimbali kwani kumekuwa na upendeleo wa hali ya juu katika ofisi mbalimbali hasa za serikali. Mfano hata katika hospital za serikali mara nyingi wale wenye pesa hupewa kipaumbele na wale viongozi wa serikali katika matibabu. Madaktari hujisahau kabisa kuwahudumia watu wa kawaida au kwa kufuata foleni iliyo halali. Vivyovivyo hata kwa upande wa askari, kupitia kwa polisi mwandishi anachimuza ujumbe jinsi askari polisi wasivyotenda haki kwa wananchi wao.  Kwa sababu ilitakiwa watuhumiwa wote wawekwe jela mpaka hatima ya wauaji ipatikane lakini, wenyewe wakawaweka wengine polisi na kumuacha pekee huyu Bi mkubwa wa Kikoko.

Aidha, utendaji kazi wa polisi kama huu upo sana katika jamii zetu polisi huwa hawafanyi kazi kwa haki hata kidogo. Polisi hawa huwa hawatendi haki hasa wakijua aliyefanya tukio hilo ni mtu ambaye yupo katika dola, polisi huwa wanapindisha maelezo na kumfanya mtu huyu asionekane na hatia. Hivi ndivyo ilivyokuwa kwa mke wa Kikoko mkubwa alitolewa kwa sababu yupo katika utawala wa Waufi, utawala usiojali wananchi wake unaowatesa na kuwaua. Hiyo ni miongoni mwa mifano miwili tu japo katika sekta mbalimbali za serikali utendaji kazi na uwajibikaji wa namna hii upo karibia sekta zote serikalini. Kama pale hospitalini Dokta Nyango akiongea na askari wa upelelezi aitwaye Manumbo. Sababu ya kumuita askari huyo na kuwa na maongezi naye katika hospitali ya Kiteto iliyopo Tabora ni tukio la kupelekewa maiti waliyoichukua makaburini wakati akina Masumbuko wanatambika na ghafla Hunudu akatokeza na kumvamia huyo dada aitwaye Nyamizi na kumpiga hadi kumtoa damu. Japo askari hao walijua amekufa lakini kumbe hajafa. Mtunzi anatuambia:

> …baada ya Hunudu kutoweka, tayari askari walifika pale makaburini na kukuta ile hali ya ajabu, Masumbuko akiwa amelowa damu mwili mzima huku pembeni kuna dada kapasuliwa, kichwani haikujulikani kama amekufa ama amezimia tu. Askari wakajenga taswira kwamba palikuwa na mauaji pale… (uk. 150)

Kupitia tukio hili la kutisha na la ajabu ndio maana waliona Nyamizi amekufa na walipofika hospitali hawakutaka Dokta apime, polisi hawa ambao ni akina Manumbo walitaka apelekwe moja kwa moja kwenye chumba cha kulazia maiti.

Mwandishi anatumia mandhari hii ya hospitali kutuonyesha tukio hili la Nyamizi kwa kukuza ujumbe ambao unawataka polisi na idara nyingine kutoingilia kazi za madaktari. Nyamizi alizimia tu mwandishi ametumia uhalisiajabu huu kwani askari wanaona amekufa lakini daktari anaona hajafa na mwisho wa siku baada ya matukio haya yote Nyamizi anakuja kujulikana hajafa wakati alipopimwa na akapata nafuu lakini anaonekana amekufa tena mtunzi ametumia umazingaobwe huu katika kuonyesha jinsi polisi wanavyojifanya wana mamlaka popote pale. Dokta anamwambia polisi Manumbo:

> ..nyinyi ni wataalamu wa maswala ya upelelezi, walinzi wa raia na mali zetu, sasa haipendezi kabisa kwa namna yeyote ile kuingilia taaluma zisizokuwa zenu”.. “….mmemleta yule dada hapa huku mkinishinishinikiza kuwa awekwe *mochwali*, bila ya kujali taratibu za kitabibu zilizopo hapa, na hata pale mlipopewa taratibu zetu mlizidi kuelekeza kwa kukaripia wataalamu. Sasa iko hivi huyo dada wala hakupoteza maisha kama unavyosema bali alipoteza kitu kingine kabisa…fahamu tu (uk 164).

Nukuu hii ya Tabibu inatupa dhamira ya kwamba polisi au taasisi nyingine yeyote hawatakiwa kuingilia shughuli ambazo si taaluma zao lazima watavuruga. Dhamira nyingine tunayoipata pia ni kwamba hata wanasiasa hawatakiwi kuingilia taaluma za watu kwani tumeona katika nchi nyingi za Afrika wanasiasa wamekuwa na nguvu kila mahali hata kufikia hatua kuharibu mambo mengine, kutokana na kwamba hawana taaluma hizo lakini wanang’ang’ania kufanya kila kitu. Ndio maana mipango mingi wanayokuwa wanaifanya bungeni haitekelezeki kwa sababu hawahitaji kuwatumia zaidi wataalamu wao walio nao maofisini. Mjadala mkubwa unaoibushwa na maelezo haya unazungukia maswala ya uwajibikaji, utaalam na matekelezo ya kiutalam, ambapo mtunzi anaonekana kudadisi ni kwa kiasi gani taaluma zinaheshimiwa na ni kwa kiasi gani kunaheshimiwa mipaka ya kitaaluma.

Haya ndio mandhari na matukio ya kijiniuchawi na ushirikina ambayo yameibua maudhui mbalimbali katika riwaya hii ya *Mzimu wa Waufi* na kuchimuza maudhui mbalimbali katika jamii. Mwingizi ametumia mandhari za kinelbelini kwa kiasi kikubwa na mandhari ya uhalisia katika kuibua maudhui haya.

## 3.5 Mandhari na Matukio ya Kijiniuchawi na Ushirikina Yalivyochimuza Dhamira na Maudhui katika Riwaya ya *Tanzia*

*Tanzia* ni riwaya ambayo inaelezea mambo mbalimbali ya kiuchawi na kiushirikina ya kutisha katika nchi ya Tanzania. Mambo haya ya uchawi yanamuhusisha mhusika mkuu Bi Masonganya aliyekuwa mchawi mkuu. Japo alikufa lakini uchawi wake alimrithisha uchawi mjukuu wake Kaguba ili auendeleze kwa kuendelea kuwaua ndugu zake na hata watu mbalimbali lakini mwisho wa siku wachawi wote wa mji huu wanakamatwa na kufa

wote. Vilevile kupitia uchawi huo mtunzi anasema waliweza kuzorotesha maendeleo ya taifa kwa kiasi kikubwa kwani uchawi huo ulitumika hata katika ofisi za serikali katika kuwaloga watenda kazi wa serikalini.

*Tanzia* ni riwaya inayosimulia matukio ya kiuhalisiamazingaombwe, yaani usawiri na uwasilishaji wa uhalisi wa kiutunzi unaojitambulisha kwa misingi ya matumizi ya mbinu mahususi kuzungumzia uhalisia wa maisha, kuangalia maisha, ulimwengu au matukio ya kawaida kwa njia mbadala. Ni utunzi unaotumia zana, mbinu, mitindo na mitazamo inayowezesha kuibuka kwa njia mbadala za kuangalia, kutafakari na kufasiri mambo ya kawaida kama vile uchawi na urogi kwa njia zisizo za kawaida. Uhalisiamazingambwe, kimsingi ni utunzi na ubunilizi nyeti na wala sio ubunilizi kengeushi. Utunzi wa kiuhalisiajabu ni utunzi unajishughulisha na maswala nyeti, ni utunzi unaoshughulisha na kufikirisha, ni utunzi unaowezesha kutajwa na kusawiriwa kwa ulimwengu wetu, kwa mahusiano yetu, kwa mitagusano yetu na mifumo yetu ya maisha kwa njia mbadala. Ni utunzi unaowasilisha na kudadisi ukweli kama tunavyouelewa.

Uhalisiajabu unaashiria, unaelekeza na unagusa ukweli, kwa hivyo, riwaya ya *Tanzia* ni riwaya ya kihalisiajabu si riwaya kwepaji (*escapist novel*). Riwaya ambayo hata katika ubanifu wake inajaribu kuwasilisha ukweli wa muongoulimwengu fulani, ulimwengu uliopo, ulioweza kuwepo au uwezekanao kuwepo, tofauti na ulimwengu wa utamaduni wengu**.** Hii ni riwaya ya kimajaribio ambapo mtunzi Maundu Mwingizi ametumia mtindo wa kijiniuchawi na ushirikina katika kuchimuza maudhui mbalimbali katika jamii, lakini zaidi kudadisi na kuchokoa ukweli wa kimahusiano kama unavyochukuliwa kuwa kila siku. Kupitia riwaya hii mwandishi anachimuza maudhui ya imani na desturi za watu katika jamii, usaliti kama uhalisi wa kimahusiano na kitagusano, udikiteta na uimla wa viongozi kama mkakati wa kiutawala, uzalendo wa wananchi, ushujaa.

Riwaya hii imetumia mandhari halisi na mandhari ya kinelbelini pia katika kuwezesha sio tu usawiri wa maswala hayo bali pia kuyawasilisha kama mambo ya kiajabu na

mambo ya kawaida kwa wakati mmoja. Mandhari halisi imetumiwa katika riwaya hii ya kijiniuchawi na ushirikina katika kuonyesha mazingira ya uhalisia yanayotumiwa ili kufanya matukio yanayofanyika baadaye kuweza kukubalika kama ya kawaida katika jamii. Kwa mfano, katika mandhari halisi katika riwaya hii ya *Tanzia* mwandishi ametumia mandhari ya mji wa Tabora, na Kigoma katika kusimulia matukio mengi sana ya kiuchawi na ushirikina yanayotukia maeneo hayo nchini Tanzania. Mwandishi ametumia mandhari halisi katika kutufanya kuamini kuwa kupitia mandhari hizi tunaweza kupata picha halisi ya mandhari ya kijiniuchawi na kishirikina katika kuchimuza maudhui mbalimbali katika riwaya hii.

Kwa hivyo, *Tanzia* kama riwaya ya kihalisiaajabu si riwaya inayojishughulisha na utunzi wa ukisiaji bali inajishughulisha na utunzi unaohadithia visa, matukio na mandhari ya matukio kutoka kwa mkabala wa watu walioko au wawezao kuwa katika ulimwengu lakini wanaotagusana na uhalisi na ukweli wa uhalisi kwa njia tofauti tofauti na njia tunazitambua kuwa bainifu. Uwepo wa wachawi, pepo, mazimwi au vizuka si njozi au ruya bali ni ubainikaji wa uhalisi/ukweli wa watu wanaoishi katika ulimwengu lakini walio na tajriba au utangamano na wachawi, washirikina, mapepo na mazimwi. Uhalisiajabu unaoonekana katika riwaya hii unasawiri ulimwengu halisi wa watu ambao ukweli na uhalisi wao ni tofauti na wetu. Hii ina maana kwamba misingi ya uhalisiajabu ya riwaya hii inajaribu kutuchorea uhalisi wa ulimwengu kutoka mitazamo na mikabala mbadala. Kwa mfano, usawiri wa wachawi na msambao wao wote katika riwaya unawasilisha ulimwengu wa kichawi na wachawi unaodhibitiwa na watu tofauti nasi. Kwa hivyo, uwasilishaji wa ulimwengu wa wachawi, mifumo ya kichawi, zana na ala za kichawi, taratibu na tamaduni za kichawi ni mambo ambayo hayapaswi kupuuzwa na kutupiliwa mbali kuwa ya kishenzi na kijinga, bali ni kwamba utunzi wa aina hii katika riwaya ya *Tanzia* ni mwaliko kwa msomaji kuupitia na kuuhisi ulimwengu wa walimwengu wengine.

Uhalisiajabu wa riwaya ya *Tanzia* unawasilisha ulimwengu mbadala kwa njia kadhaa athirifu, na kwa kiasi kikubwa uhalisi huo unabainika kwa kadri unavyolinganishwa na

uhalisi wa ulimwengu kama ulivyozoeleka. Kwa mfano mpito wa wakati haujidhihirishi kwa mfuatano wa moja kwa moja, visababishi na usababishi wa matukio kwa jumla huwa ni wa kidhahania (*conceptually subjective*) na mambo ya kimiujiza/kiajabu na ya kawaida ni mamoja. Wakati haufuatani moja kwa moja kwenda mbele, mambo na matukio yaliyopita yanajidhihirisha katika uelewa wa sasa kiajabu na mstakabali (*future*) umeishatokea tayari, uhamishaji na usogezaji mkubwa wa wakati katika masimulizi katika uhalisiajabu unawasilisha uhalisi ulio nje ya mipaka ya wakati, kwa hivyo uwepo wa mizimu, mapepo na urudiajirudiaji wa wakati badala ya upigaji hatua ni uhalisi unaofaa kukubalika na kudhibitika. Hii ndio maana, katika riwaya hii tunapata hadithi ikisimuliwa katika mandhari ya kinelibini, yaani, wahusika wanatoka katika ulimwengu halisi hadi ulimwengu wa kinjozi kupitia mambo ya kichawi na kimajini na kurejea tena katika ulimwengu wa halisi. Mwandishi anavunja mipaka ya kimwanda ili kuelezea mazingira tofauti yanayowakumba wahusika mbalimbali katika riwaya hii pia.

Kuhusu na usababishaji au kwa usemi mwingine visababishi na matokeo, dhana nzima huwa wakati mwingine inaegemezwa katika mambo yenye uwezekano finyu sana na kusababisha matokeo yanayoshuhudiwa. Kwa mfano hisia, za mtu mmoja kumuua mtu mwingine mahali pengine. Kwa sababu hii utunzi wa kihalisiajabu huyaweka sambamba mambo, hali au matukio yanayohusiana kibahati na kinasibu (*casually related*) kwa njia ambazo hazionyesha kuhitilafiana na uhalisi kama tuujuavyo. Lakini katika kujenga mahusiano haya ya kinasibu, mara nyingi maelezo yanayotolewa huwa na undani unaotusadikisha kwamba uwezekano huo upo.

Katika riwaya hii mwandishi anatuonesha mandhari na matukio ya wilaya ya Kibondo mkoani Kigoma nyumbani kwa Bi Masonganya wanaukoo wakiwa wamekusanyika wakimsubiri Bibi huyu afe maana ameumwa kwa muda mrefu. Baada ya kuona hali ya hewa imebadilika upepo mkali sana ukatokea wakajua ndiyo dalili za kufa Bibi huyu. Kwani walikuwa wanasubiria kifo cha Bibi mkubwa huyo kwa hamu ya ajabu kutokana na kwamba Bibi huyu alitesa sana wananchi wa Kibondo, wanaukoo, mpaka watu wa

serikalini aliwatesa pia. Mama huyu wakaona hafi wakaamua kumuandaa mtu kwa ajili ya kumuuwa kwa kutumia nguvu za kiuchawi. Mwandishi anasema:

> …sauti za vigeregere, nderemo na vifijo kutoka kwa wanaukoo vilizizima chumbani humo, japo havikuwa vigeregere vya furaha bali viliashiria kukamilika kwa kifo kile kilichowabidi kukilazimisha. Hawakuwa na namna nyingine zaidi ya kukilazimisha kifo kile (uk 3).

Kupitia mandhari hii na matukio haya, mwandishi anatuonyesha ulimwengu wa imani za uwezekano, kwa mfano, jinsi ambavyo mtu akiwa katili watu wanavyotamani usiku na mchana afe ili waondolewe ukatili wake. Mandhari hii na matukio haya yaliyokuwa yanaendelea nyumbani kwa Bibi huyu ni wazi kwamba wananchi na wanaukoo hawa walikuwa hawampendi kabisa huyu Bibi na ndio maana walipenda afe. Ufu ni ishara ya uondokaji, na uondokaji ni sawa na usuluhishaji wa tatizo, ndivyo ilivyo hata katika jamii zetu watu wenye tabia kama hizi za kikatili hata viongozi, wananchi hufurahia vifo vyao pindi wanapokufa. Mandhari hii ndio inakuja kuwa kijenzi kikuu cha ploti ya riwaya hii. Bila ya tukio hilo usimulizi usingeweza kuchukua mkondo wake uliopitia.

Vinginevyo, pale ambapo riwaya hii ya kihalisiajabu inaposawiri na kuwasilisha mambo kama ya wachawi, majini, sauti kutoka makaburini, miviga, sherehe au taratibu maalum za kidini au kitamaduni zilizo na uwezo wa kuondoa janga, laana, kiangazi au hata kusababisha mvua kunyesha, mambo haya yote yanawasilishwa kama mambo ya kawaida hata kama ulimwengu yanamowasilishwa ni ulimwengu wa urogi na usihiri. Ili kuyawasilisha mambo haya kwa njia inayoweza kuaminika, mtunzi wa riwaya hii ya kihalisiajabu amejaribu kuwasilisha mambo ya kawaida kama mambo ya kiajabu na mambo ya kiajabu kama mambo ya kawaida. Aidha Mambo ya kiajabu yanasawiriwa na kueleza kwa undani unaosawiana na mambo ya kawaida, kwa mfano vituko, visanga, ndumba na mizungu ya Bi Masonganya imekitwa katika uhalisi wa maisha ya kila siku, unapougua, kuugua kunaangaliwa kama jambo la kawaida, hivyo hivyo anapokufa, kifo na uhalisi wa kila siku, lakini utokawaida unajibainisha pale anapokataa maziko.

Kwa mfano, mwandishi anatuonyesha mandhari na matukio mahakamani katika wilaya ya Kibondo. Mahakamani hapo palikuwa na kesi ya ubakaji iliyokuwa inamuhusu mjukuu wa Bibi Masonganya aliyembaka msichana mmoja na alitakiwa kuhukumiwa. Siku ya hukumu ilipofika ghafla waliibuka nyuki mahakamani watu wote wakasambaratika hapo mahakamani pamoja na mafaili yote yaliyobeba kesi ya mjukuu wa Masonganya kupotea. Wale nyuki wakamfakamia Jaji aliyekuwa anahukumu kesi mpaka wakamtoa roho. Mwandishi anasema:

> Siku ya hukumu sasa Jaji akiwa anaingia mahakamani baada ya umati kufurika ndipo ghafla walipoibuka nyuki hata wasijulikane walipotokea, ikawa ni patashika ya nguo kuchanika, kila mmoja akitafuta njia yake. Kama nyuki nao huwa na vichaa, basi hawa nao walihitaji chanjo. Walikuwa wanauma ovyoovyo, na wakikuuma, hayo maumivu yake ni kama umegongwa na kiboko (uk. 4).

Ingawa kesi hii alipewa tena Jaji mwingine lakini naye siku anatokea nyumbani kwake anakwenda kwenye kesi alijikwaa akaanguka chini akafa hapohapo. Kama tulivyohoji hapo juu, mtunzi anaweza kuwasilisha mambo ya kawaida kwa njia za kiajabu, kwa mfano kufa kwa watu ni jambo la kawaida, lakini katika riwaya hii kufa kwa majaji na watu wanaohusika katika kesi ya mjukuu wa Bi Masonganya si kufa kwa kawaida. Kwa hivyo, katika mandhari hii na matukio yaliyokuwa yanaendelea mwandishi wa riwaya hii anachimuza ujumbe wa swala zima la haki katika kutekeleza sheria mbalimbali.

Michakato ya utekelezaji wa haki imekuwa ikipitia katika misukosuko mbalimbali ikiwemo watu kuchanganya sheria za nchi na maswala ya mila na desturi kiasi kwamba utekelezaji wa haki hizi unakuwa mgumu kutekelezeka. Hii inadhihirisha wazi jinsi mahakimu, mawakili na majaji wanavyokuwa wanapoteza maisha yao kwa ajili ya kutenda haki. Matukio kama haya yamekuwa yakitokea nchini Tanzania na hata Kenya hasa kwa mawakili na mahakimu, japo kwa majaji imekuwa ni kwa kiasi kidogo sana kutokana na kwamba wenyewe wana ulinzi mkali sana. Wanasheria hawa wanauawa kutokana na kesi wanazozihukumu kupitia ndugu wa mtuhumiwa au hata mtuhumiwa mwenyewe kama alifungwa na akatoka anaweza kumuuwa hakimu au wakili. Mwandishi anachimuza ujumbe unaoonyesha jinsi utendaji haki unavyokuwa mgumu

kutokana na imani za uchawi kwa baadhi ya watuhumiwa na ndugu wa watuhumiwa. Hali hii inaendelea kuwa ngumu kutokana na sababu kwamba, serikali huwa haiamini swala zima la uchawi na ushirikina na hivyo kupelekea kesi nyingi kuishia njiani.

Maswala haya ya utendaji haki yamekuwa yakileta shida hata katika ofisi nyingine za serikali pale inapotokea kiongozi aliyekuwepo mamlakani kutenda haki kwa mfanyakazi ambaye ndugu yake ni kiongozi mkubwa serikalini. Kwa hiyo hata kama mfanyakazi huyu amefanya kosa inakuwa ni vigumu kumuwajibisha kwa kuhofia kupoteza ajira.Tukio la aina hii hii pia lilitokea katika mandhari ya bafuni ambapo Binti aliyekuwa amebakwa na Ndosa mjukuu wa Bi Masonganya alianguka na kufa palepale wakati anajiandaa kwenda kwenye kesi. Mandhari hizi na matukio haya yote yaliyokuwa yanaendelea katika kesi hii yanachimuza ujumbe wa kwamba siku zote haki inapotendeka lazima kuna upande unaumia au utaumia au utapata madhara. Fauka na matukio hayo katika mandhari ya mahakamani mtunzi kupitia fikra na itikadi na matendo ya uchawi analimulika swala linalozorotesha maendeleo ya jamii na taifa kwa kiasi kikubwa kwani uchawi huo ulitumika hata katika ofisi za serikali katika kuwaloga watenda kazi wa serikalini.

Uhalisiajabu au uhalisiamazingaombwe ni utanzu bainifu wa utunzi wa fasihi unaopania kuwasilisha tajriba za maisha kutoka kwa mkabala wa ulimwengu unaowezekana, ulimwengu mbadala. Mbinu zake vilevile zinasawiana na ulimwengu huo mbadala na zinakusudia kuuhuisha ulimwengu huo wa watu wengine. Uhalisiajabu unapoangaliwa kijumla kama mbinu ya kiutunzi, basi unakuwa mbinu ya kudadisi uhalisi na ukweli wa wahusiaka, jamii na viumbe wanaoishi nje ya ulimwengu razini. Kwa mfano, katika mandhari ya chumbani kwa Bi. Masongonya ambapo ililazwa maiti yake panatokea kitu cha ajabu pindi wanapokwenda chumbani kuichukua ile maiti kwa ajili ya kwenda kuizika, wanakuta maiti imefumbua macho imewatazama.

Mtunzi anaonyesha wale watu waliokuwa wanakwenda kubeba maiti mle chumbani wakatawanyika na kukimbia kwa kuogopa. Kaka wa marehemu ikambidi atafute mtu

ambaye anaweza kumuua na kumaliza kabisa. Kwa hiyo, akaitwa Bi Kibena akaja na akaingizwa katika chumba cha marehemu watu wote wakatoka wakamuacha peke yake. Ghafla yule Bi Kibena naye akafa hukohuko chumbani kwani kulikuwa na purukushani kubwa. Ni bayana kuwa mazingira haya na matukio haya yanakuza na kuendeleza ujumbe wa kuwaonya wale watu au viongozi wanafiki ambao huwa wanajiona wenyewe ni wasafi kumbe hata wenyewe sio wasafi ndio maana mwisho wa siku huwa wanaumbuka kama Bi Kibena. Bado katika mandhari hii hii ya chumbani kwa Bi Masonganya, baada ya Bi Kibena kufa matukio mengine ya kiajabu yanatukia baada ya kwenda kumtafuta mganga mwingine kutoka sehemu ya mbali ili aweze kummalizia Masonganya kufa. Mganga huyo alipokuja alifanikiwa kumuua Bi Masonganya. Kupitia mandhari hii mtunzi wa riwaya hii anatupa ujumbe kwamba unaweza ukajiona una nguvu zaidi au una mamlaka zaidi kuliko wengine kumbe wapo walio juu yako wana uwezo wa kukuangusha. Mtunzi anachimuza ujumbe wa kuwaasa viongozi madikteta kwamba ipo siku watapinduliwa na wananchi. Kwa hiyo, wanatakiwa kuwaheshimu wananchi wanaowaongoza.

Mwandishi anaendelea kuonyesha kuwa matendo ya wahusika kwa kiasi fulani yanachochewa na mitagusano inayojibainisha katika mandhari na mazingira yao. Mazingira anamojikuta mhusika yanaathiri kwa kiasi kikubwa wasifu wake kama mhusika. Mara nyingi, wasomaji hupenda kuona mandhari yanayoweza kutambulika au hata kufikirika, lakini hili haliwezekani katika kazi ambazo haziandikwi katika misingi ya uhalisia. Mandhari huwa na elementi zinazojitambulisha. Elementi hizi ni kama vile eneo halisi la kijiografia kama nyumbani, gerezani, pangoni na msituni; au wakati ambapo tukio fulani linatendeka au kipindi maalumu cha kihistoria au kipindi cha mwaka (mfano msimu wa mvua au kiangazi) (Wamitila 2002: 29). Kujengwa kwa wahusika wa ajabu ajabu kama Bi Masonganya, Mzee Gao na Binti Sambayu katika riwaya ya *Tanzia* hakuna budi kukitwa katika mandhari yanayolandana na viumbe hao wa ajabu ajabu au wenye mambo ya kimazingaombwe. Nyumba wanazoishi, mienendo yao ya kimaisha, kufa kwao, hakuwezi kuwa kwa kawaida.

Aidha sifa zao zinaakisi ulimwengu wao na uonoulimwengu wao hauwezi kuwa wa kawaida. Kuna wakati wanaishi na kufanya matukio yao katika fikra za wahusika au wahanga wao, kupitia ndoto au nusu urazini kwani mawanda hayo ni sehemu ya maisha yao. Kwa vile mtunzi anajenga mandhari ya uhalisiaajabu, tunakutana na Kijumba cha Bi Masonganya, Binti Sambayu na Mzee Gao hazipishani sana kwani zipo katika mazingira ya kijijini na mazingira hayo hayawazuii kufanya shughuli zao. Tunaona kwa kiasi kikubwa matendo na siha ya wahusika huwa yanalandana na kushabiahana. Bila ya mandhari ya ajabu ajabu yanayolandana na sifa za wahusika inakuwa vigumu kuwaaminisha wasomaji katika muktadha wa uhalisiaajabu au uhalisiamazingaombwe. Kutokana na mandhari hizo tunaona sifa mahsusi za wahusika zinajengeka. Ni kwa vipi mandhari imesaidia kuwajenga wahusika, hulka na sifa zao inajidhihirisha katika riwaya teule za Mwingizi kama inavyodhihirika katika riwaya ya *Tanzia*. Mtoto Kaguba anachorwa na mtunzi katika *Tanzia* kama mtoto wa kawaida lakini anapoletwa katika mazingira ya kukutanishwa na mganga Gao ghafla anabadilika:

> Cha ajabu Kaguba aliingia huku akiruka kimchezo kama wafanyavyo watoto, ila alipofika tu mle sebuleni na kutupa macho yake kwa mganga, hapohapo akaamza kulia kwa hofu akitetemeka kwa woga (uk, 30).

Hivyo, muda wa kutokea tukio la kukutanishwa katika mandhari ya kuumbuliwa, uhalisia wa Kaguba unatoweka na kuvaa uhalisiajabu kiasi cha kudiriki kukubali kukiri kwamba, yeye ni muuaji.

Mwandishi vilevile anatuchorea mandhari ya kinjozi kupitia mhusika Mama Kaguba anapomuonyesha katika mandhari na matukio mbalimbali yanayomkumba mdogo wake Nyanzala akiwa anatumikishwa kiuchawi na Binti Sambayu. Binti Sambayu aliamua kumuuwa Nyanzala kwa sababu ndiye aliyeshiriki kumuua Bibi Masonganya kwa sababu alikuwa hafi haraka na alikuwa ni kero hata kwa wananchi na kwa wanaukoo. Kwa hiyo, Binti Sambayu alimuuwa Nyanzala kwa sababu alisababisha kifo cha Bi Kibena ambaye ni ndugu yake. Masonyanya asingekufa basi na Bi Kibena asingekufa. Mandhari ya ndoto hii inachukua nafasi yake katika *Tanzia* pale mama Kaguba

alipokuwa anasimuliwa na marehemu Nyanzala kupitia kwenye ndoto. Nyanzala anamwambia mama Kaguba ambaye ni dada yake jinsi anavyofanya kazi za kufyeka na kuna siku alikuwa anafyeka kwa bahati mbaya akapoteza upanga haukuonekana tena alichomwa na vijinga vya moto. Nyanzala alipokuwa akimsimulia mama Kaguba alikuwa analia sana kumbe alikuwa ndotoni halafu Nyanzala akamuaga mama Kaguba akarudi kwa Binti Sambayu. Mama Kaguba akawa anamkataza asirudi tena kwa Binti Sambayu. Mtunzi anatuonyesha jinsi mama Kaguba alivyokuwa ameshtuka usingizini anavyomkataza Nyanzala;

> "NOOO, NYANZALAAAAAA, USIENDE HUKOOOO."Sauti kali aliyoitoa mama Kaguba ndo iliyomzindua kutoka usingizini, na kujikuta akiwa kitandani amelala. Kumbe ilikuwa ni ndoto tu (uk 21).

Vilevile tukio kama hili tena limeendelea kujitokeza katika mandhari hayahaya. Tunaona nyumbani kwa marehemu Masonganya jinsi Nyembo alivyokuwa anaendelea kuwaamuru hawa wachawi akina Binti Sambayu waeleze kila kitu wanachokifanya katika mambo yao ya uchawi. Binti Sambayu akawa anaeleza mambo waliyokuwa wanafanya. Ghafla Babu Gao akamuuliza ameua watu wangapi katika kijiji hicho ndipo akaendelea kuongea na kuwataja watu waliowaua. Wananchi waliokuwepo wakapandwa na hasira wakaanza kuwachapa kwa mijeledi na mawe na marungu. Polisi wakaja kutuliza ghasia na kuwaokoa akina Binti Sambayu na wachawi wenziwe lakini wakiwa katika hali mbaya na walifia njiani kwenye gari wakiwa wanaelekea polisi.

Mandhari haya ni muhimu sana katika kukuza ujumbe wa kutojichukulia sheria mikononi pindi mtu anapokuwa anafanya mambo ambayo hayapendezi kijamii. Mfano kuna watu kama wachawi sana, wezi sana na jamii huwa inashindwa kuvumilia na inaamua kuwachoma moto au kuwakatakata kwaa mapanga. Matatizo kama haya tumeyaona nchini Tanzania katika mikoa ya ya Shinyanga na Mara. Pindi wakiona Bibi mchawi ndugu walikuwa wanashiriki kikamilifu katika kuhakikisha wanamuuawa yule ndugu yao. Kitu ambacho hakitakiwi kwenye sheria za nchi mbalimbali kumuuwa mtu. Kwani hata wale wanaoshiriki kumuuwa mtu nao huwa wanachukuliwa hatua kali

ya kufungwa kifungo cha maisha na kutumikishwa kazi mbalimbali magerezani. Watu wa aina hii wanafananishwa na Nyanzala.

Mtunzi anatuonyesha pia katika mandhari ya nyumbani kwa Bi Masonganya, Mama Kaguba anafagia uwanja. Ghafla Kaguba aNamkataza mama yake asifagie sehemu ambayo waliweka dawa ya kumzuia Kaguba asitoke usiku kwenda kwa wachawi wenziwe kwa sababu alikuwa ni kiongozi wa wachawi. Japo mama huyu alikuwa na tabia ya kumdharau na kutomsikiliza chochote atakachoongea kwa sababu ni mtoto lakini safari hiyo alimsikiliza. Mtunzi anasema:

> "Mama…! Angalia hapo unapofagia," Kaguba aliongea kwa kumtahadharisha mama yake. Kutokana na vimbwanga vya mtoto yule, sasa alikuwa si wa kupuuzwa tena kwa kila anachotaka kukisema. "Kuna nini?" mama Kaguba alisaili huku akitupia macho yake eneo hilo alilokuwa akiliswafi. "Hapo si nd'o mmechimbia ile dawa mliyopewa na yule Babu ili mnizuie nisitoke usiku! Sasa ukifagia vibaya utaifukua buree mwishowe usiku nitatoka tena." (uk. 34).

Mandhari hii na tukio hili linachimuza ujumbe wa kutowadharau watoto wadogo pindi wanapokuwa wanaongea na wazazi. Kwa sababu mara nyingi wazazi wengi wamekuwa wakipuuzia au kutokuwasikiliza watoto wanapokuwa wanaongea nao au wanapokuwa wanawasimulia kitu fulani kwa kuona kuwa watoto wanaongea vitu visivyo na maana wakati wote kumbe kuna wakati watoto wanaweza wakaongea jambo la msingi.

Vilevile, mtunzi anatuonyesha mandhari ya porini yenye matukio ya kutisha baada ya gari kuharibika walilokuwa wanaenda nalo kwa mganga wa jadi kumpeleka Mzee Mtandi kuharibika. Mzee Mtandi alipelekwa kwa mganga huyo baada ya kuanguka ghafla nyumbani kwake akiwa anawasimulia ndugu zake mambo ambayo Kaguba anataka kuyafanya pamoja na Binti Sambayu. Mzee huyu alianguka na kuzidiwa ghafla wakawa wanampeleka kwa mganga maarufu Babu Gao. Njiani kimbunga kikatokea na baada ya kimbunga hicho, gari likaharibika na dereva akashuka kutengeneza ndipo akapotea moja kwa moja ikabidi wawe wanasubiri gari zingine ziweze kuwapeleka kwa Babu Gao. Wakiwa wanasubiri, kwa bahati nzuri, gari lakini, dereva wa gari hilo

hakuwa tayari kuwapeleka kwa mganga wa jadi bali alikuwa tayari kuwapeleka mjini hospitali japo, Kungurume na mama Kaguba walipenda zaidi kwenda kwa mganga. Ikabidi mama Kaguba ambembeleze dereva na dereva akakubali lakini kila wakiwasha gari kuelekea kwa Babu Gao gari lilikuwa linagoma kabisa lakini wakishuka akina mama Kaguba gari inawaka.

Mtunzi anatumia mandhari hii na matukio haya ya kutisha kutuonyesha kwamba ni vyema tusiwatumainie sana waganga wa jadi japo wakati mwingine wanasaidia. Kinachotokea hapa ni mgongano wa imani na athari zinazohusiana na migongano hiyo. Kwani, kuna baadhi ya ndugu zetu wamekufa kwa kuamini wamerogwa hata kama tatizo alilo nalo linahitaji vipimo hospitalini lakini yeye ataenda kwa mganga wa jadi. Kupitia mandhari hayo mwandishi anatukumbusha hasa sisi Waafrika tujifunze pia kwenda hospitali pindi tuumwapo tusikimbilie kwa waganga wa asili tu kwani kuna baadhi ya vipimo na madawa wanaweza wasiwe navyo au wakawa na dawa wakakuzidishia zaidi na ukazidiwa. Japo pia kuna wakati wanafaa zaidi. Katika muktadha wa kiuhalisajabu fikra za kirazini zinatoweka. Tunaona katika mandhari na matukio ya nyumbani kwa Babu Gao baada ya kina Mama Kaguba na Kungurume kupitia katika mateso na shida mbalimbali mpaka  wakafika na mgonjwa kwa Babu Gao. Cha ajabu Mzee Gao hana hata muda wa kuwatazama. Anajibu majibu ya mkato mkato kama vile hawafahamu na wala hajawahi kuwaona wakati ndiye aliyewasaidia kuhusiana na tatizo la Bibi Masonyanya lakini alikuwa anawajibu ovyo ovyo. Mwandishi anatuambia:

> “Sasa fahamu amezipotezea huko kwenu halafu mnakuja kuzitafutia kwangu! Mi’ siwezi kuzipata naomba muondoke haraka tafadhali nina kazi nyingi za kufanya.” Heeh…!
>
> “Babu siye ni wajukuu zako wa kule kwa Bi Masonganya, au umetusahau?” Ilibidi Kungurume ajaribu kumkumbusha Babu Gao akiamini huenda wamesahaulika.
>
> “Sina wajukuu kama ninyi…na kama ni wateja wangu ni kwamba sihitaji kufanya kazi nanyi kabisa jamani mwende au mpaka niwafanyie kitu kibaya?” (uk 50).

Kupitia mandhari ya nyumbani kwa Babu Gao, mwandishi anachimuza maudhui ya ujumbe wa kutokuwa na kauli mbaya pindi unapomuona mtu ana matatizo au hana matatizo. Majibu mabaya ya mkato ya Mzee huyu yanafananishwa pia na baadhi ya watendaji kazi katika serikali nyingi Afrika hasa, madaktari na wauuguzi baadhi yao huwa na kauli mbaya kwa wateja wao pindi wanapokwenda hospitali kutibiwa. Kwa hiyo, mtunzi anachimuza ujumbe huu kuwafundisha pia hawa manesi wanapohudumia wagonjwa wao wanatakiwa kuwa na kauli nzuri. Halikadhalika mwandishi anatuonyesha mandhari na matukio ya makaburini ambapo Babu Gao alikwenda na mgonjwa pamoja na ndugu zake mgonjwa na wafuasi wake. Tunaona wakati Babu Gao alipomwambia Mzee Mtandi akae juu ya kaburi ashike kinu halafu yeye atakuwa anatwanga dawa ili aweze kupona tatizo alilokuwa nalo. Ndipo tunashuhudia tukio la kutisha pale ambapo Babu Gao alipokuwa anatwanga kwenye kinu alichoshika Mtandi na ghafla kaburi likapasuka Mzee Mtandi akatumbukia na kaburi likajifunga. Na baada ya kaburi kujifunga wakaanza kusikia ndani ya kaburi vurugu kubwa Mzee Mtandi akilalamika anateseka. Mtunzi anasema:

> Ghafla! Wakaanza kusikia *kukurukakara* na vurugu vikitokea ndani ya kaburi aliliozama Mzee Mtandi. Ilikuwa ni kama vile uchukue dumu kubwa halafu uliwekee mawe madogo na kuanza kulitikisa kwa nguvu, sasa ndivyo zile vurugu mle kaburini zilivyozizima.
>
> "*YALAAAH…UWIIIII NAKUFAAA JAMANI!*" Sauti ya Mzee Mtandi ilisikika ikitokea mle kaburini licha ya kuwa kaburi lilikuwa limejifunga. (uk 57)

Baada ya hali ya Mzee Mtandi kulalamika Babu Gao uzalendo ukamshinda, akautupa mwichi wake na kutaka kutimua mbio ndipo haraka Kungurume akamrukia na kumkaba shati. Akiwa amemkamata ghafla kaburi linapasuka na Mzee Mtandi anatokeza juu na kurushwa kwenda angani na kisha anatua chini. Mtunzi anapitisha ujumbe kupitia mandhari na matukio haya ya kutisha yanayochimuza ujumbe wa kutokuwa wasaliti pindi mambo yanapokwenda kombo. Mtunzi anachimuza ujumbe huu kuonyesha kwamba usaliti si mzuri hata kama unaona rafiki yako au ndugu yako yuko katika shida yoyote au tabu yoyote unapaswa kumsaidia mpaka hatua ya mwisho hutakiwi kumtenga

au kumkwepa. Babu Gao ameonekana si mtu mzuri ni msaliti kwani alipoona maji yamemfika shingoni alitaka kukimbia na kuwaacha wateja wake.

Kwa upande mwingine katika mandhari hii hii ya kaburini, mwandishi anapowasafirisha wahusika kutoka katika mandhari ya uhalisia hadi mandhari ya umazingaombwe, Mwingizi anakuza safari za kumtisha msomaji kutoka katika hali ya uhalisia kwenda katika hali ya umazingaombwe na kisha kurudishwa tena katika uhalisia kupitia mbinu ya ukuzaji wa safari kuwa ndefu, mizunguko mirefu ya kuwakimbiza misukule, kuwapoteza kifikra kwa muda mrefu wahusika wanaochawiwa, kupotezwa kwa muda mrefu kwa wahanga wa uchawi. Kitendo cha kuhamisha hisia kutoka zile za kuihalisia hadi za kimazingaombwe tunaonyeshwa na Mwingizi kupitia kwa Mzee Mtandi na Nyanzala. Mtunzi anasema:-

> “Kaburi lililokaliwa na Mzee Mtandi lilipoachana kama mamba na wote wakashuhudia Mzee Mtandi aliyekuwa ameketi kwenye kigoda akizama na kupotelea ndani ya kaburi pamoja na kinu chake kisha kaburi likajifunga” (uk 56).

Matukio ya kuzamishwa na kufufuliwa kaburini yanatumia dhana ya “kupotelea” ni kitendo cha kusafirishwa na matayarisho ya kuoanisha dunia hizo mbili katika fikra za wasomaji. Anapokuja kufa kiukweli Mzee Mtandi, tayari wasomaji wamekwisha kuzoea hali hiyo. Kitendo cha Mzee Mtandi kuzirai kwa muda mrefu na kupoteza fahamu ni katika harakati za kumuandaa atoke katika dunia ya kweli kwenda katika dunia ya misukule (uk 54) na pia kurudishwa tena duniani inapobidi. Mtunzi kupitia mandhari hii anachimuza dhamira ya uonevu kwa watu wasio na hatia.

Pia katika mandhari ya nyumbani kwa marehemu Bi Masonyanya kuna matukio mbalimbali yaliyokuwa yakiendelea baada ya Binti Nyembo kugundua kibuyu cha uchawi cha baba yake. Baba huyu alikuwa ni Bibi Masonyanya ambaye alikuwa ni mwanamke aliyezaa na mwanamke mwenziwe. Baada ya Nyembo kukichukua kile kibuyu cha uchawi kutokana na kusoma maelezo ya kile kibuyu yalikuwepo kwenye

shajara[8] ya marehemu Mzee Mtandi akakifukua kile kibuyu chini ya kitanda na kwenda nacho chooni kwa ajili ya kukichezesha ili ndugu zake waachiwe na wachawi. Nyembo alipokuwa kule chooni akikichezesha kile kibuyu Kaguba akawa anapiga makelele anakufa kwa sababu Kaguba ndio alikuwa kiongozi wa wachawi na ndiye aliyekuwa akikitegemea kile kibuyu.

Nyembo anapokuwa anaendelea kuchezesha kile kibuyu ndipo marehemu Mzee Mtandi na Nyanzala wanatoka mikononi mwa wachawi kule makaburini na kuja nyumbani kwa marehemu Bi Masonganya na kujificha chini ya uvungu. Wakati haya yote yakiwa yanaendelea na wale wachawi waliokuwa wakicheza makaburini muda si mrefu wakawa wanakuja nyumbani kwa marehemu Masonganya wanamtokea Kaguba na kutaka kumnyang'anya kile kibuyu. Kwa bahati mbaya walikuta tayari Mzee Mtandi kampokea. Nyembo akatoka nje kuwapokea na kuwaamrisha wakae chini. Mtunzi anasema:

> "KAA CHINI MWANGA MKUBWA WE!" Nyembo aliwakodolea macho Binti Sambayu aliyekuwa amesimama akitaka kukimbia… ikabidi nyembo aliyekuwa amewasimamia wale wachawi pale uani ampe ishara nyingine Mzee Mtandi akiwa kule msalani ili aendelele kutoa kiminyo. Naye bila ajizi akaianza kazi ile iliyozua tabu kwa wachawi wale. Walitabika vilivyo, inaonekana kiminyo kiliwazidia mpaka baadhi kutapika, huku wengine wakitokwa na haja ndogo na kubwa palepale ikiwa ni ishara mbaya kwa mchawi yeyote akikamatwa (uk 83).

Kupitia mandhari hii na matukio ya kutisha yaliyokuwa yakitokea mwandishi anachimuza maudhui ya kutokuwaonea watu wasio na hatia. Kwa sababu kuna siku wewe unayewaonea watu au unayewatesa watu utakuja kufa au utakuja kuteseka hapa hapa duniani na wale uliyokuwa unawafanyia vibaya watakushuhudia pia. Kupitia mandhari hii tunajifunza kwamba mwenyezi Mungu pia hashindwi na wachawi kwani hata wachawi nao watakufa tu. Pia kupitia mandhari hii hii na matukio haya haya mtunzi anachimuza mgogoro unaoibuka kati ya wananchi na serikali kwa kutokuamini mambo ya uchawi. Serikali nyingi duniani haziamini mambo ya uchawi ndio maana hata wananchi wanapomkamata mchawi huamua kujichukulia sheria mkononi ya

8 Shajala ni kitabu cha kutunzia kumbukumbu mbalimbali

kumuua. Kwa sababu wanaona serikali haiamini mambo ya uchawi na hakuna hatua zinazochukuliwa ndio maana wananchi wanajichukulia sheria mkononi.

**3.6 Maswala Ibuka ya Kiutunzi na Kiufasiri**

Katika sura hii tumeangazia kipengele cha mandhari na matukio ya kijiniuchawi na ushirikina yalivyowasilishwa na kuwezesha kuchimuzwa kwa dhamira na maudhui mbalimbali mseto katika riwaya za *Vita vya Mapenzi*, *Mzimu wa Waufi na Tanzia*. Kikubwa zaidi tulichokibaini ni kwamba riwaya hizi zote zimefumwa kuwasilisha matukio ya kawaida yanayowasilishwa na kusawiriwa kwa njia za kiajabu na kwa hivyo kuibua upekee, upya na uajabu. Kwa usemi mwingine, matukio ya kiajabu yanawasilishwa kama matukio ya kawaida, matukio ya mazoea, na matukio ya kila siku yanawasilishwa kwa njia za kiajabu. Ni mawasilisho ya hadithi za watu wa kawaida katika harakati zao za kawaida ila ni kwamba hadithi hizo zimenyunyiziwa vipengele vya kiajabu, wasifu wa kiajabu na utukiaji wa kiajabu. Kwa mfano, katika riwaya ya *Vita vya Mapenzi* kuna serikali ambayo iko chini ya bahari na inaongozwa na raisi jini ambaye kwa maslahi yake binafsi anamchagua kiongozi anayemtaka yeye mwenyewe ili aweze kuficha maovu yake na wananchi anaowaongoza huko chini bahari wanamkataa wanamtaka kiongozi wao. Aidha kiongozi huyu anatumia mabavu na kumfukuza yule kiongozi ambaye wananchi wanampenda ambaye ni Mzee Sufian.

Kwa upande mwingine mambo haya ya kiajabu yanawasilishwa na kuhusishwa na wahusika kama mambo ya kawaida. Katika riwaya hizi muonoulimwengu unaojitokeza unashirikisha miujiza, vizuka, wafu wanaofufuka kutoka makaburini usiku na kurudi asubuhi nyumbani katika riwaya ya *Tanzia* mfano mzuri ni Mzee Mtandi na nyanzala walifufuka na wakati walisha kufa na kuzikwa makaburini, haya yanawasilishwa kama mambo ya kawaida. Mtunzi wa riwaya hizi za kihalisiajabu ameyawasilisha mambo ya kawaida kwa njia za kiajabu na mambo ya kiajabu kwa njia za kawaida. Utambuzi huu umetuwezesha kuchambua jinsi mandhari na matukio mbalimbali ya kijiniuchawi na ushirikina yalivyoweza kuchimuzwa katika riwaya hizi na kutupatia maudhui mbalimbali. Tumebaini kuwa mandhari na matukio ya kijiuchawi na ushirikina yaliyochimuzwa katika riwaya hizi yamechangia pakubwa kukuza na kuendeleza

maudhui mbalimbali yanayopatikana katika riwaya hizi na jamii ikajifunza mambo mbalimbali kama vile athari za uongozi mbaya, athari za utandawazi katika mataifa ya Afrika, dhamira za usaliti katika maisha, athari ya migogoro ya kisiasa katika mataifa ya ulimwengu wa tatu, madhara ya wanasaisa kuingilia taaluma za watu katika utendaji wa kazi serikalini, madhara ya wananchi kujichukulia sheria mkononi, uwajibikaji katika utendaji kazi, mila na desturi mbalimbali zinavyoathiri utendaji haki, ujadi na usasa vinavyopingana, migogoro ya kifamilia, ukoo na kadhalika

Tumebaini kuwepo kwa umiujiza katika utunzi wa riwaya hizi unaojibanisha kutokana na uwasilishaji wa mambo ya kawaida kwa njia za kiajabu au mambo ya kiajabu kwa njia za kawaida. Huu ni ufundi na ustadi wa kiutunzi unaoasharia, kwa upande wa Maundu Mwingizi, utambuzi wa kuweko kwa uhalisi na ukweli katika ulimwengu halisi, kwa hivyo riwaya hizi za kiuhalisiajabu zimejaribu kuuwasilisha uhalisi huo na sio kuupotosha, zimeonyesha uwezekano wa kuwa na nguvu za kiajabu juu ya maswala ya kawaida ya kimaumbile, maswala ya kawaida ya michakato ya mahusiano ya kinafsi, kijamii na kisiasa, zimefanikiwa kuingiza umiujiza katika mambo haya ya kawaida. Kwa kuwa riwaya hizi zina wasifu wa kustaajabisha, kushtukiza na kushangaza kwa njia zinazopembeza kuaminika kwa matukio na wahusika, hata kama ni kwa dakika chache tu, lakini katika ujumla wake hii ni mikakati ya kiuchimuzi anayoitumia mwandishi kufikisha sio tu ujumbe bali pia fikira zake kwa jamii.

Kwa upande mwingine, tunaweza kuhoji kwamba, Mwingizi amefanikiwa kuuwasilisha uhalisi kwa mitindo isiyo ya kawaida. Hii ina maana kwamba pamoja na kuwepo kwa uhalisiajabu katika riwaya hizi za kimajaribio na za uhalisiamazingaombwe, uhalisi unakuwepo pia kwa kiasi kikubwa. Kwa mfano katika riwaya ya *Vita vya Mapenzi* mtunzi anatumia uhalisia pale anapowatumia mawaziri mbalimbali ambao wapo mamalakani na wanashirikiana na majambazi katika kuhujumu uchumi wa nchi. Msuko wa kawaida wa utunzi wa matukio mahususi unakitwa katika ulimwengu halisi na unakuwa ni juu ya mambo ya kawaida katika ulimwengu halisi lakini chini ya mawasilisho hayo ya kawaida, mtunzi amafuma uajabu na miujiza. Umiujiza

unajichomoza mara kwa mara katika matukio ambayo ni ya kawaida kiasi cha kuingiza hisia za kuamini na kutokuamini wakati huo huo. Kwa vyovyote vile, uhalisi kama unavyojulikana katika ulimwengu razini umetawala sehemu kubwa za riwaya hizi za kiuhalisiajabu.

Hata kama sura hii kwa kiasi kikubwa imejikita katika kuangazia mandhari, haijafungia macho kuibuka maswala mengine ibuka ya kiutunzi kama mahusiano yaliyoko kati ya miujiza na uhalisia. Kukutanishwa kwa mbinu hizi mbili kuna maana kwamba, riwaya za Maundu Mwingizi za kiuhalisiajabu zimedhihirisha kuwa na ukunjufu wa kuingiza uwezo wa kuamani kutukia kwa mambo ya kiajabu katika mambo na michakato ya kawaida, vilevile zimewesha kuamini mambo yasiyowezekana au yasiyoonekana katika ulimwengu razini unaoshawishiwa na usahihi wa kisayansi na uhalisi kama vile serikali ya budha chini ya bahari katika riwaya ya *Vita vya Mapenzi*. Hali hizi zimewezesha kubainika kwa usambamba wa mitazamo, kwa mfano uwepo wa mandhari dhahiri za kijiografia sambamba na mandhari za kinjozi, vilevile uwepo wa usambamba wa kaida zisizoelezeka kwa urahisi kama vile usafiri wa kutumia pete katika riwaya *Vita vya Mapenzi* na wizi wa mimba, mimba kuhawilishwa kutoka kwa mwili wa mwanamke mmoja hadi kwa mwanamke mwingine katika riwaya ya *Mzimu wa Waufi*.

Aidha, kiutunzi tunabaini kwamba, Mwingizi amechangia kiutekelezi uelewa wa mahali pa matukio, mahusiano na mitagusano ya watu, hali kadhalika mahali pa usawiri wa wahusika katika riwaya za kiuhalisiajabu kuwa ni kipengele cha kimsingi katika kusadikisha matokeo. Hii ina maana kwamba, hadithi za kihalisiajabu zinaweza kukitwa mahali popote. Kwa mfano, katika riwaya ya *Tanzia* kuna mahali dhahiri pa kijiografia, sehemu za nchi mijini na mashinani, misituni, barabarani, makaburini, hospitali, nyumbani kwa watu na vijumbani mwa watu. Lakini kitu kinachoibua uajabu ni angahewa au umazingira (*atmosphere*) wa mahali hapo pamoja na vidokezo vya maana halisi ya mahali. Katika riwaya hizi za Mwingizi angahewa na umazingira wa mahali unapambwa na uajabu ajabu. Hali hizi za mahali zimewezesha kuaminika kwa wahusika kwa maana kwamba wanaojitokeza katika riwaya za Mwingizi ni watu wa kawaida,

watu kama tunavyokutana nao katika hali za kawaida. Lakini kama ilivyo katika ulimwengu razini, watu katika riwaya za kihalisiajabu wana wasifu na hulka, lakini katika ujumla wao mtunzi ameingiza katika wasifu wa wahusika tabia, hulka na mienendo ya kiajabu, waangalie Sufiani katika riwaya ya *Vita Vya Mapenzi,* Hunudu katika riwaya ya *Mzimu Wa Waufi* na Bi Masonganya katika riwaya ya *Tanzia*.

Maswala mengine ambayo yameibuka, japo yatajadiliwa kwa kina baadaye ni pamoja ujitokezaji wa vipengele vya kiajabu. Riwaya hizi za Mwingine kama riwaya za kihalisiajabu zimeweza kuingiza katika misuko yao na usawiri wao wa wahusika wasifu au vipengele vya kiajabu na vya kutisha vinavyojumuisha matukio, matendo na ndoto za kiajabu. Vipengele hivi vya kiajabu vimeweza kujumuisha utosahihi au utodhahiri wa mpito wa wakati, uajabu wa matukio—kwa mfano, vurugu ndani ya kaburi lilijifunga, utingishaji wa vibuyu unaosababisha matokeo yasiyo razini, pamoja na tabia za ajabu za wahusika.

Pia pasina kuwepo kwa vipengele vya kiajabu hadithi haiwezi kuwa ya kihalisiajabu. Vivyo hivyo, riwaya hizi zimetuwezesha kubaini nafasi na uamili wa msuko katika riwaya za kiuhalisiajabu kwamba, kwa kawaida hadithi inasawiri matukio ya kawaida ya kila siku lakini yaliyonyunyiziwa vitushi vya kiajabuajabu. Pengine uajabu huo, kama ilivyodhihirika katika riwaya hizi, unahusiana na ubainikaji na udhibiti wa wakati. Katika hadithi za kiuhalisiajabu, kwa mfano katika riwaya ya *Vita vya Mapenzi*, wakati ni kitu kinachoyeyushwa na kuyumbishwa, wakati haufuatani kwa mfululizo wa moja kwa moja kwenda mbele, na hauna lazima ya kwenda mbele moja kwa moja. Inawezekana wakati ukasawiriwa kwenda nyuma au kutoka uzeeni kwenda utotoni kama ilivyo katika riwaya hizi teuleza Mwingizi.

Wakati, unapoangaliwa kwa mitazamo ya kale na sasa umeweza kuwasilishwa kwa usambamba wa sasa na kale, na mstakabali—yaani siku na miaka ya usomi, inaweza kutokea sasa au hata jana. Uhamishaji na usogezaji wa wakati katika msuko wa hadithi mara nyingi huakisi uhalisi ulio nje ya uhalisi wa kawaida. Hii ndio maana inakuwa

rahisi kuwa na uwasilishaji wa mapepo na mazimwi kwa mkabala wa wakati unajirudiarudia, wakati usiopiga hatua kwenda mbele. Kwa mitazamo mingine wakati ni kila kitu katika uhalisiajabu. Kwa misngi hii riwaya za Mwingizi zimedhihirisha mchukuano mzuri wa kiwakati, kitabia, kihali na kimwelekeo katika uwasilishaji wa matukio—ukuzaji wa wasifu pasipostahili na ubanaji wa wasifu panapostahili. Hali za kuandika zinaweza kuhusishwa na mchukuano.

Hata kama jambo hili litajitokeza tena baadaye katika tasnifu hii, tunaweza kuligusia tu hapa kwamba riwaya teuleza Mwingizi zimedhihirisha mtindo wa kiubunifu unaoaminika. Kimsingi lugha ya kiubunifu iliyotumika katika riwaya za kihalisiajabu za Mwingizi, ni lugha ya kifasihi, lugha iliyonakishiwa mapambo yanayokuza hadithi hadi kuifikisha katika kiwango cha kimiujiza. Katika hali kama hizi mtunzi hatoi maelezo kuhalalisha usahihi, uhalisi au uaminikaji wa usababishi wa matukio, matokeo au hata usawiri wa wahusika. Hadithi inakua kwa kufuata mantiki yake yenyewe kama kwamba hakuna mambo ya kimiujiza yanayojitokeza katika hadithi. Kwa kiasi kikubwa usimulizi unaojitokeza umekuwa ni wa nafsi ya tatu ambapo mtunzi kupitia kwa umahiri wake amewawezesha wasomaji kubaini hulka na hata fikira za wahusika na ndoto zao. Pamoja na kwamba uajabu na umiujiza inaweza kuachwa hivyo bila maelezo au uhalalishaji, ni sharti hadithi yenyewe iwe na mantiki inayoongoza jinsi mambo ya kihalisi na kimiujiza yanavyojitokeza, sharti kuwe na mantiki ya jinsi wahusika wanavyohusiana, jinsi matukio yanavyoingiliana bila kuzua ukinzani.

Swala lingine linalohitaji kuangaziwa linahusiana na uwepo au kutokuwepo kwa sadfa au utukizi. Uelewa wa kijumla uliopo katika tungo za kihalisiajabu unadai kwamba ni nadra sana kuwepo na sadfa au utukizi katika riwaya za kihalisiajabu kwa sababu matukio yote huwa yamefumwa kwa mtindo tata na changamano hivi kwamba yanashikanishwa kwa mduara wa aina fulani kuyafikisha katika hatima ya hadithi. Kwa sababu hii, matukio yajitokezayo kote hadithini si majaliwa, japo pia yanaweza yakawa si tofauti na majaliwa. Sharti pawe na uzi unaoishikanisha hadithi yote, unaofungamanisha matukio yote, unaoshikanisha na kuhusisha wahusika wote, kama

inavyodhihirika katika *Vita vya Mapenzi.* Matukio ya awali yanashawishi matukio ya sasa na ya baadaye, lakini pia matukio katika mstakabali yanaweza kushawishi matukio yaliyopita. Hii ina maana kwamba mambo yote yaliyo katika utungo wa kihalisiajabu yanayosiana kwa namna moja au nyingine. Hata yale mambo yanayochukuliwa kuwa duni yana maana katika mfumo mzima wa hadithi hivi kwamba yanasaidia kujenga udokezaji ambao hatimaye unawezesha kuaminika.

Kwa jumla, riwaya za Mwingizi zimefumwa kwa ustadi hivi kwamba, pamoja na kwamba matukio, wahusika na mifanyiko yote katika hadithi hizi za kiuhalisiajabu inaweza kuonekana kuwa duni, kazi hizi zinaibua maana kubwa, maana yenye umuhimu mkubwa, maana inayoweza kuashiria kwamba ulimwengu wote na binadamu wote wameunganishwa kimaisha. Kwamba kuna sababu razini za uwepo wa maisha na hivyo hivyo uwepo wa binadamu. Kuna werevu, ustadi na upambanuzi katika kuwasilisha maana katika uhalisiajabu, kama ambavyo amefanya Mwingizi. Katika usomaji wa riwaya hizi tumebainikiwa kwamba uhalisiajabu ni mfumo fumbati wa kiutunzi, ni mwelekeo wa kuangalia na kudadisi uhalisi kwa kutumia njia na mitindo pendwa ya kiutunzi (*popular forms*) au kwa kutumia mitindo na njia za kiasasi (*cultured forms*), au mitindo na njia zilizonakishiwa sana (*embellished forms*) au kwa kutumia miundo ya kishamba au miundo ovyoovyo (*rustic styles*). Katika uhalisiajabu mtunzi huukabili uhalisi na kujaribu kuurahisisha na kuuweka wazi kueleweka, hujaribu kufumbua na kugundua miujiza iliyoko katika vitu, katika maisha na katika matendo ya binadamu. Uhalisiajabu haubuni ulimwengu mbadala ila unajaribu kugundua mahusiano ya kiajabu yaliyoko kati ya binadamu na hali anamoishi. Hivyo basi riwaya hizi zimeweza kutumia mandhari ya kiajabu na ya kutisha katika kuchimuza mambo halisi yanayofanywa na binadamu maishani mwake.

# SURA YA NNE

# USAWIRI WA WAHUSIKA WA KIJINIUCHAWI NA KISHIRIKINA KAMA MKAKATI WA UCHIMUZI KATIKA RIWAYA TEULE ZA MWINGIZI

## 4.1 Utangulizi

Sura hii inachunguza na kujadili jinsi usawiri wa wahusika mbalimbali wa kijiniuchawi na ushirikina wanavyopelekea kuibua na kuendeleza maudhui mbalimbali katika riwaya teule za Maundu Mwingizi. Wahusika wanaoangaziwa na kujadiliwa hapa wanaangaliwa kuwili. Kwanza kama wahusika kwa mtazamo wa uelewa wa majukumu ya wahusika katika riwaya za jadi na pili kama wahusika wa kijiniuchawi na ushirikina wanaobeba majukumu yanayoakisi matukio ya kihalisiajabu. Hii ni kutokana na jinsi walivyochimuzwa na kupelekea kuwepo kwa maudhui mbalimbali katika riwaya zilizochunguzwa katika utafiti huu.

Wahusika wanaojitokeza katika riwaya hizi za uhalisiajabu ni watu wa kawaida, watu wastani katika shughuli na harakati zao za kila siku. Watu hawa hata hivyo, ni watu wenye nafsi mahususi, haiba tabia na hulka bainifu. Ni wahusika walio na majina binafsi, hulka na historia za familia au koo zao. Si neno kama mhusika anayeangaziwa ni nguli au ni wahusika wajenzi, bado wana wasifu huo wa nafsi, haiba, tabia na hulka. Lakini zaidi ya kuwa na wasifu huu wa kawaida, wahusika hawa katika riwaya za Maundu Mwingizi wamenyunyiziwa uajabu na uhalisiajabu ulio nje ya wasifu wa kawaida wa binadamu. Kwa njia hizi wahusika hawa wamekuzwa kuwa wahusika wa kiishara, wahusika kielelezoasilia (*archetype*). Kiutekelezi wahusika hawa wanaashiria sifa, uhalisi na mitagusano ya ki binadamu, hata pale ambapo inabainika kwamba hawajakuzwa kisaikolojia, kusawiriwa kama viumbe wasiowezekana, bado wanaweza kuashiria na kutekeleza majukumu yao ya kifasihi.

### 4.2 Uchimuzi katika Uhusika

Uhusika ni umithilishaji wa vitendo vya viumbe wa hadithini na viumbe katika ulimwengu razini. Wamitila (2003) anasema uhusika ni dhana au istilahi ambayo hutumiwa kuelezea mbinu na mikakati inayotumiwa na mwandishi kuwasawiri wahusika katika kazi yake. Baadhi ya waandishi ambao hutilia mkazo swala la uhusika huwa wanaamini kuwa jambo lililo na uzito na maana katika fasihi ni jinsi matukio yanayopatikana katika kazi yanavyowaathiri wahusika. Athari hiyo huwa na matokeo mengi kuhusu mikabala yao sambamba na matukio yaliyotokea. Hivyo basi, riwaya za kimajaribio zinakiuka mipaka ya urazini au kwamba, mipaka hii ya urazini inayumbishwa na kupembezwa na kwa njia hiyo kuwezesha usawiri mbadala wa wahusika ambao wasifu wao, nafsi, haiba, tabia na hulka zao pamoja na kuakisi wasifu wa ki binadamu, huwa na wasifu wa kiajabu wa ziada. Ndio maana katika riwaya za Mwingizi tunaona usambamba wa wahusika majini, paka na wachawi ambao wapo kwa wingi kuliko wahusika wa kawaida. Mtunzi amewatumia wahusika hawa katika kuondoa ule uzoefu wa kawaida na kutupeleka mbali katika kufikiria kwa kina nini mtunzi alikusudia kupitia wahusika hao wa kihalisiajabu katika kufikisha ujumbe wake kwa jamii.

Mwingizi amewatumia wahusika mbalimbali katika riwaya hizi teule ambapo kupitia uhusika wao amehusianisha na uashiriaji na kwa hivyo wameweza kuchimuza maudhui mbalimbali. Wahusika hawa wamekuwa nyenzo mmuhimu katika kusukuma mbele riwaya hizi za kimajaribio kulingana na uhusika wao na jinsi walivyosawiriwa kuakisi hali halisi za kiuhalisiajabu. Wahusika ni viumbe ambao japo wamekiuka mipaka ya urazini wanakusudiwa na mtunzi wa kazi hizi za fasihi ya kimajaribio wawasilishe dhana, mawazo, falsafa, tabia au mwonoulimwengu wa watu katika kazi hizi. Njogu na Chimerah (1999:45) wanasema wahusika ni sehemu ya fani na ni viumbe wa sanaa wanaobuniwa kutokana na mazingira ya msanii ambayo yanaweza kuwa ya kijiografia, kihistoria, kijamii, kitamaduni au ya kisiasa.

Japo kauli za Njogu  na Chimerah zina mashiko kwa mujibu wa ufahamu wa riwaya za jadi, katika riwaya za kimajaribio wahusika wake huwa hawabuniwi na kusawiriwa katika misingi ya vigezo hivyo hivyo, wanabuniwa katika miktadha, mazingira na nyakati zilizoyumbishwa na kukiuka mipaka ya urazini kwa sababu huwa wanakuwa sio wahusika wa kawaida. Hii ni kwa sababu wengi wao mbali na kuwa wahusika katika mazingira halisi, huwa pia ni wahusika katika mazingira ya ndotoni, viumbe katika fikira zilizo katika upeo wa uwezekano, mazingira ya uhayawani, ushetani, umaruerue, uchawi na ushirikina na umajini. Wahusika hawa wote wametokeza katika riwaya za Mwingizi wakivunja mipaka ya uhalisia na ukawaida.  Njongu na Chimerah (khj) wanaendelea kusema wahusika ni viumbe wanaopatikana katika kazi ya kifasihi, wanaotambulishwa na mhusika au msimulizi na huwakilisha sifa tofauti zinazobainika kupitia kwa matendo yao. Na kwamba dhima kuu ya wahusika hao katika kazi ya kifasihi ni kuwasilisha ujumbe wa mwandishi kwa kushirikisha matendo yao, hisia zao, ndoto na matamanio, mazungumzo na mawazo yao.

Tunaona wahusika wengi wa Mwingizi wamedhihirisha kwa upande mmoja sifa za ki binadamu na kwa upande mwingine sifa zisizo za kibinadamu wana sifa kama vile za kiunguungu zinazowawezesha wahusika hawa kuingia na kutoka katika ulimwengu razini na ulimwengu wa njozi, kuvuka mipaka inayopembeza uhalisi katika kuwasilisha tabia na matendo ya  binadamu. Wahusika hawa wa kihalisiajabu katika riwaya za Mwingizi wamekuwa ni nguzo kuu ya kusukuma hadithi mbele kinafsi, kiwakati, kimtazamo na kipahali.

Wamitila (2008:369) anafafanua kwamba, wahusika ni nyenzo kuu ya fasihi kwa sababu wao ndio dira ya matukio na matendo yanayopatikana katika kazi ya kifasihi inayohusika. Mtazamo wa dhana ya wahusika hutofautiana kutegemea mkabala anaouchukua mhakiki na nadharia ya fasihi inayohusika.  Kwa hivyo, “Mhusika ni mtendaji katika kazi ya kifasihi na huwa kielelezo cha viumbe wanaopatikana ulimwenguni ingawa si lazima sifa zote za mhusika zifungamane moja kwa moja na za wanadamu zinaweza zikafungamana na mizimu, majini, wanyama na hata viumbe

visivyo na uhai. Wahusika wanaosawiriwa wakiwa na zaidi ya wasifu wa binadamu au wasifu wa ulimwengu razini, wanakusudiwa kuonyesha sio tu ulimwengu mbadala, bali pia utendaji mbadala unaowezesha kubainika kwa ufahamu mbadala. Huu ndio uhalisi unaojitokeza katika riwaya za Mwingizi na kwa hivyo, msomaji hana budi kujiuliza wahusika wa aina hii wanachimuza nini.

Wamitila (khj) anaendelea kusema kuwa mhusika wa kihalisia husawiriwa kwa kuzingatia kanuni ya maisha halisi yaani, hutegemea kanuni ya ushabihikweli. Tunapowaeleza wahusika kama 'binadamu wa hadithini' huwa tunaegemea kanuni hii. Mhusika wa kihalisia ana sifa nyingi zinazohusishwa na binadamu katika maisha ya kila siku. Lakini, mbali na uwepo wa wahusika wa kihalisi, vilevile katika tungo za kifasihi huweza kusawiriwa mhusika wa kinjozi ambaye anahusishwa kwa kiasi na njozi au fantasia. Mhusika wa aina hii hupatikana katika ulimwengu wa ajabu au wenye sifa za ulimbwende anapoingiliana na viumbe wasiokuwa wa kawaida kama ilivyo katika riwaya za Mwingizi. Huyu ni mhusika wa kufikirika katika ulimwengu wa njozi na ndoto, mhusika katika misingi ya uwezekano. Sifa anazopewa mhusika huyu, ziwe nzuri au mbaya hukuzwa kuliko kawaida ya wahusika kihalisi. Wahusika hawa wa kinjozi hutumiwa kueleza na kuwasilisha fikira na uwazaji wa kiwango cha juu cha matukio yasiyokuwa ya kawaida. Dhana ya uhusika wa kinjozi na usawiri wa wahusika wa kinjozi ni pana mno na huweza kujumuisha bunilizi za kisayansi na kazi za kiuhalisiajabu (ambazo zinahusishwa na matukio yasiyokuwa ya kawaida na bila kutoa sababu za kutokea kwake).

Katika riwaya hizi za kimajaribio za Maundu Mwingizi, mtunzi ametumia usawiri mseto kuwabuni wahusika wake ambapo amechanganya wahusika halisi kama wanavyoweza kumithilishwa na vitendo vya ulimwengu razini, kuna wahusika wanaosawiriwa kuwili—kama binadamu razini na kama binadamu mwenye uwezo wa kiungu ungu—yaani wale wahusika wa kimazingaombwe au kifantasia. Wahusika hawa wanabadilika kutoka wahusika halisi na kuwa wa kiuhalisiajabu. Katika mabadiliko haya, mtunzi anajenga mtagusano wa maingiliano ya ulimwengu wa kihalisia na

ulimwengu wa kifantasia, ulimwengu wa kufikirika na ulio katika upeo wa uwezekano. Usawiri wa jinsi hii ndio unaomwezesha Mwingizi kuzungumzia milki na makazi chini ya bahari, uwezekano wa kuibwa kwa mimba na kufa kufufuka kwa mtu kana kwamba hilo ni tukio la kawaida. Kwa hivyo, matukio mengi ya kiuhalisiajabu, kwa kadri alivyoyabuni Mwingizi, yanatendeka wakati mhusika anapolala na anapokuwa yumo ndotoni na mengine yanatendeka mhusika akiwa macho.

**4.3 Uainishaji wa Wahusika na Uchimuzi katika Riwaya Teule za Mwingizi**

Katika riwaya teuleza Mwingizi, kuna ujitokezaji wa makundi mawili ya wahusika wa kiuhalisia na kuna wahusika wa kiuhalisiajabu au kifantansia. Yaani mhusika wa kihalisia anabadilika na kuwa jini. Katika riwaya ya *Vita vya Mapenzi* wahusika wanakuwa binadamu halisi na kuna wakati wanakuwa wahusika wa kiuhalisiajabu yaani majini au wenye nafsi mbili. Mfano wa wahusika wa aina hii ni Suhail, Mzee Sufian (aliyekuwa kiongozi mkuu wa himaya ya *Budha*), Shekhia na Takadir. Wahusika halisi miongoni mwao ni Kenjah, Joramu, Msigwa, Gosh, Miti, Mwita, Amanda, Waziri Mkuu na Wazazi wa Suhail.

Vilevile katika riwaya ya *Mzimu wa Waufi* kuna wahusika wa kihalisiajabu wenye nafsi mbili. Wahusika hao ni Hunudu, Masumbuko, Ngulunzila, Nyamizi, majini na mizimu ya Waufi, mizimu ya Waswezi. Wahusika hawa wote matukio yao hutendeka ndotoni na wengine ni majini na wachawi, na kuna wakati wanajibadilisha na kujifanya binadamu wa kawaida na kuna wakati wanakuwa ni majini. Wahusika halisia wa riwaya ya *Mzimu Wa Waufi* ni Mzee Kikoko, Jabu, Kagomba na Kishindo hawa ni baadhi. Katika riwaya ya *Tanzia* wahusika wa kihalisiajabu ni Kaguba, Bi. Masonganya, Binti Sambayu, Bi Kibena, Nyembo, Gao, Nyanzala, Mtandi na wahusika halisi baadhi ni Dereva, Mama Kaguba, Lubumbi. Mtunzi kwa kiasi kikubwa amewatumia wahusika wa kihalisiajabu na kuchanganya kwa kiasi kidogo wahusika wa kihalisia ili kutufanya tuamini kwamba mambo yanayotendeka katika mazingira ya kutisha na kuogofya yaliyoambatana na wahusika wa kiajabu. Kwa hiyo, Mwingizi ametumia wahusika wengi wa kiuhasiajabu

yaani wahusika wa kimajini, kindoto, kichawi na wa kawaida kwa kiasi kidogo, katika kuchimuza maudhui mbalimbali.

### 4.3.1 Uchimuzi wa Dhamira kwa Mkabala wa Wahusika wa Kijiniuchawi na Ushirikina katika Riwaya ya *Vita vya Mapenzi*

Katika riwaya hii ya *Vita vya Mapenzi*, Mwingizi amewasawiri wahusika wa kiuhalisia na wahusika wa kiuhalisiamazingaombwe. Usawiri wa wahusika hawa umekitwa katika matukio mengi ambayo yanatendwa na wahusika wakati wanapokuwa usingizini na mhusika anapokuwa yumo ndotoni au katika hali halisi, wahusika hawa wamechimuza sifa za kiajabu au za kifantansia mfano mhusika Sufian, Suhail, Shekhia, Atrash, Amanda. Pia mwandishi amewasawiri wahusika wake kwa kuvuka mipaka ya kijamii, kitaifa na kimataifa. Mfano wa wahusika hao ni Mzee Sufian akiwakilisha nchi ya Yemen, Joram Ndege alinakilisha nchi ya Uganda na Adams Gosh anawakilisha Ulaya. Vilevile anawataja wasaidizi wa Mzee Sufian kama watu wenye asili ya kiasia na wenye hulka za kijini, aidha wahusika hawa wamechimuza maudhui mbalimbali yanayogusa na kuichanganua jamii kwa njia anuwai na kuhusisha kadhia zinazotendeka katika maisha ya mtu kama kioo cha kumulikia maisha ya jamii pana. Katika mjadala ufuatao, tunahoji kwamba mtunzi wa riwaya hii amewasawiri wahusika kwa njia changamano yenye mwingiliano mseto wa uhalisia na uhalisiajabu ili kuwawezesha kuchimuza maudhui changamano yanayojibainisha kwa njia mbalimbali katika riwaya hii ya *Vita vya Mapenzi*. Wahusika hawa wameweza kusawiriwa na kuchimuza dhamira mseto mbalimbali.

#### 4.3.1.1 Uongozi, Usaliti, Maadili, Haki na Sheria, Ukatili, Mafao binafsi, Uwajibikaji, Mifumo ya Kiutawala na Utandawazi

Ili iweze kueleweka jinsi ambavyo maudhui haya yanavyojitokeza na kudai kuwepo katika riwaya teule za Mwingizi, kwanza kuna haja ya kuelewa na kubaini mahusiko ya taswira na ishara katika riwaya hizi za kihalisiajabu. Taswira na uashiriaji kwa jumla ni mbinu ya kimsingi inayotumika katika utunzi wa kazi za kihalisiajabu inapozingatiwa kwamba, usawiri wa mambo yasiyoeleweka, uelezaji wa kina wa mambo yenye uajabu,

na uibushaji wa mandhari za kihalisi na za kinjozi pamoja na mapito na utangamano na mandhari hizo, ni mambo ambayo ni sharti yawasilishwe kwa njia au kwa undani wa kimaelezo unaoaminika. Kwa hivyo, utumiaji wa lugha kwa undani kuibua mambo ya kiajabu, kuibua mifanyiko ya kiakili na kinjozi au kuibua ulimwengu tamanifu, ni sharti yaegemezwe katika taswira na ishara. Vivyo hivyo, usawiri wa wahusika unaegemezwa kwa misingi hii hii ya taswira na ishara.

Katika riwaya ya *Vita vya Mapenzi*, mhusika Suhail amesawiriwa kama mhusika aliyebeba dhamira mbalimbali changamano yaani ni binadamu ambaye ni nusu jini, sifa hizo zinazochangiana, zinazokinzana na zinazoshindana. Hii ni hali inayoonyesha kwamba, katika ubanifu wa maisha ya mtu binafsi, kuna mitagusano ya mambo chungu nzima, maswala ya kibinafsi yakiathiriwa au kushawishiwa na maswala ya kijamii na kiulimwengu. Huu ndio uhalisia wa maisha.  kwa mfano, kwamba litendekalo Tabora, Marekani, Uarabuni au Dar es Saalam, lina nafasi katika maisha ya Suhail, si hoja kama ni nafasi chanya au hasi. Pia mhusika huyu, anapochanganuliwa kwa kina, utukiaji wa matukio katika maisha yake unabainisha matukio yanatendeka akiwa ndotoni na pia akiwa uhalisiani.

Mtunzi anaonyesha kwamba usawiri wa aina hii unaweza kufasirika kwa njia kadha wa kadha. Matukio ya ndotoni yanaweza kuchukuliwa kuashiria ama matamanio ya mtu binafsi au mambo yaliyo katika ulimwengu wa uwezekano au ulimwengu wa kufikirika. Kwa upande mwingine, matendo ya uhalisiani yanachochea vigezo vya urazini, kukadiria uwezo, ari na juhudi za mtu binafsi katika ulimwengu wa mashindano mduara. Kwa misingi hii, Suhail kama mhusika aliyesawiriwa kuanzia mwanzo wa riwaya mpaka mwisho wa riwaya anahitaji kuangaliwa kuwili, Suhail wa urazini na Suhail wa ndotoni. Hii ndio maana kupitia usawiri wake, mhusika huyu amechimuza dhamira mseto kama vile usaliti, uongozi, maadili, haki na sheria, ukatili, mafao binafsi, uwajibikaji na mifumo ya kiutawala.

Mwanzoni mwa riwaya mwandishi, anamuonyesha Suhail akiwa katika ulimwengu halisi, anatuonyesha amemaliza masomo katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kasha anarudi kwao Tabora. Akiwa ndani ya basi amekaa kwenye kiti, kwa pembeni Mzee mmoja wa kiasia anamwangalia mara kwa mara ndipo Suhail anapatwa na hasira kwa sababu huyo Mzee anamwangalia kama anayemkagua kwa dhamira fulani. Anaamua kuchukua miwani mieusi kuvaa ili asiendelee kumwangalia. Baada ya kuvaa miwani akaona anaendelea kumwangalia ndipo akaamua kuchukua "ipad" yake na kuchomeka visikilizio masikioni ili asiendelee kumuangalia na akaamua kuwa *Bize* na muziki tu. Mwandishi anasema:-

> ….kijana wa kiti namba kumi alijisahau kabisa kuwa alikuwa safarini pamoja na jumuiya ya wasafiri wengine, akili yake ikiwa imechotwa kabisa na muziki aliokuwa akiusikiliza kutoka kwenye *ipad* yake, na akiwa katikati ya dunia yake ile ya pekee akitumbuizwa na muziki mororo huku akiwa amefumba macho kwa raha zilizomzonga, alishtushwa na mkono laini uliomshika huku ukimtikisa begani (uk 2).

Suhail anafananishwa na vijana wasiokuwa na heshima na wenye dharau kwa sababu kitendo cha kutazama halafu unafanya dharau ya kuvaa miwani mieusi na kuweka visikilizio masikioni ni ishara tosha kabisa ya dharau dharau kwa watu waliokuzidi umri. Vivyo vivyo hata kwa vijana wengi waliobahatika kuelemika mpaka chuo kikuu, wamekuwa na dharau sana hasa kwa jamii inayowazunguka na kwa wakubwa wao kwa kujifanya wamestarabika.

Kwa upande mwingine, mwandishi anaendelea kuchimiza ujumbe wa vijana kuathiriwa na utandawazi kupitia kwa mhusika Suhail. Suhail anapokuwa safarini anajisahau kabisa kwa kusikiliza muziki wa mwamuziki mmoja kutoka Marekani na hata anapoitwa na mhudumu apewe soda hasikii kabisa. Anaimba kwa sauti na kuwakera abiria wenziwe. Hii inaonyesha wazi jinsi vijana wengi wenye elimu kama Suhail wanavyoathiriwa na utandawazi kwa kutumia vibaya vifaa vya kiutandawazi. Kwa sababu kulikuwa hakuna haja ya kuweka sauti kubwa ya mwanamziki huyo wa Marekani. Aidha hii inaonyesha wazi jinsi mataifa yanayoendelea yalivyopumbazwa na utandawazi kiasi kwamba, hata

heshima inakuwa hamna tena. Mwandishi anaendelea kuonyesha jinsi Suhail alivyoathiriwa na utumaduni wa kiMagharibi kwani pamoja na yule Mzee wa kiasi kumuita jina lake alijifanya bado anaendelea kuimba huo wimbo wa Kiingereza. Mwandishi, kupitia Mzee Sufian anasema:-

> "Suhail we' ni mtundu sana…halafu leo unaonekana una furaha sana eeh?"Heh!
>
> Kijana alishangaa upeo wa kushangaa. Lile swali lilimuacha hoi, kwani kwa hakika jina lake ni Suhail.
>
> "Mnh, Mzee! We' um-umejuaje kama nina furaha…? Na…jina langu umelijuaje?"
>
> "Nimekusikia ukiimba muda mrefu tena kwa sauti ukisema *Because am happy*," Mzee alijibu huku akizidi kuchanulisha tabasamu lililomdhihirishia Suhail mawazo yake kuwa ni kweli alikuwa akiufuatisha kwa kuuimba kwa sauti ule wimbo wa *Pharrel William* uitwao *'Happy'*. Maana katika moja ya beti zilizoshiba kwa urari wa vina na mizani ndimo kuna kibwagizo kisemacho *'Because I'm happy'.* Lakini pia akaona kuwa yule Mzee hakumjibu swali lake la pili (uk. 5).

Vilevile wakati safari inaendelea, ghafla inatokea ajali ambayo inawauwa watu wengi sana. Cha ajabu Suhail alipona na akainuka. Ghafla anaonana macho kwa macho na Mzee Sufian akiwa amechoka hajitambui mwili wote umejaa damu. Akataka kwenda kumwokoa lakini ajabu yule Mzee akakataa kuokolewa. Baadaye Mzee huyo anamuonyesha Suhail begi lenye dola na Suhail anaziona na kuzitamani Mzee akaona tamanio la Suhail akampa Suhail dola hizo, akavua pete yake na kumvalisha Suhail. Suhail baada ya kuvaa pete ile akahisi ameingiwa na ganzi mwili mzima. Mzee Sufian anasema:- Lah! "Usichanganyikiwe kijana. Mimi nakufa, hilo halina pingamizi, ila nimekutunuku mwanangu. Pesa zote hizi nakutunuku wewe na mali zingine ambazo utazijua muda ukifika."Ama! uk 7.

Baada ya maneno hayo mafupi, ambayo kwa hakika Suhail alikuwa anayasikia kama yanakutokea mbali sana na pale walipokuwa, Mzee akavua pete yake kubwa yenye kito cha rangi ya njano aliyokuwa ameivaa kwenye kidole chake cha kati na kumshika mkono Suhail. Kisha akamvisha pete ile (uk 9). Katika tukio hili mwandishi anachimuza

swala la tamaa na ulafi, ujumbe ukiashiria jinsi viongozi wa bara la Afrika wanavyotamanishwa, wanavyoshawishiwa kwa vionjo mseto na hatimaye, kukuzwa kwa tamaa na kisha viongozi hao kusawiriwa walivyo na tamaa mpaka wanatawaliwa. Suhail ameonyeshwa, akatamanishwa na baada ya kupewa zile pesa akapewa masharti na Mzee huyo ya kumuoa Binti yake ili waweze kuendeleza hizo mali.

Kupitia kwa usawiri wa tukio hili na kwa kadri tukio hili linavyomhusu mhusika huyu, mwandishi analidadisi swala la mahusiano ya kiulimwengu, ulimwengu tajiri na ulimwengu masikini. Uhitaji wa Suhail ni ishara ya uhitaji wa nchi masikini. Hii inaonyesha wazi jinsi misaada ambayo viongozi wa Afrika wanaipata kutoka kwa nchi zilizoendelea inavyokitwa na kuambatanishwa na masharti, taifa husika lihusiane na taifa gani na lisihusiane na taifa gani, misaada itumike kwa njia gani na isitumike kwa njia gani. Kwa jumla, nchi masikini zinabebeshwa mizigo mizito, zinaingizwa katika mikataba yanye masharti, zinaishia kuwa mataifa huru kwa jina na bendera tu, kama Suhail alivyo kijana msomi kwa jina bila uwezo wa kutumia usomi wake kufanya maamuzi razini. Nchi zinapewa masharti magumu ambayo mwishowe wananchi wanaibiwa mali zenye thamani kubwa sana kwa sababu ya misaada midogomidogo.

Vilevile Suhail anafananishwa na viongozi ambao wakishaingia mikataba na nchi zilizoendelea wanajinufaisha wenyewe na kuwasahau wananchi wanaoendelea kupata shida, hospitali hazina dawa na barabara ni mbovu, maji ya kunywa ni shida kwa wananchi huku wenyewe wakiishi mjini na kupata kila huduma ya kimsingi inayohitajika. Jambo hili limedhihirika baada ya Suhail kupata zile dola na pete, pia kukubali kumwoa Shekhia hakurudi tena nyumbani kwao Tabora ambako ni kiJijini. Suhail aliamua kurudi Jijini Dar es Salaam na akamsahau hata mchumba wake Sharifa na akaendelea kula raha na Shekhia. Aidha kupitia usawiri wa Suhail, mwandishi anachimuza dhamira ya usaliti. Awali Suhail ni kielelezo cha wanaume wasaliti yaani wasaliti wa imani, maadili na mapenzi au ni kielelezo cha watu wasaliti—wasaliti wa ahadi, neema ya jumuia na ndoto za jamii pana. Baada ya kupata pesa hizo na pete kutoka kwa Mzee Sufian, Suhail anamsaliti mchumba wake Sharifa aliyekuwa anamsubiri Tabora na ambaye hawakuonana mwaka mzima—usaliti wa imani, pendo na

maadili. Lakini Suhail hakujali hilo anakubali kurudi Dar es Salaam kwenda kumwoa Shekhia mtoto wa Mzee Sufian aliyempa dola pamoja na pete.

Mwandishi anamchora Suhail kama mtu asiye na huruma kwani baada ya ajali kutokea ilimpasa ashirikiane na wenziwe kutoa msaada wa kubeba maiti na wale walionusurika katika ajali. Badala ya kusaidi, Suhail anadanganya ana haraka. Suhail anachimuza ujumbe wa jinsi misaada ambayo mataifa ya ulimwengu wa tatu inayotolewa na mataifa yaliyoendelea inavyokuwa na masharti kiasi kwamba mpaka inafika mahali viongozi hawa waliongia katika mikataba hiyo wanaishiwa ubinadamu na wanashindwa kabisa kuwasaidia wenzao kwa sababu masharti magumu. Ndio maana Suhail anapoambiwa na abiria wenziwe asaidie anashindwa kutokana na masharti anayopewa. Anaamua kuwadanganya abiria wenziwe kwamba hakuomba ruhusa kazini anaogopa wasije wakamuona mabosi zake kazini katika televisheni akisaidia kubeba maiti. Suhail anasema:-

> “Jamani iko hivi…nilikuwa nawahi Dodoma kuripoti kazini ambako niliondoka tangu majuzi bila ya ruhusa maalum, sasa kama nitagundulika kuwa nilikuwa safarini na nimepata ajali hii nitafukuzwa kazi hivyo nawaombeni sana mnielewe ndugu zangu, sina nia mbaya kabisa!”(uk 20).

Hali kadhalika mwandishi anachimuza dhamira ya jinsi wafanyakazi wasivyowajibika katika ofisi zao kwa kutoroka kazini bila ruhusa kupitia mhusika Suhail. Wenziwe wanapomuomba asaidie kuhudumia maiti badala yake anasema anaomba aondoke eneo lile akionekana amepigwa picha na waandishi wa habari wakati hakuomba ruhusa kazini, atafukuzwa kazi. Hii inadhihirisha wazi kabisa jinsi wafanyakazi wengi maofisini jinsi wasivyo wa kweli na hawawajibiki ipasavyo katika ofisi kwa kutoroka ofisini bila ruhusa. Kwa upande wa Suhail alitumia sababu hiyo ili kutunga uongo na ulaghai kwa abiria wenziwe wapate kumuamini kuwa anayo sababu ya dhati ya kuondoka haraka katika eneo la tukio na bila ya kujulikana kama alikuwa miongoni mwa waliopata ajali. Kwa mara ya kwanza msomaji anakutana na tabia ya Suhail, inayotuthibitishia kuwa ni muongo na mlaghai. Hivyo basi mtunzi anamtumia suhail katika tukio lililosababishwa kichawi na Sufian kuchimuza dhamira hiyo.

Suhail ameathiriwa na utandawazi sana kwani baada ya kuondoka kwenye ile ajali alielekea Dodoma mjini katika hoteli nzuri na lile begi jekundu la dola. Alipokuwa chumbani, akatafuta simu yake ili aweze kupiga. Kwa bahati mbaya ikawa ilipotea kule kwenye ajali ikabidi amuombe mhudumu wa ile hoteli ampe simu yake apige. Yule mhudumu akamuuliza unapiga laini gani Suhail akasema mtandao wa Vodacom. Yule dada mhudumu ambaye ni wa kike akasema yeye simu yake ni laini ya mtandao wa Tigo tu. Suhail akacheka sana kwani nchini Tanzania ukisema unatumia mtandao wa Tigo katika mazingira ya utani ni mtu anayefanya mapenzi kinyume na maumbile. Hii inadhihirisha wazi jinsi utandawazi kwa upande mwingine ulivyoharibu utamaduni wa waafrika. Katika tamaduni za kiafrika kulikuwa hakuna tabia ya watu kufanya mapenzi kinyume na maumbile.Tabia hii watu wameiiga kutoka katika mataifa yaliyoendelea kupitia mitandao mbalimbali ya kijamii.

Suhail anachorwa kama mhusika ambaye ana tabia ya ubinafsi ya kutothamini hata ndugu wa damu kama vile wazazi wake kutokana na pesa alizozipata. Haya ynadhihirika pale ambapo alipata ajali na wazazi wake wakaona katika televisheni wakawa na wasiwasi sana kwamba amekufa. Lakini baada ya kupatikana hewani kupitia simu yake ndipo wanajua ni mzima. Pamoja na wazazi hawa kufurahi wakamtaka arudi nyumbani, lakini hakutaka kabisa na akatoa sababu za uongo. Lengo la Suhail lilikuwa ni kuendelea kuzitumia hizo pesa Dar es salaam. Kwa mara ya pili tena, msomaji anathibitishiwa tabia ya Suhail, ya kuwa ni muongo na mlaghai. Na uongo wake hauna mipaka, baada ya kuwadanganya abiria wenzake, sasa anawadangaya wazazi wake na pia mpenzi wake.

Kuhusu swala la tamaa ya pesa na utajirisho, Suhail anajiingiza katika kundi la walio wengi ambao wana shauku ya utajirisho wa aina yeyote bila ya kujali madhara yake. Mwandishi anampamba mhusika Suhail kama kijana wa kileo katika nchi zinazoendelea ambao mfumo wa kipebari na utamaduni wa pesa umemwamba. Utamaduni huu unaendana sambamba na ubinafsi. Badala ya kufika kwa wazazi wake na kwa mchumba wake Sharifa anachotwa na tamaa ya kuwekeza fedha alizozipata haraka kwa bahati

nasibu. Fedha ambazo zina masharti lukuki na ni chanzo cha angamio lake. Kupitia kwa maelezo haya mwandishi anachimuza ujumbe wa viongozi ambao wanajilimbikizia mali kwa kuwa na majengo ya kifahari wakati kuna baadhi ya wananchi wanaishi maisha magumu, hawana nyumba, hata chakula kwao ni shida lakini viongozi hawa wana majengo ya ghorofa kila mahali katikati ya majiji. Suhail anapopata pesa kutoka kwa Mzee Sufian anaenda Dar es Salaam ananunua majengo makubwa ya kifahali na nyumba ya kifahari ya kuishi katika maeneo ya Ilala na Mbezi. Anasahau hata ndugu zake walio katika hali ngumu kuwasaidia ndivyo walivyo viongozi wengi wa mataifa ya ulimwengu wa tatu. Mwandishi anatushadidia kwa mara ya tatu tabia ya uwongo wa Suhail, pale anaposhindwa kuwaeleza marafiki, ndugu, wazazi, mchumba, na wafanyakazi wenzake chanzo cha utajiri wake mkubwa. Uongo anautunga kuwa amekabidhiwa na tajiri wa kiasia anayeishi' Uarabuni.

Vilevile Suhail anaibua dhamira ya upendeleo katika ajira. Hili linadhihirka kwa baadhi ya viongozi kuwaweka marafiki zao katika nafasi za juu serikalini. Mfano mzuri ni kama rais akipata madaraka huwaweka rafiki zake katika nafasi za mawaziri tena wengine wanakuwa hawana taaluma ya hicho wanachokiongoza. Ndivyo ilivyokuwa kwa Suhail. Baada ya kufungua makampuni mbalimbali anawaajiri rafiki zake aliyosoma nao chuo kikuu kama wafanyavyo viongozi wengi. Pia yawezekana walikuwa na taaluma hizo lakini mtunzi anataka kutuonyesha jinsi ugawanaji wa mamlaka na kazi mbalimbali serikalini ulivyogubikwa na hali ya kujuana. Japo kuweka marafiki katika kazi sio vibaya ila mara nyingi wengi wao huwa utendaji kazi usio mzuri. Mambo kama haya yanashadidia ukweli kwamba nyadhifa za uongozi wanazokabidhiwa viongozi wa Kiafrika zinatumiwa kwa maslahi ya ki binafsi, kirafiki, kiukoo na hatimaye kikabila. Nyadhifa hizo za uongozi zinatumiwa kuweka mbele neema ya binafsi na kuhalalisha unyonyaji, unyang'anyi na uporaji wa rasilimali za umma kwa manufaa hayo ya ki binafsi.

Ilipofika zamu ya kutimiza masharti ya kupewa fedha na Mzee Sufian anayemtokea katika ndoto, Suhail anajikuta hana jinsi ila kutimiza masharti hayo ambapo tayari

alishaingia katika mtego wa kurambishwa asali au kuonyeshwa utajiri. Moja ya masharti aliyopewa na Mzee huyo, ni kwenda kumtafuta Shekhia ili aweze kumuoa Binti huyo aliyekuwa na nasaba ya nusu jini. Suhail anatafuta pikipiki impeleke maeneo ya sokoni katika mji wa Bagamoyo ili aanze kumuulizia Shekhia. Anaposhuka katika pikipiki anampa pesa yule mwendeshaji pikipiki na akatakiwa arudishiwe chenji na yule wa pikipiki lakini yeye akaondoka bila kurudishiwa pesa kwa sababu ana pesa nyingi sio kama amesahau. Suhail alikuwa na jeuri ya kutokupokea chenji kwa sababu alikuwa na pesa nyingi.

Mtunzi anachimuza dhamira ya falsafa ya maskini akipata pesa nyingi bila kutegemea huwa na jeuri isiyo ya kawaida katika jamii, aidha mtunzi anaendelea kuonyesha athari hasi ya pesa kwa kuonyesha kwamba kuna baadhi ya watu wamekuwa na tabia kama ya Suhail. Suhail alipopata zile pesa kutoka kwa jini Sufian hakuona tena umuhimu wa wazazi kwani walipokuwa wanampigia simu hakuhitaji kupokea simu kutoka kwao. Aidha pesa imetumika kama chombo cha kumtenganisha mtu na jamii yake au rafiki au ndoa. Suhail alipopata zile pesa zenye masharti ya kumwoa mtoto wa Mzee Sufian ambaye ni jini na kuachana na mchumba wake wa zamani alikuwa tayari. Japo mashrti haya yalimpelekea mpaka kutafuta sababu za uongo ili asimuowe mchumba wake kwa kumdanganya mchumba wake wa zamani kwamba yeye hana nguvu za kiume kitu ambacho si cha kweli. Hii yote ni kwa sababu ya pesa kwani pesa imekuwa na nguvu kubwa katika jamii mpaka watu wanadhubutu muda wote kuongea uongo.

Kwa upande mwingine Suhail anachimuza dhamira ya viongozi wanaovuja mali za umma kwa kwa kujinufaisha binafsi. Ndivyo ilivyo kwa viongozi wengi barani Afrika ambao maisha yao ni ya kifahari na kuvuja pesa za kodi ya wananchi bila huruma wakati kuna wananchi wanateseka. Hivyo ndivyo Suhail anavyofanya kwa kuonyesha ana pesa nyingi ndio maana hakuchukuwa chenji pamoja na kuitwa achukue. Aidha mwandishi anaonyesha mitagusano ya utajiri na ulitima kwa mhusika huyu na dereva wa pikipiki kwani Suhail alikuwa anajua kabisa ana pesa nyingi ndio maana akawa anaacha chenji. Kwa mara ya nne, wasomaji wanakutanishwa na tabia ya Suhail ya

ulaghai. Mara hii anamjaribu kumlaghai Mzee Atrash ambaye ni mnajimu na mganga wa vitabu anamng'amua na kumweleza waziwazi ukweli juu ya tabia yake ya tamaa, uongo na usaliti. Tabia hizi tatu ni msingi wa anguko la kila mwanadamu na sio Suhail peke yake. Mzee Sufian na yeye pia ni muongo na msaliti. Suhail amechorwa na kusawiriwa kama mtu muongo, msaliti na mwenye tamaa. Anazungumza uongo kwa Mzee Atrash alipokuwa anaenda kuomba msaada wa kujua Shekhia anaweza akampata wapi. Lakini Suhail akajifanya anataka kwanza kujua historia ya Shekhia na Sufian baada ya kusema ukweli yeye akaongea uongo wakati anaulizwa na Mzee Atrash unawatafuta kwa nini akasema anafanya nao Biashara kitu ambacho si cha kweli.

Katika makutano haya ya Suhail na Mzee Atrash, mwandishi anachimuza mambo mengi, mambo ya kifalsafa, kimahusiano na kitajriba. Kwa mfano, kwa nini watu hawawi wakweli katika maingiliano yao na watu wengine. Kwa njia hii mtunzi analidadisi swala la uongo katika maingiliano na katika mahusiano ya watu, lakini kama inavyobainika uongo wa Suhail haumfikishi mbali, anagunduliwa mapema na kukanywa kwamba hiyo ni njia fupi tena ina hatari na fedheha. Kwa mtazamo mwingine inawezekana kuhoji kwamba kila mtanguliza na msema uongo ana la kuficha, ana hatia na uongo unakuwa ni njia ya kutangaza hatia hiyo. Kupitia kwa mhusika huyu na kwa kuangazia ni mara ngapi amesema uongo au anatoa sababu za uongo, mtunzi analiangazia swala la uongo katika mahusiano ya mtu binafsi na jamii pana, uongo katika mikataba na mahusiano ya kimataifa, uongo na athari zake katika mitagusano ya aina mbalimbali.

Katika kiwango kingine, mtunzi anachimuza dhamira ya viongozi waongo katika serikali mbalimbali katika mataifa ya Afrika kwani wengi wao wamekuwa wakihadaa wananchi kwa maneno matamu wanapokuwa wanataka kupata nyadhifa mbalimbali lakini wakipata wanasahau kabisa ahadi walizowaahidi wananchi. Suhail pamoja na kupata mali nyingi na kampuni mbalimbali na majumba lakini hakuweza hata kidogo kuwashirikisha ndugu zake kwa mali alizonazo. Jambo hili liliwashangaza hata wafanyakazi wake pindi na hasa anapotekwa na wafanyakazi wa Sufian na kupelekwa

katika jumba moja Bagamoyo. Wafanyakazi hawa wanatafuta namba za simu mbalimbali katika shajara yake baada ya yeye kutokupokea simu. Ndipo wanapata namba ya simu ya baba yake na wanampigia na kujieleza kwamba wao ni wafanyakazi wa Suhail katika kampuni zake. Mama yake Suhail alishangaa sana na kusema:

> "Sasa haya majanga mapya jamani, huyu mtoto ametoa wapi Kampuni! Na ametowekaje ghafla? Isije ikawa huyo aliyekupigia wewe ni muhalifu na ndiye amemteka mwanagu jamani…" Mama Suhail alikua akihatahata kwa maneno (uk 71).

Mwandishi anachimuza ujumbe wa ubinafsi na kwa upande mwingine masharti na mikataba inayosainiwa na Suhail kutoka kwa jini Sufian yawezekana ndiyo iliyokuwa inamtesa, kwani Suhail japo alikuwa na mali nyingi na pesa nyingi, masharti yale ndiyo yaliyokuwa yanamnyima raha na kumfanya awe mbinafsi asiyependa hata kuwashirikisha ndugu zake. Ndivyo ilivyo kwa mataifa yanayoendelea viongozi wanaposaini mikataba inakuwa na masharti sana, na masharti hayo hatimaye, yanawafanya hata washindwe kuwaeleza wananchi maswala mazima ya uwekezaji unaofanywa na mataifa yaliyoendelea katika maeneo ya wananchi wenyewe.

Tunaendelea kuona jinsi Suhail anavyotumiwa kuchimuza dhamira ya matumizi mabaya ya pesa za umma kwani anafananishwa na kiongozi ambaye anazitapanya mali za umma kwa wanawake ambao hajawaoa. Suhail anamuahidi Sharifa atampa fungu la mali zake. Anajaribu kumrubuni kwa jeuri ya pesa. Tabia ya kurubuni aliianza taratibu kwa dereva wa bodaboda alipoamua kumuachia chengi. Tabia hiyo aliitumuia pale alipokuwa na Sharifa katika nyumba ya wageni na alifanikiwa kumrubuni mwenye hoteli baada ya kufanya uharibifu ili asiweze kumuathiri kwa wazazi wake. Alikuja tena kuitumia jeuri ya pesa kumlaghai na kumrubuni rafiki yake mpendwa Msigwa aweza amhudumia kinyumba mke wake ambaya naye alishakwisha kumdanganya kuwa hana nguvu za kiume. Uongo na ubadhirifu wa mali unaendana pamoja na usaliti. Mipaka ya matendo hayo inavunjwa kupitia Suhail na Mzee Sufian.

Suhail ni mfano wa viongozi wengi wa umma ambao huchukua mali za serikali na kuzitumia kama chanzo cha hongo na rushwa. Wakiwa wanaendelea na mazungumzo katika hoteli kule Tabora, Sharifa anataka kujiua kupitia dirishani. Sharifa alitaka kujirusha kutoka juu ya ghorofa mpaka chini. Kwa bahati nzuri Suhail aliwahi kumwokoa akawa ameumia kichwani kidogo na damu zikawa zinamtiririka. Sababu ya kujinyonga ni kutokana na Suhail kutaka kumuacha na kumuoa jini Shekhia kwani jini huyo alikataa kuchanganya mapenzi na mwanamke mwingine. Hivyo basi, Suhail akaona si vyema kumwambia jinsi Sharifa alivyomkataza akamwambia hana nguvu za kiume ndio maana hawezi kumuoa. Baada ya Sharifa kuumia ikabidi ampeleke hospitali lakini, kwa kuhofia maswali mengi na taarifa ya polisi akaogopa kumpeleka hospitali ya serikali. Kwa kuwa alikuwa na pesa anaamua kumpeleka katika hospital binafsi ya dokta mkubwa sana katika mji wa Tabora. Mwandishi anasema:

> Majira ya saa mbili kasorobo usiku Suhail na Sharifa walikuwa wakiendelea kupatiwa matibabu, hawakwenda katika Hospitali ya Kitete kwa kuhofia kuzalisha maswali na mwishowe huenda taratibu za kipolisi kuingia kati hivyo walikwenda mtaa wa UJiji katika Hospitali ya Dokta mkubwa sana anayekubalika pale mkoani, na kwa kuwa pesa iliongea hivyo huduma ikaenda kwa kiwango kizuri (uk 99).

Suhail anatumia pesa zake hata kupindisha sheria kwa sababu kisheria mtu yeyote anayepatwa na matatizo ya ajali anatakiwa aende polisi ili apewe ruhusa ya kwenda kutibiwa. Lakini yeye kutokana na pesa anamuhonga dokta akamtibu Sharifa. Suhail anatumiwa kuchimuza ujumbe wa watu kutumia pesa zao katika kukwepesha sheria mbalimbali zilizowekwa na nchi. Mwandishi anachimuza madhara na manufaa ya pesa kwa maana kwamba katika kumwezesha Sharifa kupata matibabu uchanya wa pesa unajitokeza na katika kukwepa sheria madhara ya pesa yanaonyeshwa.

Mtunzi pia anachimuza dhamira ya ndoa za mitala katika jamii ya Suhail na pia katika jamii ya Masumbuko katika *Mzimu wa Waufi*. Katika *Vita vya Mapenzi* kuna aina ya ndoa ambayo mtu halisi anaoa jini. Mzee Sufian ni jini anamuoa binadamu halisi aitwaye Amanda. Suhail ni mwandamu halisi anakuja kuozwa mtu jini aitwaye Shekhia.

Lakini papohapo analazimishwa na wanajamii yake kumwoa mke wa kawaida Sharifa na hivyo kujikuta akiwa na mitala isiyotarajiwa. Dhamira inayochimuzwa hapa ni mazingira yanayoweza kuibua mitala katika jamii. Si kila ndoa ya mitala inatokana na muoaji kuwa na ridhaa ya kufanya hivyo. Pengine ni mazingira ambayo katika jamii zetu kuna ndoa nyingi za mitala ambazo ni za siri. Huu ni ukweli ambao Mwingizi anautumia kumshawishi msomaji wake kirahisi. Sababu zinazopelekea kuwepo na ndoa za mitala zinazoonekana katika *Mzimu wa Waufi* ambapo Masumbuko ni zao la ndoa ya mitala inayoridhiwa na wanajamii hususani katika mfumo jadi uliokuwepo na katika dini ya Kiisilamu. Kuingia kwa Ukristo kumeleta kikwazo katika mfumo wa mitala wa kijadi.

Ndoa ya ajabu inayosukwa na mwandishi ni pale ambapo Masumbuko anageuzwa mwanamke na jini Hunudu, ili aolewe kama sehemu ya mbinu ya kumshrutisha aingie katika mtandao wa Waufi. Ndoa ya mwanamume kuolewa na mwanamume inakubalika katika fikira za wasomaji wa Waufi katika hali ya kifantasia tu na si katika uhalisia ingawaje kwa sasa kuna shinikizo kutoka nchi za Magharibi kuhalalisha ndoa za watu wa jinsia moja. Ndoa ya mitala ya aina yake inayoonekana katika *Tanzia* ambapo Bi Masonganya ambaye ameolewa kihalali na kiuhalisia na mwanamume anayemzalia watoto, lakini kwa masharti ya mila za kichawi analazimika na yeye kuoa mwanamke anayekuja kumzaliwa mtoto na kutambulika kama baba. Ni aina ya mitala ya aina yake ambayo inakubalika kwa wasomaji tu kwa njia ya kifantasia. Ndoa hizi zimekuwa ni kiini cha migogoro kwa namna moja ama nyingine. Chimbuko la ndoa ya Shekhia inavuruga mipango ya ndoa kati ya Suhail na Sharifa na kusababisha usaliti, uzinzi, mauaji na uhasama na vifo. Mitala ya baba yake Masumbuko nayo inasababisha mvutano wa himaya ya Waufi na Waswezi katika kushurutishwa kwa utoaji wa kafara. Na mitala ya Bi Masonyanya inasababisha mgawanyiko wa familia, chuki, na mauaji. Kuzaliwa kwa Nyembo kunaashiria uchuro na baraka pia, kwani anakuja kutumika katika anguko la mtandao wa wachawi wa kibondo.

Aidha mtunzi anatuchorea ishara ya nchi zinazoendelea kuwa na wahisani wengi ambao kila mmoja anakuwa na masharti yake. Ni sawa kuwa nchi hizo zipo katika mahusiano ya mitala ya siri. Mitala katika jamii za jadi imeshamiri na jamii haikuwa inachukulia kuwa mitala ni tatizo. Kidogo kidogo utamaduni wa Magharibi na mfumo wa Ukristo unayeyusha mantiki za mitala iliyokuwa imeshamiri katika jamii za jadi. Lakini si kwamba mifumo hiyo imefanikiwa kuondoa kabisa mitala, bali imesalimisha mitala ya siri na ambayo ina hatari kama vile ilivyo mitala ya Suhail. Kwa hivyo, Suhail kama kiwakilishi cha nchi masikini kuwajibikia masharti ya nchi fulani ambayo ni tajiri na mfadhili, kwa hiyo anapewa masharti yenye vizingiti vizito kwa ajili ya kukubali kupewa misaada japo kwa masharti ambayo yana mateso. Nchi nyingi katika mataifa ya ulimwengu wa tatu zimekuwa zikiyumba kutokana na misaada inayopewa ya masharti mpaka wanashindwa kuwa na maamuzi yeyote yale katika baadhi ya vitu. Nchi hizi zimekuwa zikipewa masharti katika nchi zao na wakati mwingine rais asipokuwa na msimamo anaweza hata akahalalisha swala la ndoa ya jinsia moja kama ambavyo mataifa yaliyondelea yanavyolipa kipaumbele swala hili la ndoa ya jinsia moja.Kwa hiyo, mtunzi amemchora Suhail kama nchi inayowajibikia masharti hayo.

Suhail anaona umuhimu wa wazazi wakati tayari amefunga harusi na jini Shekhia. Na wakati anafunga harusi hakuwaambia wazazi wake kutokana na kwamba alishakuwa na mchumba mwingine Tabora na wazazi wake wanamfahamu mchumba huyo. Lakini pamoja na kuona umuhimu huo wa wazazi, bado anaendelea kuwa jeuri na kutomuacha Shekhia. Kutokana na wazazi wake kumtaka amuoe Sharifa anaingia katika mgogoro mkubwa wa nafsi kutokana na mkataba aliyosaini na Mzee Sufian ulikuwa ni kumuoa Shekhia. Kwa hiyo, hakutakiwa kuoa mwanamke mwingine. Suhail anashurutika katika hali hii kusafiri kwa kutumia pete ya kimajini kwa dakika chache kutoka Tabora mpaka Dar es Salaam kwa ajili ya kumuomba Shekhia ruhusa amuoe Sharifa kwani anaogopa kuachiwa radhi na wazazi wake na anawapenda wazazi wake. Pamoja na kwamba Suhail alifunga ndoa na kufanyiwa harusi na Shekhia lakini kwa ajili ya kuwafurahisha wazazi wake lakini ndoa ilikuwa ngumu sana kwani masharti aliyopewa na Shekhia

hakupaswa kufanya mapenzi na Sharifa jambo ambalo lilikuwa gumu sana kwa mkewe Sharifa.

Kwa upande mwingine mtunzi alitaka kuchimuza dhamira ya wazazi kutokuwashurutisha watoto wao kuoa wanawake wanaowataka wao kutokana na urafiki wao wenyewe. Kwani Suhail alikuwa anafuata maagizo kwa wazazi wake na hali anajua ni jambo ambalo haliwezekani. Lakini kikubwa mno hapa ni kuangalia kwa undani swala zima la usaliti, uongo na tamaa. Sharifa ni muhanga wa usaliti, uongo na tamaa ya Suhail. Hivyo hata ndoa hiyo ni mtego wa kumuangamiza tu. Kinachojitokeza hapa kwa ujumla ni swala la mgongano wa matakwa binafsi na matakwa ya jamii. Shekhia ni mke wa matakwa binafsi ya kuridhisha tamaa zake na si mapenzi ya dhati. Sharifa ni mke wa matakwa ya jamii yanayoridhisha na kudhihirisha mapenzi ya dhati waliyoyalea. Mhusika anajikuta katika njia panda ya kuchagua penzi la fedha na penzi la dhati. Mgongano huu upo hata kwa viongozi wetu wanapojikuta wakishurutishwa kutimiza masharti ya wale wanaowafadhili hali ya kuwa masharti hayo hayana maslahi mapana na jamii zao.

Tabia ya uongo wa Suhail inaanza kuota mizizi katika maswala ya ndani ya kifamilia kiasi cha kuwaathiri wanaomzunguka akiwemo mkewe Sharifa na rafiki yake Msigwa. Anakiuka maadili ya dini ya kiislamu kuwa na wake wawili bila Sharifa kujua kama kuna mke mwenziwe ambaye ni nusu jini. Hili linadhihirika katika jamii zetu kwani kuna wanaume wa kiislam huoa wake wengi bila kuwaambia wake zao. Kwa sababu kisheria katika dini hii wanaruhusiwa kuoa wanawake hadi wanne ili mradi wawashirikishe mke au wake zao kwa kuwaambia kwamba anaye mwanamke mwingine lakini, Sharifa hakuambiwa kuwa kuna mwanamke mwingine. Kwa mujibu wa kauli za Mbiti (1975:104) kijana anapofikia kubalehe anawajibika kuoa au kuolewa. Swala la kuoa au kuolewa ili kujenga familia ni sehemu muhimu ya mzunguko wa maisha ya mwafrika. Ndoa huchukuliwa kama tendo takatifu ambapo kila mtu mzima hana budi kulitekeleza jukumu hilo. Yeyote yule akiwemo Suhail, haruhusiwi kukataa kuoa mbele ya jicho la wanajamii. Ndoa ni daraja kati ya walioondoka na wale wanaokuja kuzaliwa.

Ni kiungo kati ya kifo na maisha. Kitendo cha kuchaguliwa mchumba na wazazi si kitendo kigeni. Mwiko mkubwa ni kuoana ndugu wa damu ambapo kupitia Mwingizi tunastajaabishwa kugundua kuwa ndugu wa damu wa tumbo moja wanakuja kuolewa na kaka yao. Kinachofuatia mara baada ya ndoa ni wanajamii kutegemea matunda ya ndoa ambayo ni watoto. Pakikosekana hilo kinakua ni chanzo cha ugomvi mkubwa ndani ya ndoa. Bila ya kuwa na ndoa ni mapungufu mbele ya wanajamii wa kiafrika, lakini mapungufu zaidi ni pale anapokosekana mtoto wa kuendeleza ukoo au kuunganisha kifo na maisha.

Suhail amechorwa kama mpatanishi na msuluhishi wa matatizo ya ndoa kwani Msigwa na mkewe walipokuwa na ugomvi mkubwa kwa sababu mke wa Msigwa alikuwa ana miaka miwili ndani ya ndoa na hakubahatika kupata mtoto. Hivyo, Msigwa anamfukuza mkewe. Suhail alikuwa anaelekea kwa Msigwa akamkuta mke wa Msigwa kwenye kituo cha daladala au matatu na mizigo. Ndipo Suhail akamrejesha kwa Msigwa ili waweze kumaliza mgogoro wao. Kwa upande mwingine mtunzi anachimuza dhamira ya umuhimu wa watoto katika familia nyingi za kiafrika. Familia huwa ndoa zinazodumu na kuwa na amani hata katika swala la unyumba kutokana na kujaliwa kuwa na watoto. Kwa kiasi kikubwa katika jamii nyingi za kiafrika ndoa zisizokuwa na watoto huwa hazidumu na hata zikidumu nyingi huwa ni kuvumiliana tu siku. Suhail amechorwa kama msuluhishi katika ndoa hii ambayo ugomvi wao mkubwa unatokana kutopata mtoto.Wakati huo huo Suhail anapotekeleza majukumu ya kuwa msuluhishi, yeye pia ana matatizo yake ya kindoa ambayo ni makubwa zaidi kuliko kitendo cha kukosa mtoto. Kitendo cha kupanga mbinu ya kumruhusu mke wake wa ndoa kuingilia kwa mara ya kwanza na rafiki yake huku akiendeleza tabia yake ya uongo, tamaa na usaliti ni kitendo ambacho kinamjengea chuki mhusika Suhail na wasomaji wake. Wasomaji hawamwonei huruma anapofikia hatua ya kutubu na kufariki kwa kihoro kwani tayari wamekwisha tayarishwa na mwandishi kuchoshwa na tabia ya uongo na usaliti wa Suhail.

Katika swala la ugomvi kati ya Msigwa na mkewe kunaibuka swala la msingi katika jamii za waafrika kuwa maisha hayana budi yaendelee katika mzunguko wa wazee kurithiwa na watoto kupitia ndoa na uzazi. Kwa upande waliomo katika ndoa, jambo kubwa ambalo halina budi kutimizwa katika ndoa ni tendo la ndoa. Inapotokea ugumba au ukosefu wa nguvu za kiume kati ya mmoja wa wazazi, mbinu hutafutwa kuziba pengo hilo. Katika mazingira ya sasa kuna ugumu katika kufanikisha azma ya kupatiwa mtoto kwa njia ya kumpatia mtu au ndugu yako "akusaidiye" uzazi kwa siri. Mila za kurithi mjane au kuoa ndugu wa mke anapofariki ni sehemu ya uendelezaji wa fikra ya mzunguko wa maisha katika falsafa ya kiafrika kwa mujibu wa mtazamo wa John Mbiti (khj). Kuruhusu ndoa za wake wengi ni sehemu ya kuhakikisha uzazi unakuwepo kwa wingi. Suhail anaitumia nafasi ya utamaduni na mila iliyoshamiri katika jamii za jadi kumtaka rafiki yake Msigwa "amuolee" mke wake.

Kwa vile si sehemu ya mila ya sasa, Msigwa anashtuka na kukataa hadi pale anapolainishwa na jeuri ya pesa ambayo ni mila ya kisasa. Anakubaliana na hilo kwa shingo upande. Na kwa upande wa mke wake Sharifa yeye analikubali jambo hiloili kumsitiri mume wake na aibu ya jamii tu na sio kwa sababu ya mapenzi yake kwa Msigwa. Watoto ni nembo ya ndoa. Ndoa zinavunjika kwa wingi katika jamii inapotokea hakuna mtoto anayezaliwa. Watoto huchukuliwa kama kiongeza hadhi cha jamii na familia husika. Kwa sasa zipo njia za kitaalamu ambazo zinatokana na teknolojia za kusaidia kupatikana uzazi kwa wagumba. Pengine hii ndio sababu iliyopeleka jamii ya Suhail kuliona swala la kupata mtoto na kuishi na ugumba ni kitendo kinachoweza kutatuka kitaalamu. Tofauti na kizazi cha baba yake Masumbuko katika *Mzimu wa Waufi*. Katika kufuma mahusiano ya aina hii, Mwingizi anafanikisha ustadi wa msuko wa riwaya za kihalisiajabu kupitia asasi ya ndoa.

Katika jamii za kiafrika tunategemea kuwa vijana wanapofikia kubalehe na wakiwa wazima wa maumbile hawana budi kuoa au kuolewa. Suhail, Shekhia na Sharifa mbele ya wazazi wao wamefikia hatua ya kuoa na kuolewa. Njia kuu ya kuifikia ndoa ni kupitia kupangwa na wazazi na hilo si jambo la ajabu ingawaje taratibu hizo kwa sasa

zinafifia. Lakini upangaji katika riwaya ya *Vita vya Mapenzi* unamshtua msomaji pale jini anapompangia mwanadamu aoe. Kwa kutumia ishara za nyota ya shamsi inakuwa ni kigezo Mzee Sufian kumchagulia Suhail kumuoa Binti yake Shekhia huko ujinini. Wazazi wa Sharifa na wazazi wa Suhail huko kwao Tabora wanafikia uamuzi wa kuwaozesha watoto wao kwa vile muda umefika na hawaoni sababu ya kucheleweshwa kwa ndoa hiyo. Hii ni kutokana na umuhimu wa wazazi na familia hizo kulinda heshima zao na kuendeleza kizazi chao. Wasichokijua ni kuwa Suhail tayari amekwsiha oa jini na hataki tena kumwoa Sharifa. Anatumia hila kuishi naye kwa kuwaliwaza wazazi wake lakini ukweli katika ndoa hiyo wanaujua watu wawili tu, Sharifa na Suhail.

Uajabu ajabu unajitokeza pale wanapotaharuki kuwa mambo mengi yaliyo zaidi ya yale tunayoyaona kwani Suhail anawaowa ndugu wawili bila yeye kujua na kati ya ndugu hao mmoja ni jini-nusu ambaye ni Shekhia na mwingine ni binadamu wa kawaida ni Sharifa. Kwa hiyo, mtunzi ameenda mbali zaidi kwa kumtumia mhusika ndugu mwingine ambaye ni jini mtu katika kuchimuza ujumbe wa kwamba, si vizuri kuolewa au kuoa bila kumfahamu mtu unayemuoa au kuolewa na mtu ambaye ndugu zake huwafahamu vizuri. Shekhia na Sharifa wamejikuta kuwa ndugu, Shekhia na Sharifa ni mtu na mdogo wake kutoka katika tumbo moja na Suhail ni mtoto wa mama yao mkubwa, walikuwa hawajuani Suhail anaumia sana baada ya kujua hilo. Suhail anasema;

> Mungu wangu ina maana Shekhia na Sharifa ni ndugu? Tena wa mama mmoja! Alilopoka Suhail Bila ya kutegemea, mara akaishiwa nguvu na kujikuta anaporomoka juu ya kochi. Ni fedheha kubwa kushuhudia ndugu wa mama mmoja kuwa ni wake wa mume mmoja! Halafu wanakuja kugundua hili mkiwa wote muwajawazito (uk 280).

Taharuki hii inawatokea wananchi wanapokuja kujua kuwa viongozi waliowaamini kwa muda mrefu wamekuwa wakiwasaliti kwa muda mrefu.

Kizazi cha wanadamu kinawawakilisha akina nani? Kizazi cha majini kinawawakilishi akina nani? Kwa nini majini, wachawi na mitandao kama ya Black Scorpion katika *Vita vya Mapenzi* wanatokea kwa hila na hawaonekani waziwazi? Kwa nini majini

wanatawala fikira na ndoto za wanajamii. Ndoto zinazoibuka na kuwa ni za kweli? Maswali haya yanazua fikira kuwa Mwingizi anatumia taswira za majini na wanadamu katika muktadha wa nchi zinazofanana na himaya ya Budha inayotegemea nguvu za pete kwa ustawi wao na nguvu za utawala. Pete au kibuyu ikiwa ni nguvu ya rasimali ambayo huwapa wenye kumiliki nguvu za kifedha na kitawala. Rasilimali hizo hugombaniwa baina ya nguvu hizo mbili. Ndoa yao ni ya mashaka kwani ina masharti na si ya mapenzi ya kweli. Ndoa ya dhati kama ile ya Sharifa na Suhail yaani viongozi na wanajamii hairuhusiwi kuwepo. Majini au mabeberu maana wa wanajamii akina Suhail kuwatumikia wananchi wao. Wanachotakiwa kufanya ni kuwa chini ya himaya ya Budha, Waufi au Wachawi.

Nguvu ya pesa anayoipata Suhail ni mfano wa kutimizwa kwa masharti ya kupewa fedha hizo na mabwanyenye na mabeberu. Ni misaada yenye mitego na masharti yasiyo na maslahi kwa wanajamii walio wengi. Suhail anatumia pesa zake hata kupindisha sheria kwa sababu kisheria mtu yeyote anayepatwa na matatizo ya ajali anatakiwa aende polisi ili aweze kupewa kibali cha kwenda kutibiwa. Lakini yeye anamhonga dokta na anamtibu Sharifa. Tukio hili linaonyesha mambo mengi yakiwa ni pamoja na udhaifu wa binadamu kujikweza kwa sababu ya kuwa navyo na kwa hivyo kukiuka wajibu, staha na sheria. Mali na hususan pesa zinakuza kiburi, purukushani, majivuno ya kutojali kufanya mambo kadri yanavyostahili. Kwa mfano, Suhail anakuwa mwepesi wa kupuuza sheria na wajibu na kwa sababu hiyo Suhail anasawiriwa kama kielelezo cha rushwa katika jamii. Suhail anachimuza ujumbe wa watu kutumia pesa za hongo katika kukwepesha sheria mbalimbali za nchi.

Kadri msomaji anavyofuatilia wasifu, hulka na maingiliano ya Suhail na marafiki zake, jamii yangu na umma mpana kwa jumla, msomaji anabaini kuwa unafiki ni moja kati ya wasifu wa kimsingi wa Suhail. Kupitia kwa usawiri huu, Mwingizi anazichambua dosari za viongozi kukosa uadilifu na uwajibikaji ndio maana maeneo yao wanayoyaongoza hayaridhishi kwani viongozi wanajinenepesha wenyewe bila kujali wananchi wao. Haya yote yanasababishwa na kufuata masharti na mitandao ya majini, wachawi na wahujumu

uchumi kama ilivyo katika riwaya teule za Mwingizi. Suhail anasema:- "Aah baba hizo ni imani potofu tu, kama watapatikana viongozi wenye dhamira safi hakika patabadilika tu" (uk. 81).

Mwingizi anaona kwamba, kupatikana kwa viongozi ambao watakuwa na dhamira safi na wawajibikaji ndio kunaweza kuleta mabadiliko katika maeneo wanayoishi. Sehemu nyingi za Afrika hakuna maendeleo na hasa kuhusu huduma za jamii kama vile barabara, shule, hospitali na ofisi mbalimbali za serikali zina majengo ya zamani sana. Viongozi wanaingia mamlakani kwa dhamira ya kujineemesha wenyewe. Jambo hili linadhihirika pale ambapo Suhail anatoka Dar es Salaam na kwenda kumsalimia baba yake. Baada ya mgogoro mkubwa na baba yake wa kumuomba arudi nyumbani baada ya kupata ajali akachanganyikiwa na pesa za kimajini za Mzee Sufian. Ndipo wakiwa wanaongea Suhail anashangaa kuona mji wa Tabora haujabadilika na barabara ni mbaya kama zamani. Ila viongozi wanajineemesha wenyewe.

Mtunzi amemsawiri mhusika Suhail kama mtu mbinafsi, kama mhusika mwenye nafsi mbili kwani kuna wakati ni jini na kuna wakati ni binadamu wa kawaida, pia Suhail amesawiriwa kama mtu ambaye amevuka mipaka ya kijamii, kitaifa na kimataifa kwani anafanya matukio yake akiwa katika jamii yake nchini Tanzania na wakati huohuo anasafiri kimajini na kwenda katika nchi nyingine ya Yemen. Kuvuka mipaka ya kutenda mambo yake ni kubainisha jinsi mitandao ya utandawazi na ubeberu isivyo kuwa na mipaka, na haijali rangi, jinsia, umri, kabila, dini au itikadi ya kisiasa. Aidha mtunzi kupitia uhusika changamano wa Suhail ameweza kuchimuza dhamira mbalimbali kama vile usaliti, haki na sheria, mafao binafsi, ukatili, maadili, uwajibikaji na kadhalika.

#### 4.3.1.2 Maslahi binafsi, Ukoloni Mamboleo, Unyonyaji, Uwajibikaji na Malezi

Usawiri wa Mzee Sufian katika riwaya hii ni usawiri mseto, unaokita katika uhalisi na katika uhalisiajabu. Mzee huyu yeye ni jini tena ni jini mwenye asili ya kiasia kutoka nchini Yemen. Mwandishi ametumia uhusika huu wa kijini katika kuchimuza maudhui

mbalimbali. Mhusika Mzee Sufian amekuwa ni mhusika mwenye nafsi mbili kwa kiasi kikubwa amekuwa mhusika wa kiuhalisiamazingaombwe kwani matukio yake mengi anayatenda akiwa amevaa uhusika wa kiuhalisiamazingaombwe. Na kwa upande wa uhusika wa kiuhalisia ametumika kwa kiasi kidogo sana, hasa pale inapodhihirishwa kwamba ana unasaba na Suhail na familia yake. Mhusika huyu pia amevuka mipaka ya kijamii na kimataifa kwani kuna wakati anafanya matukio yake akiwa Tanzania na wakati huohuo akiwa Yemen na wakati huohuo akiwa baharini katika himaya ya Budha.

Kupitia kwa uhusika changamano wa Mzee Sufian matumizi anachimuza dhamira kama za maslahi binafsi, ukoloni mamboleo, unyonyaji, utandawazi, uwajuibikaji na malezi. Aidha Sufian anavuka mipaka ya uhusika wa kawaida katika kutupeleka mbali zaidi kutokana na mtunzi kumsawiri kama mhusika changamano ili kuonyesha kwamba katika ulimwengu wa kawaida mambo haya yapo lakini yamekitwa katika uhalisiamazingaombwe ili kumfikirisha msomaji kuona kwa namna nyingine jinsi ulimwengu ulivyogubikwa na mambo fulani fulani mazito.

Mzee huyu ni miongoni mwa abiria waliokuwa katika basi alilopanda Suhail kurudi kwao Tabora. Na ndiye anasababisha ajali kwa nguvu zake za kijini ndipo aweze kumpa Suhail dola nyingi za kimarekani na masharti ya kumuoa Binti yake ambaye naye ni nusu jini na anamkabidhi pete ili aweze kuisimamia miradi mbalimbali. Mwandishi kupitia Mzee Sufian anachimuza dhamira ya jinsi mataifa yaliyoendelea yanavyotumia nafasi zao katika kunyanyasa na kuyafanya mataifa ambayo hayajaendelea yaendelee kuwa masikini kwa kuendelea kutoa misaada ambayo hatimaye,yanafaidi zaidi ya mataifa. Kitendo chake cha kumshurutisha Suhail kwa hila, (kwa kumtegea begi la fedha} na kusababisha ajali, kinaonyesha ni kwa kiasi gani walio na nguvu za kifedha na tamaa ya ubinafsi walivyo na mbinu na mikakati ya kushind. Hawajali madhara yanayoweza kusababishwa na hatua zao ikiwemo kuua halaiki ya watu na hata kusababisha maafa, magonjwa, mauaji ya kimbari au vita vya wenyewe kwa wenyewe ilimradi wanafanikisha miradi na mipango yao kupitia watu wachache kama Suhail. Mzee Sufian ni mwakilishi wa mitandao ya kibwanyenye inayonyemelea

rasilimali za umma au za nchi masikini kwa njia ya kuwalagahai viongozi na wananchi wapokee fedha na kusaini mikataba hewa. Pete ni mkataba aliosaini Suhail ambao una masharti ya kafara la damu ambalo ni sawa na rasilimali za taifa.

Caufield (1997) anaonya kwamba, watu matajiri hufanya hila ya kuendeleza utajiri wao zaidi kwa njia ya kuwakandamiza walio maskini kupitia misaada kwa mataifa yanayoendelea yenye masharti magumu sawa na kumuua ndugu yako. Caufield anatuonyesha jinsi mataifa yaliyoendelea yanavyotuchagulia misaada kwa ajili ya manufaa yao na hata wakati mwingine tukipewa misaada tuliyoomba, masharti huwa makubwa sana na yanayogharimu mataifa yanayoendelea. Maelezo haya ya hali halisi za kimahusiano kati ya nchi za ulimwengu yanaakisiwa na usawiri wa mhusika Mzee Sufian. Sufian anafananishwa na viongozi wa mataifa yaliyoendelea wanaotumia nafasi na nguvu zao katika kuhakikisha wanazidi kupata faida kubwa. Sufian anampa Suhail msaada wenye masharti, miiko na mikataba, msaada ambao hatimaye unamrambisha starehe na ufahari wa muda na machungu na kite kwa upande mwingine na kisha unamsababishia umauti. Fauka ya kuwasilishwa kama taswira ya mataifa yaliyoendelea, mtunzi pia anamsawiri Sufian kama mfano wa viongozi waliomo katika mataifa yanayoendelea ambao hutumia nafasi pia katika kuwanyanyasa wananchi na wengi wao hutumia njia mbalimbali katika kuwahadaa wananchi na kujilimbikizia mali kwa kujifanya wanatoa vimisaada vidogovidogo kwa wananchi.

Mtunzi anatupeleka mbali katika kuonyesha jambo ambalo si la kawaida katika ulimwengu halisi yaani ajali inasababishwa kimajini, na mhusika anayesababisha ajali papohapo anakufa lakini baadaye anaenda kuonekana mzima sehemu nyingine. Aidha Mzee huyu anauwa watu wengi kwa makusudi kabisa kwa ajili ya kumpa dola na pete Suhail katika kuendeleza miradi yao. Mzee huyu kupitia ajali hii anachimuza ujumbe wa jinsi mataifa yaliyoendelea yanavyokuwa radhi kukuza hali za uhitaji bandia katika mataifa machanga kama vile kusababisha uhaba wa vitu fulani vinavyozalishwa au vinavyopatikana katika nchi zilizoendelea, kupiga vita tiba za kiasili ili kukuza masoko ya kuuza dawa za viwandani ambavyo wanavimiliki wao au hata kuwaua watu

wengi wa Afrika kupitia mauzo ya silaha ili kuendeleza uhasama waliouzua wenyewe na kuchochea misukosuko katika nchi zinazoendelea kwa ajili ya maslahi yao binafsi. Aidha mataifa hayo yanawauwa watu wa Afrika kupitia wawekezaji wao wanaokuja kuwekeza katika nchi za Afrika wamekuwa wakisababisha wananchi wengine kufa kutokana na athari za uwekezaji wao unaojumuisha uharibifu wa mazingira unaotokana na uchimbaji madini, uharibifu wa hewa kutokana na moshi wa viwanda vyao, magonjwa yanayosababishwa na kemikali za madawa ya kuuwa wadudu katika mashamba ya maua, uharibifu wa vyanzo vya maji kutokana na uingizwaji wa maji machafu yanayoelekezewa katika makazi ya watu kutoka katika viwanda vyao.

Mfano mzuri upo katika makampuni yanayowekeza katika rasilimali kama vile za madini au viwanda ambavyo kwa kujali masalahi yao, wanasababisha uharibifu wa mazingira katika maeneo waliyowekeza na uharibifu wa afya ya wanajamii. Hiki huwa chanzo cha vifo kwa baadhi ya wananchi katika sehemu ambako wamewekeza. Kunawepo na mivutano baina ya vikundi vya kutetea haki za kibinadamu, wizara husika na viongozi wa makampuni hayo katika kuzingatia haki za kibinadamu, afya na maslahi ya wananchi. Mzee Sufian hajali ni watu wangapi watakufa katika basi lile ili mradi malengo yake ya kujilinda kupitia Suhail yanatimia. Anakufa kimazingaombwe katika ajali kabla ya kuenda sehemu nyingine kuwaangamiza wengine. Ndivyo mataifa haya yaliyoendelea yanavyofanya kwa nchi maskini. Umazingaombwe unaosawiriwa katika tukio hili umedhamiriwa kuwezesha tafakuri ya kutathmini mahusiano katika viwango na daraja nyingi. Katika daraja ya mtu binafsi, pengine mtunzi anatusukuma kujiuliza binadamu anahitaji kumwaga damu kiasi gani ya binadamu wenzake ili kukidhi au kuridhisha maslahi ya ki binafsi. Katika daraja ya mahusiano ya kimataifa, ikizingatiwa kwamba Sufian anatoka katika himaya kwasi akilinganishwa na Suhail, mtunzi anaibua haja ya kudadisi faida zinazoletwa na misaada ya kigeni zinapolinganishwa na madhara yanayoletwa na misaada hiyo. Kwa usemi mwingine, kuna haja kujiuliza ni wapi inafaa kuweka mipaka kati ya neema za ki binafsi na mafao ya kijamii.

Kitendo cha Mzee huyu kusababisha ajali kwa nguvu za kichawi katika basi lile inaonyesha wazi kabisa basi lile limetumika kama chombo cha kuwaangamiza waafrika kwa kutumia mali zao, viwanda vinavyojengwa katika makazi ya watu, pia unyanyasaji kwa waafrika wanaofanya kazi katika migodi na viwanda vyao. Mzee Sufian ameonekana kuwa ni mtu asiye na huruma kabisa hasa pale anapoendeleza mambo ya kumhakikishia ujiendelezaji wake mwenyewe. Pia Mzee huyu anachimuza dhamira ya kuonyesha kwamba katika biashara za kimataifa, hasa zile zilizokitwa katika uwekezaji wa kiunyonyaji, faida na tija ya kibiashara inawekwa mbele zaidi kuliko maisha ya binadamu. Hali kadhalika, Mzee Sufian anachimuza maudhui ya jinsi maisha ya wanyonge yanavyotolewa kafara ambapo watu wanakufa kama watu binafsi, kama wawakilishi wa tabaka, nchi au taifa. Vifo vya wananchi hawa, kama wanavyowakilishwa na abiria katika basi, ni virutubishi tu katika biashara za kimataifa. Kwa njia hii, Sufian anasawiriwa kama kielelezo cha viongozi barani Afrika na jinsi walivyo makatili kupitia hiyo ajali ya gari kwani viongozi hawa wako tayari kuwaangamiza wananchi wao kwa ajili ya kung'ang'ania na kudhibiti nyenzo na mihimili ya madaraka, kudhibiti mifumo na michakato ya kubuni sera, kudhibiti na kuelekeza watekelezaji wa sera na mipango ya kiserikali, na wanafanya haya kwa makusudi wakijua fika kwamba ndani ya vitendo vyao kumekitwa maslahi fiche ya ki binafsi. Kwa hivyo, mauaji na maangamzi ya wanachi yaliyodhahiri na yasiyo dhahiri, ni mkakati tata wa kuendeleza mafao ya ki binafsi kwa viongozi wengi wa Afrika.

Fauka ya dhamira hizo tunapata dhamira nyingine Bagamoyo nyumbani kwa Mzee Sufian. Kunatokea msiba wa mke wa Sufian aliyekufa kwa kuzolewa na kimbunga kimazingaombwe, jambo ambalo si la kawaida. Mzee Sufian alikuwa amesafiri wakati wa tukio hili na aliporudi, alikuta majirani wamemzika mkewe baada ya kumsubiri kwa muda wa wiki mbili bila kurudi. Mwandishi anasema:

> …baadaye wazee wakasogea tena pale, wakamstiri mama yule ili wamsubiri mumewe arudi lakini haikuwa hivyo, ilichukua takriban siku mbili bila ya mumewe ambaye ni baba yake na Shekhia kurejea hivyo viongozi wakaamua kwenda kumzika tu yule mama huku wakimchukua Shekhia kipindi hicho akiwa mdogo sana. Wiki mbili baadaye ndipo yule Mzee alirejea, alipofika akapewa taarifa za tukio lile lakini cha ajabu hakuonekana kushtushwa sana na habari zile, ni kama vile aliyekuwa akijua kila kilichotokea, alichokifanya akaenda kwa

> majirani tu kutoa shukrani zake kwa kumsitiri mkewe kisha akamchukua mwanaye (uk. 41)

Mwandishi anachimuza ujumbe wa jinsi viongozi wengi barani Afrika wanavyosababisha maafa kwa familia zao katika vita vya kugombea madaraka au kuendelea kuwepo madarakani kwa muda mrefu. Mzee Sufian anasababisha kifo cha mkewe Amanda katika vita vya kuwania uongozi na uongozi wa Budha. Sufian anamuua mkewe anayempenda sana kwa ajili ya maslahi yake kibinafsi ya kung'ang'ania uongozi. Ndio maana hata aliporudi na kukuta wamemzika mkewe hakushtuka kwa sababu alikuwa anajua yeye ndiye aliyesababisha kifo hicho. Mtunzi kupitia tukio hili la mke wa Sufian anachimuza dhamira ya jinsi baadhi ya matajiri wengi wanaopata utajiri kwa njia isiyo halali wanavyowauwa ndugu zao wanaowapenda ili waweze kupata utajiri. Jambo linalojitikeza hapa ni mvutano kati ya nguvu ya maslahi binafsi dhidi ya maslahi ya umma au familia.

Swala lingine ambalo mwandishi anaonekana kulipa msisitizo ni uendelezaji wa ya mifumo binafsi, yaani uendelezaji wa maslahi ya ki binafsi pasina kujali mifumo hiyo inamwathari nani na nani tena kwa njia gani. Ni wazi kwamba mwandishi anaidadisi mifumo hii binafsi hasa kwa kujaribu kudhihirisha kuwa imeanza kusambaratisha jamii ya mtunzi. Ulimbikizaji wa mali na maisha ya ufahari yasiyojali jamii na ndugu wa karibu ni mabadiliko yanayotokea kwa wingi katika jamii yake. Kwa kumtumia Mzee Sufian, Suhail, na Shekhia, mtunzi anatuchorea mabadiliko ya mtazamo na uonoulimwengu unaowakumba wanajamii yake. Mifumo ya kiuchumi na kijamii na kitamaduni inabadilika, ambapo ile jamii inayothamini utu, maadili, na ustaarabu umebadilika. Mtunzi anakiuka mipaka katika kuweka sifa changamani kwa mhusika mmoja ambaye wakati huohuo anachorwa kama mtu mwenye sifa hasi na wakati huohuo anachorwa kama mtu mwenye sifa chanya.

Mzee Sufian alikuwa na ugomvi mkubwa na kiongozi awa majini aliyekuwepo mamlakani katika himaya ya Budha. Ugomvi huu ulisababishwa na kiongozi ambaye

muda wake wa kuwepo mamlakani ulikuwa umeisha lakini akawa amemuaandaa kiongozi mwingine wa kushika madaraka yake. Japo viongozi wengi na wanahimaya ya Budha walikuwa wanamtaka Mzee Sufian ndiyo awe kiongozi wao. Siku zote kiongozi anayefanya kazi vizuri wananchi humpenda sana na humtaka ashike nafasi kubwa zaidi kama ya urais. Ndivyo ilivyokuwa kwa Mzee huyu wanahimaya walimpenda sana. Mwandishi anasema:-

> Sasa ilipoanza kukaribia kipindi chao cha uchaguzi kila kikundi kikawa kinamuandaa Jini aliyeonekana kuwa na uwezo wa kuukwaa uongozi wa juu wa himaya hiyo ya Budha. Sasa kiongozi anayemaliza muda wake naye akawa anamuandaa jini aliyemtaka yeye ili aje amuachie madaraka hayo kwa ajili ya kuficha maovu yote aliyokuwa akiyafanya kipindi cha utawala wake. Wakati huohuo wanahimaya wengine wa Budha nao walikuwa wamemuandaa jini mwingine aje ashike madaraka hayo, Jini huyo aliitwa Sufian Bin Shamhurish!" (uk. 52).

Aidha mwandishi anachimuza maudhui ya viongozi kurithishana madaraka kwa kujuana, kwa kupuuza na kukiuka katiba na sheria za nchi, kwa kukaidi maafikiano na matarajio, na zaidi hata kwa kubadilisha katiba za nchi zao ili wajihakikishie kusalia mamlakani. Hapa mtunzi anaendeleza dhana ya kwamba hivi ndivyo ilivyo katika mataifa ya Afrika. Mzee huyu pia amesawiriwa kama kifani cha viongozi wawajibikaji katika nafasi zao. Alipokuwa katika utawala wa Budha yeye alikuwa ni mkuu wa kitengo cha ulinzi na utajiri na alikishika kitengo hicho kwa umakini wa hali ya juu kiasi cha kuwafanya wananchi wake kumpenda sana kutokana na uwajibikaji wake katika utendaji kazi wake. Wakamtaka agombee nafasi ya juu zaidi, mwandishi anasema:-

> …. Mzee Sufian Shamhurish ndiye alikuwa mkuu wa kitengo cha ulinzi na utajiri, na alikishika kitengo hicho kwa umakini wa hali ya juu kiasi cha kufanya baadhi ya majini wenziye wamteue yeye ashike nafasi ya juu ya utawala huo. Hapo sasa ikawa ni vita ya ushindani baina ya makundi mawili hasimu. Kundi la Mzee Sufian na kundi la kiongozi anayemaliza muda wake. Ikawa ni mshikemshike almanusura ya kuuwana (uk 53).

Mzee Sufian anachimuza ujumbe wa kiongozi asiyekubali kushindwa pamoja na kwamba ana mapungufu baada ya wapinzani wake, rafiki zake na kiongozi aliyeko

mamlakani kumtafuatia sababu ili asiweze kushika nafasi hiyo. Baada ya kuona Mzee Sufian ana nguvu za kuushinda utawala uliopo mamlakani wakaamua kumuundia kashfa kubwa itakayopelekea kumnyima sifa za kuwa mgombea wa nafasi hiyo ya juu kabisa katika himaya yao. Ndivyo ilivyo katika mataifa mengi katika kipindi cha uchaguzi inapotokea kuna mgombea anayekubalika sana na wananchi wapinzani wake humuundia kashfa chafu ili asikubarike. Mtunzi anavuka mipaka kwa kutuonyesha kwamba kinachomfanya Sufian asipate uongozi ni kwa sababu ana mpenzi ambaye siyo jini anayeishi duniani kwa hiyo Sufian hutoroka na kwenda duniani kutembea naye halafu hurudi. Kitu ambacho si cha kawaida lakini mtunzi amempa uhusika mseto mhusika Sufian katika kuchimuza maudhui haya.

Mtunzi anaendelea kuonyesha kuyumbishwa kwa mipaka katika kuweka uchangamani wa matukio kwa kuendelea kumuonyesha mhusika Sufian anavyoishi chini na ndani ya bahari na duniani pia katika matukio yake mbalimbali. Mtunzi anasema baada ya Mzee Sufian kushindwa na washirika wa kiongozi aliyeko mamlakani anaamua kuondoka huko chini ya bahari kwenye himaya ya Budha na kuja duniani kusubiri kipindi cha huyo kiongozi aliyeteuliwa na kiongozi aliyeko mamlakani kimalizike ndipo aweze kurudi tena kwa ajili ya kugombea nafasi hiyo. Mwandishi anasema:-

> Bwana Sufian hakukubali kushindwa akapambana kujisafisha kwa muda mrefu sana Bila mafaniko, ndipo akaamua kutoroka na kundi la wafuasi wanaomuunga mkono, akatorokea duniani huku lengo lake likiwa ni kuishi huku kwa muda wote wa kumalizika kwa utawala wa huko kwao ili hapo ndipo arejee ghafla kutwaa madaraka (uk 53).

Kupitia nukuu na maelezo haya Mzee Sufian anachimuza ujumbe wa viongozi ambao hawakubali kushindwa kwa namna yeyote ile kwani huamini kwamba hakuna kiumbe asiye na udhaifu. Vivyo hivyo hata kwa viongozi mbalimbali pindi wanaposhindana ili kupata nafasi ya juu kabisa serikalini, hutumia hata mbinu ya kuwachafua wenzao kwa kuwatafutia makosa madogomadogo sana ili wasiweze

kushika nafasi hizo. Mzee Sufian anachorwa kama mtu wa aina hiyo asiyekubali kushindwa kwa namna yeyote ile. Mbali na kuchimuza wasifu, tabia na matamanio ya mtu binafsi, Mzee Sufian anachimuza kanuni za kiutawala katika nchi za ulimwengu wa tatu yaani uongozi katika misingi ya maslahi ya mtu binafsi au makundi mahususi ya kijamii na sio uongozi katika misingi ya sera, ruwaza na mipango.

Mzee Sufian anachimuza pia maudhui ya viongozi wanyonyaji na wasio na huruma kwa wananchi wao. Kwani baada ya kuondoka Budha anaondoka na pete ambayo ndiyo iliyokuwa na kazi kubwa kule Budha kiulinzi na kiuchumi. Pete anayoiiba Mzee Sufian ni kitu ambacho kina uwezo mkubwa kuliko hata binadamu kitu ambacho katika hali ya kawaida hakiwezekani. Pete hiyo ilikuwa inaleta utajiri mkubwa katika himaya hiyo. Mwandishi kupitia Sufian anachimuza dhamira ya viongozi ambao pindi wanapoona wanashindwa kushika nyadhiifa kubwa serikalini na hasa za urais huamua kutoroka na mali nyingi zenye thamani nyingi kwenda katika nchi nyingine. Mfano mzuri ni rais wa Gambia, Yaya Jammeh aliyeongoza kwa muda wa miaka ishirini. Lakini aliposhindwa na mpinzani wake Adam Barrow, akaamua kukimbilia nchi nyingine pamoja na dola milioni kumi na magari ya kifahari mengi baada ya kushindwa kuchaguliwa kwa mara nyingine. Kwa hivyo, mtunzi katumia pete aliyoondoka nayo Mzee Sufian katika kutufikirisha zaidi juu ya mienendo ya baadhi ya viongozi wa mataifa ya Afrika walivyo wa binafsi na wenye tamaa iliyopitiliza.

Ndivyo ambavyo Mzee Sufian alivyoondoka na uchumi wa nchi ile ya Budha na kuiacha nchi ile ya kimajini na wananchi wake wakiteseka kwa sababu aliondoka pamoja na pesa nyingi sana. Mwandishi anasema:-

> Kikubwa kilichowafanya wahangaike kumtafuta ni kwamba bwana Sufian alitoroka na kitu adhimu sana kwa mustakabali wa himaya yao, kitu ambacho ni kama roho ya himaya yao, kitu ambacho kinayabeba na kuyaongoza maisha ya himaya yao kiulinzi na kiuchumi. Kitu hicho kilikuwa ni Pete Kubwa isiyokuwa na rangi maalum, Iliitwa *‘Khatam Budha’* Pete hiyo alikuwa akiimiliki bwana Sufian kwa kuwa Kitengo cha Ulinzi na Fedha kilikuwa chini yake yeye hivyo

> akapata fursa ya kutokomea nayo duniani, sasa Wanahimaya wa Budha wakaingiwa na hofu kuwa hawana Ulinzi tena wala hawawezi kupata mali kubwa kubwa za baharini na ardhini kwa kuwa zana yao hawapo nayo tena (uk 54).

Mtunzi anaonyesha uhusiano wa kiduara yaani matukio yanafanyika hapa Tanzania halafu muda huohuo yanafanyika nchini Yemen. Ndivyo matukio haya yalivyokuwa yanafanywa na Mzee Sufian kutokana na kukimbia na uchumi (pete) wa himaya ya Budha. Serikali ya Budha ikawa inamtafuta kila mahali alipo ili imwangamize, akakimbilia Yemen. Himaya ya Budha wakabahatika kumuona kwa kutumia nguvu za kimajini. Ndipo vita ikawa kubwa sana huko Yemen kati ya utawala wa Budha na Sufian. Ndipo ile pete ikawaka mishale ya ajabu mkononi kwa Suhail huko Dar es Salam kuashiria Mzee Sufian ana matatizo ikabidi Suhail amtafute huko na akampata. Kukawa na vita vikali kati ya askari wa himaya ya Budha na Sufian pamoja na Suhail.

Hili linadhihirisha wazi unapoiba au unapoharibu uchumi wa nchi na kuondoka nao kwa madai kuwa hautapatikana au kwa kuwa wewe ni kiongozi mkubwa serikalini hawataweza kukukamata si kweli. Baadhi ya viongozi wa nchi za Africa pindi wanapoondoka mamlakani hukimbia na pesa, mali nyingi za umma na kwenda nchi nyingine. Hata hivyo wamekuwa wakikamatwa na kurudisha baadhi ya mali. Hivyo Mzee Sufian alifikiri kwamba uongozi wa Budha hautamkamata kwa kuondoka na pete yao ya ulinzi. Mwandishi anaonyesha jinsi alivyokutwa nchini Yemen na utawala wa Budha. Kadhalika Mzee Sufian anafananishwa na wanasiasa ambao wanapoona serikali inawafuatilia katika vitega uchumi vyao wanaamua kuandika majina ambayo si yao na kupeleka baadhi ya pesa na mali zao katika nchi nyingine ili wasiweze kukamatwa. Ndivyo ilivyokuwa kwa Mzee Sufian alipoondoka na pete ambayo ni uchumi na ulinzi wa himaya ya Budha na kuupeleka duniani kisha kumpa Suhail ili yeye aonekane hana mali.

Mzee Sufian anachimuza dhamira nyingine chanya kwani anaonekana ni baba mzuri katika ulezi anamhasa mwanaye Shekhia kwa kosa la kumtesa mumewe na anamwambia anapaswa kuwa mvumilivu. Mzee Sufian anamwambia mwanaye baada ya kulalamikiwa kwamba Suhail amemfanyia kitu kibaya. Baba huyu anaonekana kuwa na malezi mazuri sana kwa Binti pasipo kumtetea. Kwani kuna wazazi wengine wamekuwa wanawatetea watoto wao hata kama wanafanya ujinga kwa waume zao. Lakini kwa Mzee huyu imekuwa tofauti kabisa anamuonya mwanaye aacha tabia ya kutomhuheshimu mumewe. Mtunzi kupitia mhusika Sufian aliye na sifa za uhusika wa nafsi mbili yaani kuna wakati anakuwa mtu halisi na kuna wakati anakuwa mhusika wa kimazingaombwe ama kimajini ameweza kuchimuza dhamira mseto kama vile ukoloni mamboleo, maslahi binafsi, uongozi, unyonyaji, uwajibikaji na malezi. Usawiri wa mhusika huyu umekitwa katika misingi ya mitagusano ya uhalisia na uhalisiajabu katika kuchimuza mambo ya msingi ambayo mengine yanazikumba nchi zinazoendelea.

#### 4.3.1.3 Mapenzi, Pesa, Utandawazi, Nafasi ya Mwanamke na Familia

Baadhi ya maswala ambayo mtunzi anayachanganua ni maswala yanayohusiana na mapenzi, pesa na mifanyiko ya kifamilia. Inawezekana kuhoji kwamba, Maundu Mwingizi anatafakari jinsi pesa inavyoathiri mahusiano ya kimapenzi na kifamilia kwa njia zilizo chanya na wakati huo huo njia hasi. Mahusiano kati ya Shekhia na Suhail na kati ya Sharifa na Suhail kwa upande mwingine yanashawishiwa, yanayumbishwa na yanaathiriwa na maswala ya pesa. Ili kuchimuza maswala haya, mtunzi amewatumia wahusika mseto wanaotangamana na kuwa na mitagusano changamano katika familia na jamii kwa jumla. Kwa mfano, Shekhia ni mtoto wa Mzee Sufian, yeye ni ni mtu-jini (nusu mtu na ni nusu jini), kwa sababu baba yake alikuwa ni jini na mama yake alikuwa ni binadamu wa kawaida. Shekhia anaingia kwenye mahusiano ya kimapenzi na Suhail bila Suhail kujua kama ni jini-mtu. Shekhia wakati anasoma Chuo Kikuu cha Dar es Salaam alikuwa na mahusiano ya kimapenzi na Suhail. Suhail alikuwa na mahusiano na Shekhia kwa lengo la kupata pesa kwa sababu Shekhia alikuwa na pesa nyingi. Na baada ya kumaliza chuo akaachana na Shekhia kwa sababu alikuwa na mpenzi wake Sharifa.

Suhail pamoja na kumwacha Shekhia, anakutana kisadfa na kimajini na baba yake Shekhia katika basi na wanapata ajali akiwa anarudi kwao Tabora baada ya kumaliza masomo japo Suhail alikuwa hamjui baba huyo. Ndipo baba yake Shekhia akampa dola nyingi pamoja na pete kwa sharti la kumuoa mwanaye na kuziendeleza mali alizoondoka nazo kwenye himaya ya Budha. Suhail anakubali pasipo kujua kwamba Shekhia aliyekuwa mchumba wake chuoni ndiye mtoto wa Sufian. Shekhia anachimuza ujumbe wa kukiuka utamaduni wa kiafrika kwa kitendo cha kumtongoza mwanamume kwani, alipokuwa anasoma Chuo Kikuu cha Dar es Salaam alikuwa anampenda sana Suhail. Shekhia akaamua kumtongoza Suhail kwa sababu alikuwa ana pesa Suhail anamkubali kwa tamaa ya pesa lakini alikuwa hampendi kutoka moyoni. Mwandishi anasema:

> Baada ya kipindi kirefu cha urafiki wa kawaida, hisia za kimapenzi zikaanza kuchepua moyoni mwa Shekhia ambaye licha ya utamaduni wetu wa kitanzania kuwabana watoto wa kike kuzianika waziwazi hisia zao kwa wanaume, yeye alijieleza kwa Suhail. Tamaa ya pesa ikamfanya Suhail akose kipingamizi dhidi ya mrembo huyo. Baada ya kuhitimu masomo ndipo sasa Suhail akaiweka wazi sura yake ya upande wa pili kuwa hakumpenda kwa dhati Shekhia, na kwamba ana mchumba wake huko Tabora…akamtelekeza Shekhia na kuingia mitini (uk 58).

Hali hii inadhihirisha wazi si jambo la kawaida katika utamaduni wa kiafrika mwanamke kumtongoza mwanamume lakini mabinti wengi siku hizi wanatongoza wanaume na kuna wanawake watu wazima wenye pesa nyingi wanatongoza watoto wadogo na kutembea nao. Vitendo vyote vya kimapenzi na kimahusiano vinavyotendwa na Shekhia kama vile ujasiri wa kumtongoza Suhail, kumwekea masharti ya kimahusiano na vingine, vimekitwa katika misingi ya kuwa na umiliki mkubwa wa pesa. Kwa hivyo, makuzi ya Shekhia ni makuzi ya kifedha tofauti na makuzi ya Suhail. Hapa kunachimuzwa swala la nafasi ya pesa katika ulezi na makuzi ya mtu binafsi. Shekhia anaonekana kuwa mwanamke katili kwa mumewe kwani anamtishia mumewe kwamba anakufa endapo ataoa mwanamke mwingine. Wakati Suhail akiwa na mchumba wake aitwaye Sharifa kwa muda mrefu hata kabla ya kwenda Chuo Kikuu na ilitakiwa amuoe Shekhia kwa nguvu zake za kimajini na kiuchawi anafanya juu hadi anampata Suhail. Shekhia anamsababishia ugonjwa mbaya sana mke mwenziwe aitwaye Sharifa kwa kutumia majini ili afe.

Dhamira hii ya ukatili wa mwanamke huyu ipo sana katika jamii zetu kwa wake wenza. Wanawake zaidi ya mmoja. Wake wenza hugombana mpaka kufikia hatua hata ya kuuana kwa kutumia uchawi na ushirikina. Lakini ugomvi huu hauchipuki kwa sababu ya hisia za kimapenzi, Sharifa kama mke mwenza ni tishio dhidi ya umiliki wa fedha na utajiri, tishio dhidi ya ujasiri alio nao Shekhia. Kwa hivyo hapa, pesa inahusika sio tu kutawala michakato ya kimahusiano, inakuwa ndio msingi hasa wa kimahusiano, ginavunja misingi ya kitamaduni, inavunja maadili ya kusema ukweli, inakuza uongo, ujanja na hadaa, pesa inakuza dharau, chuki na kisasi. Hivyo basi mtunzi anaonyesha dhahiri jinsi pesa ilivyo na nguvu ya kufanya kila kitu isipokuwa kununua uhai.

Shekhia anatumiwa kuchimuza dhamira ya wanawake ambao siyo watiifu kwa waume zao, alikuwa anamjibu mumewe majibu ambayo si mazuri. Katika utamaduni wa Afrika wanawake wanatakiwa kuwaheshimu na kuwatii waume zao. Pia mila na desturi za kiafrika pia humtaka mwanamke kutii mumewe kwa kila kitu. Japo utamaduni huu kwa sasa umeingiliwa na utandawazi sana ndipo wanawake huona ni kawaida kumtukana mwanamume wakati si vizuri kabisa. Swala ibuka katika tabia hii ya Shekhia ni swala la ujasiri alionao sio tu kukiuka utamaduni na maadili bali pia ujasiri wa kujenga misingi na mitazamo mipya ya kimahusiano, kwa maana kwamba aliye na pesa anaweza kuhiari kukiuka maadili, kupuuza wajibu na kudhuru wakati anapotaka kufanya hivyo. Shekhia japo alikuwa katili lakini alijutia makosa yake na akamuuomba mumewe amsamehe. Kwani Shekhia alitambua kwamba pesa si kitu ila utu na ubinadamu ni muhimu sana tunapoishi hapa duniani ndio maana aliamua kumuomba msamaha Suhail. Shekhia anatufundisha kwamba pindi unapoona unakoseakuomba msamaha ni jambo zuri sana na haijalishi una hadhi gani.

Shekhia anaonekana kama mwanamke shujaa kwani aliungana na baba yake katika kuhakikisha anapambana na utawala wa Budha ulioko baharini na ambao ulikuwa na tabia ya kurithishana uongozi kwa kujuana. Shekhia alikuwa ni mwanamke pekee aliyesimama upande huo mpaka dakika ya mwisho. Shekhia anachimuza dhamira ya nafasi ya mwanamke katika maswala ya kisiasa na uongozi kwa kuonyesha kwamba,

wanawake wanapaswa kuwa mstari wa mbele katika kutetea haki bila kuogopa kitu chochote kutoka katika wapinzani wao.

Kupitia mhusika Shekhia, mwandishi anaonyesha nafasi ya mwanamke katika jamii. Shekhia amechorwa kwa upande chanya kama mwanamke shujaa, na anayekubali makosa na kuomba msamaha kwa mumewe. Lakini pia mtunzi amemsawiri Shekhia kwa upande hasi kama mwanamke aliyeathiriwa na utandawazi ambaye anakiuka mila na desturi za utamaduni wa kiafrika kwa kumtongoza mwanamume na kutumia pesa zake katika kumtawala mwanamume. Hivyo basi Shekhia anatumia pesa kama kitu cha kuwatesa wasio nazo. Muhimu zaidi mtunzi anaibua ukweli kwamba licha ya asilia yake, Shekhia anaukubali na kuuridhia ubinadamu ikizingatia kwamba ana hisia za ki binadamu, anatambua makosa na kuomba msamaha, anatambua uwezo na udhaifu wa pesa, anakubali ukewenza na kwa hivyo kukubali utamaduni. Pengine kwa njia hii, mtunzi anaonyesha ushindi wa ubinadamu dhidi ya uhayawani, urazini dhidi ya umazingaombwe.

**4.3.1.4 Mapenzi, Uaminifu, Utiifu, Migongano kuhusu Dini, Heshima, utamaduni na Usaliti**

Mtunzi katika riwaya hii kupitia kwa usawiri wa mhusika Sharifa amechimuza dhamira mseto mbalimbali. Dhamira hizo ni pamoja na mapenzi, uaminifu, utii, utamaduni, migongano katika dini na usaliti. Mwingizi anachimuza uhusika wa Sharifa kwa kumwona kama ni binti ambaye alikuwa mwaminifu katika mahusiano yake ya kimapenzi na Suhail, mtiifu kwa watu na kwa mama yake wa kambo, aliyempenda sana Suhail hata anakubali kuolewa naye hata kama ana matatizo. Kwa mfano, Sharifa alikuwa ni mchumba wake Suhail toka wakiwa wanasoma sekondari na hata Suhail alipofaulu kwenda chuoni bado walikuwa ni wachumba japo Suhail alimsaliti kwa kuanzisha mahusiano na Shekhia.

Aidha tunaona kwamba pamoja na kwamba mtunzi amemjenga Sharifa kwa njia chanya kama hizi, swala la kwamba Suhail—mwanamume—alifuzu kwenda chuo kikuu na

Sharifa—mwanamke—hakwenda chuo kikuu, anaachwa nyumbani akisubiri kuja kuolewa na Suhail baada ya Suhail kumaliza masomo ya Chuo Kikuu, ni swala linaloweza kutiliwa shaka. Hatujui kwa nini Sharifa hakwenda Chuo Kikuu kwa maana haisemwi kwamba alianguka mitihani au hakuwa na ustahili wa kwenda chuo kikuu, au kama alishindwa na gharama za masomo ya chuo kikuu. Hii inaonyesha jinsi Mwingizi anampembeza mwanamke katika maswala ya masomo na nafasi stahiki katika jamii. Vilevile usawiri huu wa Sharifa unaibua ukinzani fiche katika mitazamo ya mtunzi, kwa nini Shekhia anakwenda chuo kikuu na sio Sharifa? Hapa panaibuka mambo mawili kinzani, upembezi wa wanawake na uchomozi wa ubabedume.

Mtunzi anamtumia mhusika wa kawaida kwa kumchanganya na kumhusianisha na mhusika wa kimazingaombwe kwa lengo la kuonyesha kwamba, mambo yanayotendeka ndotoni au katika ulimwengu wa kimajini na kichawi yanasawiriwa na kuakisiwa katika ulimwengu wa kawaida. Kwa kuwatumia wahusika changamani yaani jini na mtu wa kawaida (yaani Sharifa na Shekhia kuolewa na mume mmoja). Kuna uwezekano kwamba, ndoa hii inajaribu kuonyesha ufinyu wa kimpaka uliopo kati ya binadamu wa kawaida na ulimwengu wa uhalisiajabu na pengine swala la kifalsafa linaloibuliwa ni, binadamu ni nani kama anatawaliwa na kushawishiwa na mawazo na uhalisi wa kimazingaombwe. Aidha mwandishi anamsawiri Sharifa kama Binti mwenye nidhamu sana japo alikuwa anaishi na mama wa kambo lakini anamuheshimu na kumpenda sana. Hii ni tofauti na watoto wengine ambao wanapokuwa wanaishi na mama wa kambo huwa hawawaheshimu. Kwa njia hii mwandishi anamhusisha Sharifa na utiifu, unyonge, na ukunjufu, namna ya kuhalalisha na kumwandaa Sharifa kuolewa.Mwandishi anasema:-

> Sharifa alikuwa akiendelea na usafi wa nyumba huku mama yake akiwa jikoni akiungurumisha chakula, Sharifa alikuwa ni msichana mchapakazi sana licha ya kuwa muajiriwa lakini siku za Jumamosi na Jumapili badala ya kupumzika tu yeye hupendelea kujishughulisha na majukumu ya pale nyumbani ili kuwasaidia wazazi wake hasa mama yake (uk. 12).

Kupitia Sharifa mwandishi anachimuza dhamira ya jinsi dini za kigeni zilivyoleta migogoro katika familia na hata katika jamii. Sharifa alikuwa ni mwislamu na alifuata dini ya mama yake, baba yake alikuwa ni Mkristo. Kitu ambacho alitofautiana na mama yake wa kambo ni dini tu ya kiislamu kwani mama yake wa kambo alikuwa ni mkristo na alimpenda sana Sharifa na alitaka awe mkristo. Mwandishi anasema;

> Malezi hayakuwa magumu kwa Bi mkubwa huyu dhidi ya Sharifa isipokuwa sehemu moja tu; Kadiri Sharifa alivyokuwa akikua, aling'ang'ania kufuata dini ya mama yake mzazi ambayo ni uislamu, ingawaje hata hakumjua mama yake huyo ambaye alitoweka kitambo kirefu katika mazingira anayoyajua Mzee Fungameza peke yake. Japo Mzee Fungameza alikuwa ni Mkristo tena aliye Mzee wa kanisa, alijikuta akilazimika kumuacha Bintiye huyo afuate dini ya mama yake (uk 13).

Mtunzi anahoji kwamba, mahusiko ya dini katika maswala ya kifamilia yanaweza kuwa chanya au hasi kutegemea ni kwa kiasi gani wanafamilia wako tayari kuvumiliana na kuheshimu dini na imani za wanafamilia wengine. Hapa mwandishi anaonyesha jinsi uvumilivu wa dini unavyoweza kudumishwa pasina kuingilia mahusiano ya kifamilia na kijamii. Kwa kiasi fulani mwandishi anaonyesha kwamba dini inaweza kuwa kikwazo, ikizingatiwa pale mwandishi anaonyesha jinsi baba yake Sharifa alivyoacha kumfanyia sherehe Binti yake kutokana na tofauti za kidini. Kupitia Sharifa mwandishi anachimuza ujumbe unaonyesha jinsi ambavyo kuna uwezekano wa dini za kigeni kama vile za kikristo na kiislamu kuleta migogoro mingi katika jamii hasaikiwa zinatumiwa vibaya, kama vile kwa misingi ya kibaguzi katika maswala ya ndoa na familia kwa ujumla.

Sharifa amechorwa kama Binti mwenye upendo na mapenzi ya kweli. Anampenda Suhail toka wakiwa shuleni na alivumilia hata Suhail alipokuwa chuoni. Japo Suhail anamsaliti lakini yeye alikuwa na mapenzi ya dhati. Sharifa ameonyesha wazi kuwa upendo wake kwa Suhail haukuwa wa vitu kama pesa au mali. Huu ni ule upendo wa kuamua kumfia mtu hata akiwa katika hali ngumu kiasi gani kimaisha. Mwandishi anasema;-"… Kama ungempasua Sharifa katikati ya moyo wake basi ungekuta jina la Suhail limeandikwa kwa wino wa dhahabu kwa jinsi alivyompenda." (uk. 12).Upendo huo pia umebainishwa (uk. 94) kwani Sharifa alitamka wazi wazi kuwa ni bora afe kuliko kumkosa Suhail Sharifa anasema ...Sina tena thamani duniani, hivyo

nitakuacha na pesa zako na wanawake zako uendelee nao kwa uhuru, mimi bora tu sasa nife nikapumzike" (uk. 94).

Hii ni kuonyesha wazi kuwa Sharifa hakumpenda Suhail kwa sababu ya pesa bali alichotaka ni upendo kwake. Hakika huu ni upendo usiopimika ambao ni tofauti na ule wa mama yake. Mathalani kutokana na mapenzi ya dhati aliyokuwa nayo Sharifa hata aliposikia Suhail amepata ajali aliumia sana. Hii ni tofauti sana na mabinti wa sasa kwani wengi wamekuwa si wavumilivu katika swala zima la uchumba hasa katika kuwasubiri wenza wao. Inawezekana kwamba kupitia kwa usawiri wa Sharifa, mtunzi analitafakari swala la ubinadamu na utu, kwamba licha ya ulimwengu mpana kuonekana kushawishiwa na mambo ya mpito, bado humu ndani mna binadamu wa kawaida, binadamu ambao bado hawakuathirika na vishawishi vya mpito, binadamu wanaothamini binadamu wenzao kama binadamu kwa sababu wanatambua udhaifu wa binadamu kushawishiwa na kukengeushwa na uhalisi.

Swala hili la mapenzi ya dhati kwa Suhail linampelekea Sharifa mpaka anataka kujinyonga baada ya Suhail kukataa kumuoa kutokana na masharti aliyopewa na jini Sufian. Kwa mfano, walipokuwa katika hotel Suhail, alipokuwa akimwambia atafute mwanamume mwingine wa kumuoa kwa kumdanganya kwamba hana nguvu za kiume, Sharifa alikuwa radhi kuvumiliana naye katika hali hiyo. Lengo lake lilikuwa ni kumdanganya lakini si kweli, alikuwa na mahusiano na Shekhia jini mtu. Ndipo Sharifa kwa kuwa alikuwa anampenda sana Suhail akataka kujiangusha chini kutoka katika ghorofa ya juu kwa kuumizwa moyo na Suhail kwani alimsubiri kwa muda mrefu matokeo yake anamdanganya hana nguvu za kiume.

Sharifa amesawiriwa na mtunzi kama mwanamke mwenye msimamo katika swala zima la mapenzi na mtu mwenye heshima na nidhamu kwa mama yake wa kambo. Ni mhusika anayeathirika kisaikolojia kutokana na kusalitiwa na mpenzi wake Suhail kama ambavyo mabinti wengine wanavyofanyiwa na baadhi ya wanaume ambao wanapopata elimu huwasahau wapenzi wao wa zamani na kuwaoa wenzao wasomi. Kwa hivyo mtunzi ametumia ubunifu wa kuyumbishwa kwa mipaka ya usomi, tabaka, familia na dini kwa kuonyesha kwamba, Sharifa anapitia matatizo mbalimbali ni kutokana na

kwamba penzi lao lilionyesha uwezo wa kudumu lichakuingiliwa na vishawishi vya kijini. Swala zima la uhai kushirikishwa katika umajini linaibua uhalisi wa kibinadamu wa kutelekeza, kunyanyanyapaa na kumnyanyasa mtu wa karibu au hata mwandani kama alivyofanywa Sharifa. Aidha mwandishi kupitia Sharifa anachimuza dhamira ya uvumilivu katika daraja ya maisha ya mtu binafsi, uvumilivu kama familia na vilevile uvumilivu katika viwango vingine kama kwa wale viongozi wanaosalitiwa na wenzao katika kipindi cha uchaguzi ambao wanayumbishwa na upepo kwa kutafuta mahali ambapo watapata uraisi wa kupata nyazifa mbalimbali za kisiasa hasa kwa kutumia njia zisizo halali.

#### 4.4.1.5 Mapenzi, Dini na Familia

Maundu Mwingizi ni mtunzi aliye na mtazamo mpana wa mwingiliano wa maswala ya ki binafsi na maswala ya kijamii. Miongoni mwa maswala anayoyapigia darubini ni maswala ya dini katika michakato na mitagusano ya kinafsi na kifamilia. Hoja ya kimsingi inayoibuka ni kwamba dini ni kiungo cha kimsingi katika mahusiano ya kifamilia, malezi na makuzi ya watoto. Pamoja na hivyo, ni dhahiri kwamba, mtunzi anahoji kwamba licha ya manufaa yapatikanayo kutokana na dini, dini zinaposhindana katika kiwango cha familia zinaweza kusababisha athari hasi. Jukumu hili la kuchimuza maswala ya dini katika ulezi na makuzi linaendelezwa kupitia usawiri wa mhusika Fungameza. Fungameza ni baba yake Sharifa. Baba huyu alipokonywa mke na jini Sufian kutokana na kwamba Sufian alikuwa na pesa nyingi za kumuonga huyu mke wa Fungameza aitwaye Amanda. Fungameza alikuwa akiishi Tabora pamoja na mwanaye Sharifa. Mzee huyu ni baba ambaye alikuwa na upendo kwa mvyele[9] mwenziwe ambaye ni baba yake Suhail japo watoto wao walikuwa ni wachumba tu bado hawajaoana. Mzee huyu alikuwa anamtafuta Suhail alipopata ajali kwa ajili ya kujua amepona au amekufa akawa anampa matumaini Mzee Kusekwa na anamsaidia pesa kwa ajili ya nauli ya kwenda kumfuatilia Suhail.

9 BAKITA 2015:747 Mvyele Mzazi wa kiume au wa kike wa baba au mama wa mtu

Fungameza anatumiwa kuchimuza dhamira ya madhara ya dini za kigeni na wakati huohuo anauona umuhimu wa dini hizi za kigeni. Katika swala la kuona kwamba dini hizi zina madhara ni kutokana na kutokuwa na dini moja na mwanaye na anashindwa kumfanyia sherehe pindi anapokwenda kuolewa. Na si kwamba anaweka pingamizi mwanaye asiolewe na mwislamu bali ni kutaka kuhofia wakristo wenziwe wakimwona anamfanyia sherehe ya mwanaye itaonekana amekiuka imani hiyo. Dini hizi za kigeni kwa kweli zimeendelea kuleta migongano mingi ya kijamii, kifamilia na kiukoo kwani watu wengine wamekuwa hata wakishindwa kufunga ndoa kutokana na utofauti wa imani katika dini. Japo kwa upande mwingine dini ilipokuwa inatumika vizuri imeweza kuleta faida kwa kuwafanya watu kuwa na maadili mema katika jamii.

Mwingizi anaipa asasi ya dini umuhimu wa pekee katika riwaya zake. Mzee Fungameza ni kiongozi wa kanisa na ameoa mke mkristo lakini anaishi na mtoto wake Sharifa ambaye bado ameendelea kuwa na dini ya mama yake ya Kiislamu. Mchanganyiko wa imani tofauti katika jamii ya mtunzi ni jambo analosisitizia na kulipa kipaumbele kuwa jamii haina budi kukubaliana na matokeo hayo ya kihistoria. Anawaunganisha wanajamii wake kupitia mila, matambiko na jadi za Kiafrika. Wakati wahusika wanajikuta wakiwa na mikwaruzo ya hapa na pale inayotokana na tofauti za kiitikadi, mtunzi anazivunja tofauti hizo kwa kumfanya Mzee Kikoko kumwomba msamaha mkwewe mkristo aitwaye Judith na kusameheana katika mikwaruzo yao.

Hii ni ishara ya kutaka wanajamii waishi pamoja kwa misingi ya utu, amani na kuvumiliana licha ya kuwa wafuasi na waumini wa dini mbalimbali. Jambo la msingi ni kwamba dini ikitumiwa vizuri inasiadia katika swala zima la uadilifu, maadili uekevu na inapotumika tofauti ndio panaibuka mambo lukuki ya kuiona dini kama chombo hasi. Tunamwona Kasisi na Sheikh ni washiriki wakubwa wa himaya ya Waufi. Himaya ambayo imewakusanya wanasiasa, wasomi, vijana, watu wa jinsi mbalimbali, rangi, kabila zote, wafanyabiashara, na wafadhili wakiwa na lengo moja la kunyonya walio wengi. Hivyo, dini si kigezo cha wema na utu tu wakati mwingine hutumika kwa mambo ambayo siyo mema japo jamii imekuwa ikijuam kwa kiasi kikubwa dini ni kitu

kizuri katika swala zima la maadili. Kinachowaunganisha watu wote hao ni tamaa ya kujilimbikizia mali na kuwafisadi wanajamiii walio wengi. Anachokisisitiza mtunzi ni kuwa tamaa, ufisadi na udhalimu wote hauna mwisho mwema. Anazichora tanzia za madhalimu ambapo tunaona Amanda, Mzee Sufian, Suhail, Takadir, Msigwa, wote wanaishia tanzia katika riwaya ya *Vita vya Mapenzi.*

#### 4.3.1.6 Maendeleo, Uwajibikaji na Uzohali wa Vyombo vya Kiserikali

Kusekwa ni baba yake Suhail. Mzee huyu alikuwa akiishi Tabora, mkazi wa sehemu za nyanjani. Kupitia kwa usawiri wa Kusekwa, mwandishi anachimuza ujumbe wa wananchi kuwajibika katika kuleta maendeleo katika maeneo yaona wala wasitegemee serikali. Mzee huyu anazungumza maneno haya akiwa na mtoto wake Suhail baada ya mwanaye kushangaa kwa nini mji wao haubadiliki tu toka siku nyingi. Mzee huyu anaonyesha kuyumbishwa kwa mipaka kati ya ukale na usasa, kati ya mwana na baba katika kuliangazia na kulidadisi swala la uwajibikaji katika maendeleo. Ni kweli kwamba, kwa sababu ya kuwepo kwa sera zisizo na maono, uwezo na ari ya wananchi kujituma kujifanyia mambo yao unalemazwa ndipo maendeleo yanazorota katika miji wanakoishi. Ukosefu huo wa maendeleo mara nyingi hulaumiwa kwa kutolewa vizingizio visivyo na mantiki. Kwa mfano, ufu na utepetevu wa maendeleo katika riwaya hii unadaiwa kuwa unatokana na ushawishi wa jini Sharifu jambo ambalo kweli. Jini huyu amewaingia vichwani na kusababisha wasijishughulishe na maendeleo. Suhail anamwambia nani ni dhamira safi ya viongozi italeta maendeleo. Baba yake anamjibu na kumwambia kwamba “Siyo viongozi tu, yatupasa wananchi sote tuwe na nia ndo mabadiliko yatakuja.” (uk 81).

Mzee huyu anaona kwamba mabadiliko hayawezi kuletwa na viongozi tu pasipo wananchi wenyewe kushiriki na kushirikishwa katika kubuni sera, kujenga ruwaza, kupendekeza mikakati na kukuza hisia za umiliki wa maendeleo na mabadiliko wanayotaka. Wananchi wana uwezo wa kuamua na kupendekeza maendeleo wanayotaka, wana uwezo wa kumchagua kiongozi ambaye ataleta mabadiliko chanya yaliyo na na tija ya pamoja na kiongozi waliomchagua asipoleta mabadiliko wana

uwezo wa kumuondoa pia. Mzee huyu anaona jini Sharifa limewapumbaza wananchi kiasi kwamba wanakuwa wanaendelea kuwachagua viongozi wa binafsi wasiopenda maendeleao katika maeneo na ndio maana baadhi ya mahitaji ya msingi wanayakosa. Aidha kwa upande mwingine mtunzi kupitia Mzee huyu anaona si hivyo tu, pia wananchi wanatakiwa nao kuwa wawajibikaji katika serikali zao.

Kusekwa ni baba ambaye alikuwa mlezi mzuri kwa mwanaye Suhail. Hata ilipotokea Suhail kupata pesa katika hali na mazingira ya kutatanisha, Kusekwa hakuzaliwa na utajiri huo wa ghafla wa mwanaye, hakupenda hizo pesa badala yake alimkanya mtoto amwambie chanzo cha hizo pesa za ghafla na yeye alikuwa mwanafunzi juzi tu sasa atakuwa amezipata wapi pesa za ghafla. Ndio maana hata mkewe alipokuwa anazifurahia zile pesa Mzee yule aliendelea kuonyesha msimamo kwa kumwambia ukweli. Mzee Kusekwa anasema:-

> "We' mama Suhail acha kupenda sana hela we' mwanamke zitakuja kukutokea puani, unamjua huyo mtu anayempa tu mwanao mali kiajabuajabu mpaka unashaBikia tu? Badala uhoji umekalia ulimbukeni tu." Akageuza macho yake mpaka kwa Suhail akataka kuhoji juu ya hizo nyumba inazosemekana nazo ni za kwake lakini akajua tu jibu litakuwa kama la kwenye umiliki wa kampuni kwamba ameziandikisha kwa jina lake lakini si za kwake akajua ameshafilisiwa hoja akatulia na kuanza tena (uk. 83).

Mzee huyu alihitaji kujua vizuri chanzo cha pesa za mwanawe kwa sababu alihisi asije akawa anafanya biashara za madawa ya kulevya au akawa yumo katika jinai ya aina fulani. Lakini tunaona pesa zile za Suhail zinaonekana hazikuwa za kiuhalali na mwisho wake anakufa kwani ziliibwa kutokana na maswala ya kisiasa huko katika himaya ya Budha. Hivyo basi kupitia kwa mhusika Kusekwa mtunzi anaweka wazi kwamba siku zote maendeleo yanaletwa na wananchi wenyewe kupitia katika ari zao, maono yao, ruwaza zao na malengo waliyonayo pamoja na kushiriki na kushirikishwa katika maswala mbalimbali kama kuchagua viongozi ambao watajali maslahi ya wananchi kuliko maslahi yao binafsi. Watu wanapaswa kujitokeza kwa wingi kupiga kura katika kuwachagua viongozi wao wanaona watawasaidia katika kuleta mandeleo wasiishie tu

kulalamika wakati kuna mambo huwa wanayakosea wenyewe. Pia, Kusekwa anaendelea kuona kwamba jamii nayo inatakiwa kujishughulisha katika kuleta maendeleo mbalimbali.

### 4.3.1.7 Malezi na Makuzi ya Watoto

Mwandishi amechimuza dhamira mbalimbali kupitia kwa usawiri wa mhusika mama Fungameza, dhamira hizo mseto ni pamoja na malezi na makuzi bora ya watoto. Mama huyu alikuwa ni mama mwenye malezi bora. Alikuwa ni mama wa kambo wa Sharifa na alimlea mtoto huyu vizuri kama mtoto wake wa kumzaa tofauti na mama wengine wa kambo. Mama huyu anaidhihirishia dunia kwamba si mama wa kambo wote ni wakali hawawapendi watoto wa wanaume zao. Lakini mwandishi anaonyesha jinsi alivyomlea mtoto huyu vizuri japo si wake. Mwandishi anasema:-

> Hakika Bi mkubwa huyu alimpenda sana Sharifa, alimpenda kama Binti yake wa kumzaa mwenyewe, hata majirani wote wakaamini kuwa ni mwanaye wa kumzaa na pia humuita *'Mama Sharifa'*. Ukweli wa mambo ni kwamba Sharifa hakuwa mtoto wa kuzaliwa na Bi mkubwa yule kwani wakati mama huyu anaolewa na Mzee Fungameza, alimkuta Sharifa akiwa ameshazaliwa japo alikuwa angali mdogo sana, mtoto wa miaka kama minne tu hivi. Akamlea mwenyewe tangu hapo mpaka naye akajaaliwa kupata mtoto wake waliyemwita Florida (uk. 13).

Mwandishi anadhihirisha wazi jinsi baadhi ya mama wa kambo walivyo na mapenzi mema kwa watoto wa waume zao. Pia mama huyu ameonekana kuwa si mlezi tu kwa Sharifa hata kwa mwanaye aliyemzaa aliweza kumlea vizuri kwa kuwafundisha wote pamoja na mtoto wake maadili mazuri ya kuishi pia na watu vizuri. Aidha, mama huyu alikuwa ni mama mwenye upendo wa dhati kwani baada ya kusikia Suhail amepata ajali alijaribu kutumia kila mbinu kuhakikisha anambembeleza Sharifa asijisikie vibaya. Na aliweza kushirikiana na mumewe kuhakikisha wanachanga pesa na kumpa Mzee Kusekwa kwa ajili ya kwenda kufuatilia ajali aliyokuwa ameipata Suhail.

Siku zote mwanamke mlezi mzuri kwa wanawe ni mwanamke bora katika familia kwani watoto wengi wameweza kuharibika wakati mwingine ni kutokana na malezi mabovu ya wazazi. Hasa mama akilegea basi na mtoto huyumba zaidi katika familia hasa hizi familia za kiafrika. Mama Fungameza ni mwanamke mlezi mzuri kwa wanaye na asiye na ubaguzi. Kutokana na usawiri huu wa Mama Fungameza, mtunzi anajaribu kutafakari juu ya maswala mengi ya kijamii yakijumuisha ulezi, makuzi, mila, desturi na michakato ya kijamii kama vile uana-wakambo. Kuna pia swala la ulezi wa ki binafsi na ulezi wa kimajumui, ulezi katika misingi ya maadili na ulezi katika misingi ya mali na pesa. Kwa upande mwingine kuna swala la mahusiano ya kifamilia, ni nini hasa kinadhibiti mahusiano ya kifamilia.

**4.3.1.8 Utiifu na Ulezi**

Mwandishi kupitia kwa usawiri wa nafasi na uhusika wa Nadege Ndatabaye anachimuza dhamira mseto kama vile utiifu na ulezi. Mtunzi anamsawiri mhusika huyu kuwa ni mtu mtiifu na mtimizaji wa majukumu yake kama mama na mke katika familia. Anaonekana kuguswa na kubaini ukweli wa kuwa yeye ni pacha na Amanda akiyekuwa mke wa Fungameza, na mke wa Sufian. Anajikuta katika mduara wa kitanzia, sawa na fumbo la Edipode katika tamthiliya ya *Mfalme Edipode.* Edipode anatairiwa kumuua baba yake na kumuoa mama yake na maisha yake yote anajikuta akifanya jitihada za kuukwepa utabiri huo ambapo badala ya kukwepa ndipo anaingia katika mtego na mwisho anaamua kujitoboa macho asiuone uharibifu wake.

Aidha kwa mama Suhail yeye hatabiriwi hatima yake ila anajikuta katika mduara wa kuolewa na mume wa dada yake na kuzaa kijana anayekuja kuwaoa dada zake. Aibu aliyoipata inamfanya awe na huzuni maishani mwake. Anakuwa mkweli na kukubali aibu yake na ukoo wake kwa ujumla. Inapofika tanzia ya mwanawe Suhail anajikuta hana nguvu ya kuizuia bali kukubaliana na hatima hiyo. Anapokuja kutambua chimbuko la mali ya mwanawe, hapendezwi na hilo, na anaamua kuwasamehe mabinti zake na kuulea ujauzito wa kaka yao.

#### 4.3.1.9 P Usaliti wa Kindoa, Tamaa ya Pesa na Mali isiyohalali

Dhamira hizi zimechimuzwa na kupitia mhusika Amanda ambaye alikuwa ni Mnyarwanda na ambaye alikuwa ni pacha na mke wa Kusekwa. Alikuja Tanzania kwa ajili ya kumtafuta pacha mwenziwe ambaye alikuja siku nyingi Tanzania. Walikuwa na mawasiliano lakini baadaye wanapoteana naye baadaye mawasiliano yake kupotea ikabidi aje kumtafuta kwa njia ya kujifanya anafanya biashara na akakutana na Fungameza, wakapendana na wakawa wapenzi, wakafanikiwa kuzaa mtoto mmoja aitwaye Sharifa. Baadaye, mama anatamani pesa isiyo halali akamuacha mumewe na mtoto mdogo akaenda kuolewa na jini ambaye ndiye Mzee Sufian na wakazaa naye mtoto mmoja aitwaye Shekhia ambaye ni jini mtu. Jini Sufian huyu huyu ndiye anasababisha kifo chake. Kwa njia hii, mtunzi anatuumbia wahusika wa kimazingaombwe wanavyofanikiwa kuoana na watu wa kawaida. Amanda anakuwa muhusika wa majaribio kwa kule kufanikiwa kuzaa mtoto jini na mtoto wa kawaida bila ya kujitambua. Anavunja mipaka ya wahusika wa kijini na wale wa ki binadamu. Mtunzi anafanya hivyo ili kuonyesha kwamba, mambo ambayo katika hali za kawaida hayawezekani, katika riwaya za kihalisiajabu yanawezekana.

Mwandishi kupitia uhusika wa mama huyu anachimuza dhamira ya tamaa ya pesa inavyoweza kumtumbukiza mtu katika mtego wa maangamio. Kitendo chake cha kumkimbia Mzee Fungameza ni sawa na kitendo anachokuja kukifanya Suhail mtoto wa dada yake wa kumkimbia mwanawe Sharifa na kumuoa mwanawe mwengine Shekhia. Kilichosababisha kifo cha Amanda ni kujiingiza katika mtego wa vita vya majini. Kupitia mhusika huyu, mwandishi anachimuza maswala ya tamaa ya mali katika misingi ya mtu binafsi, maswala ya vita vya kikabila, usambaratikaji wa familia kutokana na siasa potovu za kikabila katika kiwango cha taifa. Kwa njia mbalimbali mwandishi anahoji kwamba maisha ya watu binafsi yanaweza kuathairiwa kwa njia chanya au hasi kutokana na michakato ya siasa za kitaifa na hata za kimataifa.

#### 4.3.1.10 Uwajibikaji, Uchonganishi, Kisasi, kutokuwa na Msimamo katika Ndoa na Mafao binafsi, utandawazi

Mwingizi amemsawiri mhusika Msigwa kumechimuza dhamira mseto au dhamira za kimwingiliano. Msigwa ni muhusika ambaye mara anakuwa mtu mwema na muwajibikaji katika utendaji kazi wake, mara anachimuza dhamira za uchonganishi, kisasi na mafao ya ki binafsi. Lengo la mtunzi kufanya hivyo ni kuonyesha kwamba kuna binadamu katika dunia hii mara wanakuwa wema na kuna wakati wanakuwa wabaya kabisa kuliko tusivyotegemea. Msigwa amesawiriwa kama mwanamume asiye na msimamamo katika mapenzi kwani, alikuwa na mke wake aitwaye Specyoza na kwa bahati mbaya kwa muda wa miaka miwili, hawakujaliwa kupata mtoto lakini alimpenda sana mkewe hakujali kutopata kwake mtoto. Kutokana na ndugu zake na hasa dada zake kumshinikiza amwache mkewe aowe mwanamke mwingine ndipo naye anabadilika na kuanza kumchukia mkewe kwa kumtafutia visa vingi vingi kumsingizia ana mahusiano ya kimapenzi na mtu mwingine ili amfukuze na mwisho wa siku akamfukuza.

Msigwa anachimuza dhamira ya kutokuwa na msimamo katika kumtetea na kumpenda mkewe kwani miaka miwili ya ndoa ni michache sana katika kuvumilia kupata mtoto, alitakiwa avumilie. Msigwa alitakiwa amtete mke wake lakini yeye aliwasikiliza dada zake na akaamua kumfukuza mke wake. Msigwa anaonekana kutokuwa na mapenzi ya dhati kwa mkewe na ni mwongo kwani anadiriki kumsingizia mkewe kuwa ana mahusiano na mwanamume mwingine wakati si kweli. Kwa misingi ya undani, hapa mtunzi analitafakari swala la uchonganishi katika familia, swala la utasa na uendelezaji kizazi, uzazi na kuwepo kwa watoto kama mihimili na udhibiti wa familia. Msigwa anatumia mitandao ya simu vibaya katika kuwagombanisha watu. Kwani anaonekana ana uwezo wa kuandika ujumbe kwenye simu ya mtu na kutuma kwa mtu mwingine bila mwenye simu kujua na kusababisha migogoro.

Msigwa anaweza kuandika ujumbe kwenye simu ya mkewe ili aonekane ni malaya. Ujumbe unaonyesha mkewe anafanya mapenzi nje ya ndoa wakati mkewe simu yake

haikuwa hewani aliisahau kwa kaka yake Morogoro. Vile vile anaandika ujumbe tena na kujifanya Sharifa na ujumbe huo unaenda kwa Suhail ukimtukana ukionyesha umetoka kwa mkewe Sharifa. Msigwa akaandika ujumbe mwingine tena unaotoka kwa Suhail unakwenda kwa mkewe akimfukuza nyumbani kwake wakati anasafiri na kusababisha ugomvi mkubwa na Sharifa kuondoka kwenda kwa wazazi wake. Kwa hiyo Msigwa amekuwa anatumia mitandao hiyo kuwakosanisha watu kama vile wameandika ujumbe kwenye simu zao kumbe hawajaandika.

Kupitia kwa mhusika Msigwa, mwandishi anachimuza ujumbe wa jinsi watu wanavyokuwa wanatumia mitandao ya simu vibaya katika kuwagombanisha watu. Mtunzi anaonyesha jinsi utandawazi ulivyoleta athari chanya na hasi katika mitandao ya kijamii kwani watu wengine wamekuwa wakitumia mitandao hii ya kijamii hasa katika kuleta migogoro mbalimbali katika jamii hasa kwa upande wa ujumbe japo hata katika upigaji lakini katika ujumbe ndio zaidi. Kwa hiyo watu wamevunja mipaka ya matumizi ya simu kwa kutumia simu kinyume kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia yaliyopelekea utandawazi. Pia Msigwa anafananishwa na rafiki ambaye ni mwongo wala hana subira kwani baada ya kukosana na Suhail aliamua kumuandika mwenziwe kwenye magazeti mbalimbali mambo ambayo si ya kweli. Mfano katika gazeti la *Haki* aliandika kwamba utajiri alionao Suhail ni kutokana na kuwaibia abiria wenziwe ndio maana amekuwa tajiri kitu ambacho si cha kweli zile pesa alipewa na jini Sufian. Vile vile akaandika tena katika gazeti la *Mdadisi* kwamba utajiri alionao Suhail ni kutokana na kuuza madawa ya kulevya. Yote haya aliyafanya Msigwa kwa ajili ya kulipiza kisasi kwa kuwa alikuwa na ugomvi na Suhail.

Mwandishi anamchora Msigwa kama mtu asiyekuwa mwadilifu katika utendaji kazi wake katika kampuni ya *Tawakadabra* kwani, anaandika habari nyingi katika magazeti ambazo si za kweli na kuisabaBishia kampuni hasara kubwa sana. Meneja wa kampuni anayofanyia kazi Msigwa anasema:-

> Ooh yeah, okay hakuna kikubwa sana zaidi ya yeye kutoka nje ya makubaliano yetu yaliyo ndani ya mkataba wake, kwa kifupi hakuwa mwadilifu na hakuwa makini hivyo habari zake mara kwa mara zilitutia hasara na kutugombanisha na watu. Na mara kadha tulipokea barua za onyo kuhusu tatizo hilo ambalo kimsingi lilisabaBishwa naye (uk 191).

Waandishi wa habari wa namna hii wapo katika jamii. Kwa hiyo wanapaswa kubadilika na kuandika mambo ambayo ni ya kweli si kuandika katika magazeti mambo ambayo hawana uhakika nayo ili mradi wauze magazeti.

Ujasiri pia ni dhamira nyingine iliyochimuzwa kupitia kwa Msigwa. Mwandishi ameonyesha ujasiri hasa kwa kufichua maovu yanayofanywa na wanasiasa katika jamii. Alikuwa mwandishi hodari aliyetumia magazeti kwa kuonesha yale mabaya yanayofanywa na wanasiasa wanaowasaliti wananchi wao. Msigwa anamwambia Suhail:-

> Iko hivi, nadhani unajua jinsi ambavyo mimi nimekuwa target kwa wanasiasa na vigogo mbalimbali kwa kufichua maovu yao magazetini (uk 145).

Hapa ni wazi kuwa Msigwa ni jasiri kwani ameamua kujitoa mhanga kufichua maovu yote yanayofanywa na viongozi. Mwandishi amechimuza dhamira hii kupitia kwa mhusika Msigwa inayohusiana na wajibu na majukumu ya vyombo vya habari kuitumikia na kuiwajibikia jamii. Vyombo vya habari vinapotumiwa kwa njia nzuri vina wajibu mkubwa katika kuiasa, kuionyesha, kuitahadharisha na kuiongoza jamii. Vyombo vya habari ni sawia na upanga unaokata pande zote kutegemea unavyotumiwa.

Kwa upande mwingine mwandishi amemsawiri Msigwa kama mtu ambaye anatumia mtandao wa ofisi kwa maslahi yake binafsi kwa kutengeneza ugomvi na watu ambao ana uhasama nao. Kupitia kwake mwandishi anachimuza dhamira ya baadhi ya watu na viongozi wanatumia mali za umma kwa maslahi yao binafsi kitu ambacho hakitakiwi. Hivyo basi mtunzi kupitia mhusika huyu ameweza kuionyesha jamii jinsi baadhi ya watu kuna wakati wanakuwa wema na kuna wakati wanakuwa si watu wema lakini wanasaidia jamii zao na pia wanatekeleza maslahi yao binafsi.

#### 4.3.1.11 Hekima, Busara na Ukweli katika Mahusiano

Mwingizi kupitia kwa usawiri wa Mzee Atrash anachimuza dhamira mbalimbali ambazo zinajenga jamii kwani Mzee huyu amesawiriwa katika kuchimuza dhamira za hekima, busara na ukweli katika mahusiano. Atrash ni Mzee aliyekuwa akiishi Bagamoyo, ni Mzee wa siku nyingi anayejua vizuri mji wa Bagamoyo yeye ni mganga wa jadi, na ni mtabiri. Mzee huyu alijenga nyumba yake karibu na kwa Mzee Sufian Bagamoyo. Mzee Atrash alikuwa anamfahamu vizuri sana Mzee Sufian toka alivyokuwa akiishi huko baharini kwenye himaya ya Budha na mpaka alivyokosa uongozi huko Budha na kuamua kukimbilia duniani na uchumi wa Budha.

Mtunzi anatumia uajabu katika kuonyesha kwamba Mzee huyu ni binadamu wa kawaida na wakati huohuo ni mtu asiye wa kawaida. Mzee huyu anafahamu historia ya majini wote wanoishi baharini akiwemo Mzee Sufian vizuri kabisa. Mtunzi ametumia mbinu ya uyumbishwaji wa mipaka ya urazini katika kuonyesha kwamba matukio yote yanayotendeka katika himaya ya *Budha* kawaida na yanayofanywa na Mzee Sufian anayajua vizuri sana kitu ambacho si cha kawaida katika ulimwengu wa kawaida kwa mtu wa kawaida. Hivyo, mtunzi anaonyesha uajabu alionao Mzee huyu katika kuchimuza dhamira mbalimbali. Mwandishi kupitia kwa Mzee huyu anaitahadharisha jamii kwa wale watu wasiopenda kusema kweli, wasaliti na wenye tamaa anawaonya na kuwasisitiza sana wawaache uongo. Mzee huyu alimkataza Suhail asizungumze habari za uongo na hatimaye akafa kwa sababu ya kuendelea kusema uongo. Suhail alimfuata Mzee Atrash Bagamoyo ili aweze kumwambia historia ya Sufian na Shekhia ambao ni majini, yeye akaenda kusema uongo anatafuta hawa watu kwa ajili ya kufanya nao biashara. Mzee Atrash anasema: ...“Utanielewa tu, kwani athari za mtu muongo, msaliti, na mwenye tamaa huzijui?” (uk. 48).

Maneno haya aliyasema Mzee Atrash baada ya kumwambia Suhail habari zake zote Suhail kuwa alipewa pesa na pete na Mzee Sufian. Na Mzee Sufian ni jini wala sio binadamu alitoroka baharini baada ya ugomvi mkubwa katika himaya ya Budha wa kung’ang’ania madaraka ndio maana akaja duniani ili aweze kumpa mtu pete ambayo ni

ulinzi wa Budha na pesa kwani, binadamu ilikuwa si rahisi majini kumuona kuliko jini mwenzao. Kwa hiyo, Mzee huyu kupitia uajabu aliokuwa nao anasawiriwa kwa kuonyesha busara na hekima kwa kumuhusia kijana yule aache kuongea uongo. Mwandishi anachimuza dhamira hizi kwa kuitahadhirisha jamii kuepukana na tabia kama ya Suhail kwani uongo si mzuri.

Aidha mtunzi anawatahadharisha hata viongozi ambao ni wanafiki ambao wanafikiri mambo mbalimbali waliyoyatenda na wanayoendelea kuyatenda wananchi hawayafahamu kumbe wanayafahamu na itafika wakati wananchi watachoka na kufanya maamuzi ambayo si mazuri. Kwa hiyo mtunzi kupitia Mzee Atrash anaonyesha wazi jinsi waganga wa jadi walivyo karibu na majini na mizimu katika utendaji kazi wao kwani huwa wanaelewa mambo mbalimbali yanayotendwa na wachawi pamoja na mizimu, kupitia mambo hayo ya kimazingaombwe ambayo amesawiriwa. Hivyo basi mhusika huyu ameweza kuonyesha wazi kwamba siku zote njia ya mwongo huwa ni fupi.

#### 4.3.1.13 Misukosuko ya Kindoa na Mahusiano ya Kifamilia

Mwandishi amechimuza dhamira za misukosuko ya kindoa na mahusiano kwa kumsawiri mhusika Specyoza. Specyoza alikuwa ni mke wa Msigwa ambaye alikaa na mumewe kwa muda wa miaka miwili Bila kupata mtoto. Kutokana na kukaa miaka miwili bila kupata mtoto dada zake Msigwa wakataka kaka yao amfukuze ili aowe mwanamke mwingine. Ndoa katika jamii za kiafrika zina umuhimu wa pekee. Umuhimu wa kwanza kwa mujibu wa Mbiti (1975:110) ni kuzaa watoto. Jamii hutegemea wanapofunga ndoa watu wawili basi jukumu lao ni kuzaa kuendeleza kizazi cha jana, cha leo na kesho.

Ukamilifu wa ndoa unapatikana pale tu kutopatikana kwa mtoto. Wanajamii hawataihesabia kuwa ndoa imekamilika hadi apatikane mtoto. Mtoto ni ukumbusho wa wazee waliokufa. Hupewa jina la mzazi aliyepita na huwapa heshima wazazi katika jamii. Hivyo kukosekana kwa mtoto kwa miaka miwili katika ndoa ya Specyoza na

Msigwa ni tatizo la wanafamilia yake. Kitendo cha mawifi kuingilia ndoa ya kaka zao kinapata uhalali kutokana na jamii kukubaliana uoni wa maana na madhumuni ya ndoa katika jamii yao. Mwandishi kupitia Specyoza anachimuza maudhui ya jinsi waafrika wengi wanavyopenda watoto tena si watoto wachache bali wengi, huona kuwa kuoa sio shida ila pindi ndani ya ndoa mwaka ukipita bila kubeba mimba wengi huanza kuona ni shida kubwa sana. Wengine uvumilivu huwashinda mpaka inafikia hatua kutoka nje ya ndoa kwa ajili ya kutafuta mtoto.

#### 4.3.1.14 Uwajibikaji wa Kiusimamizi na Unyenyekevu

Uwajibikaji mzuri katika utendaji kazi husaidia katika kusukuma maendeleo katika kazi yeyote ile ofsini. Miongoni mwa dhamira ambazo mtunzi amesiwasilisha kupitia kwa usawiri wa ofisi alikokuwa anafanya kazi Msigwa. Kassa ni meneja aliye mnyenyekevu na husikiliza matatizo ya watu katika ofisi yake. Na endapo mfanyakazi hatawajibika katika utendaji kazi wake humuonya na asiposikia humfukuza kazi kama alivyofanya kwa Msigwa pindi, alipokuwa anamuonya aache tabia ya kuandika hadithi zisizo na ukweli lakini yeye alikuwa anaendelea kuandika na akaamua kumfukuza kazi baada ya kuandika habari za Msigwa zisizo na ukweli ndani yake.

Kassa amechimuza dhamira ya uwajibikaji katika utendaji kazi ofisini. Ameionyesha jamii kwamba hata kama mtu ni maarufu kiasi gani endapo atakuwa amefanya kosa, anatakiwa kuadhiiwa bila kupendelewa. Mwandishi anaendelea kuchimuza dhamira hii ya uwajibikaji na usimamizi mzuri kwa kusema hata kwa viongozi wakubwa serikalini wanatakiwa wasiogope kutenda haki pale inapotokea kiongozi mwenzao amefanya kosa na yeye ndio kiongozi mkuu anapaswa kumwajibisha pasina kuogopa cheo chake, au uwezo wake kifedha. Mfano mzuri nchini Tanzania ni rais aliamua kumwachisha kazi ya uwaziri wa Nishati na Madini rafiki yake mpendwa baada ya kugunduliwa utendaji kazi wake si mzuri.

#### 4.3.1.15 Uwajibikaji na Mitandao ya Jinai katika Jamii

Dhamira hizi za uwajibikaji kwa upande mmoja na uibukaji wa mitandao ya jinai katika jamii kwa upande mwingine, zimechimuzwa mhusika Inspector Leonard Kenjah.

Kenjah ni askari polisi aliyekuwa anafanya upelelezi katika kesi ya marehemu Msigwa ili kutafuta kufuatilia wamemuua Msigwa. Mwanzoni alikuwa anahisi ni Suhail lakini baadaye ikasemekana muuaji ni Joram Ndege wa kikundi cha *Scorpion*. Na alimuuwa Msigwa kutokana na mambo waliyokubaliana kuandika yanayohusiana na siasa tu yeye akaandika mambo mengine. Kenjah anawajibika vizuri sana katika kazi yake kwa kufuatilia kwa hali na mali wahalifu wote ikiwa ni pamoja na aliyemuuwa Msigwa. Utendaji kazi wa inspector huyu na uwajibikaji wake unazorota kutokana na baadhi ya viongozi wakubwa serikalini kushirikiana na wahalifu. Mwandishi anasema;

> Simu ya inspekta Kenjah iliita, alikuwa sajent Malumbo akipiga kutoa taarifa, Kenja alikuwa akiisubiri kwa hamu simu hiyo maana zile namba za magari alizotumiwa kwa ujumbe kama alivyoagizwa hazikuwa na majibu ya haraka, hazikuwa za serikali wala za watu binafsi. ….ndiyo sajent Malumbo aliwajua mawaziri, mfanyabiashara mmoja, pamoja na kamanda wa polisi. Akamwambia inspekta Kenjah. Inspekta Kenjah akajibu hii sasa ni hatari. Naomba muendelee kumfuatilia Joram hao wengine achaneni nao (uk. 237).

Siku zote serikalini utendaji kazi huwa unazorota kutokana na baadhi ya viongozi kuwa marafiki wa wahalifu. Vivyo hivyo mambo kama haya tunaona yapo sana nchini Tanzania polisi na baadhi ya viongozi serikalini wanashirikiana na wahalifu katika kufanya uhalibifu wa mali ya umma kwa kuuza madawa ya kulevya. Tunamuona inspecta Kenjah anawaamuru askari wake wasaidizi waachane na baadhi ya viongozi wa serikali waliowaona wakishirikiana na Joram kwa kuogopa. Kwa sababu viongozi hawa ni watu wakubwa sana serikalini na wana uwezo wa kutumia mamlaka yao kwa kumfukuza kazi. Kwa hiyo, Kenjah anaona ni heri aachane na viongozi hawa na ashikwe mtu ambaye si kiongozi serikalini ambaye ni Joram.

Kwa upande mwingine nchi za Afrika huwa na utawala mbovu kutokana na kwamba, viongozi wamepewa kinga ambazo zinawafanya polisi wasiwe na mamlaka nao. Kwani Inspekta Kenjah kwa upande mwingine, anashindwa kuwaruhusu askari wake wawakamate wale mawaziri kutokana na sababu kwamba, hawana mamlaka ya kuwakamata. Mwandishi kupitia Kenjah anaonyesha jinsi inavyokuwa kazi ngumu kwa

polisi kutenda haki kutokana na viongozi wakubwa serikalini kujipa kinga ambazo zinawafanya wawe huru kufanya maovu ya kila aina na kuwachafua wenzao katika swala zima la kisiasa. Utendaji kazi wa polisi wengi unakuwa mgumu kutokana na aina ya utawala tulionao katika mataifa yanayoendelea na ndio maana polisi wamekuwa ni wa kulaumiwa sana na wananchi kwa kutokutenda haki lakini kumbe sio wao wakati mwingine mamlaka za juu zimekuwa zikiwatumia vibaya na wanaogopa kukakataa kutokana na kuogopwa kufukuzwa kazi.

### 4.3.1.16 Mali ya Umma, Mauaji na Ufadhili wa Kisiasa, Mahusiano kati ya Wahalifu na Vigogo Serikalini

Miongoni mwa dhamira mseto zingine zilizochimuzwa katika riwaya hii ni pamoja na maswala mazito ya kisiasa yanayopelekea uharibifu wa mali ya umma pamoja mauwaji kwa ajili ya maslahi binafsi ya viongozi wa kisiasa katika kung'ang'ania madaraka. Mwandishi anachimuza dhamira hizi kupitia mhusika Joram Ndege na Adams Gosh. Joram Ndege ni mhalifu kutoka nchini Uganda na amekuja Tanzania kwa ajili ya kazi hiyo tu. Joram anatumiwa na baadhi ya viongozi serikalini katika kufanya uhalifu mbalimbali. Viongozi hao ni mawaziri mbalimbali katika idara zinazoingiza uchumi mkubwa na zinazoshughulika na pesa. Mwandishi anasema:-

> ….upande wa kulia mwa Ibrahimu waliketi watu watano; mhe Hamid Humud (naibu waziri wa nishati na madini), Mhe Abdiroush Warriya (naibu waziri wa fedha) Moris Kungurume (mfanyaBiashara wa madini…upande wa kushoto nako kulikuwa na vibopa watano; kamanda Katinda Kuya (mkuu wa polisi kanda maalum), Joram Ndege (muuwaji wa kutumainiwa),….Adams Gosh (muwakilishi wa nchi ya Ugiriki ambao ndiyo inafadhili kikundi hicho) (uk 235).

Mwandishi kupitia Joram Ndege anaonyesha wazi jinsi inavyokuwa vigumu sana kwa mataifa yanayoendelea katika kuendelea kwani viongozi wapo mamlakani kwa ajili ya maslahi yao binafsi wakati kuna wananchi wanaoteseka. Viongozi hawa wa serikali wanarubuniwa na mataifa yaliyoendelea kwa vijisenti kidogo sana kwa kudhaminiwa katika maswala ya uharifu ili waweze kupita kisiasa na waendelee kuwanyonya

wananchi kwani tunamuona Adams Gosh ambaye ndiye mfadhili wa mtandao huo kutoka Ugiriki naye yupo katika kikao hicho cha kupanga mikakati mbalimbali ya kuwasaidia viongozi waliopo mamlakani waendelee kubaki ili na nchi hiyo ya Ugiriki iendelee kunufaika kwani ukiingia utawala mpya itakuwa kazi sana katika kufanikisha mipango yao. Hali hii ni mbaya sana na inapelekea mataifa yanayoendelea kuwa maskini na kuuana kwa sababu huyu anayefadhili mtandao huu anaweza akasabaBisha vita vikali sana kati ya viongozi walioko mamlakani na wale wanaotetea wanyonge kushindwa kuingia mamlakani katika chaguzi. Kwa sababu wale walioko mamlakani watahakikisha wanaiba kura kwa kupewa misaada na mataifa yanayoendelea ili waendelee kuwakandamiza wapinzani wao na waendelee kuwepo mamlakani kwa ajili ya kufanya ubadhalifu.

Joram Ndege na Adams Gosh wamebeba uhusika wa kutumiwa na wanasiasa katika kufanya uhalifu ili waendelee kunufaika. Na Adams Gosh amebeba uhusika unaochimuza jinsi mataifa yaliyoendelea yanavyoyadhulumu mataifa maskini katika kuendelea kwao kwani sababu ya kufadhili mitandao hiyo ya kijambazi na kiuaji ni kutaka waendelee kuchukua mali ghafi za nchi Bila huruma kama vile madini na wanyama pori, ndio maana waziri wa nishati na madini alikuwepo katika mtandao huo pia. Pia tunaona hata polisi wameendelea kuwa bega kwa bega na watuhumiwa hata katika vikao vya kuhakikisha serikali inabaki mamlakani nao wapo pia wakiungana na mawaziri pamoja na muuwaji Joram. Kuhakikisha wanaendelea kuilinda serikali iliyopo mamlakani iendelee kufanya maovu.

Mhusika Joram analipwa pesa nyingi na viongozi wa serikali kwa ajili ya kumuuwa Msigwa na mambo mengine ya kihalifu. Joram amechorwa kama mtu katili asiye na huruma yuko tayari kwa gharama zozote kuhakikisha anauwa watu wote wanaotaka kuwafuatilia katika mtandao wao. Ndivyo wafanyavyo viongozi wengi wa mataifa yanayoendelea; wanapoona kuna mambo wanashindwa kuyafanya kutokana na baadhi kuwekewa vizingiti hutumia wauaji kuwauwa watu wa aina hiyo ili waendelee kujineemesha. Mhusika huyu anajibadilisha na kufanya kazi ambazo mtu kama yeye

hawezi kufanya. Anajibadilisha na kujifanya mfanyakazi wa usafi katika hoteli anayoishi akawa anadeki wakati polisi wanamtafuta na wanampita wanajua siyo yeye kumbe ni yeye. Hii inadhihirisha wazi jinsi wahalifu mbalimbali wanavyotumia mbinu mbalimbali katika kufanya uhalifu ilimradi wasikamatwe. Na si wahalifu wanaotumiwa na serikali tu pia na wale ambao wanaishi kwa njia ya kufanya uhalifu.

**4.3.1.17 Ung’ang’aniaji Madaraka na Urithishanaji Uongozi**

Mwandishi ameendelea kuionyesha jamii kwamba pamoja na jitihada mbalimbali za kupambana ili kuondokana na umaskini inakuwa ni ngumu sana katika baadhi ya mataifa kutokana na migongano ya maslai binafsi ya viongozi walioko mamlakani. Viongozi hawa wanatumia nguvu nyingi sana kuhakikisha wanabaki mamlakani, au wanashindania ndugu zao washinde hata kama hawana vigezo. Au wanawapa uongozi wale ambao wanajua ni rafiki zao ili waendeleze maovu ya kuwakandamiza wanyonge ambao ndio wananchi. Mtunzi anaonyesha uyumbishwaji wa mipaka kati ya uhalisi na uhalisiajabu kwa kuonyesha serikali iko chini ya bahari na ni serikali ya kimajini na ina viongozi mbalimbali ambao ni majini na wameshika nyadhifa mbalimbali. Kwa mfano, mwandishi kupitia kiongozi wa himaya ya Budha ameweza kuchimuza dhamira za ung’ang’aniaji madaraka na urithishanaji uongozi. Huyu ni rais wa serikali ya Budha ambayo serikali hiyo ipo chini ya bahari yeye ni kiongozi mkuu wa majini katika himaya hiyo. Kiongozi huyu muda wake wa kuongoza ulikuwa umekwisha akamtafuta kiongozi mwingine atakayemrithi ili aweze kuficha maovu yake aliyokuwa anayafanya kipindi cha utawala wake.

Kiongozi huyu wa kimajini anachimuza dhamira ya viongozi ambao wanapeana madaraka kwa lengo la kulindana. Kwa sababu muda wake umekwisha na himaya ilikuwa inamtaka kiongozi mwingine atawale ambaye ni Sufian aliyekuwa anapendwa na watu wengi. Kwa kuwa kiongozi huyu alipokuwa mamlakani alifanya maovu mengi sana anamtaka yule ambaye atamfichia maovu yake. Ndipo inatokea vita kubwa sana kati ya serikali iliyoko mamlakani na wale wapinzani. Kimsingi usawiri wa kiongozi huyu wa kimajini unachimuza na kuakisi mambo yanayotokea katika hali halisi katika

mataifa ya Kiafrika, ujumbe unaotolewa hapa ni kwamba chanzo cha vita vingi vya kisiasa katika nchi za Afrika ni kwa ajili ya kuficha maovu, na maraisi kung'ang'nia madaraka, kugoma kuwapa wapinzani nafasi inapotokea wameshindwa. Vita kati ya Sufian na mahasimu wake kutoka himaya ya Budha vinaakisi hali inayosakini katika mataifa mengi ya Afrika. Swali linalojitokeza ni kama viongozi wanapokuwa mamlakani watekeleza majukumu ya kiutawala au wanaendeleza maslahi na mafao ya ki binafsi. Sio ajabu kwamba vita vingi katika mataifa yanayoendelea vinatokana na mivutano kati ya maslahi ya ki binafsi na neema ya umma.

**4.3.1.18 Utendakazi, Uwajibikaji na Rushwa**

Mwingizi anaonyesha wazi kukerwa na tabia ya baadhi ya polisi kupenda rushwa katika utendaji kazi wao. Anaona kwamba, siku zote rushwa ni adui wa haki. Polisi wamekuwa na tabia hii kutokana na mfumo uliopo mamlakani wa kupenda rushwa ndio maana hawaoni shida kuomba rushwa kila mahali. Kilingo ni mhusika ambaye kupitia uhusika wake amechimuza dhamira za utendakazi, uwajibikaji na rushwa. Kilingo alikuwa ni mfanyakazi wa kampuni ya Suhail, ni mfanyakazi ambaye alikuwa anamsaidia bosi wake katika matatizo mbalimbali. Hata alipokuwa akitaka kufanya maamuzi mabaya kutokana na Msigwa kumwandika vibaya katika magazeti yeye alikuwa anamshauri asiende kumuua Msigwa na badala yake afuate sheria.

Kilingo anachimuza dhamira ya utendakazi mbovu wa baadhi ya askari katika swala zima la kutoa na kula rushwa. Kilingo aliyasema maneno haya baada ya askari walipokuja kumchukua Suhail hospital bila hata kutoa sababu ya kumkamata Suhail. Kwa sababu kisheria unapomkamata mtu unatakiwa pia umwambie na kosa alilolifanya lakini askari hao wanapoelezwa na baadhi ya marafiki wa Suhail hawakutaka kusema sababu ya kumkamata Suhail. Hali hii imedhihirika kwa askari wengi sana nchini Tanzania na hata Kenya. Wanapomkamata mtu hata kama wa uhakika ni yeye, huwa hawamwambii kosa lake ili weweze kupewa kwanza kitu kidogo ndipo waweze kusema tatizo. Hapa mtunzi anaongelea maswala ya kimsingi yanayojumuisha rushwa, uwajibikaji, athari za rushwa katika uongozi na utendakazi, kulemazwa kwa taasisi

zilizojukumishwa kutekeleza majukumu mahususi, kulemaza utekelezwaji wa sheria na kwa njia hiyo kuruhusu njia na taratibu zisizo halali kutawala.

#### 4.3.1.19 Migongano ya Uongozi na Maslahi ya Ki binafsi

Siku zote katika utendeji kazi kwa upande wa viongozi wa kisiasa au hata wa kawaida lazima kutakuwa kuna baadhi ya watenda kazi wanataka haki itendeke. Japo viongozi wa aina hii huwa ni wachache lakini hawakosekani katika kuhakikisha wanapambana mpaka tone la mwisho la damu yao. Ndivyo ilivyokuwa kwa mhusika waziri mkuu ambaye anaonekana kuwa na msimamo mkali bila kuyumbishwa na mtu yeyote. Baada ya kuwagundua wanaohusika na mtandao wa *scorpion* ni viongozi wa serikali tena ni mawaziri wake anaamua kuita kikao cha viongozi wake wakiwemo na maaofisa usalama. Waziri mkuu huyo bila hata woga alianza kuwataja mawaziri wake wanaohusika na mtandao kwa ajili ya kuusaka urais.Waziri mkuu anasema:-

> "Kumezuka vikundi na mitandao ya wasaka urais ambao hufanya hila chafu na ikibidi hata hudiriki kuuwa ili kujiweka katika mstari mzuri wa ushindi. Sasa kufuatia hali hiyo mambo yamekuwa makubwa inabidi sisi tuliyoitana humu tunaoaminiana tushirikiane kuwang'amua na kuwashugulikia wapuuzi hawa wachache" (uk 281).

Waziri mkuu anamteuwa IGP aweze kuwataja na anaanza kuwataja kwa kusema miongoni mwa hao mawaziri ni waziri wa fedha, wa nishati na madini ndio waliokuwa wanahusika na mtandao huo ili waendelee kuwapo katika siasa na waendelee kufanya ubadhilifu wa pesa ya umma. Mwandishi kupitia waziri mkuu huyu anachimuza maudhui ya jinsi viongozi wakubwa serikalini wanavyoshirikiana na wahalifu kutoka katika nchi nyingi katika kuleta vita, na sio vita tu hata katika kufanya ubadhilifu wa mali ya umma kwa maslahi yao binafsi kupitia kwa mfadhili wao Adams Gosh aliyetumwa kutoka nchini Ugiriki. Si hivyo tu, mwandishi anaonyesha jinsi mataifa yaliyoendela yanavyoendela kutawala mataifa ya Afrika. Lengo la kufadhili mtandao huo ili hatimaye wazinyonye nchi hizi za Afrika na pia wasababishe vita wakati waafrika wanaendelea kugombana wao wanakuwa wanajichumia mali zao.

#### 4.3.1.20 Hila katika Ushindani wa Kisiasa

Mwandishi anaonyesha wazi katika swala zima la ushindani wa kisiasa katika nchi nyingi kumekuwa na tabia ya viongozi wanaousaka urais kuchafuana kwa namna yeyote ile. Hii si kwa nchi za Afrika tu hata katika mataifa yaliyoendelea pia yana tabia hiyo japo tunatofautiana njia zinazotumika katika kuchafuana. Mwingizi anachimuza dhamira ya hila katika ushindani wa kisiasa kupitia kwa wahusika Sostenes Mitti na Fortunatus Mwita ambao ni mawaziri, Sostenes alikuwa ni waziri wa fedha na Fortunes Mwita alikuwa ni waziri wa nishati na madini. Viongozi hawa wote walikuwa katika idara nyeti, na walikuwa wanatumia mtandao wa *Black Scorpion* kuwachafua wenzao katika ushindani wa kisiasa ili wenyewe waweze kuchukua urais na waendelee kufanya ubadhirifu katika nchi. Kutokana na kukithiri kwa tabia yao hiyo Waziri mkuu alijua mchakato wao mzima baada ya upelelezi. Wakaitisha kikao kwa ajili ya kujadili na wakahukumiwa adhabu ya kifo kutokana na kwamba katika mtandao huo waliweza kuwaua watu wengi sana akiwemo Msigwa ndio maana wakahukumiwa kunyongwa. Mawaziri hao wamebeba uhusika ambao unachimuza dhamira mbaya ya viongozi ambao wanang'ang'ania madaraka kwa lengo la kuendelea kujinufaisha wenyewe kwa kutumia njia ya kuwachafua wenzao. Siasa za aina hii nchini Tanzania zipo sana na hata Kenya zipo sana wako tayari hata kumwaga damu wanasiasa ili waweze kuyashibisha matumbo yao.

#### 4.3.1.21 Utendakazi wa Vyombo vya Dola

Mwandishi anachimuza dhamira za utendakazi wa vyombo vya habari kupitia wahusika Ustadhi Chaullah na Muokota Makopo. Kwani mbinu hii imetumiwa na serikali katika jitihada za kuhakikisha wanakamata wahalifu pasipo wenyewe kujua ili kufanikisha utendakazi wao. Mhusika aliigiza anaokota makopo ya maji na Ustadhi Chaullah aliigiza kama shehe. Lakini wahusika hawa ni wahusika ambao wapo katika kitengo cha upelelezi na ndio waliofanikisha zoezi la kumkamata Joram Ndege. Huyu mhusika aliyekuwa anaokota makopo, alikuwa anajifanya kama chizi na alikuwa anaokota makopo akiwa nje ya hoteli aliyokuwa anakaa Joram Ndege kwa lengo la kumkamata Joram Ndege. Huyu ustadhi alikwenda hotelini kujua chumba alichokuwa anakaa

Joram na akafanikiwa wakati anatoka akakukutana na Joram, na Joram hakujua kama anatoka kwenye chumba chake. Alipotoka nje akaenda kwa mpelelezi mwenziwe dereva *taxi* akakaa ndani ya gari na akampa yule mpelelezi mwenziwe Muokota makopo yaani chizi *laptop* alizozichukua chumbani kwa Joram wakaendelea kukaa na dereva *taxi*. Joram akatoka hotelini kwa kuhofia anaweza akakamatwa baada ya kusikia polisi wanamtafuta akakimbilia nje kupanda taxi. Na *taxi* ya kwanza kuiona ilikuwa ni ile ya akina Ustadhi Chaullah. Ustadhi Chaullah alikuwa amekaa kiti cha nyuma, Joram akapanda mbele ndipo gari likaondoka akawa anamwambia dereva akimbize gari alipogeuka nyuma ya kiti akamkuta Ustadhi Chaullah ndipo wakaanza kupigana. Ustadhi akampigia simu Inspeta Kenjah kwa ajili ya kuja katika eneo la tukio wakati Joram alishakuwa amekufa.

Mwandishi kupitia wahusika hawa anachimuza dhamira ya ushujaa na uwajibikaji katika utendaji kazi kutokana na mbinu waliyoitumia kwa mtu ambaye ni muuwaji lakini hawakuogopa. Pia mwandishi anawataadharisha watu wenye tabia kama Joram kuacha mara moja kwa sababu mbinu walizozitumia polisi mpaka kumkamata Joram Ndege zinaonyesha wazi kabisa hakuna kinachoshindikana kwa polisi wakidhamiria kwa maarifa yeyote yale wanaweza kupambana ili mradi uongozi uliopo mamlakani uwe upande wao.

Mtunzi kupitia riwaya hii ya kimajaribio ameweza kuwasawiri wahusika mbalimbali katika kuchimuza dhamira mseto mbalimbali ambazo zimeweza kujenga na kuendeleza mapambano mbalimbali. Katika kukabiliana na matatizo yanazozikumba kwa kiasi kikubwa nchi ambazo zinaendelea na kwa kiasi kidogo nchi ambazo zimeendelea. Mtunzi amewasawiri wahusika wa kijiniuchawi na kishirikina kwa misingi ya kiuhalisiajabu na wahusika wa kawaida kwa ajili ya kuonyesha mambo ambayo yanafanyika katika jamii kupitia kwa wahusika hao. inakuwa ni vigumu kuyaeleza kwa njia ya kawaida ndio maana akatumia mtindo ili kuchimuza dhamira mbalimbali kama vile za ubadhilifu wa mali ya umma, rushwa, uongozi mbovu, hila katika ushindani wa kisiasa, athari za utandawazi, mahusiano ya kifamilia, ukoloni mamboleo, ukabila,

udini, hekima, usaliti, maswala ya kindoa, ung'ang'aniaji wa mamlaka, ujambazi, uuaji, na utendakazi wa vyombo vya dola.

### 4.3.2 Uchimuzi wa Dhamira kwa Mkabala wa Wahusika wa Kijiniuchawi na Ushirikina katika Riwaya ya *Mzimu wa Waufi*

Mtunzi katika riwaya hii ya kimajaribio ya *Mzimu wa Waufi* ameweza kuchimuza dhamira mbalimbali kwa kuwasawiri wahusika mbalimbali wa kiuhalisi na wengine walio na nafsi mbili. Mtunzi ametumia wahusika wa kijiniuchawi katika kuangazia maswala mbalimbali yanayokumba watu binafsi, familia, jamii na mataifa yanayoendelea kwa kiasi kikubwa. Mtunzi ametumia mtindo huu wa kuwatumia wahusika wa kifantansia kitaswira na kielelezo asilia katika kuelezea hali halisi ya maswala mbalimbali katika jamii zetu. Mtunzi amewasawiri wahusika kwa mtindo changamani na kwa ubunifu mkubwa katika kuhakikisha wanabeba majukumu mseto kutokana na kusawiriwa kwa uchangamani unaoleta dhamira mbalimbali katika riwaya hii ya kimajaribio. Wahusika wengi sana wamesimuliwa matukio yao wakiwa ndotoni. Miongoni mwa dhamira mseto zilizochimuzwa na mtunzi kupitia wahusika wake ni pamoja na matatizo ya kisaikolojia katika ngazi za watu binafsi, matatizo ya kifamilia, kijamii na kitaifa hasa kwa kuangazia ukoloni mamboleo, uhuru wa bendera, utaifa, ukatili, manyanyaso na maonevu.

#### 4.3.2.1 Kuathirika kisaikolojia, Ukoloni Mamboleo, Utaifa na Uhuru wa Bendera

Kwa upande mwingine mtunzi anasawiri mhusika Masumbuko na kumbebesha dhamira mseto za uathirikaji wa kisaikolojia, ukoloni mamboleo, utaifa na uhuru wa bendera. Masumbuko ni mhusika wa kimaajabu ambaye kupitia kwake, matukio mengi ya kiuchawi yanaswiriwa akiwa ndotoni na uhusika wake umekuwa ukipitia katika mitagusano mbalimbali ya kisaikolojia na king'amuzi bwete. Masumbuko ni kijana aliyezaliwa kimaajabu baada ya mimba ya mama yake mzazi kuchukuliwa na mke mwenziwe ambaye ni mke mkubwa katika ndoa yao. Bi Mkubwa huyu hakubahatika kushika mimba toka alipoolewa ndio maana mumewe akaamua kuoa mwanamke mwingine ambaye ndiyo mke mdogo. Mke mdogo huyu alibahatika

kubeba ujauzito lakini baada ya miezi mitano, mimba hiyo ikahamia kwa mke mkubwa naye akajifungua mtoto aitwaye Masumbuko. Kwa hiyo, kukawa na ugomvi mkubwa kati ya wa Waufi na Waswezi kwani mke mkubwa alitokea katika utawala wa Waufi na mke mdogo kwenye utawala wa Waswezi.

Mtunzi katika riwaya hii amemsawiri mhusika Masumbuko katika kuchimuza dhamira ya kuathirika kisaikolojia pasina kutegemea kwa kusababishiwa matatizo ambayo yamesababishwa na wazazi, hali hii imemuathiri Masumbuko kwa kiasi kikubwa kwani amekuwa ni mtu wa kuumia nafsi yake na mpaka anafikia hatua ya kumlaumu mungu kuzaliwa kupitia katika misukosuko mingi. Mtunzi kupitia Masumbuko anachimuza dhamira ya jinsi ambavyo hata watoto wengine au watu wazima wengine wanavyoathirika kisaikolojia kutokana na wazazi aidha anaweza akawa mama alipata mimba pasipo kutarajia akamzaa mtoto na kuamua kuishi naye peke yake labda kutokana na mzazi aliyempa mimba kuikataa. Hivyo basi hupelekea mama huyo hata akija kumzaa mwanaye hatataka amfahamu baba yake kwa sababu hakumlea kitu ambacho kinapelekea watoto au watu wa namna hii kujisikia vibaya kwa kulelewa na mzazi mmoja na wakati wazazi wote wapo au kutomjua baba yake pale anapoona wenziwe wanafurahia maisha ya kuwa na baba.

Mwanzoni mwa riwaya mwandishi anatuonyesha Masumbuko akiwa ndotoni katika Himaya ya Waufi huko baharini na Hunudu. Viongozi wa Waufi wanawatesa sana vijana mbalimbali. Anawaona vijana wakiwa wamefungwa kamba wakibanwa taya zinazoshikilia midomo yao. Aidha Masumbuko anawaona watu wengine wakiokwa katika moto kama mikate. Mwandishi anasema:-

> Miongoni mwa adhabu alizozishuhudia, aliwaona watu wakikatwa ndimi zao, na kuhisi maumivu makali mno, kitu cha ajabu hakuna aliyekuwa akiwahurumia hata pale walipokuwa wakiomba radhi kwa makosa waliyoyafanya na kuhitajia msaada! Pia alishuhudia watu wengine wakiokwa katika moto mkali kama mikate au ndafu ilhali wenyewe wakiwa hai bado. Wapo aliowaona wakipigiliwa misumari katikati ya vichwa vyao (Utosini), Ubongo na damu vikiruka juu na kutapakaza anga (uk 2-3).

Usawiri wa Masumbuko ni usawiri changamani tena usawiri wa vidato kwa maana kwamba matukio anakohusika Masumbuko yanaweza kufasiriwa kutoka ndani kwenda nje, yaani kutoka kuakisi unafsi hadi kuakisi taswira na kielelezo asilia. Kwa hivyo katika daraja moja, mwandishi kupitia mhusika Masumbuko anachimuza jumbe ambazo zinakita katika siasa kama vile kunaonyesha jinsi utawala wa mabavu unavyonyanyasa wananchi wake pindi wanapoandamana kwa ajili ya kutaka kuuondoa utawala wa kimabavu. Vijana wale wanaoteswa na akina Hunudu na wenzake ni wale wanaowakilisha wale wananchi wanaoteswa na utawala wa kimabavu kwa ajili ya kuacha tabia za kuanzisha maandamano ya kupinga utawala kandamizi.

Mwandishi anaonyesha jinsi vijana wanavyokatwa ndimi zao kwa ajili ya kupinga utawala wa kibabe wa Waufi. Mwandishi anaonyesha jinsi viongozi wanavyowanyamazisha wananchi kwa kuwakata ndimi zao wale ambao wapo katika mstari wa mbele kupinga utawala wa mabavu kwa kuwafunga jela au kuwatishia maisha yao. Ndio maana vijana hawa wanakatwa ndimi zao ili wasizungumze mambo yanayofanywa na viongozi makatili. Aidha mtunzi anaonyesha wazi kabisa migomo mingi ya kisiasa vijana ndio hutumiwa katika maandamano.

Masumbuko akiwa bado yuko ndani mapango baharini, anafikishwa katika sehemu nyingine ambapo anamshuhudia kijana mmoja kutokana na kukiuka masharti ya dini hii ya Waufi anachinjwa kama kuku halafu kiongozi wa Waufi Hunudu, anakunywa damu yake na anampa Masumbuko ainywe. Mwandishi anachimuza dhamira ya jinsi watetea haki katika nchi wanavyokufa katika mikono ya nduli hawa. Tumeona watu wanaotaka mabadiliko katika serikali na hasa katika nchi za Afrika wakihukumiwa kunyongwa hadi kufa na maiti zao kutupwa maporini au zisionekane kabisa. Hili limedhihirishwa hata katika nchi ya Tanzania kwani baadhi ya viongozi katika vyama vya upinzani na kiongozi wa chama cha madaktari mwaka 2014 waliteswa na kutolewa meno na kisha kutupwa porini kwa sababu ya kushinikiza mgomo wa wafanyakazi wa idara ya afya. Hali hii hujitokeza pindi wanapofuatilia haki zao na kuelezea maovu yanayofanywa na serikali.

wamekuwa wakiuliwa na miili yao kukutwa porini kutokana na kuzungumzia mambo maovu yanayofanywa na serikali. Mauaji yametumiwa kama mkakati wa kufikia malengo yao ili yatimie.

Masumbuko anaambiwa anywe ile damu ya yule kijana ili na yeye aachane na mambo ya upinzani ajiunge na dini ya Waufi. Mtunzi ametumia dini ya Waufi kumaanisha utawala wa kimabavu kwani hii dini ya waufi si dini bali ni kikundi cha wachawi. Huku Masumbuko akiwa anakataa kujiunga na utawala huo dhalimu akiwa anang'ang'anizwa kunywa hiyo damu ndipo ghafla akashtuka na kujikuta kumbe alikuwa usingizini anaota. Wakati mambo haya yote yakiwa yanaendelea kumbe alikuwa akiota ndoto. Mtunzi anatumia ndoto katika kuwasawiri wahusika wake kwa kuwaonyesha kwamba mambo mengi wanayoyatenda wakiwa usingizini na wanaota ndoto, lakini kwa ufahamu kwamba ndoto haitokei katika ombwe tupu, inashawishiwa na matukio halisi au matukio yaliyo katika upeo wa uwezekano, matukio razini. Matumizi ya ndoto katika miktadha hii yanakusudiwa kuyumbisha mipaka ya urazini na uhalisiajabu lakini wakati huo huo ndoto inatumika kujenga taswira ya uwezekano wa mambo sampuli hiyo kutokea au kuwa yamewahi kutokea. Kwa njia hii, mtumzi anachimuza dhamira hii ya utawala wa kimabavu kwa kutumia ndoto. Lakini mbali na mambo haya ya kindoto kufasirika kisiasa, inawezekana kuyadadisi kutoka mkabala mwingine, kama vile kuuliza swali la kimsingi, binadamu anashurutika kutenda nini au kutesa kwa namna gani ndipo aweze kuridhisha uchu wake wa mali au hadhi.

Athari za dini za kigeni kwa waafrika ni nyingi. Dini hizo ni Uislamu na Ukristo. Zimegawanya jamii ya Waafrika katika makundi na vipande vidogo vidogo vinavyotofautiana. Mpasuko upo katika ngazi ya mtu binafsi anapojikuta akiwa na mchanganyiko wa itikadi unaogombania nafasi pale anapotaka kupitishisha hukumu juu ya swala linalomtinga liwe la kijamii, kisiasa, kiuchumu au kimaadili. Achague uoni upi katika kila muktadha huwa ni kitendawili anachokutana nacho mwafrika kila dakika katika jamii ya sasa. Je tayari ana majibu ya maswali mtambuka ya kimaisha yahusuyo

ubaya, uzuri, haki, amani, upendo, usawa, furaha, huzuni, na kifo. Si rahisi kupata majibu au ufumbuzi wa moja kwa moja kwa vile dini, mifumo jadi na usasa wa Kimagharibi yote inagombea pata majibu kwa uoni wake. Masumbuko baada ya kuota ile ndoto alimsimulia mkewe na mkewe akamwambia wamuite Mchungaji amuombee lakini, Masumbuko hakupenda kuombewa. Mke wa Masumbuko anasema;

> ..nitaenda kwa Mchungaji kumwambia aje kukufanyia maombi." Walijaribu kufarijiana mtu na mkewe japo Masumbuko hakupenda kusikia maswala ya kuombewa na Mchungaji kwa kuwa yeye imani yake ni tofauti na ya mkewe, ila mkewe alikuwa akiona maombi ndiyo njia pekee ya kumnusuru mumewe kutokana na imani ya dini yake. Wamekua wakiishi pamoja kwa ndoa ya Bomani (uk 5).

Kwa hiyo, mhusika Masumbuko amesawiriwa kama mtu ambaye ameathirika na mseto wa uoni wa dini katika ngazi ya familia yake, wazazi wake na yeye na nafsi yake. Mtunzi kupitia Masumbuko anachimuza dhamira hii ya athari za utamaduni wa kigeni baada ya ujio wao wamesababisha migogoro mingi sana katika familia, ukoo na hata jamii kwani Masumbuko hataki kuombewa na mchungaji ili aache kuota hizo ndoto kwa kuwa yeye ni mwislamu. Hivyo basi, mwandishi anamsawiri Masumbuko kupitia ndoto anazoziota katika kuchimuza dhamira hii ya athari za dini za kigeni. Masumbuko akiwa yumo ndotoni anakutana na Hunudu kijana wa utawala wa Waufi akimtaka amtoe mwanae kwa sababu ametoa siri ya Waufi. Ndipo Masumbuko akawa anakataa, hivyo Hunudu akamwambia kwa sababu umetoa siri zetu kwa kumwambia mkeo lazima utoe kafara ndio kupona kwako. Mwandishi kupitia Masumbuko anaona jinsi Masumbuko alivyokuwa na msimamo. Kwa sababu hakutaka kujiunga na Waufi kulingana na kwamba walikuwa na tabia mbaya ya kuwatesa wananchi wasio na hatia. Ndio maana hata anapoambiwa atoe kafara anagoma kwa sababu hayuko tayari kujiunga na utawala kandamizi. Hilo linadhihirika hata katika serikali nyingi duniani. Pindi anapotokea mtu au kiongozi anatoa siri za serikali hufuatiliwa na hata kuangamizwa katika baadhi ya mataifa.

Aidha mtunzi anaendelea kuchimuza dhamira ya itikadi na msimamo mkali kupitia kwa mhusika Masumbuko. Masumbuko mtu ambaye ana itikadi kali asiyekubali kuyumbishwa kwa chochote ndio maana hayuko tayari kutoa kafara. Masumbuko anaonyesha jinsi ambavyo yuko tayari kutetea haki za wanyonge bila kuyumbishwa na kitu chochote hata kama atauliwa lakini ameonyesha msimamo katika kutetea haki za wanyonge wasio na hatia. Masumbuko hakuyumba katika maswala ya imani tofauti na mkewe. Msukumo kutoka kwa baba yake haumfanyi atengane na mkewe na hivyo kuthibitisha msimamo wa mwandishi juu ya jamii yake yenye tofauti mbalimbali ambazo anazizika na kushabikia umoja, upendo na kuvumiliana kwa wanajamii yake kwa kuanzia yeye mwenywe kumvumilia mkewe na imani yake tofauti na yeye. Anamtetea hadi dakika ya mwisho na picha inayojengwa na mtunzi kwa wanajamii yake. Tuishi kwa kutofautiana lakini si kwa kufarakana.

Mtunzi kupitia mhusika Masumbuko anachimuza dhamira ya matumizi ya kafara. Sasa swala la kafara katika jamii ya mtunzi bado limeshika kasi. Ingawaje wahusika mbalimbali wanaonekana kuwa na dini za kigeni lakini bado imani yao katika maswala ya matambiko na makafara ipo. Kafara ameizungumzia Mwingizi kuanzia katika riwaya ya *Vita vya Mapenzi*. Kafara la damu ya mbuzi inatolewa kwa mara ya kwanza wakati wa ndoa ya Shekhia na Suahail ikiasisiwa na Mzee Sufian, Mara kadhaa Suahail anajaribu kutoa kafara la mnyama lakini Takadiri anamcheka na kumwambia ukweli kuwa pete inataka kafara la mtu wake wa karibu. Kafara linajitokeza katika *Mzimu wa Waufi* ambapo Masumbuko anatakiwa kutoa kafara ya watoto wake na anakataa.

Kwa upande wa *Tanzia* kafara inatolewa kunusuru uhai wa Mzee Mtandi anayechukuliwa katika matambiko makaburini ambapo sababu za kifo chake ndiko zilikoanzia (uk 60). Swala la kafara au matambiko ni kiunganisho cha wanajamii ya Mwingizi. Imani hii inawahusu wale wenye dini pia. Ni moja ya ada ambayo bado ipo hai na inatokeza katika uuwaji wa *maalibino* katika jamii ya Mwingizi. Wanaouwa *maalibino* kwa visingizio mbalimbali ni watu wenye dini za kileo. Hivyo imani yao mseto inawapelekea katika kuwa na imani na vijisehemu vya ada ya matambiko katika

maisha yao. Mwingiliano wa siasa na imani za jadi bado unajitokeza katika Afrika na jamii ya Mwingizi. Wanasiasa wanatabia ya kutoa kafara katika kipindi cha chaguzi. Bi Masonyanya ingawaje alikuwa mchawi lakini alikuwa anatembelewa na wanasiasa kwa wingi kuwasaidia katika kazi zao na kupata vyeo.

Masumbuko akiwa anasubiri daladala za kwenda nyumbani kwake kituoni ghafla gari inasimama katika kituo cha matatu au daladala na ilikuwa inaendeshwa na mwanamke. Yule mwanamke anamwita aingie kwenye gari lakini Masumbuko anasita kidogo kwa sababu alikuwa hamfahamu yule mwanamke. Mwanamke akajifanya anamwambia Masumbuko hunikumbuki? Mimi ni mteja wenu wa Mpesa katika kampuni yenu huwa ninajaza pesa katika kampuni yenu. Masumbuko hakumkumbuka lakini ikabidi ajifanye kama anamfahamu. Baada ya kuingia ndani ya gari akakumbana na kijana anayeitwa Hunudu katili ambaye huwa anamtokea kila siku kwenye ndoto na ni jini na kumbe na yule dada alikuwa ni jini pia wamekuja katika ulimwengu wa kawaida kwa ajili ya kutimiza azma yao ya kukutana na Masumbuko. Hunudu anakutana na Masumbuko kiuhalisia kwani siku zote hukutana na Masumbuko ndotoni katika sehemu mbalimbali za kutisha na kuogofya. Lengo la mtunzi kufanya hivi ni katika kuonyesha kwamba mambo yote yanayotendeka ndotoni yanapatikana na uhalisiani au yanashawishiwa na matendo ya uhalisini. Kwa hivyo, katika misingi hii inasadikika kuhoji kwamba mtunzi anatafakari juu ya ufinyu wa kimipaka kati ya uhalisi wa kindoto na uhalisi wa uhalisia. Ukweli unaobainika katika ndoto za mtu binafsi unatofautiana vipi na ukweli ambao mtu anakumbana nao katika maisha ya kawaida. Je inawezekana kwa hivyo ndoto ikawa ni kiashiria cha uhalisia.

Mwandishi kupitia Masumbuko anachimuza dhamira ya kutokuwaamini wanawake katika maeneo mbalimbali kwani wanawake wamekuwa wakitumika katika matukio mbalimbali ya uhalifu, pia ni walaghai. Wanawake wamekuwa wakitumika sana katika kufanikisha zoezi la ujambazi kwa sababu mtu anaweza akamwangalia mwanamke na akaona hawezi kufanya mambo kama hayo lakini kumbe mwanamke hutumika kama chambo cha kuteketeza watu kiurahisi kwa njia ya ujambazi. Ndivyo

ilivyokuwa kwa Masumbuko kwani alivyomuona mwanamke mrembo akaona hawezi kufanya chochote kumbe kuna mwanamume ndani ya gari kwenye kiti cha nyuma ambaye ni jini Hunudu. Mwandishi anachimuza maudhui ya kuporomoka kwa maadili ambako ndio kumepelekea hata wanawake kuwa majambazi kwa kushirikiana na wanaume kwa kumtumia jini Hunudu na jini mwanamke ambaye ndiye alikuwa naye siku ile alipombeba Masumbuko.

Kupitia kwa usawiri wa Masumbuko mwandishi anaonyesha jinsi baadhi ya watu maskini wanavyoishi maisha magumu katika nyumba za kupanga ambapo wanatumia bafu moja wapangaji wengi na bafu lenyewe ni dogo na juu halijaezekwa. Bafu hilo ndilo alilokuwa analitumia Masumbuko kuoga na ghafla akiwa amejipaka mapovu ya sabauni mwili mzima anashangaa amehamishwa kimajini mpaka kwenye bafu zuri la watu matajiri, bafu ambalo lina marumaru na mapambo mbalimbali ya dhahabu na amebadilishwa jinsia na kuwa wa kike akiwa anaandaliwa kwa ajili ya kwenda kuolewa. Mwandishi anamtoa Masumbuko katika hali ya kawaida na kumhamisha kwa njia ya kimazingaombwe, hadi sehemu ambayo ni nzuri na ambako hata Masumbuko mwenyewe hajui yuko wapi. Mwandishi anamtumia Masumbuko katika tukio hili la kiajabu pengine ili kuashiria kutoridhishwa kwa binadamu na hali yake ya sasa na kwa hivyo, akawa katika ndoto za matamanio ya mambo bora zaidi. Ndio maana mtunzi anamtoa Masumbuko katika bafu la kimaskini ambalo juu liko wazi na kumpeleka katika bafu zuri lenye marumaru na anabadilishwa jinsia na kuwa mrembo kwa kuashiria anayatamani maisha mazuri zaidi ya yale aliyonayo ambayo ni magumu sana. Huu ni uhalisi wa maisha ya kila binadamu kwamba tumo katika ndoto ya matamanio, ndoto ya kusahulisha ugumu na ukata wa hali zetu za sasa na kuota kujipata katika hali zilizo bora zaidi. Kwa hivyo, ndoto na uhalisia ni mambo yanayopishana.

Kwa upande mwingine mwandishi kupitia Masumbuko anachimuza ujumbe wa jinsi sehemu nyingi za nchi za ulimwengu wa tatu kwa jumla na hususani Tanzania, watu walivyo maskini hasa hayo maeneo ya Buguruni, ambako alikuwa anaishi

Masumbuko walikuwa wanakaa katika nyumba ndogo na wanatumia choo na bafu wapangaji wengi wakati kuna sehemu viongozi kama akina Hunudu wanatumia mabafu yenye dhahabu ndani wakati wananchi wao wanateseka. Aidha mwandishi anaendelea kumuonyesha Masumbuko akiwa anapodolewa na Bi mkubwa mmoja hivi ghafla anatokea jini Hunudu ambaye Bi mkubwa huyu alisema ndiye atakuja kumuoa Masumbuko lakini, Masumbuko hakujua ni Hunudu. Ndipo Masumbuko akamuona Hunudu akachanganyikiwa sana na kumuita jina lake Hunudu kwa kumwambia kwa nini anamtesa na kumbadilisha jinsia na kuwa wa kike. Ndipo Hunudu ambaye ni jini anamwambia Masumbuko kwamba "…kama ungekubali kujiunga na Waufi na ukatoa kafara tuliyoitaka kwako wala tusingefika huku lakini kwa kuwa hutaki basi utakuwa hivi hadi kufa kwako!"(uk. 62).

Masumbuko anatumiwa kuchimuzwa maudhui ya jinsi Serikali iliyoko mamlakani ilivyo na uwezo wa kuwatesa wananchi wake pindi wanapokataa kuonewa na utawala uliopo mamlakani. Utawala huu hutumia nguvu nyingine za ziada hata kumdhalilisha huyu mwananchi wa hali ya chini ili mradi abadili msimamo wake. Ndivyo ilivyokuwa kwa Masumbuko. Lakini pia mateso haya yanaweza kuendelezwa kitabaka, kwamba walio na mali na pesa, pia wana uwezo na mamlaka; na kwa hivyo kama wana kiburi na inda wanaweza kuwatesa walio chini yao. Vilevile mwandishi anachimuza dhamira ya jinsi haki isivyotendeka katika ofisi mbalimbali iwe ni ofisi ya Serikali au hata ofisi ya mtu binafsi utakuta mfanyakazi anafukuzwa kazi bila kupewa barua ya onyo au kupewa taarifa anashangaa tu amefukuzwa kazi. Jambo hili limedhihirika kwa Masumbuko kwani baada ya kuumwa majini alikuwa haendi ofisini. Lakini siku anayoenda ofisini alimkuta rafiki yake nje akamwambia ameshafukuzwa kazi kwa hiyo hana haja ya kwenda ofisini kuomba msaada wowote. Ndivyo ilivyo katika ofisi nyingi wafanyakazi wananyanyaswa sana, kutokana na kutojua sheria zao wanaamua kuvumilia hivyo hivyo na kuendelea kunyanyaswa.

Mwandishi anatumia ndoto ya mhusika Masumbuko kuchimuza maswala ya haki na dhuluma kwa watu wasio na hatia ambapo anaonyesha tukio la ajabu na la kutisha katika kuangazia mambo hayo ya msingi. Anamuonyesha Masumbuko akiwa katika ndoto akiwa amechukuliwa na Waufi na kugeuzwa kuwa ng'ombe kwa ajili ya kwenda kuchinjwa na Hunudu. Ndipo Waswezi ambao ndio asili ya mama yake asilia wanapambana na Waufi katika kumrudisha Masumbuko ili arudi katika himaya yao. Waswezi wanafanikiwa kwa umoja wao kumwokoa Masumbuko. Masumbuko anashtuka kutoka usingizini anajikuta yuko Tabora kwa Waswezi wakati alikuwa Dar es Salaam na amegeuzwa kuwa ng'ombe. Kwa kutumia ndoto na kumfikirisha msomaji kuona vitendo vya kiuhalisiaajabu ambapo mtu wa kawaida anageuzwa ng'ombe na kukaribia kuchinjwa, mwandishi anamweka msomaji katika fikra pana zaidi. Inakuaje mtu ageuzwe ng'ombe? Na ishara ya ng'ombe ni ipi?

Kitendo cha kumgeuza mtu ng'ombe ni kumfanya kwanza atii mamlaka iliyo juu yake. Na kila ng'ombe anavyozidi kunona ndivyo anavyokaribia kuteuliwa kuwa kafara au kitoweo cha kuuzwa. Jamii inayogeuzwa ngo'mbe inatumikishwa kwa manufaa ya wenye ng'ombe ambao ni mabeberu wanaomiliki njia kuu za uchumi na ustawi. Katika mfumo wa ukoloni na hata baada ya ukoloni na kipindi cha ukoloni mamboleo wanajamii wapo katika harakati za kutokugeuzwa ng'ombe. Wachichanjaji wapo tayari kutekeleza azma ya kufaidika na ngombe bila ya kujali kuwa ng'ombe anakaidi au la. Hakuna lugha ambayo ng'ombe wanaweza kuzungumza na kusikiwa na mchinjaji.

Swala zima la kuchinjwa kwa ng'ombe, ambaye ni Masumbuko aliyegeuzwa ni swala changamano na tata. Kugeuzwa ng'ombe kunaweza kuashiria kushushwa hadhi, kukumbushwa kuwa mtu yupo lakini kwa maslahi ya mtu mwingine. Inawezekana pia ikaashiria kunyang'anywa uwezo, hususani sauti na fikira razini za kuweza kujitetea. Kwa hivyo swala hili linapukuzwa na kuangaliwa katika kiwango cha mahusiano ya kijamii, linaashiria mahusiano ya kiuwezo na kimafao. Vilevile linaweza kuangaliwa katika ngazi ya kitaifa kisiasa ambapo inawezekana kuhoji kwamba linaashiria utabaka, uwezo na mamlaka, kwamba mambo haya yananufaisha upande mmoja wakati ambapo

yanadhalilisha vilevile. Kwa hiyo mtunzi anampa msomaji taswira ya mahusiano baina ya wakandamizaji na wakandamizwa kupitia taswira ya ng'ombe. Kwa ujumla jitihada za wanajamii ya Waswezi ni kuzuia ng'ombe wasichinjwe au wanajamii kugeuzwa kuwa ng'ombe. Wachinjaji ni sawa na watu wa himaya ya Waufi. Mwandishi anachimuza dhamira ya kwamba, ipo siku watawala wa kimabavu na watakuja kushushwa chini na wanyonge watatawala kwani siku zote haki huwa haipotei, bali hucheleweshwa tu.

Mwandishi kupitia Masumbuko na Hunudu, anakinzanisha pande mbili za wakandamizwaji na wakandamizaji. Kwa kuwakutanisha viumbe vya asili tofauti, Masumbuko kwa upande wa kundi la wanadamu waliombwa kwa udongo, ambao kuangamizwa kwao ni kwa njia ya kufa kwa kuzikwa na Hunudu kiumbe jini ambaye kuangamizwa kwake ni kwa njia ya nuru au moto, Mwingizi anatusomesha ugumu wa makundi ya wakandamizaji katika maumbile na mitazamo yao kuweza kuungana au kuwa na uswahiba na makundi ya wakandamizaji ambao maumbile yao na malengo yao ni tofauti. Ni taswira pana inayopambanisha malengo, matarajio, na mitazamo yao haiwezi kuungana au kufanana kwa hali yoyote ile kama ilivyo maumbile ya mwanadamu na majini. Urafiki au mahusiano yao yanawezeshwa kupitia uhalali wa kiuhasiliamazingaombwe. Uhalali huu unasababisha hata maingiliano ya kimwili (kuoana) na kiakili (katika ndoto au fikra) baina ya makundi ya wahusika wa kiuhalisia na wale kifantasia.

**4.3.2.2 Manyanyaso, Maonevu, Uwajibikaji na Ukatili**

Mtunzi amemsawiri mhusika Hunudu kuchimuza maudhui mbalimbali. Huyu ni mhusika jini ambaye amebeba uhusika changamano. Hunudu ni kiongozi wa kitengo cha mateso katika mzimu wa Waufi. Yeye ndiye aliyeteuliwa kuwashughulikia wahalifu ambao wamekwenda kinyume na makubaliano ya mzimu wa Waufi, kwa mfano Masumbuko na wengineo. Maswala ibuka na ya kimsingi katika usawiri wa Hunudu yanahusiana na wasifu wa kimsingi wa uongozi—sera na matekelezo yake, mipango ya mtu binafsi na mipango ya kiutawala, hulka za watawala na mahusiano yao na

watawaliwa. Katika misingi hii, mwandishi kupitia kwa usawiri wa Hunudu anachimuza ujumbe wa jinsi utawala wa Waufi usivyo na huruma kwani hunyanyasa wananchi wale ambao wanatoa siri za serikali ya Waufi.

Hunudu alikuwa anatumiwa na Serikali ya Waufi kwa ajili ya kuwatesa wananchi wanaokwenda kinyume na kuwaonyesha wengine mateso yale ili waogope na wasiende tofauti na Serikali hiyo. Katika hali hii inawezekana kuhoji kwamba, zipo serikali au hata watu binafsi ambao sera yao ya uongozi ni kujenga woga kupitia vitisho na vitendo halisi vya mateso na manyanyaso. Hili ni jambo linaloakisiwa katika familia, katika jamii na katika hata viwango vya serikali. Aidha mwandishi, kupitia kwa usawiri huu huu, anamwonyesha Hunudu kupitia Masumbuko akiwa kwenye ndoto akiwapa mateso mengi wale wote wanaokwenda tofauti na Serikali ya Waufi. Mwandishi anamuonyesha Hunudu jinsi alivyo mnyanyanyasaji na muonevu wa watu wasio na hatia. Hunudu katika sehemu nyingi katika riwaya hii anaonekana kuwa ni mtu katili, muuaji, jeuri, na hata asiye na chembe ya huruma ili mradi tu anatekeleza matakwa ya viongozi wake. Hunudu anampeleka Masumbuko kumwonYesha vijana walio katika mateso ndani ya kitengo chake ili kumwogofya (uk 2).

Hali kadhalika vijana hawa ni wanyonge na wasio na hatia. Ni wawakilishi wa tabaka la chini ambao wanateswa bila ya kuwa na watu au mtu wa kuwatetea. Hii ndio hali halisi katika jamii zetu kwa sasa. Wapo watu wa tabaka la chini wengi ambao hawana mtetezi katika uonevu au unyanyasaji wanaoupata. Mfano, wananyimwa na kuhiniwa mengi—hawapati huduma za kimsingi, hawana miundo msingi ya kufaa, hawazifikii huduma za kisheria au wanapozifikia, wanapembezwa mahakamani, kwenye vituo vya polisi n.k. Mfano, kwa sasa ni kawaida kusikia polisi kampiga mtuhumiwa hadi kufa. Upo uonevu pia katika ukurasa wa 145 na 148 ambao bado unafanywa na Hunudu kwa kumuua Mzee Kishindo kwa kutumia radi. Kitendo cha kutumia hali ya mazingira kama mvua, radi, kimbunga, upepo kama kiangamizo cha watu kinawezekana tu katika muktadha wa kiuhalisiamazingaombwe. Radi inaweza kuleta madhara katika jamii na kuharibu mali

na watu, lakini kutumika kwake kwa maksudi katika kumlenga mtu maalumu ni mbinu inayokubalika katika riwaya za kiuahalisiaajabu.

Aidha kinachojitokeza ni kuwa mazingira yanageuzwa kama silaha ya kutimizia malengo ya kusababisha tanzia. Je, mtunzi anakusudia nini kumtumia Hunudu kumdhuru Mzee Kishindo kwa radi? Kwanza anatupa picha kuwa wako viumbe wenye uwezo wa kutumia hali ya mazingira kama radi, mvua, mionzi ya jua au upepo kwa manufaa ya kuangamiza kutokana na kiwango cha teknolojia walionacho watumiaji wake. Kwa vile jamii ya Mwingizi ipo katika kipindi cha mabadiliko ya kuingia katika teknolojia ambapo ni kweli nguvu zinatokana na maumbile zinaweza kutumika kwa faida ya wanadamu au hasara, anatupa fursa wasomaji kufikiria matumizi yenye faida zaidi kuliko hasara ya kuangamizana. Wale wanaotumia nguvu hizo kwa kuwaangamiza wenzi wao ni maadui wa maendeleo ya jamii wawe ni wachawi, majini au wanadamu wabaya. Hunudu anazitumia nguvu zake za kutawala radi na maumbile mengine kuwatesa akina Masumbuko. Ujuzi wa "teknolojia" ya kutumia maumbile kama radi au upepo isitumike na wenye nguvu na ujuzi huo kukandamiza wengine haswa nchi zinazoendelea. Mwandishi anasema:-

> "Acha kulia we' mtoto wa kiume, kuwa makini usije ukakiuka masharti na taratibu zetu nawe ukaingia katika adhabu kama hizo unazoziona…hao ni wabishi waliokaidi maagizo yetu, na hayo ndiyo malipo yao." Hunudu alimkanya Masumbuko kwa dharau na kutokujali kabisa (uk 3).

Hunudu kama walivyo wajuzi wa "teknolojia" ya nguvu za asili; kama zilivyo nchi zenye nyuklia dhidi ya nchi ambazo hazina teknolojia ya nyuklia, zinakuwa na sauti katika Umoja wa Mataifa dhidi ya nchi nyingine. Zipo nchi chache tu zenye ujuzi wakupeleka roketi katika anga za juu, sawa na akina Hunudu wenye kumiliki nyenzo za maisha chini ya bahari. Katika kuwa na teknolojia ya anga kunapelekea maisha mataifa machache kuwa na nguvu za kijeshi na sauti dhidi ya mataifa mengine yasiyo na uwezo huo. Mwingizi anawataka wasomaji wake wavuke mipaka ya fantasia na kuingia katika mipaka ya kiuhalisia sawa na Shaaban Robert anavyowapeleka wasomaji wake katika *Kusadikika* na *Kufikirika* kuingia katika dunia ya kiuhalisia wakati wa kujadili mandhari na matukio ya kifantasia.

Nchi zenye uwezo wa kiteknolojia au tabaka la wasomi lenye uwezo linakuwa sawa na Hunudu pale wanapotumia ujuzi wao kwa kuzipa masharti magumu na uwiano usio sawa wa kibiashara katika masoko ya dunia. Hununua bidhaa zisizowekea ubunifu kwa bei ya chini na kuwauzia Bidhaa hizo hizo kwa bei ya juu pale zinapoongezea thamani. Aidha mtunzi anatudhihirishia hali ilivyo kwa uwazi, badala ya viongozi kuwa mfano mwema kwa watawaliwa, wanakuwa vikwazo katika uendelezaji wa taifa kwa kuwaangamiza wananchi chipukizi ambao wamejaa imani na matumaini ya kubadilisha sura za jamii zetu kama alivyokuwa anafanya Hunudu kwa wale vijana mle chini ya bahari. Hunudu ni mfano wa kiongozi barani Afrika aliyejaa ukatili, aliyewaangamiza wananchi ambao nia yao ilikuwa kuleta mabadiliko.

Mtunzi anaonyesha kuyumbishwa kwa mipaka kwani anamuonyesha Hunudu akiwa chini ya bahari kama kiongozi wa majini wenziwe akiwasomea ratiba ya kazi na shughuli mbalimbali zinaendelea huko chini ya bahari katika mazingira ambayo si ya kawaida watu kuishi chini ya bahari. Kwa mfano, Hunudu anaowasilishwa kama kiongozi mwajibikaji katika utendaji kazi wake. Anapanga ratiba ya wafanyakazi wake ya wiki nzima ili wajue nini cha kufanya kila siku. Hunudu anamwambia Masumbuko:-

> Taratibu zetu ziko kama ifuatavyo, Huwa tunakutana mara tatu kwa wiki ambapo siku ya Jumamosi ni siku yetu ya kufanya Ibada maalumu hukuhuku chini ya mapango ya bahari. Siku ya Jumatatu ni siku maalum ya kutoa kafara ya damu na adhabu kwa yeyote atakayekiuka miongozo yetu ikiwemo kutokutunza siri, kutokuhudhuria ibada, pamoja na kukataa kutoa kafara, n.k. Siku ya Alhamisi ni siku ya kutoa hukumu za makosa na kusikiliza shida mbali mbali pamoja na kupokea mashitaka mapya" (uk 1-2).

Mwandishi kupitia Hunudu anaonyesha namna mifumo kandamizi ilivyo na taratibu ambazo zina lengo moja tu la kuwaangamiza wale ambao hawafanani nao kimaadili, kimielekeo, kimalengo na kimikakati. Bila ya kujali wapi mtu anakotokea akikubaliana na malengo na taratibu za kikandamizaji anaingizwa katika kundi. Kwa kutumia mfumo wa dini, Mwingizi anajenga hoja kuwa wakandamizaji wana dini iliyo kamili yenye taratibu za ibada kama ilivyo dini za Kijadi, Kikristo na Kiislamu. Ubepari au

ukandamizaji ni mfumo unaonyonya jamii nyingine "damu" au rasilimali. Mwingizi ametumia metonumia ya kikoa cha mfumo wa ibada wenye siku maalumu, matambiko, hukumu na desturi zake kulinganisha na mfumo wa ukandamizaji wa wenye nguvu dhidi ya wanyonge. Ukatili wa Hunudu ni ukatili wa mfumo huo. hii ni ishara ya upebari hauna sura ni mfumo usiojali utu.

Mwandishi anamtumia Hunudu kuonyesha jinsi alivyo katili na akitumia himaya yake kuwakandamiza watu wasio na hatia pindi wanapokataa kufuata masharti yake. Ndivyo ilivyo hata katika mataifa haya yanayoendelea ambapo viongozi hutumia mamlaka yao katika kuwakandamiza wananchi wasio na hatia. Hunudu amekuwa akiwatesa watu sana hasa waliokuwa wanawafuatilia katika utawala wao na waliokuwa wanakiuka baadhi ya mambo yao. Mtunzi anamsawiri Hunudu kama mtu mgandamizaji na katili kwa watu katika kuhakikisha anatetea kubakia mamlakani. Pia Hunudu anatumia pete kama kinga ya utawala wake kwani alitumia pete katika kumbadilisha Masumbuko kutoka jinsia ya kiume hadi ya kike na kumpeleka kwa viongozi wenziwe ili waweze wamwonye. Pete ni ishara ya nguvu na uwezo. Ni ishara ambayo Mwingizi ameitumia pia katika *Vita vya Mapenzi*. Mwandishi anaonyesha jinsi Serikali hutumia mabavu kwa baadhi ya vitu kama kinga katika utawala wao ili wasitoke mamlakani na waendelee kuwanyanyasa wananchi.

Pia mtunzi kupitia pete anayoitumia Hunudu, anachimuza dhamira ya baadhi ya viongozi wengi wa kiserikali katika nchi za Afrika ambao wamekuwa ni watu wa kutegemea mambo ya kishirikina katika utawala wao. Wamekuwa hawawezi kukaa mamlakani pasipo kutegemea ushirikina na hata katika chaguzi zao pia hutegemea mambo ya kishirikina. Kwa hiyo Hunudu amekuwa akitumia pete hiyokama kinga kwa ajili kudumisha utawalawa Waufi. Vilevile Hunudu pamoja na kushindwa na Waswezi na hatimaye kumchukua Masumbuko bado Hunudu haamini anaendelea kuwafuatilia Waswezi. Mwandishi anachimuza dhamira ya viongozi ambao wanaposhindwa madaraka na wapinzani wao huwa hawakubali kwa kuamini kwamba utawala unachukuliwa huendelea kuusakama utawala uliopo mamlakani. Hunudu apandishwa

vyeo mara kwa mara kutokana na utendaji kazi wake mzuri wa kuhakikisha anapanga mipango mizuri ya kazi na kuwaangamiza wale wote wanaofuatilia utawala wao. Mwandishi anachimuza ujumbe wa jinsi viongozi mbalimbali wanavyotakiwa kufanya kazi kwa umakini ili waweze kupandishwa vyeo kutokana na utendaji kazi wao.

Hunudu ni kiongozi asiyependa usaliti. Ndio maana hakuwa na hata chembe ya huruma alimuua mama Masumbuko, kwa ajili ya kukiuka masharti waliokubaliana na Waufi kwamba akijifungua Masumbuko amtoe kafara. Mwandishi anasema:-

> Jicho la Hunudu likakutana na mama Masumbuko (aliyeiba ujauzito), inaonekana hakutaka kuchelewesha mambo, akarukia upande ule aliyoko Bi mkubwa yule na hapohapo kitendo bila kuchelewesha akaingiza mkono katika suruari yake akatoa kitu chenye ncha kali, bila huruma akamkandamizia katika jicho (uk. 216).

Haya yote yalipokuwa yakiendelea kule makaburini ndipo akaamua amuue kabisa mama Masumbuko kwa sababu ndiye aliyesababisha Waufi wakashindwa. Mimba ilipohamia kwake, ilitakiwa amtoe Masumbuko akiwa mdogo ndipo aendelee kuzaa watoto wengine. Msomaji anapelekwa makaburini ambako wanazikwa wafu. Badala ya kuwa ni sehemu ya malalo ya wafu, makaburi yanageuzwa na Mwingizi kuturudisha katika imani za Waafrika kuwa ni sehemu ya mpito tu. Maisha hayaishii kaburini bali ni sehemu moja wapo ya kuubadilisha mwili na kuwa kivuli na roho. Kaburini ni sehemu ambako inachukuliwa kama sehemu ya mizimu kwa hivyo ni sehemu mojawapo ya matambiko, uuguzi na ulozi. Makaburini panakuwa ni uwanja wa vita baina ya wauguzi na walozi.

Mandhari hayo yanatumiwa na mtunzi kama jukwaa la matukio ya kijamii na kitamaduni. Anguko la ishara ya makaburi ni anguko la mila na desturi za Waafrika. Makazi ya wafu yanapewa hadhi kubwa katika jamii za kiafrika. Hii inatokana na imani kuwa watu hawafi na roho zao bado zipo. Kitendo cha roho kutoka katika mwili ni hatua moja tu ya mabadiliko ya mtu kutoka hatua moja kwenda nyingine. Misukule ni viumbe ambavyo mtunzi anatuthibitishia kuwa mtu anapitia hatua katika kuzaliwa,

kukua na kufa. Msukule unarudishiwa roho pale inapofufuliwa kama alivyofanyiwa Mzee Mtandi au Nyanzala. Makaburi yanatumika kama sehemu muhimu za ibada. Mizimu hukumbukwa kwa kufanyiwa makafara katika makaburi. Aidha kwa upande mwingine mwandishi anaikumbusha jamii kuepukana na usaliti wa aina yeyote kwani usaliti si mzuri na mtu msaliti hupata madhara makubwa kama yaliyomkuta mama Masumbuko kutoka kwa mizimu ya Waufi au Suhail katika *Vita vya Mapenzi*. Japo usaliti wa mama Masumbuko ni usaliti ambao aliufanya pasipokupenda kwani ilikuwa ni vigumu kumuuwa mtoto ambaye amemzaa na ameteseka naye kwa muda mrefu. Hapa mtunzi anaikanya jamii iepukane na mikataba ambayo masharti yake huwa ni magumu kuyatimiza lazima utimizaji wa masharti hayo hugharimu baadhi ya maisha ya watu kama ilivyokuwa kwa mama Masumbuko na mateso aliyokuwa anayapitia mwanaye.

Hunudu anapata funzo kubwa pamoja na Waufi baada ya Waswezi kumung'oa jicho lingine la pili na kumtupa porini. Mwandishi anachimuza ujumbe wa kila mtenda mabaya malipo huwa hapa hapa dunia. Hunudu alikuwa anajivunia sana nguvu za kimajini na kichawi alizokuwa nazo akahisi hakuna mtu atakayeweza kumshinda. Lakini ilifika siku akashindwa na akateketezwa na mahasimu wake na kutupwa porini na kuliwa na wanyama wakali. Mtunzi kupitia Hunudu anachimuza dhamira ya viongozi ambao huongoza nchi kimabavu, kwa kutesa wananchi na kung'ang'ania mamlakani kwa muda mrefu mwisho wao huwa ni mbaya na huacha uongozi kwa aibu na wengine hata huuliwa kwa ajili ya kung'ang'ania uongozi wakati utendeji kazi wao ni mbovu kabisa.

#### 4.3.2.3 Ukorofi, Ukandamizaji, Dini na Dhuluma dhidi ya Wanawake

Miongoni mwa maswala ambayo Mwingizi ameyashughulikia katika riwaya ya *Mzimu wa Waufi* ni pamoja na ukorofi katika mahusiano ya kijamii, ukandamizaji usioweza kuhalalishwa na dhuluma dhidi ya wanawake. Ili aweze kuyafikia malengo haya, mtunzi amemsawiri mhusika aliye na wasifu wa ukorofi, ukandamizaji na mwenye uonevu kwa wanawake. Mhusika huyu ni Mzee Kikoko ambaye japo haonekani kwa msambao

mpana ni miongoni mwa wahusika ambao licha ya udogo wa nafasi wanazochukua katika hadithi, wanaibuka na kutekeleza majukumu makubwa ya kidhamira. Mzee huyu alikuwa ni baba yake Masumbuko. Mzee Kikoko anapuuza maswala ya fasiri ya ndoto kuwa na uhalisia. Pia Mzee huyu hakubaliani na mitazamo ya kiimani inayokinzana baina yake na mkwewe Judith. Kwa imani aliyonayo Judith yupo katika dini yenye uoni tofauti wa kiulimwengu na dini yake au ya mwanawe Masumbuko. Haamini kuwa watu wenye mitazamo tofauti ya kiuonulimwengu wanaweza kuishi pamoja. Linapozuka tatizo la mwanawe Masumbuko, lawama zote anamtupia mkwewe Judith. Mzee Kikoko anadiriki kumtukana Judith na kumuita shetani ambaye kwa mbazi za kibiblia au korani shetani ni kiumbe aliyemshawishi Adamu kuvunja amiri ya Mungu akiwa na Hawa. :-

> “Hivi we mtoto ni *Shetani* au?” Judith akapatwa na mshangao kusikia maneno hayo, ikabidi akae kimya kidogo akitafakari huo ushetani wake ni nini! “Naongea na wewe, nakuuliza we’ ni Shetani?! Nani kati yangu mimi au mama yake Masumbuko aliyekuambia ulete wachungaji wamuombee mwanangu?! (uk 38).

Si kwa Judith pekee bali Mzee Kikoko anamwambia mama Zani; “We *mchawi* nilikuambiaje nataka mwanangu apone nguruwe we..” (uk 45). Alwatan Kikoko hakuishia tu hapo katika kuzungumzia maswala ya kichawi. Alipokwenda katika duka la Shehe Jabu. Mzee Jabu anamwambia:- “Karibu Alwatan Kikoko ….. Karibu uketi kwenye kiti chako cha uvivu. Mzee Kikoko anasema, hapana nimeghairi, wala sikai tena, kuna *mchawi* humu……” (uk 52)”. Maneno haya yalimtoka tena Alwatan Kikoko baada ya kufika dukani kwa Sheikh Jabu na kumkuta Mzee Kishindo ambaye ni hasimu wake naye yupo hapo. Na ukirejea uk. 39 katika ugomvi wa mama Zani na Alwatan Kikoko kwa kile alichofanya Mama Zani kumleta mchungaji Jofrey kumwombea Masumbuko. Mzee Kikoko anasema:-

> “. . . Ama kweli nimeamini mchawi ni binadamu, paka anatumwa tu! Kumbe wewe na Mzee Kishindo ndio mnanilogea mwanangu halafu mnajifanya kuwaleta hao wachungaji…”(uk 39).

Uchimuzi wa maneno ‘mchawi’ na ‘shetani’ kupitia kinywa cha Mzee Kikoko si kwa bahati nasibu. Mwingizi anawataka wasomaji wake kukariri imani ya ushirikina inayonasibishwa na uchawi na ushetani. Swala hili kwa mujibu wa Mbiti (1975:166), lina chimbuko lake katika imani za waafrika kuwa iwapo jambo limekwenda vibaya katika familia au jamii ni lazima pana sababu. Linapokuwa jambo lenyewe ni baya kama kuugua au kufikwa na maafa, basi sababu za uchawi au ulozi zinapewa kipaumbele. Mzee Kikoko anatumika kubaini kundi kubwa la wanajamii ambao bado wana imani kuwa janga linapotokea basi kuna “mkono wa mtu”. Imani ya uchawi inatokana na kuamini kuwa kuna nguvu za siri na ujuzi wa mazingaombwe au uchawi kwa baadhi ya watu wachache ambao wanazitumia nguvu hizo kuwadhuru wenzi wao.

Babu Gao na Ustadh Atrash wanazitumia nguvu za elimu.Mtunzi amechimuza swala la ulozi na uchawi kwa wingi kupitia kinywa cha Mzee Kikoko, hii ni kuonyesha kupitia sauti yake juu ya tatizo la uchawi katika jamii yake. Katika kijiwe cha BBC kule Shinyanga, Mzee Kakoko anazungumzia uwezekano wa kijana wake kulogwa. Alimuita mkwewe Judith kuwa ni mchawi kwa kumuita Mchungaji amuombee. Vilevile alimwita Mzee Kishindo kwamba naye ni mchawi kwa sababu Masumbuko alikwenda kuomba asaidiwe matatizo kwa anayoyapata. Na alinyanyuka kijiweni kwa kisingizio kwamba kuna mtu mchawi pale akimaanisha Mzee Kishindo. Uchimuzi wa aina hii ni dalili kuwa jambo hilo linamkera sana mtunzi. Swala la uchawi na nani mchawi katika mazungumzo haya lina maana pana, ikizingatiwa kwamba Judith anaitwa mchawi, kwa njia hii uchawi unahusishwa na wanawake. Lakini inapozingatiwa kwamba uchawi unaangaliwa kwa njia hasi, wachawi nao wanaangaliwa kwa njia hasi ikiwa na maana kwamba wanawake wanaangaliwa kwa njia hasi. Nafasi ya wachawi katika jamii hii ni nafasi ya pembeni, hivyo ndivyo ilivyo pia nafasi ya wanawake.

Aidha dhana hii uchawi inachimuza dhamira ya migongano na mitagusano mbalimbali katika jamii na ambayo watu wengi huipitia katika maisha. Wakati mwingine mtunzi hutaka kuonyesha kwamba kuna matatizo madogo madogo sana katika jamii endapo yasipopata suluhu mapema huleta migogoro ya muda mrefu na hatimaye watu kukosana

na mpaka kuuwana. Kwa upande mwingine mtunzi kupitia Mzee Kikoko anachimuza dhamira ya jinsi watu wanavyoamini mambo ya uchawi na hata kuleta migogoro mikubwa sana katika jamii. Kuna watu katika jamii huwa hawaamini vipimo na majibu ya daktari wanapoambiwa tatizo fulani limetokana na kitu fulani. Ajabu yake hudiriki kuwasema ndugu zao au marafiki zao wamewaloga. Na hata wengine, kwa mfano, Tanzania hudiriki hata kuwaua wale wanaowahisi kuwa ni wachawi.

Mtunzi anaibua maswali mengi na nyeti juu ya jamii yake, uchawi na ushirikina na mwonoulimwengu unaotumiwa kupima ukweli na uongo, kama mchakato wa kutatulia shida za ki binafsi, za kifamilia na za kijamii. Kwamba uchawi uwe unakiriwa na wanajamii au unasemwa kichini chini ni uhalisi uliopo ila haujulikani ni kwa kiasi gani unaakisi na kutatua matatizo ya jamii. Lazima pawe na sababu nzuri kueleza ni kwa nini uchawi unajitokeza katika takriban mazungumzo na maingiliano ya kila namna. Mzee Kikoko amechorwa kama mtu asiye na subira na Mzee katili pia kwani alikuwa akipigiwa simu na mkwewe juu ya ugonjwa wa Masumbuko na kabla hajamaliza kuongea alikuwa anamkatisha na kumtukana. Baada ya mkwe wake kumwambia Masumbuko alipatwa na matatizo akiwa njiani anatoka kwa Kishindo anakasirika sana na akanyanyua simu na kumpigia Mzee Kishindo na kumtukana matusi bila hata salamu. Mzee Kikoko anasema;

> “Tena ngoja, umenikumbusha” Mzee Kikoko baada ya kusema hayo akatoa simu yake na kumpigia Mzee Kishindo. “Asalamu alaykum Bwana Kikoko” “Hakuna cha Salam hapa, hivi unanitaka nini na maisha yangu we’ Kishindo?”
>
> “Hebu punguza spidi kwanza kaka, kuna nini hasa?”
>
> “Nipunguze spidi ya nini? Reli haina bamzi hii, miye nakuja moja kwa moja huko ulipo ili unieleze ni kiherehere gani kilichokutuma kwenda kumueleza upuuzi wako Mwanangu? Wewe unaweza kuyajua matatizo ya Mwanangu kuliko mimi mzazi wake? (uk 40).

Mzee Kikoko akiwa Buguruni kwa mwanaye ghafla Masumbuko anapotea kimiujiza akiwa bafuni anaoga. Mzee Kikoko na wenziwe wanafungua bafu na kumkuta hayupo kaondoka kimajini. Mzee Kikoko anaamua kumpiga Judith aseme wapi mwanaye

amekwenda wakati wote walikuwa sebuleni wakati Masumbuko anakwenda kuoga. Kutokana na ugomvi huo mama mwenye nyumba anaamua kumtukana Mzee Kikoko kwa kitendo alichokifanya cha kumpiga mkwewe. Ndipo Mzee Kikoko anamtukana mama Jay na kumwambia kwamba "Huna hata haya wakiitwa wenye nyumba na wewe utatoka na hiki kibanda chako cha kuoshea maiti?" (uk 67). Hali hii inadhihirisha wazi kabisa ni vigumu watu wa tabaka la chini kujikwamua kutoka katika hali ngumu walimo kutokana na kwamba wenyewe kwa wenyewe hawana umoja wanadharauliana, kwa mfano, Mzee Kikoko na mama Jay wote ni maskini kwani mtoto wake Masumbuko kapanga kwa mama Jay nyumba ya kawaida na kama angekuwa na uwezo angepanga nyumba kubwa na nzuri.

Mtunzi anatumia ukaidi na maneno ya uchawi ambayo muda wote hayamtoki Mzee Kikoko kinywani katika kuonyesha kwamba wakati mwingine umaskini walio nao watu katika jamii ambao unapelekea hali ngumu ya maisha kwa baadhi ya wanajamii ndio unaopelekea ugomvi na vita wakati wote na kuchukiana bila sababu. Kwa usemi mwingine, umasikini hudumaza akili, hupunguza uoni na hata uwezo wa kupima mustakabali wa maisha utakavyokuwa. Kwa hivyo, kwa maskini inakuwa rahisi kulaumiana, kujiingiza katika imani za jadi, pengine imani na dini bandia na kwa njia hiyo hutekwa akili na kuachwa kuishi maisha ya kutarajia pasina kujua kinachotarajiwa kitafika lini. Kwa misingi hii, Mzee huyu ametumiwa na mtunzi kusawiri hali ngumu walizonazo wananchi zinazowafanya wakati wote wawe na misuguano ya kimaisha hasira katika kuona kwamba huenda kuna siku watafanikiwa kutoka katika hali ngumu ya maisha waliyonayo. Hali hizi za ukata na ulitima[10] haziruhusu maskini kuona imani za uchawi kuwa kipingamizi katika kujikomboa kwao bali wanaziona imani hizi kama njia mbadala na mkakati wa kufikia mambo mema. Lakini kwa upande mwingine, hili ni jambo ambalo mwandishi analipigia kelele na kukikemea ikizingatiwa kwamba, hatimaye, uchawi na imani za kichawi zinashindwa.

10 Ulitima ni hali ya kuwa katika shida za kiuchumi au kutokuwa na uwezo wa kifedha au wakati mwingine wa kukosa mahitaji ya msingi

Mzee Kikoko anaonekana kujua sheria vizuri kwani askari wanataka kumkamata kwa kosa la kufanya ugomvi kwenye nyumba ya watu baada ya mtoto wake Masumbuko kuchukuliwa kimiujiza na jini Hunudu. Mzee Kikoko anawaambia askari kwa nini hawajitambulishi wanaanza tu kumkamata. Ndipo Mzee Kikoko anakataa anawaambia wajitambulishe na waonyeshe vitambulisho vyao, na pia waseme wanamkamata kwa kosa gani? Mwandishi anachimuza ujumbe wa umuhimu wa kujua sheria ili usinyanyaswe. Kwa hivyo, ni vyema watu wote wakazijua haki kupitia kujua sheria vizuri. Hii itawasaidia kutokuonewa. Kupitia Mzee Kikoko mwandishi anasema:

> "Sio nimeridhika lazima utambue majukumu yako na ufuate taratibu za kazi yako, sasa usipojitambulisha nitakutambuaje kama wewe ni askari? Kama ni hizo bunduki na sare hata wahalifu pia huwa wanazitumia, na wao wakijifanya ni maaskari wanakamatwa na tunaona kwenye vyombo vya habari" (uk. 69).

Kupitia nukuu hii mwandishi anaonyesha jinsi raia wengi wanavyotumia sare za jeshi na bunduki katika kufanya uhalifu. Kwa hiyo ni vema kufanya uchunguzi wa kutosha mtu anapokuwa anajitambulisha kuwa yeye ni askari polisi. Maana kuna wakati mwingine watu wamekuwa wakitumia sare za kijeshi na kipolisi katika kufanya uhalifu sehemu mbalimbali.

Mzee Kikoko ni kiwakilishi cha tabaka la wahafidhina, yaani tabaka la watu wasiotaka mabadiliko kiasi cha kung'ang'ania msimamo wa kumkataa mkwe wake mwenye imani tofauti na yeye mpaka inafikia hatua anamnyang'anya mke wa Masumbuko vitambulisho vyote vya banki na kumwambia kwamba, hana chake kwa hiyo, aondoke na aache kuishi na mtoto wake. Mzee Kikoko pamoja na kuwanyanyasa Judith na Mzee Kishindo mwisho wa siku mizimu ikaonyesha chanzo cha ugonjwa wa Masumbuko ni mizimu ya Waswezi na Waufi baada ya mama Masumbuko kukataa kumtoa Masumbuko kafara. Baada ya mambo haya yote kujulikana Mzee Kikoko anaumwa ugonjwa wa ajabu na anaambiwa tiba ya ugonjwa wake ni kuwaomba msamaha wale wote aliowakosea akiwemo na mkwe wake Judith la sivyo atakufa. Ndipo Mzee huyu akaamua kumwomba msamaha Judith. Mwandishi kupitia Mzee Kishindo, anachimuza ujumbe wa kwamba, chochote kibaya umfanyiacho mtu hapa

duniani, malipo huwa hapa hapa duniani. Kwa upande mwingine mtunzi anawakumbusha viongozi ambao ni makatili na wakaidi ambao wanawaonea wananchi na wanajua kabisa wanachokifanya si sahihi na inastaili waache kwani na wao mwisho wao mara nyingi huwa unakuwani mbaya.

Mtunzi anaonyesha kuyumbishwa kwa mipaka ya wakati kwa kuchanganya swala zima la ukale na usasa kwani kuna wakati Mzee Kikoko anaonekana kuwa mdhalilishaji na muonevu wa wanamke. Alwatan Kikoko anaonekana kuwa ni mtu mwenye mtazamo wa kizamani kwa kuona mwanamke ni kiumbe duni na asiye na maamuzi yeyote na anayepaswa kuwa chini ya mwanamume wakati wote. Tazama majiBizano yake na mama Jay huku mama Jay akilalama;

> "Hivi we Mzee una matatizo ya akili… Unanitusi mimi we mwanamke? Nakutusi ndio huna akili, mtu mzima ovyo kazi kuonea tu wanawake, kama una nguvu sana si ukaombe usajili wa ndondi huko na wanaume wenzio" (uk. 66-67).

Maneno haya yalimtoka mama Jay baada ya kumwona Kikoko akimpiga mama Zani ambaye ni mkwewe. Kikoko hakuishia hapo bali yapo matumizi ya maneno makali juu ya mama Zani katika ukurasa wa 38 mfano; Mzee Kikoko anasema "Hivi we mtoto ni shetani au!. Pia katika ukurasa wa 39. "bado anamporomoshea mama Zani maneno makali anamwambia "Mpumbavu mkubwa wewe". Matumizi ya maneno kama haya kwa Mzee kama Alwatan Kikoko tena mbele ya mkwewe si sahihi kabisa. Hii inadhihirisha wazi kuwa Alwatan Kikoko ni mtu wa dharua kwa wanawake. Kama wafanyavyo baadhi ya wanaume katika katika jamii kwa wanawake.

**4.3.2.4 Upendo, Hekima, Umuhimu wa Kuomba Msamaha na Uvumilivu**

Mtunzi anaendelea kuchimuza dhamira mseto mbalimbali kupitia kwa mhusika Mzee Kishindo. Mzee huyu anachimuza dhamira ambazo zinamakinikia ujenzi wa jamii ya watu ambao wanatakiwa kuwa na tabia kama za Mzee Kishindo. Mzee Kishindo amesawiriwa katika kubeba dhamira za upendo, hekima na uvumilivu. Huyu ni Mzee ambaye alikuwa na huruma na upendo kwa Masumbuko pindi Masumbuko

alipomfuata na kumwambia ndoto anazoota za kutisha kuhusu dini ya Waufi. Mzee huyu anaonyesha hali ya uajabu kwa kumuelezea Masumbuko kisasili ambacho kinahusu chanzo cha jina lake kwa kumwambia chanzo cha jina lake Masumbuko ndio chanzo cha matatizo yake kwani mama aliyenaye si mama yake wa asili, mama yake wa asili ni mke mdogo wa Kikoko. Na Mzee huyu kutokana na kadhia anayoipata Masumbuko, anamwonea huruma na kumwambia atafute pesa kwa mizimu ya mama yake asilia kwa Waswezi ili aweze kuepuka mateso ya Waufi.

Hapa kunaibuka swala la utangamano uliopo kati ya watu walio hai na mizimu ikizingatiwa kwamba uponyaji wa Masumbuko utawezeshwa tuna mizimu. Huu ndio muonoulimwengu wa jamii hii ambapo kunaibuka fahiwa kwamba uhai na ufu ni mkufu mmoja mduara, kwamba waliokufa wanashawishi walio hai na walio hai wanawategemea wafu. Mzee huyu anachimuza dhamira ya upendo kwani pamoja na baba yake Masumbuko kumtukana na kumdhalilisha hata kumpiga lakini alikuwa na roho ya upendo ya kumsindikiza Masumbuko kwa mama yake wa asili. Japo wakiwa njiani waliweza kuvamiwa na Waufi. Waufi walitumia radi kumuua Mzee Kishindo kwa hiyo hawakuweza kufika Tabora kutokana na kifo hicho. Mzee huyu anakufa akimsaidia Masumbuko. Kinachojidhirisha hapa ni matumizi ya maumbile kama radi katika kutekeleza tukio katika usimulizi. Kwa hivyo kupitia Mzee huyu, mtunzi anaonyesha matatizo mengi walionayo binadamu wakati mwingine ni kujisahau mambo waliyoyafanya kipindi cha zamani ambayo si mazuri baadaye yanakuja kuleta matatizo kwa vizazi vyao vijavyo. Kwani Mzee Kishindo anamshangaa Mzee Kikoko pale anapomwambia kuwa yeye ni mchawi wakati chanzo cha matatizo ya majini aliyonayo mwanaye kinafahamika. Mzee Kishindo anasema;

> "Hivi Kikoko uko timamu kichwani mwako wewe? Miye nimroge mwanao ili iweje? Huwajui wachawi wa mwanao? Au unajichetua tu, sasa kama wewe ni jemedari na una nguvu sana kwa nini usimdhibiti huyo aliyesababisha yote hayo? Yaani unahangaika kukinyoosha kivuli wakati uliopinda ni mti?!"(uk 53).

Mzee Kikoko kasahau kabisa matatizo yanayompata mwanaye kutokana na usaliti wa mke wake mkubwa. Mzee Kishindo anauawa kwa kupigwa na radi kiuchawi na

jini Hunudu sababu ya kutoa siri za Waufi kwa Waswezi. Mtunzi anatuonyesha kufutika kwa mipaka baina ya uhai na ufu kwa kumtumia mhusika ambaye alishakufa lakini akafufuka kwa lengo la kuchimuza ujumbe wa umuhimu wa msamaha. Katika imani za Waafirka wafu hufa kimwili lakini pia wanaweza kuwa katika hali ya kivuli chao au katika umbo la misukule. Katika imani za Waafrika mizimu, misukule au vivuli vyao ni sehemu muhimu ya mduara wa maisha. Hivyo mwandishi anadiriki kumtumia mtu aliyefufuka kuja kutoa ujumbe kwani mtu huyo tayari amekwishapanda daraja la kuwa ni nyenzo ya mawasilano baina ya nguvu za juu za ujaala na wanadamu. Ugomvi kati ya Mzee Kikoko na Judith ni kutokana na tofauti za mitazamo na mionoulimwengu iliyosimikwa na mifumo dini katika jamii ya mtunzi.

**4.4.2.5 Udhalimu, Hekima, Busara na Usaliti**

Mwingizi ameweza kutumia ubunifu wa hali ya juu kiasi kwamba, tunaona jinsi uhalisiajabu katika riwaya zake ulivyoweza kudhihirika kupitia kisasili cha chanzo cha Masumbuko kuitwa Masumbuko kupitia kwa Binti Kapemba. Miongoni mwa dhamira mseto alizozimakinikia Mwingizi kupitia kwa usawiri wa mama huyu ni pamoja na dhamira ya udhalimu, hekima na busara pamoja na usaliti. Mwingizi amemsawiri mhusika huyu kwa kuonyesha jinsi nafsi za wanawake wengi zinazovyoumia pale inapotokea wanakosa watoto mpaka inafikia hatua ya kutumia uchawi ili waweze kupata watoto kwa njia ya udhalimu. Binti Kapemba ni mke mkubwa wa Mzee Kikoko ambaye aliiba mimba ya mwenziwe kwa njia ya uchawi. Mimba ya mke mwenziwe ilipokuwa na miezi mitano ikahamia kwake kupitia mizimu ya kwao ya Waufi.

Mama huyu anapojifungua anamwita mwanaye Masumbuko kutokana na kadhia aliyoipata hadi anampata mtoto huyu. Pamoja na kufanikiwa kumpata mtoto alipewa masharti amtoe kafara halafu ndipo aendelee kuzaa watoto wengine lakini yeye hakufanya hivyo. Ndipo Masumbuko akawa anateswa na Waufi. Matendo ya ajabu ya kuhamisha mimba ni sehemu ya mbinu kuu ya riwaya za uhalisiajabu. Kinachoibuliwa katika sehemu hii ni kwamba dunia ya umazingaombwe inaingiliana na dunia ya uhalisia. Mimba wanapata wanawake, ni uhalisi wa maisha. Lakini katika

muktadha wa uhalisiajabu mimba yaweza kupatikana bila ya mwanamume kuwepo (angalia Masumbuko alivyogeuzwa mwanamke) na pia yaweza kuhamishwa kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mtu mwingine. Mimba katika masimulizi haya ya kihalisiajabu, ni taswira na fumbo lililo na maana pana.

Mimba ni matokeo ya juhudi, mimba ni ahadi na matumaini, mimba ni hakikisho la uendelezaji kizazi, mimba ni maisha, tegemeo na nguzo. Mimba inaashiria mambo mengi, inaashiria uwezekano mpana. Kwa hivyo, kupitia tukio na kioja cha uibwaji wa mimba, Mwingizi anachimuza dhamira mseto, kuvunjika kwa matumaini, kutamaukwa na kuvunjwa kwa ahadi, hivyo wizi huu wa mimba unaashiria miongoni mwa mambo mengi jinsi wanasiasa wengi wanavyofanya wanapoona wameelemewa katika swala zima la siasa katika chaguzi mbalimbali, huiba na kunyang'anya kutoka kwa wengine. Huona njia rahisi ya kupata kura ni kuhakikisha wanatumia njia mbalimbaliza hila na ujanja katika kufanikisha hatima yao ya kushinda kwa kuiba kura.

Kwa upande mwingine, mwanamke anayeiba mimba ya mke mwenzake anachimuza ujumbe wa jinsi wanawake wasiozaa wanavyopata shida katika familia zao. Hili lilidhihirika kwa mke mkubwa huyu baada ya wazazi wa mumewe shemejize kumtaka mtoto wao amfukuze huyu mwanamke aowe mwanamke mwingine kwa sababu hazai. Hali kama hii hujitokeza kwa wanawake wengi ambao bado hawajabahatika kupata watoto wanavyoteseka kwa ndugu wa mwanamume hasa kwa upande wa Afrika. Hapa mwandishi anaangazia maswala mengi ya kifamilia na kijamii kama vile umuhimu wa kizazi na uendelezaji kizazi, kutambuliwa na kuheshimiwa kwa mwanamke kunafungamnishwa na uzazi kwamba watoto ndio wanaompa mzazi heshima na utumbuzi katika jamii. Hali kadhalika, linaibuka swala la utulivu, heshima na utangamano wa kifamilia katika misingi ya uwepo wa watoto. Thamani ya mtu inapimwa kwa mizani ya uwepo wa watoto.

Mtunzi anatumia uibwaji wa mimba hii katika kuchimuza ujumbe wa jinsi mataifa yaliyoendelea yanavyokuwa na tamaa ya maliasili nyingi za Afrika hata kufikia wakati

kutengeneza mikakati ambayo wataitumia mpaka kuhakikisha wananufaika na baadhi ya uchumi wa Afrika. Vilevile mtunzi kupitia mkasa huu anaonyesha jinsi jamii nyingi za kiafrika zinavyoona kukamilika kwa mtu yeyote ni kuendeleza kizazi kwa kuzaa watoto, na inapotokea kuwa mtu habebi mimba basi huonekana ni mtu ambaye hajakamilika. Kwa mintarafu hii mtunzi anaonyesha jinsi watu wanavyothamini sana utamaduni na inapotokea mtu ameenenda kinyume na makubaliano baadhi katika utamaduni huadhibiwa na miungu kama ilivyokuwa kwa mama Masumbuko. Halikadhalika mtunzi anaendelea kuonyesha kwamba mimba ni taswira ya neema ambayo mataifa yanayoendelea yanaitamani sana neema hiyo pasina kujua kwamba neema hiyo imebeba maangamizi. Kwani neema hiyo katika mataifa yaliyoendelea hutumiwa kama chambo cha kufanikisha hatima ya mambo yao wanayotaka katika kuendeleza nchi zao. Nchi zinazoendelea huwa zinafika mahali zinashtuka kutokana na neema hiyo kutokuwa neema ni maigizo wakati wameshadhulumiwa sana.

Kwa upande mwingine mama huyu anaonekana kuwa na hekima na busara kwa kumsihi mumewe aache kufanya baadhi ya vituko alivyokuwa anavifanya. Japo mumewe alikuwa mkorofi na jeuri lakini aliweza kumsihi na kumvumilia. Mwandishi anasema;

> Mkewe alijaribu kumnasihi ili atumie busara katika kulitatua swala lile, lakini kwa Mumewe alikuwa akitwanga maji kwenye kinu, kwani mumewe ndiyo alizidi kujaa jazba (uk.41).

Hii inaonyesha wazi kabisa mama huyu alikuwa na busara ndipo maana alikuwa anamsihi mumewe aache kumtukana Mzee Kishindo matusi kama yale. Bibi huyu anakuwa na mgogoro na viongozi wa Waufi kwa sababu alisaidiwa kupata mtoto na akaambiwa akikua anatakiwa kutoa kafara lakini yeye akakaidi na akaacha kumtoa Masumbuko kafara na wakaamua kumtoa mwenyewe. Mtunzi anachimuza ujumbe wa kukaidi masharti ambayo mataifa yaliyoendelea hutoa kwa mataifa yanayoendelea na baadhi ya nchi hukataa masharti hayo. Mfano mzuri ni nchi ya Zimbambwe ambayo iligoma kuingia mikataba yoyote na mataifa yaliyoendelea na mpaka leo bado wanasonga mbele pamoja na kwamba hawategemei misaada yoyote

kutoka katika mataifa yaliyoendelea. Japo pia wana changamamoto nyingi lakini wana uhuru wa kufanya maamuzi.

**4.3.2.6 Uvumilivu, Umoja ni Nguvu**

Mwingizi ameweza kugusia pia maswala ya uvumilivu na kuonyesha kwamba umoja ni nguvu siku zote. Mwingizi kupitia kwa mhusika Binti Fundikira amechimuza dhamira za uvumilivu na umoja. Mtunzi kupitia uibwaji wa mimba ya Binti Fundikira anachimuza dhamira ya baadhi ya wanasiasa kuwa wavumilivu katika maswala mbalimbali ya kisiasa kwani katika mataifa yanayoendelea wanasiasa wengi wameshindwa kuwa wavumilivu wa kisiasa kutokana na kuumizwa na wapinzani wenzao na hatimaye kusababisha machafuko katika nchi zao hasa katika kipindi cha uchaguzi katika swala zima la uibaji wa kura. Lakini mtunzi anaikumbusha jamii kuwa na uvumili na kuendelea kuwa na umoja ili kuleta amani katika nchi hizo.

**4.3.2.7 Swala la Wanasiasa au Watu Kuingilia Taaluma zisizo zao, Uwajibikaji na Utendakazi**

Mwingizi ameweza kuchimuza maudhui mengi kupitia usawiri wa wahusika wa kifantansia. Maudhui hayo kwa namna moja au nyingine yameweza kugusa jamii kwa kiasi kikubwa katika nyanja mbalimbali kama vile nyanja za kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni. Miongoni mwa maswala ambayo amechimuza kupitia kwa usawiri wa mhusika daktari ni swala la wanasiasa au watu kuingilia taaluma zisizo zao, uwajibikaji na utendakazi. Daktari ni mhusika ambaye alikuwa ni daktari mkuu katika hospitali ya Kitete alikopelekwa Nyamizi baada ya kupigwa na Hunudu kule kwenye viwanja vya mizimu wakati wanamsimika Masumbuko kuwa kiongozi wa Waswezi.

Mtunzi anaonyesha jambo la ajabu katika kuonyesha kwamba mambo haya yanatendwa katika jamii kwa kuonyesha jinsi Hunudu anavyowatumia polisi kimajini hadi wanampeleka hospitali Nyamizi na kulazimisha waganga na manesi wamweke kwenye chumba cha maiti wakijua amekufa baada ya kukatwakatwa na mapanga na Hunudu. Cha ajabu madaktari waligundua bado hajafa ila amezimia. Ndipo daktari

huyu akamwita afande Manumbo kujibu tuhuma ambazo walizifanya na askari wenziwe za kung'ang'aniza maiti kupelekwa chumba cha maiti wakati mtu bado hajafa. Daktari huyu anamwambia Afande Manumbo kwamba;

> ..nyinyi ni wataalamu wa maswala ya upelelezi, walinzi wa raia na mali zetu, sasa haipendezi kabisa kwa namna yeyote ile kuingilia taaluma zisizokuwa zenu".. "….mmemleta yule dada hapa huku mkinishinikiza kuwa awekwe chumba cha maiti, Bila ya kujali taratibu za kitaBibu zilizopo hapa, na hata pale mlipopewa taratibu zetu mlizidi kuelekeza kwa kukaripia wataalamu. Sasa iko hivi huyo dada wala hakupoteza maisha kama unavyosema bali alipoteza kitu kingine kabisa…fahamu tu (Uk 164).

Mwandishi kupitia daktari huyu anachimuza ujumbe wa watu kutokuingilia taaluma za wenzao. Utakuta mtu ana taaluma nyingine lakini anang'ang'ania kufanya jambo ambalo halipo katika taaluma yake. Mfano mzuri, wanasiasa wengi hupenda kuingilia taaluma ambazo si zao. Wanasiasa huwa wana tabia ya kuwaahidi wananchi kwamba baada ya muda fulani barabara itakuwa tayari au maji yatakuwa tayari katika maeneo yenu bila kuongea na wataalamu wa maswala hayo kwamba muda huo vitu hivyo kama vitakuwa vimekamilika, ili wawe na ahadi za ukweli lakini wenyewe hawajali hilo ili mradi wapite. Lakini dhamira nyingine inayojitokeza ni mgongano kati ya tiba jadi na zile tiba za kisasa. Yapo maneno ambayo tiba hizi zinaweza kusaidiana. Ambapo uvumbuzi katika tiba jadi huweza kusaidia ugunduzi wa tiba katika utabibu wa kisasa. Lakini ieleweke kuwa tiba jadi ina sehemu inayohusu ulozi na sio uganguzi. Katika sehemu hii ya ulozi ndipo tunakutana.

#### 4.3.2.9 Kutokutenda Haki katika Ofisi

Mtunzi amechimuza dhamira ambazo zinaonyesha jinsi watu wanavyodhulumiwa haki zao na hawana pa kusemea katika ofisi mbalimbali iwe ni serikalini au taasisi za kibinafsi. Jovaiven Kitale ni bosi wa Masumbuko, Mkurugenzi wa kampuni ya Birimuye. Mkurugenzi huyu ni mzungu na ndiye aliyemwachisha kazi Masumbuko kwa sababu alikuwa anaumwa ugonjwa unaotokana na majini, ugonjwa ambao kuna wakati unamfanya mzima na kuna wakati akiwa ndotoni ugonjwa huu humrudia tena na jini Hunudu humtokea. Jini huyu humfanya akimbiekimbie ovyo ovyo kwenda mapangoni

kwenye majini wenziwe wa Hunudu. Bosi huyu aliamua kumsimamisha kazi bila hata kumwandikia barua ya onyo wala barua ya kumfukuza kazi. Kitale anamfukuza kazi Masumbuko kwa kuwaambia rafiki zake wamwambie.

Mwandishi kupitia bosi huyu, anachimuza ujumbe wa utendaji haki mbaya, kwani kumekuwa na kesi nyingi katika nchi ya Tanzania kwa baadhi ya makapuni yanayomilikiwa na wageni wa kizungu, kichina na kihindi kuwafukuza wafanyakazi bila hata kuwapa barua ya onyo. Bosi akiamka akikuta umefanya kosa au anahisi umefanya kosa anakufukuza hata kama alikupa mkataba. Haki imekuwa haitendeki kabisa kwa hawa watu. Yaani wanakuwa wanaendelea kutawaliwa katika nchi yao kwa kutumia njia kama hizi. Pia hata kwa baadhi ya watendakazi wa serikali wamekuwa na tabia hii pia ya kuvunja sheria kwa kufukuza fukuza wale wote ambao wana makosa ambayo wakati mwingine yanahitaji onyo lakini wamekuwa wakiwafukuza.

Pia mwandishi kupitia ndoto hizi anazoota Masumbuko mpaka kumpelekea bosi wake kumfukuza kazi, anachimuza dhamira ya unyonyaji unaofanywa na mataifa yaliondelea kupitia akili za wazawa. Bosi huyu amechorwa tu kama mzungu ambaye anakutana na mfanyakazi mwenye majini. Mtunzi anaonyesha jinsi mataifa yaliyoendelea yanavyotumia akili za waafrika katika kuwapumbaza kisaikolojia waafrika ili weweze kuwanyonya kiurahisi. Ugonjwa huu wa Masumbuko unatumiwa kama ni njia mojawapo ya kuwapumbaza waafrika kwa lengo la kuwanyonya na wakishaona waafrika hawa wameweza kujitambua hujifanya hawahitaji uhusiano wowote katika maswala ambayo walikuwa wanayafanya kwa sababu wameshajua mbinu zote tayari. Aidha mtunzi anaonyesha ugonjwa huu ni ile hali ya kutojitambua katika kufanya baadhi ya mambo. Kitu ambao kinapelekea wanasiasa wengi kuungana na mataifa yaliyoendelea kwa ajili ya kupata misaada lakini pindi mtu anapopata utambuzi juu ya kitu ambacho anadhulumiwa mataifa haya huwa wakali na wakati mwingine husitisha misaada ghafla Bila sababu za msingi.

Kwa hiyo mtunzi anaonyesha matukio ya kimajini kwa kuvuka mipaka kwa kumshirikisha mzungu kwa kuonyesha kuyumbishwa kwa mipaka ya utaifa na uzao kwa kuwatumia watu wa mataifa yaliyoendelea kutofurahishwa wanapoona waafrika wamejitambua huchukia, hutaka waafrika waendelee kuwa vizuuu na watumwa katika kuendeleza mataifa yao. Mtunzi amefanya hivyo katika kuonyesha jinsi mataifa yaliyoendelea yanavyojifanya baadhi ya vitu katika mataifa yanayoendelea hayavifahamu kumbe si kweli wanafahamu na ndio ambao wamewafanya waafrika wawe kama walivyo hivi leo.

**4.3.2.10 Unyonyaji na Kuthamini Utamaduni wa Kiafrika**

Mzee Kagomba ni Mzee anayewaoana waganga wa jadi kama suluhisho la matatizo ya Masumbuko ya kuwa na majini. Ndio maana Mzee huyu anamlazimisha baba yake Masumbuko aende kwa waganga kwa ajili ya kupata tiba. Lakini Mzee Kikoko anakuwa mbishi kwenda kwa waganga kwa sababu anahisi mwanaye hajarogwa. Kwa hiyo mtunzi kupitia Mzee Kagomba anachimuza ujumbe wa ufinyu wa kifikra katika kujisimamia katika mataifa ya ulimwengu wa tatu katika kufanya maamuzi mpaka kuona mataifa yaliyoendelea ndio yanaweza kumaliza matatizo yao. Kwani kitendo cha kuona hakuna msaada mwingine wa kumaliza matatizo yao isipokuwa kwa kuomba misaada katika mataifa yaliyoendelea hupelekea nchi masikini kuwa masikini zaidi wakati mataifa yaliyoendelea yanaendelea kuneemeka.

Mtunzi Mwingizi kupitia Mzee Kagomba anachimuza ujumbe wa utamaduni wa Kiafrika kuathiriwa na ukoloni mamboleo kwa namna nyingine. Kwani kabla ya ujio wa wageni mbalimbali wa kizungu kutoka katika mataifa mbalimbali kulikuwa na utamaduni ambao watu waliamini katika vitu mbalimbali kupitia waganga wa jadi. Mfano mtu alikuwa akiota ndoto ambazo zina utata alikuwa akipelekwa kwa mganga halafu mganga akatafsiri na kile atakachokitafsiri kilikuwa kinatokea kweli. Tofauti na sasa kwani watu wamekuwa wakiamini katika dini mbalimbali mfano dini ya kiislamu na dini ya kikristo. Ndio maana hata ndoto za ajabu alizokuwa anaota Masumbuko walikuwa wanaitwa wachungaji na mashehe kwa ajili ya

kumuombea lakini matatizo yake hayakwisha hata kidogo. Maingiliano haya yamepelekea hata watu kuona matatizo yote yaliyopo duniani yanaishia kanisani au misikitini wakati huenda wangeomba kwenye miungu na mizimu ya mababu matatizo huenda yangeisha.

Hoja ya Mwingizi ni kuonyesha kuwa ingawa jamii yake imeingiliwa na tamaduni, mifumo na itikadi ya kigeni, bado anaona kuwa kiunganisho pekee ni mfumo jadi unaotoa tafsiri ya maisha kwa Waafrika. Mfumo huo hauwezi kuachwa ghafla au kubadilishwa bila ya kuathiri vizazi vilivyopo na kuleta mgawanyo katika jamii. Iwapo vijana wanafuata mabadiliko na wazee bado wanang'ang'ania na wanaona ni haki yao kuuongoza vizazi vya leo bila shaka migogoro huzuka. Anachokijenga mtunzi ni kuwa mabadiliko yatokee ndani ya mfumo wenyewe taratibu na wanajamii wapate fursa ya kujadiliana na kujiandaa na mabadiliko hayo. Upandikizaji wa utamaduni na desturi za Kimagharibi katika jamii za Kiafrika kwa vyovyote vile utaleta misuguano ya kimtazamo na kuigawa jamii. Suluhisho la mwandishi ni kuvumuliana na kama ambavyo Judith alivyoamua kumsamehe Mzee Kakoko huku mzimu au kivuli cha Mzee Kishindo kikishuhudia na kuthibitisha kuwa hata mizimu imeridhia kuwepo kwa suluhu kwa wanajamii walio na mitazamo tofauti ya kupandikizwa kutoka nje. Suluhisho siyo kukwaruzana bali ni kukubaliana kuwa na suluhu na kuungana katika mambo ya msingi kama vile matambiko.

#### 4.3.2.11 Mapenzi ya Dhati, Dini na Uvumilivu

Mwingizi amemtumia Judith kuudhihirishia ulimwengu kwamba pamoja na kwamba, mwanamke anaweza akapitia matatizo mbalimbali kutoka kwa wakwe zake lakini akavumilia na akampenda mumewe. Ndivyo ilivyokuwa kwa mhusika Judith pamoja na kupitia misukosuko mingi ya utofauti wa dini mpaka kupelekea kukosana na baba mkwe wake aliendelea kuvumilia.  Mwingizi kupitia mhusika Judith amechimuza dhamira za dini, mapenzi ya dhati na uvumilivu wa mwanamke. Judith ni mke wa Masumbuko. Mwanzoni mwanamke huyu amechorwa kama mwanamke mwenye mapenzi ya dhati kwa mumewe asiyeyumbishwa na chochote pamoja na tofauti zao za kidini

lakini alimpenda sana mumewe. Aidha pamoja na baba mkwe wake kumtesa kwa kumtukana matusi kedekede, aliendelea kuvumilia.

Pia mwandishi kupitia Judith, anachimuza maudhui ya madhara ya dini za kigeni, kwani mwandishi anaonyesha jinsi Judith anavyogombana na baba mkwe wake kwa sababu ya kumwita mchungaji na kumwombea mtoto wake. Dini inamfanya Judith aonekane mchawi na achukiwe na baba mkwe wake. Vilevile wakati Masumbuko alipokuwa anasumbuliwa na majini ya Waufi, Judith aliendа kumwita Mchungaji lakini Masumbuko hakupenda. Mwandishi kupitia mhusika Judith anaonyesha jinsi hizi dini za kigeni zilivyoleta migogoro katika familia mpaka kusababisha ndoa ya Masumbuko kuvunjika. Pia mwandishi anaonyesha jinsi swala la dini lilivyoleta mgogoro mkubwa kati ya Judith na baba mkwe wake mpaka baba huyo akawa hawasiliani na mkwe wake kwa sababu hampendi kwa ajili ya tofauti za kidini.

Hali kadhalika mwandishi anachimuza dhamira ya uvumilivu pamoja na kwamba, baba mkwe wake alikuwa akimtukana lakini hakuacha kumheshimu na kumpenda baba mkwe huyo. Mzee Kikoko alikuwa hataki hata kidogo kumsemesha Judith lakini baada ya kwenda bafuni na kumkuta mwanaye Masumbuko aliyekwenda kuoga hayupo, ndipo akaamua kwa hasira kumuuliza mkwewe Judith, Judith anaitika kwa nidhamu kwa baba mkwe wake; hakujali kama alimtukana kwa kumwambia atoke nje ya nyumba na aachane na mwanaye. Kwa hivyo ugonjwa huo wa majini aliyokuwa nao Masumbuko unapelekea migogoro hiyo yote kati ya Jidith na mkwewe.

### 4.3.3 Uchimuzi wa Dhamira kwa Mkabala wa Wahusika wa Kijiniuchawi na Ushirikina katika Riwaya ya *Tanzia*

*Tanzia* ni riwaya ambayo kwa kiasi kikubwa imetawaliwa na matukio ya kichawi na kishirikiana kiasi cha kuogofya. Mwingizi amewasawiri na kuwatumia wahusika mseto katika kuchimuza dhamira mbalimbali mseto katika riwaya hii. Wahusika wake wamebebeshwa dhamira changamano kama utata wa ujitambuzi wa kisaikolojia,

uongozi na uwajibikaji, ufahamu na ujitambuzi wa kijamii, ufasiri mbadala wa maswala ya maingiliano ya kijamii, utekelezaji wa majukumu katika nyadhifa mbalimbali, maadili katika mitagusana na maingiliano ya kijamii, mifumo ya kiutawala, usaliti, uwajibikaji, mafao binafsi, haki na sheria. Pia katika riwaya hii kumekuwa na wahusika wa kiuhalisia na wahusika wa kiuhalisiamazingaombwe kwani matukio mengi yamekuwa yakitendwa na wahusika wakati wanapolala, mtu anakuwa yumo ndotoni na matukio mengine yakitendwa katika ulimwengu wa kawaida. Wahusika hawa wamekuwa wakichimuza maudhui mbalimbali yanayogusa jamii.

Lakini, kabla ya kulizamia swala la uchimuzi wa dhamira na maudhui katika riwaya hii, kuna haja ya kuibua mjadala wa kijumla kuhusiana na nafasi, uamili, utumiaji na ushirikishwaji wa ndoto, uchawi na imani za mizungu katika tungo na bunilizi za uhalisiajabu. Kimsingi, mambo haya yanatumikizwa kama mkakati wa kufanya uhalisiajabu kutambulika kama usimulizi kinyume au usimulizi mbadala wa kuangazia mifumo ya kijamii inayojumuisha mifumo ya kiutawala kama vile ukoloni, ukoloni-mamboleo na mifumo ya kiutawala baada ya ukoloni katika mataifa mengi barani Afrika. Kwa hivyo, uajabu, uchawi na umizungu wote unatokea katika uhalisiajabu kama ilivyo katika *Tanzia* na ni mfumo fungamani wa kiuandishi unaokwenda kinyume na misimamo rasmi ya kufafanua, kueleza na kufasiri mambo, matukio na tajriba za ki binadamu katika harakati za kila siku. Ni mfumo unaojaribu kuziba mianya ya uhalisi wa maisha, mianya ya kihistoria, mianya ya kimtazamo kuhusiana na tajriba mseto za binadamu.

Uwepo wa mambo ya kiajabu kama vile wahazigi, ndoto, safari za ruya na matekelezo ya kinjozi hutekeleza majukumu ya kujaliza tajriba za ki binafsi katika fasiri rasmi za mambo. Watunzi wa fasihi ya kihalisiajabu, kama alivyo Maundu Mwingizi, huasi dhidi ya uwepo wa uhalisia mmoja kwa kila mtu katika jamii au ufasiri mmoja au ufasiri rasmi wa matukio, badala yake watunzi hawa huhiari kuvunja na kuvuka mipaka ya ufahamu wa yaliyopita, yaliyopo na pengine yajayo katika maingiliano na mitagusano ya ki binadamu. Kwa sababu ya kupania kutekeleza majukumu haya, watunzi hawa wa

uhalisiajabu huakisi katika tungo zao tamaduni na imani za kichawi na mizungu, huakisi uwezekano wa mambo na matukio ya kinjozi kusawiana na matendo na matukio ya uhalisiani, huakisi mifumo ya kijamii inayokwenda kinyume na taratibu za kitawala au kiserikali.

Uhalisiajabu, inaweza kudaiwa unaibuka katika misingi ya uwepo wa utohakika, misingi ya kutilia shaka kama mambo ndivyo yalivyo kwa kweli.  Kwa hivyo, utohakika wa ni nini kilicho sahihi na nini si sahihi katika jamii mara nyingi huchochea kuibuka kwa miungano, imani na dini bandia zinazoahidi mafao ambayo ni nadra kutolewa na watawala kama vile kukata minyororo ya umasikini, kuingia katika utajiri, kujenga uthaBiti juu ya mambo mengi na kukuza uwezo wa kufanikiwa katika kila jambo. Kwa hivyo, ushirikishwaji wa uchawi na mizungu katika tungo za kihalisiajabu huwezesha kutolewa kwa maelezo na fasiri za jamii zilizo na rusu na safu nyingi.

Uchawi na mizungu katika tungo za kihalisiajabu, kama ilivyo katika riwaya teuleza Mwingizi, ni mkakati unaowasilisha ufahamu na ujitambuzi wa ki binafsi na kijamii. Hii inatokana na ufahamu kwamba uchawi na mizungu huashiria uwepo wa nguvu na ushawishi wa kichawi na kiajabu ulio nje ya udhibiti wa uwezo wa ki binadamu kama vile, uwezo wa uchawi kuibua hofu na kitete na zaidi kuibua vitisho na hatari dhidi ya taratibu na mipangilio rasmi ya kijamii. Wachawi, warogi na wanga mara nyingi wanahusishwa na nuksi kama vile kusababisha utokeaji wa njaa, kiangazi, magonjwa, miduwazo, mafarakano na mivutano katika familia, koo na jamii; kwa jumla mambo yanayotibua na kuboronga taratibu za kijamii, na huwa yanakubalika kwa urahisi kuliko mambo yanayotegemea ithibati za kisayansi. Kwa misingi hii, wachawi wanawasilisha kikundi cha kijamii kinachotambuliwa lakini kinachopembezwa na kutengwa na ilhali uwepo wa kikundi hiki hauonekaniki. Kama ilivyo katika riwaya za jadi, katika tungo za kiuhalisiajabu yapo pia mahusiano kati ya uchawi na nuksani, hali inayofanya motifu ya uchawi—uwe chanya au hasi—kupatikana katika aina zote hizi za utunzi.

Utumiaji wa uchawi, mizungu na uajabu katika bunilizi za kijadi au za kimajaribio ni mbinu zilizotumika kwa muda mrefu kuonyesha kwamba mambo haya ni kimbilio pale ambapo wanajamii wanahisi uwepo wa ukosefu wa usalama, ukosefu wa umadhubuti wa miundo ya kijamii, uwepo wa hatari zinazoeleweka na zisizoeleweka na uwepo wa shaka na hofu katika maisha ya binadamu. Katika hali kama hizo, uchawi na mizungu huwasilishwa kwa njia chanya na wakati mwingine njia hasi—kama vile wachawi kuchukuliwa kuwa na uwezo wa kuua au kudhuru watu, kuua mifugo, kuwafanya watu kuwa wazimu, kuharibu mimea/mazao shambani, kuchochea vimbunga, kuamsha ashiki isipostahili, kuleta ugumba na maovu mengine mengi.

Kwa hivyo, wachawi wanawasilishwa kama watu majasiri wanaokwenda kinyume na kaida na maadili ya jadi na yaliyozoeleka kama vile ustaarabu na uungwana na badala yake kujitosa kufurahia, kushangilia na kusherehekea maovu, kushiriki kihalisi katika umwagikaji wa damu ya binadamu kwa njia za kafara na mauaji na vilevile kujishughulisha na uchafu wa aina nyingi kama njia mbadala za kukabiliana na uhalisi wa maisha. Woga ambao watu huwa nao kuhusu wachawi unatokana na imani kwamba, wachawi wana nguvu asilia za kimaumbile za kuweza kudhuru, kutumia sumu, nuio na tabano[11], miti shamba na vitu vingine vingi wanavyoweza kuuhusishwa na uchawi au vinavyochukuliwa kuwa vya kichawi. Katika jamii nyingi unaweza kutabakishwa matapo mawili ya kimsingi; uchawi hasi, ule unaodhuru na unaohusishwa na wanawake ilhali uganga—unaotazamwa uchawi chanya—unahusishwa na wanaume. Kwa njia hii, uchawi unaweza kuangaliwa kama utaratibu wa kuitabakisha jamii kwa misingi ya kijinsia. Vilevile uchawi unaweza kuangaliwa kwa njia chanya kama utabakishaji mpya wa kijamii.

Kuna uwezekano kwamba, uchawi na urogi ukaangaliwa kwa mitazamo chanya na baadhi ya watu katika jamii na kwa hivyo kuchukuliwa kuwa kinga na utaratibu wa kulatamia. Kwa sababu hii inawezekana kuhoji kwamba wakati mwingine watunzi wanaushirikisha uchawi katika kazi zao kwa nia ya kupendekeza kutambuliwa na

11 Tabano ni maneno maalumu yanayosemwa ili kumtakia mgonjwa nafuu katika uganga wa jadi

kukubaliwa kwa makundi yaliyotengwa kijamii na wakati huo huo kupindua taratibu tawala zinazokubalika kijamii. Kwa kuyapa sauti makundi yasiyokuwa na sauti au fursa ya kutoa sauti katika jamii, makundi yaliyopembezwa na kutengwa kutoka kwa mifumo tawala ya kijamii. Makundi yanayohusishwa na uchawi yanapata fursa ya kudhihirisha ukweli wao kwa njia huru badala ya kuhukumiwa kwa misingi ya vitendo, imani na maadili yao hasa kutokana na mitazamo ya nje.

Uchawi unaweza kuangaliwa kama mbinu na mkakati wa kuilinda nafsi ya mtu binafsi, kuikinga jamii kutokana na vitisho vya aina nyingi, kuwalinda marafiki na hata kuilinda familia, hii ni hali inayokwenda kinyume na imani zilizoko kwamba, wachawi ni wauaji wa watoto, waasi wa jamii, na wazinzi. Katika riwaya hii ya kihalisiajabu ya *Tanzia*, inawezekana kuhoji kwamba Mwingizi anajaribu kuwasilisha ukweli kinzani ambapo kwa upande mmoja anawasilisha usawiri wa wachawi kama usawiri wa wanawake waovu, wauaji na wapinga maendeleo. Na upande mwingine upo uwezekano kwamba mtunzi anaendeleza pasina kujua chukulizi potovu kumhusu mwanamke—chukulizi za uasi, uzembe, ukahaba na uzinzi. Hii inadhihirika katika riwaya hii ikizingatiwa kwamba, wapo wanawake wachawi wanaopenda uchawi na wengine wasiopenda. Vilevile, katika riwaya hii uchawi umeenea na kusambaa pote, uchawi ni kisabaBishi cha matukio mengi na vilevile uchawi ndio tiba. Mtunzi kupitia riwaya hii ya kiuhalisiajabu, ameonyesha jinsi usawiri wa wahusika unavyokiuka mipaka ya kirazini, kiwakati na kipahali na kuwafanya wahusika hao kuwa na majukumu mseto yanayoweza kudhiBitiwa kihalisi na majukumu yanayoweza kufikiriwa kuwa katika upeo wa uwezekano.

**4.4.3.1 Maadili, Uongozi, Ukatili, Uwajibikaji na Mahusiano ya Kikazi**

Mtunzi kupitia riwaya hii ya kiuhalisiajabu, ameonyesha jinsi usawiri wa wahusika unavyokiuka mipaka ya kirazini, kiwakati na kipahali na kuwafanya wahusika hao kuwa na majukumu mseto yanayoweza kudhibitiwa kihalisi na majukumu yanayoweza kufikiriwa kuwa katika upeo wa uwezekano. Mtunzi ameonyesha jinsi matukio ya kiuhalisiajabu, kupitia mhusika Bi Masonganya Binti Kalukalange, yalivyo na uwezo

wa kukiuka mipaka kati ya ukale na usasa, ustaarabu na ushenzi, uhalisia na ndoto. Kwa kumtumia mhusika huyu Bi Masonganya Binti Kalukalange, mtunzi ameweza kuchimuza na kuibua maudhui ya imani za watu juu ya mihimili ya mduara wa maisha, kwamba watu wenye heshima zao wanawatumainia waganga wa jadi katika maisha yao ya kazini, katika maisha yao ya kifamilia na kijamii, katika hatamu na harakati zao za uongozi na katika mahusiano yao ya kila siku hususan na viongozi serikalini.

Mtunzi kupitia Bi Masonganya Binti Kalukalange anawapa somo na tafakuri wasomaji wake juu ya taratibu na ada za uchawi na madhara yake kwa jamii. Watu binafsi, familia na jamii nzima kwa jumla inaingia hofu kwani uchawi unatishia mihimili, nguzo na taratibu za uhai wa wanajamii na unarudisha nyuma maendeleo. Uchawi unakuwa kikwazo, kipingamizi na kizingiti kinachozuia fikira razini za kimahusiano na kimaendeleo. Kupitia Bi Masonganya Binti Kalukalange, mfumo mzima wa tiba chanya na bandia pamoja na ulozi unafafanuliwa. Elimu anayoitoa mtunzi ni kielelezo cha kutafuta suluhisho, kwanza kuwawezesha masikini kuzitambua hali zao, kuzifafanua hali na kuelewa vyanzo vya hali hizo. Pili, kuangaziwa kwa uchawi, imani za kichawi, taratibu za mizungu na ulozi ni hatua ya kijasiri katika kulikabili jambo ambalo waandishi wengi wanalikwepa.

Mtunzi kupitias uhalisiajabu anafanikiwa kuwakaribisha wasomaji wake katika kiini cha elimu hiyo huku akiwawezesha kujenga tafakuri na ujasiri wa kudadisi nafasi, uamili, na uwezo wa uchawi katika kushawishi na kuelekeza matekelezo ya kimaendeleo katika daraja za watu binafsi, familia, jamii na taifa. Mtunzi habanwi na haja ya kutoa uhakikisho wa yale anayoyasimulia bali kwa kutumia leseni ya ubunifu wa kifasihi anayaweka wazi mambo yanayotisha, ukatili, unyama, na imani ambazo zimekuwepokwa njia ya mbano katika vichwa vya wasomaji wake kwa muda mrefu lakini zikakosa ujasiri wa kuzianika peupe. Imani ya uchawi si ngeni na bado uchawi ni mfumo wa fikira mbadala ulio na mashiko, ushawishi na utegemezi kwa mambo mengi ya ki binafsi, kifamilia na hata kijamii. Ni kwa njia ya kumuangamiza Bi Masonganya ambapo mtunzi anawapa matumaini wasomaji wake juu ya kuanguka kwa mfumo huo.

Anawatoa hofu ya uwezekeno wa kuliondoa tatizo la ushirikina na ulozi katika jamii yake.

Aidha, mtunzi kupitia Bibi huyu, anachimuza ujumbe wa jinsi wananchi wanavyokerwa na baadhi ya viongozi kukaa madarakani kwa muda mrefu huku wakiwatesa wananchi. Hii inasawiriwa na ukweli kwamba, kifo na ufu wa Bibi huyu pamoja na mtandao wa mambo yote anayoyasimamia au kuyawakilisha, yanasubiriwa kwa muda mrefu, hata juhudi za kutaka kumuua zinatatizwa kwa njia nyingi. Hii ni sawia na hali ya viongozi kusalia mamlakani miaka nenda miaka rudi hadi inafika mahali wananchi wanaamua kuwaua au kuwafukuza ikulu kama ilivyokuwa kwa raisi wa Ivory Coast (Laurent Gbagbo) ambaye alikaa muda mrefu mamlakani na alikuwa ni katili na mnyonyaji. Kwa hiyo, wananchi wakaandamana mpaka ikulu kwenda kumfukuza kutokana na kuchoshwa na utawala wake mbovu.

Vilevile mwandishi kupitia Bibi huyu, anachimuza dhamira ya ung’ang’aniaji wa madaraka kwa wale viongozi wanaokuwa wamezeeka lakini wanakuwa bado wanataka kuongoza. Kupitia Bibi huyu mtunzi anaonyesha jinsi viongozi hawa wanapokuwa wazee inafika mahali hawawezi kufanya kitu ndipo wanapoamua kutafuta mtu yule ambaye anaweza akatunza siri zao na akaendelea na yeye pia kuongoza kwa kutumia taratibu za kiongozi aliyepita. Viongozi wa aina hii wapo sana katika mataifa ya Afrika wanakaa madarakani mpaka umri wa uzee unawakuta wakiwa madarakani na huona hakuna mtu anayeweza kuwatoa, sababu ya kung’ang’ania mamlakani ni kutokana na kwamba wakati mwingine wanakuwa wanawanyanyasa sana wananchi kwa ajili ya kujilimbikizia mali ndio maana wanaona wakiondoka watakosa kinga.

Halikadhalika, kupitia Bibi huyu mtunzi anamsawiri jinsi alivyokuwa na roho ya udikteta au ukatili kwani yeye kumuua mtu kwa njia ya uchawi ni kitu cha kawaida. Ilikuwa mtu akimkosea kidogo asipokwenda kuomba radhi alikuwa anamuua. Au ilikuwa mtu akihitilafiana na ndugu zake alikuwa anauliwa. Hali hii ilitokea pale ambapo mjukuu wa huyu Bibi alikuwa na kesi ya kubaka alimbaka

mwanafunzi, lakini kesi hii ilipotea kutokana na kwamba waendesha kesi wote, Bibi huyu aliwaua. Miongoni mwao ni mahakimu wawili na Binti mwenyewe aliyebakwa aliuawa kichawi. Kwa hiyo mwandishi kupitia kwa usawiri wa Bibi huyu anachimuza dhamira ya makuzi mabaya kwani anaonekana ni Bibi ambaye anakumbatia maovu sana kwa wajukuu zake kwa kuonyesha wazi kwamba kosa alilolifanya Ndosa yeye anaona ni la kawaida kutokana na jinsi alivyomlea toka akiwa mdogo katika makuzi mabaya. Kutokana na malezi hayo mabaya ndio maana anaamua kumkingia kifua Ndosa kwa kuhakikisha anawaua wale wote wanaohusika na kesi yake hiyo ya kubaka.

Kwa upande mwingine, kitendo cha kuwauwa kwa makusudi watu wasio na hatia alichokuwa akikifanya Bibi huyu ni kielelzo cha dhamira ya ubinafsi na uonevu kwa baadhi ya watu katika jamii. Mfano mzuri kuna baadhi ya viongozi katika jamii huwauwa watu kwa ajili ya maslahi yao binafsi ya kutaka kupata nafasi za uongozi katika sehemu mbalimbali hususani katika siasa. Mauaji ya *Albino* na vikongwe nchini Tanzania kwa visingizio vya ushirikina havina mantiki yoyote. Kwani wanasiasa wengi katika kuzilinda nafasi zao serikalini katika mataifa ya Afrika wamekuwa wakiwauwa baadhi ya wapinzani wao au watu wanaoleta vizuizi ambavyo vitawafanya wasibaki mamlakani. Wanasiasa hawa hutumia hata mbinu ya kuuwa ili waendele kubaki mamlakani na ambao wanaotaka kuingia pia hutumia mbinu hiyohiyo ya mauaji pale wanapoona wanapata vikwamizi. Dhamira ya kurithishana mifumo kandamizi pia inajitokeza.

Aidha, wakati mwingine mtunzi kupitia mama huyu anachimuza dhamira ya migongano ya kimaslahi katika mataifa yanayoendelea na mataifa yaliyoendelea. Kwani mataifa yaliyoendelea wakati mwingine hutumia mauaji kwa kusababisha migogoro katika mataifa ya Afrika kwa lengo la wao kunufaika, ndio maana panatokea vita katika mataifa yanayoendelea wakati mwingine wao huwa ndio watoaji wa huduma katika mapigano hayo. Wakati mwingine husababisha migogoro hii kwa ajili ya maslahi yao binafsi. Mfano mzuri nchini Libya mataifa yaliyoendelea yalihakikisha yanafanya juu

chini Rais Gaddafi na wanaomuunga mkono wanakufa ili waweze kunufaika na malighafi ya mafuta inayopatikana Libya.

Vilevile mtunzi kupitia mama huyu anachimuza dhamira ya uwajibikaji wa watu binafsi na uwajibikaji wa kitaasisi katika maswala mbali mbali kuzorota kutokana na vizuizi mbalimbali. Anaonyesha jinsi taasisi kama serikali kupitia majaji wake wanavyoshindwa kuiendesha kesi kutokana na kulogwa na upande wa mtuhumiwa. Pia shahidi aliyebakwa na yeye anakufa kwa kulogwa. Hapa kuna utata wa sababu zilizopelekea kufa kwa mashahidi na majaji. Je, ni kweli watu wanakufa kwa sababu ya nguvu za kishirikina? Swali hilo ni la msingi kwa wasomaji wa Mwingizi. Iwapo mifumo ya kitaasisi inaingiliwa na imani za kishirikina na kushindwa kufanya kazi yake, ni kwamba kuna kushindwa kwa mihimili ya utafutaji haki katika jamii. Hali hiyo ikiruhusiwa kuwepo katika jamii, ni kwa vipi jamii hiyo itaendelea na kupata ustawi?Je ni nani wa kulaumiwa iwapo akina Bi Masonganya wanakuwa juu ya sheria na wanaogopewa na hata viongozi wa siasa? Viongozi wa serikali wanapokwenda kuomba msaada kutoka kwa watu kama Bi Masonganya:

> Hata uwe na kesi ya namna gani endapo utamfuata kumtaka msaada, naye akaamua kuivalia njuga kesi hiyo basi piga geuza utashinda tu. Mpaka viongozi wakubwa serikalini wanaouhusudu ushirikina huwasili kwa Bi Masonyanya kufanyiwa *ndumba* (uk.3).

Swala la Bi Masonganya kuua sio tu majaji bali mashahidi na mlalamishi katika kesi na kwa njia hii kuonekana kuushinda mkondo wa sheria, ni swala tata kulielewa. Haijulikani kama mtunzi kupitia Bibi Masonganya anaikejeli mifumo ya kitaasisi hususan mifumo ya kisheria, au kama mtunzi anachimuza udhaifu wa mifumo ya utawala katika jamii nyingi za kiafrika. Isipokuwa labda ichukuliwe kwamba Bi Masonganya anajistarehesha na shamrashamra za mauaji kwa sababu anaweza. La sivyo, wingi huu wa vifo kwa sababu za kichawi, hauelekei kuwa na maana. Msomaji anaachwa kujiuliza kwa nini vifo vingi kiasi hiki? Karibu katika kila sekta za uchumi na za kijamii, ushirikina na uchawi vinatawala fikra na matendo ya wanajamii.

Kwa mintarafu hii, mtunzi anaonyesha uibukaji wa taratibu mbadala za kukabiliana na uhalisi wa maisha pale palipo na taratibu maalum na zilizozoeleka baada ya kuona njia rasmi haiwezi kukidhi matakwa ya masikini kwa hivyo wanaona ni heri kutumia njia nyingine isiyo rasmi. Kwa hiyo, nyazifa mbalimbali za uongozi huwafanya baadhi ya viongozi kuamua kutumia njia ambayo si rasmi katika kuhakikisha wanapata au wanalinda nafasi zao mamlakani. Vilevile kuwatumaini hawa waganga wa jadi kunatokana na mifumo iliyopo ya ushindani katika nyazifa mbalimbali.Si rahisi kuziondoa fikra za kichawi na kishirikina katika jamii iliyodumisha mfumo huowa kufikiri, kufasiri na kutenda mambokwa muda mrefu. Kitendo cha kutaka kumuua Bibi Masonganya kinaweza kutafsiriwa kuwa ni jitihada za muda mrefu za wanajamii waliochoshwa na tabia zinakwamisha na kudumaza maisha yao.

Mtunzi anaonyesha kushindwa Bi Masonganya kufa moja kwa moja kutokana na kumeza dawa ya kurefusha maisha ni ishara kwamba wenye mifumo hiyo hujiwekea kinga na kufanya jitihada za kuhakikisha mfumo unaowasaidia hauondoki kwa urahisi. Kitendo cha kutaka kumtapisha ni sawa na jitihada za kuleta mapinduzi ya kiafrika na kitabia. Mifumo hiyo inarithishwa kizazi hadi kizazi kwa hiyo Bi Masonganya alishamrithisha mjukuu wake Kaguba. Kitendo cha kurithishana uchawi ni kitendo cha kidikteta na swala mtambuko katika medani za kisiasa ambapo viongozi wengi wa Afrika hung’ang’ania madaraka hadi pale wanapoondelewa kwa nguvu. Mfumo dhalimu hauwezi kuondoka kwa njia za rahisi. Hakuna budi watu kujitolea mhanga, hivyo kifo cha Masonganya ni mfano wa wanamapinduzi wanaojitoa muhanga.

Fauka ya maudhui yote hayo yaliyochimuzwa kupitia kwa Bibi Masonganya kwa upande mwingine tunamuona mtunzi amekuwa akionyesha nafasi hasi kwa kiasi kikubwa kwa mwanamke kwani katika riwaya hii  wachawi wote ni wanawake na wanaume wamechorwa kama waganga wa kuwakamata hao wachawi. Kwa hiyo, mtunzi anachimuza dhamira ya kumdunisha mwanamke kila mahali yaani kuona kwamba mwanamke amekuwa ni chanzo cha maovu mengi kila mahali kama ilivyo kwa Bi Masonganya ambaye ni mchawi anauwa watu. Bi Kibena alikuwa mchawi na Binti

Sambayu alikuwa mchawi pia. Na ukijaribu kuangalia wachawi hawa wanawake wote ni viongozi katika himaya hizo za kichawi. Hivyo basi, katika riwaya hii ya *Tanzia* nafasi ya mwanamke imechorwa hasi na mwanamume chanya.

**4.4.3.2 Uongozi wa Kiimla na Usaliti**

Riwaya za kimajaribio huwa na maswala ya kifantansia, huwa na hali za kuvunjwa kwa mipaka kati ya jambo moja la kihalisia na kuibushwa kwake kwa hali nyingine isiyo ya kawaida; kama vile katika hali ya kawaida tusingetegemea mtoto wa miaka minne kuwa kiongozi wa wachawi na kurithishwa uongozi wa kichawi na Bibi yake. Pia mtoto mdogo kuzungumza kwa mama yake mambo ya kichawi ambayo katika hali ya kawaida hayawezekani, lakini mtunzi amemsawiri na amemtumia mhusika Kaguba kuchimuza dhamira mbalimbali kupitia uhusika wake wa kichawi. Kaguba huyu ni mjukuu wa Bibi Masonganya ambaye alimrithisha uchawi ili akifa aweze kuendeleza uchawi huo. Mtoto huyu ni mdogo sana wa miaka lakini mwandishi amemsawiri na kumpa wasifu na hulka iliyopita umri wake na amemtumia kuchimuza maudhui mbalimbali. Mtoto huyu anamkanya mama yake mzazi kwa kitendo alichokifanya na ndugu zake kwa kumtumia Nyanzala mtoto wa mwisho wa Masonyanya kumuuwa mama yake kwa kuchomeka mwichi karibu na kitanda alipolala baada ya kushauriwa na mganga wa jadi wafanye hivyo. Kaguba anasema:-

> “Mama ujue mi’ n’namuonea huruma sana ma’mdogo Nyanzala,” Kaguba alisema kwa sauti kiasi cha kufanya kikao kipige kimya kidogo huku watu wote wakimuangalia kama kituko vile kwa ile kauli yake aliyoitoa baada ya kuona mama yake hamjibu chochote. Wakajikuta wote wamecheka! uk. 13.

Mtunzi kupitia maelezo ya Kaguba na kupitia tukio la Nyanzala la kumuuwa mama yake, anachimuza dhamira ya tamaa ya watu kuhiari kuua kama ishara ya mageuzi ya ghafla kwa kuchoshwa na uhalisi wa hali iliyopo katika maisha ya mtu binafsi, katika familia mahususi, katika ukoo, jamii au serikali iliyopo mamlakani. Kwa njia hii inawezekana kuhoji kwamba mtunzi anayawasilisha mauaji ya kichawi kama suluhisho, hususan pale ambapo kunaonekana kuna sababu ya kushawishi mauaji hayo. Matatizo kama haya ya imani za kichawi, taratibu na mifumo ya fikira za kichawi yapo sana katika mataifa ya Afrika kwani watu hufikia mahali mpaka kuamua kuwauwa wanao,

jamaa zao au hata pale inapowezekana hata viongozi waowalioko mamlakani kwa sababu huona hakuna njia nyingine mbadala zaidi ya kuuwa ili waweze kuondokana na hali zinazowatanza hata haja ya kumweka madarakani kiongozi wanayemtaka. Ndivyo wanafamilia hawa walivyofanya kumuua Bi Masonyanya na yote aliyoyawakilisha katika jamii yake.

Kwa upande mwingine si jambo la kawaida kwa mtoto mdogo kuongea maneno mazito kama haya, hili ni jambo la ajabu. Lakini mtunzi ametumia uyumbishwaji wa urazini kwa kumkweza kimawazo na kimaadili mtoto huyu kuonyesha kwamba japokuwa kiongozi wa utawala kandamizi, Masonganya, wanajamii wamefanikiwa kumuua lakini mtoto huyu anaendelea kutumika kama miongoni mwa wafuasi wa Bibi huyu ambao wanaendelea kuwanyanyasa wananchi. Kwa usemi mwingine, kuiondoa mifumo ya fikira, imani za kichawi na kishirikina, mitazamo ya ulimwengu, taratibu za kimahusiano na mifumo mbadala ya ufafanuzi na ufasiri wa mambo si hatua ya mara moja, ni mchakato wa siku nyingi, tena kwa tahadhari kwamba mambo haya yamekita mizizi na visalia vipo. Hii ndio maana Kaguba anaendelea kumwambia mama yake kwamba usiku kucha hajalala kwani wachawi wote walikuja kumpitia lakini alishindwa kutoka kwa sababu ya dawa iliyowekwa mlangoni na Babu Gao. Na kabla mama yake hajamjibu akamwambia mama yake kwa majivuno akisema kwamba "…unajua mi' nd'o mkubwa wao tangu mlipomuua Bibi maana alishanikabidhi vitunga vyake vyote vya uchawi. Mama mi' mwenziyo ni bosi we' nidharau tuu" (uk. 35).

Kaguba anawakilisha viongozi visalia ambao fikra, mienendo, wasifu na hulka zao huwa zimekwama katika taratibu na mifumo iliyopitwa na wakati au iliyopinduliwa, wana majivuno nje ya mipaka ya uhalisia wao, au wanakuwa watu wenye majivuno ambao na hupenda kuonekana kila mahali kuwa ni viongozi na ilhali siku zao zimepita. Pia mwandishi ameonyesha wachawi wenziwe na Kaguba wakimuomba wamkate Nyanzala ulimi kwani toka wamemchukua duniani hawakumkata ulimi lakini Kaguba anakataa wasimkate ulimi mpaka atakapokuwepo mwenyewe. Mhusika Kaguba anawakilisha viongozi ambao hawagawi madaraka kwa wenzao yaani wamebeba

madaraka yote wenyewe.  Kwa hiyo hata kama amesafiri hakuna kitu kitakachoendelea mpaka arudi, kitu ambacho si kizuri kwani inachangia kurudisha maendeleo nyuma. Kwa sababu kazi nyingi hazitaweza kufanyika bila kiongozi mkuu kuwepo. UlimBikizaji wa madaraka unasababisha utendaji kazi kutokuwa na ufanisi kwa sababu ni chanzo cha umangimeza katika jamii.

Vilevile Kaguba akiwa na Binti Sambayu usiku baada ya Binti Sambayu kuja kumwambia kwamba wachawi wenzio wana shida. Kwa hiyo alikuwa anamwomba aende akasikilize shida zao, ndipo Kaguba anasema:-

> "Watangazie wachawi wote kuwa Jumatano nitatoka na nitakuja kusikiliza shida za kila mtu, nadhani msiba utamilizika siku ya Jumanne hivyo mpaka kufikia Jumatano nitakuwa nimepata nafasi ya kukichimbua hicho Kibuyu…ila kwa sasa msiruke umbali mrefu, muishie mikoa ya jirani tu…nawatakia uwangaji mwema." Kaguba alimuaga Binti Sambayu (uk 37).

Mwandishi kupitia mtoto Kaguba, anaonyesha ni kwa kiasi gani anawajali watu wake anaowaongoza kwa kuwaambia wawe wavumilivu ataenda kusikiliza shida zao. Kaguba anachimuza dhamira ya uongozi bora kwa kuwajali wananchi. Hivyo, kiongozi yoyote anapaswa kuwajali wananchi wake. Hata kama ana shida au matatizo anatakiwa aweke kipaumbele kwa wananchi wake. Ndivyo ilivyo hata katika ngazi ya familia baba anatakiwa kuijali familia yake katika kuhakikisha wanapata mahitaji yote ya msingi. Lakini kwa upande wa mataifa yetu ya ulimwengu wa tatu imekuwa ni tofauti, marais wako madarakani kwa ajili ya maslahi yao  binafsi hawana muda wa kujali wananchi wao wapo ili mradi washibishe matumbo yao.

Aidha Mzee Mtandi, kaka yake marehemu, anabaini kwamba kila siku usiku Binti Sambayu anakuja kiuchawi kuongea na Kaguba. Kuna siku aliwasikia wakiongea kuhusu majani ya vimbusi yanayoua watu na yapo chumbani alipokuwa analala Masonganya na sasa wapo ndugu zake waliokuja kwenye msiba wanalala tena huko chumbani kwa hiyo anashindwa kuyatoa ili awauwe ndugu zake.  Hivyo basi, Mzee Mtandi aliposikia aliamua kesho yake kuitisha kikao cha ndugu zake na kwenda

kuyatafuta hayo majani ili wajikinge. Kwa bahati mbaya wakati wanajadiliana kulikuwa na paka aliyekuwepo hapo na wao hawakuwahi kuhisi chochote kama paka huyo ni Kaguba anayejibadilisha ili aweze kusikia njama zao na kuweza kuwangamiza. Wakapanga mipango ya kuwangamiza wachawi wasijue yule paka atakwenda nje kumwambia Kaguba. Paka yule alitoka haraka nje na kwenda kumwambia Kaguba aliyekuwa anacheza na wenziwe nje juu ya njama za Mzee Mtandi na ndugu zake.

Mwandishi kupitia Kaguba, anachimuza ujumbe wa jinsi viongozi au watu wanavyokuwa wasaliti katika mambo mbalimbali. Mnaweza mkakaa mkajadiliana kitu fulani mwisho wa siku kitu hicho mnakuta tayari adui zenu wanajua au watu ambao hawakutakiwa kujua wanajua kupitia baadhi ya viongozi au watu mliokuwa nao kwenye kikao. Mfano mzuri ni katika yale mataifa ambayo kila siku huwa na vita. Viongozi baadhi wanakuwa wanatoa siri za vikao kwa maadui zao, huwa wapo kwa maslahi yao binafsi na kusababisha wenzao kuteketea.

**4.4.3.3 Unafiki na Ukoloni Mamboleo**

Riwaya teule za Mwingizi zimeweza kuangazia mambo ambayo katika ulimwengu wa kawaida ni vigumu kuyaamini kutokana na riwaya hizi kuwa za kimajaribio na kusheheni mambo ya kiuhalisiajabu kama nadharia ya uhalisiajabu isemavyo. Kwani tunaona mipaka katika mahusiano kati ya binadamu na wanyama inayumbishwa ili kuwezesha kutangamana kwa binadamu na wanyama hasa katika maingiliano ya ubadilishanaji mawazo, katika kuwezesha wanyama kuzipata fikra za binadamu na binadamu kuwatuhumu wanyama kwa kuhusika katika mambo ya ki binadamu. Tunaona riwaya hii ya *Tanzia* imeweza kumtumia mhusika paka katika kufikisha ujumbe wa kuitahadharisha jamii.

Mhusika paka aliyekuwa anayeishi nyumbani kwa Bi. Masonganya anajukumishwa kutekeleza majukumu mbalimbali na katika utekelezaji wa majukumu hayo anawezeshwa kuchimuza maudhui ya aina mbalimbali. Japo watu wote walikuwa wanajua ni paka wa kweli, kumbe paka. Alikuwa paka -mtu ambaye Bibi huyu

alikuwa anamtumia katika maswala yake ya uchawi. Baada ya Bibi Masonganya kufa paka huyu alibaki nyumbani. Kwa hivyo wanandugu walipokuwa wanakaa vikao wanajua ni mnyama kumbe siyo mnyama. Paka huyu alikuwa anaendelea na uchawi kwa kutoa taarifa ya mambo yaliyokuwa yanaendelea katika nyumba ile iliyokuwa imegubikwa na swala zima la uchawi. Paka huyu ndiye aliyepeleka taarifa kwa Kaguba kuwa Mzee Mtandi alisikia walipokuwa wanaongea na Binti Sambayu jinsi ya kutumia vimbusi ili kuhakikisha wanawateketeza wachawi wote na pia na wao wasidhurike. Mwandishi kupitia paka huyu, kwanza anaakisi uhalisi wa imani zilizoko katika jamii hasa kuhusiana na mahusiano yaliyoko kati ya wachawi na wanyama, hususan paka na fisi ambao wanatumikishwa na wachawi.

Pili, mwandishi anahuisha imani hizi katika maandishi na kwa hivyo, kuhoji kwamba, licha ya mambo haya kubanwa katika vikao vya kawaida vya mazungumzo, uwepo wa imani hizo bado ungalipo. Tatu, kwa kumtumia paka mtunzianachimuza dhamiramseto kama vileuwezekano wa kuishi na adui yako lakini usimjue kwani siku zote binadamu ni wabaya sana kama wanyama tu. Paka huyu walikuwa wanaishi naye kama mnyama kumbe si mnyama yupo kwa ajili ya kutoa siri na kuzipeleka kwa wachawi wenzie.

Nne, katika kiwango cha taswira, paka huyu ni masalia ya mfumo uliopita, mfumo ulioendelezwa na Bi Masonyanya na wafuasi wake, sawia na kuondolewa kwa mfumo wa ukoloni lakini bado kukawa na masalia ya fikra na taratibu za utenda kazi, au kuondolewa kwa mfumofulani wa kiserikali lakini bado kukawa na masalia hasa ya wale walionufaishwa na mifumo hiyo iliyopinduliwa. Kwa hiyo kupitia mhusika paka mwandishi ameweza kuonyeshasio tu wembamba wa mipaka kati ya binadamu na wanyama bali pia uwezekano wa taswira zinazowasilishwa na paka katika daraja ya maisha ya watu binafsi, familia, jamii na taifa. Kiubunifu, uwepo wa paka unatekeleza majukumu sawia na yale ambayo yangetekelezwa na wahusika binadamu, kwa hivyo, kutokuwepo na kutokuonekana kwa Bi Masonyanya hakufifilishi uovu uliotekelezwa na bibi huyu, kwani paka anaendelea kubeba dhamira ambazo binadamu wa kawaida angezibeba.

Kwa upande mwingine, paka huyu anachimuza ujumbe wa masalia mbalimbali yanayobaki katika baadhi ya mifumo ya kimahusiano kati ya watu, familia, marafiki, jamii na katika uongozi wa kiserikali katika nchi nyingi duniani. Mfano mzuri inapotokea mtu kashinda uongozi hasa katika maswala ya kisiasa na kumwamngusha kiongozi aliyekuwa mamlakani, unaweza ukakuta bado watu atakaowachagua huyu kiongozi mpya kufanya nao kazi, baadhi watakuwa ni masalia ya kiongozi aliyeshindwa na kuendelea kusababisha utendajikazi kuzorota. Aidha mtunzi anaonyesha mfumo mzima wa kiutawala bado una masalia ya kikoloni. Kwani ukuloni ulimalizika lakini bado ukoloni mamboleo upo. Ndio maana watu hawana amani katika nchi zao, kwa sababu ya vita vinavyosababishwa wakati mwingine na baadhi ya viongozi kwa ajili ya ubinafsi wao. Viongozi wanajilimbikizia mali huku wananchi wao wanateseka wanaingia mikataba mbalimbali na mataifa yaliyoendelea kwa ajili ya kuendelea kujinufaisha wenyewe. Kwa hiyo tunasema tuna uhuru lakini ni uhuru wa bendera masalia ya ukoloni bado yapo.

**4.4.3.5 Ushujaa, Usaliti na Utawala Kandamizi**

Mwingizi katika riwaya hii ya kimajaribio anajaribu kudhihirisha wazi jinsi mambo ya kimazingaombwe na ya kiajabuajabu yanavyochimuzwa na kuibua maudhui mbalimbali kupitia kwa mhusika Babu Gao. Gao ni Mganga wa jadi aliyetafuatwa na wanaukoo wa Bi Masonganya kwa ajili ya kuhakikisha wanamuuwa Bi Masonganya baada ya kukaa kwa muda wa siku saba amekufa lakini wakitaka kwenda kumzika anafumbua macho. Babu huyu alikuwa anapatikana katika kijiji cha mbali sana. Kwa hiyo walikwenda kumtafuta kwa gari na walipokaribia kufika nyumbani kwa Bibi Masonganya alimwamuru dereva amshushe atembee kwa miguu na kikapu chake kichafu akiwa amekishika mkononi. Alipofika msibani aliingia kwa marehemu Bi Masonganya na akawaamuru wafiwa watoke nje ili aweze kumtapisha huo uchawi Bibi huyu unaomfanya kila wanapotaka kumzika anafufuka.

Babu Gao anafananishwa na mwananchi ambaye hapendi utawala wa mabavu ndio maana alijitahidi kwa hali na mali ahakikishe amemuua Bi Masonganya. Pia mwandishi

kupitia kikapu kile kichafu alichokibeba Babu Gao wakati anaagua anafananisha kikapu kile na watu wanyonge wanaoungana kwa pamoja katika kuundoa utawala kandamizi japo wana hali ngumu ya maisha. Babu huyu anafanya juu chini katika kuhakikisha anawasaidia wanyonge hawa kuepukana na utawala kandamizi wa Bibi Masonganya. Maswala mengine yanayoibushwa na Babu Gao ni pamoja na swala ya kutafuta usaidizi kutoka nje pale ambapo watu katika hali zao za kawaida wanaona taratibu zao, mikakati yao na jitihada zao zinashindwa kuwafikisha kwenye neema wanayoisaka. Kwa hivyo, Babu Gao ni taswira ya msaada chanya kutoka nje unaofanikisha maslahi ya watu. Inawezekana pia kuhoji kwamba kwa njia fulani fulani, Mwingizi anaendeleza falsafa na imani za ubabedume hasa msomaji anapodadisi usambamba uliopo kati ya Bi Masonganya—mwanamke mchawi anayedhuru na kuua pasina sababu na hapa Babu Gao—mwanamume mganga anayeleta uponyaji, nafuu na matumaini. Hapa uchanya wa usawiri unahusishwa na mwanamume na mitazamo ya kiume ilhali usawiri hasi unahusishwa na mwanamke na mitazamo ya kike—uharibifu!

Mganga huyu anaonekana kuwa msaliti kwani baada ya kukubali kumtibu Mzee Mtandi kwa dawa za miti shamba. Kwa kumpeleka makaburini na kumweka juu ya kiti katika kaburi mojawapo, na kumwambia ashike kinu ili yeye awe anatwanga dawa kwenye kinu hicho alichokuwa ameshika Mzee Mtandi. Ndipo Mzee huyu alipokuwa akiendelea kutwanga ghafla kinu na Mzee Mtandi wakazama ndani ya kaburi halafu na kaburi likajifunga. Baada ya tukio hilo ndipo Babu Gao akataka kukimbia na kuwaacha Kungurume na dada yake baada ya tukio hilo la kimazingaombwe na kichawi kutokeza katika hali ya kuogopesha.

Mwandishi kupitia Mzee huyu anachimuza dhamira ya usaliti, kwani kuna baadhi ya watu mnaweza mkawa pamoja katika maswala mbalimbali lakini akiona mambo yanakwenda kombo anaamua kuwasaliti wenzake. Mfano mzuri hata viongozi hasa wabunge wanapotaka uongozi hupenda sana kuwa karibu na wananchi lakini wanapopewa uongozi huwadharau wananchi waliowachagua na kutingwa na shughuli zao binafsi. Na wakati mwingine jambo la kushangaza ni viongozi hawa

wanapokwenda katika majimbo yao yaliyowapigia kura,  huandamana na magari mengi na polisi wengi wa kuwalinda kiasi cha kuonyesha kwamba hawana imani na wapiga kura hao. Huu ni ubadhirifu wa mali za umma kwa sababu wakati wanapoomba kura huwa hawana ulinzi wowote na hukaa hata vilabuni na kunywa pombe za asili lakini wakishakuwa viongozi, huwasaliti wananchi kwani wananchi hawawezi kuwa na uhuru tena wa kuongea na kiongozi huyu kwa kuhofia usalama wao.

Kwa upande mwingine, Babu huyu anatumiwa kuchimuza dhamira ya ukombozi. Hili ni jambo linaloakisiwa katika matendo na majukumu anayotakeleza Mzee huyu katika kadhia zilizoletwa na Bi Masonganya. Kwamba, baada ya uchawi wa Bibi huyu kukithiri mipaka, kuwaua wanakijiji bila sababu razini ati kwa sababu anajisikia kuua tu, ujio wa Babu Gao ndio unaoleta matumaini. Hii ni sawia na hali zinavyokuwa katika mataifa ya ulimwengu wa tatu ambapo juhudi za ukombozi kama hazikuchipuka ndani ya nchi, huwa kuna uwezekano wa misaada ya ukombozi kutoka nje ya nchi. Katika mataifa haya ya ulimwengu wa tatu, kumekuwa na viongozi ambao wao walijiona kuwa ni miungu watu waliokuwa wanawanyanyasa wanachi wao Bila hata huruma. Mfano mzuri ni Iddi Amini aliyekuwa Raisi wa Uganda aliwatesa sana wananchi wake lakini alikuja kupatikana kiongozi aliyeweza kumpindua mamlakani. Kiongozi huyu aliwauwa vilema na watu wengine bila huruma kwa ajili ya maslahi yake binafsi kama alivyokuwa Bi Masonganya.

#### 4.4.3.6 Unafiki

Miongoni mwa dhamira ndogo ndogo zinazopatikana katika riwaya ya *Tanzia* ni swala la unafiki. Unafiki unadhihirishwa na mama Kaguba ambaye badala ya kumshtumu mwanawe kwa kurithi uchawi analisimamia swala la kufukuzwa na kushutumiwa kwa Nyembo kama kiini cha uchawi na mrithi wa mama yake Bi Masonganya. Kitendo anachokifanya kinaashiria swala ambalo lipo katika jamii ambapo wakosaji wakiwa wanamuhusu kidamu inakuwa vigumu kuwachukulia hatua.  Kitendo cha unafiki anakionyesha Bi Masonganya pale anaposhindwa kumchukulia hatua mjukuu wake aliyeshtakiwa kwa ubakaji.  Swala la unafiki katika uongozi ni jambo la ubia. Si kwa

jamii za kiafrika pekee. Kinachotakiwa ni kuwa na mfumo wa wazi unaozuia mianya ya mapendeleo ya ki binafsi.

**4.4.3.7 Malezi, Utendajikazi Kuzorota kwa Haki**

Mtunzi ameweza pia kuangazia mambo ambayo yanatendeka katika jamii ili kuangazia ya kwamba, kuna matukio yanayofanywa kiuhalisia na kifantansia. Mtunzi kupitia mhusika Ndoza anaonyesha jinsi baadhi ya watu wasivyokuwa na nidhamu kwa kitendo cha kubaka. Ndoza alimbaka msichana mmoja aliyekuwa akipita na safari zake akamwita kwenye pagara akambaka. Na baada ya kubaka Ndoza alipelekwa polisi kasha mahakamani. Siku ya kezi yake kuzikilizwa mahakamani bibi yake Masonganya alituma nyuki wengi kiuchawi wakaenda kumuuma jaji na waliokuwa wanasikiliza kesi. Siku nyingine tena akatafutwa jaji mwingine lakini akawa anajiandaa kwenda kwenye kesi ghafla akateleza akiwa anatembea na kufa, kwa hiyo kesi ikashindwa kuendelea.

Mwandishi kupitia kijana huyu anachimuza dhamira ya jinsi ya watu mbalimbali wanavyofanya makosa na wanawatumia watu wengine wawasaidie katika kuficha makosa hayo. Linaibuka pia swala la watu binafsi kuboronga mipango na malengo ya taasisi za dola kama njia ya kulinda na kujihakikishia maslahi ya ki binafsi. Uborongaji huo unafikia hata kuua wale waliojukumishwa kutekeleza majukumu na mamlaka ya taasisi wanazoziongoza. Hii inadhihirika kutokana na jinsi majaji walivyouwawa ili kushinda kesi au kukwamisha kesi hiyo ya ubakaji kuendelea. Hali hii ipo sana hata kwa viongozi mbalimbali serikalini hufanya makosa makusudi pia kwa sababu wana kinga ndio maana hawaogopi.

Swala hili la kuingiliwa kwa mifumo ya kitaasisi na taasisi zenyewe kwa ajili ya kukwepa haki, ni swala mbalo limeenea sana katika nchi nyingi za ulimwengu wa tatu. Mfano mzuri ni nchi ya Tanzania mtu anaweza kuendesha gari bila kufuata sheria za barabarani lakini kwa kuwa ndugu yake ana cheo kikubwa serikalini anaachiwa au kwa kuwa ndugu yake ni polisi anaachiwa. Mambo kama haya yanapelekea utendaji kazi katika usalama wa barabarani kuzorota na kusababisha ajali nyingi kutokana na magari

mabovu kutembea barabarani kwa sababu wana kinga.Vilevile mwandishi anachimuza dhamira ya wananchi kuchangia katika uvunjaji wa haki. Kupitia tukio hili la kichawi ni wazi kabisa hapo haki kutendeka itakuwa vigumu kutokana na kwamba majaji wote wamekufa; na shahidi namba moja amekufa. Kwa hiyo kesi kuendelea itakuwa ni vigumu. Na utekelezaji wa haki hautakuwepo tena upande wa mlalamikaji. Aidha mtunzi kupitia tukio hili la ubakaji liliopelekea matukio mengine anachimuza dhamira ya jinsi wafanyakazi wengi wa serikali wanavyofanya kazi katika mazingira magumu. Na hii si kwa majaji tu katika nchi za Afrika bali hata kwa wafanyakazi wengine wa idara zingine wakiwemo walimu na madaktari na manesi; wote wanafanya kazi katika mazingira hatarishi na wengine magumu na wanapokea mishahara midogo sana lakini bado wanakuwa ni wahanga wa maisha yao.

#### 4.4.3.8 Haki, Sheria na Mafao ya Ki binafsi

Siku zote utendaji haki umekuwa mgumu katika ofisi mbalimabli kutokana na watu wenyewe kuvuruga haki inapotakiwa kutendeka. Mfano mzuri ni majaji na mawakili ambao wamekuwa wakifanya kazi katika mazingira magumu kutokana na watu kutopenda haki itendeke. Japo kuna baadhi ya majaji na mawakili ambao huivunja haki wenyewe kutokana na kupokea rushwa, lakini pia wananchi nao huchangia katika kuhakikisha haki haitendeki. Mfano mzuri majaji wawili waliokuwa wanahukumu kesi ya ubakaji ya Ndoza.  Majaji hawa walikufa wakati wakijiandaa kutoa hukumu ya kesi ya Ndoza. Waliuawa kiuchawi na kimazingaombwe na Bibi Masonganya ambaye mjukuu wake alikuwa mtuhumiwa wa ubakaji.

Mwandishi kupitia majaji hawa na shambulio hilo la nyuki anachimuza dhamira ya wanasiasa kuingilia taaluma za majaji. Nyuki waliomshambulia jaji ni wanasiasa wanaowashambulia majaji pindi wanapotaka kutenda haki katika maswala mbalimbali ya nchi. Mfano mzuri hata nchini Tanzania majaji wengi wamekuwa hawana sauti hasa kwa viongozi wa kisiasa au hata katika kesi za chaguzi mbalimbali majaji wamekuwa kama bendera zinazofuata upepo kwani hawana sauti hasa kwa chama kinachokuwa mamalakani. Na hiyo ni kutokana na kwamba Raisi ana mamlaka makubwa sana ndiye

anayewachagua majaji wote nchini Tanzania kiasi kwamba majaji hawa hawawezi kufanya kazi kwa maamuzi yao.

#### 4.4.3.10 Sheria, Migongano katika Familia na Uongozi wa Kurithishana

Miongoni mwa dhamira zinazochimuzwa na Mwingizi ni dhamira ya uvunjaji wa sheria, migongano katika familia, Uongozi wa kurithishana. Dhamira hizi zimechimuzwa kupitia kwa mhusika Nyanzala ambaye matendoyake mengine yamekuwa katika ulimwenguni halisi na ndotoni kupitia kwa wahusika wengine. Nyanzala ni mtoto wa Masonganya ambaye alimuuwa mama yake kutokana na kuhofia mama yake asije akamrithisha uchawi baada ya kuona anachelewa kufa. Kupitia mhusika huyu mtunzi anachimuza dhamira ya kurithishana uongozi katika baadhi ya nchi jambo ambalo linapelekea demokrasia kukosekana kwani ukoo mmoja ndio unaongoza milele mfano wa nchi hizo ni kama United Arab Emirates, Saudi Arabia, Switzerland, Oman, Qatar na Iran. Kwa hivyo, mtunzi anaonyesha wazi kwamba, kuna baadhi ya watu ambao hawako tayari au hawapendi uongozi wa kurithishana japo wapo katika nchi ambazo zina mfumo huo wa kisiasa.

Aidha kwa upande mwingine, Nyanzala anachimuza dhamira ya baadhi ya viongozi wengi wa mataifa ya ulimwengu wa tatu ambao wapo mamlakani wengi wao ni wale ambao wana mfumo wa kuandaliwa kuja kuwa viongozi. Ndio maana utakuta kama baba aliwahi kuwa waziri na mtoto pia atakuja kuwa waziri au atashika nafasi kubwa serikalini, au kwa mfano kama baba alikuwa raisi na mtoto naye atakuja kugombea au kuwa raisi. Kwa hiyo siku zote ukoo mmoja unaendelea kunehemeka kwa kila kitu katika nchi hizo. Ndio maana Nyanzala alikuwa anataka kuteketeza kabisa uongozi wa aina hiyo. Kitu cha ajabu na cha kushangaza Binti huyu naye anakufa akiwa usingizini ndugu zake wanasikia kifo chake kinatangazwa msikitini asubuhi ya saa kumi na moja wakati wamelala naye humo humo ndani na hawajui nani ametangaza. Na baada ya kuwauliza hata nao msikitini wanashangaa ni nani ametangaza, kilikuwa ni kitu cha ajabu sana katika ulimwengu. Baada ya tangazo hilo ndugu hao walikimbia kitandani kwa Nyanzala kumwangalia wakakuta alishakufa. Mwandishi anachimuza ujumbe wa

jinsi ambavyo watetea haki katika maswala ya kisiasa wanavyokufa siku zote kwani hukutwa tayari wametupwa sehemu fulani pasipokujua nani amewauwa au wakati mwingine hupotea kabisa bila kuonekana milele.

**4.4.3.11 Mitandao ya Udhalimu na Unyanyasaji**

Mhusika Binti Sambayu ni kielelezo cha wafuasi wa mitandao ya uchawi na udhalimu wa wanajamii. Mitandao hiyo ni mipana na inataratibu zake maalumu. Chuki baina ya wanajamii ni chanzo cha mauaji na kutesana. Dhamira inayoonekana hapa ni sababu ambazo mtunzi anazitoa zinazosababisha kulogana. Kwa mara nyingine tena mtunzi anachukua fursa ya uhuru wa kifasihi kupitia mtindo wa uhalisaajabu, kuwasomesha wasomaji wake juu ya dhana ya misukule na uwangaji. Katika usimulizi wa mwandishi miviga ya uchawi inadhihirishwa, taratibu na hatua za kuwaingiza watu katika ngazi ya misukule vilevile inaratibiwa na mwandishi. Picha anayomwachia msomaji ni jinsi ada na desturi hizo zinavyotegemea nguvu za kiza kama alivyo kwa Mzee Sufiana na Hunudu katika riwaya za *Vita vya Mapenzi* na *Mzimu wa Waufi*.

Aidha kitendo cha kufufua maiti halisia na kumrudisha duniani marehemu aliyekufa kinakubalika katika dunia ya kiuhalisiajabu na dunia ya ndoto. Kwa mujibu wa mtunzi, yote hayo yanawezekana katika riwaya zake za kimajaribio. Kitendo cha Nembo kumbana Binti Sambayu, kiongozi msaidizi wa wachawi hadi kukubali kutoa siri za mtandao wao, ni ishara ya kuanguka kwa imani hizo katika jamii ya mtunzi. Dawa ya uchawi na wachawi ipo, kwa kutumia kibuyu cha Masonganya, Mzee Mtandi na Nyanzala ambao wanafanikiwa kuuangusha utawala wa Bi Masonganya na mfumo wa ushirikina usiokuwa  na tija kwa jamii.

**4.4.3.12 Unyanyapaaji, Elimu, Ukombozi na Nafasi ya Mwanamke**

Mtunzi ameendelea kusawiri mambo ya kutisha na ya ajabu kupitia mhusika Nyembo ni mtoto aliyezaliwa katika mazingira uatanishi ya kimazingaombwe. Nyembo ni mtoto wa Bi Masonganya ambaye alizaliwa katika mazingira ya ajabu. Bi Masonganya anaamuliwa na wachawi wenziwe aowe mwanamke wakati na yeye ni mwanamke. Hii

ilikuwa ni sheria ya wachawi kwamba, kiongozi yeyote wa wachawi lazima aoe hata kama yeye ni mwanamke. Ndipo Bi Masonganya anamuoa Bi Masunga na kuzaa naye mtoto aitwaye Nyembo. Kwa sababu hii, Masonganya ndiye babake Nyembo, Masonganya ni Baba yake. Binti huyu alikuwa akiishi na mjomba wake marehemu Mtandi. Baada ya ndugu zake kumnyanyapaa sana, Bibi Masonganya anamwomba kaka yake huyo Mtandi aishi naye. Nyembo akiwa kwenye msiba wa Mzee Mtandi anabahatika kuona shajala aliyokiandika Mzee Mtandi kabla hajafa. Anaona jinsi alivyoandika kuhusiana na majani ya kimbusi ambayo yanaweza kuwa kinga katika familia yao dhidi ya wachawi.

Kupitia Nyembo mwandishi anachimuza dhamira ya elimu. Anamsawiri Nyembo kama mkombozi wa jamii ambaye anaonyesha umuhimu wa elimu katika jamii ambayo haioni umuhimu wa elimu katika kuhakikisha anawateketeza wale wote wanaozorotesha maendeleo ya elimu katika sehemu mbalimbali. Mtunzi kupitia Nyembo anaonyesha jinsi watoto wengi wanavyoacha shule kwa sababu ya mimba. Wengine kufanya kazi za kuzurura mitaani kwa kuhakikishwa wanachukuliwa hatua wale wote walioshiriki kwa namna moja ama nyingine katika kuzorotesha maendeleo ya elimu. Ndio maana mtunzi ametumia uyumbishwaji wa mipaka kupitia kuzaliwa kwake yaani baba na mama yake ni wanawake. Jambo ambalo ni la ajabu katika jamii yeyote katika kuchimuza maudhui ya elimu kama njia mojawapo ya ukombozi.

**4.4.3.13 Wasomi na Imani za Uchawi na Busara**

Mtunzi kupitia mhusika dereva anamshangaa Kungurume kwani ni msomi lakini anaamini mambo ya uchawi na ushirikina. Mhusika dereva alikuwa na safari zake ghafla, akawakuta porini Kungurume na dada yake wakiwa wameweka pembeni gari yao ambayo ilikuwa imembeba Mzee Mtandi ikiwa inampeleka kwa mganga wa jadi Babu Gao. Mzee Mtandi anapoteza fahamu katika mazingira ya kiajabu wakati akiwasimulia ndugu zake habari za Binti Sambayu na Kaguba alizozisikiliza usiku. Dereva anasimamisha gari na kuwauliza wana shida gani wakasema wanaelekea kwa mganga wa jadi kumpeleka kaka yao ambaye ni mgonjwa sana. Ndipo dereva akashangaa sana na kumtaka Kungurame wamrudishe mgonjwa hospitali mjini na si

kwa mganga la sivyo hawataweza kumbeba. Dereva akaendelea kumwambia Kungurame kwamba anamshangaa anaonekana ni msomi lakini anaamini mambo ya uchawi. Mwandishi anaonyesha dhamira ya baadhi ya watu kutoamini uchawi jambo ambalo ni la kweli uchawi upo tena wasomi wengi huutumia uchawi huo katika mambo yao mbalimbali. Ndio maana viongozi wengi wanapotaka kupandishwa vyeo au kupata nyazifa fulani hujishughulisha na mambo ya uchawi na ushirikina. Halikadhalika pamoja na dereva huyu kumsema Kungurume, pamoja na usomi wake, anaamini mambo ya uchawi na ushirikina. Alikubali na kuwapeleka kwa Babu Gao lakini kila alipowasha gari yake lilikuwa linagoma. Hii ilikuwa tosha kumdhihirishia dereva huyu kwamba, uchawi upo na watu wanaamini katika uchawi na ushirikina.

**4.4 Hitimisho**

Katika sura hii tumeangazia kipengele cha wahusika jinsi walivyoweza kusawiriwa na kuchimuza maudhui mbalimbali katika riwaya ya *Vita vya Mapenzi*, *Mzimu wa Waufi* na *Tanzia*. Kikubwa zaidi tumechambua jinsi wahusika mbalimbali wa kijiniuchawi na ushirikina walivyoweza kusawiriwa katika riwaya hizi na kutupatia maudhui mbalimbali. Tumebaini wahusika hawa waliosawiriwa katika riwaya hizi wamechangia pakubwa katika kukuza na kuendeleza maudhui mbalimbali yanayopatikana katika riwaya hizi. Na jamii ikajifunza mambo mbalimbali kama vile umuhimu wa utamaduni wetu Afrika, jinsi ukoloni mamboleo unavyoendelea kutuathiri, athari za dini za kigeni Afrika, athari za uongozi mbaya, athari za utandawazi katika mataifa ya Afrika, dhamira za usaliti katika maisha, athari ya migogoro ya kisiasa katika mataifa ya ulimwengu wa tatu, madhara ya wanasiasa kuingilia taaluma za watu katika utendaji wa kazi serikalini, madhara ya wananchi kujichukulia sheria mkononi, uwajibikaji katika utendaji kazi, mila na desturi mbalimbali zinavyoathiri utendaji na upatikanaji wa haki. Swala la ujadi na usasa na mikinzano ya kidini na kiitikadi.

# SURA YA TANO

# ISHARA NA UASHIRIAJI KAMA MIKAKATI YA UCHIMUZI KATIKA RIWAYA TEULE ZA MAUNDU MWINGIZI

## 5.1 Utangulizi

Sura hii inaangazia swala la ishara na uashiriaji kama mikakakati ya uchimuzi katika riwaya za Maundu Mwingizi. Ili maswala haya ya ishara yaweze kuzungumziwa na kuchakatwa kwa kina, mijadala ya sura hii itajikita katika motifu ya safari, mapito, usakaji na ndoto/njozi—ikizingatiwa kwamba mna safari, mapito na usakaji wa kihalisi, na vilevile safari, mapito na usakaji wa kinjozi, kijini na kiuchawi katika riwaya hizi. Mijadala ya sura hii tumeielekeza katika kuchanganua kupitia mbinu za kisemiotiki. Motifu mbalimbali kama kanikinzani za njozi na uhalisia, wahusika watu na majini watu/mizuka, mandhari halisi na zile za kufikirika, matukio ya kichawi/kiwanga na yakinifu yanajadiliwa katika riwaya teule za Maundu Mwingizi za *Vita vya Mapenzi* (2012), *Mzimu wa Waufi* (2013) na *Tanzia* (2015). Vile kulivyo na mapito ya kihalisi na mapito ya kimazingaombwe ndipo kunapojitokeza vifo halisi na vifo vya kijini. Hali hizi zimewezesha kujadiliwa kwa mapana kwa dhana za ishara na uashiriaji unaowezeshwa na kifo, ufu na ufufuo,  pete, mizimu, mimba, kimbunga, moshi, mwanga, giza, tiba, misitu, mito, mapango, makaburi, paka, kikapu kichafu, kukatwa ndimi na miktadha mingine ya kijini na kichawi.

## 5.2 Uhalisiamazingaombwe Katika Ishara na Uashiriaji katika Riwaya za Mwingizi

Mwingizi ametumia umazingaombwe kwa kiasi kikubwa katika riwaya zake zote katika kuashiria matukio mbalimbali yanayopelekea kuibua maudhui mbalimbali ambapo matukio haya yanaonyesha kwamba, kuna uoanishaji wa matukio ya kihalisi na yale ya kimazingaombwe yanayochangia sababu za vifo, njia za utajirisho, utatuaji wa kesi za kimahakama, uzazi, sababu za ajali, ulimbikizaji wa fedha, maisha ya mijini na vijijini, imani za kidini, upeanaji wa majina ya sehemu na watu, njama na usaliti. Kazi hizi zimetamalaki aina mbalimbali za ishara ambazo tunaziweka katika mafungu ya ishara za kiuasili zinazomakinika (rangi za vitu, maumbile kama radi, vimbunga, upepo, kiza na

mvua za kutisha), ishara za vitu vya kawaida vinavyopewa sifa za ziada kama vile pete, usinga, vibuyu, na mikoba ya kiuganga. Ishara dhahania kama zile zinazoambatana na majina ya miji kama vile Bagamoyo na Kigoma, na sifa za mijini na mikoani (vijijini) kuwakilisha uoni wa aina mbili tofauti au majina ya wahusika yenye siri kama vile Masumbuko. Kuna ishara ambazo zinaambatana na uchoraji wa wahusika wa kawaida lakini wenye tabia za usiri kama vile viongozi wa dini wanaowasaliti waumini wao, na wale ambao si viumbe wa kawaida kama vile wanga, wachawi, majini, misukule na mizuka. Kuna ishara za vifo, kuna matendo ya kitabibu/madhara ya kawaida na utabibu wa kimazingaombwe unaoshirikisha mbinu zisizo za kawaida kama vile kukata ndimi, kupoozesha mtu kwa ishara za rangi ya pete na kuagua makaburini. Kuna vita vya kitikadi za kichawi, kidini, kitabaka, kisiasa na kimapenzi.

Mwingizi ametumia umazingaombwe kwa kiasi kikubwa katika riwaya zake zote katika kuashiria matukio mbalimbali yanayopelekea kuibua maudhui mbalimbali yanayojikita katika maswala ya kuichora jamii yake yenye mseto wa imani na itikadi, mifumo mseto ya kifikra, mionoulimwengu, mifumo ya maingiliano na mitagusano ya kijamii na mifumo ya kisiasa na kiuchumi. Riwaya za *Vita vya Mapenzi* (2012), *Mzimu wa Waufi* (2013) na *Tanzia* (2015) ni riwaya za mkondo wa kiuhalisiamazingaombwe kwa upande mmoja lakini pia tunaweza kuziweka katika fungu ambalo Wamitila (2008: 118) ameliita fungu la riwaya za kinjozi au kifantasia. Sababu za kuziweka riwaya hizo chini ya mkondo wa kiuhalisia mazingaombwe ni kutokana na jinsi riwaya hizi teule zilivyoundwa na kuwa na msuko wa kimajaribio na vilevile kusheheni maswala yanayochukulia mipaka baina ya udhahania na uhalisia kuwa ni mdogo sana. Kwa maneno mengine, uhalisia mazingaombwe unadhihirika katika kazi teule tunazozimakinikia katika sura hii. Sifa bainifu ya kazi hizo ni kwamba zina hali nyingi ambapo usababishaji na matokeo ya usababishaji huo yanakwenda kinyume na urazini na mantiki, kuna ujitokezaji wa matukio ya kiajabuajabu ya kimazingaombwe ambayo si rahisi kuelezeka kwa kutumia kanuni za kiyakinifu. Mfano kuruka kwa upepo, kufa na kufufuka, kivuli cha maiti kuwa mbadala wa maiti, watu wanaoaguliwa kutumbukia

makaburini na kuzua vurumai humo ndani, kuishi chini ya bahari, ndoto za ukweli, kujigueza maumbile.

Katika riwaya hizi tunakutana na usimulizi wa kiuhalisia ambao unawashawishi wasomaji kiyakinifu kwa kutaja mandhari halisi (Ubungo, Tabora, Kigoma, Dar es Salaam, Bagamoyo). Kuna wahusika halisi kama polisi, madereva wa teksi, abiria, vifaa vya kisasa kama vile simu za Voda na Tigo, magari ya kawaida kama Landrover, boda boda na mabasi halisi, lugha ya kawaida ya mitaani (na ile ya miktadha rasmi mfano mahojiano ya polisi au daktari). Mbinu hii inaoanishwa na usimulizi wa kidhahania kama vile masimulizi katika ndoto, misukule, uchawi, majini, mizuka, kupaa, nguvu za vibuyu, pete, usinga na mikoba ya uganga. Vitendo vya kupigwa bila ya kuonekana mpigaji bali kudhihiri kwa athari ya kipigo kwa njia ya damu, kuruka kwa njia ya upepo kwa nguvu ya pete, mwanamke kumzalisha mwanamke mwenziwe ni miongoni mwa matukio yasiyo ya kirazini. Karibu kila tukio lina mseto wa mambo halisi yanayochanganywa na mambo ya kustaajabisha.

Kwa hiyo, wasomaji wanavutwa katika usomaji wao kuingia katika aina mbili za uoni. Njia hizo za uoni zinachanganywa kiasi cha kuwa na mipaka midogo mno. Kuna matukio ya kichawi au kimazingaombwe yanayotumia nguvu za maneno tu ambapo ishara za kisitiari huchukuliwa kuwa ni sehemu ya uhalisia. Kwa ujumla mwandishi analeta mapinduzi ya kifikra badala ya kuegemea tu katika fikra yakinifu anachombeza utata wa kiyakinifu anaokuja kuuthibitisha kimantiki kiasi cha wayakinifu kama vile maaskari au wapelelezi au wasomi kama vile Masumbuko na Suhail wanakuja kukubaliana na mantiki na kutumbukia katika dunia ya uoni kuwili. Kazi nzima zinaumbwa na ishara jumui (bia), ishara mahsusi na visaasili. Na mwishoni muda wa matukio umejidhihirisha kuwa ni wakati uliopo lakini ukirejelea nyakati zisizo na ukomo na zinazobeba historia.

Riwaya teule Mwingizi zinaingia katika fungu la uhalisiamazingaombwe kwa sababu ya kuwa na mtindo wa uajinabishaji ambao mwandishi anautumia kuwatatiza kifikra

wasomaji wake wasitoe majibu ya haraka haraka kila tukio linapojiri. Wasomaji wanapewa mafumbo na kuachwa katika hali ya hatihati hadi hapo mwandishi anapolifungua fumbo; panapokuwa na uzazi wa kawaida anaupindua na kuonyesha usiri uliojificha ndani yake, panapokuwa na mauaji ambayo kwa mujibu wa taratibu rasmi wahusika hukamatwa kwa vielelezo maalumu lakini mwandishi anawapa wasomaji upande wa pili wa sarafu na kuonyesha ni kwa kiasi gani vipimo yakinifu si pekee vya kuvitegemea kwani vina uwezo wa kuwatia hatiani wasiouhusika. Kwa mfano, katika riwaya ya *Mzimu wa Waufi* tunawaona Masumbuko na babu yake wanahusika katika mauaji ya Nyamizi. Ukweli ni kwamba walikutwa makaburini lakini kwa kuwa walikuwa wameshika panga wakiwa na damu kidogo katika nguo zao, ndio maana wakaonekana wamehusika kumbe hawajahusika na aliyehusika ni Hunudu (Uk 148). Vilevile kifo cha Mzee Kishindo wanahusishwa Mzee Kikoko na Masumbuko wakati si wahusika bado mhusika ni Hunudu. Kwa upande mwingine, katika *Vita vya Mapenzi* Suhail anahusishwa na mauaji ya Msigwa wakati mhusika wa mauaji ya Msigwa ni Joram Ndege lakini kwa kuwa mpaka umauti unamkuta Msigwa walikuwa na ugomvi na Suhail ndio maana suhail akahisiwa amehusika na mauaji hayo.

Panapokuwa na wanajamii ambao wanaonekana mbele ya macho ya wasomaji kuwa wana majukumu fulani kama vile viongozi wa dini, wanausalama, madaktari, wasichana warembo, au watoto na vilema, mwandishi anawageuzia upande wa pili wasomaji wake na kuibua sura halisi za wahusika hao na kubainisha usaliti na unafiki wao kwa jamii. Kemeo lake ni kuwa uongo, udhalimu, na uonevu havina nafasi ya kushinda dhidi ya ukweli na haki. Mfano mzuri ni baadhi ya viongozi wa dini ambao ni wanafki ni Sheikh Mwinyigoha na mchungaji Geofrey ambao wanatumia dini katika kufanya maovu (MW uk 5). Aidha nguvu hizo siku zote zitakuwa katika kanikinzani na mwisho wa yote anatoa hitimisho la ushindi wa nguvu za mkono wa kulia yaani nguvu za ukweli, usawa na haki. Katika mambo ambayo anawaaminisha wasomaji wake kiyakinifu, mwandishi anayavunja kidhahanifu.

Madhumuni ya mwandishi ni kuoanisha itikadi na imani za kidini, kuwasilisha mifumo mbadala wa uwazaji na maingiliano, kuibua imani na mitazamo ya kisiasa na kitamaduni katika jamii yake, na kuijenga jamii yake katika muktadha wa umoja na kuvumiliana na mseto wa tamaduni kupitia matukio na fikra za kiuhalisia na zile za kimazingaombwe. Funzo analotupa ni kuwa si rahisi kwa Mwafrika kuikwepa asili yake ikiwa ni pamoja na fikra za kidhanifu kama vile mazindiko, tafsiri za ndoto, fikra za maisha baada ya kifo, ushirikina na ujaala. Japo swala la tafsiri za ndoto halipo tu kwa Waafrika tu hata kwa jamii nyingine swala hili huwa lipo. Kwa upande wa fungu la riwaya za Maundu Mwingizi kuwa katika mkondo wa kinjozi au kifantasia. Hapa tunakubaliana na maelezo ya Wamitila (2008:118) pale anapoziweka katika fungu la riwaya za kiwakati riwaya zenye kuchimuza kwa wingi tegemeo la ishara za njozi kama kiini cha usimulizi. Huwezi kuepuka kukutana na njozi au maruweruwe katika riwaya zote tatu tulizozituea. Katika riwaya ya *Vita vya Mapenzi*, Suhail anatokewa na jini-mtu katika njozi mara kwa mara na jini mtu (Mzee Shamhurish Bin Sufian); Mama Kaguba katika *Tanzia* (Uk:20) "anaota ndoto mbaya' ambayo ni sehemu ya "mawasiliano ya kihisia". Masumbuko naye anakuwa katika ndoto za kiuhalisia ambapo mara kwa mara anatokewa na hasimu wake Hunudu katika *Mzimu wa Waufi*.

Kuhusiana na matukio muhimu ya kinjozi au KIutopia, Wamitila (2003) anafafanunua kuwa riwaya za kinjozi zinaepuka kujikita katika kanuni za kijarabati au za ulimwengu halisi. Kwa hivyo sifa za uhalisia, uishara, unjozi na umazingaombwe; zina mfano katika riwaya ambazo mifano yake ni riwaya teule za Maundi Mwingizi. Hatuwezi kutenganisha uashirishaji wa njozi na uhalisia au umazingaombwe katika riwaya hizi. Kila moja ya mbinu inajitegemeza katika mbinu kinzani au ya kinyume. Mhusika anapoota jambo fulani inakuwa ni sehemu ya mawasiliano ya kihisia yenye ukweli na udhihirisho halisi. Mwotaji hapaswi kupuuza fikra, mawazo na ujumbe anaoletewa au kitendo anachofanyiwa katika ndoto husika. Anapojaribu kukwepa kutekeleza matakwa ya ndoto hiyo anajikuta katika matatizo. Lakini si rahisi kwa wanajamii kuamini ndoto hizo kirahisi hivyo mhusika wa ndoto anakuwa na safari ndefu ya kudhihirisha ukweli au uhalisia wa ndoto yake. Hii huifanya ploti ya riwaya ijiegemeza katika ndoto hizo

kama ilivyo katika riwaya zote teule za Mwingizi, Wahusika wanaonekana kutawaliwa na ndoto kwa kiasi kikubwa.

Katika ndoto kunakuwa na umazingaombwe na uajabuajabu ambapo kwa jicho la ujarabati au uhalisi si rahisi kukubaliana na ujumbe wa ndoto hizo. Ndoto haiwezi kuwa ndoto bila kukitwa katika uhalisi, wa aina fulani wa kiyakinifu au wa kidhahania. Vivyo hivyo, ndoto haiwezi kutafsiriwa pasina kujengewa muktadha, na muktadha haujengeki katika ombwe tupu ila katika uhalisia wa aina fulani wa kiyakinifu au wa kidhahania. Hivyo ndoto inaweza kuangaliwa kuwili; kama ukweli wa maisha unaojikariri katika ndoto au kama ishara inayobashiria matukio ya baadaye katika mustakabali wa maisha ya mtu. Hivyo ndoto ni sifa za kazi za uhalisiaajabu au umazingaombwe ambazo zinaunganishwa na sifa za kinjozi. Kwa mantiki hii, tunaziweka riwaya hizi katika fungu la riwaya za ishara za kinjozi za uhalisiamazingaombwe.

Mseto huu wa mambo na ndoto unadhihirika katika sura hii. Katika riwaya hizi teule kuna utokeaji wa maswala ya kidhahania yanayooanishwa na ukweli wa kiuhalisia. Mbinu hii inamruhusu mwandishi huyo kuihoji mifumo ya kisiasa, kiuchumi, na kijamii kiundani bila ya kubanwa na mitazamo ya kiyakinifu na jicho kali la mifumo ya kibabe na utawala. Mwandishi anathubutu kukiuka ukweli wa kiuhalisia na kuingiza maswala ya kimazingaombwe na mifumo ya kijaala ili aweze kujitosa kuzungumzia maswala ya kweli, maswala ya kufikirika, maswala yaliyobanwa yasizungumziwe kwa sababu za aina mbalimbali na pengine kuzungumzia maswala yanayokera mifumo ya kiserikali na hivyo uhalisiajabu unakuwa mkakati wa kukwepa mkono wa sheria. Katika riwaya zake za *Vita vya Mapenzi* (2012), *Mzimu wa Waufi* (2013) na *Tanzia* (2015) Mwingizi, anachimuza mandhari, wahusika, usimulizi wa matukio ya kweli na yale ya kufikirika kiasi cha kuwafanya wasomaji wasione tofauti kati ya dunia ya kidhanifu na dunia ya kiyakinifu; na kati ya watu waliokufa na walio hai.

Wahusika wafu wanatekeleza majukumu na wanakubalika na tofauti kati ya ndoto na uhalisia inavunjwa. Kwa mfano, Mzee Kishindo na Nyamizi katika riwaya ya *Mzimu wa*

*Waufi* ni wahusika waliokufa lakini baadaye, wanakuja kutokeza duniani wakiwa hai. Mzee Kishindo alifufuka kwa ajili ya kumtaka Mzee Kikoko atubu dhambi za unyanayasaji aliokuwa anamanyia mkwe wake na kwake pia, halafu akapotea tena. Vivyo vivyo na Nyamizi naye alikufa lakini akawa anaonekana kuwa hai. Kwa upande wa *Vita vya Mapenzi* Mzee Sufian anakufa kimajini na baadaye anaendelee kuishi na anatenda matendo mengi kupitia ndoto. Pia katika riwaya ya *Tanzia*, tunamwona mhusika Nyanzala anakufa lakini anakuwa anawatokea baadhi ya watu ndotoni, na anaendelea kuishi huku akifanya kazi kwa watu. Kwa hivyo, kuwepo kwa wahusika walio wafu, misukule, mizimu, watu waliohai, watu majini, na wanga ni sehemu muhimu ya uchoraji wa wahusika. Kuwa na matukio yatokeayo katika ndoto inayogeuka ukweli kama ilivyo kwa Nyamizi katika riwaya ya *Mzimu wa Waufi*, ni sehemu muhimu ya masimulizi katika riwaya hizi. Ili kufanikisha malengo yake, Maundu Mwingizi ameitumia mbinu ya ishara na uashiriaji kwa wingi. Kuna aina mbalimbali za ishara anazozitumia kama vile ishara zinazowashaBihisha wanyama (ngombe, mbwa, paka), majina ya wahusika (mazingira, rangi, vitu vya kuundwa na wanadamu kama vile pete, kikapu, chungu, usinga na vibuyu).

**5.3 Mwegemeo wa Kisemiotiki katika Riwaya Teule za Maundu Mwingizi**

Kwa miaka kadhaa imechukuliwa kwamba kila mfumo wa alama katika jamii, uasili, na utambuzi wake ni sehemu ya kikoa cha semiotiki. Taaluma ya semiotiki inawavutia wahakiki wanaotaka kuchambua alama na ishara kwa ujumla. Hivyo nadharia hii imesaidia kuchanganua ishara katika kazi hii ambazo ni jambo moja kuwakilisha jengine, yaweza kuwa neno, usemi au taswira. Kwa mujibu wa Umberto (1976) anasema semiotiki ni nadharia ya mfumo wa alama au ishara. Na kwa maneno ya Wamitila (2003:190, 191), anatufafanulia kuwa semiotiki ni nadharia ya kimuundo inayojishughulisha na "ishara na maana ya ishara hizo katika kazi ya fasihi". Nadharia hiyo inaangazia uashiririaji na jinsi kazi hiyo ya fasihi inavyowasiliana na wasomaji wake. Hii ni maana ya Wamitila katika muktadha wa kifasihi lakini pia semiotiki hujishughulisha pia na maswala mbalimbali ya kiisimu.

Katika mawasiliano ya aina mbalimbali baina ya mwandishi na wasomaji, uashiriaji ni njia mojawapo ya mawasilano hayo. Jambo la msingi analolisisitiza Wamitila ni kwa mhakiki kuchunguza au kujiuliza ni kwa nini kazi hizo "zina maana zilizonazo kwa wasomaji wa kazi hizo". Maswali yetu katika sura hii yamekitwa katika kujiuliza ni kwa nini mwandishi ameacha njia nyinginezo za mawasiliano na wasomaji akaamua kutumia nyenzo ya uashirishaji. Katika uashirishaji hatutajikita katika ishara za waziwazi zenye kuonekana pekee kama vile ishara ya pete au kimbunga, bali hata ishara za kidhahania kama vile majina ya majazi (Masumbuko, Bagamoyo, Mlingotini) na maana ya ziada ya majina hayo.

Katika fasihi uishara unafanya kazi kwa ndani ili kuoanisha usimulizi na maudhui. Kwa mfano, katika riwaya za Maundu Mwingizi kifo kinatumika katika kuashiria mambo mazito yanayotendekeka katika jamii. Katika usimulizi wa riwaya zake, uishara umezalishwa kupitia istiara mseto ambapo uhusiano wa kiuhalisia unahusianishwa na uhusiano wa kiistiara. Istiara inakuwa ni njia ya kuongezea taarifa zaidi ya kimaudhui. Hata hivyo, istiara inaiwekea mipaka uwezo wa kueleweka. Katika ngazi nyingine, istiara inageuka na kuwa alama ya uishara unaofanya kazi bila ya kukusudiwa, kwa sababu katika riwaya za Mwingizi ishara nyingi hadithini zimebeba maana zaidi ya moja, ni ishara fumbati. Mfano ni ishara kama za kifo, pete, mwangaza na giza. Ishara hizo zipo katika riwaya hizi na zimekuwa na maana zaidi ya moja. Aidha katika riwaya ya *Tanzia*, mtunzi ametumia ishara ya mwanga kama njia moja wapo ya kuwatoa watu ujinga na kama njia ya ukombozi katika jamii ya Kibondo baada ya kuteswa kwa muda mrefu na wachawi ambao hatimaye wanakufa.

Kwa mujibu wa Griffen (1997) na Wamitila (2003:68 69), wanasema dhana za ishara na uashiriaji zinalenga katika kubainisha kitu fulani kuwakilishwa na kingine. Kuwakilishwa huko kunaweza kuwa ni kutokana na uhusiano uliopo kati ya vitu viwili au uwezo wake wa kuibua fikira fulani katika akili ya msomaji. Zipo ishara bia ambazo huweza kutambuliwa na watu popote pale walipo. Ishara ya pete inaweza kuwakilisha ndoa katika mtazamo wa ishara bia lakini pete hiyo hiyo yaweza kuwakilisha nguvu za kiza au kuwakilisha bahati kutegemea muktadha unaohusika. Kwa mfano, pete inaweza

kuwa ishara ya mkatale, mkataba funge wenye masharti kama inavyotokea katika ndoa, mke kufungwa kwa mume na mume hivyo hivyo. Inaweza pia kuwa ishara ya ahadi. Ishara ni kitu kimoja kinachosimamia kingine kama kitu, mtu au wazo. Aidha kitu chochote kile kinaweza kuwa ishara kutegemea muktadha na mawasiliano yanayokusudiwa. Kwa mfano, pete inavyotumika katika *Vita vya Mapenzi*, inatekeleza majukumu mbalimbali kama vile kumwacha mtu katika njia panda kama ilivyomfanya mhusika Suhail alivyoachwa njia panda na Mzee Sufian. Pete imetumika kama chanzo cha uchumi katika himaya ya Budha, vilevile pete imetumika kama chombo cha kumfanya mtu kuingia katika mikataba fulani fulani na hatimaye mikataba hiyo inakuja kumnyonya.

Mwanadamu ndio chimbuko la ishara katika miktadha kadha wa kadha. Na lugha ni muundo wa kuwasiliana kwa njia ya ishara. Maundu Mwingizi ameweka kipaumbele katika matumizi ya ishara, hususan katika uundaji wa majina, rangi, matambiko, utabibu, mizimu, miungu, na hata matukio aina aina. Ingawaje riwaya zake teule zina vipengele na mbinu nyinginezo kama vile semi na methali, visaasili, usimulizi, na umazingaombwe lakini tumeamua kupitia mkondo wa kisemiotiki kubaini mbinu ya ishara na uashiriaji katika kuibua dhamira za mwandishi. Uishara ni tabaka la ndani la maana analokusudia mwandishi. Tabaka la kwanza ni la kawaida ambalo maana yake iko wazi, na tabaka la pili ni pale taswira na vitu vinawakilisha dhana na hisia. Vitu kama vile pete hutumika katika hali ya kawaida kubainisha urafiki, alama ya uchumba na mapenzi, ufunge katika ndoa, ahadi ya uaminifu na uwekaji mipaka ya mahusiano. Lakini pete inapotumikishwa katika bunilizi, inaweza kutumiwa kitaswira kumaanisha nguvu za kijaala na utajirisho, ambapo katika hali kama hizi pete inachukua maana ya ziada, inafanywa kuwasilisha maana ya ziada, maana isiyo ya moja kwa moja, kwa mfano katika riwaya ya *Vita vya Mapenzi* na *Mzimu wa Waufi* pete imetumika kama taswira ya nguvu ya kijalaa za kuwakinga na kuwarahisishia watu mambo, kuwanyooshea matukio mbalimbali, mfano mzuri ni pete ya Sufian aliyokuwa anavaa Suhail ilikuwa ni kama kama ulinzi wao dhidi ya maadui zao.

Matumizi haya ya pete yametumika kijaala pale Mzee Sufian anapokuwa Yemen na ghafla anavamiwa na mahasidi wake akina Komandoo Takadir kwa ajili ya kumwangamiza Mzee Sufian na kuchukua pete. Lakini kutokana na pete ile kuwa na nguvu za kijaala na ilikuwa imevaliwa na Suhail ambaye alikuwa nchini Tanzania pete ile iliwaka miale myekundu ikiashiria kuna hatari kubwa sana inamkuta Mzee Sufian. Suhail anatumia pete hii hii kumsafirisha hadi nchini Yemen kwa muda wa dakika kumi na tano tu. Pia Masumbuko alipokuwa amewekwa mahabusu kwa ajili ya kuhisiwa kuhusika na mauaji ya Kishindo, pete aliyokuwa amevaa ilionyesha rangi nyekundu kuashiria hasidi wake Hunudu anakuja kumuangamiza. Kwa upande wa utajirisho pete hii imetumika kama chombo kinacholeta uchumi mkubwa katika himaya ya Budha. Serikali ya Budha inaitumaini kwa kiasi kikubwa na kuona hawawezi kupata maendeleo yeyote pasipo pete. Kwa hivyo, pete ni nguzo, mtaji na mfumo wa kupata mali, kitega uchumi.

Kupitia kazi teule za Mwingizi tunashuhudia kwa wingi uziada huo wa maana katika vitu mbalimbali.Uziada huu wa maana si kitu kinachojitokeza moja kwa moja ila ni kitu kinachojibainisha kiishara. Vivyo hivyo ndivyo ilivyo pale mtunzi anapowatumia wanyama na viumbe majini kama vile misukule na vivuli vya watu waliokwisha kufa. Uhalisi wa sehemu ya sanaa jadiya unaojitokeza katika uandishi wa kimajaribio na kihalisiajabu ambapo wahusika hao wamepewa majukumu ya kibidamu na wanahesabika ni sehemu ya maisha ya kawaida ya binadamu, ni mbinu iliyotamalaki katika riwaya za Mwingizi. Wahusika hao wana dhima ya kiishara vilevile kupitia utashihisi wao. Usanaa jadiya haupo peke yake bali tunakutana na usimulizi wa visaasili unaongazia maswala ya kiibada na matambiko.

Katika *Vita vya Mapenzi*, *Mzimu wa Waufi* na *Tanzia* kunafanyika matambiko ya jadi yenye kuashiria na kuelezea historia ya kikundi na mtazamo ulimwengu wao. Kitendo hicho kimezinyanyua riwaya za Maundu Mwingizi kuwa ni vielelezo vya mafunzo kuhusu majini, mizimu na wanga. Ni vipengele vya kitamaduni ambavyo kueleweka kwake kumekuwa katika hali ya uficho na kuhisihisi tu miongoni mwa wanajamii katika

nchi ya Tanzania. Ndani ya matambiko na ibada za jadi kuna taratibu za kuomba zenye kuchimuza miviga, mavazi na ishara mbalimbali. Hata hivyo, uishara haukujitegemeza katika taratibu za kijadi pekee, muingiliano wa tamaduni ngeni umepelekea kuingiza tamaduni za Kikristo, Kiislamu na umagharibi kiasi cha kufanya utambulisho wa jamii zilizokusudiwa katika riwaya teule na hasa Wanyamwezi wa Tabora na Waha kuwa na maingiliano na tamaduni nyenginezo. Tangu zamani vyanzo vya weledi wa maisha na utambulisho wa Mwafrika. Ni njia ya kuhifadhi historia na utambulisho na umekuwa ukitegemea sanaa kupitia ishara, hasa za wanyama wanaowakilisha asili ya watu, kupitia visaasili, miviga, lugha na majina.

Katika riwaya za Maundu Mwingizi kuna ishara nyingi zinazotumika. Zipo ishara zenye kumakinikia hali ya uasili wa mwanadamu na mwingiliano wa mifumo mbalimbali ya kijamii. Kwa mfano, wahusika huweza kuwakilisha vipengele mbalimbali vya jamii, ambapo wanyama, majini, mizuka kuweza kuteuliwa kuwakilisha majukumu yao kupitia ujumbe wa kiishara. Tukilinganisha na riwaya maarufu ya George Orwell ya *Shamba la Wanyama* ~~( )~~ tunaona wanyama kama nguruwe wanawakilisha viongozi walafi, na wanyama kama vile mbwa kuwakilisha vyombo vya dola na wanyama wengineo kuwakilisha wafanyakazi wavuja jasho ambao ndio wanaofanya kazi na kuhenyeka. Mwingizi naye anafuata mbinu kama hiyo ambapo badala ya wanyama anatumia wafu, mizimu, majini na misukule.

Wakati usimulizi wa Mwingizi umejikita katika miji halisi kama vile Tabora, Bagamoyo, Dar es salaam, Kigoma, Baharini, mibuyuni, maporini, mijini, sehemu hizo ni viwakilishi tu kwani ubaya, udhalimu, dhuluma, usaliti, na unyanyaswaji ni matendo bia yanayoweza kutokea katika sehemu yoyote ile duniani. Hivyo, uashirishaji unaweza kuwakilisha mfumo wa siasa, utamaduni na uchumi uliopo sehemu mbalimbali duniani. Kama Orwell (khj) anavyoweza kuwashangaza wasomaji wa pande mbalimbali za dunia na ndivyo hivyo naye Mwingizi anastahiki kuingia katika kundi hilo. Kwa misingi hii, fasihi inamtaka msomaji azame kwa kina katika fikra ili aweze kubaini ni nini kinakusudiwa katika usemi fulani au taswira fulani ina maana gani. Kuzama kifikra

hakuna budi kushawishiwa na kuwepo kwa ishara zinazoweza kumshughulisha msomaji. Uashiriaji unaweza kupatikana katika usimulizi wa aina mbalimbali kwani ni vigumu kwa kazi ya fasihi kukamilika bila ya kutumia aina fulani ya ishara. Uashirishaji ni matumizi ya ishara kuwakilisha mawazo ya kiajabuajubu, hisia na hali ya fikra katika sanaa au fasihi. Kazi za kiishara za kiuhalisia mazingaombwe zinaibua fikra za kimapinduzi zinazopingana na itikadi zilizozoeleka. Katika riwaya teule za Maundu Mwingizi, mtunzi huyu chipukizi amejaribu kuziibua dhamira mbalimbali kwa mtindo wa uashiriaji wa matukio madogo madogo.

Aidha uashiriaji huu unadhihirika katika riwaya za Maundu Mwingizi na ni muhimu kuzichanganua ili kuweka bayana dhamira na maudhui yake yanayoibushwa na ishara hizo. Mfano mmojawapo ni katika tukio la ajali katika riwaya ya *Vita vya Mapenzi* ambapo Mwingizi analitumia tukio hilo kuchimuza mtego wa kijaala ambao unamkumba Suhail unaotegwa na Mzee Sufian ambaye ni jinni. Mzee Sufian anatumia udhaifu wa Suhail wa tamaa ya pesa kumnasa ili amsaidia kupigana vita yake na majini wenziwe. Ili aweze kuzitumia pesa hizo anapewa sharti la kuvaa pete anayotakiwa aitumie kivita au kuvuta bahati. Sharti jingine gumu analopewa ni kumuoa Binti ya Mzee Sufian aitwaye Shekhia ilhali akiwa na mchumba wake wa muda mrefu aitwaye Sharifa. Kwa hivyo, katika hali ya ndoto na maruweruwe Suhail anatambua kuwa Mzee Sufian anamjia kimazingaombwe na hakuwa mtu halisi bali kiumbe cha ajabu kinachojiugeuzageuza. Tukio la ajali ingawaje ni la kiuhalisia lakini ndani yake kuna matukio yasiyo ya kiuhalisia kama vile kupewa begi jekundu lenye pesa lakini ni yeye peke yake ndio aliyeweza wa kuliona. Japo Suhail alikuwa yupo njia panda na haelewi begi lile mwisho wa siku litakuja kumgharimu kwani begi lile lilikuwa ni la rangi nyekundu likiashiria kwamba linadumishwa kwa misingi ya umwagikaji damu, linatolewa kwa Suhail katika hali na miktadha ya umwagikaji damu na kwamba, kutakuja kuwa na umwagikaji wa damu itakayotokana na matumizi ya pesa hizo.

Hivyo basi, begi hilo jekundu ni ishara ya hatari ambayo baadaye ilimpelekea hadi umauti wa Suhail. Kiubunifu, wekundu huu wa damu na hatari unatawala matukio

mengi katika riwaya nzima ikizingatiwa kuna idadi kubwa ya vifo na mauaji yanayojitokeza katika riwaya nzima, mifumo ya mahusiano ambayo karibu yote haina mwisho mwema, inaishia katika umwagikaji wa damu au kifo—angalia kilichomleta Sufian duniani kutoka himaya ya Budha, mahusiano ya kisiasa yaliyoishia kwa umwagikaji wa damu, ndoa ya Sufian na mkewe, mahusiano ya Msigwa na wenziye, mahusiano ya Joram na mtandao wake, damu—kifo, damu—kifo. Kwa upande mwingine, wakati Suhail akipanga hila za kumkwepa Mzee Sufian anajikuta anapambana naye katika ndoto na kiuhalisia. Hivyo basi, mtunzi katika riwaya zote hizi anatumia ishara tata katika usimulizi wake. Ishara hizo zinawakilisha hali ya kisiasa, kijamii na kidini katika jamii yake ya sasa.

### 5.4 Mbinu za Kiishara na Uashiriaji katika Riwaya za Maundu

Mwingizi ametumia ishara kwa wingi katika riwaya zake teule kwa mfano, katika riwaya ya *Vita Vya Mapenzi* ambapo amejiegemeza katika muktadha wa Tanzania bara na miji ya Dar es salaam, Dodoma, Morogoro, Tabora na kitongoji cha Bagamoyo. Safari ya Suhail Bin Kusekwa kutoka Dar es Salaam hadi Tabora inakumbana na masaibu ya ajali ya ajabu ya kupangwa. Mpangaji anayekufa kifo cha hadaa ni Mzee Sufian ambaye anamlenga Suhail ili atimize malengo yake ya kumsaidia kupigana vita na majini wenziwe huku akimlinda Binti yake Shekhia. Safari hiyo ni ya kiishara na pale anapopotea kimiujiza huku akiwa tayari amekwisha mkabidhi mkoba mwekundu wenye pesa na pete ya ajabu ya *Khatam Budha*. Kwa nini safari hii ni ya kiishara? Kwa sababu lengo la safari hii lilishakuwa limepangwa kwa ajili ya kusabaBisha mauaji ili hatimaye Mzee Sufian aweze kumkabidhi Suhail pete na kuwekeana mikataba mbalimbali ya kumuoa Binti yake. Hivyo basi, Suhail na wasomaji wanagutushwa kuwa safari hiyo ilipangwa. Ni safari ya kuashiria makabidhiano ya mkataba kati ya mwanadamu mteule wa dunia halisi na dunia ya ujini. Kinachofanikisha hayo ni hulka ya usaliti, uongo na tamaa ya wanadamu ya utajirisho. Sifa za Suhail zilizopelekea kuchaguliwa na Mzee Sufian kuwa mrithi wa pete na mkwe wake ni kule kuwa na nyota ya ‘Shamsi” (jua) ambayo ina uwezo wa kuwaangamiza majini. “Nyota ya *Shamsi* ni nyota yenye nuru ya jua (uk. 55)” katika elimu ya unajimu.

Vilevile, kwa upande wa riwaya ya *Tanzia*, kuna ada na miviga ya kichawi inayoelezwa kwa kina kwa njia ya uashiriaji. Wachawi wana taratibu za kiishara wanazozitumia katika utekelezaji wa ibada zao. Ishara huanzia kwa mtoto anapozaliwa hadi vifo vya mauzauza na misukule. Kuna taratibu za mwanamke kiongozi wa kichawi kuoa mwanamke mwenzake na kumpatia ujauzito kwa njia ya kimiujiza na kuzaliwa mtoto aitwaye "Nyembo" ambaye anakuja kuishi maisha halisi na anakuwa ni chimbuko la anguko la mtandao wa uchawi huko Kibondo baada ya kugundua siri yao kupitia kibuyu alichokiacha Bi Masonganya. Riwaya imelandana na (anuani) jina la kitabu *Tanzia* kwani matukio ya ajabu ya vifo, na misukule yanayoleta hofu na mashaka, misiba ya maajabu, ikiwa imegubikwa na siri katika ndoa ya mke kwa mke (uk. 56), kifo cha Bi Masonganya, mjukuu wake kurithi mkoba wa kichawi, na siri ya vifo vya mfululizo. Vifo vyote hivyo ni vifo vya kiishara ambapo wafu wanakuwa katika dunia ya uhalisi na udhanifu.

Katika *Mzimu wa Waufi* (2013) usimulizi umejikita katika ishara zenye nguvu ya ujaala zinazotawala mustakbali wa maisha ya mhusika mkuu Masumbuko ambaye anaishi kama mnyama anayesakwa kuuawa na yeye akiwa ni mtu wa kufanya jitihada za kuwakwepa wawindaji wake. Tabia yake na mustakbali wa maisha yake haupo mikononi mwake pekee. Anatizamwa na nguvu zilizopo juu yake, nguvu za kijaala zinazowakilishwa na pande mbili zinazovutana; mzimu wa Waufi na mzimu wa Waswezi. Masumbuko anawakilisha jitihada za watu wasio na hatia na wasio na upande wowote wanaounga mkono wakivutwa na nguvu hizo za ujaala. Nguvu hizo zipo ndani ya mifumo ya itikadi za dini ya Kikristo na Kiislamu. Mwandishi anataka kutuonyesha kuwa dini za kigeni na zile za asili zina maingiliano na si rahisi kwa zile za kigeni kuzifuta zile za asili moja kwa moja. Migongano ya itikadi za kidini na kimitazamo inakuja kuunganishwa na kupunguzwa nguvu zake wakati mwandishi anapoonyesha suluhisho kuwa ni kuishi pamoja bila ya kubaguana katika misingi ya itikadi ya mtu kupitia ndoa ya Judith na Masumbuko.

Kwa ujumla kupitia riwaya hizi teule, mtunzi Maundu Mwingizi anatumia ishara mbalimbali kufumbata dhamira zake na kuwafikirisha wasomaji ili kuwafahamu wahusika na matendo yao. Motifu ya pete, motifu ya safari za ajabu, uzazi wa kiajabuajabu, mashtaka, utajiri, ndoto na ukwepaji wa ujaala inakuwa ni sehemu ya masimulizi yake. Kwa ujumla, Mwingizi anatumia motifu ya kifo na ufufuo kama kielelezo cha kutokuzika fikra za udhanifu zinazotawala maisha ya kila siku ya wanajamii. Anaonyesha kuwa fikra hizo hazijali kuwa mtu amejiunga na dini mpya au amekuwa mwanasiasa au msomi. Elimu, siasa na itikadi zote zimeathiriwa na mfumo fikra wa jadi unaotafsirika kama ushirikina lakini wenye mashiko kwa wanajamii wa rika mbalimbali, jinsia, tabaka, na itikadi. Vilevile katika riwaya hizi kupitia anuani zake, *Vita vya Mapenzi*, *Tanzia* na *Mzimu wa Waufi*, mwandishi anawadokezea wasomaji wake kuwapo katika hali ya misuguano, vifo na imani ya jadi ya maisha baada ya kifo.

Kimsingi, majina yanatabiri muktadha wa kitamaduni na migongano ya wanajamii. Mwingizi anaandika katika karne hii ya utandawazi na usasaleo akiangazia maswala ambayo pengine yangechukuliwa kuwa yamepitwa na wakati. Swala la mizimu ni ukumbusho kuwa jamii yake bado inazo taswira za kimetafizikia zinazoizonga. Hivyo ustaarabu wa mwafrika hauwezi kutenganishwa na imani yake ya jadi. Uteuzi wa anuani hizo zinazolandana katika riwaya zake teule unawakumbushia wasomaji kuwa bado jamii yao ipo katika lindi la mawazo na mifumo ya kijaala. Kwa upande mwingine, mwandishi anajivunia historia na mila yake inayoingiliwa na tamaduni za kigeni. Anafikisha ujumbe huo kwa njia ya kuchanganya mandhari na usimulizi unaorejelea usasa na mseto wa ukale kwa kunyesha kwamba maisha ya wanajamii yake ya sasa yamefungana na mifumo kale ya ujaala. Anabaini mifumo hiyo na jinsi inavyorithishwa kutoka kizazi hadi kizazi. Anachoshindwa mwandishi ni kubaini waziwazi kuwa mfumo jadi na fikra za kishirikina, mduara wa kijaala wa ufufuo wa nafsi, kuzaliwa upya, na imani ya mizimu imetokomea kabisa kupitia suluhisho na uangamizo wa Bi Masonganya, Mzimu wa Waufi na Himaya ya *Budha*. Je, vifo vya Mzee Sufian, Suhail, Komando Takadir Al Harabi, Masumbuko, Bi Masonganya, Kaguba, Mtandao wa Black

Scopion, Meno ya Dhahabu (Joram Ndege), na wengineo ni suluhisho la kudumu la ubadhirifu wa mali, wivu, ushirikina na uonevu? Je, kizazi cha kesho kirithishwe mifumo ipi ya thamani na itikadi kwa sasa? Imani ya Waafrika juu ya mizimu, uchawi, misukule, majini, bahati kupitia pete, iendelee au itokomezwe? Ni kwa vipi utandawazi ni suluhisho la mapinduzi ya kifikra na kitamaduni katika dunia ya mwandishi? Mfumo wa ubepari unaosisitiza ubinafsi na ulimbikizaji wa mali kama unavyodhihirika katika riwaya ya *Vita vya Mapenzi*, unazifaa jamii za kiafrika?

Kwa upande mwingine mifumo ya dini na itikadi ngeni zinaboresha au kudumaza fikra za vizazi vijavyo? Majibu ya maswali haya ni sehemu ya majadiliano yetu ya sababu za matumizi ya ishara mbalimbali katika riwaya za *Vita vya Mapenzi*, *Tanzia* na *Mzimu wa Waufi* katika sehemu ya 5.4.1 hii katika Riwaya teule za Maundu Mwingizi zinampa msomaji uwanja mpana wa kuzitafsiri ishara kwa mujibu wa lugha aliyoitumia mwandishi na upana wa mawazo yake. Usimulizi wake umejaa ishara na uashiriaji ulioibuliwa kutoka katika visaasili, historia na mitazamo ya kimaadili. Ishara kuu anazozitumia Mwingizi zimejadiliwa kwa undani katika sehemu zifuatazo.

### 5.4.1 Kifo kama Ishara na Uashiriraji

Jambo moja linalojitokeza kwa kiasi kikubwa, kwa upana na urefu katika riwaya teule za Maundu Mwingizi ni kifo, si hoja vifo vilivyopo vinasababishwa na nini. Msambao huu mpana wa vifo unaishia kumfanya msomaji kujiuliza maswali kwa nini vifo vingi jinsi hii? Kuna vifo kutokana na mauaji, vifo vinavyosababishwa na magonjwa, vifo kutokana na uchawi na umajini, kuna vifo halisi na vifo vya kinjozi. Wingi huu wa vifo unaelekea kushawishi chukulizi kuwa vifo vinatumika kueleza uhalisia wa maisha na vilevile vifo vinatumika kimkakati kama ishara inayochimuza maswala, dhamira na maudhui ya aina nyingi.Wingi huu wa vifo unashiwishi pia chukulizi kuwa katika riwaya za Maundu Mwingizi, kuna motifu tawala ya kifo. Kwa hivyo, uashiriaji wa dhana ya ufufuo na maisha baada ya kifo umetamalaki. Sababu za utukiaji wa kifo ni nyingi na zinazosukumwa na mambo mseto kama chuki, wivu, tamaa za ki binadamu na viumbe jini vinapewa nafasi kubwa katika riwaya hizi teule. Mwingizi anakihoji kifo na

maisha kwa ujumla, katika muktadha mpana wa mzunguko wa maisha na maisha baada ya kifo.

Kifo kinabebeshwa ishara mbalimbali katika jamii ya Maundu Mwingizi, kama ilivyo katika kazi mbalimbali za fasihi. Motifu ya kifo katika riwaya ya *Tanzia* imeanzia kwenye anuani ya kitabu ambayo inaashiria kifo. Dhana nyenginezo za *mkanyafe* (mkufu wa kifo), *vibumbasi* (majani ya kupoza makali ya kibuyu cha *sambamfinyu*), kibuyu, pete, chungu cheusi, rangi nyekundu na nyeusi, kofia, pete, vilemba, kitambaa, begi, mawingu na kiza, vimbunga, kivuli cha wafu, musukule, kukatwa ulimi, shanga nyekundu, nyama za watu, mti wa *mpigi* (wa kuongeza maisha), damu ya kafara, usinga, matambiko, mizimu, radi, ng'ombe wa kafara, na moshi. Mtunzi anaona kifo ni siri nzito inayowasumbua wanadamu. Kuna kila sababu za kutafuta sababu za kifo iwe ni kwa uchawi au maradhi ya kawaida. Wanajamii wana jukumu la kufanya jambo lolote lile kukicheleweshа kifo lakini umri unapozidi mno ina kuwa kero kwa wanajamii kama ilivyotokea kwa Bi Masonganya katika *Tanzia*.

Kifo kinaoanishwa na dunia mbili—dunia ya baharini na ile dunia ya bara. Katika dunia ya baharini kuna viumbe majini ambao kifo chao si cha kuzikwa makaburini au ardhini bali ni kwa njia ya kuchomwa moto na kuwa majivu. Katika upande wa viumbe vya bara wakiwemo wachawi, na watu wa kawaida wao hufa kwa njia nyenginezo na kuzikwa makaburini. Katika *Tanzia, Vita Vya Mapenzi* na *Mzimu wa waufi*, wahusika mbalimbali kama vile Nyanzala, Masumbuko na Suhail wanaoteshwa ndoto zinazonasibishwa na vifo. Mawasiliano ya kijaala yanayotoa maonyo ya maafa yanayotarajiwa. Si ajabu kwamba, kwa mapana na marefu ya riwaya hizi, lugha ya mwandishi imetawaliwa na sitiari, na semi zinazochimuza na pia zinazoakisi vifo kama vile;

a) Ukimwona nyani Mzee porini ujue kakwepa mishale mingi (uk. 54, MW)

b) Dhoruba ilipo ndipo shwari ilipo (uk. 54, MW)

c) Hakuna ajuaye kesho hata mtunzi wa kalenda (uk. 3, T)

d) Mfu aliye hai (uk.10, T)

e) Nyoka ndani ya mtungi wa udongo (uk. 29,T)
f) Kunguru mwoga huishi miaka elfu moja (uk. 39.T)
g) Kitanda usichokijua hukijui kunguni wake (uk. 40 ,T)
h) Mwanamume kwa mwanamke ni sawa na mfupa kwa fisi (uk. 41,T)
i) Ukitaka kumuua nyani usimwangalei usoni (uk. 45,T)
j) Siku nitakayolalia mkono kaburini (uk. 92, VM)
k) Suhail na Sharifa wakawa mithili ya chui na paka (uk. 116, 149 ,VM)
l) Akumulikaye mchana usiku atakuunguza (uk. 170, VM)

Mifano hii ya semi, methali na vijembe iliyotumika katika riwaya za Mwingizi yote kwa pamoja inasisitiza kuwepo kwa mahusiano hasi, uadui, kifo, moto, ufu, dhoruba, na maafa ya kila aina. Si semi zinazoonyesha hali ya amani na upendo. Hivyo zinaashiria tanzia kwa ujumla.

Ngano ya ng'ombe wa kafara ambapo Masumbuko anageuzwa kihila kuwa ngombe wa kuliwa kijini ni sehemu ya uashiriaji wa vifo katika riwaya ya *Mzimu wa Waufi* (uk 107-109). Matangazo ya vifo (tanzia) kupitia spika za misikitini (uk. 15) na kwa wapiga mbiu (uk. 53) katika riwaya ya *Tanzia* zinajielekeza katika kuleta habari za huzuni tu na wala si taarifa za furaha katika masikio ya wasomaji. Riwaya zimejaa kelele za vifo na mateso ya maumivu makali; "YALAAH.. UWIII NAKUFAA JAMANI (uk. 51T), kelele za TANZIA..! TANZIA…! TANZIA…! (uk. 53), sauti ya maumivu ya Kaguba alipobanwa na Nyembo kupitia kibuyu "Akkhhhh! OHHHHHHKH KHHHHH NA KUFAAAAA.." (uk. 63 T) au YUKO CHOONI ANATAKA KUNIMALIZAA AKKHH Uhuuaakh! Uk.67 T) na UWIIII JAMANI TUNAKUFAA NYANZALAAA!" (uk. 69 T). Na katika *Mzimu wa Waufi* mwandishi anatumia herufi kubwa kuwatahadharisha juu ya hatari inayowakabili kwa kauli ifuatayo: "TAWANYIKENI JAMANI HUNUDU WA WAUFI HUYO! (uk. 214 MW).

Vifo vimetapakaa na damu inamwagika katika riwaya hizo. Wasomaji wanaona damu za Masumbuko, Amanda, Mzee Sufian, Suhail, Nyanzala, Babu Mtandi, Msigwa, Karim

bucha, au Joram Ndege. Wahusika wengi wanahusika katika maombolezo, wengine ni wahanga wa maafa, na wengine wako katika kundi la wauwaji (Bi Masonganya, Jemadari Takadiri, Nyembo, Kaguba, Binti Sambayu, Babu Gao na Joram Ndege). Kila tukio lao linaandamana na umwajikaji damu. Ishara ya vifo ndiyo inatawala katika riwaya za Mwingizi. Msomaji anaachiwa fikra za kifo na hatima ya maanguko kwa watu au viumbe waovu. Dhana za kifo, roho na nafsi hazikwepeki katika maandiko ya Mwingizi na fasihi ya Kiswahili kwa ujumla. Uchunguzi wa utokeaji wake unathibitisha umuhimu wake. Mfano mzuri katika shairi la Mulokozi & Kahigi (1995:2). Katika shairi la'**Vuteni Makasai'**; ambapo kifo kimepambwa kama jambo linaloogofya ambapo mabaharia wanaaswa kujiokoa nacho;

"Mungu mwenye enzi ametujalia!"
Amiri wao mwongofu akalia,
"Rabsha hii ametuondoloea,
Adha ya mauti katupitishia!"

Roho imechorwa kama kitu kinachotoka na kurudi ndani ya mwili. Kuna kivuli cha mwanadamu ambacho kinaweza kuwepo duniani kikitembea na kwa wenye macho wakaona ni kiwiliwili halisi. Hali imeonekana kupitia Marehemu Nyamizi katika *Mzimu wa Waufi*. Usemi wa usinirushe roho ni maarufu. "Na roho yangu yote umeirusha" Mulokozi & Kahigi 1995:16). Katika Shairi la **Dawa Mbili** wanazungumzia fumbo la mtu aliyetaka kutafuta dawa ya maisha;

Dawa ya kago la mauti asife.
Palipo na giza na matope pia
Na kifo daima chakufuatia (1995:27).

Dawa hiyo aliipata Bi Masonganya katika riwaya ya *Tanzia* (uk. 7) anatumia mti wa *mpigi* anaweza kuishi hadi pale alipotapishwa. Na pia tunamwona Mzee Sufian "anakufa" na kufufuka. Teknolojia ya misukule nayo ni mazingaombwe ya vifo, ambapo katika macho halisi watu wanakuwa wamekufa lakini kwa walio na utalamu wa ulozi kinakuwa ni kivuli tu wanachokiona. Watu wanaweza kufa kiishara tu badala ya kufa kihalisia. Kwa njia hii, Mwingizi anajiingiza katika mjadala tata wa maswala ya kifo bila kujibana katika falsafa maalumu kama walivyo waandishi kadhaa wa fasihi ya Kiswahili.

Wasomaji wa kazi za Kezilahabi wamekuwa wakishangaa namna anavyolivalia njuga swala zima la kifo japo wasomaji huona kwamba Kezilahabi anaona maisha hayana maana kutokana na mtazamo wake hasi kutokana na maisha. Na kwa upande mwingine, Kezilahabi amejikita katika falsafa ya udhanaishi inayomfanya mwanadamu aone maisha hayana maana. Japo sehemu kubwa ya maandishi yake yamejikita katika kujadiliana ana kwa ana na taasisi hiyo. Ingawa hatoi majibu ya moja kwa moja, kutokupata majibu kutoka dhna ya kifo kunamwacha msomaji na dukuduku na hofu ya kuwa bado taasisi hiyo haishikiki. Na kwa upande wa Mwingizi yeye anajikita zaidi katika kukizungumzia kifo kama njia ya kumwacha mtu katika njia panda. Wakati mwingine kifo kwa Mwingizi kimetumika kama ishara ya ukombozi kwa hivyo waandishi hawa wanaothubutu kuichokoza chokoza ili mradi tu waondoe hofu yao wenyewe juu ya dhana nzima ya kifo na roho na hatimaye tunaona kazi zao zote zimetawaliwa na dhana hii na na hiyo yote ni kutokana na kwamba, waandishi hawa wote ni wanamajaribio.

Mwingizi anahoji mamlaka na kazi za Mungu katika *Vita vya Mapenzi* na uwezo wake wa uponyaji: “Hivi Mungu huyu aliweza kuumba mbingu na kuitandika angani bila ya kuweka nguzo inayoonekana kuizuia atashindwa kukuponya wewe? (uk. 263). Maswali mengi hayajibiwi, kwa mfano kwa nini tunakufa, tunakwenda wapi baada ya kifo, roho ni nini? Je, nafasi ya roho kwa mwili ni ipi? Kuna sehemu chache tu ambapo Mwingizi anajaribu kutoa madokezo ya namna ya kuwaua majini tofauti na kuwaua wanadamu. Je, majini ni ishara ya akina nani? Mabeberu au mifumo ya tafakuri? Mwingizi anazipitisha hukumu kwa waovu hapa duniani kupitia riwaya zake. Hasuburi kesho hivyo himaya ya Waufi, Mtandao wa *Black Scopion*, Wachawi wa Kibondo, wanaangamia katika riwaya zake. Huko ni kutoa suluhisho jepesi. Je, dunia yake inaelea katika amani, haki na ukweli?

Kivisto (2014) anasema kwamba, wanafasihi wengi hutumia vifo katika kazi zao za fasihi kama kipengele kimojawapo katika maisha kwa lengo la kuashiria matukio mbalimbali yanayotendeka katika jamii. Kivisto anaendelea kusema kwamba, kifo

katika fasihi ya kimajaribio na kihalisiajabu hubeba maana zaidi ya moja kwa lengo la kumfikirisha msomaji kwenda mbali zaidi kuhusu matukio mbalimbali katika jamii. Kwa hiyo, tunaona pia katika riwaya za kimajaribio za Mwingizi kifo kimetokea kikiashiria maana mbalimbali na kuibua maudhui mbalimbali. yanayoashiriwa kupitia ishara hiyo ya kifo. Hivyo mtunzi ametumia ishara mbalimbali za kifo katika kuashiria mambo mbalimbali kama ifuatavyo:- kwanza, ishara hii ya kifo imetumika kama kitu cha kuangamiza mataifa ya ulimwengu wa tatu. Mfano, katika uk. 10-11 katika riwaya ya *Vita vya Mapenzi* mtunzi anamwonyesha Mzee Sufian amekufa baada ya kumpa Suhail pesa na kumpatia masharti mbalimbali ili aweze kuyatekekeza na anakufa wakati Suhail hajaelewa vizuri hayo masharti ambayo anampa ya kumuoa Binti yake ambaye ni jini. Kifo kinatumika kama ishara kuashiria hali ya kumuacha mtu katika njia panda na hali unafahamu fika kuna kitu kizuri unakitaka kutoka kwake. Mzee Sufian alikufa katika ajali ile ya basi kimajini na kumuacha Suhail njia panda lakini mwisho wa siku alifufuka na kumtaka Suhail aendelee kutekeleza masharti waliyokubaliana japo Suhail alikuwa haelewi ni masharti gani.

Mtunzi kupitia ishara hii ya kifo anachimuza dhamira ya mikataba mbalimbali ambayo huwahusisha watu na watu katika familia, ukoo, jamii na hata kujenga mahusiano ya kimataifa. Kwa mfano, mataifa ya ulimwengu wa tatu ambayo viongozi wake wanashinikizwa au kushawishiwa kusaini mikataba wakiwa hawaelewi vizuri mikataba hiyo inahusu nini hasa halafu uhalisi wa unapoanza kubainika, mikataba hiyo inawaangamiza na kuwaacha njia panda na ilhali mataifa haya yaliyoendelea, yaliyo na uwezo na mamlaka yanaendelea kuneemeka. Vilevile mtunzi ametumia kifo kama ishara ya watu kujifunza. Suhail aliugua ugonjwa wa kimajini usiojulikana kutokana na kwamba alishindwa kutimiza masharti ya kuwauwa ndugu zake ili damu zao ziendelee kuleta mali nzaidu. Kutokana na kushindwa kutimiza masharti hayo inamlazimu afe yeye mwenyewe na kuziacha mali alizokuwa anazidhibiti.

Kwa hiyvo, mtunzi anaonyesha kifo kuwa ishara ya kuiasa jamii kwa wale wanaopenda utajiri kwa kutumia njia zisizo halali. Kwamba, wajifunze mwisho wake huwa ni

mbaya. Aidha kifo kimetumika kama adhabu kwa wale wanaoenenda kinyume katika maswala mbalimbali kupitia kwa mhusika Suhail. Kwa upande mwingine kifo cha Suhail ni ishara na hatima ya maisha ya Suhail hapa duniani. Mtunzi kupitia kifo hiki anaashiria kwamba, unaweza ukafanya mambo mengi sana ukiwa hai, yaani ukawa muongo sana kama alivyokuwa Suhail, ukawa laghai sana kama alivyokuwa Suhail lakini kifo ndicho kitakachokuwa hatima ya mambo yako yote mazuri au mabaya. Mtunzi anaonyesha kifo cha Mzee Sufian pia katika riwaya ya *Vita vya Mapenzi* kama ishara tosha katika kuchimuza maudhui ya madhara ya ulaghai. Kifo chake cha pili cha jini huyu kilitokea nyumbani kwa Suhail akiwepo na Mzee Fungameza ambaye yapata miaka mingi alidhulumiwa mke na Mzee Sufian kutokana na kumpa pesa nyingi mke wa Fungameza aitwaye Amanda. Mtunzi anaonyesha kwamba yawezekana mataifa yaliyoendelea yatakuja kujutia kwa ulaghai zinayofanyia mataifa yanayoendelea. Hali kadhalika katika riwaya ya *Vita vya Mapenzi* mtunzi anaonyesha kifo cha Joram Ndege na Msigwa ni vifo ambavyo vinaashiria dhamira ya ukombozi katika serikali na katika jamii. Msigwa anakufa akiwa katika kundi la *Scorpion* na aliuliwa na Joram Ndege kwa ajili ya kuchanganya kazi zake binafsi na kazi yao.

Pia Joram Ndege anakufa kwa ajili ya tuhuma za kumuua Msigwa na kushirikiana na mawaziri katika idara nyeti ambayo wanatumia mali za wananchi katika kujineemesha wenyewe.Vifo hivyo vya Joram na Msigwa vilipelekea viongozi hawa wabadhirifu wa mali za umma kufungwa kifungo cha maisha na serikali na wananchi wanufaika na maliasili zao. Kwa hiyo, vifo hivi vinachimuza dhamira ya ubadhilifu wa mali ya umma na kujilimbikizia mali kwa kushirikiana na wahalifu yaani wauwaji katika kutafuta nafasi mbalimbali mamlakani. Katika hali hii, mtunzi anatumia kifo kama ishara inayokita kuwili—kifo kama chanzo cha kuasisiwa neema ya pamoja na kifo kama kikomo cha dhuluma, maonevu na wizi wa haki.

Aidha mtunzi ametumia ishara ya kifo (uk.185) katika riwaya ya *Mzimu wa Waufi* anapomuonyesha Mzee Kishindo amekufa kwa kupigwa radi kiuchawi na jini Hunudu akiwa na Masumbuko porini wakati anampeleka nyumbani kwao kwenye mizimu ya

mababu zake. Kifo cha Mzee ni ishara ya ukombozi kwani baada ya kufa Mzee Kishindo, ilimbidi Masumbuko ahangaike mpaka ahakikishe anaenda kuonana na mizimu ya babu zake kutokana na kuteseka kwa muda mrefu na hatimaye kufanikiwa kuwa kiongozi wa Waswezi ambao wameteswa kwa muda mrefu na Waufi. Kwa upande mwingine, kifo hiki cha kiajabu cha Mzee Kishindo kinachimuza ubedhuli na roho mbaya waliyokuwa nayo wanasiasa pindi wanapotaka nafasi katika nyadhifa mbalimbali serikalini ambapo hutumia hata mbinu ya mauaji katika kulinda nafasi zao.

Pia mtunzi anaonyesha ishara ya kifo katika riwaya ya *Mzimu wa Waufi* (uk.118) pale ambapo Hunudu anapompiga Nyamizi kwa panga na watu wote wakajua Nyamizi amekufa. Askari wanafika pale na kutaka kumpeleka katika chumba cha kuhifadhia maiti bila ruhusa ya daktari. Kifo hiki cha Nyamizi japo alikuwa hajafa alikuwa amezimia tu, ni ishara ya kuchimuza ujumbe wa polisi kutokutumia nguvu na kutoingilia taaluma za watu mahali ambapo si sahihi. Askari wa wanaingilia taaluma ya kitabibu wakati wao sio madaktari na kung'ang'ania kumpeleka katika chumba cha kuhifadhia maiti mtu ambaye hajafa. Ilitakiwa madaktari wampime kama amekufa au ni hai. Mtunzi anaonyesha jinsi askari wanavyotumia zaidi nguvu badala ya akili katika sehemu ambazo hazihitaji nguvu. Kupitia kifo cha Nyamizi mtunzi anataka kutuonyesha jinsi polisi wanavyotumiwa na wanasiasa katika kuwanyanyasa wananchi wasiokuwa na hatia kabisa. Nyamizi alikuwa katika utawala wa Waswezi; utawala ambao ulikuwa unaonewa sana na mahasimu wao Waufi.

Fauka na vifo hivyo vilivyotangulia, Mwingizi katika riwaya ya *Tanzia* ametumia kifo kama ishara ya njia mojawapo ya kuleta ukombozi katika jamii ile ya Kibondo iliyokuwa imetawaliwa na uchawi uliokithiri kuanzia kwa watoto wanaonyonya. Katika uk. 1, mtunzi anamuonyesha marehemu Bi Masonganya amekufa lakini wanapokwenda kumzika anafufuka kwa sababu hajakaBidhi uchawi wake kwa mtu mwingine. Kutokana na uelewa anaoibusha mtunzi ni kwamba kwa mujibu wa sheria za kichawi, mchawi yeyote anayekufa sharti akabidhi uchawi kwa mtu mwingine kabla hajafa. Hii inaashiria taratibu na tamaduni za kurithisha mamlaka, wajibu au nyadhifa. Lakini

kuhusiana na kifo cha Bi Masonganya, mtunzi anaonyesha kuwa kifo hiki kilikuwa ni ishara ya ukombozi kwa sababu mtoto aliyemwachia au aliyerithishwa uchawi ule alizembea zikagundulika njia zake zote pamoja na wachawi wenziwe na kupelekea hata ugomvi wachawi wote wa Kibondo kukamatwa. Kifo cha Bibi huyu kimechimuza dhamira ya ukombozi kwa sababu aliwauwa na hata wafanyakazi wa serikali kama majaji wawili na watu wengine katika jamii ya Kibondo. Ukombozi huu Unaweza kuowa ni wanajamii, kuzinduliwa na kuondoshwa katika tamaduni za kishenzi; tamaduni zinazowakwamisha watu katika kutafuta heri ya maisha, tamaduni zinazopinga maisha na kukwamisha maendeleo.

Kwa upande mwingine, mtunzi ametumia kifo kama ishara ya kuona kwamba maisha hayana maana kwani Suhail alikuwa anaugua ugonjwa ambao ulimuhangaisha bila kupata tiba. Pamoja na kwamba, alikuwa tajiri, ugonjwa huo wa kimajini ulimtesa sana mpaka akafikia hatua ya kukata tamaa. Ukimrejelea Kierkegard (1849) na wenzake wanaona kwamba maisha hayana maana kama maisha yangekuwa na maana basi Suhail angepona. Kwa hivyo kifo katika riwaya hii ya *Vita vya Mapenzi* kinachimuza dhamira ya kifo hakichagui mtu yeyote yule hata kama ni tajiri utakufa tu. Hivyo basi, maisha yana usambamba na mlandano na kifo, kifo hakijui tajiri, kifo hakijui maskini. Ndio maana tunaonyeshwa nyumbani kwa Suhail katika uk. 263 kukiwa na kila kitu cha thamani isipokuwa ugonjwa ndio unaomtesa kiasi cha kuashiria kwamba maisha hayana maana. Kwa jumla, mwandishi ameonyesha vifo vinavyotokana na umajini, uchawi, ulozi, kiinimacho kama ishara mbalimbali za ukombozi kwa wanajamii wanateseka. Maswala ya uchawi na kuwakamata wachawi wote na kuacha kizazi kisicho na wachawi ni kati ya ishara hizo. Maswala haya ya uchawi, ulozi au kiinimacho, huwa yamejenga imani, tamaduni, falsafa na mitazamo ya ulimwengu iliyo na athari hasi kwa kiasi kikubwa. Kwa hiyo, ishara hii ya kifo imetumika kama mbinu ya kuwakomboa watu kutoka katika minyoronyoro fulani fulani ya kiimani na kimtazamo.

### 5.4.2 Njozi kama Ishara na Uashiriaji.

Mwaingizi ameweka wazi tofauti baina ya uhusika wa kimazingaombwe na ule wa kiuhalisia Anajaribu kuichora jamii yake inayoogelea katika dunia zote mbili. Jamii

yake inashindwa kutenganisha miktadha hiyo miwili ya kiuhalisia na kimazingaombwe. Katika hali ya mseto huu Suhail anapambana na Mzee Sufian katika ndoto. Anapoamka badala ya kuchukulia kuwa hiyo ilikuwa ni ndoto tu au jinamizi yeye anazifasiri ndoto hizo kuwa ni za kweli na ujumbe wake ni halisi. Hivyo anakuwa anaishi katika dunia mbili kwa pamoja ambapo ndoto inachukua nafasi ya mawasiliano halisi ya kiishara kati ya viumbe vya kimazingaombwe na viumbe halisia. Mtunzi kwa kumweka Suhail katika hali hii tatanisha, inaashiria kwamba mtunzi analizamia swala la vishawishi na mihimili inayochangia kufanikiwa kwetu maishani au kushindwa kwetu. Kuna uwezekano mkubwa ziko sababu zilizo nje ya uwezo wa binadamu lakini sababu nyingine za mafanikio au kushindwa kwetu kama binadamu zimo katika akili zetu kwa kuzingatia jinsi tunavyoufasiri ulimwengu, jinsi tunavyofikiri na kukabiliana na matatizo au shida za maisha yetu. Kwa hivyo, baadhi yetu tunaamini uwezo wa kubadili na kuyapa mwelekeo maisha yetu upo mikononi mwetu na wengine wetu huamini kila litutendekealo ni majaliwa.

Kuna wahusika wa kinjozi katika riwaya teule za Mwingizi. Hawa ni wahusika ambao wanahusianishwa kwa kiasi kikubwa na njozi au fantasia. Wahusika Mzee Sufian na Komandoo Takadir katika *Vita vya Mapenzi* na Hunudu katika *Mzimu wa Waufi* ni wahusika wa kinjozi na viumbe wasiokuwa wa kawaida. Wana uwezo usio wa kawaida kama vile kuruka angani kwa kasi, kuwangamiza maadui zao bila ya kuonekana katika njozi tu na wana uwezo wa kujigeuza maumbile yao. Mhusika Masumbuko katika riwaya ya *Mzimu wa Waufi* anapewa jina linaloakisi historia ya uzazi wake uliokuwa wa shida na uliopatikana kwa taabu. Historia ya uzazi wake inatokana na mama yake Bi Kapemba aliyekuwa hana uzazi. Aliamua kwenda kwa Mzimu wa Waufi kuomba mtoto. Lakini sharti alilopewa na mizimu hiyo ni la kumtoa kafara mtoto huyo wa kwanza. Anakataa kutenda hilo kwa mapenzi ya mtoto wake; badala yake anatoa sadaka inayokubaliwa kwa masharti kwamba, atakapopata wajukuu, awatoe kafara. Baada ya Masumbuko kupata watoto “Mzimu wa Waufi unahitaji kafara yao” (uk 88).

Motifu ya njozi imetawala kazi zote za Mwingizi. Msomaji anavutwa kuunganisha njozi na uhalisia kiasi cha kushindwa kubaini kile kinachotokea haswa pale viumbe kama majini au wachawi wanapokuwa na mawasiliano na binadamu wa kawaida. Suhail anatokewa na Mzee Sufian katika njozi na kupewa amri na kuteswa kwa njia hiyo pale anapoonekana akitaka kukwepa kufuata masharti anatokewa na ndoto. Mfano katika riwaya ya *Vita vya Mapenzi* mtunzi anasema;-

> "Kama utakuwa makini sidhani kama yatakayotokea kama yale ya kule nyumbani kwako Mbezi. Kauli ile ikamfanya Suhail sasa athibithitishiwe kichwani mwake kuwa lile tukio lilimtikoea usingizini lilikuwa ni la kweli kama alivyoamini,uk 64)"

Motifu ya ndoto inatawala kazi za *Vita vya Mapenzi, Tanzia* na *Mzimu wa Waufi*. Hunudu anamtokea Masumbuko kindoto katika *Mzimu wa Waufi*. Matumizi ya njozi katika riwaya za Mwingizi yanaweza kuangaliwa kuwili; kama kiashiria cha maudhui na dhamira na kwa upande mwingine, kama kiashiria cha kiubunifu. Matumizi ya njozi yanampa mtunzi uhuru na mwanda mpana na kusema chochote na kwa njia yoyote ile, kusema kilicho halisi na kusema kilicho katika uwezekano wa kufikirika. Njozi inawezesha mambo ya mbali kuletwa karibu na ya karibu kupelekwa mbali kama inavyodhihirika katika ndoto za Suhail.

Katika *Tanzia* ndoto ya kiishara inayootwa na mama Kaguba inasimuliwa na mwanawe Kaguba aliyekuwa mtoto wa ajabu aliyerithishwa uchawi na Bi Masonganya;

> "Halafu huyu ma'mdogo Nyanzala tatizo lake ni kiburi sana, shauri yake watamuua bure, ye 'ameambiwa awaambie tu mumlipie upanga wa watu alioupoteza halafu ye' anakuja kusema mpaka hayo mambo mengine ya kuteswa na Bi Kibena. Wakimsikia tuu shauri yake tuu" (uk 20).

Ishara ya ndoto ya mtu mwingine inasimuliwa na kutafsiriwa na mtoto wa miaka minne aliyekuwa na uwezo wa kutambua ndoto zilizootwa na mtu mwingine. Hii ni sehemu ya maajabu ya masimulizi ya Mwingizi. Hivyo kitendo cha mwanawe kusimulia "kitu ambacho amekiota yeye" kimemthibitishia kuwa haikuwa ndoto ya kawaida bali ni

ndoto yenye uhalisia. Akiwa katika selo, Suhail anajikuta akiwa katika nusu ndoto ndani ya *Vita vya Mapenzi.*“Alikuwa kama anayeota ndoto mbaya sana ambayo ilimtaabisha mpaka akashituka kuotka usingizini na kukutana uso kwa macho na Komandoo Takadiri Uk 229.”

Katika *Mzimu wa Waufi* sehemu kubwa ya masimulizi ya matendo ya mhusika mkuu, masimulizi yanamwonyesha akiwa na hali ya ndoto;

> “Kukurukakara hiyo sambamba na kelele za kupinga kunywesha damu ya mtu ndizo ambazo zilimshtua Masumbuko toka usingizini! Haraka akinuka na kuketi huku akitweta. Akageuka huku na kule, akiwa bado anahema juujuu. Akajiona yupo chumbani mwake juu ya kitanda, ndipo akagundua kwamba yupo ndotoni” (uk. 4).

Ndoto zote katika riwaya teule ni za kutisha, zenye kuibua maudhui ya kuashiria maafa yenye ishara za damu na vifo. Licha ya kuashiria mambo mabaya, ndoto hizi zinatumikishwa kuvunja mipaka iliyopo kati ya uhalisi na ndoto. Kwa mfano, katika ndoto inayorejelewa hapa juu, kumetajwa mambo kama vile, “kelele, unywaji wa damu, uzindukaji pamoja na kukataa kunywa damu”, mambo ambayo japo yanatukia katika ndoto ni mambo ambayo uelewa wake unahusishwa na hali halisi za kilimwengu. Kwa mfano, hata katika hali ya kindoto, mhusika anafahamu razini ya kutambua kwamba, unywaji wa damu ya binadamu ni mwiko. Kwa hivyo, mipaka kati ya uhalisia na ndoto inakuwa finyu sana.

### 5.4.3 Pete Kama Ishara na Uashiriaji

Pete anayovishwa Suhail katika *Vita vya Mapenzi* ni pete ya *Khatam Budha* ambayo ni ishara ya ulinzi na utajiri. Pete hiyo inabadilika rangi kutokana na muktadha na matukio yanayomzunguka mvaaji. Pete ina masharti ya kunyeshwa damu kila mwezi. “Naam ni damu ya mbuzi, sasa vua pete yako kisha uiweke humo ndani ya bakuli (uk 66).” Pete hiyo inatumika kama ishara ya maangamizo na neema. Inajenga maudhui ya kuwaangamiza watu wabaya, wasaliti na waongo.

Mtu anapolazimika au kulazimishwa kuivaa ni sawa na kuhakikisha kuwa anaendeleza matakwa ya waliomvisha au alioingia nao mkatabani. Hakuna nafasi ya kuisaliti. Ni ishara ya kufungwa, kudhibitiwa kihali na kimawazo, kutawaliwa kifikira na kiutendaji,

yaani kubanwa kwa uhuru wa kufikiri na kutenda, kuondolewa na pengine kudhibitiwa kwa hiari ya mtu binafsi kutenda. Kwa mfano, Suhail anapojitokeza katika hali zake mbali mbali za kiutendaji, hapana shaka kwamba Suhail ni chombo tu, hakuna alitendalo kwa kuamua kwa njia razini ila kwa kuelekezwa, kutishwa au kushawishiwa. Anatawaliwa katika kila hali na hata anapotumia uongo na ulaghai, ni kwa sababu ya kuogopa matokeo yaliyo kinyume na matakwa ya waliomvisha pete au kukiuka masharti ya hao hao waliomvisha pete. Kwa hivyo, swala zima la pete linapohamishiwa katika miktadha ya kihalisi, linaashiria mambo haya haya ya kutawaliwa na kudhiBitiwa katika misingi ya mtu binafsi, jamii na hata taifa.

Vilevile pete hiyo inaashiria kielelezo cha ulaghai, mikataba hewa, na kufungamanishwa na matajiri na walio na uwezo. Suhail anaingizwa katika vita ambayo si yake—anashirikishwa na kuathirika katika vita ya kitabaka, vita ya binadamu na majini, vita ya majini kwa majini, vita ya kijinsia yakizingatiwa mahusiko yake katika mahusiano na Shekhia na Sharifa, vita ya kifamilia, vita ya kiutambuzi, vita vya kitaifa, vita vya kiuzao, vita ambapo mahusiko yake ni kama chombo tu. Kila anapotumia nguvu zake kujinasua kutoka mitego mbalimbali, mafanikio yake ni duni sana au hata hakuna mafanikio. Kwa mfano, alipougua ugonjwa usiojulikana hatima yake ni kaburini tu. Mwanga wa pete wa kijani ni ishara ya uponyaji (uk. 216 VM). Na mwanga mwekundu wa pete ni ishara ya hatari na vita. Mwandishi anasema:-

> “Pete ilibadilika kuwa rangi nyekundu “Nakumbuka kwenye maelezo Suhail macho yakamtoka, ni kweli wakati anavikaBidhi vitu vyake kaunta, Pete ilikuwa na rangi ya kijani. Kubadilika kwa pete kuwa rangi nyekundu ilikuwa ni ishara ya hatari (uk 210).”

Suhail amevishwa pete ya kijani aliyokuwa akiitumia kama video ya kuyaangalia mambo na yaliyokuwa mbali yaliyokuwa ya hatari na misukosuko;

> Suhail alipoipokea tu akaivaa kidoleni kama vile anayeijariBisha kisha akakibenjua kitufe kidogo sana kilichopo kwa upande wa nyuma wa kile kitocha rangi nyekundu ili aweze kuona ni hatari gani inayomnyemelea (uk. 211)”

Pete imetumiwa kama ishara na zana ya ulinzi na kiona mbali cha kimiujiza. Kuvikwa pete hiyo ni ishara ya kukabidhiwa madaraka ya kiutawala na umiliki wa rasilimali, lakini kama chombo tu kwa sababu mali na rasilimali hizo zinadhibitiwa kwa njia fiche na wamiliki. Ni alama ya uongozi wa umma kwa maana ya kutumikishwa na kuoneshwa ilhali waongozao ni wengine. Katika riwaya ya *Tanzia* hakuna pete ila kuna kibuyu cha *sambamfinyu* na mkufu wa kifo uitwao *Mkanyafe*:

> "Sambamfinyu ni kibuyu kikuu cha kichawi kilichosheheni kila aina ya ulozi ambao ndio ngao kuu ya hayati Masonyanya ambayo ameacha amemkaBidhi mjukuu wake huyo Kaguba (uk 33)."

Kibuyu hicho kama ilivyo pete kikiangamizwa ama kwa kuchomwa moto au kutupwa chooni kinaashiria anguko la wachawi wote wa Kibondo. Pete ambayo majini ya himaya ya Khatam Budha walikuwa wakiitafuta kwa udi na uvumba, ni ishara ya anguko lao kiuchumi na kiutawala iwapo itaangukia mikononi mwa binadamu wanaoneka kumudu kuzima nuru ya majini. Kwa upande wa mkufu wa kifo wa *Mkanyafe* (uk. 81) katika *Tanzia*, ni kielelezo cha utafutaji ukweli na kuna nguvu za kumwangamiza jini au mchawi yeyote anayedanganya au kulaghai umma.

Ishara ya pete inaonekana tena katika riwaya yake ya *Mzimu wa Waufi* ambapo Masumbuko ali mwanamume anayeoteshwa kufanywa mwanamke aitwaye Shamsa na kupangiwa kuolewa na mwanamume chini ya usimamizi wa Hunudu kama sehemu ya adhabu ya kukataa kujiunga na himaya ya Waufi. Baada ya kuonyesha dalili za kukubaliana, Hunudu anamvisha pete Masumbuko. Mtunzi anasema "katika kidole cha kati, mara ghafla akaanza kubadilika na kurudi katika maumbile yake ya awali, lakini ghafla akaanza kujisikia vibaya mwili mzima…kama mtu anayekaribia kukata roho (Uk 75)." Pete anayovikwa Masumbuko ni pete ya kijini na inatumika kumtibu na kumrudishia hali yake ya kijinsia. Kama ambavyo Shekhia alivyotumia pete yake kumponyesha Sharifa ndivyo jini Hunudu alivyofanya. Pete hiyo aliyovikwa ndotoni anakuja kujikuta nayo "mkononi katika kidole chake cha kati cha mkono wa kulia (Uk 77)." Pete hiyo haionekani kwa watu wa kawaida. Kila aliyeingizwa katika kundi la Waufi alikuwa na "pete kubwa nyekundu" akiwemo Sheikh Mwinyigoha. Ishara ya pete

katika riwaya za *Vita vya Mapenzi* na *Mzimu wa Waufi* zinakitwa katika kubainisha mambo mengi mseto; mkataba kati mvaaji na aliyemvalisha kama vile kundi la majini au mitandao ya siri, utawala, udhibitiwaji na uelekezwaji, utumikishwaji na ufiche wa mambo mengi na hasa yasiyo halali.

Katika riwaya ya *Vita vya Mapenzi* tunaona ukutanaji wa Suhail na Sufian ulikuwa katika mazingira ya sadfa kwa Suhail lakini kwa upande wa Sufian alikwishakuyajua mazingira ya kukutana kwake na Suhail kwa kutumia nguvu zake za kijini. Kwa hivyo, wanakutana katika gari na gari linapata ajali pasipo Suhail kuelewa chochote kinachoendelea kwani abiria wengine wanakufa. Mzee huyu anakuwa katika hali mbaya na Suhail anatoka mzima. Mzee huyu anajitahidi kuhakikisha anamkabidhi Suhail pete na pesa katika mazingira ambayo si ya kawaida, mazingira ya kutisha na kuogofya, mazingira ya umwagikaji damu na ufu.

Mtunzi anaonyesha kwamba, hii inaashiria mikataba inayoasisiwa na kuibuka katika hali kama hizi ni mikataba hatari itakayosababisha umwagikaji wa damu na vifo. Si ajabu huo ndio uliokuwa uhalisi wa maisha ya Suhail. Ni kitu cha ajabu sana kufanya mikataba kama hiyo katika mazingira na miktadha ya ajali, hasa ajali ambapo kuna umwagikaji wa damu na vifo vya watu. Lakini pamoja na kumkabidhi pete hiyo, mtunzi anaonyesha kuna masharti ambayo amepewa na ahakikishe anayatekeleza masharti hayo. Kwa mfano, katika uk. 9 mtunzi anasema:-“Mzee Sufian akavua pete yake kubwa yenye kito cha rangi ya njano aliyokuwa ameivaa kwenye kidole chake na kumshika Suhail mkono, kisha akamvalisha”. Mtunzi anatuonyesha kwamba kile kitendo cha kumvalisha Suhail pete na kumpa masharti mbalimbali kilikuwa kinashiria makubaliano mazito kati ya Sufian na Suhail bila yeye mwenyewe Suhail kujua kwamba hayo makubaliano ya pete na masharti yatakuja kumuangamiza. Aidha mtunzi anaonyesha uvukaji wa mipaka katika hayo makubaliano kwani Suhail ni mwafrika na Mzee Sufian yeye ni muasia anatoka nchini Yemen wanakutana katika mazingira tatanishi na siku hiyo hiyo wanaingia katika makubaliano. Hivyo basi mtunzi kupitia ishara hii ya pete

anachimuza dhamira ya unyonyaji kwani pete huvaliwa na watu wenye mikataba fulanifulani.

Kwa upande mwingine mtunzi ametumia pete kama ishara ya kuonyesha kwamba Suhail na Mzee Sufian wamekubaliana mpaka kufa katika kutimiza masharti aliyompa ndio maana akaamua kumvalisha pete ya kuonyesha ishara ya makubaliano yasiyovunjika. Mwandishi kupitia pete anaashiria wazi jinsi mataifa yaliyoendelea yanavyotumia njia mbalimbali katika kuhakikisha wanaingia mikataba na mataifa yanayoendelea ili waweze kuzinyonya nchi hizi, kwani pete inaonyesha ni makubaliano na masharti wanayoyatoa nchi ambazo zimeendelea kwa nchi zinazoendelea katika kuhakikisha mikataba yao haivunjiki. Aidha mtunzi anaonyesha wazi kabisa njia mbalimbali wanazozitumia katika unyonyaji huu ni kutengeneza mazingira na kuhahakisha wanazubaisha waafrika kwa kutumia mbinu mbalimbali za kuwaangamiza kifikra ili wasiweze kuhoji viongozi wao mambo mbalimbali yanayoendelea kwa kuwapumbaza. Ndio maana ile ajali ya wale abiria waliokuwepo kwenye gari na wakapata ajali na kuuwawa lakini Suhail anapona na Sufian anakufa ni ishara ya kuwaangamiza waafrika kifikra ili waendelee kudumaa na wenyewe wakiendele kuchota maliasili zetu.

Vinginevyo huenda mtunzi anaonyesha pete Suhail aliyopewa na Mzee Sufian hubadilika rangi kutokana na matukio kuna wakati wakiwa wanafuatiliwa na maadui zao yaani serikali ya himaya ya Budha, huwa ya rangi nyekundu na wakati kuna amani pete ile huwa inakuwa na rangi ya njano. Mtunzi ametumia pete kama ishara ya ukombozi na ambayo huwaweka tayari Mzee Sufian na majini wa himaya ya Budha kupambana pale wanapofuatiliwa katika mipango yao. Mtunzi kupitia pete hii anachimuza dhamira za ukombozi kwani pete hii ilikuwa ikitumiwa na akina Sufian kwa ajili ya kujikomboa na mahasimu wao. Aidha mwandishi ametumia tena pete kama ishara ya kuchumiza maudhui mbalimbali kama vile uendelezaji na uimarishaji wa maslahi binafsi, ulinzi au kinga na utajiri, uwepo wa mitandao siri lakini inayokwenda sambamba na mitandao rasmi ya kijamii. Katika (uk. 52) mwandishi anaonyesha kuwa

pete ndicho chanzo kikubwa cha uchumi katika himaya ya Budha, jambo ambalo ni la kimajini, linaweza kukubalika. Pete ndio iliyokuwa ikibeba uchumi wa himaya ya Budha na watu walikuwa wanagombana kwa ajili ya maslahi yao binafsi kila mtu anataka kujineemesha yeye mwenyewe kutokana na uchumi mkubwa uliopo kupitia pete hiyo .

Mtunzi ametumia pete kama ishara ya neema na utajiri mkubwa katika himaya ya Budha na ndio maana kila mtu alikuwa anang'ang'ania kubaki mamlakani ili aendelee kufaidi utajiri huo. Mzee Sufian aliondoka na ile pete akaenda kumpa Suhail naye Suhail akaweza kutajirika sana kwa ajili ya hiyo pete. Lakini pia pete hii imetumika ni kama kinga ya kichawi na kimajini katika kuwalinda wale wote wanaoufuatilia uchumi wa Mzee Sufian kwani kitu chochote kibaya kilichokuwa kinataka kuwakumba pete ilitoa ishara ya hatari. Katika hali hii, pete ni fumbo la kimsingi linalohitaji kufumbuliwa ili kuelewa jinsi uchumi wa kifamilia, kitaifa na kimataifa unavyoathiriana. Vilevile pete imetumika kama ishara ya usaliti na chanzo cha migogoro katika familia kwani sababu ya Suhail kumuacha mchumba wake ni kutokana na makubaliano ya pete ambayo alipewa na Sufian. Miongoni mwa masharti aliyopewa kuhusu na pete hiyo ilikuwa ni kumuoa Shekhia na kumuacha mchumba wake wa zamani Sharifa. Pete ile iliweza kuleta pia mgogoro mkubwa sana kati ya Suhail na wazazi wake pindi walipomtaka amuoe Shekhia mchumba wake wa siku nyingi. Aidha ndoa hii inakuwa ngumu kwa ajili ya mkataba wa pete ndivyo mataifa yanaendelea pia viongozi wake wanakuwa katika wakati mgumu kwa wananchi wao kutokana na masharti ya mikataba waliyopewa na wawekezaji pamoja na mataifa yaliyoendelea yanayotoa misaada kwa nchi maskini.

Mtunzi anatumia pete kama kitu ambacho kina uwezo mkubwa wa kimaajabu katika kutatua matatizo mbalimbali. Pete inatumika kumwokoa Sufian kutoka katika mikono ya mahasimu wake huko nchini Yemen. Mtunzi anaonyesha kwamba, pindi Sufian alipokuwa anapigwa na mahasimu wake pete ile aliyokuwa ameivaa Suhail iliweza kuwaka rangi nyekundu ikiashiria kuna matatizo makubwa yametokea kwa Mzee

Sufian. Ndipo Suhail akaitumia ile pete kufika mpaka nchini Yemen kwa dakika kumi na tano tu. Mtunzi kupitia ishara hii ya pete anachimuza ujumbe wa jinsi ambavyo viongozi wengi au hata watu maarufu hutumia nguvu za kichawi na kishirikana katika kujikinga na mahasimu wao au katika kuzilinda nafasi zao ili waendelee kubaki mamlakani.

Aidha katika riwaya ya *Vita vya Mapenzi* pete imetumika kama ishara ya uchimvi kwani imekuwa ikiashiria majanga mbalimbali ambayo yataotokea mbele. Mfano mzuri ni wa Suhail alipofanya mapenzi na Sharifa pete ya Shekhia iliwaka moto ikiashiria kuna ukiukwaji wa makubaliano ya masharti aliyopewa Suhail na Sufian pamoja na mwanaye Shekhia, hivyo pete ilikuwa ni kama kitu cha kutahadharisha. Mfano mwingine ni pindi Suhail alipoongea uongo kwa Mzee Atrash, pete ile iliweza kumuonyesha rangi nyekundu kwa kuahiria kwamba jambo analolifanya si zuri na hatimaye, kitamletea matatizo. Uashiriaji wa matukio ya mbele ya pete hii umechimuza dhamira ya kuwaagiza watu waache kwani mwisho wa uongo huwa si mzuri kama ambavyo imemtokea Suhail mpaka akafa sababu kubwa ni uongo.

Aidha pete imetumika kama ishara ya utumwa kwani Suhail alikuwa anateseka kwa sababu ya masharti ya hiyo pete na pindi alipokuwa anakwenda kinyume na makubaliano ya hiyo pete alikuwa anapata madhara. Pete hii inamfanya Suhail awe mtumwa kwa sababu chochote kile kibaya kilichokuwa kinatendeka ambacho kilikuwa kinyume pete ile iliwaka kuashiria kuna tukio liko mbele yake anatakiwa aende akapambane nalo. Mfano alipokuwa anafanya maandalizi ya harusi yake na Sharifa pete ile ilionyesha hatari ikamlazimu awahi nchini Yemen kumuokoa Mzee Sufian. Mtunzi kupitia pete hiyo anachimuza dhamira za ukoloni mamboleo kwa mataifa ya ulimwengu wa tatu kwani japo ukoloni mkongwe umeondoka lakini ukoloni uliobaki ni mbaya zaidi, umewafanya waafrika kuwa watumwa katika nchi zao wenyewe kwa kuwafanya vizuu wa kifikra.

Katika riwaya ya *Mzimu wa Waufi* pete imeashiria kinga. Mtunzi anamwonyesha Masumbuko akibadilika kutoka ile hali ya usichana na kuwa mwanamume baada kuvalishwa pete na jini Hunudu (uk.75). Kwamba pete kama kinga na chombo ambacho kinawasaidia watu kutoka katika hali ngumu ya maisha au matatizo mbalimbali. Mtunzi kupitia ishara ya pete anachimuza dhamira ya kinga mbalimbali ambazo watu hujiwekea katika biashara zao au maofisini mwao ili waendelee na wasisumbuliwe na mahasidi wao. Mtunzi anaendelea kutumia ishara ya pete kama chombo ambacho hutumika na viongozi wengi serikalini katika kuzitetea nafasi zao. Wafuasi wote wa Hunudu walikuwa wana pete na kama kuna kitu cha hatari mbele yao pete ilikuwa inaonyesha miale ya rangi nyekundu ili waweze kujikinga. Mtunzi anaonyesha jinsi viongozi wengi serikalini hutumia uchawi na ushirikina kama kinga ya kuzitetea nafasi zao. Kwa hivyo, katika hali hizi, pete ni kitu sawia na mtandao wa kimahusiano yawayo yoyote yale, yawe na tija au yawe na shari. Ikumbukwe kwa umbo la pete ni umbo duara, na mduara unaibua imani za aina nyingi katika jamii mbalimbali.

Mtunzi bado anaendelea kuchimuza dhamira ya maslahi binafsi na migongano ya kidini. Pete iliweza kuleta migongano mikubwa katika jamii na hasa katika swala la dini, kwani pindi alipoitwa mchungaji amwombee Masumbuko, naye mchungaji naye alionekana amevaa pete hiyo hiyo ya kijini alivyovalishwa Masumbuko na Hunudu. Watu wote walikuwa hawaioni. Hata baba yake Masumbuko isipokuwa Masumbuko tu ndio alikuwa anaiona. Shehe mwingine alipoitwa kumsomea kisomo kule hospitalini, alionekana amevaa pete hiyo hiyo ya kijini. Mtunzi anaonyesha jinsi ambavyo hata viongozi wa dini huwa wanaenda kinyume na dini na wapo katika dini kwa ajili ya maslahi yao binafsi. Tazama dondoo ifutayo imedhihirisha haya;

> Macho yake yalitua katika pete kubwa nyekundu. Haraka akayarejesha macho yake kwenye kidole chake cha kati, akaitazama pete yake akagundua inafanana sana na ile ya Sheikh Mwinyigoha *Ni pete ya Waufi!* Yaani unapokuwa na pete hiyo unamaanisha wewe ni mwanachama tayari……Noooooo" Masumbuko alipiga kelele huku akimsonta kidole Sheikh Mwinyigoha, watu wote walitahayari, viti vikawa vichungu wakasimama juu, lakini Sheikh Jabu alikuwa ni jasiri sana aliendelea kumshika Masumbuko huku akimtupia swali "Wewe Masumbuko una matatizo gani "Huyu Mzee hafai kuwa Sheikh huyu,

> nawaeleza si Sheikh huyu, naye ni mfuasi wa Waufi! Mnaona pete yake hiyo na hii yangu waliyonivisha inavyofanana?"(uk. 79)

Mwandishi anamwonyesha Masumbuko anawashangaa viongozi hawa wa dini wanaotumia pete kama ishara ya kufanya mambo ambayo ni kinyume na dini zao. Mtunzi kupitia ishara hii ya pete anaonyesha jinsi viongozi wengi wa dini jinsi walivyo wanafiki nje wanafanana na kondoo kumbe ndani ni mbwa mwitu. Baadhi ya viongozi wa dini wamekuwa wakitumia dini na vyeo vyao katika kujitafutia mali kwa njia mbalimbali zisizo halali. Aidha mtunzi anatumia pete kama ishara ya udhibiti wa kiuchumi na ishara ya udhibiti wa maslahi ya ki binafsi kwa kuonyesha viongozi hawa wa dini jinsi wanavyofanya maovu yao mbalimbali na wanatumia mgongo wa dini ili watu waweze kuwaamini na waweze kukubalika katika kuhakikisha wanaendelea kudhiBiti uchumi wao.

Kwa upande mwingine pete imetumika kama ishara ya maafikiano, kwani Hunudu alimpa pete Masumbuko kwa makubaliano ya kujiunga na dini ya Waufi japo Masumbuko hakuwa tayari lakini alijikuta tayari ameshaingia maafikiano na Hunudu mpaka anampeleka chini ya bahari kwa ajili ya kumuonyesha milki walizonazo na watu wanaokiuka masharti yao wanavyoteswa. Mtunzi kupitia ishara hii ya pete anachimuza dhamira ya viongozi wasiojitambua wanaoingia mikataba na mataifa yaliyoendelea wakifurahia na baadaye masharti yale yanakuja kuwatesa wananchi kwa kuchukuliwa mali zao au kupewa masharti ambayo yataendelea kuzidunisha hizi nchi maskini.

Pete imetumika kama ishara ya kivuko kati ya ulimwengu halisi na ulimwengu wa kimazingaombwe. Matukio mengi yamekuwa yakifanyika kutokana na pete yalikuwa yamechanganyikana kati ya ulimwengu halisi na ulimwengu wa kimazinagaombwe. Pete ile iliweza kumsaidia Suhail na Mzee Sufian wakati wanapambana na mahasimu wao katika mazingira ya kimajini. Hivyo basi ikamlazimu Suhail atoke duniani kwa kutumia pete hiyo na kwenda sehemu ya tukio baya kwa kutumia muda wa dakika kumi na tano. Mtunzi kupitia pete hii anachimuza dhamira ya migongano ya maslahi kwa

sababu pete hiyo imetumika zaidi katika kuonyesha inasaidia watu waendelee kuneemeka.

### 5.4.4 Rangi kama Ishara na Uashiriaji

Tunapozungumzia ishara za rangi kupitia kazi teule za Maundu Mwingizi tunajikita katika rangi nyekundu, nyeusi, kijani, nyeupe na njano zikichimuzwa kwa wingi kuashiria mambo mbalimbali ikiwemo ishara za kifo, uponaji, utakaso, hali ya kawaida na ubaya au ulozi. Macho ya wasomaji yanapelekewa kuangazia rangi mbalimbali zinazochimuzwa kwa wingi zikiwa zinalenga kuashiria maswala mbalimbali. Begi jekundu la pesa katika *Vita vya Mapenzi* linakabidhiwa kwa Suhail na kiumbe jini-mtu, Mzee Sufian wakati akiwa katika dakika za kukata roho akizungukwa na damu nyingi. Begi lenye rangi nyekundu linajenga ishara ya damu na uhatarisho;

> Suhail akijaribu kupingana na ukweli kwamba Mzee Shamhurishi ameshakata roho, ghafla alipatwa na ujasiri akalifunga vizuri begi jekundu lenye pesa akalivaa mgongoni kisha akachukua begi dogo jeusi akalibeba mkononi na kuanza kutoka nje ya basi (uk18).

Kitendo cha kukubali kulichukua "begi hilo kubwa jekundu" la kiajabu, ni kujiingiza katika himaya ya udhalimu na utumwa wa maisha ambapo maisha yake yatakuwa yanadhitiwa na kutawaliwa kwanjia fiche. Anakabiliwa na masharti yanayokuja kumtumbukiza katika usaliti wa kuhitilafiana na wanajamii, marafiki, familia yake pamoja na mpenzi wake Sharifa. Pesa aliyokabidhiwa katika begi jekundu inaonyesha sio tu tamaa ya pesa bali pia tamaa ya makuu mengine hali inayoishia kuashiria mabadiliko ya nafsi ya Suhail kama mtu binafsi, mabadiliko ya mtazamo wake wa ulimwengu, kuwapembeza wanafamilia na wanajamii waliowengi kwa sababu ya ushawishi wa mfumo wa uchumi anaojitambulisha nao kwa sasa na unaotawaliwa na pesa. Rangi nyekundu inamkumbusha msomaji kuwa ingawa pesa zimo kwa wingi lakini zinazungukwa na damu na hatari kubwa. Ishara ya wekundu inapaswa kumshitua msomaji kuwa kuna jambo la hatari ambalo limeizungukia hizo fedha nyingi;

> "Cha ajabu kila abiria akiliangalia lile begi dogo jeusi tu, na hakuna hata mmoja aliyejishugulisha kuangalia lile begi kubwa jekundu lilikuwa mgongoni ambalo ndilo hasa lenye pesa (uk 21)"

Abiria walio wengi ambao ni wa kundi kubwa la tabaka tawaliwa, linashindwa kuuona mfuko mkubwa mwekundu. Kwa kuwa wanajishughulisha na kibegi kidogo cheusi. Hapa mwandishi anatupa taswira ya kiini macho ambacho wanajamii wengi wanashindwa kuiona rushwa kubwa na kujishughulisha na wizi mdogo mdogo au rushwa ndogo ndogo ambayo haina athari kubwa kwa jamii si kubwa. Rushwa kubwa hufanywa na viongozi wachache lakini athari yake kwa uchumi na michakato mingi ya kijamii ni kubwa mno. Kupiga vita rushwa ndogo, japo ni muhimu katika kukuza maadili, hakusaidii kuijenga jamii husika kwa njia chanya. Aidha mabadiliko yangeweza kupatikana iwapo wananchi au abiria walio wengi wangefanikiwa kuuona mzigo mkubwa wa rangi nyekundu wenye pesa nyingi mno ambazo mhusika Suhail angeshindwa kujieleza kwa waandishi wa habari, wananchi waliomzunguka au vyombo vya usalama na vile vya harakati za kupambana na wahujumu uchumi. Mfuko mkubwa mwekundu unaachiwa ukaeneze sumu yake katika jamii. Suhail anakubali kuwa tayari kulitekeleza hilo baada ya kunasishwa katika mtego wa tamaa.

Ishara ya "begi jekundu" inajirudia katika *Mzimu wa Waufi* wakati ambapo Masumbuko aliyekuwa akisafiri kutoka Dar es Salaam kuelekea Shinyanga. Kuwaona wazazi wake Mzee Kikoko na Mkewe Bi Kapemba aliye mke mkubwa na ili apate kuwahadithia mkasa wa utata wa ndoto yake, anaonekana akishuka katika basi akiwa na "Begi lake dogo jekundu" (uk.11). Wekundu huo huo bado unaendelea kuashiria hatari, maangamio na ufu. Rangi nyekundu inaonekana tena katika kito cha pete ya "Khatam Budha" katika riwaya ya *Vita vya Mapenzi* pale mhusika mkuu Suhail anapokaBidhiwa na Mzee Shamhurish pete hiyo. Pete hiyo inaonekana ikiwa na rangi ya njano;

> "Mzee akavua pete yake kubwa yenye kito cha rangi ya njano aliyokuwa ameivaa kwenye kidole chake cha kati na kumshika mkono Suhail, kisha akamvisha pete ile (uk 9)."

Maelezo anayopewa kuwa pete hiyo ina kazi mbalimbali ikiwemo kukuongoza, kukulinda na kukupatia mali. Sharti kuu analopewa pamoja na kupewa mali na pete ni kuwa hana budi amuoe Binti yake aitwaye Shekhia anayeishi Bagamoyo ili kumwepuka Binti yake huyo kuja kuolewa na majini. "Pete ya *Khatam Budha* ni pete ya kijini yenye kubadilika rangi tofauti tofauti" (uk 54), ni kiini cha ploti nzima ya riwaya hiyo kwani inatafutwa na majini wa baharini hali ya kuwa kiongozi wa majini haya aliasi na kuja kujificha duniani katika mji wa Bagamoyo na Yemen akihofia kuuawa na majini wenziwe wanoitaka pete hiyo iwe kama zana ya ulinzi na mali. Mzee Sufian anamtafuta mwanadamu anayeonekana kuwa na nyota ya nuru kuwa na uwezo wa kijini kupitia pete. Alimfuatilia Sufian anayesadikika kuwa na nyota ya "Shamshi" kuwa ni kiumbe anayefaa zaidi kupewa pete hiyo na hivyo kumsaidia yeye Mzee Shamhurishi kupigana na majini wenziwe.

Vilevile katika kutaharuki kwa inspekta Kenjah juu ya rangi ya pete anauliza swali lifuatalo kwa Suhail. "Nakumbuka kwenye maelezo Suhail uliandikisha kuwa una pete ya rangi ya kijani, sasa mbona hii ni nyekundu?" Suhail hashituki kubadilikabadilika kwa pete hiyo, ila anashituka kwa vile "hiyo rangi nyekundu ikitokea tu ujue kuna hatari…hakujua ni hatari ipi inayotaka kutokea" (*Vita vya Mapenzi*: 210)". Mabadiliko ya pete kuwa nyekundu ni ishara ya vita, damu na maafa. Wakati akiwa katika mazungumzo ya kutubu mbele ya wanafamilia yake, Suhail anaona pete ikibadilika rangi. "Akiwa katikati ya simulizi yake, mara pete yake ikabadili rangi na kuwa nyekundu. Ishara ya hatari! (uk 274)." Utabiri huo unathibitishwa na taarifa za Shekhia kuwa baba yake Mzee Sufian anauawa. Hivyo anaomba msaada kwa Suhail aende kumuokoa baba mkwe wake. Waliokuwa na pete katika riwaya ya *Vita vya Mapenzi* ni Suhail na Shekhia. Shekhia anaitumia pete hiyo katika kumdhuru mke mwenziwe Sharifa kwa ugonjwa wa kiharusi pia anaitumia pete hiyohiyo katika kumponyesha kwa kuibadilishabadilisha rangi;

> "Alipokibenjua tu kito cha pete ikatoka miale ya hafifu ya rangi ya kijani, akailekezea kwa Sharifa kwa sekunde kadhaa kisha akaondoka harakaharaka na kutoka kabisa wodini (*Vita vya Mapenzi*: 216)."

Rangi ya kijani inachukua dhima ya uponyaji badala ya rangi nyekundu inayoashiria hatari na vita. Sharti la kuipa nguvu pete hiyo ni kuilisha kila mwezi kafara la damu (uk. 264). Kafara lenyewe ni la damu ya mwanadamu ambaye ni ndugu yako wa karibu.

Matumizi ya rangi nyekundu katika riwaya za Maundu Mwingizi yanaakisi hali mbalimbali za kimaisha. Rangi nyekundu haijitokezi mara zote kama maisha yalivyo. Maisha yana vipande vya furaha na vipande vya huzuni. Kubadilika badilika kwa rangi ya kito cha pete ni ishara ya maisha yalivyo na tabia ya binadamu kwa ujumla. Shekhia aliyekuwa amepania kummaliza Sharifa kwa kumuua anabadilika moyo na kuingia na roho ya huruma na kuamua kumponyesha kwa kubadili miale na kuifanya ya kijani. Anapokuja kugundua kuwa Sharifa ni ndugu yake wa mama mmoja anajutia kitendo alichokitaka kukifanya cha kumuua dada yake wa tumbo moja pamoja na mtoto tumboni.

Rangi nyekundu ni rangi ya damu. Inatumika katika kafara la uuaji. Mzee Sufian anapomkaBidhi Suhail mke wake Shekhia anampa sharti kwanza avue pete hiyo na kutia katika bakuli la damu. “Ni kitu gani hicho ndani ya bakuli? Naam ni damu ya mbuzi…sasa vua Pete yako kisha uiweke humo ndani ya bakuli” (uk 66). Kilichotokea ni kitendo cha ile damu kumezwa na ile pete. Sharti hilo anapewa alifanyie kazi kila mwezi bila ya mafanikio. Hata hivyo wekundu unaoshwa na weupe. Pete iliwekwa katika bakuli la maziwa na bakuli jengine la damu likiwa tupu. Komandoo Takadir, alivamia bakuli la damu akidhania ndani yake kuna pete. Kitendo cha kuvamia bakuli la damu ni kupofuka kwa fikra zake ambazo muda wote zilikuwa katika kuangamiza. Rangi ya suluhu ni rangi ya maziwa ambayo ni nyeupe. Badala ya pete kunyweshwa damu, ilinyweshwa maziwa na hivyo kufanikiwa kuwaangamiza maadui haswa Komandoo aliyeshindikana aitwaye Takadir. Suhail anapewa jukumu la kumuangamiza Takadir “kwa miale ya moto iliyochanganyika rangi nyekundu, kijani na nyeusi (uk. 278).”

Rangi nyingine iliyotumikishwa kwa mapana katika riwaya za Maundu Mwingizi, ni rangi nyeusi. Mara nyingi rangi nyeusi ni kielelezo cha ghubiko, utata, kiza au usiku. Huweza vilevile kumaainisha ubaya au maafa. Hivyo rangi nyeusi hufasirika kwa mujibu wa muktadha wa usimulizi na kwa mujibu wa namna mtunzi anachokusudia kukiwakilisha. Katika *Tanzia* chungu cheusi na kibuyu cheusi vinatumika katika kuwadhuru watu kiuchawi;

> "Wachawi wakalisogelea kaburi la hayati bwana Mtandi na kuanza kubinuka tena mahepe yao. Dakika chache tu Binti Sambayu akakipiga kwa nguvu chungu cheusi juu ya kaburi lile ba papohapo kaburi likapasuka na kuachia kijinjia chembamba (uk 61)"

Weusi wa chungu ni ishara ya ubaya, ulozi na vita. Kwa upande mwingine kibuyu kidogo alichokuwa nacho Bi Sambayu, nacho kinaelezewa na mtunzi kuwa kimehifadhiwa katika kapu lenye rangi ya kaki iliyogeuka na kuwa nyeusi kwa uchafu:

> "..kisha akaingiza mkono kwenye kikapu chake cha rangi ya kaki kilichoathiriwa na uchafu mpaka kikaonekana ni cheusi, akakiweka kile kibuyu na kisha akatoa kitu kama mkufu hivi uliosukwa kwa ukindu, akamvisha Binti Sambayu shingoni (uk 80)."

Unasibishaji wa uchafu na weusi ni taswira inayogonga vichwani mwa wasomaji. Mtunzi anaoanisha uchafu na weusi katika muktadha wa ulozi, ufufuaji na vifo. Haya ni mambo ambayo kwa usemi mwingine yanaashiria kudumaa kwa mawazo na maono ya watu katika jamii au makundi fulani ya jamii na ndio sababu ya kutoendelea. Kwa pamoja tunaona mlandano wa rangi mbalimbali; za njano, nyekundu na nyeusi katika pete ya Khatam Budha katika riwaya ya *Vita vya Mapenzi*, na kwa upande mwingine, kibuyu cha uganguzi cha Babu Gao katika riwaya ya *Tanzia* kilichovikwa "shanga za rangi za njano, nyekundu na nyeusi (uk 28)." Tafsiri ya uchangamano wa rangi inahusiana na kazi na dhima ya pete katika *Vita vya Mapenzi* na kibuyu katika *Tanzia*. Hizi ni dhima za kuponya na kudhuru kwa pamoja. Ikiwa ni rangi nyekundu pekee basi inakuwa ni dhima ya kuuwa na kuangamiza; ikiwa ni ya njano ni dhima ya maisha ya

kawaida na tiba zake, ilhali nyeusi pekee ni dhima ya kuloga na kuangamiza kiulozi kama ilivyo chungu cheusi cha wachawi wa Kibondo.

Kwa upande wa rangi nyeupe tumeiona sana katika mavazi yenye kuashiria ucha Mungu, furaha na utakatifu. Wakati wa harusi ya Suhail na Shekhia walikuwepo watu tisa waliovaa mavazi meupe;

> "Likikuwa ni kundi la watu kama tisa hivi, wakiwa wamevaa kanzu nyeupe huku wamejitanda vilemba vya rangi ya kijani wote kwa pamoja. Walikuwa ni watu wenye asili ya kiasia (uk 62)."

Rangi nyeupe na ya kijani zinaashiria upendo, amani, furaha na utakatifu. Anapoivaa kanzu "nyeupe pee" (uk. 245), Ustadh Hussein Chaullah anaonekana pia akiwa na "tasbihi" na saa ya rangi ya almasi.  Hali ya weupe pee ni ishara ya kuutafuta utakatifu na usafi wa mwili na roho. Mavazi meupe hupendelewa kuvaliwa na viongozi wa dini walio "wachamungu".  Lakini pia katika mazingira mengine rangi nyeupe inaashiria uponyaji. Yalipoletwa maziwa, Ustadh Chaullah alibaini siri ya tiba ya maziwa ilivyo (VM uk. 278). Anasema kwamba, "kuna siri kubwa ndani ya maziwa, siri ya kiafya na kitabibu."

Msomaji anaposoma riwaya za Maundi Mwingizi rangi inayotawala kwa wingi kupitia vito na damu za makafara ni rangi nyekundu. Rangi nyekundu na nyeusi ni rangi za ushetani, nguvu za giza, ushenzi na usaliaji nyuma kimaendeleo ilhali rangi nyeupe ni rangi ya afya, maisha, uangavu, uokovu na umalaika. Ushetani unatawala kazi zake na kiashirio kinachompelekea kiongozi mmoja wa serikali kuwafokea viongozi wengine:

> "Shut up, haya niambie nani msafi humu kati yenu? Kila mmoja ana yake aliyoyafanya kwa njia yake katika kujihakikishia analinda ugali wake…nani asiyetaka madaraka humu? Nani asiyetaka mali humu? " (uk. 286).

Hili ni hitimisho linaloashiria kuchimuza kwa wingi wa rangi nyekundu na nyeusi katika riwaya za Mwingizi za *Vita vya Mapenzi*, *Tanzia* na *Mzimu wa Waufi*. Anachokifanya Mwingizi si kuwakaribisha moja kwa moja wasomaji wake katika

madimbwi ya damu, bali kwa kutumia ishara ya wekundu na weusi anachombeza hatari zilizomo katika jamii yake kwa kuashiria kupitia matumizi ya rangi. Kila rangi anayoitumia hususan nyekundu, nyeusi na kijani mtunzi alikusudia kufikisha ujumbe wake wa mafao au madhila yaliyopo katika jamii yake. Anapokufa Suhail na Mzee Sufian ingawa walikuwa wakipigana dhidi ya Komandoo Takadir, hawaponi katika hukumu yao kwani nao walikuwa katika njia ya maangamizi kwa sababu kwa kiasi kikubwa maisha yao yalijaa unafiki, uongo, hadaa, kiburi na usaliti. Anapokuja Ustadh Chaula na kanzu nyeupe pee anawakilisha mkono wa haki na ukweli. Bila ya hofu anatekeleza kazi ngumu ya kusema na kufufua ukweli kwa kuangamiza uovu na uongo na usaliti.

Aidha weusi mkubwa na kiza kilichotanda kilikuwa kinawekwa na viongozi wasaliti chini ya mtandao wa *Black Scopion* (*Vita vya Mapenzi*: 286). Maana ya "Black" ni nyeusi. Walikuwa wanawatia kiwingu wanajamii ili kuendelea kupiga hatua kimaisha na ustawi kwa kuwahujumu kiuchumi. Kiza kingine kilikuwa kinawekwa na himaya ya *Khatam Budha*. Nao walibidi waangamizwe kwa damu ili weupe utawale na uondoe kiza. Kiza na weupe ni nguvu mbili ambazo haziwezi kuchanganyika. Nguvu ya weupe inapambana na nguvu ya weusi. Wahusika weupe wanawakilishwa na Ustadh Chaulla, ambaye naye anafanya kazi ya usalama wa taifa kwa siri, Mwanadada Lillian Ufoo naye anawakilisha weupe, na uzuri lakini akiwa kwa siri na yeye ni mwanausalama. Hii ikiwa ni siri yake.

Kwa upande mwingine Mzee Kusekwa bila ya kujijua anawaozesha mtu na dada yake na anamwoa Mama Kusekwa ambaye ni nduguye na Amanda. Viongozi wenye majina ya mficho ni wawakilishi wa kiza na wanapokuja kufichuliwa wanaonekana ni walakini katika jamii. Katika riwaya hizi za Mwingizi, ishara ya rangi inachukua nafasi muhimu katika kufikisha ujumbe. Ni taswira ya dunia ilivyo. Dunia isiyo na rangi moja na iliyo tata na mafumbo mengi tata. Kuna kuingia usiku baada ya mchana na kisha usiku tena kabla ya kupambazuka.  Weupe na weusi unowakilishwa na usiku au kiza unakuja kuondolewa na weupe wa mwanga. Anapokufa Bi Masonganya katika riwaya ya

*Tanzia*, kiza kinatanda kabla ya mwanga kuingia. Lakini mwanga unakuja na siri nzito inayoficha kiza kingine kizito cha maafa ya wanafamilia.

Rangi nyekudu licha ya fahiwa nyingi za uashiriaji, ni rangi ya damu. Mateso na vifo vinavyotokana na umwagikaji damu vinatapakaa katika riwaya za Mwingizi. Suhail akiwa kizuizini anapigwa na Komandoo Takadir na kutapakaa damu. Amanda anachukuliwa juu na kimbunga na kurudishwa chini akiwaamekufa. Msigwa anakufa akiwa na majeraha ya risasi yaliyomtoa damu nyingi, Mzee Sufian na Komandoo Takadir wanaangamizwa kwa moto mwekundu wakiwa wameloa damu. Ujumbe tunaoupata ni kuwa tamaa ya pesa na mali inapelekea kutoweka kwa utu, ubinadamu, uungwana na ustahili na badala yake kuotesha kutokwa damu nyekundu ambayo hatima yake ni kuangamia. Damu zinazowatoka wahusika ndani ya *Vita vya Mapenzi* ni malipo ya matendo ya tamaa, uongo na usaliti. Zana ya pete inawakilisha hali za wanajamii, yaweza kupewa kafara la damu kwa mwenye kutaka kuitumia kwa mauaji na maangamizi au kwa kafara la maziwa kwa mwenye kutaka kuitumia kwa ajili ya utakaso, kutafuta haki na kujirudi. Kito cha pete hakina rangi maalumu bali inategemea nia ya mvaaji.

**5.4.5 Mazingira kama Ishara na Uaishiriaji wa Uasilia**

Mazingira yametumika kama shara na uashiriaji. Riwaya za Mwingizi zimeonekana katika ishara zinazohusianishwa na hali ya hewa kama ukungu, upepo, mbalamwezi, upinde, vimbunga, mvua, na kiza, nuru. Ni sehemu muhimu katika kuashiria tanzia na maangamizo ya baadhi ya wahusika wakuu katika riwaya teule za Mwingizi. Nyingi ya ishara hizi huonekana katika kipengele cha mandhari. Kama zilivyo ishara mbalimbali, kuna kubaini hali ya ukweli na ile ya kuwakilisha aina fulani ya maana za ziada. Ishara hizo hufanikiwa iwapo mwandishi atazitumia kufikisha pande zote mbili za maana bila ya kuwashurutisha wasomaji kubaini maana hizo. Tunapenda kuthibitisha katika sehemu hii kuwa Maundu Mwingizi amefaulu kufikisha kwa wasomaji wake aina zote mbili za maana zinazokuwa ni kielelezo cha ujumbe anaoukusudia. Katika *Vita vya Mapenzi* (uk 276) Mwandishi anachorea wasomaji upepo usiokuwa wa kawaida;

> “Wakati hayo yakiendelea ghafla hali ikabadilika ukasikika upepo mkali ukivuma huko nje, vumbi la haja likitimka. Milango ikijibamiza. Upepo ulikuwa mkali sana kiasi cha kufanya uingie mpaka barazani….ilikuwa ni kimbunga kikubwa kilichofuatiwa na harufu kali ya marashi iliyotanda takribani kwa dakika tano!”

Upepo huu unaashiria mapambano ya majini wawili katika viwiliwili vya Mzee Sufian Bin Shahurish na Komando Takadir Al harab. Hivyo kimbunga hakiashirii hali ya kawaida ya mvua na dhoruba itokanayo na mabadiliko ya hali ya hewa, bali nguvu za viumbe majini ambao maumbo yao si sawa na ya wanadamu. Lakini kwa vyovyote vile uelewa unaojengwa kwa kutumia mambo haya ya kimaumbile kama kimbunga, unatokana na ufahamu wetu na mazoea ya hatari na maangamizi yanayosababishwa na kimbunga, hasa kimbunga kinapokuja kwa mpigo wa nguvu, madhara yake hayatamaniki.

Ishara ya giza ni ishara bia yaani ni ishara ambayo hujulikana na jamii mbalimbali duniani kote. Hivyo basi ishara ya giza katika kazi za fasihi hutumiwa kusimamia hali ya kutojua au ujinga hali ya kughuBikwa, hali ya ukosefu wa ufahamu. Kwa upande mwingine Lawrence (2001: 2) anasema giza ni ishara ya hofu, hatari na hali ya kukosa matumaini. Katika riwaya hii ya kimajaribio na kihalisiajabu ishara ya giza imechimuza maudhui mbalimbali. Ishara hizi za giza zimetumika tena katika riwaya ya *Mzimu wa Waufi (*uk. 150 na uk. 213) ambapo mtunzi anaonyesha ishara ya giza kama elimu ya kutojitambua. Mara akina Hunudu wanapowapeleka watu katika utawala wao huwaingiza katika giza kubwa kwa muda fulani kwa maana huwapa elimu ya kutojitambua ili kuwatumia vilivyo ili wasijue uwazi pamoja na ukweli. Mtunzi kupitia ishara hii anachimuza dhamira ya kutojitambua mtu anapokandamizwa kutokana na kufifiishwa kwa vimisaada vidogovidogo. Mataifa yanayoendelea yamekuwa hayajitambui kutokana na vimisaada wanavyopewa na mataifa yaliyoendelea.

Kimbunga kinachorwa na Mwingizi kama ishara pale ngano ya angamizo la mke wa Mzee Sufian Mama yake Shekhia. Usimulizi huo unafanywa na msichana msusi wa Bagamoyo,

> "..basi mwenzangu siku moja kilitokea kimbunga kikali yaani kama kilichotumwa vile kikazipitia nyumba zote mpaka kwa akina Shekhia. Kilipofika uani kwao kikamvaa mama yake na Shekhia akiwa anapika hapohapo uani, cha ajabu waliokuwa jirani na nyumba hiyo wanadai ndani ya vumbi lile la kimbunga waliona kama taswira za watu kadhaa hivi japo haikua rahisi kuwang'amua waziwazi kutokana na vumbi kubwa kuchachamaa, na ghafa kimbunga kile kikasambaa kwa mtindo wa kwenda hewani.. kikapaa pamoja na mama Shekhia!... nusu saa baada ya kimbunga kupotea watu wakiwa wamefurika uani kwa akina Shekhia wakishangaa muujiza huo ndipo tena ghafla kikatokea kisanga kingine, ukadondoka mwili wa mama Shekhia ukitokea angani huku ikiwa umeachana na roho.. (uk. 41).

Kimbunga cha ajabu kinanasibishwa na mwendo wa majini na viumbe wasiokuwa wa kawaida lakini wenye uwezo wa kuwaangamiza wanadamu.

Katika riwaya ya *Tanzia*, mtunzi anatumia ishara za upepo mkali, ukiambatana na usiku wa kiza kinene;

> "Upepo ule mkali uliendelea kuvuma mithili ya kimbunga huku baridi kali ikiwa imeshtadi kwelikweli (uk 1)."

Upepo huo haukuwa wa kawaida kwani kipindi hicho kilikuwa ni cha kiangazi katika mji huo wa Kibondo. Siri kubwa ya mabadiliko ya hali ya hewa ya kiasi cha kuogofya ilitokana na imani kwamba, Kikongwe Bi Masonganya aliyekuwa mchawi maarufu alikuwa anakata roho. Ndugu, watoto, wajukuu na vitukuu vyake walimfanyia dawa ya kumtoa roho ili asimrithishe mtu uchawi wake. Kwa hivyo, mtunzi analizungumzia swala la kuvunja na kutupa mifumo ya kishenzi inayokwamisha watu katika maendeleo yao. Ingawaje ishara ya kimbunga na upepo mkali hunasibishwa na mwendo wa majini, lakini binadamu pia huweza kupata nguvu hizo iwapo atapewa kupitia kifaa kama vile pete ya ajabu ya kijini ya "Khatam Budha" (*Vita vya Mapenzi*), nguvu za kiwanga za

kuruka angani kwa ungo (*Mzimu wa Waufi* na *Tanzia*). Suhail alimudu kwa msaada wa pete kusafirishwa saa tisa za usiku kutoka Tabora hadi Dar es salaam:

> "Hakua na usafiri wowote zaidi ya pete yake iliyomtoa pale Tabora kwa kasi ya ajabu baada ya kuiamrisha tu kufanya hivyo. Moja ya faida ya pete ilianza kuonekana! (uk.100)"

Safari ya upepo kupitia pete ya ajabu, Suhail ambaye ni mwanadamu, anafanikiwa kwa dakika kumi na tano tu kuwasili Yemen kutokea Tanzania anakwenda kumsadia mkwe wake Mzee Sufian kupigana vita na majini watatu waliokusudia kumuangamiza;

> "Na ndani ya takriban dakika kumi na tano, Suhail alikwisha wasili nchini Yemen na kujitoma moja kwa moja katika jumba lile la zamani la makumbusho, na bila ya kupoteza muda akaingia mpaka ndani kabisa huku hofu ya ki binadamu ikianza kumezwa na ujasiri wa kijini kutoka katika pete aliyoivaa (uk 100-101)".

Katika riwaya ya *Tanzia*, mwandishi Mwingizi anawachorea wasomaji wake taswira ya usiku wenye giza kuu na dhoruba za mvua kali katika mji wa Kibondo ikiashiria kufariki mtu mkubwa, Bi Masonganya Binti Kalukalange ambaye inasemekana alikuwa mchawi aliyebobea katika taaluma hiyo. Mvua kubwa inayonyesha na giza totoro ni ishara anayoitumia mwandishi kuwapa wasomaji wake picha ya huzuni na maafa yanayoikabili jamii hiyo. Ni alama inayofasirika na wanajamii wa Kibondo kuwa ni mawasiliano ya nguvu za ujaala. Kimbunga kikali kiliishambulia teksi waliokuwemo Mzee Mtandi na nduguze Mama Kaguba na Kungurume wakati wakimpeleka kwa mganga aitwaye Babu Gao;

> "Walipofika katika moja ya mapori kadhaa ambapo ilikuwa wakilimaliza tu pori lile wangewasili nyumbani kwa Babu Gao, ndipo kilipoibuka Kimbunga kikali kilichoishambulia ile teksi mpaka ikapoteza uelekeo na kuzima (uk 37)."

Kimbunga hicho si cha kawaida bali ni cha mashambulizi ya akina Kaguba na Binti Sambayu na wachawi wengine. Ishara ya kimbunga hainasibishwi na hali ya hewa bali hutafsirika kama dalili ya vita na kifo kinachomnyemelea mgonjwa.

Aidha kwa upande mwingine, giza limetumika kama ishara ya kukosa matumaini kwani mataifa mengi ya Afrika wananchi wake wamekata tamaa na hawana matumaini kwa sababu wamejawa na hofu kubwa juu ya viongozi wao. Viongozi hao hawana msaada kwao na pindi wanapotaka kuandamana kwa ajili ya kupata haki zao wamekuwa wakinyamazishwa na wengine kuuliwa na wengine kutishiwa maisha. Kwa hivyo hali imezidi kuwa tete na kuendelea kukosa matumaini kabisa na huona heri jana yao kuliko leo yao.

Kwa upande mwingine, mtunzi ametumia giza katika tukio hili la kina Hunudu huashiria hali ya wanataaluma kutojua umuhimu zao. Wanashindwa kutekeleza majukumu yao kwa jamii na taifa, kwani walichobaki nacho ni vyeti na viwango vya elimu visivyo na tija kwani muda wote huonekana kutukuza mambo ya kigeni na kudharau ya kwao. Katika uk. 213 katika riwaya ya *Mzimu wa Waufi* mtunzi anaonyesha Hunudu akileta giza kubwa walipokuwa wanamzika Nyamizi halafu mbele ya lile giza kuna mwanga. Hii inaonyesha wazi kabisa wasomi wamepewa elimu ili waweze kujitambua lakini bado wanapenda kukaa gizani wakati mbele yao kuna mwanga. Mfano mzuri ni kuwa hakuna nchi ambayo imeendelea duniani pasipo kutumia lugha ya kwao lakini wasomi wengi ndio wamekuwa msitari wa mbele katika kutetea lugha za kigeni jambo ambalo linapelekea kuzorota kwa maendeleo katika nchi zao. Hii ni kwa sababu hata lugha nayo ina mchango mkubwa katika ukuzaji wa maendeleo. Kwa hivyo, elimu tuliyoipata bado haijaweza kutufikisha kwenye mwanga.

Vilevile mwandishi anaonyesha kuwa Waswezi pia hutumia mwanga au nuru kama ishara ya elimu ya kujitambua. Kwa mfano katika (uk. 214 na 215) tunaona Hunudu amewavamia Waswezi makaburini katika mazishi ya Nyamizi aliyeuawa na Hunudu. Kijana huyo katili alikuja kwa njia ya giza. Ingawa wakati wa mapambano yakiendelea ndani ya giza lililoletwa na Hunudu, wazee wa Kiswezi waliendelea kupambana kurudisha mwanga. Mwandishi anasema;

> "…wakafanikiwa kwani ndani ya muda ule wa mapambano mwanga ukarudi na kila mmoja sasa akamwona Hunudu vizuri lakini inaonekana kuwa Hunudu hakutaka mwanga kabisa katika kutimiza mauaji aliyoyakusudia…" (uk. 215).

Kwa mantiki hii ishara ya giza ni ishara ya waovu, ya kuwatoa watu ufahamu. Lakini kwa Waswezi ishara ya mwanga ni elimu ya utambuzi na uwazi pia. Ndio maana baada ya kukandamizwa kwa muda mrefu na Waufi wananchi wanapata elimu ya kujitambua wanapambana na serikali iliyopo mamlakani na wanafanikiwa kuwaondoa Waufi.

### 5.4.6 Mandhari za Mijini na Vijijini kama Ishara na Uashiriaji

Katika riwaya ya *Vita vya Mapenzi*, Mzee Sufian akiwa katika dakika za mwisho za "kukata roho" alipopata ajali safarini kutoka Dar es Salaam na nje kidogo ya mji wa Dodoma, anamkabidhi Suhail pete na mkoba mwekundu uliojaa dola za kimarekani ili awe mrithi wake na mkwe wake. Mali na pete anazokabidhiwa ni kwa masharti kwamba amuoe Binti yake aitwaye Shekhia anayeishi Bagamoyo. Kitendo cha kuutaja mji wa Bagamoyo kinapelekea wasomaji waushabihishe mji huo na imani za uchawi vichwani mwao. Jina Bagamoyo linasawiriwa katika visaasili vya Waswahili na matukio ya imani za majini na uchawi. Ipo miji mingine kadhaa kama vile Giningi, Gambush, Tanga, Sumbawanga katika nchi ya Tanzania ambayo hulandanishwa na imani za misukule, uchawi na viumbe vya kiuhalisiamazingaombwe kama majini. Mji kama wa Bubwini unatajwa pia katika *Vita vya Mapenzi* kuwa una sifa za ulozi na uganguzi, "Haikuhitaji msaada wa mpiga ramli kutoka Bumbwini" (uk. 193).

Vilevile matukio ya uchawi na harakati za majini zinazungumziwa katika miji ya Sokotra nchini Yemen, Mlingotini mjini Bagamoyo, Tabora, na Kibondo na Kigoma (katika *Tanzia*). Lakini linapotajwa Jiji la Dar es Salaam na vitongoji vyake vya Mbezi, Magomeni, Buguruni, *Break point*-Kijitonyama na Ilala, Banana, Gongo la Mboto, TMJ Hospital na Hospitali ya Amana katika riwaya zake teule, msomaji anavutika kuona taswira ya uhalisia wa mandhari hizo kichwani mwake. Ni miji na vitongoji halisi lakini vinavyoashiria hekaheka, misukosuko na kila sifa za kimji ikiwemo sifa za

kupungua kwa maadili na maisha yenye athari za kiMagharibi ikiwemo kusikiliza nyimbo za Pharrel William, msanii wa Marekani (*Vita vya Mapenzi*: uk 4-5).

Kitendo cha Shekhia katika *Vita vya Mapenzi* kuwapita wazee kutoka Tabora bila ya kuwasalimia ingawaje alionekana kwa nje kuwa ni mstaarabu kimavazi kwa kule kuvaa hijabu nyeusi na mtandio. Kilitafsiriwa na wazee hao kuwa hiyo ni tabia ya umji ambayo haijali ustaarabu, heshima baina ya rika;

> "….Kitendo cha kuwapita bila ya hata salamu wazee wale ambao bila shaka ni wa umri wa sawa na wazazi wake yeye ilitilia shaka uungwana wake. Lakini labda hiyo ndiyo hali ya Jijini tofauti na huko mikoani watokeapo au pengine naye ameachanganywa na kuuguza (uk 206).

Wazee wa Tabora walichukuliwa kuwa bado wana heshima na nidhamu ya kimaisha. "Kwa nidhamu ya wazee kitabora haikuwa rahisi kuingia chumbani kwa watoto wao… (*Vita vya Mapenzi*: 266)." Kwa wazee wa kimkoani bado walikuwa ni washika dini. Mzee Fungameza kwa kuwa alikuwa mzuri wa dini ya Kikristo ambaye pia ni Mzee wa kanisa huko kanisani kwao Tabora akaanza kuporomosha maombi huku akisaidiwa na mkewe. Mzee Kusekwa naye kwa imani ya dini yake ya Kiislamu akawa anafanya dua kwa mwanaye (uk. 234)" Huu ni uthibitisho wa mwandishi unaoashiria kuwa bado kuna imani kwa wazee wa mikoani au mikoani kwa ujumla. Kwa njia hii, "Umji" na "umikoani" unakinzwanisha hapa. Watu wa mikoani wanachukuliwa kuwa bado wanashikilia maadili ambayo yanaoneka kuporomoka kwa kasi katika maeneo ya mijini. Maisha ya mji yanapambwa na pilikapilika na hekaheka za kutafuta riziki kwa wakaazi wake huku;

> "Kelele za muziki, pilikapilika za vyombo vya usafiri, mpishano wa waungwana na washenzi humfanya hata yule mwenye mawazo na changamoto lukuki za kimaisha naye kujiliwaza japo kidogo kiasi cha kuyasahau matatizo yake uk (259)."

Lakini ishara inayojengwa na mwandishi kuhusu miji ni ile ya sifa ya "uswahilini' iwe ni Tabora, Dar es Salaam au Bagamoyo. Suhail anapewa funzo kuhusu sifa za

uswahilini kupitia akina dada aliokutana nao akimtafuta Shekhia mjini Bagamoyo; … "Iko hivi kaka hapa Bagamoyo pia kuna pahala panaitwa Magomeni wanapotoka watoto wa Kiswahili, hatuna maana ya Magomeni hiyo ya huko Dar!" (*Vita vya Mapenzi*: 38), Inapotajwa uswahilini kwa mji wa Tabora, makazi ya wazazi wake Suhail mjini Tabora, kunaashiria makazi ya 'uswahilini'; "Kwa kawaida ya maisha ya uswahilini" (*Vita vya Mapenzi*: 114) ikiashiria makazi ya wazazi wa Suhail pale Tabora na pia Sharifa anamtambia mumewe kuwa yeye mtoto wa uswahilini kule Tabora, "Hapana chezea watoto wa uswahilini" (Vita *vya Mapenzi*: 118). Dhana ya eneo la uswahilini lina maana pana ya maisha ambayo si ya 'uhindini' au 'uzunguni' yaani kwa watu weusi wenye historia ya wakati wa ukoloni na ubaguzi wa makazi na matabaka. Kumbusho kwa vizazi vijavyo juu ya matabaka ya kijamii yaliyosababisha wananchi kuchukua hatua za kupigania uhuru wao wa kujitawala kutoka katika makucha ya wakoloni ili kuondoa adha hiyo iliyokuwa ikiwakabili.

Ishara ya umiji na umikoani, kama ilivyo "uswahilini" na "ushenzini" ni vielelezo vinavyoakisi historia ya jamii na bado vipo katika jamii ya sasa kama alama za kijiografia. Lakini pia kwa sasa uswahilini haimaanishi sehemu ya watu weusi pekee, bali ni maeneo ya mjini wanaoishi watu wa aina fulani wanaochukuliwa kuwa nimasikini tena "wajanja wajanja". Ni kutokana na picha ya umikoani na umijini ambapo, mtunzi anamjengea msomaji wake ishara ya mabadiliko ya kiuchumi, kijamii na kiitikadi. Kiuchumi inaelekea mjini kuna harakati za kiuchumi tofauti na zile za mikoani au vijijini.

Suhail anafungua kampuni kadhaa, huku akiishi maisha ya kifahari katika vitongoji vya Mbezi na Ilala, viongozi wa Scorpion wanaendesha magari ya kifahari aina ya *Landcruisers G8*, *Prado*, na *Rangerover* (uk. 233). Magari haya yanaashiria kutononoka, kuwa ngazi ya juu na watu wenye nafasi na kipato cha juu. Magari kama hayo si ya watu wa kipato cha chini na yanaashiria nguvu za kiutawala na ulafi wa mali za umma. Suhail anathibitisha tofauti za umiji na umikoani pale anaporudi kwao na kujisemea kuwa, "Duh jamani Tabora yetu haibadiliki kabisa! Nilitegemea kuwa

nitakuta hali imebadilika hata kidogo lakini wapi! (*Vita vya Mapenzi*: 81). Hali hiyo inasingiziwa na wazee hao kuwa pengine ni kutokana na nguvu za ujaala kuwa yupo "Sharifu aliuachiaga laana mji huo zamani (uk 81)". Imani anazozipinga Suhail kwa wazazi wake kuwa ni imani potofu wakati huo huo yeye mwenyewe akiamini na kufuata imani za majini na makafara ya pete.

### 5.4.7 Wanyama na Viumbe Majini kama Ishara na Uashiriaji

Kuna matukio kadhaa katika Vita *vya Mapenzi*, *Tanzia* na *Mzimu wa Waufi* yanayowashirikisha wanyama. Kwa mfano, kuna viumbe majini na mizimu/wanga /misukule na pia kuna wanyama kama mbuzi, kuku na paka wanatumika kwa makafara. Katika riwaya ya *Vita vya Mapenzi*, Mwingizi anawatumia wahusika wawili Mzee Sufian na kijana Suhail. Mzee Sufian ni jini anayejigeuza mwanadamu na kuja kuoa na kuishi miongoni mwa watu. Kipo kipindi haonekani waziwazi ila kwa njia ya ndoto, na kipo kipindi anajidhihirisha waziwazi kwa watu bila ya kificho katika umbo halisi la mwanamume mtu mzima au kijana. Kifo chake hakiji kwa njia ya ajali bali kwa kuangamizwa na moto kupitia pete ya ajabu.

Kijana Suhail anaonekana waziwazi kama mhusika halisia. Wahusika hawa ni wa pande mbili katika jamii. Katika mahusiano ya nguvu zao, Mzee Sufian anaonekana kuwa na nguvu za ziada za kuweza kujigeuza jini na kutenda matendo yasiyo ya kiurazini machoni pa watu. Kwa nguvu hizo anamshawishi kwa hila Suhail na kumtaka afuate matakwa yake. Pale anapoonyesha ubishi anaadhibiwa hapo hapo kwa nguvu za ajabu. Nchi zinazoendelea zinapokataa masharti ya nchi za kibepari zinaadhibiwa kwa kuwekewa vikwazo na kunyimwa au kunyang'anywa misaada. Mtego wa misaada ya fedha na utajirisho unapelekea kupoteza nguvu za kuhoji na kujadiliana katika biashara za soko la dunia, kama inavyoashiriwa na Mzee Sufian mwenye asili ya kiasia na Suhail mwenye asili ya kiafrika.

Mhusika Mzee Sufian anapambanishwa na jini mwenziwe, Komandoo Takadiri anayeitafuta pete ili kudumisha utawala wa majini waishio katika himaya ya *Khatam*

*Budha* chini ya bahari. Vita vyao ni vya kiishara kwani vinawakilisha viongozi wenye tamaa ya kutawala na kuwa na nguvu za kuangamiza waliowengi. Hakuna mwema kati yao, Mzee Sufian anamtumia Suhail kwa matakwa yake, na Komandoo Takadir anataka kuwaangamiza Suhail na himaya nzima ya Mzee Sufian bila ya huruma. Maisha ya hatihati yanamghubika Suhail akiwa katika njia panda. Tayari amekwisha ingia mkataba wa kukubali kupokea pesa na pete kwa masharti kwamba ni lazima amuoe Shekhia Binti jini kutoka Bagamoyo. Anatembea na siri kubwa ya juu ya chimbuko la utajiri wake kiasi kwamba hawezi kuelezea kwa wafanyakazi wake au ndugu zake. Anaingia katika mkataba wa ndoa asiyoitarajia na kuacha kutekeleza ahadi yake kwa mchumba wake wa uhalisia Binti Sharifa.

Ndoa ya Suhail na Shekhia ambaye ni mtu jini ni ishara ya ndoa hewa isiyo na penzi la dhati. Ni sawa na mikataba ambayo viongozi wetu wanaingia na makampuni au nchi zenye kuweka mbele faida wanayopata zaidi ya kuwasaidia wananchi walio wengi. Ndoa hii ni ya masharti, ya kupangiwa na isiyo na furaha ndani yake. Katika jamii za waswahili kuna ndoa iitwayo 'ndoa ya mkeka' ambayo hufungwa kwa kuwalazimisha wanandoa kuoana bila ya wao kupanga bali hutokana na shinikizo la wazazi. Shinikizo linalosababisha kuingia mikataba hewa kati ya baadhi ya viongozi na mabepari ni sawa na rushwa au hongo. Aidha Mzee Sufian akiwa ni mtoa hongo au rushwa na Suhail akiwa ni mpokeaji kwa faida yake binafsi huku akiwaangamiza wanajamii yake na nafsi yake. Anajiangamiza kiitikadi na kuingia katika ulimwengu mpya. Itikadi ya kunyonywa inajidhirisha na kupewa nafasi katika jamii ya Suhail. Jamii inaelezewa kiuhalisia kwa kutumia miji halisi ya Morogoro, Dar es Salaam, Dodoma, na Tabora. Pia wakiwa wahusika halisi na wale wa kimazingaombwe. Lugha ya kisasa ya "Voda" na "Tigo" na mazingira ya vijana ya kimuziki na kimavazi na kitabia.

Vyote hivyo vinaashiria kuwa anayoyazungumzia Mwingizi yapo katika jamii ya watu wa sasa ya baada ya ukoloni au jamii ya utandawazi. Mfumo wa kiuchumi na kijamii katika riwaya zake unaakisi maisha ya leo ambayo mbali na kwamba kuna kuingia kwa wingi kwa ada na desturi zinazopingana na mila za jadi na fikra za kidhahania, bado

mwandishi anawakumbusha wasomaji wake kuwa fikra hizo za kidhahania kama vile za misukule, uchawi na umazingaombwe bado zipo na si rahisi kuziondoa kabisa. Zimejikita katika mawazo na mifumo fikra ya wanajamii yake. Kitendo cha Mzee Sufian kutoonekana maiti yake wakati wa ajali, kitendo cha mkoba wake kutokupekuliwa na abiria waliomshuku Suhail kuwa anataka kutoroka na mali za majeruhi na abiria wengine, kitendo cha Mzee Sufian kuingia chumbani kwa Suhail bila ya kupitia mlangoni na kuingia chumbani kimazingaombwe. Na kitendo cha Suhail kujikuta akiwa na pesa halisi ambazo amekabidhiwa na jinimtu ni ishara ya kuwa Suhail tayari amekwisha ingia katika dunia mpya yenye mseto wa uhalisia na umazingaombwe. Dunia ya ndoto na urazini au dunia ya ulaghai na ukweli ndiyo inayojenga msuko wa riwaya za Mwingizi kiasi cha kumfanya msomaji kukubaliana na hali hiyo ya mandhari mbili za kidhania na kiuhalisi. Mwingizi hampi nafasi msomaji kuhoji dunia ya urazini na ile isourazini.

Wahusika wa kijini/kiwanga/kivuli wanakuwa ni wa kiishara kwa kule kuwa na mikondo miwili ya mawasiliano. Mkondo wa kihalisia na ule wa kimazingaombwe lakini wenye uhalisia. Katika mikondo ya kimazingaombwe wanakuwa na mambo yao ya kijini na katika mkondo wa uhalisia wanakuwa katika maumbo ya wanadamu wa kawaida. Uwezo wao wa kujibadilisha unaelezwa katika *Vita vya Mapenzi* (uk.194) kama ifuatavyo;

> “Hata ungeambiwa usingeamini, yule alikuwa ni komandoo Takadiri Al Harabi aliyejibadili na kuwa katika umbile lile la kike ili aweze kuishi vizuri katika kisiwa kile alichohisi kumpata Mzee Sufian pamoja na *Khatam Budha*.”

Mwingizi anatuundia wahusika wa kiishara na kimiujiza katika *Tanzia.* Mtoto wa Bi Masonyanya aitwaye Nyembo ni mtoto wa kiishara. Ndugu zake wa ukoo mmoja na wanajamii yake wanajua siri ya uzazi wake kuwa ni mtoto aliyezaliwa kupitia ndoa ya mwanamke na mwanamke mwenziwe;

> "..Naam Bi Masonganya ni baba yake kabisa na Nyembo. Unaweza kushangazwa na hilo lakini hivyo ni miongoni mwa vimbwanga lukuki vya hayati Bi Masonganya. Watoto wote wa Bi Masonganya walimchukulia Nyembo kama ni kielelezo cha uchawi uliokubuhu wa mama yao kiasi cha kuwafanya waoneshewe vidole kila wakatizapo mtani wakiwa na Nyembo" (uk 55).

Ujumbe wa mwandishi kwa wasomaji ni kwamba, jamii ya wachawi ina taratibu za kuozeshana wanawake kwa wanawake. Upatikanaji wa mtoto unakuwa kwa nguvu za kichawi na baba wa mtoto huyo anakuwa ni yule gwiji wa uchawi wa kike ambaye haoni ubaya kuliweka wazi jambo hilo kwa jamii. Mtoto Nyembo ni ishara ya uchawi uliokubuhu na ushahidi wazi kuwa uchawi upo una maarifa ya aina fulani.

Kundi la watu wafu (misukule) na wachawi wao hutupa taswira ya kutisha ya kuwepo kwa ufufuo na nguvu za kufisha kimiujiza walizonazo wachawi. Katika *Tanzia* tunaonyeshwa namna taratibu za kuwageuza watu na kuwadhuru kichawi zinavyofanyika hatua kwa hatua. Humdhuru mtu kwa kutumia taaluma yao ya uchawi inayotegemea vibuyu vyenye zana za ulozi. Humuua na kisha kumfufua na kumkata ulimi kabla ya kumtumikisha katika kazi zao. Wafu wa kiishara huitwa misukule na tayari tunaonyeshwa wahusika wawili Mzee Mtandi na Bi Nyanzala wakiwa katika hatua za kugeuzwa misukule. Wanapofanikiwa kutoroka kwa nguvu za kibuyu kiitwacho "kisambamfinyu" (uk. 33), hawajakatwa ulimi, Mtandi na Nyanzala wanatoroka kutoka himaya ya wachawi na kukimbilia nyumbani kwao ambako hakuna aliyewaamini kirahisi kuwa ni wazima. "Wote wakimkimbia Mzee Mtandi wakiamini kuwa msukule umewatokea (uk75)."

Jamii ya mtunzi katika *Tanzia*, *Mzimu wa Waufi* na *Vita vya Mapenzi* ipo katika lindi la misuguano ya kimetafizikia. Imani ya uwepo wa maisha baada ya kifo, inahojiwa kwani watu wanashindwa kuamini juu ya tukio la ufufuo wa kichawi. Inapozuka ndoto ya maruweruwe ni baadhi tu ya wahusika huamini juu ya uhalisia wa ndoto za kijini. Mhusika anaporuka kwa nguvu za pete na kuagua kwa uwezo wa pete, jamii ya wachache tu ndio inayoamini hivyo na wengi hutaharuki ingawaje wana ithibati tosha katika imani zao kuwa kuna kifo, ufufuo, malaika, majini au mashetani. Na sasa

inapotokea kuwa wafu wanafufuka, na kuwa kuna vifo vya umazingaombwe kama ilivyokuwa kwa Mzee Sufian, Mzee Mtandi na Bi Nyamizi ambavyo havikubaliki katika akili ya kawaida lakini vinakubalika katika simulizi za Mwingizi.

Kwa upande wa ishara za wanyama, Mwingizi anawatumia wanyama katika riwaya teule. Katika *Vita vya Mapenzi*, Suhail anaonekana akitoa kafara la mbuzi. Komandoo Takadir anamcheka Suhail kwa kuandaa kafara la damu ya mbuzi badala ya damu ya mwanadamu;

> "Ghafla Komandoo Takadir akageuza macho yake na kuliangalia bakuli lile lenye damu likiwa katika kona ya nyumba ile, akaangua kicheko cha nguvu na kusema "Suhail u mjinga sana, unatoa kafara ya damu ya mbuzi halafu unataka upone! Mtoe baba au mama yako! (uk. 277).

Katika visasili vya jamii ya mwandishi, mnyama sungura anachukuliwa kuwa mjanja. Hivyo, ni kawaida kusikia mwanadamu akipewa sifa hiyo ya ujanja wa sungura anapopewa mwanadamu. Katika *Vita vya Mapenzi* (uk 233), Inspekta Kenjah anamlelezea muuaji wa kukodishwa aitwaye Joram Ndege kuwa "Huyo ni mjanja zaidi ya sungura itakuwa anapoteza malengo tu." Ni kawaida katika visaasili vya Waswahili kumchukulia mnyama mbwa kuwa ni wa thamani ya chini. Anapoitwa Sharifa kuwa ni mbwa na hali ya kuwa aliheshimu ndoa yake hadi kukubali matakwa ya Suhail ya kumtaka akutane kimwili na rafiki yake Msigwa kwa kisingizio cha kukosa nguvu za kiume. "Haya we bwana nataka unijuze juu ya huo u-mbwa uliombatiza huyu Binti" (uk. 163). Maneno hayo ni ya Mzee Kusekwa akimuuliza Suhail amthibitishie ukweli wake. Kitendo cha kumnasibisha mwanamke na mnyama "mbwa" ni cha kumdhalilisha. Si ishara chanya. Mwingizi anaunganisha ubinadamu na ujini na kwa kiasi uhayawani, kupitia Shekhia na pia kupitia uzazi wa Shekhia na Suhail. Sifa za mtoto wa kichawi Nyembo wa Bi Masonganya aliyempata kupitia mke wake aitwaye Binti Masunga ni aina ya mtoto wa kiishara. Mtoto huyu ndiye anayekuja kuwa jasiri mkubwa kiasi cha kufanikiwa kuvunja himaya ya wanga na wachawi wa Kibondo.

Fauka na wanyama hao katika (uk. 39 katika riwaya ya *Tanzia* mtunzi anamtumia paka katika riwaya hii katika kuwakilisha binadamu ambao ni wanafki. Kulikuwa na kikao cha wanafamilia wakijadiliana juu ya Kaguba aliyerithishwa uchawi na Bi Masonganya jinsi anavyoongea na wachawi wenziwe. Ndipo wakiwa wanajadiliana wakiwa na paka na, walijua ni mnyama tu, kwani siku zote wanaye hapo nyumbani. Kumbe si mnyama ni mtu ambaye pia Bibi Masonganya alikuwa akimtumia kumletea umbea iwapo anatetwa. Mhusika paka ameonyesha kuyumbishwa kwa mipaka kwani katika hali ya kawaida, paka hawezi kuwa na uwezo wa kusikiliza maneno na kuyapeleka sehemu nyingine. Mtunzi ametumia mbinu hii ya uhalisiajabu katika kuchimuza dhamira ya binadamu wanafiki kwani aliyasikiliza mazungumzo na baadaye akakimbia nje kumwambia Kaguba yote waliyokuwa wanayazungumza. Wapo binadamu wa namna hiyo mnaweza mkawa mnapanga mipango na ni siri lakini akatoa siri nje. Kwa hiyo mtunzi ametumia sitiari ya paka katika kuwaonya watu wenye tabia hiyo ya unafki.

Wanyama wengi walinatajwa katika riwaya za Mwingizi ni wale ambao wamo katika ngano, semi na visaasili vya Waswahili. Katika semi tunakutana na wanyama kama paka (paka aliyejeruhiwa VM uk.108), popo (alichungulia chini kama popo VM uk. 240) au simba (aliunguruna kama samba MW uk. 168). Ishara za wanyama hawa zimetumika kama sehemu ya usimulizi. Wahusika wanyama wanawakilisha aina mbalimbali za haiba katika jamii. Katika *Mzimu wa Waufi* (uk 103) wasomaji wanakutana na mnyama wa ajabu mweusi anayemtishia na kumpoteza Mzee Kishindo;

> "..Masumbukoo Kimbia!" Mzee Kishindo alipayuka kwa hofu, wakatimua mbio za hatari, wao mbele yule mnyama nyuma. Spidi ya mnyama ilikuwa kubwa kuliko yao, ingawaje walijitahidi kukimbia lakini mnyama yule mwenye hasira alizidi kuwasogele, nao hawakukata tamaa, wakizidi kukimbia huku wakipiga yowe" (uk 103).

Mnyama mweusi ni ishara na mazingaombwe si mnyama halisi. Ila kitendo cha kutishia kilikuwa ni cha kweli. Rangi nyeusi ni ishara ya kiza, ulozi na uadui. Rangi nyeusi kwa mnyama ni rangi ya "zohali" inayokusudia kuangamiza na kuleta maafa. Kwa hivyo, matumizi ya wanyama katika kazi hizi, mbali na kuwakilisha wanyama kweli ikizingatiwa kwamba kuna maingiliano kati ya wanayama na binadamu, kuna mifumo

ya imani inayojengwa kuhusiana na maingiliano hayo. Hii ina maana kwamba, binadamu daima yuko katika aina fulani za mawasiliano na wanyama.

### 5.3.8 Majina ya Watu na Mahali kama Ishara na Uashiriaji

Kuna wahusika wa kiishara wanaokuwa sehemu ya uashiriaji katika kazi ya fasihi. Wahusika wa kijadi kama vile Bibi Masonganya anakuwa ni mhusika wa kiishara—kwa maana kwamba anawakilisha mifumo ya imani hususan imani za uchawi, ulozi na ufu, taratibu za kufikiri, mitazamo na miuonulimwengu, taratibu za kimahusiano. Uwepo wa Bibi Masonganya ni uwakilishi wa uwepo wa mifumo mizima ya mambo mseto, mifumo inayoendeleza au kudumaza jamii. Kwa mfano, mingi ya mifumo inayowakilishwa na Bibi Masonganya ni mifumo bubu ikizingatiwa kuwa anaua kwa ajili ya kuua tu, faida zinatokana na mauji hayo hazionekani aslani! Anguko lake ni kiashirio cha ufaji wa imani ya kishirikina na kuondoka kwa adha ya maafa ya kilozi katika mji wa Kibondo. Anapokufa watu wanafurahia kifo chake. Wahusika wa kiisitiara ni sehemu ya mfumo wa uashiriaji.

Katika *Vita vya Mapenzi*, mwandishi anatuchorea makazi ya Mzee Sufian huko Bagamoyo. Ni mji wa ujinini ambao uko chini kwa chini. Suhail anapelekwa na mtumishi wa Kiarabu siku yake ya harusi na Shekhia. Nyumba ya Mzee Sufian ni jengo lililochakaa kwa nje lakini nadhifu na la ajabu kwa ndani. Iliwachukua dakika kadhaa kuteremka ngazi chini kwa chini hadi kufikia sehemu ya nyumba yenye milango ya nakshi ya rangi ya dhahabu, mazulia makubwa mekundu na taa za umeme. Nyumba si ya kawaida ni nyumba ya kijini. Kutokana na mbinu za usimuliaji za Mwingizi, picha anayoachiwa msomaji ni nyumba ya kifahari na isiyo ya kawaida. Nyumba inasemekana ipo Bagamoyo ingawa kwa maelezo inaoneka kuwa ipo chini ya ardhi au baharini. Chumba cha Suhail na Shekhia kimejipambanua kama chumba cha kifahari na cha watu wa tabaka la juu. “kilikuwa ni chumba cha hadhi ya nyota tano kama ingekuwa ni Hotelini (uk 65)”. Nyota tano ni ishara ya chumba cha hadhi ya juu na cha kifahari kabisa.

Maeneo mahsusi kama vile ya hospitali, sehemu za starehe, nyumba za ibada, vituo vya usalama, mahoteli na nyumba za wageni, Ikulu yametajwa kuashiria kuwa kazi hii ni ya kisasa na matukio yake ni ya hivi karibuni. Mhusika mkuu Suhail anaonekana anaasafiri katika miji ya Dar es salaam, Morogoro, na Dodoma kwenye *Vita vya Mapenzi*, lakini katika *Tanzia* na *Mzimu wa Waufi* ni miji ya Kigoma na Tabora ndiyo inayotamalaki. Kuna nchi za nje zilizotajwa katika riwaya za Mwingizi. Nchi hizo ni Yemen na Rwanda. Lakini pia miji hiyo imenasibishwa na utambulisho wa Utanzania, Uarabu, na Unyarwanda.Majina ya mwanzo yanaakisi mabadiliko ya kijamii na kitamaduni katika historia ya Tanzania.

Athari za kubatizwa na kusilimishwa zinajidhihirisha dhidi ya wanaofuata dini za jadi kupitia majina kama vile Nancy Kileo, Frank Mkali, Lilian Ufoo ambayo yanawakilisha ubatizwaji. Majina ya Rasheed, Salumu Marando, Ustadh Hussein yanawakilisha usilimisho na Kasa Kilingo Mkude, yanawakilisha koo za wahusika n.k. Wapo waliotajwa kwa vyeo vya kilakabu kama vile *Komandoo*, lakini wapo walioongezewa na mwandishi lakabu za *Alhaji* (Rage) *Ustadh, Mzee, Sheikh,* na *Mzee wa Kanisa* kuonyesha nafasi na hadhi zao katika jamii.

Katika *Vita vya Mapenzi* anaashiria kundi la vijana ni kundi maalumu ambalo linategemewa katika jamii yeyote. Lakini "wanasiasa wakishaona kipindi cha uchaguzi kinaanza na ndio wanajifanya kuwajali na kuwawezesha vijana. Vijana ni ishara ya taifa la kesho", ni tabaka linalochukuliwa kuwa ni la uzalishaji mali lakini pia ni tabaka linalorubuniwa kirahisi (uk. 91). Kwa upande mwingine mtunzi katika riwaya ya *Mzimu wa Waufi*. Mtunzi anaowaonyesha vijana ambao hawakuwa tayari kurubuniwa na wanasiasa kwa kukaidi kujiunga na dini ya Waufi, dini ambayo ilikuwa inatawala na kuongoza kwa mabavu wananchi wake, vijana hawa wanateswa kwa kuminywa taya zao ili wakukubali kujiunga na utawala wa kidhalimu lakini hawako tayari mpaka dakika ya mwisho. Japo mtunzi katika *Vita vya Mapenzi* anaonyesha jinsi vijana walivyokuwa wepesi kurubuniwa. Lakini kwa upande wa pili katika riwaya ya *Mzimu*

*wa Waufi* anaonyesha wapo ambao hawapo tayari kutumiwa na wanasiasa mpaka dakika ya mwisho hata kama wanateswa.

Aidha mambo haya yamekuwa yakidhihirika zaidi katika mataifa ya ulimwengu wa tatu kwani wanasiasa wamekuwa wakiwatumia vijana katika shughuli zao za kisaiasa. Hata wakati mwingine inapotokea ushindani katika siasa inakuwa vigumu kwa vijana hutumika katika kuvuruga amani ya nchi kutokana na kile wanachokitaka wanasiasa hao. Mkataba wa ndoa kati ya Suhail na Shekhia umeandaliwa katika nchi ya *Khatam Budha* (sawa na mikataba ya nchi nyingi zinazoendelea kuandaliwa Ulaya na kwingineko (uk. 64). Lakini mikataba hiyo wanayoingia viongozi, ni mikataba hewa na watu wengi hawayajui masharti na vipengele vyake au wanafanya maksudi kukubaliana na masharti kwa tamaa ya utajirisho.

### 5.3.9 Tamaa ya Ukwasi na Ubinafsi kama Ishara na Uashiriaji

Katika riwaya teule za Mwingizi, anausawiri mfumo wa uchumi na mabadiliko katika jamii ambapo pesa na ubinafsi unatawala. Kila kitu ni pesa, jamii imetumbukia katika utamaduni wa pesa iwe ni mikoani, mijini na vijijini. Katika *Vita vya Mapenzi* tunaonyeshwa nguvu ya pesa wakati Sharifa na Suhail wanagombana kufikia hatua ya kutaka kujiua na kusababisha Sharifa kuumia. Ndipo Suhail anatumia pesa zake katika kuhakikisha anafanikisha matibabu ya Sharifa bila kwenda polisi na mambo yasijulikane pia. Suhail anasema;

> “Kaka usijali kuhusu kila kilichoharibika nitakulipa gharama zote na za usumbufu.., tusaidie ili niwahi kumpeleka hospitali huyu Binti. Baada ya maelezo yale Suhail akamsogelea jamaa yule kisha akamwambia neno kwa sauti ya chini akijaribu kumshawishi kuwa atampoza pesa kidogo mbali ya hizo za matengenezo ya dirisha ili tu asitoe habari ile (uk 98).

Tunaonyeshwa “kwa kuwa pesa iliongea hivyo huduma ikaenda kwa kiwango kizuri (uk. 99).” Kwa hivyo pesa inaashiria kwamba ndio kila kitu katika maswala mbalimbali.

Katika riwaya ya *Vita vya Mapenzi*, genge la *Black Scopion* linaashiria, ni kiwakilishi cha mkusanyiko wa mafisadi wa kila aina. Walikuwa wamejipanga. Mwandishi anasema;

> "Upande wa kulia mwa Ibrahim waliketi watu watano; Mhe. Hamid (naibu waziri wa nishati na madini), Mhe. Abdiroush Warriya (Naibu Waziri wa Fedha), Moris Kungurume (MfanyaBiashara wa madini), na Charles Bikoraimana (MfanyaBiashara wa maswala ya usafiri wa majini). Upande kushoto Pia kulikuwa na vibopa watano Kamanda Katinda (Mkuu wa polisi kanda maalumu), Joram Ndege (Muuwaji wa kutumainiwa), Bi Kapemba Kitivo (Mkuu wa mkoa wa Musoma), John Patrick Massawe (Kiongozi wa chama cha Upinzani), Msimbe Abrams (mbunge wa mkoa wa Manyara) na Adams Gosh (Muwakilishi wa nchi ya Ugiriki ambayo ndiyo inaofadhili kikundi hicho).

Katika kundi hilo kila sekta muhimu ikiwemo ya vyama vya upinzani na wizara nyeti serikalini zimehusishwa ili kuashiria kuwa mtandao wa hujuma unawakilishwa katika sekta mbalimbali. Mafanikio ya hujuma zao yanapatikana iwapo kuna ushirikiano kutoka katika kila sehemu nyeti serikalini ikiwemo vyombo vya usalama. Kwa hiyo wale wanaopewa dhamana ya kuwatumikia wananchi, ndio walio mstari wa mbele katika kuwahujumu kwa tamaa ya pesa na ubinafsi.

Tamaa ya pesa na ubinafsi inamkumba mhusika Suhail katika *Vita vya Mapenzi*, pale anapokuwa katika usafiri wa kuteimbelea familia yake mjini Tabora anapokutana na Mzee Sufian. Anakubali kushawishiwa kuchukua pesa na pete ya Khatam Budha. Msimamo wa mwandishi unaashiria wazi kuwa ni vigumu kuukwepa mtego wa pesa;

> "Mzee aliona hamaniko la Suhail lakini hakujali. Bila shaka alilitegemea kwani lile begi jekundu lilikuwa limesheheni pesa mpaka juu tena zikiwa ni dola mia tu za kimarekani" (uk 9).

Kitendo cha kuhamanika baada ya kuonyeshwa pesa kinamkumba Suhail na wanajamii walio wengi. Ilibidi aondoke katika eneo la ajali na lile begi na kuahirisha safari ya kuelekea Tabora na kuwahi Dar es Salaam kwenda kuzihifadhi zile pesa na kuanza kuwekeza haraka. Jeuri ya pesa inadhihirika kwa magari ya kifahari walionayo wajumbe

wa *Black Scopion—Landcruiser G8, Prado na Rangerover* (uk. 233). Nyumba ya Mzee Sufian kule Bagamoyo, yenye milango ya dhahabu na ghorofa za chini kwa chini, nyumba za Suhail za Mbezi na Ilala, na meno ya dhahabu ya jambazi Joram Ndege. Nguvu ya pesa ndiyo chimbuko la Amanda kumkataa Mzee Fungameza baada ya kuishi pamoja na kumzaa Sharifa. Amanda, mkimbizi wa Kinyarwanda, alirubuniwa na Mzee Sufian ambaye walikuja kupata mtoto nusu jini aitwaye Shekhia. Msuko wa pesa katika kushawishi mahusiano ya kifamilia, kimapenzi na kibiashara unasaidia kujenga mtandao wenye wasifu mahususi lakini zaidi ya hayo unasaidia kuchimuza ujumbe, nasaha, falsafa pamoja na tahadhari kwamba hatima ya tamaa ya pesa ni umauti na maangamio;

> "Nilimkanya Amanda kuwa asipapatike na fedha za mtu asiyemjuwa lakini akanipuuza, hakujuwa kama anakikimbilia kifo" (uk 279).

Pesa ni chanzo cha kuhadaa. Pesa za Sufian zinawahadaa Suhail na Amanda na wote wanaangamia. Kwa upande mwingine, mtunzi anatumia pesa kama ishara ya kufikia mambo mazuri yanayojumuisha neema na mafao ya ki binafsi, mafanikio na ufanisi wa kijamii. Kwa upande mwingine, mtunzi ametumia pesa kama ishara ya kumpeleka mtu pabaya kutokana na njia za upatikanaji wa pesa hizo kama ilivyokuwa kwa baadhi ya wahusika katika riwaya teule. Kwa jumla, katika riwaya za Maundu Mwingizi, hususan *Vita vya Mapenzi*, pesa inaeleweka kwa njia nyingi mseto—pesa kama pesa, pesa kama ishara, pesa kama mfumo, kama mkakati wa kufanikishia mambo, pesa kama kitambulisho cha nafsi na tabaka na kama kielelezo cha tabaka.

### 5.3.10 Mifumo ya Dini na Itikadi kama Ishara na Uashiriaji

Mojawapo wa maswala ya kimsingi yanayomakinikiwa katika kazi teule za Mwingizi ni swala kuhusiana na dini, lakini ndani ya dini hizo, mtunzi anayadadisi maswala mengine nyeti kama vile imani, itikadi, tamaduni, desturi na mitazamo ya kilimwengu na hasa kwa kadri inavyohusika katika kushawishi maisha katika jamii. Kwa misingi hii, Mwingizi ameziunganisha na kuzikutanisha dini mbili kuu za Uislamu na Ukristo katika familia moja. Mzee Fungameza ambaye ni kiongozi wa kanisa anaishi na Binti yake aitwaye Sharifa ambaye ni Muislamu. Dua za pamoja zinaombwa wakati wa

kumuuguza Suhail. Mzee Fungameza akisali Kikristo na Mzee Kusekwa akiomba dua Kiislamu. Wote wakishirikiana kumuombea nafuu mgonjwa wao Suhail. Hii ni ishara ya rai ya Mwingizi kuwa panapotokea mitihani ya kimaisha tusahau tofauti zetu na kutimiza lengo au kuondoa hatari inayotukabili. Kwa upande mwingine ni vema kuepukana na maswala ya udini katika mausala mbalilmbali ya msingi na si dini tu bali hata swala la ukabila ni vyema kuliweka kando pale yanapokuja maswala ya msingi yanyohusiana na uhai wa mtu au mstakabali wa Taifa.

Ingawaje kimbembe cha dini hakionekani kama maudhui makuu katika riwaya za Mwingizi ishara za wahusika na majengo ya misikiti, makanisa na matambiko zinaashiria kuwa jamii anayoizungumzia wafuasi wa dini na imani mbalimbali lakini wote wanaishi kwa pamoja. Inapotokea kubaguana suluhisho halina budi itafutwe. Katika *Mzimu wa Waufi*, Mzee Kikoko anamkataza mkwewe Judith asimulete mchungaji kumuombea mtoto wake Masumbuko, ambaye ni Mwislamu. Wachungaji na Masheikh ambao ni viongozi wa jamii, wanapatikanaa wamo katika mitandao ya uangamizaji wanajamii. Sheikh Mwinyigoha ana pete ya kito chekundu inayoashiria kuwa yeye ni mwanachama wa mtandao wa Waufi (uk. 79).

Dini zinadhihirika katika matambiko, ibada, sala, dua, majina ya wahusika, vyeo vyao kijamii, na majengo. Ukweli unaashiria kuwa ingawa kuna dini za kisasa katika mazingira ya wanajamii wa mwandishi (Uislamu na Ukristo), lakini wote kwa pamoja bado wanaunganishwa na imani za dini za jadi kupitia kuamini uwepo na utendakazi wa dhana za misukule, uchawi, wanga, na hata nguvu za majini na mashetani. Katika kulinda umoja wa familia yao katika *Mzimu wa Waufi* methali ya Kinyankole inatumika kuwausia ndugu kutokutoa siri nje ya familia. Kuna mchanganyiko wa maadili ya kijadi, maadili ya dini mpya za Uislamu na Ukristo na utamaduni wa Magharibi. Wanajamii waliowengi wana imani za kuwepo kwa nguvu za ujaala. Swala la tofauti za imani za kidini zinaibuliwa na mwandishi katika riwaya ya *Vita vya Mapenzi*;

Kama mume na mke japokuwa walikuwa na tofauti kubwa mbili, tofauti ya utaifa na dini zao. Bwana yule alijiona mwenye bahati sana kwa kumpata mwanamke yule aliyefadhaisha wanaume wengi kwa uzuri na mvuto wake.. (uk. 50)"

Katika kuibua falsafa ya wanajamii na itikadi zinazolenga katika mwono ulimwengu wao, Mwingizi ananukuu misemo na methali mbalimbali ambazo wahusika wake wanazitumia katika mazungumzo yao kuashiria mambo mbalimbali. Baada ya kuona hatari ya tamaa ya fedha alizokuwa nazo Suhail, mwandishi anatoa onyo la nguvu ya fedha katika *Vita vya Mapenzi* kupitia usemi wa "Waswahili wanaosema pesa hupasua mwamba! (uk. 29)", Na alipotaka kumpasha Suhail juu ya hatari aliyoingiza kwa tamaa ya pesa, Mwingizi anamtumia msusi wa Bagamoyo kumpiga kijembe Suhail, "…hii ndio bwagamoyo yakhe karibu sana ulidhani umeopoa chombo basi umeopolewa (uk 43)." Hilo ni onyo la kimaadili ambalo linatolewa kwa njia ya kejeli na kijembe.

Waganga nao wana nafasi sawa na Masheikh na Makasisi katika kuwaongoza wanajamii na kuwajenga kiroho. Mganga wa unajimu Mzee Atrash Jamadu wa Mlingotini Bagamoyo anasawiriwa akitoa maonyo yake yaliyolenga katika kukemea tamaa, uongo na usaliti alivyokuwa anavifanya Suhail. Mzee Atrash anasema;

"Huwa siongelei habari za mtu ovyoovyo, na wala huwa sitoi habari nyeti kama hizi zihusuzo faragha za watu kwa mtu asiyekuwa makini, kwa mtu muongo, kwa mtu msaliti na mwenye tamaa. (uk 47)."

Hizo ni sifa alizoziainisha na ambazo zilimkaa vyema Suhail katika kuashiria matendo yake. Maneno ya kuonya juu ya kufanya mema na kukataza ubaya ni kazi tunayoitegemea kufanywa na viongozi wa dini na wazee katika jamii. Lakini katika jamii ya Mwingizi mtu yeyote yule ana nafasi ya kuonya na kutoa mwongozo wa maadili mema. Nafasi ya wazazi nayo bado inasisitizwa na mwandishi kiasi cha wanajamii kuendelea kuogopa laana ya wazazi. Mzee Kusekwa anamtishia mwanawe Suhail kumlaani anaposhindwa kwenda Tabora kutimiza ahadi ya kumuoa Sharifa.

> “Na kwamba labda siyo mimi Kusekwa, huyu mtoto atakoma na mimi siku akitia mguu wake tu Tabora hii anakutana na ndoa na huko Dar atarejea na mke asinichezee mimi. (uk. 69).

Kuna methali ya Kiswahili isemayo mtoto hakui kwa mzazi, japokuwa Suhail Kusekwa amekwisha kuwa mtu mzima mwenye maamuzi yake, nguvu ya wazazi bado ipo na inaenziwa katika jamii yake. Kukiuka amri ya mzazi kunaashiria ni kukaribisha ghadhabu ya mzazi ambaye inasemekena ana nguvu za kutoa laana inayoweza kumdhuru mtoto huyo.

Katika vitendo vinavyoashiria kuwepo kwa nguvu za ujaala na zenye kupewa mamlaka ya ki binadamu na kiungu ni pale Suhail anapoiamrisha pete kama vile inayosikia itoe adhabu na hukumu. Khatam Budha komesha*!* (uk. 113). Hali hii ya uhuishaji wa vitu vinavyoaminiwa na baadhi ya wanajamii katika riwaya za Mwingizi ni pale kibuyu kinaposemeshwa chooni ili kuwaangamize wachawi wa Kibondo katika riwaya ya *Tanzia*. Katika mila na desturi za mizimu ya wachawi wa Kibondo, kuna utaratibu wa kumwoza kiongozi wao mke hata kama kiongozi huyo ni mwanamke.

Kwa hiyo ndoa ya mwanamke na mwanamke inajidhihirika katika *Tanzia* pale Bi Masonganya anapomuoa Masunga Binti Kalombolu. Wanafanikiwa kupata mtoto kwa njia za kichawi na mtoto huyo kuitwa Nyembo. Kwa hivyo “Bibi Masonganya alikuwa ni Baba”..baba aliye mwanamke (uk 57).”Hakuna dini kati ya Uislamu na Ukristo inayoruhusu ndoa za namna hii. Ndoa hii inapatikana tu katika mila na desturi za wachawi wa Kigoma. Kitendo cha ndoa ya mwanamume aliyegeuzwa mwanamke nacho kinajitokeza katika riwaya ya *Mzimu wa Maufi* pale Masumbuko anapomgeuzwa Masumbuko kuwa mwanamke aitwaye Shamsa kama adhabu ya kukaidi kuwa mwanachama wa Waufi (uk 72-73). Wasomaji wanapigwa na mshangao wanapomwona Masumbuko akiwa katika umbo la mwanamke:

> “Haya jiangalie una uanamume gani hapo ulipo?!... Mara wale makungwi walipotoka tu nje ya chumba kile, naye akainama akaichukuwa Khanga yake na kujifunga kifuani mwake, akijuwa mambo yameshavurugika (uk73).”

Na katika ndoa ya aina nyengine ni ile ya mwanadamu kuoa jini. Katika *Vita vya Mapenzi*, Mzee Sufian ambaye ni jini anamuoa Amanda ambaye ni mwanadamu. Wakati Suhail ambaye ni mwanadamu anamuoa jini ambaye ni Shekhia mtoto wa Mzee Sufian. Aina hizi tatu za ndoa si za kawaida lakini mtunzi anazifanya ni ndoa za kawaida katika riwaya zake za kiuhalisiamazingaombwe. Maadili ya kijini na kimizimu ndio yanayoruhusu kufanyika kwa ndoa za namna hiyo. Picha ya mfumo dini mseto inapambuniliwa na mtunzi ambapo katika mazishi ya Mzee Mtandi (uk. 60) anazikwa Kiislamu ambapo wanawake walibaki majumbani walisindikiza jeneza kwa macho. Lakini Mzee Mtandi anachukuliwa katika matambiko makaburini ambapo sababu za kifo chake ndiko zilikoanzia. Katika *Tanzia* tunaonyeshwa ibada za kichawi zinazofanyika usiku wa kiza ambapo wachawi wanafanya ibada hiyo katika kaburi la hayati Mtandi huku wakiwa uchi mtupu (uk 60);

> "Kila mmoja alijiachia na kuserebuka atakavyo bila ya kujali ni athari gani atakayoacha kutokana na kubinuka akiwa mtupu mbele ya wenziye ambao wenigne ni wa jinsi tofauti na yake."

Hali hiyo ya imani za mizimu ya kichawi yenye kufuata dini zao inabainishwa pale Binti Sambayu anapojieleza alipokamatwa kwa uchawi na kuadhibiwa:

> "..Sisi ni wachawi ambao tulirithishwa tu uchawi kutoka kwa wazazi, mababu na maBibi zetu. Uchawi wetu uko chini ya mzimu mkubwa uitwao GULUGUJA. Tumefunzwa na kukuzwa katika tamaduni za kichawi mpaka tukafuzu. Wengi wetu tuliinigzwa humu tungali watoto wadogo japo kuna baadhi walishawishiwa na kuingizwa katika kikundi chetu cha uchawi wakiwa watu wazima…"

Dini ya uchawi ni sehemu ya dini za jadi ambazo wanajamii wakiwemo wale ambao wanaonekana katika macho ya watu na utambulisho tofauti kama vile Usheikh, Ukasisi, Usomi au Uaskari wakiwa hawana mahusiano na mitandao hiyo. Lakini mwandishi anawaumbua kupitia simulizi ndani ya *Tanzia*. Kitendo cha Babu Gao kukilipua kibuyu cha uchawi ni ishara ya anguko la wachawi wa kila aina:

> "Wakati kibuyu kikiteketea kwa moto huku nyumbani, upande wa pili huko wachawi wote waliokuwa ndani ya gari la Polisi walianza kuhangaika na kutaabika kwa maumivu yaliyosababishwa na kuteketezwa kwa kibuyu chao, hatimaye nao wakatekekea na kufa wote. Cha ajabu kuna baadhi ya watu waliokuwa majumbani mwao, nao walikuwa ni wachawi hivyo kudhihiri kuwa nao walikuwa ni wachawi tu japo siku ile wao hawakutoka kwenda kuwanga (uk 83)."

Hii inaashiria kwamba, watu walio wengi ni watu wenye kufuata imani mseto. Imani inayochangana imani ya dini za kigeni na itikadi mbalimbali ikiwemo itikadi za mizimu na hata itikadi za kichawi ambazo ndio mihimili ya himaya ya Waufi, *Khatam Budha* na wachawi wa Kibondo. Ndani ya mfumo wa dini za mizimu tunaonyeshwa mizimu ya aina mbili: "Mzimu .... uitwao Kasomangila, mzimu huo upo chini ya Waswezi (uk. 87)" dhidi ya Mizimu wa Waufi. Mzimu hiyo inaashiria mizimu ya wema na maovu.

Falsafa ya mwandishi yenye inayoangazia maadili kwa wanajamii yake ni pale anapouzungumzia ukweli kupitia mbazi ya milima;

> "Siku zote ukweli huwa umejificha mbali sana milimani hivyo ili kuufikia na kuupata, yapasa usafiri mpaka huko ukautafute...hii ina maana kwamba ukweli siku zote haupatikani kirahisi ndiyo maana ya kuwa uko mbali huko mlimani…, ukweli ni kitunguu, kadri unavyoendelea kumenya maganda ya vitunguu na kufikia kiini chake, ndivyo kitunguu hivyo kitakavyozidi kukutoa machozi.(uk .221)"

Falsafa ya mwandishi kupitia maneno ya IGP yanamtia moyo Inspekta Kenjah kutafakari juu ya kuutafuta ukweli. Hapa Mwingizi anatuleleza sisi wasomaji juu ya falsafa ya ukweli na ugumu wake katika kuubaini. Kwa kutumia taswira za "milimani" na "vitunguu", ukweli unaashiria sura mbili. Sura ya kwanza ni vigumu kuupata kwa rahisi, na sura ya pili ni pale unapojaribu kuutafuta, ukaumizwa lakini inabidi unahitaji uvumilivu.

Kwa misingi hii, Mwingizi hakujifunga na mfumo wa dini moja au itikadi yenye mlengo wa aina moja. Kama jamii yake ilivyo ametumia kila fursa yake kupenyezea mitazamo anuai ya uono ulimwengu katika jamii yake. Kuna misemo, ngano, nahau, za jamii yake kutoka kwa wasusi, wanausalama, wanadini, waganga wa jadi na hata wananchi wa kawaida (wazee). Mtazamo wake ni kuunganisha jamii yake yenye tofauti mbalimbali za watu kidini, kirika, kijinsia, kielimu, kiuwezo na kimtazamo. Anachoashiria mtunzi ni kutaka kujenga jamii yenye kuvumilia na kuwa na tofauti zao

za kionaulimwengu. Kimsingi mambo matatu ameyasisitizia kuwa ni ya kuchungwa nayo ni kuepuka uongo, usaliti na tamaa.

### 5.3.11 Hitimisho

Katika riwaya teule za Mwingizi, kumedhihrika aina mbalimbali za ishara na uashiriaji kuanzia rangi, wahusika wanyama na majini, majina ya maeneo, dini, ndoto, fedha, pete na kifo. Kwa ujumla ishara zote zinaelekea kudhirisha motifu mbalimbali kuanzia motifu ya kifo, ufufuaji, ibada na mawasiliano ya kihisia n.k. Funzo la mwandishi ni kuwa wakati tumegubikwa na maswala ya kiuhalisia na mtazamo ulimwengu wake, tusisahau kuwa wanajamii bado wapo katika lindi la dunia ya udhanaishi inayoamini maswala ya maisha baada ya kifo, imani za kishirikina kama chanzo cha maafa na maradhi na nuksi. Ni riwaya zinazolilia kuwepo kwa amani, haki, utu, na maendeleo ya watu. Kinacholalamikiwa na mwandishi ni kuwa tumewasahau wananjamii walio wengi na tunawaachia wakiteseka katika imani za kiza. Masimulizi yake yamekusanya matukio yanayoonekana ni ya kawaida katika jamii yenye sura mbili za uhalisia na usiri. Kuna kupigania umoja wa wanajamii yake waliogawika katika makundi na mionoulimwengu tofauti tofauti. Moja ya mkakati wake aliourudia rudia ni ule wa kutumia uashiriaji wenye sura mbili za ufafanuzi wa majukumu na dhima zake. Kuna mpaka uliowekwa na mwandishi baina ya uhalisia na umazingaombwe.

## SURA YA SITA

## MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 6.0 Utangulizi

Katika sura hii ya utafiti huu tumewasilisha matokeo ya utafiti kuhusu Jiniuchawi na Ushirikina kama Mkakati wa Uchimuzi katika Riwaya teule za Mwingizi. Aidha uchambuzi wa data katika utafiti huu umeweza kubainisha kwamba, mandhari na matukio ya kijiniuchawi na kishirikina, wahusika na ishara mbalimbali ni mambo yaliyochimuza maudhui na dhamira mbalimbali katika riwaya hizi za kimajaribio. Hivyo, sura hii inaeleza kwa muhtasari matokeo ya utafiti na mapendekezo kwa utafiti wa baadaye.

### 6.1 Muhtasari wa Matokeo

Utafiti huu umeonyesha wazi kwamba, riwaya tulizozitafiti ni za kimajaribio kama sura ya kwanza ilivyojieleza katika usuli wa utafiti. Katika sura ya pili tumeeleza dhana ya uchimuzi wa jiniuchawi na ushirikina kama kipengele cha uhalisijabu katika kuangalia historia ya riwaya za kimajaribio. Tumeona jinsi riwaya teule zilivyochimuza maswala mbalimbali kupitia vipengele vya mandhari, matukio, wahusika na ishara mbalimbali na kutupatia maudhui mbalimbali. Tumetekeleza madhumuni haya katika sura ya tatu, ya nne na sura ya tano ambapo tumeonyesha jinsi vipengele vya mandhari, matukio, wahusika na ishara vimeweza kuchimuzwa katika riwaya za kijiniuchawi na ushirikina. Kwa kufanya hivyo, tumebaini kuwa vipengele hivi vyote vimeweza kuchimuza maswala mengi ya msingi na nyeti ambayo mbali na kukumba jamii zetu, hujitokeza pia katika mataifa ya Kiafrika.

Aidha katika uhakiki wa riwaya za *Vita vya Mapenzi*, *Mzimu wa Waufi na Tanzia* kama riwaya za kimajaribio zilizosheheni mambo ya uchawi na ushirikina, tumebaini kuwa kwa kiasi kikubwa msuko, mtindo na muundo wa riwaya hizi ni tofauti na riwaya za kawaida kwa kuzingatia vipengele vya wahusika, mandhari, matukio na ishara. Riwaya hizi zimesheheni sifa mbalimbali za riwaya ya kimajaribio na kihalisiajabu kwani

masimulizi yake yamekuwa yakijikita katika maswala ya kijiniuchawi na ushirikina, mandhari ya kutisha na kuogofya, maswala ya visasili, maswala ya ndoto kuchanganyika na uhalisia, na wahusika wa kutisha wa kimajini na kichawi, hizi ni baadhi tu ya sifa hizo kwani, sifa nyingi tumejadili katika sura ya kwanza na ya pili kwa undani zaidi.

Katika sura ya pili tulielezea dhana ya uchimuzi kama kipengele kimojawapo katika riwaya za kimajaribio ambazo humfikirisha zaidi msomaji kwani msomaji wa riwaya hizi lazima atulie na afikirie kwa umakini kwa sababu watunzi wa riwaya hizi hutumia lugha ya kificho na humtaka msomaji atakafakari zaidi juu ya maswala mazito na ya msingi katika jamii. Vilevile tumeonyesha utanzu huu wa riwaya ya Kiswahili unakua kila siku kwa sababu ya matumizi ya mitindo mipya ya uandishi. Utafiti wetu umebaini ukweli huo kupitia riwaya za Mwingizi. Mtunzi amesimulia matukio katika kiwango cha kutisha na cha kuogofya hasa katika kuwajenga wahusika walio na wasifu mseto kama vile vile binadamujini au jini binadamu, mandhari changamani ya kihalisia na kimazingaombwe, ya uwepo hai na uwepo ndotoni, ya uhalisini na mizimuni; na kwa upande mwingine matumizi ya ishara zilizochimuza maudhui mbalimbali na mazito katika jamii. Matumizi ya ishara zisizo za kawaida yamechangia kwa kiasi kikubwa kusukuma riwaya za kimajaribio kwani ishara hizi zinamfikirisha msomaji na kumfanya atafakari mambo makuu yanayotendeka katika nafsi zetu, katika familia zetu, katika jamii zetu, katika mataifa ya ulimwengu wa tatu na katika ulimwengu kwa jumla.

Mtunzi amefanikiwa kuyazungumzia masula haya ya msingi kutokana na kutumia mbinu ya kijiniuchawi na ushirikina katika uwasilishaji wa maudhui yake jambo ambalo lingekuwa gumu kama angetumia mtindo wa kawaida au wa jadi katika uandishi wake. Aidha, mtunzi ametumia ukweli wa kibunilizi katika kuangazia tena maswala haya haya na jinsi yanavyosababisha matatizo katika maisha wa watu binafsi, familia, jamii na ulimwengu wa tatu na hata kusababisha kutokea kwa vita vya watu wa nasaba moja, jamii moja au taifa moja kuuwana wenyewe kwa wenyewe. Kwa mfano, mtunzi ameonyesha baadhi ya wahusika ambao wameingia nchini Tanzania na kuolewa na

watanzania kutokana na kukimbia vita vya wenyewe kwa wenyewe nchini Rwanda. Haya ni baadhi ya maswala ambayo yamejadiliwa kwa kina katika sura ya tatu, nne na ya tano.

Katika kufanikisha malengo yetu ya utafiti tulitumia nadharia mbili. Nadharia ya kwanza ni Nadharia ya Uhalisiajabu na nadharia ya pili ni Nadharia ya Semiotiki. Kwa upande wa nadharia ya uhalisiajabu, imesaidia, uchambuzi wetu wa kimaudhui na kidhamira kwani, tumeona mandhari yenye matukio na wahusika wa kiajabuajabu yaani wa kimajini na kishirikina kuanzia mwanzo hadi mwisho wa riwaya zetu. Wahusika wanabadilikabadilika na kuchukua nafsi zaidi moja tofautitofauti na kutenda mambo ya kushtua na kuogofya. Kutokana na madhumuni yetu, tumebaini kwamba riwaya hizi tatu zinaingiliana na kuchangiana kwa kiasi kikubwa katika kuchimuza maudhui mbalimbali. Aidha vipengele vya uhalisiajabu ni vingi katika riwaya hizi teule hasa katika kipengele cha wahusika, mandhari na matukio. Aidha kwa upande wa Nadharia ya Semiotiki tumeona ishara mbalimbali za kiajabuajabu zilivyotumiwa na mtunzi katika kuashiria maswala mbalimbali ya msingi. Mtunzi ametumia ishara mbalimbali katika kuchimuza maudhui tofautitofauti.

**6.2 Upimaji wa Madhumuni**

Katika utafiti huu tumejadili madhumuni makuu matatu. Madhumuni ya kwanza yalikuwa ni kuonyesha mandhari na matukio ya kijiniuchawi na ushirikina yalivyochimuzwa na kuendeleza maudhui mbalimbali katika riwaya za Mwingizi. Na madhumuni ya pili yalikuwa ni kubainisha jinsi wahusika wa kiuhalisiajabu walivyoweza kutumiwa kimkakati kwa kuhusianishwa na vipengele vya jiniuchawi na ushirikina katika kuchimuza na kuendeleza maudhui anuwai katika riwaya za Mwingizi. Madhumuni ya tatu yalikuwa ni kujadili maudhui mbalimbali yaliyochimuzwa katika riwaya za Mwingizi kupitia uashiriraji wa ishara mbalimbali.

Madhumuni haya matatu yameweza kuchimuza maudhui mbalimbali katika riwaya hizi za kimajaribio. Kwa mfano, mandhari na matukio yaliyokuwa yanatendeka katika

mazingira hayo mtunzi ametumia ubunifu katika kusawiri maswala ya msingi ambayo yanahusisha mitagusano mbalimbali ya kimaisha kupitia mazingira ya kutisha, mazingira dhahania na mazingira ya kawaida. Mtunzi amewasuka wahusika mbalimbali wenye nafsi mbili mbili yaani wakati mwingine wanakuwa ni binadamu halisi na wakati mwingine wanakuwa ni majini katika kuchimuza maswala ambayo yapo katika jamii na katika mataifa ya ulimwengu wa tatu. Hali kadhalika katika kuchimuza maudhui mbalimbali mtunzi ametumia ishara mbalimbali katika kuashiria mambo mbalimbali.

Miongoni mwa maudhui yaliyochimuzwa kupitia mandhari, matukio, wahusika na ishara katika riwaya hizi teuleza kimajaribio ni nafsi ya maisha ya mtu binafsi katika mitagusano anuwai ya kifamilia, kijamii, na kitaifa; wasifu na uamili wa uongozi, ambapo mtunzi anaonyesha jinsi viongozi wa serikali katika mataifa ya ulimwengu wa tatu wanavyokuwa wa binafsi, wanaong'ang'ania mamlakani, wasiopenda kutenda haki na wanaendesha mifumo yao ya kiutawala kimabavu, wasaliti na wanafiki, hawajali maslahi ya wananchi, wanaosaini mikataba isiyo halali ya maliasili za wananchi kwa ajili ya kujinufaisha wenyewe, mahusiano kati ya wahalifu na viongozi serikalini, mauaji ya watu wasio na hatia kwa ajili ya maswala ya kisiasa, ubadhirifu wa mali ya umma, rushwa na hila katika ushindani wa kisiasa. Kwa upande chanya katika dhamira hii ya uongozi mtunzi ameonyesha viongozi wachache ambao ni wazalendo na wawajibikaji wanaotanguliza maslahi ya watu wao.

Vilevile kupitia wahusika, mandhari na ishara mbalimbali zimechimuza dhamira nyingine kama vile za ukoloni mamboleo ambapo tunaona baadhi ya wahusika wakiathiriwa na utandawazi na kujikuta wakiwadharau wanajamii wenzao kutokana na kuiga mambo ya kizungu. Dhamira nyingine ni malezi, jamii imekumbushwa kuwa na malezi mazuri kwa watoto hata pindi watakapokuja kuondoka watoto waweze kuishi vizuri na kila mtu katika jamii. Dhamira nyingine zilizochimuzwa ni madhara hasi ya utandawazi katika mataifa ya ulimwengu wa tatu, mwanamke kuonekana ni kama kiongozi na kwa upande mwingine mwanamke amedunishwa kama kiumbe dhaifu kwa

kufanyiwa manyanyaso. Mfamo mzuri ni Mzee Kikoko alivyokuwa anamtesa mkwe wake.

Vilevile dhamira nyingine zilizochimuzwa ni migongano ya dini ambayo chanzo kikubwa ni majilio ya wageni (wakoloni) mpaka inafikia hatua wahusika wanatupiana vijembe na lugha za picha katika kusimangana kwa kuoana dini tofauti kati ya mkristo na muislamu. Mtunzi anaonyesha dhamira ya mapenzi ya dhati na mapenzi ya tamaa ya pesa kupitia kwa wahusika majini katika mandhari za kutisha. Aidha mtunzi anaonyesha jinsi maswala ya ukabila yanavyopelekea hata vita kutokea, mfano nchi ya Rwanda. Lakini kupitia dhamira hii ameyakumbusha pia mataifa ya ulimwengu wa tatu waache ukabila kabisa kwani ukabila husababisha maafa makubwa sana. Tupochunguza kwa makini sana migororo mingi katika mataifa ya Afrika inasababishwa na swala zima la ukabila kwa kiasi kikubwa. Hivyo mataifa haya yakitaka kuepuka janaga hili ni lazima waachane kabisa na ukabila.

Fauka ya hayo, mtunzi anachimuza dhamira nyingine ya uhuru wa bendera. Mtunzi anaonyesha jinsi mataifa ya ulimwengu wa tatu yalivyo na uhuru wa bendera kwani mambo mengi ya msingi pamoja na maamuzi ya baadhi ya mambo hutegemea katika mataifa yaliyoendelea yaani ukoloni bado upo japo hauonekani waziwazi kama vile kipindi cha zamani. Aidha mtunzi anawakumbusha wazee katika jamii wawe na hekima na busara ili vijana waweze kujifunza mambo mazuri kutoka kwao. Wanachimuza wawe na umoja na uvumilivu katika maswala mbalimbali katika jamii, kuwa wawajibikaji na watendakazi wazuri, kuthamini utamaduni wa kiafrika, kuwa na maadili kwa wale viongozi na wanajamii kwa ujumla, kuepukana na uongo, kuona tahamani ya elimu na waepukana unyanyapaaji.

Kimsingi, ujiniuchawi na ushirikina umesawiriwa kimkakati kuchimuza maswala mseto ya kimaudhui na kidhamira na mkakati huu umechukua nafasi kubwa katika uendelezaji wa riwaya hizi teule za kimajaribio za Mwingizi katika kiwango cha mandhari, matukio, wahusika na matumizi ya ishara kwa kiasi ambacho dhamira za mtunzi zinajitokeza.

Kwa jumla, utafiti huu unahoji na kusisitiza kwamba, Maundu Mwingizi hazungumzii ujiniuchawi na ushirikina kwa ajili ya kuzungumzia mambo hayo tu, bali ujiniuchawi na ushirikina ni mkakati wa mwendelezo, mkakati wa ukuzaji, mkakati wa msuko na mkakati wa uchimuzi unatilia mkazo kwamba uchimuzi ndio nguzo kuu ya uendelezaji wa riwaya hizi za kimajaribio.

**6.3 Mapendekezo**

Matumaini yetu ni kwamba, utafiti huu utakuwa msingi bora wa uchanganuzi wa uchimuzi katika riwaya za kimajaribio zilizosheheni maswala ya uchawi na ushirikina. Kwa kuwa utafiti wetu ulihusu dhana ya uchimuzi katika riwaya hizi, bado tafiti zaidi zinahitajika kwa kuzingatia mielekeo mingine ya kiuhakiki katika riwaya hizi. Kwa sababu hiyo tumependekeza utafiti zaidi juu ya mambo yafuatayo:

Katika uchunguzi wetu tuligundua kwamba riwaya hizi zinaweza zikahakikiwa kwa kuangalia kwa kina katika kipengele cha lugha yaani katika kuangalia uchimuzi katika kiwango cha lugha kwa ujumla. Yaani, uchimuzi katika lugha kisintaksia, kifonolojia na kimofolojia na kisemantiki. Kwa kuwa hakuna utafiti wowote uliofanywa kuhusu riwaya hizi, ni vyema watu wakafanyia utafiti riwaya hizi za kimajaribio katika kuangalia sifa muhimu za riwaya hizi. Riwaya hizi pamoja na kuwa za kimajaribio, zinaweza kuhakikiwa kwa njia mbalimbali kama vile kuzihakiki kama riwaya za kisaikolojia, kimapinduzi au kifalsafa.

Pia utafiti mwingine unaweza ukafanywa ili kubainisha dhima za ukiushi na ukinzani katika riwaya za kimajaribio zikiweno hizi za Mwingizi. Aidha utafiti mwingine unaweza ukafanyiwa kuangalia dhana ya uchimvi katika kuendeleza maudhui mbalimbali katika riwaya hizi na zile zinazofanana na hizi. Kwa upande mwingine, riwaya hizi zinaweza zikahakikiwa kama riwaya za kihalisiajabu katika karne ya ishirini na moja katika uendelezaji wa fasihi ya Kiswahili.

## MAREJELEO


Abrams, M.H. (1971). *A Glossary of Literary Terms*. New York :Holt Rinehart and Winston.

Aston, E. na Savona, G. (2005).*Theatre as a Sign –System*: *A Semiotics of Text and Performance*. London & New York: Routeledge.

Alexander, M. (1990). *Flights from Realism*. London: Edward Anold.

Arnold, S. (1988). *African Literature in the 20c by Leonard SKlein*: Harpenden. Herts: Olcastle 1988.pp 214-220.

Bakhtin, M.M. (1975). *Questions of Literature and Aesthetics*, (Russian) Moscow: Progress.

Brabencova, L. (2011).*Different Concerpt Of Magic Realism in Selected Works by Saleman Rushidie and Graham Swift*, Charles University,

Brain, J L (1981). *Witchcraft and Development*. Dar es Salaam University; Press Limitted: London

Barthes, R. (1994).*The Semiotic Challenge*. Berkely: University of Califonia Press.

Baudelaire, Charles. (1857). *Les Fleures du Mal.* Paris: Auguste Poulet-Malassis.

Ben Okri (1991).*The Famished Road*, Jonothana Cape, UK

Bin Nasir, Sayyid Abdalla Bin Ali. (1977). *Al-Inikishafi. Catechism of a Soul*. Nairobi, Kampala &Dar es Salaam: East African literature Bureau.

Birkerts, Sven (1993).*"Symbolism," Literature: The Evolving World*. Boston: Allyn and Bacon.

Caufield, C (1996). *Masters of Illusion: The World Bank and the Poverty of Nations*. New York: Henry Holt.

Chanady, Amaryll Beatrice (1985). *Magical Realism and the Fantastic*.New York Garland Publishing Inc .

Chandler, D. (1992). *Semiotics The Basics,* London: Routledge Press.

__________ (2002).*Semiotics*: *The Basics,* 2nd Edition. London: Routledge.

__________(2005).*Semiotics for Beginners*. Aberyswyth University. Available at:http://www.aber.ac.uk/media/Documents/S4/semo1.html. (Accessed: 12 January, 2014)

Cirlot, Juan E. 1962. *A Dictionary of Symbols*. London: Routledge & Kegan Paul.

Cluysenaar, A. (1976). *Introduction to Literary Stylistics*. B.T Batsford, Limited: London

Cooper, B. (1988*). Magical Realism in West African Fiction*. New York: Routledge.

__________(1998). *Magical Realism in West African Literature*: *Seeing with aThird Eye*. New York: Routledge.

Danow, K.D. (1995). *The Spirit of the Carnival; Magical Realism and the Grostesque.* Kentucky University of Kentucky Press.

DiYanni, R. (1998). *Literature:Readings Fiction, Poetry and Essay*: (4) Boston: Macgraw hill

De Saussure, F. (1966). *A Course In General Linguistics* (W. Baskin, Trans.). New York: McGraw-Hill. Engels

EBinger, E (2000). An Examination of the Use of Magic And Madness as Narratives Devices In The Novel 0f Grazia Deledela and Tom Morrison, Carifonia State University. Unpublished

Encarta Encyclopaedia (2002). New York. Microsoft Company Limited.

Erlich, V. (1969). *Russian Formalism*. 3rd Edition. The Hague: Mounton & Co.N.V Publishers

Fokkema, D.W. & Kunne-Ibsch, E. (1979).*Theories of Literature in the Twentieth Century*. USA:.Hurst & Company.

Freeman, D.C. (1970).*Linguistics and Literary Style*. University of Massachussets: Holt Rhinehart and Winston

Frey, na wenzake. (1985). *The Harpe Handbook of Literature*: New York. Harpe Collins.

Garvin, Paul L. (ed.) 1964. *A Prague School Reader on Aesthetics, Literary Structure and Style*. Washington: Georgetown University Press.

Griffen, E. M. (1997*). A First Look At Communication Theory*. New York: McGraw-Hill Companies Inc.

Gromova, M.D. (1998). Nagona and Mzingile*:* Novel Tale or Parable, *Afrikanistische Arbeitspapier 55.73-78*

__________(2002). *Post Modernistic Elements in Recent Swahili Novels*. Nairobi: (Haijachapishwa).

Hakemulder, J (2007). “Tracing Foregrounding in Responses to Film” In *Encyclopedia of language and linguistics*, pp. 546-551, Vol. 4. 2nd edition. Oxford: Elsevier

Hussein, I. N. (1969). *Kinjeketile*. Dar es Salaam: Oxford University Press.

____________(1971). *Mashetani*. Nairobi/ Dar es Salaam: Oxford University Press.

Ismail, Bin Hassan. (1969). The Medicine Man: *Swifa ya Nguvumali*. (ed.) Lienhardt Oxford: Clarendon Press. Kanar

Jakobson, R. (1968). "Language in Relation to Other Communication System" in Jakobson (1971b), pp 697-708.

___________(1987). *Language in Literature*. K. Pomorska & S. Rudy (Eds.). Cambridge, Harvard University Press.

Jameson, F.(1972). *The Prison-House of Language*: Princeton NJ Princeton (2) University Press.

Jefferies, L na Mcintyre (2010).*Stylistic*: cambrigde university press

Kazungu, K. E. (1982).Deviation and Foregrounding in chosen Swahili literary texts. MA Thesis UON, Unpublished

Kezilahabi, E. (1990). *Nagona*.Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

____________ (1971). *Rosa Mistika*: Nairobi. Kenya Literature Bereau.

____________ (1975). *Dunia Uwanja wa Fujo*: Nairobi, Vide-Muwa Publishers Limited.

____________(1979). *Gamba la Nyoka*: Eastern African Publications.

____________(1990). *Nagona:* Nairobi, Vide-Muwa Publishers limited.

____________ (1991). *Mzingile*.Dar es Salaam: Dar-es-Salaam University Press

Kennedy, X. Joseph & Gioia, Dana (Eds.) 2005. *Literature: An Introduction to Fiction, Poetry and Drama*. New York: Longman.

Kiende M, F. (2012). Dhana ya Uchimuzi katika Uendelezajiwa Riwayaya Kimajaribio ya Mafamba.Tasnifu ya Uzamili. Chuo kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Kilanga, B.S.(2015).Ishara katika kaptula la max na kijiba cha moyo:mtazamo wa kisimiotiki, haijachapishwa, chuo kikuu cha Nairobi

Kivisto, S.( 2014). *Death in Litereture*.London & New York: Routeledge

Lakoff, G. and Johnson, M. (1980).*Metaphor We Live By*. Chicago: University of Chicago Press

Leech, G.N. (1969).*A Linguistic Guide to English Poetry*. London: Longman Group Ltd.

Leech, G.N. na M. A. Short, (1981).*Style in Fiction: An Introduction to English Fictional Prose.* London: Longman

Lwendo, H. (1994). Mapepo Na Majini. *Jarida La Kichungaji Juzuu No 1* Chuo cha Theolojia Makumira

Lugwiri, P. O. (2011). "Sitiari, taashira na tashBiha katika Uwasilishaji wa Dhamira katika *Utenzi wa Tambuka*: Uhakiki wa kimtindo." Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Madumula, J. S. (2009).*Riwaya ya Kiswahili.* Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Magaju, J. (2004). *Uhalisiajabu kati ya Riwaya ya Babu Alipofufuka* (2001) ya S.A Mohamed na *Bina-Adamu!(*2002) ya K.W Wamitila. Tasnifu ya M.A Chuo kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Massamba David, P. B. (2004).*Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam:Tuki.

Mason, M. (2010). Sample Size and Saturation in PhD Studies Using Qualitative Interviews, katika *Forum: Qualitative Social Research*, No. 11(3) pg. 73-96.

Mark, G. (1995). Postmodern Semiotics: Material Culture and the Forms Of Postmodern Life. Oxford: Basil Blackwell.

Martindale, C (2006). Response: Psychological Foundations of Literary Theory: *Journal of Literary Theory,* Department of Psychology . University of Maine.

Mazrui, A. (1982).*Kilio cha Haki*. Nairobi: Longman.

Mazrui, A. Na Njogu, K. (2001*). Sudana*. Nairobi: Longhorn Publishers. cha Nairobi.(Haijachapishwa).

Mbatiah, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi**:** Standard textbook Graphics and Publishers.

Mbatiah, M. (2006).*Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Standard Text Books and Publishing.

Mbiti, S. John (1975). *Introduction to African Religion*, Praeger, New York,

Mbogo, E. (2008), *Ngoma ya Ng'wanamalundi*, Nyambari Nyangwine Publishers, Dar es Salaam.

Meyer, M. (2002). *The Bedford Introduction to Literature*: London, Bedford and Martins

Miall, D. S., & Kuiken, D. (1994). Beyond Text Theory: Understanding literary response. Discourse Processes, 17, 337-352.

Mkangi, K. (1984). *Mafuta.* Nairobi. East African Educational Publications

____________(1995).*Walenisi*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Mkufya, W.E (1999).*Ziraili na Zirani***.** Dar es Salaam: Hekima Publishers.

Mlacha, S.A. (1991). *Linguistic Study of the Novel:*Verlag Schreiber Publishers, Berlin.

Mohamed, S. A. ( 1980).*Utengano*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Mohamed, S. A. (1995).*Amezidi.* Nairobi: East African Education Publishers.

___________ (2001).*Babu Alipofufuka*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

__________(2006). *Dunia Yao*.Nairobi. Oxford University Press.

___________ (2011).*Kimya Kimya Kimya*. Nairobi: Longhorn Publishers.

__________(2012). Mhanga wa Nafsi. Oxford University Press

Morris, C.W. (1938). Foundations of Theory of Signs (*International Encyclopedia of Unified Science1-2)* Chicago: University of Chicago Press.

Moussa, I. (2012). *Hybridizing Politica Criticism in the Postcolonial African Novel*: *Magical Realism as Aesthetic of Necessity*. Unpublish Dissertation; University of North Carolina Greenborn

Msokile, M. (1993).*Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*: East Eduction Publisher Nairobi

Mwingizi, M. (2012). *Vita vya Mapenzi*. Bagamoyo: Gama Printers

___________(2013). *Mzimu wa Waufi*. Bagamoyo; Gama Printers

___________(2015).*Tanzia*. Bagamoyo; Gama Printers

Mukarovsk, J. (1977). *The Word and Verbal Art.* J. Burbank & P. Steiner (Eds. and Trans.). New Haven and London: Yale University Press.

Mukuthuria, M (2007). Upekee wa Utenzi wa Swifa ya Nguvumali, katika *Nordic journal African studies 16 (3): 298-313*

Mulokozi, M. (1979). *Mukwava wa Uhehe*.Nairobi: East African Pulishing House.

Mulokozi, M.M na Kahigi, K.K. (1995). *Malenga wa Bara*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Mung'ong'o, C. G. M (1977). *Mirathi ya Hatari*, Dar es Salaam Tanzania: Publishing house.

Mwanjiru, M.J (2013). Uhalisia na Uhalisiajabu katika Riwaya ya Babu Alipofufuka na watu wa Gehenna, Tasnifu ya uzamili. Chuo kikuu

Nabukonde, L.(2001). *Symbolism in Ugandan Poetry:* Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu (haijachapwa) Chuo Cha Kikuu Nairobi,

Nauta, D. Jr. (1972).*The Meaning of Information*. The Haque: Mouton:

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi*: *Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

__________ (2008). *Ufundishaji wa Fasihi*: Nadharia na Mbinu. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Nyabunga, A. (2005). *Uhakiki wa Bina- Adamu! (2002) na Musaleo*! (2004) za K.W Wamitila. (Haijachapishwa)

Okri, B. (1991). *The Famished Road*. New York: N.A Talese.

Olali, T. (2008). *Mafamba*.Nairobi.Jomo Kenyatta Foundation.

________(2010). Structure and Anti-Structure of a Swahili New Novel: Astylistic Analysis of *Babu Alipofufuka*

________(2012). *Watu wa Gehenna*. Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.

Omar, C.K. (1993). *Uchawi na Ushirikina*, Mwanza; Inland Press

Paris, Bernard J. (1974). *A Psychological Approach to Fiction*. Bloomington: Indiana University Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Peirce, C.S. (1931). *Collected Papers* ;Cambridge; Harvad University Press.

Perrine, L. (2014). *Literature Structure*, *Sound*, *sense*: Boston, Wadsworth. afrikanistik. gko.uni-leipzig.de/swafo/images/documents. Iliyopakuliwa 20/12/2016 saa 10 jioni.

Robert, S. (1952). *Adili na Nduguze*, Macmillan; London.

_________(1951). *Kusadikika*, Nelson; Nairobi.

_________(1946). *Kufikirika*, Oxford; Nairobi.

Robson, C., (2007). *How to do a Reserch Project: A Guide for Undergraduate Students*, Carton Victoria: Blackwell Publishing.

Roh, F. (1925). *Nach-Expressionismus-Magischer Realismus*. Leipzig. Krinkhardt & Biermann

Sebeok,T. A. (1974). *Studies in Semiotics*: *Contributions to the Doctrine of Signs*. Indiana: University Press.

___________(1977). *A Perfusion of Signs*. Boomington: Indiana University Press.

Scholes, R. (1974). *Structuralism in literature*. New Haven, CT: Yale University Press

Selden, R. (1985) *An Introduction to Literary Criticism.* New York: Harvester Wheatsheaf.

Selden, R. (1988).*The Theory of Criticism fron Plato to the present*:A reader.AddisonWesley Longman Ltd.

Senkoro, F.E.M.K. (1995). "E.Kezilahabi Shaaban Robert wa Pili"*Katika Kioo cha Lugha*: Juzuu 1, Na 1.Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

__________ (2007)."Uhalisiamazingaombwe katika Fasihi ya Kiswahili" *katika .Kioo cha Lugha* Juzuu na 5, kur 1-12

___________(2011). *Fasihi*. Dar Es Salaam.  KAUTTU

Shemwita, S (2015). Itikadi katika Tamthiliya za Emmanuel Mbogo: Utafiti Linganishi wa Ngoma ya Ng'wanamalundi na Fumo Liongo. Tasnifu Haijachapishwa.Chuo Kikuu Huria cha Tanzania

Shorter, A. (1988). African Culture and the Christian Church. London: G. Chapman

Snowden, R. (2006). *Freud-The Key Ideas:* (*Teach Yourself Series)* London; Hodder Education.

Solomon, J. (1988). *The Signs of Our Times: The Secret Meanings of Everyday Life*. New York: Harper & Row.

Sperber, na wenzake. (1986). *Relavance Communication and Cognition*: London, Black Well.

Strecher, M. C. (1999). Magical Realism and the Search for Identity in the Fiction of Murakami Haruki, *Journal of Japanese Studies*, Volume 25.Foundation

Shklovsky, V. (1965). *Art as Technique*. In L. T. Lemon & M. J. Reis (Eds. and Trans.), *Russian formalist criticism: Four essays. Lincoln, NE: University of Nebraska Press. (Original work published 1917.)*

Thiong'o, G. (196i). *Nimelogwa Nisiwe na Mpenzi. Dar es Salaam:* East African Literature.

___________ (2005). *Wizard of the Crow*.New York: Pantheon

Thomas, A.S. (2001). *An Introduction to Semiotic*: (Toleo la Pili) University of Toronto Press, London.

Todorov, T. (1982).*Theories of Symbols*: Ithaca, Ny Cornell University Press.

Ullmann, S. (1964).*Language and Style*. Great Britain: Oxford Basil Black well

Umberto, E. (1976). *A Theory of Semiotics*: Bloomington in Indiana University Press, London Macmillan.

Van Peer, W. (1986). *Stylistics and Psychology: Investigations of Foregrounding*. London: Croom Helm.

Van Peer, W. & J. Hakemulder (2006). Foregrounding. In K. Brown (Ed.), *Encyclopedia of language and linguistics*, , *Vol. 4. 2nd edition*. Oxford: Elsevier. pp. 546-551

Van Peer, W. & J. Hakemulder (2007).Complexity and Foregrounding: In the Eye of the Beholder? . In K. Brown (Ed.), *Encyclopedia of language and linguistics, Vol. 4. 2nd edition*. Oxford: Elsevier. pp. 546-551

Vutagwa F.L (2013). Sifa za Uhalisiajabu na Umuhimu wake katika Utenzi Mwanafatuma: Tasnifu ya uzamili. Chuo Kikuu cha). Nairobi. (Haijachapishwa

Wafula, R. M. (2003). *Uhakiki wa Tamthilia Historia na Maendeleo yake*, Jomo KenyattaFoundation, Nairobi Kenya

Wafula R. M. na Njogu K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi. Jomo Kenyata Foundation.

Walibora, K. na Said, M. (2007). *Damu Nyeusi na Hadithi nyingine*: Nairobi, Jomo Kenyatta Foundation. Nairobi:

Wanyonyi, M. C. (2011). "Uhakiki wa riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* na Said Mohamed: Mtazamo wa Saikolojia Changanuzi". Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa.)

Wa Mutiso, Kineene. (1996). Archetypal Motifs in Swahili Islamic Poetry: Kasida ya Burudai.Tasnifu ya Shahada ya Uzamifu ambayo haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Nairobi

Wamitila (2002). *Bina-Adamu!* Nairobi: Phoenix Publishers.

_______(2004) *Zimwi La Leo:* Phoenix Publishers

________(2003a). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia.* Nairobi: Focus Books.

_______(2003b). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi.* Nairobi: Focus.

________(2003c). Influence or Intertextuality? A Comparative Study of Kezilahabi's Nagona and Mzingile and Juan Rulfo's Pedro Paramo. *Kiswahili 66:49-58*

_________(2004). *Musaleo!* Nairobi. Vide-Muwa Publishers.

_________(2007). " Narrative Structure and Metaphor:Towards a New Aesthetics of the *Kiswahili* Novel" in Vol 70. *Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili,* Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, pg 67-75.

________(2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi.* Nairobi: Vide-Muwa Publishers Limited.

Wellek, R. na Warren, A. (1948).*Theory of Literature*, Harcourt, Brace and Company: New York.

Wellek, R. (1988). *The Crisis in Comparative Literature: Concepts of Criticism*. Stephen G. Nichols, Jr. New Haven: Yale UP, 282-95.

Were, A. (2012) "Fani katika *Kilio cha Haki* na *Kijiba cha Moyo.*"Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa.)

Wright, W. (1975*). Sixguns and Society: A Structural Study of The Western*. Berkeley: University of California Press.

Zamora P.L. & B.W. Faris (1995). *Margical Realism:Theory, History and Community*. Duke University Press Ltd. London.

## KIAMBATANISHI NAMBA 1: ORIGINALITY FORM

**UNIVERSITY OF NAIROBI**

**Declaration of Originality Form**

This form must be completed and signed for all works submitted to the University for examination.

Name of Student NEEMA GEORGE MTURO

Registration Number C80/99107/2015

College HUMANITIES AND SOCIAL SCIENCE

Faculty/School/Institute FACCULT OF ART

Department OF KISWAHILI

Course Name PHD OF PHILOSOPHY IN KISWAHILI STUDIES

Title of the work: JINIUCHAWI NA USHIRIKINA KAMA MKAKATI WA UCHIMUZI KATIKA RIWAYA ZA MAUNDU MWINGIZI

**DECLARATION**

1. I understand what Plagiarism is and I am aware of the University's policy in this regard
2. I declare that this THESIS (Thesis, project, essay, assignment, paper, report, etc) is my original work and has not been submitted elsewhere for examination, award of a degree or publication. Where other people's work, or my own work has been used, this has properly been acknowledged and referenced in accordance with the University of Nairobi's requirements.
3. I have not sought or used the services of any professional agencies to produce this work
4. I have not allowed, and shall not allow anyone to copy my work with the intention of passing it off as his/her own work
5. I understand that any false claim in respect of this work shall result in disciplinary action, in accordance with University Plagiarism Policy.

**Signature** ____________

**Date** 12/11/2016

## KIAMBATANISHI NAMBA 2: TURNITIN ORIGINALITY REPORT

JINIUCHAWI NA USHIRIKINA KAMA MKAKATI WA UCHIMUZI KATIKA RIWAYA TEULE ZA MAUNDU MWINGIZI

ORIGINALITY REPORT

| 7% | 7% | 1% | 3% |
| --- | --- | --- | --- |
| SIMILARITY INDEX | INTERNET SOURCES | PUBLICATIONS | STUDENT PAPERS |

PRIMARY SOURCES

| | | |
| --- | --- | --- |
| 1 | erepository.uonbi.ac.ke<br>Internet Source | 2% |
| 2 | kiswahili.uonbi.ac.ke<br>Internet Source | 1% |
| 3 | www.qucosa.de<br>Internet Source | 1% |
| 4 | repository.out.ac.tz<br>Internet Source | 1% |
| 5 | deusdeditmahunda.blogspot.com<br>Internet Source | <1% |
| 6 | Submitted to Eiffel Corporation<br>Student Paper | <1% |
| 7 | Submitted to University Der Es Salaam<br>Student Paper | <1% |
| 8 | Submitted to University of Nairobi<br>Student Paper | <1% |
| 9 | Submitted to Mount Kenya University | |